
Ellen G. White Estate
Tumaini la Vizazi Vyote
ELLEN G. WHITE

# Tumaini la Vizazi Vyote

Ellen G. White

2001

Copyright © 2021
Ellen G. White Estate, Inc.

# Information about this Book

## Overview

This eBook is provided by the Ellen G. White Estate. It is included in the larger free Online Books collection on the Ellen G. White Estate Web site.

## About the Author

Ellen G. White (1827-1915) is considered the most widely translated American author, her works having been published in more than 160 languages. She wrote more than 100,000 pages on a wide variety of spiritual and practical topics. Guided by the Holy Spirit, she exalted Jesus and pointed to the Scriptures as the basis of one's faith.

## Further Links

A Brief Biography of Ellen G. White
About the Ellen G. White Estate

## End User License Agreement

The viewing, printing or downloading of this book grants you only a limited, nonexclusive and nontransferable license for use solely by you for your own personal use. This license does not permit republication, distribution, assignment, sublicense, sale, preparation of derivative works, or other use. Any unauthorized use of this book terminates the license granted hereby. (See EGW Writings End User License Agreement.)

## Further Information

For more information about the author, publishers, or how you can support this service, please contact the Ellen G. White Estate

at mail@whiteestate.org. We are thankful for your interest and feedback and wish you God's blessing as you read.

# Contents


Information about this Book . . . i
1 — Kristo Kabla Hajaja Duniani . . . 13
Mbinguni Kanuni hii ilivunjika! . . . 14
Toleo la Hiari . . . 15
Alitendewa kama tulivyostahili . . . 17
2 — Watu Ambao Wangalipokea . . . 18
Jinsi walivyopotosha Huduma ya Hema Takatifu . . . 19
Kutazamia Masihi wa Uongo . . . 20
3 — Dhambi ya Binadamu na “Utimilifu wa Wakati” . . . 21
Wengi walitamani Mkombozi . . . 21
Jinsi Shetani alivyokuwa karibu kufaulu . . . 23
Mungu auhurumia ulimwengu uliopotea . . . 23
4 — Kuzaliwa Zizini . . . 25
Wachungaji wa kondoo tu, walijali . . . 26
5 — Yusufu na Mariamu Wamweka Wakfu Yesu . . . 28
Mheshimiwa Simeoni Alimtambua Yesu . . . 29
Uchungu ambao Mama wa Kristo hana budi kuufahamu . . . 30
Jinsi kila mtu atakavyo jihukumu . . . 31
6 — Tumeiona Nyota Yake . . . 32
Safari ya Usiku . . . 33
Wivu wa Herode Uliamishwa . . . 33
Hakuna mtoto wa Kifalme . . . 34
Herode afanya Mauaji ya kutisha . . . 35
7 — Mtoto Yesu . . . 37
Viumbe vya asili vilifunua wito wa Biblia . . . 38
Kristo aliheshimu kazi kama Seremala . . . 39
Mwimbaji Mchangamfu . . . 39
8 — Kuhudhuria Katika Pasaka . . . 41
Wazazi wake wafadhaika . . . 43
Yesu alimsaidia mama yake . . . 44
9 — Matatizo ya Kristo Wakati wa Utoto . . . 46
Jinsi Yesu alivyowaheshimu wote . . . 47
Matatizo ya Yesu na jamaa yake . . . 48
Kwa nini ilimpasa awetofauti na wengine? . . . 49

10 — Sauti Nyikani . . . 51
Zakaria aliona shaka . . . 52
Elimu ya Yohana isiyo ya kawaida . . . 53
Isaya afafanua maneno . . . 54
Ukingoni mwa Mapinduzi . . . 55
Maonyo makali ya Yohana kwa wanafiki . . . 56
11 — Ubatizo wa Yesu . . . 58
Kristo asiyekuwa na dhambi, abatizwa . . . 59
Mbingu yatia Sahihi . . . 60
12 — Majaribu . . . 61
Shetani alikusudia kufaulu . . . 62
Alichukua Hali zote za kibinadamu . . . 63
Jaribu la kutia shaka . . . 63
Udhalimu bila Kiasi . . . 65
13 — Ushindi . . . 67
Kuthubutu kuingia katika Uwanja wa Shetani . . . 68
Kristo asingeweza kununuliwa . . . 69
Shetani huduma kuwa Adui Aliyeshindwa. . . . 69
14 — Tumemwona Masihi . . . 71
Wengi leo wanashindwa “kumwona” Kristo . . . 72
Sura ya Kristo Haikupambanuliwa . . . 73
Yohana awaelekeza wanafunzi wake kwa Yesu . . . 74
Maombi ya siri ya Nathanael yalisikiwa . . . 76
Hoja yenye nguvu zaidi . . . 77
15 — Yesu Ahudhuria Harusi . . . 79
Imani ya Mariamu yapata thawabu . . . 81
Kristo alivunja mtengano wa matabaka . . . 82
16 — Kristo Akabili Machafuko Hekaluni . . . 85
Udhalimu wa kifedha kazini mwa Mungu . . . 85
Hekalu latakaswa kwa kuwako kwake Bwana . . . 87
Kabla ya Hukumu ya Mwisho . . . 88
Mwanzo wa Kumkataa Kabisa Kristo . . . 90
17 — Nikodemo Amwendea Yesu Wakati wa Usiku . . . 93
Siri ya kuzaliwa upya inaelezwa . . . 95
Nikodemo aanza kuona mwanga . . . 96
18 — Yeye Hana Budi Kuzidi Bali Mimi Kupungua’ . . . 100
Kielelezo cha Yesu cha kuepuka kutokuelewana . . . 101
19 — Yesu na Mwanawke Mwenye Waume Watano . . . 103

Usikizi wa Mwanamke Umeamshwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . 104
Siri ya mambo yake ya nyuma . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 104
Mzunguko wa Mavuno ya Injili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 107
Kristo avunja ukuta wa chuki . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 108
20 — “Msipoona Ishara na Maajabu” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 110
21 — Bethzatha na Sanhedrin . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 113
Siri ya kuponywa kiroho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 114
Kanuni zisizokuwa na maana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 115
Watu wamkusanyikia Yesu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 116
Yesu alitegemea uwezo wa Baba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 117
Ufufuo wa Uzima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 119
Mahakama yashindwa kumtisha Yesu . . . . . . . . . . . . . . . . . 120
22 — Kifungo na Kifo cha Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 122
Uchungu mkali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 123
Yesu atoa vithibitisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 124
Hakuna mtu mkuu zaidi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 125
Zaidi ya Nabii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 126
Sababu ambayo Kristo hakumwokoa Yohana . . . . . . . . . . . 128
23 — Jinsi Danieli Alivyomtambua Yesu kuwa ni Kristo . . . . 130
Nabii Danieli Alitabiri Kazi ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . 131
24 — “Je, Huyu Siye Mwana wa Seremala?” . . . . . . . . . . . . . 133
Yesu alifunua hali yao halisi mbele yao . . . . . . . . . . . . . . . 135
25 — Mwito Kando ya Bahari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 138
Uovu ulifunuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 139
Thawabu ya Kujitolea . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 140
Jinsi Watumishi halisi wanavyofundishwa . . . . . . . . . . . . . 141
26 — Siku za Shughuli na Raha katika Kapernaumu . . . . . . . 142
Hakuna Mashaka wala kusitasita . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 143
Shetani atenda kazi kwa kujificha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 145
27 — Mwenye Ukoma wa Kwanza Kuponywa na Kristo . . . . 148
Jinsi Kristo anavyo safisha moyo kutokana na dhambi . . . . 150
Mzigo wa dhambi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 151
Kuponya kiroho kila mara hutangulia kuponya kimwili . . . 153
28 — Mathayo: Kutoka Kutoza Ushuru Mpaka Mwanafunzi 155
Jaribio la Kufarakisha wanafunzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 156
Uvuli Mzito . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 157
Viriba vipya kwa divai mpya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 159
Hatari ya kushikilia mawazo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 159

29 — Yesu Aiokoa Sabato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 161
Ishara ya Mwongofu wa kweli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 162
Fundisho la Sabato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 162
Yesu aliponya kwa makusudi siku ya Sabato . . . . . . . . . . . . 164
Wanyama walitunzwa sana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 164
30 — Awekea Mikono Mitume Kumi na Wawili . . . . . . . . . . . 167
Mwenye imani Haba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 168
31 — Mahubiri Mlimani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 170
Kristo alikatisha tamaa tumaini la ukuu wa duniani . . . . . . 171
Roho tulivu humtukuza Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 172
Makutano walishangaa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 173
Kina na Upana wa Sheria ya Mungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 176
Hakuna udhuru kwa majaribu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 177
32 — Afisa wa Jeshi Aomba Msaada Kwa Ajili Mtumishi Wake . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 180
Mtu mfu amefufuliwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 181
33 — Jinsi Yesu Alivyojihusisha na Matatizo ya Jamaa . . . . . 184
Uwezo Mpya watawala . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 186
Ndugu halisi wa Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 187
34 — Nira Yake ni Laini na Mzigo Wake ni Mwepesi . . . . . . 189
Kile Kinachotuchosha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 190
Jinsi Nira yake inavyorahisisha kazi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 191
35 — Kutuliza Dhoruba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 193
Yesu alijali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 193
Ushirikina ulikuza hofu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 196
36 — Mguso wa Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 199
Imani hai huponya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 201
37 — Wainjilisti wa Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 202
Lazima tukabiliane na upinzani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 204
Tutafanyaje majaribu yatujiapo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 205
38 — Kristo na Wanafunzi Wapumzika . . . . . . . . . . . . . . . . . 208
Pumziko liliwaburudisha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 209
Usikose kuongea na Mungu kwa sababu ya shughuli nyingi mno . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 210
39 — "Wapeni Ninyi Chakula" . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 212
Fundisho muhimu la utunzaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 214
Namna tunavyorudia kutoamini kwa Adrea . . . . . . . . . . . . . 215
40 — Usiku Ziwani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 217

Dhoruba mioyoni mwa wanafunzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 219
Kujiinua na kuanguka kwa Petro . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 220
41 — Hatari Katika Galilaya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 222
Matumaini ya ubinafsi hayakutimiz.wa . . . . . . . . . . . . . . . . 223
Mbingu zinapoanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 225
Uzima katika Neno . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 226
Maneno ya Kristo yafarakisha wengi . . . . . . . . . . . . . . . . . 227
Kweli haikukubalika . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 228
Upendo katika mambo yote . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 229
42 — Kristo Atabiri Juu ya Maanguko . . . . . . . . . . . . . . . . . . 231
Ghadhabu ya Majasusi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 232
43 — Kristo Avunja Ubaguzi wa Mataifa . . . . . . . . . . . . . . . . 234
Imani katika Kristo ilimpatia hoja ya ajabu . . . . . . . . . . . . 236
44 — Ishara ya Kweli . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 238
Ukoo wa utawala watoa changamoto kwa Kristo . . . . . . . . 239
Ushahidi wa kweli, kwamba Kristo alitoka kwa Mungu . . . 240
Kujidanganya kwa ubinafsi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 241
45 — Kuonyeshwa Mbele Fumbo la Msalaba . . . . . . . . . . . . . 243
Kristo ndiye Mwamba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 245
Wanafunzi hawakutazamia juu ya kuja kwa msalaba . . . . . 246
Shetani alikuwa akijaribu kumfikia Kristo . . . . . . . . . . . . . 247
46 — Yesu Ageuka Sura . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 250
Petro alichanganyikiwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 251
47 — Kupingana na Roho za Mashetani . . . . . . . . . . . . . . . . . 254
Imani Hutuunganisha na Mbingu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 255
48 — Nani Aliye Mkubwa Zaidi? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 258
Mashindano ya Kushindania Ukuu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 259
Jambo lolote likoseshalo litupwe mbali . . . . . . . . . . . . . . . 262
Haja ya uangalifu wa huruma . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 263
49 — "Mtu Akiwa na Kiu, na Aje" . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 265
Nia ya ubinafsi yadhihirishwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 267
Wasiwasi wa watu ulitulizwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 268
50 — Katikati ya Mitego . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 270
Mawazo yaliyopotoka kuhusu Masihi na kuja kwake . . . . . 271
Uwezo wa kupambanua Wema na Ubaya . . . . . . . . . . . . . . 272
Yesu akishughulikia kesi ya uzinzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 273
51 — Nuru ya Uzima . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 276
Swali kuhusu kurithi Utume . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 278

Yesu hakuwa na dhambi . . . . . . . . . . 278
Mtu aliyezaliwa akiwa kipofu . . . . . . . . . . 280
Muujiza siku ya sabato . . . . . . . . . . 281
Mwujiza haukanushiki . . . . . . . . . . 282
52 — Mchungaji, Mungu . . . . . . . . . . 284
Wajibu wa Mchungaji Mwaminifu . . . . . . . . . . 285
Kwa nini Kondoo wake humfuata kwa furaha . . . . . . . . . . 286
Kristo bado ni Mchutigaji wetu binafsi . . . . . . . . . . 286
53 — Safari ya Mwisho Kutoka Galilaya . . . . . . . . . . 288
Wasamaria waliamini upendo wa Yesu . . . . . . . . . . 290
Waongon wa Dini waliwapotosha watu wengi kumkataa Kristo . . . . . . . . . . 290
Siri ya Uwezo wa Binafsi . . . . . . . . . . 291
54 — Msamaria Mwema . . . . . . . . . . 294
Ondoa Giza kwa kuruhusu Nuru . . . . . . . . . . 295
55 — Si Kujionyesha kwa Nje . . . . . . . . . . 298
56 — Upendo wa Yesu kwa Watoto . . . . . . . . . . 301
Kielelezo kwa akina Mama na Baba . . . . . . . . . . 302
57 — Kijana Tajiri Mtawala Amepungukiwa na jambo Moja 305
Je, Yesu alidai yasiyowezekana? . . . . . . . . . . 306
58 — Kufufuliwa kwa Lazaro . . . . . . . . . . 308
59 — Makuhani na Wakuu Wanaendelea na Njama Yao . . . . 315
Jinsi Roho Mtakatifu alivyojaribu kuwasaidia . . . . . . . . . . 316
60 — Cheo Kikuu Ni Kipi? . . . . . . . . . . 318
Ufalme wenye Kanuni Tofauti . . . . . . . . . . 319
61 — Mtu Mfupi Aliyekuwa Mashuhuri . . . . . . . . . . 321
62 — Mariamu Ampaka Yesu Mafuta . . . . . . . . . . 324
Kwa nini Yuda alichukizwa . . . . . . . . . . 325
Mariamu alitii maongozi ya Roho Mtakatifu . . . . . . . . . . 326
Yuda alitoka katika mwaliko huo kufanya njama ya kumsaliti Yesu . . . . . . . . . . 327
Yesu Kwa Kweli Hakuthaminiwa . . . . . . . . . . 328
Jinsi Mungu anavyotenda . . . . . . . . . . 329
Jinsi kiburi cha Simon kilivyoshushwa . . . . . . . . . . 331
63 — Yesu Atangazwa Kuwa Mfalme wa Israeli . . . . . . . . . . 333
Kwa nini Yesu alikubali hoi hoi hizo . . . . . . . . . . 334
Hakuna msururu wa maombolezo katika ushindi huu . . . . . 335
Yesu Atokwa Na Machozi . . . . . . . . . . 336

64 — Watu wa Kuangamia . . . . . 340
Kwa nini mtini huo ulilaaniwa . . . . . 341
65 — Hekalu Latakaswa Tena . . . . . 345
Makuhani na wakuu wanyamazishwa . . . . . 348
Jiwe geni lilokuwa mfano wa Kristo . . . . . 350
Jinsi ya kujengeka baada ya kuvunjika . . . . . 351
66 — Kristo Akabiliana na Adui Zake . . . . . 353
Ufufuo wa wafu, fundisho lenye utata . . . . . 354
Mawazo ya Mungu yakalibisha tabia . . . . . 354
67 — Yesu Azuru Hekalu Mara ya Mwisho . . . . . 358
Sadaka isiyo na Kifani ya Mjane Maskini . . . . . 360
68 — Wayunani Walipotaka "Kumwona Yesu" . . . . . 365
Sauti ya Mungu Ilisikika . . . . . 367
69 — Dalili za Kuja Kwa Kristo Mara ya Pili . . . . . 369
Karne za giza za mateso . . . . . 371
Ishara katika Mbingu . . . . . 372
Kuzidi kupita kiasi kwa uovu wa siku za mwisho. . . . . . 373
70 — Kristo Ashirikiana na Wenye Dhiki na Masikini . . . . . 376
Jinsi ya kutomjali Kristo . . . . . 378
71 — Mtumishi wa Watumishi . . . . . 380
Mwujiza mkuu wa Mioyo Iliyobadilika . . . . . 382
72 — Meza ya Bwana Yaanzishwa . . . . . 386
Kielelezo cha Kristo, hukataza kutenga . . . . . 388
Sababu za kuadhimisha meza ya Bwana . . . . . 389
73 — "Msifadhaike Mioyoni Mwenu" . . . . . 392
Faida ya ajabu ya Maombi . . . . . 393
Jinsi Roho Mtakatifu Anavyofanikisha Kazi va Kristo Kwa Ajili Yetu . . . . . 395
Kusudi Kuu la Roho Mtakatifu . . . . . 396
Dhambi ya Siri ya Petro . . . . . 398
74 — Pambano la Kutisha Katika Gethsemane . . . . . 403
Jaribu la Kutisha . . . . . 404
Yesu Alitamani Huruma za Kibinadamu . . . . . 405
Wakati Hali ya Baadaye ya Ulimwengu ilipotetemeka kwenye Mizani . . . . . 406
Jinsi Sala ya Kristo Ilivyojibiwa . . . . . 407
75 — Kesi Batili Dhidi ya Yesu . . . . . 410
Malaika Wangalifurahi Kumwokoa Kristo . . . . . 412

Kayafa Katibu Kuamini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 415
Udhalimu wa Hukumu ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 416
Petro Ashindwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 417
Jitihada Dhati Kutaka Kumhukumu Yesu . . . . . . . . . . . . . . . 418
76 — Jinsi Yuda Alivyopoteza Roho Yake . . . . . . . . . . . . . . . . 420
Kutenda Kinyume cha Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 421
Nafasi ya Mwisho ya yuda Kutubu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 422
Uchungu wa Majuto ya Yuda . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 423
77 — Kristo Ashtakiwa Mbele Ya Gavana Wa Kirumi . . . . . . 425
Pilato Asadiki kuna Njama . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 427
Yesu Ajaribu Kumwokoa Pilato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 427
Wengine walitetemeka Mbele ya Yesu . . . . . . . . . . . . . . . . . 430
Nafasi ya Mwisho ya Pilato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 431
Pilato Hakuweza Kuona Matokeo ya Baadaye . . . . . . . . . . . 432
Kuridhia Kwaelekeza Katika Maangamizi . . . . . . . . . . . . . . 433
Wema wa Yesu kwa Pilato . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 434
78 — Yesu Afa Juu Ya Kalwari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 437
Hukumu Pana Zaidi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 438
Uchungu Wa Mama Wa Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 439
Mwizi Mmoja Aliyesulibiwa Aamini . . . . . . . . . . . . . . . . . . 441
Mzigo wa Kuogofya Alioubeba Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . 444
Nafasi ya Mwisho Kuonyesha Huruma ya Kibinadamu . . . 445
Kristo Afa Kifo cha Ushindi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 446
79 — Jinsi Kifo Cha Kristo Kilivyomshinda Shetani . . . . . . . 448
Dunia Tamasha; Mbingu Watazamaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . 449
Jinsi Haki Ilivyochangamana na Rehema . . . . . . . . . . . . . . . 451
“Mtindo Mpya” wa Uongo wa Shetani . . . . . . . . . . . . . . . . . 452
80 — Yesu Apumzika Katika Kaburi La Yusufu . . . . . . . . . . . 454
Wanafunzi Wakata Tamaa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 456
Msaada Kutoka Sehemu Isiyotazamiwa . . . . . . . . . . . . . . . . 457
81 — “Bwana Amefufuka” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 459
Kayafa Ahimiza Udanganyifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 460
Dhamana ya Ufufuo Wetu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 461
Wengi Walifufuka Pamoja na Yesu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 461
82 — “Mama Unalilia Nini? . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 463
83 — Kutembea Kwenda Emau . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 467
Bila Kutambulika, Yesu Afafanua Maandiko . . . . . . . . . . . . 468
Mioyo Yao Ilivutiwa Kwa Mgeni Huyu . . . . . . . . . . . . . . . . 469

84 — Kristo Aliyefufuka Atokea . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 471
Tutawatambua Wapendwa Wetu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 472
Mungu Peke Yake Aweza Kusamehe . . . . . . . . . . . . . . . . . . 473
85 — Kando Ya Bahari Tena . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 475
Petro Alirudishwa Katika Hali ya Kutumainika . . . . . . . . . . 476
Kristo Aeleza Jinsi Petro Atakavyokufa . . . . . . . . . . . . . . . . 478
86 — "Enendeni . . . Mkawafanye Mataifa Yote" . . . . . . . . . . 480
Roho Mtakatifu Afanikisha Kazi Yao . . . . . . . . . . . . . . . . . . 482
Maisha ya Afya ni Sehemu ya Injili . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 483
Injili Ilivyo Na Uwezo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 484
87 — Kristo Aingia Mbinguni Kwa Ushindi . . . . . . . . . . . . . . 486
Alipokewa Kwa Magari ya Malaika . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 487
Hofu ya Wanafunzi Ilitoweka! . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 488

Tangu mwanzo wa historia ya ulimwengu watu wote, waume kwa wake, wamekuwa wakitazamia viongozi wakuu, majemadari, wenye maarifa, walimu na wataalam wakitumaini kuwa mtu fulani katika hawa ataweza kupata uvumbuzi wa matatizo ya maisha, na kupata dawa ya kuleta amani, afya, ya kuridhisha kila mtu.

Lakini ni Mtu mmoja tu aliyezaliwa katika nchi aliyeweza kutoa jawabu na dawa ya kutatua matatizo haya yanayowahangaisha wanadamu. Kuzaliwa kwake kulibadilisha si utaratibu wa ulimwengu tu, bali hata uhusiano wa mtu na mtu, na kwa wagonjwa na wenye dhiki. Aliwawia watu wengi kuwa tumaini lao na kuwaletea amani ya kweli, wale wanaofuata mafundisho yake.

Kitabu hiki maarufu kinachonunuliwa kwa wingi kinaeleza habari za Mtu huyu asiye wa kawaida kwamba ni nani na watu wote waume kwa wake wawezavyo kukutana naye leo.

# 1 — Kristo Kabla Hajaja Duniani [9]

Milele hata milele Yesu Kristo yuko katika umoja na Baba. Alikuwa sura ya Mungu, nuru ya upendo wa Mungu, ing'aayo mng'aro wa utukufu wake. Ili kuufunua upendo na utukufu wa Mungu, alikuja katika ulimwengu wetu wa giza. Kwa hiyo Ulitabiriwa kwamba, "Nao watamwita jina lake Immanuel, . . . yaani Mungu pamoja nasi." Mat. 1:23; Isaya 7:14.

Yesu alikuwa "Neno la Mungu" Mawazo ya Mungu yalisikika ndani yake. Ufunuo huu haukutolewa kwa wanadamu waliozaliwa katika dunia tu. Dunia yetu ndogo ndicho kitabu kidogo cha kusomwa na walimwengu. Waliokombolewa na wale wa dunia ambazo hazikuanguka watauona msalaba wa Kristo ambao ndio elimu yao na wimbo wao. Wataona kuwa utukufu ung'aao katika uso wa Yesu ni utukufu wa kujitoa kwake binafsi kwa upendo. Wataona kuwa kanuni ya mbinguni na ya duniani ni upendo wa kujitoa nafsi. Upendo huo "usiojitafutia mambo yake" hutokana na Mungu nao umedhihirishwa kwa njia ya Yesu, ambaye ni mpole na mnyenyekevu.

Mwanzo Kristo aliuweka msingi wa dunia. Mkono wake uliiweka dunia katika anga na kuyaweka maua katika nchi. Aliijaza nchi na uzuri, na anga na wingi wa nyimbo. Zaburi 65:6; 95:5. Juu ya vitu vyote aliandika upendo wa Baba.

Sasa dhambi imechafua kazi safi ya Mungu, hata hivyo maandiko hayo ya upendo wa Mungu yanadumu kuwako. Hakuna kitu cha ubinafsi kilichoko isipokuwa moyo wa binadamu ndiyo umejazwa na ubinafsi. Kila mti na kichaka na jani hutoa, vitu vya asili vya uhai ambavyo bila hivyo mwanadamu au mnyama hawezi kuishi, na mwanadamu na mnyama huhudumia miti na vichaka na majani.

Bahari hupokea maji katika vijito toka nchi, lakini hupata maji [10]
hayo ili kutoa. Mvuke unaopanda kutoka baharini huinyoshea nchi na kuiburudisha, ili iweze kutoa machipukizi. Malaika walioko kwenye utukufu furaha yao ni kutoa. Huleta nuru kutoka juu na kuwasaidia wanadamu wapate kumfuata Kristo.

Lakini tukiacha hayo yote, tunamwona Mungu ndani ya Yesu. Tunaona kuwa utukufu wa Mungu kutoa. "Siutafuti utukufu wangu wenyewe, ila utukufu wake aliyenituma" Maneno hayo aliyasema Yesu. Yohana 8:50; 7:18. Kristo alipokea kutoka kwa Mungu ili apate kutoa. Kwa njia ya Mwana, maisha ya Baba huwafurikia wote. Kwa njia ya Mwana huduma ya upendo hufurika kwa wote, hivyo kwa njia ya Kristo mzunguko wa manufaa ya Kristo hukamilika.

### Mbinguni Kanuni hii ilivunjika!

Dhambi ilianza katika ubinafsi. Lusifa, ambaye ni Kerubi wa kusitiri, alitamani kuwa wa kwanza mbinguni. Alitafuta kuwavuta viumbe wote wa mbinguni wamwache Muumba wao, akajitafutia heshima yake mwenyewe. Alimtupia Muumbaji malaumu maovu kwa uongo, aliwatatanisha malaika na kuwatia mashakani juu ya neno la Mungu. Wakaanza kuona mashaka kuhusu wema wa Mungu. Shetani akawashawishi wamheshimu Mungu kuwa ni mkatili asiye na huruma, wala hasamehi. Kwa njia hiyo aliwadanganya malaika. Kwa njia hiyo aliwadanganya wamdamu pia. Hivyo giza likaufunika ulimwengu.

Ulimwengu ulikaa gizani kwa kutomwelewa Mungu na tabia yake. Ili kurudisha ulimwengu kwa Mungu ilipasa nguvu ya Shetani ya kudanganya ivunjwe. Jambo hili lisingetendwa kwa kutumia nguvu. Mungu alitaka huduma ya upendo tu, na upendo usingepatikana kwa kutumia nguvu na uwezo. Upendo tu, ndiyo utawaamsha watu. Kumjua Mungu ni kumpenda. Tabia yake lazima ipambanuliwe na ile ya Shetani. Yule ajuaye urefu na kina cha upendo wa Mungu ndiye tu anaweza kufanya hivyo.

Mpango wa wokovu wetu haukuanzwa wakati ule Adamu alipoanguka dhambini. Ulikuwa mafunuo ya siri iliyofichika tangu zama za milele. Warumi 16:25. Ilikuwa ni ufunuo wa nambo Yaliyofichika kale na kale katika kiti cha enzi cha Mungu. Mungu aliiona dhambi ikitokea, naye akafanya matayarisho ya kuikabili dhambi hiyo. Aliahidi kumtoa mwana wake wa Pekee. Yohana 3:16.

Lusifa alikuwa amesema, "Nitapandisha kiti changu juu kupita
[11] nyota za Mungu . . . Nitafanana naye aliye juu". Lakini Kristo
ambaye ni sura ya Mungu alijitoa mwenyewe, akatwaa umbo la mwanadamu ambaye ni mtumwa, akiwa na umbo la mwanadamu

akajinyenyekeza mpaka kufa, naam kifo cha msalaba." Isaya 14:1, 3, 14; Wafilipi 2:6, 7.

### Toleo la Hiari

Yesu angeweza kuendelea kushikilia utukufu wa mbinguni. Lakini alichagua kushuka chini kutoka katika kiti chake cha enzi, ambako alitawala malimwengu yote, ili alete uzima kwa watu waliopotea.

Karibu miaka 2000 iliyopita sauti ilisikika mbinguni, ikisema, lakini mwili uliniwekea mimi .... Tazama nimekuja (katika gombo la chuo imeandikiwa) niyafanye mapenzi yako, Mungu.' Waebrania 10:5-7. Kristo alikuwa karibu kuja katika ulimwengu wetu, akiwa katika hali ya kibinadamu. Kama angekuja na utukufu wake, jinsi alivyokuwa hapo kwanza kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu huu, sisi tusingaliweza kuuvumilia utukufu huo, ila tungeliteketezwa tu. Utukufu wake ulifunikwa kabisa, na Uungu wake ukafichwa, akawa katika hali ya kibinadamu hasa.

Kusudi kubwa hili lilikuwa likionekana kwa njia ya mifano tu. Kichaka kilichowaka moto, ambapo Kristo alionekana kwa Musa, kilimwonyesha Mungu. Kichaka cha kawaida ambacho hakikuonekana na mvuto wowote, kilifunika ukuu wa Mungu. Mungu alifunua utukufu wake kwa Musa kwa njia ya kichaka kiwakacho moto, ili Musa apate kuona na kuishi, asife. Vivyo hivyo na nguzo ya wingu wakati wa mchana, na nguzo ya moto wakati wa usiku, zilifunika utukufu wa Mungu, ili wanadamu wapate kuangalia na kuishi, wasife. Hali kadhalika Kristo naye alikuja katika hali ya kibinadamu, ili watu wamwangalie, wasife. Alikuwa ni Mungu aliyekuja katika hali ya kibinadamu, ambaye utukufu wake ulifunikwa, ili awakaribie watu wenye matatizo, wenye dhiki. Katika safari ya Waisraeli ya kutangatanga jangwani mfano wa Mungu, ambao ni hema takatifu ulikuwa pamoja nao. Soma Kutoka 25:8. Hivyo Kristo aliweka hema lake kando ya mahema ya watu ili kuzoeana na sisi. "'Naye Neno akafanyika miwili, akakaa kwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee, atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.' Yoh. 1:14.

Tangu Yesu alipokuja na kukaa na sisi, kila mtu ambaye ni mzao wa Adamu atafahamu kuwa Mwumbaji wetu ni rafiki wa wenye

[12] dhambi. Kila aina ya mvuto wa Kimungu katika maisha ya Mwokozi alipokuwa hapa duniani, tunaona kuwa, “Mungu pamoja nasi”.

Shetani anaeleza sheria, au kanuni ya Mungu ya upendo kana kwamba ni kanuni ya ubinafsi. Asema, haiwezakani sisi kuishi. Anguko la mzazi wetu Adamu, Shetani alimlaumu Mungu kana kwamba ndiye aliyesababisha. Hivyo anawaongoza watu waone kuwa Mungu ndiye asili ya dhambi, masumbuko, na kifo. Yesu alikuja kusahihisha udanganyifu huo. Alivyoishi kama mmoja wetu aliwaonyesha jinsi ya kuishi kwa kutii amri za Mungu. Kwa hiyo alitwika hali yetu yote na kuishi maisha yetu kamili. “Alifananishwa na ndugu zake katika mambo yote.” Waebrania 2:17. Kama tungepaswa kukabili jambo lolote ambalo Yesu hakulipitia ndipo Shetani angesema kuwa uwezo wa Mungu hautoshi kutusaidia. Kwa hiyo “Yesu alijaribiwa katika mambo yote, kama sisi.’ Waebrania 4:15. Alishinda kila jambo ambalo sisi tungekutana nalo. Hakutumia uwezo mwingine ambao sisi hatuwezi kuupata. Kwa kila jaribu alilishinda kwa uwezo aliopata kutoka kwa Mungu. Hakulalamikia kanuni ya Mungu kamwe. Na maisha yake yashuhudia kuwa hata sisi tunaweza kushinda tu kama yeye, kwa uwezo ule ule; na kuiti sheria ya Mungu.

Katika hali ya ubinadamu, Kristo aligusa, ubinadamu; na katika hali ya Uungu, alishikilia kiti cha enzi, cha Mungu. Akiwa kama binadamu alituwekea kielelezo cha utii; na akiwa Mungu Mwana, alitupa uwezo wa kutii. Kwetu alisema, “Nimepewa uwezo wote mbinguni na duniani pia.’ Mat. 28:18. ‘Mungu pamoja nasi’, ndio uhakika wa kutuokoa dhambini, yaani uhakika wa uwezo wa kutii kanuni za mbinguni.

Kristo alitufunulia tabia iliyo tofauti na ile ya Shetani. “Alipoonekana na hali ya ubinadamu, alijinyenyekeza, akawa mtii hata kufa, kifo cha msalaba.” Wafilipi 2:8. Kristo alitwaa hali ya mtumwa, akatoa dhabihu, na yeye mwenyewe akiwa ndiye Kuhani, na dhabihu hiyo ni mwili wake mwenyewe. “Alichubuliwa kwa sababu ya maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake.” Isaya 53:5.

## Alitendewa kama tulivyostahili

Kristo alitendewa jinsi tulivyostahili sisi, ili sisi tutendewe kama alivyostahili Yeye. Alihukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu, akashiriki adhabu yetu ili sisi tuhesabiwe haki yake, ambayo sisi hatuna ushirika nayo. Alikufa kifo chetu, ili sisi tupate uzima wake. "Kwa kupigwa kwake tumepona." Isaya 53:5.

Lilikuwa kusudi la Shetani kuleta utengano wa milele baina [13]
ya Mungu na watu, lakini kwa kutwaa hali ya kibinadamu, Kristo Mwokozi wetu alijiungamanisha na watu kwa kifungo kisichoweza kukatika kamwe.' Mungu aliupend aulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee' Yohana 3:16. Alimtoa si kwa kutufia tu, bali kwa kujiungamanisha na ubinadamu milele.

"Kwa ajili yetu amezaliwa mtoto, ukuu utakuwa begani mwake." Mungu amejitwalia ubinadamu kwa njia ya Mwanawake, naye amechukua hali hiyo mpaka katika mbingu za juu kabisa. "Mwana wa binadamu" ataitwa wa ajabu, Mshauri wa ajabu, Mungu hodari, Baba wa milele, Mkuu wa amani.' Isaya 9:6. Yeye aliye mtakatifu, asiyekuwa na doa lolote, asiyechafu-liwa na kitu chochote, ajitengaye na dhambi, haoni haya kutuita sisi ndugu zake. Waebrania 7:26; 2:11. Mbinguni kunahusiana na ubinadamu, na ubinadamu unakumbatiwa na mbingu kwa upendo.

[14] ## 2 — Watu Ambao Wangalipokea

Kwa muda wa miaka elfu moja na zaidi, Wayahudi walikuwa wakimtazamia Yesu aje. Walakini alipokuja hawakumfahamu. Hawakumwona kuwa anao uzuri wowote hata wamtamani. Isaya 53:2. "Alikuja kwa watu wake, na watu wake hawakumpokea." Yohana 1:11.

Mungu aliwachagua Waisraeli kati ya mataifa, ili wahifadhi mifano na unabii vinavyoelekeza kuja kwa Mwokozi ulimwenguni. Waebrania walipaswa kumdhihirisha Mungu katika mataifa. Katika kumwita Abrahamu, Bwana alisema, "Katika wewe jamaa zote za dunia zitabarikiwa." Mwanzo 12:3. Bwana alitangaza kwa njia ya nabii Isaya kwa watu wote." Isaya 56:7.

Lakini Waisraeli walikazana na ufahari wa dunia tu, wakafuata njia za mataifa ambayo ni makafiri. Mungu aliwatumia ujumbe wa maonyo kwa njia ya manabii, lakini ilikuwa kazi bure. kila mara waliposhtushwa na kurudi kwa Mungu muda mfupi, baadaye waliasi vibaya tena.

Kama Waisraeli wangalikuwa waaminifu kwa Mungu, angaliwafanya wawe wakuu kuliko mataifa yote. Mataifa ambayo yangesikia amri hizi wangalisema, "Kweli taifa hili kubwa, ni taifa lenye hekima na lenye ufahamu." Torati 26:19; 4:6.

Lakini kwa ajili ya kutokuwa waaminifu kwao, makusudi ya Mungu kwao yaligeuka kuwa taabu na mateso. Walipelekwa Babeli, na kutawanywa katika mataifa yote. Walipoomboleza kwa ajili ya kuteketezwa kwa hekalu, kwa njia yao elimu ya Mungu iliwafikia mataifa makafiri. Ibada za kikafiri ziliachwa na kuigiza zile za Mungu. Waebrania waliwaonyesha njia iliyoagizwa na Mungu. Wenye elimu wengi walijifunza njia za Mungu, na kuona ahadi za kuja kwa Mkombozi.

Watu wengi katika mataifa hayo walikotawanywa, walipoinuka
[15] kuushambulia ukweli, watu hawa waaminifu walifika mbele ya
wafalme na watawala, ili kuifikisha nuru ya kweli. Kwa njia hii

wafalme wakuu walimkiri Mungu na uweza wake, ambaye watumwa wa Kiebrania humwabudu.

Wakati wa karne zilizofuata kutekwa kwenda Babeli Waisraeli walipona kuabudu sanamu, na imani yao iliimarika, wakawa watiifu kwa Mungu. Lakini wingi wa watu hali ya ubinafsi ilidumu kuwatawala. Walimtumikia Mungu kama njia ya kujipatia ukuu wa taifa. Hawakuwa nuru ya ulimwengu tena, bali walijitenga na kujifungua ili wasipate majaribu. Mungu aliwazuia kuungana na mataifa ili wasipotoshwe. Lakini fundisho hili lilipotoshwa kabisa.

Walidhani ni kujenga ukuta imara kati yao na wakafiri. Wayahudi walikuwa na wivu, kwamba Bwana asiwahurumie mataifa kama wao.

## Jinsi walivyopotosha Huduma ya Hema Takatifu

Baada ya kurudi kutoka katika utumwa huko Babeli walijenga masinagogi katika nchi yote. Katika masinagogi hayo sheria ya Mungu ilifundishwa na Makuhani na waandishi. Shule za kufunza mambo ya haki zilifunguliwa. Lakini wakati wa utumwa huko Babeli watu wengi waliambukizwa desturi za kikafiri, nao waliingiza desturi hizi katika huduma za dini.

Kanuni za ibada na huduma zake zilikuwa zimeanzishwa na Kristo mwenyewe. Kanuni hizo zilikuwa zikimwonyesha Yeye na kufanya huduma kuwa maarufu. Lakini Wayahudi walipoteza maana yake ya kiroho, wakawa wakijiendeshea ibada tu isiyokuwa na maana yoyote, huku wakiamini kafara na kushika kanuni tu, kana kwamba watapata faida kwavyo. Badala ya kumwangalia yule anayeonyeshwa na vitu hivi, wao wakaamini vitu hivi tu. Wakajitungia kanuni zaidi ili kufanya mambo yawe bora. Kadiri shughuli hiyo ilivyokuwa, ndivyo upendo kwa Mungu ulivyopungua.

Watu waliotumainia mambo hayo zaidi, waliona kuwa hakuna utulivu mioyoni mwao. Na Shetani akawakatisha tamaa kabisa, hata wakawa na mawazo yaliyo kinyume cha Mungu, mpaka imani ya Waisraeli ikawa aibu tupu. Shetani alitaka kuwaaminisha watu kuwa matakwa ya Mungu hayawezekani kutii. Akasema kuwa, hata Waisraeli wameshindwa kuyashika, akatangaza kuwa, hata hawakushika sheria ya Mungu.

## Kutazamia Masihi wa Uongo

Wayahudi hawakufahamu majilio na kazi ya Masihi.
[16] Hawakutafuta ukombozi kutoka dhambini, ila walitafuta kuokolewa na utawala wa Warumi. Walitazamia Masihi atakayewainua na kuwafanya kuwa taifa mashuhuri. Hivyo ndivyo njia iliandaliwa ya kumkataa Mwokozi.

Wakati wa kuzaliwa kwa Kristo, taifa la Wayahudi lilikuwa mikononi mwa mabwana wageni, nao walikuwa wakihangaika katika mashindano ya ndani kwa ndani. Warumi waliowatawala, walimwongoa kuhani mkuu, na cheo chake kilishindaniwa kwa rushwa na mara kwa mara kwa mauaji. Hivyo kazi ya ukuhani ilizidi kuharibika zaidi na zaidi. Watu walikuwa katika hali ngumu ya ukorofi, huku wakitozwa kodi nzito na Warumi. Taifa zima lilikuwa katika msukosuko hasa, nchi ilijaa na kutokuridhika, choyo, uasi, ufedhuli. Kila mahali kulikuwa na hali ya ubariki kiroho. Katika giza lao na mateso yao, walitamani kuwa na mtu atakayewaondolea hali hiyo na kumsimamisha mfalme wa Israeli. Kwa hiyo waliutafsiri kufuatana na hali yao ya ubinadamu.

## 3 — Dhambi ya Binadamu na “Utimilifu wa Wakati” [17]

Adamu na Hawa waliposikia ahadi ya Mwokozi atakayekuja, walimtazamia kwa upesi sana. Walimpata mtoto wao wa kwanza, wakitumaini kuwa huenda yeye ndiye Mkombozi. Lakini hao waliopata ahadi ya Mkombozi, walikufa bila kuona matimizo ya ahadi hiyo. Ahadi ilirudiwa kusemwa tena kwa wazee na manabii, ili kuifanya upya. Hata hivyo hakuja. Unabii wa Danieli ulitaja wakati wa kuja kwake, lakini ujumbe wake haukutafsiriwa wote vyema. Karne na karne zilipita. Na mkono wa mtesi ulizidi kuwa mzito kwa Waisraeli, na watu wengi walikuwa tayari kusema, “Siku zinakawia, na njozi haitimizwi.” Ezekieli 12:22.

Lakini kama nyota katika mzunguko wake, kama ilivyoamuriwa, kusudi la Mungu halijui kuharakisha, wala kuchelewa. Katika baraza la mbinguni, kuja kwa Kristo kuliamuliwa na kupangwa hasa. Wakati saa kuwa ya mbinguni itakapotima, Yesu, ambaye ni Masihi atazaliwa katika Bethlehemu.

“Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwana wake.” Wagalatia 4:4. Ulimwengu ulikuwa tayari kwa kuja kwa Mkombozi. Mataifa yalikuwa yameunganika chini ya serikali moja. Lugha moja ilijulikana kila mahali. Wayahudi wote toka kila mahali walikusanyika Yerusalemi kwa sikukuu yao ya kila mwaka.

Watu hawa waliporudi mahali pa mtawanyiko wao walipeleka habari za kuzaliwa kwa Masihi ambaye amekuja.

Desturi ya kikafiri ilikuwa ikitoweka katika watu. Watu walitamani dini itakayowaridhisha. Watu waliokuwa wakitaka kujua zaidi, walikuwa wakimtafuta Mungu, ili wapate kuelewa yatakayotokea, baada ya kufa.

### Wengi walitamani Mkombozi [18]

Imani ya Wayahudi ilififia sana, na matumaini yao yalikoma, hayakuweza kuwamulikia hali ya siku za mbele. Kwa wengi wao,

kifo kilikuwa tukio la siri. Mbele yao waliona giza tu na wasiwasi. watu walikaa tu chini wakiwa na wasiwasi bila hakika ya mambo yajayo. Walingojea kwa hamu kuu kumwona Mkombozi atakayewaletea ufumbuzi wa mambo yajayo.

Nje ya nchi ya Uyahudi kulikuwako na watu waliokuwa wakitafuta ukweli wa mambo. Kwa watu kama hao, walivuviwa Roho Mtakatifu. Maneno ya unabii yaliwaamsha; wakawa na tumaini la mambo ya mbele. Hawa walikuwa watu wa mataifa, siyo Wayahudi.

Kwa miaka mamia Maandiko Matakarifu yalitafsiriwa katika lugha ya Kiyunani (Kigiriki), ambayo ilikuwa ikizungumzwa katika dola ya Kirumi. Wayahudi walikuwa wametawanyika kila mahali, kwa kutekwa, na matumaini yao juu ya Masihi ajaye, yaliaminiwa na baadhi ya watu wa mataifa pia. Katika watu ambao waliona vibaya kwa jinsi Wayahudi walivyoiga desturi za kikafiri, walikuwa wakichunguza Maaandiko kuhusu kuja kwa Masihi kuliko walimu wa Kiisraeli.

Miongoni mwa watu waliotumaini kuwa Masihi atawaokoa toka dhambini, walichunguza kwa makini kuona asili ya mafanikio ya Wayahudi. Lakini Wayahudi walikazana tu kujitenga na mataifa mengine, wala hawakutaka kuwajulisha elimu ya Mungu, jinsi walivyoipokea wao. Unabii ulielezea kwa njia ya alama ambazo zote zilikuwa zinaelekeza kwa yule ajaye, yaani Masihi. Mafundisho lazima yatolewe kwa lugha ya kibinadamu. Kristo ajaye lazima aeleze mafundisho yaliyo dhahiri, yenye kufahamika wazi ili kupambanua makapi na ngano, ambayo yalivuruga mambo, na kuyafanya kuwa hayana maana.

Baadhi ya Wayahudi walisimama imara na kuyatunza maagizo ya Mungu kamili. Hawa waliimarisha imani yao kwa njia ya kusoma maneno yaliyosemwa na Musa, kuwa; "Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu kama mimi; msikieni katika mambo yote atakayonena nanyi." Matendo 3:22. Walisoma jinsi Mungu atakavyomtia mafuta mtu, "ahubiri habari njema kwa wanyenyekevu, "kufunguliwa kwa; kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa." Isaya 61:1, 2. "Atafanya hukumu katika nchi, visiwa vitangojea sheria yake." Isaya 42:4. Mataifa yataijilia nuru yake, na wafalme wataujilia mwanga wa kuzuka kwake." Isaya 60:3.

[19] Maneno ya Yakobo ya wakati akifa yaliwapa tumaini. "Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, wala mfanya sheria katika miguu

yake, hata Shillo aje." Mwanzo 49:10. Taabu ya Israeli ilishuhudia kuwa Masihi anakaribia kuja. Kulikuwa na kutazamia kwingi sana kuja kwa Mkuu atakayekuja kuusimamisha ufalme katika Israeli, naye atakuja kama Mkombozi wa taifa.

### Jinsi Shetani alivyokuwa karibu kufaulu

Utimilifu wa wakati umekuja. Ubinafsi umedhiliwa kwa muda mrefu, kwa ajili ya maasi, ya kukutazamia kuja kwa Mkombozi. Shetani alikuwa akijitahidi kufanya shimo la kuvukia liwe refu zaidi, ili isiwezekane kuvuka kutoka duniani hata mbinguni. Amewaingiza watu dhambini. Ilikuwa nia yake kufanya uvumilivu wa Mungu ukome, hata awaachilie watu mbali katika mikono ya Shetani.

Juhudi ya Shetani ya kuutwaa ulimwengu karibu ilifaulu. Ni kweli kwamba katika kila kizazi, hata katika mataifa, kulikuwa na watu wenye kumcha Mungu. Lakini watu hawa walichukiwa sana. Wengi wao wlaiteseka sana kiasi cha kuuawa. Giza hilo ambalo Shetani alilitia ulimwenguni lilizidi kuwa kubwa zaidi.

Shetani alishinda vita katika kuwapotosha Waisraeli, wasiwe na imani. Wakafiri walikosa wa kuwafundisha, kwa hiyo wakazidi kuharibika. Kosa ni la Waisraeli. Kanuni ya kutegemea matendo mema ili yampatie mtu nafuu, ni kanuni ya dini za kikafiri. Kanuni hiyo iliingia hata kwa Waisraeli, ikawa ndiyo dini yao.

Wayahudi wameudanganya ulimwengu kwa kuwapa dini ya kuiga, ambayo ni potofu. Wamekataa kujitoa kwa Mungu kamili, ili wawape walimwengu wkovu, badala yake wamekuwa vyombo vya Shetani kuwaharibu. Watu ambao waliitwa na Mungu wawe nguzo na msingi imara, wamegeuka kuwa watenda kazi wa Shetani, wakiukosesha ulimwengu, uone kwamba mungu hana haki, ila ni mdanganyifu. Makuhani hekaluni walipotosha kazi ya ukuhani. Utaratibu uliowekwa na Mungu mwenyewe, ukageuzwa kuharibu watu na kuwapofusha tu. Mungu hana la kumfanyia mtu zaidi kwa njia hii.

### Mungu auhurumia ulimwengu uliopotea

Vitu vyote vya kumharibu mtu vimetumiwa na Shetani, na Mwana wa Mungu akiutazama ulimwengu kwa huruma, akaona

jinsi watu wamekuwa mateka ya Shetani kwa ukatili. Wameharigika
[20] na kudanganyika, wamo katika msafara wa dhiki wakienda kifoni, wala hawana tumaini wanauendea usiku ambao haupambazuki.

Miili ya binadamu imekuwa makao ya mashetani. Ufahamu, na nguvu za kufikiri, vyote vimepotoka, kama mtu aliyepagawa. Chapa ya Shetani ilichapika katika miili ya watu. Mwokozi wa ulimwengu hushangaa kiasi gani aonapo hayo yote!

Dhambi zimekuwa sayansi, na maovu yamekuwa sehemu ya dini. Uasi na ukatili vinashindana na mbingu. Dunia zisizofanya dhambi huangalia na kuona jinsi Mungu atakavyowafutilia mbali watu wa ulimwengu. Na kama akifanya hivyo, Shetani yuko tayari kuendeleza maazimio yake hata mbinguni. Alikwisha kutamka kwamba serikali ya Mungu ina walakini. Kama ulimwengu ungaliangamizwa, Shetani angemlaumu Mungu zaidi na kuongeza maasi yake katika dunia nyingine.

Lakini badala ya kuufutilia mbali ulimwengu Mungu alimtuma Mwana wake ili kuuokoa. Njia ya kuuokoa ilitayarishwa. Utimilifu wa wakati ulipofika, nao ulifika. Mungu akaja ulimwenguni. akamwaga ulimwenguni gharika ya neema ya kuponya, ambayo haitamalizika kamwe; mpaka mpango wa wokovu utimie. Yesu alikuja ili kurudisha sura ya Muumbaji, na kuwafukuzailia mbali mashetani waliojidai kutawala, na kutuinua juu kutoka mavumbini, na kutengeneza tabia zetu zifanane na tabia yake.

# 4 — Kuzaliwa Zizini [21]

Mfalme wa utukufu alishuka chini sana ili kuwa mwanadamu. Utukufu wake ulifunikwa kabisa bila kuonekana. Yesu alikusudia kwamba, pasiwepo kitu chochote kwake chenye kuwavutia watu, ili wamwendee. Watu wenye kumfuata wavutwe kwake na usafi na ukweli wa ujumbe wa Injili tu. Alitaka watu wamwamini kwa ushahidi wa neno la Mungu peke yake.

Malaika waliangalia ili waone jinsi watu wa Mung wampokeavyo Mwana wake; aliye na hali ya ubinadamu. Katika nchi ambapo nuru ya unabii imeng'aa malaika wlaikuja. Walikuja bila kuonekana katika Yerusalemi, na kuhudumu katika nyumba ya Mungu.

Kuja kwa Kristo kulikuwa kumetangazwa kwa Zekaria, aliyekuwa nabii akihudumu katika madhabahu. Tayari mtangulizi wa Kristo alikuwa amezaliwa, na habari za kuzaliwa kwake na kazi yake ilikuwa imetangazwa. Walakini Yerusalemi haikuwa na habari, wala haikuwa tayari kumpokea Mkombozi. Mungu aliwaita Wayahudi wapate kueneza habari za kuja kwa kristo, kwamba atazaliwa katika mlango wa Daudi, walakini hawakuwa na habari kwamba kuja kwake kumekaribia.

Katika hekalu dhabihu zilizokuwa zikitolewa asubuhi na jioni, zilielekeza juu ya Mwana-kondoo wa Mungu, hata hivyo hakuna matayarisho yoyote yaliyofanywa kwa kumpokea. Makuhani na walimu, walikariri sala, ambazo hazina maana yoyote kila siku, na kufanya huduma na kushika kawaida za ibada, lakini bila kutayarisha matokeo ya kuzaliwa Kristo. Hali ya usingizi ile ile ilifunika nchi nzima ya Israeli. Hali ya ubinafsi na kushughulikia mambo ya ulimwengu, vilifunga miyo ya watu wasiweze kusikia furaha iliyokuwa ikifurahiwa na mbingu. Watu wachache tu walitamani kuona mambo yasiyoonekana.

Malaika walifuatana na Yusufu na Mariamu katika safari ya [22]
kutoka Nazareth kwenda katika mji wa Daudi. Amri ya Rumi ya kuwaandikisha watu wote ilikuwa imetangazwa katika dola yake

yote mpaka Galilaya. Mfalme Augustus akakwa mjumbe wa Mungu kumleta mama wa Yesu huko Bethlehemu. Alikuwa wa ukoo wa Daudi; na Mwana wa Daudi lazima azaliwe katika mji wa Daudi. Nabii alisema, "Kwako (Bethlehemu), atakuja . . . mtawala wa Israeli; ambaye kwenda kwake kumekuwa tangu zamani za kale tangu milele." Mika 5:2.

Lakini katiia mji huu wa utawala, Yusufu na Mariamu hawakujulikana, wala kujali wa na mtu. Wakiwa wamechoka, na hawana mahali pa kukaribishwa, Yusufu na mkewe walijikokota wakipita katika njia nyembamba mpaka upande wa mwisho wa mji huko mashariki, wasione mahali pa kulala usiku. katika nyumba ya wageni hapakuwako nafasi. Katika banda la wanyama ndipo wlaipata nafasi baada ya kuhangaika sana. Na hapo ndipo Mwokozi alizaliwa.

Habari hii iliifurahisha mbingu mno. Watakatifu kutoka katika dunia zisizoanguka walivutwa kuja katika dunia yetu. Katika vilima vya Bethlehemu lilikuja jeshi la malaika. Lilikuwa linangoja ishara ili lipate kutangaza habari hii ya kuzaliwa kwa Masihi katika ulimwengu.

Waongozi wa Israeli wangalijiunga katika furaha hii pia. Lakini walipitwa bila habari yoyote. Wale waliokuwa wakitafuta nuru na kuiamini kwa furaha, nuru ya urukufu kutoka kaika kiti cha enzi cha Mungu iliwang'aria. Soma Isaya 44:3; Zaburi 112:4.

## Wachungaji wa kondoo tu, walijali

Katika uwanda ambapo Daudi alikuwa akichungia kondoo, wachungaji waliokuwa wakikehsa usiku, waliongea habari ya ahadi ya Mwokozi, wakaomba sana ili apate kuja. Ndipo malaika wa Bwana akawajia, akawaambia, "Msiogope, maana nawaletea habari njema, itakayokuwa furaha kwa watu wote. Maana amezaliwa Mwokozi kwa ajili yeny leo katika mji wa Daudi, naye ndiye Yesu Kristo Bwana."

Kwa maneno haya, njozi ya utukufu ikajaza mawazo ya wachungaji waliokuwa wakisikiliza. Mkombozi amekuja! Kuja kwake kutakuwa na uwezo, na ukuu, na ushindi. lakini malaika waliwatayarisha ili wamtambue Mwokozi katika mahali hafifu alikozaliwa. "Mtamkuta mtoto amevikwa nguo za kitoto, amelazwa horini."

[23] Mjumbe wa mbinguni ametuliza mioyo yao, na hofu zao. Ame-

waonyesha namna ya kumwona yesu. amewaonyesha muda wa kumfahamu. Halafu uwanda wote ukaangazwa na nuru ya majeshi ya Mungu. Nchi ikanyamaza kimya, na mbingu ikatulia ili kusikiliza wimbo:"Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

Laiti watu wangeweza kuuelewa wimbo huo leo! Kama ungeimbika ilivyo ungeweza kuenea mpaka mwisho wa wakati, na ungetoa mwangwi wake mpaka kona za nchi.

[24] ## 5 — Yusufu na Mariamu Wamweka Wakfu Yesu

Wakati Yesu alipotimiza siku arobaini baada ya kuzaliwa kwake, Mariamu na Yusufu walikwenda Yerusalemu ili kumkabidhi kwa Bwana, na kutoa sadaka. Jinsi Kristo alivyokuwa badala ya binadamu lazima aambatane na sheria katika mambo yote. Alikuwa ametahiriwa tayari, kuambatana na sheria.

Kama sadaka ya mama, kulitakiwa kutolewa kondoo wa kuteketezwa, au hua kwa ajili ya sadaka. Sadaka hizi zingekuwa hazina kasoro, maana zinamwakilisha Kristo. Yeye alikuwa 'Mwana kondoo asiyekuwa na mawaa." 1 Petro 1:19. Alikuwa kielelezo cha jinsi Mungu alivyokusudia ubinadamu kuwa kufuatana na utii kwa sheria yake.

Kuweka wakfu mzaliwa' wa kwanza, kulianza zamani sana. Mungu aliahidi kumtoa mzaliwa wa kwanza ili kuokoa ulimwengu, wenye dhambi. Tendo hili ilipaswa kuheshimiwa na kila mtu kwa ajili ya kumtoa mzaliwa wa kwanza. Naye angekuwa kuhani; kama mfano wa Kristo kati ya watu.

Jambo hili lilielekea kwa Kristo wima namna gani! Lakini makuhani hawakuona maana yake, ni kama wamezuiwa na pazia. Kila siku kuhani alifanya mfano huu bila kujali wazazi, labda wawe ni matajiri au wakuu. Yusufu na Mariamu walikuwa maskini, na kuhani aliwaona kama watu wa Galilaya tu, wamevaa mavazi ya kawaida.

Kuhani alimshika mtoto mikononi mwake na kumwinua madhabahuni. Baada ya kumrudisha kwa mama yake, aliandika jina, "Yesu" katika orodha yake. Hakufikiri kuwa mtoto anayemwandika liikuwa Mtukufu wa mbinguni, aliye asili ya ukuu wa Wayahudi.

Mtoto huyu ndiye aliyesema kwa Musa, "Mimi Ndiye."
[25] Aliyewaongoza Waisraeli kama wingu na kama nguzo ya moto. Ndiye alikuwa Tunu ya watu wote, shina la Daudi, mwenye kung'aa, Nyota ya asubuhi. Mtoto mchanga huyu ndiye alikuwa tumaini la wanadamu walioanguka. Atalipa kafara ili kuuokoa ulimwengu wote.

Lakini ingawa kuhani hakuona kitu chochote kwake kilichomvutia, wakati huo hakupita bila kumtambua Kristo. Kulikuwa na mtu katika Yerusalemu jina lake Simeoni . . . Roho Mtakatifu alikuwa pamoja naye. Naye alifunuliwa na Roho Mtakatifu kwamba, hatakufa, kabla hajamwona Kristo.

### Mheshimiwa Simeoni Alimtambua Yesu

Simeoni alipoingia hekaluni, alijisikia kikamilifu kwamba, mtoto aliyetolewa na kuwekwa wakfu kwa Bwana, ndiye aliyeahidiwa na kungojewa kwa muda mrefu. Kuhani ambaye alipigwa na bumbuazi walishituka na kuingiwa na kiwewe cha furaha. Alimchukua mtoto mkononi mwake, hali akijaa furaha kubwa sana, ambavyo hajapata kuwa nayo. Alipomwinua mtoto, ambaye ni Mwokozi kuelekea mbinguni, alisema, Bwana, sasa mtumshi wako, na alale kwa furaha na amani, kama neno lako lilivyo: maana macho yangu yameona wokovu wako, uliowaandalia watu wote, ambayo ni nuru ya kuwaangazia watu ambao ni wa mataifa, na utukufu wako kwa watu wako Israel.

Wakati Yusufu na Mariamu walipokuwa wamesimama hali wakiyastaajabia maneno hayo, alimwambia Mariamu, "Angalia, mtoto huyu amewekwa ili kuwaangusha na kuwainua watu wengi katika Israeli na ishara inenwayo (Wewe upanga utakupasua moyo wako pia) ili mawazo ya wengi yapate kufunuliwa.

Vile vile Anna, nabii mke aliingia, akayaunga mkono maneno ya Simeoni. Uso wake uling'aa kwa utukufu, akatoa shukrani kwamba, ameruhusiwa kumwona Kristo Bwana.

Watu hawa wanyenyekevu, wamejifunza unabii. Lakini makuhani walidhani kuwa walikuwa na unabii wa thamani, kumbe hawakutembea katika njia ya Bwana. Macho yao hayakufunguliwa ili waone nuru ya maisha.

Hivyo ndivyo ilivyo hata leo. Wakaaji wa mbinguni wameleta mambo yote, ambayo wenye dini wangaliongozwa na waongozi wao kuyafuata. Watu wanamkiri Kristo katika historia. Lakini Kristo kuhusu ufukara na mateso, hawamkubali. Inakuwa hali ile ile iliyokuwako katika muda ule wa miaka elfu mbili iliyopita.

Mariamu alipokuwa akimwangalia mtoto mchanga mikononi [26]
mwake, na kuyakumbuka maneno ya wachungaji, alikuwa na tu-

maini la hakika. Maneno ya Simeoni yalimkumbusha maneno ya nabii Isaya: Watu waliokaa gizani, wameona nuru kuu nao wanaokaa katika uvuli wa mauti, nuru imewazukia. "Tumezaliwa mtoto, nasi tumepewa mtoto wa kiume, na ukuu utakuwa begani mwake, jina lake ataitwa Wa ajabu, mshauri wa ajabu, Mungu hodari, Baba wa milele, Mkuu wa amani." Isaya 9:2-6.

### Uchungu ambao Mama wa Kristo hana budi kuufahamu

Hata hivyo Mariamu hakuelewa kazi ya Kristo. Simeoni ametabiri kwamba yeye ni nuru ya kuwaangaza mataifa; na malaika walitangaza kwamba kuzaliwa kwa Kristo kutawafurahisha mataifa. Mungu alikusudia kuwa yeye atakuwa Mwokozi wa ulimwengu. Lakini muda mrefu utapita bila watu kufahamu hivyo, hata mama wa Yesu pia.

Mariamu hakuona ubatizo wa mateso, ambao Masihi mwenye kutawala kiti cha enzi cha Daudi atakaobatizwa. Katika maneno ya Simeoni kwa Mariamu: "Upanga utakuingia rohoni mwako pia." Kwa rehema za Mungu, alimjulisha Mariamu, mama wa Yesu, matatizo ambayo ameanza kuyaona tayari.

Simeoni alisema, "Tazama, mtoto huyu amewekwa ili kuwaangusha, na kuwainua wengi wa Israeli. Wataanguka na kuinuka tena. Hatuna budi kuanguka juu ya Mwamba wa kuvunjika kabla hatujainuliwa katika Kristo. Nafsi lazima kuondolewa kabisa. Wayahudi hawataipokea heshima itokanayo na unyenyekevu. Kwa hiyo hawatampokea Mwokozi.

Kwamba mawazo ya wengi yapate kufunuliwa. Katika nuru ya maisha ya Mwokozi, watu wote, tangu Mwumbaji, hata mkuu wa giza wafunuliwe. Shetani amemtaja Mungu kuwa ni wa binafsi. Lakini kipawa cha kumtoa Kristo kilionyesha kuwa, ingawa Mungu huchukia dhambi, ni imara kuliko mauti. Kule kuchukua ukombozi wetu, Mungu hatazuia chochote mpaka ukombozi utimilike. Utajiri wote wa ulimwengu amenipa Kristo. Mungu husema, "Tumia utajiri wote, niliokupa ili kuwavutia watu wajue kuwa hakuna upendo mkuu kuliko huu niliowapeni. Furaha kamili itapatikana katika mimi tu.

### Jinsi kila mtu atakavyo jihukumu

Pale katika msalaba wa Kalwari, upendo na ubinafsi ulisimama [27] uso kwa uso. Yesu aliishi tu kuwabariki na kuwafariji, na kule kumwua, Shetani alidhihirisha chuki yake kwa Mungu. Asili ya uasi wake ni kumwondoa Mungu, na kumharibu Mwana wa Mungu.

Kwa maisha ya kifo cha Kristo, mawazo ya wanadamu yalipambanuliwa. Maisha ya Yesu yalikuwa ni wito wa kujitoa nafsi na kushirikiana katika taabu. Wote waliomsikia kwa Roho Mtakatifu walivutwa kwake. Wanaoabudu nafsi na wa utawala wa Shetani. Katika mtazamo wao kwa Kristo, watajidhihirisha wanakosimama. Kwa njia hii kila mtu atajihukumu mwenyewe.

Siku ya mwisho ya hukumu, msalaba utasimamishwa, na kuhusika kwake kwa watu kutaonekana kwa kila mtu. Kabla njozi ya msalaba wa Kalwari na yule aliyesulubishwa kwake, wenye dhambi watasimama, huku wamehukumiwa tayari. Watu wataona matokeo ya uchaguzi wao. Kila swali kuhusu mashindano haya litakuwa dhahiri. Mungu hataonekana na lawama yoyote kuhusu maendeleo ya dhambi, na asili ya dhambi. Itaeleweka kwamba katika serikali ya Mungu, hakuna kasoro yoyote, wala hakuna sababu ya kunung'unika. Wote wenye haki na waasi pia watasema: "Ni za haki, na za kweli njia zako, ee Mfalme wa watakatifu . . . Hukumu zao zimedhihirika." Ufunuo 15:3, 4.

## [28] 6 — Tumeiona Nyota Yake

"Sasa, wakati Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi, siku za mfalme Herode, mara wakaja Mamajusi (watu wenye hekima) kutoka mashariki huko Yerusalemu wakisema, "Yuko wapi aliyezaliwa, Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tumeiona nyota yake upande wa Mashariki, nasi tumekuja kumsujudia."

Mamajusi hawa wa mashariki wamo katika kundi la watu wenye mali, na wenye hekima na wataalam. Baadhi yao walikuwamo watu watawa, waliojifunza na kuchunguza mambo ya asili. Nao waliheshimiwa kwa ajili ya utawa wao na hekima yao. Katika watu wa tabia hii ndimo mamajusi hao walitoka waliokuja kwa Yesu.

Mamajusi hawa walipochunguza nyota za mbinguni waliona utukufu wa Mungu, ambaye ni Muumbaji. Walipojifunza juu ya elimu hiyo, na walipata ujuzi kamili, waligeukia maandiko ya Waebrania ili wayaelewe. Katika nchi yao kulikuwako na manabii waliotabiri juu ya kuja mwalimu wa asili ya Mungu. Utabiri wa Balaam ulikuwa ukipokelewa na vizazi kwa muda wa kane nyingi. Lakini katika Agano la kale, mamajusi walijifunza kuwa kuja kwa Mwokozi kulikaribia. Ulimwengu wote utajazwa na utukufu wa Bwana.

Mamajusi walikuwa wameona nuru ya ajabu huko mbinguni, wakati Utukufu wa Mungu ulipoangaza katika vilima vya Bethlehemu. Nyota yenye kung'aa ilionekana na kuangaza kwa muda. Jambo hilo lilivutia watu na kuwafikirisha. Nyota hiyo ilikuwa ni kundi la malaika wengi wenye kung'aa, lakini mamajusi hawakujua jambo hili. Lakini waliona kuwa ilikuwa nyota yenye jambo maalum kwa ajili yao.

Nyota hiyo isingekuwa ni mjumbe kuhusu Masihi aliyeahidiwa?
[29] Soma Hesabu 24:17. Mamajusi walipokea nuru ya mbinguni iliyotumwa kama mjumbe wa kweli sasa iling'aa kwao zaidi. Kwa njia ya ndoto waliagizwa waende kumtafuta Mkuu aliyezaliwa.

Nchi ya mashariki ilijaa na vitu tele vya thamani, kwa hiyo mamajusi hawakuondoka kwenda na mikono mitupu. Utajiri mkubwa

kabisa ulitwaliwa kuwa sadaka ya kwenda nayo. Walimpelekea yeye yule ambaye watu wote hubarikiwa naye.

### Safari ya Usiku

Ililazimika kusafiri wakati wa usiku ili kuona nyota, ambazo ndizo zinazowaongoza, lakini kila kituo wasafiri hao walichunguza jinsi unabii usemavyo. Walihakikishwa kuwa walikuwa wakiongozwa na Mungu. Safari yao ilikuwa ya furaha, ingawa ilikuwa ndefu.

Walifika katika nchi ya Israeli, huko Yerusalemu, ndipo nyota ilitua juu ya hekalu. Basi waliharakisha kusonga mbele, wakiamini kuwa watasikia habari za kuzaliwa kwa Masihi zikizagaa pote. Lakini kwa mshangao wao, hawakuona hali yoyote ya kusisimua kwa ajili ya kuzaliwa kwa Masihi.

Makuhani walikuwa wakishughulika na dini yao tu, huku wakiwatenga Wagiriki na Warumi, wakiwalaumu kuwa ni wenye dhambi. Mamajusi hawakuwa waabudu sanamu, lakini machoni pa Mungu walionekana kuwa wenye hali bora zaidi kuliko hao waliokuwa wakiitwa wenye dini, walakini walionekana kwa Wayahudi kama wakafiri. Maswali yao kuhusu kuzaliwa kwa Masihi hayakujibiwa.

### Wivu wa Herode Uliamishwa

Ujumbe wa kigeni wa mamajusi uliwataharuki watu sana, walioishi Yerusalemu. Ujumbe huo ulipenya mpaka katika jumba la Mfalme Herode. Habari za uvumi zilizokuwapo, zilimfanya Herode ashuku mashambulio fulani. Kwa kuwa yeye alikuwa mwenye damu ya kigeni, alichukiwa sana na watu, ila usalama wake ulikuwa kwa Warumi tu. Lakini mtawala huyu mpya alikuwa na madaraka makuu, maana alikuwa amezaliwa katika ukoo wa mfalme. Herode alishuku kuwa makuhani wana njama pamoja na wageni kuchochea ghasia ili kumwondosha katika ufalme. Akiazimu kuupinga mpango huo kwa ujanja mwingi, aliwaita makuhani, akawauliza kuhusu mahali atakapozaliwa Masihi.

Ulizo hili lililotoka utawalani, ambalo limeulizwa na wageni, lil-
iumiza kiburi cha walimu wa Kiyahudi. Uzembe wa kutojali unabii, [30]
ulimkasirisha mfalme. Alidhani kuwa wanajaribu kuficha ukweli,

jinsi ulivyo. Kwa amri ya kifalme hawawezi kuthubutu kuzembea. Kwa hiyo aliwaamuru wachunguze na kujua mahali mfalme anayetazamiwa atakakozaliwa. Nao wakamwambia, "Katika Bethlehemu ya Yuda; maana imeandikwa na manabii: "Wewe Bethlehemu, nchi ya Yuda, ingawa u mdogo wewe, kati ya wakuu wa Yuda, Kwako atatoka mtawala, atakaye wachunga watu wangu Israeli."

Sasa Herode aliwaita mamajusi kwa siri. Hofu na ghadhabu ilikuwa imemjaa. Lakini alijisimikiza, asionekane, akajifanya kana kwamba anamtukuza, Kristo aliyezaliwa. Aliwaagiza wageni wake, "Pelelezeni kwa bidii, mambo ya mtoto na mtakapomwona, niarifuni na mimi mahali mlipomwona, ili nami nikamsujudie."

Makuhani hawakuwa gizani kama walivyojifanya. Habari iliyoletwa na malaika kwa wachungaji; ilikuwa imejulikana Yerusalemu, lakini Mafarisayo waliipuuzia. Ingaliwapasa wao kuwaongoza mamajusi katika safari yao, ili kuwapeleka kwa Yesu. Lakini badala ya wao kufanya hivyo mamajusi ndio walikuja kuwashtusha, kuhusu kuzaliwa kwa Masihi.

Kwa habari iliyoletwa na wachungaji na mamajusi ilikuwa sahihi, wangaliwakanusha makuhani wanaojidai kuwa ndio watoa habari za kweli ya Mungu. Walimu hawa walioelinmika wasingaliinamia wakafiri ili kuwasikiliza. Walisema kuwa, isingaliwezekana Mungu awapite, na kuzungumza na wachungaji wajinga, au na watu wasiotahiriwa. Wasingalishughulika kwenda hata Bethlehemu kuona kama habari hizo ni kweli. Hivyo wakawaongoza watu waone kuwa habari za kuzaliwa kwa Yesu ni hadithi tu za kuchekesha. Hapa ndipo ilikuwa mwanzo wa kumkana Yesu, kwa Mafarisayo na marabi. Ukaidi wao ulikuwa na kuwa chuki ya kumchukia Mwokozi.

Mamajusi waliondoka peke yao kutoka Yerusalemu. Kivuli cha usiku kikaingia. Lakini kwa furaha yao, waliona nyota tena, iliyowaongoza kwenda Bethlehemu. Waliondoka Yerusalemu wakiwa na matumaini zaidi kuliko walivyoingia, hali wakishangazwa na hali ya kutoamini kwa Wayahudi.

### Hakuna mtoto wa Kifalme

Katika Bethlehemu Yusufu na Mariamu hawakupata mlinzi yeyote wa kuwahudimia pamoja na mtoto wao, ambaye ni Mfalme.
[31] Hakuna heshima yoyote waliyopata. Yehova alikuwa katika kitanda

kidogo embacho ni hori na wazazi wake ndio walikuwa walinzi wake peke yao. Je, hili ndilo angepaswa kutendewa, yule atakayewainua mataifa ya Yakobo, na kuwa nuru ya mataifa, mpaka mwisho? Isaya 49:6.

Walipofika katika nyumba, walimwona mtoto mchanga, akiwa na Mariamu mama yake. Walianguka wakamsujudia. Halafu walimtolea zawadi, ambazo ni dhahabu, na uvumba, na manemane. Lo, walikuwa na imani kubwa kiasi gani! Mamajusi bila kumwendea Herode kama alivyokusudia, walijiandaa kurudi kwao, baada ya kufaulu kumwona Masihi. Walikuwa wameonywa katika ndoto kuwa wasimrudie Herode. Wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.

Kwa njia ile ya ndoto Yusufu alionywa kwamba, amchukue mkewe Mariamu na mtoto Yesu wakiimbilie huko Misri. Yusufu akaondoka bila kukawia, akakimbilia mahali pa usalama.

Hoja ya mamajusi na hali ya kuchangamka iliyokuwapo, pamoja na wivu wa Herode viliwafanya watu watafakari kuhusu tukio hilo lilotukia, maana watu walichunguza unabii uhusikao.

Shetani alikazana kuzuia mwanga wa Mungu usiwaangazie walimwengu, huku akitumia hila yake ili iwezekane kumharibu mwokozi. Lakini Mungu asiyesinzia, wala kulala, aliandaa kimbilio katika nchi ya mataifa, ili Mariamu na mtoto wapate kukimbilia. Na kwa zawadi zilizotolewa na mamajusi, zilipatikana fcdha za kusafiria mpaka Misri" katika nchi ya ugeni.

## Herode afanya Mauaji ya kutisha

Herode alingojea kurudi kwa mamajusi, akiwa Yerusalemu Muda ulipopita bila kupata lolote, tuhuma yake ilizidi. Je, walimu wa Kiyahudi wamemfunulia mipango yake au mamajusi wameulaghai? Aliwaza akachanganyikiwa. Akaazimu kuchukua hatua ya nguvu.

Maaskari walitumwa kwenda Bethlehemu kuwaua watoto wote wenye miaka miwili na kurudi chini. Nyumba za mji wa Daud;l uliokaa kitulivu kwa miaka 600 kabla haujafunguliwa kwa nabii, ulishuhudia maovu hayo. Unabii ulisema kuwa, "katika Rama zilisikika sauti za kilio na maombolezo makuu. Raheli akiwalilia watoto wake, asikubali kufarijiwa, maana hawapo."

Ajali hii Wayahudi walijiletea wenyewe. Wamemkataa Roho Mtakatifu, ambaye ndiye ngao yao. Wamechunguza unabii na ku-
[32] utafsiri kama wapendavyo wenyewe, kwamba wao wanapendelewa, na mataifa mengine la. Wamechochea chuki ya mtawala wao. Kwa njia ya kumweleza Kristo kimakosa na kazi yake pia, Shetanii. aliazimu kumharibu Mwokozi, lakini badala yake maafa yamewageukia wenyewe.

Mara baada ya kuwaangamiza watoto, Herode alikufa kifo kibaya sana. Yusufu bado yuko Misri. Malaika akamwagiza arudi katika Israeli. Kuhusu Yesu, ambaye ni mirithi wa kiti cha enzi cha Daudi Yusufu alitamani kuishi Bethlehemu. Lakini alipojua kuwa Arklao mtoto wa Herode anatawala badala ya baba yake, aliogopa asije akafanya yale yale ya baba yake. Yusufu alionyeshwa mahali pa salama zaidi, Nazareti. Hapa ndio Yesu alipokulia kwa muda wa miaka karibu thelathini, ili neno litimie kuwa: "Ataitwa Mnazerayo." Galilaya kulikuwa na mchanganyiko wa mataifa kuliko Uyahudi. Kwa hiyo Wayahudi hawakupashughulikia.

Hivyo ndivyo Mwokozi alivyopokelewa, alipokuwa ulimwenguni. Mungu hakumwaminisha Mwanawe mpendwa kwa binadamu, hata alipokuwa akiwashughulikia kuhusu wokovu wao. Aliwaamuru malaika kumhudumia Yesu, mpaka atimize kazi yake, na kufa mikononi mwa wale aliokuja kuwaokoa.

## 7 — Mtoto Yesu [33]

Utoto na ujana wa Yesu uliishia katika kijiji kidogo cha milimani cha Nazareti. Alikulia katika kijiji cha mtu mashuhuri, mwenye ufundi wa vitu vya useremala, akitukuka katika kijiji cha Nazareti kisichokuwa na sifa nzuri.

Mtoto alikua na kuongezeka nguvu za mwili na za kiroho pia, akiwa na hekima, maana neema ya Mungu ilikuwa pamoja naye. Luka 2:52 Mawazo yake yalikuwa wazi sana yenye kuwaza kamili kupita umri aliokua nao. Uwezo wake wa mwili na akili viliongezeka kabisa katika hali yake ya kitoto.

Tangu utoto wake Yesu alionyesha tabia ya kupenda mambo manyofu, uvumilivu, kutokuwa na harara wala wasiwasi, hakuwa na mashaka kwa lolote. Alisimama katika kanuni bila kutikisika. Maisha yake hayakuwa ya ubinafsi hata kidogo.

Mama yake aliangalia jinsi Yesu alivyoendelea na hali yake, naye akamtia moyo kuendeleza hali bora hiyo. Kwa njia ya Roho Mtakatifu, Mariamu alipata hekima ya kumwongoza Yesu katika tabia hiyo. Naye alimtambua Mungu kama Baba yake.

Siku hizo Kristo alipokuwa mtoto, mafundisho ya vijana yalikuwa ya bora mradi tu. Mapokeo yalikuwa yamechukua mahali pa maandiko matakatifu.

Mawazo ya vijana yalijazwa na mambo ya uchumi tu, ambayo hayakutambuliwa huko mbinguni kuwa ndiyo mafundisho yafaayo. Wanafunzi hawakupata nafasi ya kuzungumza na Mungu wakiwa katika hali ya ukimya ili wasikie sauti yake ikinena nao kimya. Kwa hiyo wakajitenga na kisima cha hekima. Yale yaliyodhaniwa kuwa ndiyo mafundisho muhimu, yalikuwa sumu mbaya kuzuia maendeleo ya vijana. Mawazo yao yalidumaa na kufinyika.

Mtoto Yesu hakupata mafundisho katika masinagogi yaliyokuwa [34]
yakiendesha shule. Mama yake alimfundisha mambo ya manabii, ambayo ni maandiko matakatifu. Alivyoendelea kukua, hakutaka kutafuta mafundisho yaliyokuwa yakitolewa na walimu wa Kiyahudi. Hakupenda mafundisho ya jinsi hiyo. Ujuzi wake katika

mambo matakafifu wakati wa utoto wake, ulionyesha jinsi alivyopenda kujifunza neno la Mungu.

### Viumbe vya asili vilifunua wito wa Biblia

Mbele ya macho yake kulikuwa vitu vingi sana, ambavyo viliumbwa na Mungu. Yule aliyeviumba vitu vyote, alisoma maandiko yake mwenyewe aliyoandika katika nchi, bahari na angani. Alikusanya hazina ya sayansi kutoka katika mimea, wanyama, na watu. Mifano aliyopenda kutumia katika mafundisho yake ya kufafanua ukweli, yalionyesha kwamba aliunganisha mambo ya kiroho na viumbe vya asili na katika mazingira ya kila siku maishani.

Yesu alipokuwa akijaribu kufahamu sababu za mambo kadha wa kadha, ya mbinguni ndio yalikuwa msaidizi wake. Tangu mwanzoni kabisa alikuwa akizidi kukua kiroho, akiwa na neema na elimu ya kweli.

Kila mtoto anaweza kupata elimu, sawa na Yesu alivyopata. Tunapojaribu kuhusiana na Baba wa mbinguni, malaika watatusogelea, mawazo yetu yataimarishwa, na tabia zetu zitainuliwa na kutakaswa. Tutafanana naye zaidi na azaidi. Tunapotafakari uzuri, na ukubwa wa viumbe, mawazo yetu hupanda kwa Mungu. Roho zetu hupata kicho, nia zetu huimarishwa ili kumwendea Mungu, kwa njia ya kazi zake. Kushirikiana naye kwa njia ya sala, hukuza akili na nia kabisa.

Yesu alipokuwa mtoto alifikiri kama mtoto, na kunena kitoto, lakini hakuna na alama ya uovu katika hali yake, alikuwa na hali ya Mungu tu, ila hakutengwa mbali na majaribu. Wenyeji wa Nazareti walijulikana kwa ajili ya uovu wao. Soma Yohana 1:46. Ilimlazimu Yesu kujiangalia sana, ili ajikinge na maovu hayo. Alikabiliwa na mambo yote yanayotukabili sisi, bila kupotoka, ili awe kielelezo halisi kwetu, tangu utoto, hata ujana, na utu uzima.

Tangu utoto wake, Yesu alikuwa akilindwa na mbingu, kwa njia ya malaika, walakini maisha yake yalikuwa ya mashindano makali na uovu. Mkuu wa giza hakubakiza kitu chochote asichotumia kumpinga Yesu.

[35] Yesu alifahamu hali ya umasikini, na kuzoeana nayo, pamoja na kujinyima. Hali hiyo ilimfaa sana na kumlinda. Hakujishughulisha na hali yoyote potovu. Yesu hakushughulika kutafuta starehe, map-

ato, wala heshima, au raha, maana vitu hivyo vingekuwa mtego wa kumtia dhambini. Ni Kristo peke yake aliyeishi katika mji mwovu wa Nazareti kwa miaka karibu thelathini, bila kutenda dhambi. Jambo hili ni kanusho kubwa kwa wenye udhuru wa kutenda dhambi wakisingizia mahali, kazi, mali au bahati.

## Kristo aliheshimu kazi kama Seremala

Yesu alikuwa amiri jeshi huko mbinguni, na malaika walikuwa wakifanya mapenzi yake; na sasa alikuwa mtumishi mtiifu kazini. Alifanya kazi kwa mikono yake pamoja na Yusufu. Hakutumia miujiza ya mbinguni kumsaidia kufanya kazi. Alitumia nguvu za mwili, ili awe na afya ya kumwezesha kutenda kazi barabara.

Hakuwa mzembe katika shughuli, hata kushika vyombo vya kazi ya useremala. Alikuwa kamili katika kazi kama alivyokuwa kamili katika tabia. Aliweka kielelezo kwamba kazi yapaswa kutendwa kwa ukamilifu, maana kazi ni kitu cha heshima. Mungu aliiweka kazi kuwa kitu cha mbaraka. Na mfanya kazi hodari tu ndiye anayepata furaha maishani. Mungu huwakubali watoto na vijana wanaofanya kazi kamili nyumbani kwao, huku wakishiriki mizigo ya kazi pamoja na baba zao na mama zao. Yesu alikuwa mwaminifu na hodari katika kazi. Alitarajia mambo makuu, kwa hiyo alijaribu mambo makuu pia. Alisema, "Inanipasa kufanya kazi zake aliyenipeleka, wakati kungali mchana." Yohana 9:4. Yesu hakuepa kazi yoyote, au wajibu kama watu wengine wafanyavyo leo, huku wakijiita kuwa wafuasi wake. Kwa kuwa huepuka wajibu huu, watu wengi ni dhaifu, wala hawafai kitu, nao huonekana kutofaa wakati wa shida. Uhodari na uwezo ulioonekana kwa Kristo unaweza kuwa wetu pia, kwa kufuata hali ile ile Kristo aliyofuata. Neema aliyopata ni kwa ajili yetu.

Mwokozi wetu alishiriki mambo mengi ya kimaskini. Wale wanaoelewa hali kamili ya Kristo, hawataona kuwa utajiri unafaa kuliko umaskini.

## Mwimbaji Mchangamfu

Kila mara Yesu alionyesha furaha ya moyo wake kwa njia ya kuimba Zaburi, na nyimbo nyingine za mbinguni. Mara kwa

mara wenyeji wa Nazareti walimsikia akiimba nyimbo za sifa. Wenzake walipo kuwa wakilalamika kwa sababu ya kuchoka,
[36] walichangamshwa kwa nyimbo alizoimba.

Kwa miaka yote aliyokaa Nazareti, maisha yake yalikuwa ya kusaidia na kufariji wengine. Alisaidia wazee, wenye huzuni, wenye kulemewa na dhambi, watoto katika michezo yao, viumbe vidogo vidogo, wanyama wenye taabu. Kila mara wote walimfurahia popote anapokuwa. Anayeusimamisha ulimwengu, alishuka chini kumhudumia ndege aliyeumia. Hakuna kitu kilichopitwa bila kuhudumiwa.

Hivyo ndivyo alivyokuwa mwenye hekima., na kimo akimpendeza Mungu na watu pia. Alijionyesha kuwa mwenye huruma kwa wote. Hali yake na mahali pake, vilikuwa mibaraka ya wote. Mara kwa mara siku ya sabato aliitwa kusoma maneno ya manabii, na watu walifurahia mambo hayo sana.

Walakini katika muda huo wote wa kuishi Nazareti, hakutenda tendo lolote la mwujiza, wala hakuwa na cheo chochote. Maisha yake ya utulivu yalifundisha fundisho la maana sana. Maisha ya kutoiga mambo ya kubuni, na ya ovyo huwa na maana sana kwa watoto, na kuchunguza viumbe vya Mungu hupanua mawazo zaidi.

Yesu ni kielelezo chetu. Katika maisha ya nyumbani ndiye wa kuigwa na watoto wote na vijana. Mwokozi aliwatendea maskini wema kabisa, ili kutuonyesha jinsi ya kutembea pamoja na Mungu. Kazi yake ilianzia na uaminifu katika kazi za nyumbani, fundi anayeshughulika ili apate chakula.

Wakati alipokuwa akifanya kazi ya useremala, alikuwa akifanya kazi ya Mungu hasa, sawa kama angejishughulisha kuwahudumia makutano. Kila kijana anayefuata kielelezo cha Yesu, cha kuwa mwaminifu na mtiifu, na mpole katika maisha ya nyumbani, atahusika na maneno haya: “Tazama mtumishi wangu nimtegemezaye, mteule wangu, ambaye nafsi yangu yapendezwa naye.” Isaya 42:1.

# 8 — Kuhudhuria Katika Pasaka [37]

Wayahudi mwaka wa kumi na mbili ulikuwa ndio mgawanyiko kati ya utoto na ujana. Katika kawaida hii, Yesu alikuwa na haki ya kwenda kuhudhuria pasaka pamoja na Mariamu mamaye, na Yusufu, maana alikuwa amefikisha umri unaotakiwa.

Safari ya kutoka Galilaya mpaka Yerusalemu ilichukua sku kadhaa. Wasafiri iliwapasa kujiunga katika kundi kubwa ili kujilinda. Wanawake na wazee walipanda punda, au gari la kukokotwa na ng'ombe. Njia ilikuwa ya mitelemko na miamba. Watu wengine walitembea kwa miguu. Njiani kulikuwa na maua na hali safi, na nyimbo za ndege. Wazazi waliwaeleza watoto wao maajabu ya Mungu, kadiri wahvyosafiri. Maadhimisho ya pasaka yalianza tangu taifa la Israeli lilipotoka Misri kwenda Kanaani. Siku ya mwisho ya utumwa wao huko Misri, Mungu aliwaagiza Waisraeli kujikusanya, kijamaa na kuchinja mwana kondoo. Baada ya kunyunyiza damu ya kondoo katika vizingiti na miimo ya milango, basi walikula nyama ya kondoo iliyookwa na mikate isiyochachwa, na mboga chungu. "Hii ndiyo pasaka ya Bwana." Kutoka 12:11. Panapo usiku wa manane wazaliwa wa kwanza wote wa Misri waliuawa. Ndipo Waebrania walitoka katika nchi ya Misri wakiwa taifa linalojitegemea.

Pasaka ilifuatiwa na siku kuu ya muda wa siku saba. Siku kuu hiyo ilikuwa ya mikate isiyochachwa. Maadhimisho hayo yote yalionyesha kuja kwa Mwokozi. Kondoo wa kuchinjwa, mkate usiochachwa, malimbuko, vilionyesha Mwokozi. Lakini wakati wa Kristo, sikukuu hizo zote hazikuwa na maana yoyote, ilikuwa kawaida au desturi tu, iliyokuwa ikifanywa na watu. Haikuonyesha lolote kuhusu Mwana wa Mungu!

Mara ya kwanza mtoto Yesu alilitazama hekalu. Aliwaona
makuhani wenye kanzu nyeupe wakifanya huduma zao, mwanakon- [38]
doo akilazwa madhabahuni akiwa ametolewa kuwa kafara. Aliona
huduma ya pasaka ikifanywa kwa uzuri na utaratibu hasa. Kila siku
aliona maana ya yote hayo kwa uwazi zaidi. Kila tendo lilielekea
hasa juu yake. Mwamko mpya ulionekana kwake. Alijifunza katika

hali ya kimya juu ya matatizo. Siri ya kazi yake ilifunuliwa kwake kama Mwokozi.

Mawazo yake yalichangamka kwa maajabu ya mambo aliyoona, hata akawa kama mtu aliyepigwa bumbuazi, ila wenye kuabudu walipotoka na kwenda, alibaki nyuma akitafakari.

Katika mkutano huu wa pasaka, wazazi wake walitaka kumleta Yesu kwa walimu wakuu wa Israeli. Walitamani apate kuadibika kutokana na walimu hawa wakuu. Lakini Yesu alifundishwa na Mungu hekaluni kuwa yale aliyopokea, lazima ayapitishe kwa wengine.

Chumba kilichoungwa katika hekalu, kiliwekwa ili kiwe shule. Hapo mtoto Yesu aliingia na kuketi katika miguu ya walimu wakuu waliojifunza sana. Alikuwa akiwahoji maswali mbalimbali, kama mtu atafutaye hekima. Alikuwa akiwauliza mambo ya unabii na mambo yaliyotokea, kuhusu Masihi.

Maswali yake yalieleza ukweli wa ndani; ambayo yalikuwa hayaeleweki, lakini yanahusu wokovu. Maswali yake yalionyesha jinsi walimu hawa walivyokuwa gizani, kuhusu unabii wa kuhusu kuja kwa Masihi. Walionekana kuelewa vipya kuliko jinsi walivyoelewa hapo mwanzo. Walimu hao walizungumza juu ya hali mpya ambayo italetwa na kuja kwa Masihi. Lakini Yesu alielekeza unabii wa Isaya unaotaja juu ya mateso ya Mwana Kondoo wa Mungu. Isaya 53.

Walimu wakuu hawa, walimwuliza maswali, nao walishangazwa na majibu yake. Kwa unyenyekevu alieleza maana yake, ambayo wao hawakuwa na habari. Kama wangalifuata mwongozo wa unabii wangalikuwa na matengenezo halisi katika mambo ya dini wakati huu, na Yesu alipoanza huduma yake, wengi wangalikuwa tayari kumwamini.

Walimu hawa waliona nuru ya unabii ndani ya mtoto huyu wa Galilaya. Walitaka kukanusha elimu yake, maana wao ndio wangempatia maarifa hayo.

Maneno ya Yesu yaliwakoroga sana, ambavyo hawajakorogwa na maneno ya mtu yeyote. Mungu alikuwa akitaka kuwapa nuru kwa njia hiyo, ingawa walikuwa waongozi. Kama Yesu angalijaribu kuwafundisha, wangalimkatalia mbali. Lakini wao walijisifu
[39] kuwa ndio wanamfundisha yeye, na kujaribu maarifa yake kuhusu maandiko. Upole wa Yesu na hali yake ya neema, vilipunguza chuki

yao. Mawazo yao yalifunguliwa kuona neno la Mungu dhahiri, na Roho Mtakatifu alisema ndani yao na kuwaongoza.

Waliona kuwa matazamio yao ya kuhusu Masihi hayakuwa ya kufuatana na unabii, lakini hawakukubali kuwa walitafsiri unabii vibaya.

### Wazazi wake wafadhaika

Wakati ule walipotoka Yerusalemu kurudi nyumbani, Yusufu na Mariamu hawakuweza kumwona Yesu. Msukosuko wa safari uliwabana kiasi cha kutoshughulika kumwangalia mpaka kukachwa. Halafu hawakuona mtu wa kuwasaidia. Wao walidhani kuwa Yesu yumo katika msafara; kwa hiyo hawakuwa na wasiwasi. Lakini sasa mashaka yao yakaamka. Wakatetemeka, walipokumbuka jinsi Herode alivyojaribu kumwua wakati wa utoto wake. Wasiwasi ukawajaa tele.

Walianza kumtafuta, huku wakirudi kuelekea Yerusalemu. Siku ya pili, kukasikiwa sauti yake katika hekalu. Kumbe alikuwa katika shule ya walimu. Mama yake alisema kwa sauti ya kukemea: “Mtoto, kwani umetutendea hivi? Tazama baba yako na mimi tumekutafuta kwa huzuni sana.”

Yesu akajibu, “Kwani kunitafuta, hamjui kuwa inanipasa kuwa katika nyumba ya Baba yangu?” Walipoonekana kutofahamu maana yake, alielekeza kidole mbinguni. Uso wake uling’aa. Uungu uling’aa katika ubinadamu. Wamesikia maongezi yake na walimu wakuu, nao walishangaa kwa maswali yake na majibu.

Yesu alikuwa akishughulika na kazi aliyokuja kufanya; lakini Yusufu na Mariamu hawakujali kazi zao. Mungu amewaheshimu sana kwa kuwapa kazi ya kumtunza Yesu. Lakini walimpoteza mtoto kwa muda wa siku nzima, na hata walipomwona hawakufahamu kazi yake.

Lilikuwa jambo la kawaida kwa wazazi wa Yesu kumheshimu kuwa mtoto wao. Katika mambo mengi, hali ilikuwa hiyo kuwa kama mtoto wao tu, hivyo ilikuwa vigumu kumfahamu kuwa ni Mwana wa Mungu. Maneno ya upole aliyowaambia, yalikusudiwa kuwajulisha kuhusu kazi yake takatifu, na yao pia. jawabu la Yesu kwa mamaye, lilionyesha kuwa alifahamu uhusiano wake na Mungu. Mariamu hakufahamu maneno hayo yana maana gani;

lakini alielewa kuwa Yesu ni mwana wa Yusufu, na kuwa anakubali kuwa ni Mwana wa Mungu.

[40] Kutoka Yerusalemu, Yesu alirudi nyumbani na wazazi wake, akawa anawatii na kuwasaidia. Kwa muda wa miaka kumi na minane, Yesu alijulikana kuwa mwana wa Yusufu, mtoto wa Nazareti, akiwa mwenyeji na rafiki wa Nazareti.

Yesu alikusudia kurudi Yerusalemu katika hali ya ukimya pamoja na wale waliojua siri ya maisha yake. Kwa njia ya pasaka, Mungu alitaka kuwakumbusha watu wake kazi ya ajabu juu ya ukombozi wao kutoka Misri. Katika kazi hii alikusudia kuwaonyesha ahadi ya ukombozi kutoka dhambini. Damu ya Kristo ingewaokoa. Mungu alitamani wajifunze kazi ya Kristo kuhusiana na ukombozi wao kutoka dhambini. Lakini watu walipokwenda kutoka Yerusalemu mambo ya safari tu ndiyo yalikuwa katika nia zao, huduma waliyofanya ilisahauliwa. Hata Mwokozi hakufikiriwa.

## Yesu alimsaidia mama yake

Walipotoka Yerusalemu, Yesu alitumaini kuwaelekeza wazazi wake juu ya unabii unaohusu mateso ya Mwokozi katika msalaba wa Kalwari. Alitumaini kupunguza huzuni ya mamaye. Alikuwa akimfikiria sana. Maana Mariamu atakuwako kuyaona mateso yatakayompata. Na Yesu alitaka afahamu kazi yake hasa, ili wakati huo asije akazimia kwa huzuni. Kama angefahamu kazi yake, angemsaidia jinsi gani kustahimili mateso ya Yesu! Kule kutojali wajibu wao kwa siku moja Yusufu na Mariamu, walimpoteza Mwokozi. Lakini iliwachukua siku tatu kumwona. Ndivyo ilivyo hata kwetu pia. Kwa njia ya maongezi hafifu, au kutojali maombi, tunaweza kumpoteza Mwokozi na inaweza kutuchukua siku nyingi kumpata tena.

Lazima tujihadhari tusije tukamsahau Yesu, tukapata hali ya kuwa wazembe, bila kuwa na mwungano wa mbingu kwa njia ya malaika. Viumbe hawa watakatifu hawawezi kutukumbusha mahali tulipomwacha Mwokozi, wala kututia hamu ya kuwa naye tena.

Wengi huhudhuria ibada za dini, na kujiburudisha kwa neno la Mungu, lakini kwa kutojali maombi ya kujitoa, hupoteza mibaraka. Kwa njia ya kujitenga na Yesu, huzuia nuru yake kutuangazia.

Inatufaa sana kuwa na saa moja kila siku kutafakari maisha ya Kristo. Tuyatafakari hatua kwa hatua, hasa maisha yake ya mwisho.

Ndivyo matumaini yetu kwake, na upendo wetu kwake vitavuviwa Roho Mtakatifu. Kwa kuitazama tabia yake, tutabadilishwa; kufanana hivyo na kutoka utukufu hata utukufu. 2 Wakorintho 3:18.

[41] # 9 — Matatizo ya Kristo Wakati wa Utoto

Katika shule za masinagogi, wanafunzi wakiwa chini ya waalimu wa Kiyahudi, walifundishwa kushika kawaida zisizokuwa na hesabu kwa wingi, ambazo kuhesabiwa kuwa ndizo za dini kamili, zenye kuonyesha kuwa watu hawa ni washika dini hasa. Lakini Yesu hakushughulika na mambo kama hayo. Tangu utoto wake, Yesu hakuhangaika na kawaida hizo. Maandiko matakatifu ndiyo yalikuwa masomo yake ya kawaida, na maneno, “Ndiyo asemavyo Bwana”, ndiyo yalikuwa kinywani mwake daima.

Aliona kuwa watu walikuwa wakijitenga na neno la Mungu, ila tu wakishika kawaida ambazo hazina faida yoyote. Katika huduma zao ambazo si za imani, hazikuwaletea utulivu rohoni mwao. Hawakujua uhuru wa roho unaoletwa na neno la Mungu linapoaminiwa. Ingawa Yesu hakukubaliana na halli hiyo kuchanganya neno la Mungu, na hadithi za kibinadamu, walakini hakuwashambulia walimu hao, wala kawaida zao. Walipomlaumu kwa hali yake tofauti na wao, alileta neno la Mungu kuwa ndiyo msimamo wake.

Yesu alijaribu kuwapendeza wale aliokutana nao. Kwa kuwa alikuwa mtu mwungwana sana, waandishi na wazee walidhani kuwa ataweza kugeuzwa upesi na kufuata kawaida zao. Lakini aliwauliza mahali wanaposoma katika maandiko, mambo hayo. Yeye alitii kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu, lakini hadithi za wanadamu hakuzijali. Yesu alionekana kujua Maandiko kutoka mwanzo mpaka mwisho, naye aliyatumia katika ukweli wake. Walimu wa Kiyahudi, yaani walimu wakuu, walijidai kuwa wao ndio wawezao kuyafafanua Maandiko katika ukweli wake. Walijua kuwa wasingeweza kupata neno katika mandiko liwezalo kukubaliana na mambo yao. Hata hivyo walichukizwa kwa sababu Yesu alipingana
[42] nao. Walipokosa kumvuta Yesu, waliwaambia wazazi wake kuhusu ukaidi wa mtoto wao, hivyo Yesu akakabiliwa na magombezo ya Yusufu na Mariamu.

Tangu utoto wake, Yesu alianza kujitegemea na kujenga tabia yake. Kulitii Neno la Mungu, kulikuwa jambo muhimu kwake, kuliko neno lolote, hata upendo kwa wazazi wake haukuweza kumgeuza, asitii Neno la Mungu. Lakini hali ya walimu wakuu kulimsikitisha sana, akawa na huzuni katika maisha yake, Alijifunza fundisho gumu la kukaa kimya na kuvumilia sana.

Ndugu zake, yaani wana wa Yusufu waliungana na walimu wa Kiyahudi. Waliyaheshimu mapokeo ya wanadamu zaidi kuliko neno la Mungu, na walimlaumu Yesu kuwa ni mkaidi. Lakini ujuzi wake uliwashangaza marabi kwa jinsi alivyokuwa na majibu yake. Walakini hawakujifunza kuwa alikuwa akiwafundisha. Walitambua kuwa aliwazidi katika ujuzi, wala hawakuelewa kuwa asili ya ujuzi wake ni wapi.

## Jinsi Yesu alivyowaheshimu wote

Kristo alikuta dini imezungushiwa ua, kama ni kitu kisichotaka kuonekana katika maisha ya kila siku. Ua huo yeye aliubomoa. Badala ya kujifungia ndani ya chumba ya kujitenga na watu, ili kuonyesha tabia ya mbinguni, alifanya kazi ya kusaidia watu. Alifundisha kuwa dini siyo kitu cha muda fulani, na wakati fulani tu, ila ni huduma ya wakati wote. Jambo hili lilikuwa kemeo kubwa kwa walimu wa Kiyahudi na mafarisayo. Jambo hili lilionyesha kuwa dini yao ni mfano tu, ilikuwa kinyume cha utauwa. Liliamsha uadui, kwa vile walivyotaka kuwalazimisha watu kufuata desturi zao.

Yesu alikuwa na fedha kidogo tu, kwa hiyo hakuwa na kitu cha kutoa. Kwa hiyo kila mara alikataa chakula ili kiwasaidie wahitaji zaidi yake. Wakati ndugu zake walipowakemea maskini, yeye aliwafariji na kuwatia shime. Kwa wahitaji aliwapa ingawa kikombe cha maji baridi, na chakula kidogo alicho nacho.

Mambo kama hayo yaliwachukiza ndugu zake. Kwa kuwa walikuwa wakubwa kuliko yeye, waliona kuwa ingempasa Yesu kuwaheshimu na kuwatii. Walimlaumu kwa kujikuza kuliko wote hata na walimu wake pia. Kwamba anajitukuza kupita makuhani, hata kupita watawala. Mara kwa mara walimtisha, lakini aliwapita akiwasomea Maandiko, na kuyafanya kuwa ndiyo mwongozo wake.

[43]

## Matatizo ya Yesu na jamaa yake

Ndugu za Yesu walimwonea wivu, na wakaazimu kutokubaliana naye kwa vyo vyote. Hawakuelewa tabia vuke, Mabishano makubwa yalikuwako kati yao. Alikuwa Mwana wa Mungu, walakini alikuwa mtoto wa

Ibinadamu tu. Kama mwumbaji, nchi ilikuwa katika uangalizi wake, walakini ufukara ulikuwa ndio maisha yake. Hakutafuta ukuu wa dunia hii, ila aliridhika tu na hali yoyote ya chini kabisa. Mambo haya yaliwachukiza ndugu zake. Hawakuridhika na hali yake ya unyofu, hata anapoonewa. Yesu hakueleweka kwa ndugu zake, kwa kuwa hakuwa kama wao. Kwa kutazama kwa watu, walikuwa kinyume cha Mungu, wala hawakumtegemea katika maisha yao. Mfano wa dini waliokuwa nao, haukuwatakasa kamwe. Tabia zao zilikuwa vile vile tu. Kielelezo cha Yesu, kwao kilikuwa chukizo la daima. Alichukia dhambi, na hakutaka kuona mambo maovu. Kwa kuwa maisha ya Yesu yalichukia dhambi, ndiyo sababu alipingwa. Uaminifu wa Yesu na hali yake isiyo na ubinafsi, vilikuwa dhihaka kwao. Uvumilivu wake na wema wake ulihesabiwa kama woga.

Uchungu wote unaompata binadamu, hakuna sehemu ambayo haikumpata Yesu. Wengine walimdharau kwa ajili ya kuzaliwa mahali hafifu. Hata katika utoto wake alikabiliwa na mashutumu na dharau. Katika hayo yote, kama angejibu vibaya, kutenda vibaya, angeliangukia mbali, wala asingelikuwa kielelezo kamili kwa binadamu. Angelishindwa kutimiza mpango wa wokovu. Kama angelikubali dhambi hata ndogo mno, Shetani angalishangilia na ulimwengu ungalipotea. Kila mara aliyesabiwa kuwa mwoga, kwa ajili ya kutoshirikiana na ndugu zake, katika mambo maovu. Kila mara jibu lake lilikuwa, Imeandikwa, "Kumcha Bwana ndiyo hekima, na kujitenga na uovu ndio ufahamu.' Ayubu 28:28. Wengine walimfurahia, lakini wengi wao hawakumfurahia, maana maisha yake yalikuwa shutumu kwao, kwa vile alivyokuwa na hali ya unyofu kuliko yao. Vijana walimfurahia, lakini wengine hawakufurahia hali yake ya kutokubaliana nao kufanya mambo ya upuzi. Walipomtaka kwenda naye mahali pasipofaa, Yesu alijibu, Imeandikwa, "Kijana ataisafishaje njia yake? Kwa kulishika neno lake. . . Nimelishika neno lako moyoni mwangu, nisije nikakutenda dhambi." Zaburi 119:9, 11.

Mara nyingi aliulizwa, “Kwa nini wewe u tofauti na sisi?” Alisema, Imeandikwa, ‘Heri wazitiio shuhuda zake. Naam, [44]
hawakutcnda ubatili, wamekwenda katika njia zake.” Zaburi 119:1, 2.

Wakati alipoulizwa kuwa, kwa nini hujiungi na watoto wenzako wa Nazareti katika michezo, alisema: Imeandikwa “Nitajifurahisha sana kwa amri zako. Sitalisahau neno lako.” Zaburi 119:16.

Yesu hakupigana, au kudai ili apatiwe haki yake. Hakulipa kisasi alipotendewa vibaya, ila alivumilia ujeuri huo tu. Mara nyingi aliulizwa kuwa, “Kwa nini unakubali ufedhuli unaofanyiwa hata na ndugu zako?” Alisema, Imeandikwa: “Mwanangu usisahau mafundisho yangu, shika amri zangu .... Rehema na kweli zisifarakane nawe. Zifunge shingoni mwako. Ziandike juu ya kibao cha moyo wako. Ndivyo utakavyopata kibali na akili nzuri, mbele za Mungu, na mbele za wanadamu.” Mithali 3:1-4.

### Kwa nini ilimpasa awetofauti na wengine?

Njia ya Yesu, haikueleweka hata kwa wazazi wake. Alionekana kama mtu aliyetengwa. Saa zake za furaha zilionekana wakati alipokuwa peke yake, akitafakari viumbe. Asubuhi na mapema, kila mara alikutwa mahali pa peke yake akiomba, na kusoma neno la Mungu. Kutoka katika hapo alikuja nyumbani kuendelea na shughuli zake za kila siku.

Mariamu aliamini kuwa mtoto mtakatifu aliyemzaa, ndiye Masihi bila shaka, walakini hakuthubutu kusema hivyo. Katika maisha yake yote alikuwa mshiriki wa mateso. Mariamu aliangalia kwa huzuni jinsi alivyokuwa akitendewa mambo ya ujeuri; katika utoto, na ujana wake wote. Kwa kuona alivyokuwa akitendewa isivyo haki, Mariamu pia alikuwa katika hali ya msukosuko daima. Alishughulika na maangalizi ya kuwalea watoto ili wawe na tabia njema. Watoto wa Yusufu walifahamu hayo, na kwa kutaka kumsaidia walitaka Yesu awe kama wao pia.

Kila mara Mariamu alimwonya Yesu, alimtaka akubaliane na mambo ya waalimu ya Kiyahudi ambao ni walimu wakuu. Lakini yeye hakukubali kugeuza tabia yake ili kupunguza matatizo yanayomkabili, maana kwa kufanya hivyo angalihafifisha kazi ya Mungu. Makuhani na walimu walipomtaka amrekebishe Yesu alikuwa katika

matatizo makubwa sana. Lakini alitulia aliposoma neno la Mungu linalomwunga mkono.

Wakati mwingine Mariamu alisitasita baina ya Yesu na ndugu zake, ambao hawakuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, lakini ushahidi ulikuwa wazi kuwa yeye ni wa Mungu. Maisha yake
[45] yalikuwa kama chachu katika jamii. Aliishi kati ya watu wafedhuli, wajeuri wasiokuwa na huruma, wakafiri, wapotevu, lakini yeye hakuchafuliwa na maovu hayo. Alichanganyika na watu wa kila hali: Askari, Wasamaria, Wapuuzi, wakulima, wenye jeuri, lakini akiwa safi. Alisema maneno ya huruma alipowaona watu katika laabu. Alijifunza upendo wa Mungu katika viumbe.

Aliwafundisha kujiangalia kuona vipawa walivyopewa. Alifundisha kuwa kila dakika ina thamani, nayo ingeonekana kuwa ni mali kuu, inayopaswa kutumiwa kwa makusudi matakatifu. Hakumwona mtu yeyote kuwa hana faida; ila alimtia nguvu kila mtu na tumaini. Akawaambia kuwa, kila mtu anaweza kupata na kutenda mambo ya faida. Kila mtu anaweza kupata tabia halisi ya kumfanya kuwa mwana wa Mungu. Kila mara alikutana na watu waliofungwa na minyororo ya Shetani, akawafariji na kuwatia tumaini.

Watu wengine Yesu aliokutana nao walikuwa katika vita na mwovu Shetani. Aliwatia moyo wasikate tamaa, maana malaika wa Mungu wako upande wao, nao watawawezesha kushinda. Wote aliowasaidia, walimtumaini, na kuona kuwa huyu ndiye msaada wetu.

Yesu alikuwa tayari kumsaidia kila mtu katika tatizo lolote alilo nalo. Kila mtu alipata utulivu rohoni mwake. Hakuna mtu aliyesema kuwa ametenda mwujiza, ila tu maneno ya amani na huruma na ya kutia nguvu na tumaini. Nguvu ya kuponya ilitoka katika kinywa chake. Hivi kwa njia hii aliwatumikia watu tangu utoto wake.

Hata hivyo, katika maisha yake, tangu utoto, ujana, na utu uzima, Yesu aliishi peke yake. Katika uaminifu, na usafi wa roho, hakuwa na mwenzake. Soma Isaya 63:3. Alijua kuwa pasipo makusudi kamili katika tabia na kanuni, ulimwengu ungepotea. Akijitoa kamili juu ya kuokoa ulimwengu, aliendesha mpango wote katika maisha yake, apate kuwa nuru ya wanadamu.

## 10 — Sauti Nyikani [46]

Kutoka katika watu waaminifu wa Israeli, ndimo mtangulizi wa Yesu alimotokea. Mzee Zakaria aliyekuwa kuhani, na mkewe Elizabeti, wote wawili walikuwa watawa. Na katika maisha yao ya utulivu, nuru iliwaangazia, kama nyota zinazoangaza katika giza. Kwa wazee hawa wawili, walipewa ahadi ya kuzaa mtoto, wa kiume; ambaye atatangulia mbele ya Bwana, ili kumtengenezea njia."

Zakaria alikuwa amekwenda Yerusalemu ili kuhudumu kwa juma lake moja katika hekalu. Akiwa amesimama madhabahuni katika patakatifu, ghafla alimwona malaika wa Bwana, amesimama upande wa kuume wa madhabahu. Zakaria amekuwa akikuombea kuja kwa Mwokozi kwa muda mrefu. Sasa sala hizi karibu zitajibiwa.

Zakaria alipata habari ya kufurahisha: Kwamba, "Usiogope, Zakaria; maana sala zako zimesikiwa, mkeo atakuzalia mtoto wa kiume, nawe utamwita jina lake Yohana. . . . Atakuwa mkuu mbele za Bwana, naye hatakunywa mvinyo, au kileo cho chote, naye atajazwa na Roho Mtakatifu. . . . Naye, atatangulia mbele ya Bwana mwenye nguvu za Eliya, ili kuwageuza baba kuelekea watoto wao, na wakaidi kuelekea hekima ya watawa, kutayarisha watu kwa ajili ya kuja kwake Bwana. Zakaria akasema kwa malaika, Nitajuaje jambo hili? Maana mimi ni mzee, na mke wangu ameendelea kuzeeka.?"

Kwa muda kitambo mzee huyu alisahau vile Mungu alivyoahidi, kwamba anao uwezo wa kutimiza kila jambo. Tofauti yake ya kutoamini na ile ya Mariamu ni kubwa kiasi gani! Mariamu alisema, "Tazama mimi ni mjakazi wako Bwana, iwe kama usemavyo." Luka 1:38. Kuzaliwa kwa mwana wa Zakaria, kama vile kuzaliwa kwa mwana wa Ibrahimu, na kwa Mariamu kulikusudiwa kutoka fundisho kubwa. Kwamba: lile tusiloweza kulifanya sisi hufanywa [47]
kwa uwezo wa Mungu ndani ya kila mtu anayeamini. Kwa njia ya imani, mwana aliyeahidiwa alizaliwa. Kwa njia ya imani uwezo wa kiroho hupatikana. Na sisi huwezeshwa kufanya kazi ya haki.

Miaka mia tano iliyopita, malaika Gabriel alikuwa amemjulisha Daniel unabii unaoendelea mpaka kwa kuzaliwa kwa Kristo. Kule kujua kuwa wakati wa kuja kwa Kristo kumekaribia, ndiko kulimfanya Zakaria aombe kuhusu kutokea kwa Masihi kudhihirike Sasa malaika yule yule aliyetoa unabii huu amekuja ili akutangaze kutimia kwake.

### Zakaria aliona shaka

Zakaria aliona shaka kwa neno la malaika. Kwa hiyo alipigwa kuwa bubu mpaka kuzaliwa kwa mtoto. Malaika alisema: "Angalia utakuwa bubu mpaka kuzaliwa kwa mtoto, kwa sababu hukuyasadiki maneno yangu, ambayo yatatimia kwa wakati wake." Katika huduma hii, ilikuwa kazi ya kuhani kuomba kwa ajili ya kusamehewa, na kwa ajili ya kuja kwa Masihi, lakini Zakaria alipojaribu kufanya hivyo, hakuweza kutamka neno. Alipotoka mahali patakatifu uso wake ulikuwa unang'aa kwa utukufu wa Mungu, na watu walidhani kuwa ameona njozi humo hekaluni. Zakaria alibaki kuwa bubu, ila alizungumza na watu kwa njia ya ishara tu, kuwaeleza mambo aliyoona na kusikia humo hekaluni.

Baada ya kuzaliwa mtoto aliyeahidiwa, ulimi wake ulifunguliwa. Mambo haya yote yalienea katika nchi yote ya Yuda, na wote walioyasikia waliyaweka katika mioyo yao, huku wakisema, "Mtoto huyu atakuwaje?" Mambo haya yote yahelekeza juu ya kuja kwa Masihi.

Roho Mtakatifu alimjaza Zakaria, naye akatabiri kuhusu kazi ya mwanae itakavyokuwa: "Wewe mtoto utaitwa nabii wake Aliye Juu, Maana utatangulia m bele ya Bwana ili kutayarisha njia yake. . . . Kutoa maarifa ya ukombozi kwa watu wake kwa njia ya kuondolewa dhambi zao."

Mtoto akakua, akawa na nguvu rohoni, naye akawa jangwani mpaka siku ya kutokea kwake kwa Israeli." Mungu alimkabidhi mwana wa Zakaria, kazi kubwa nmo, ambayo haijakabidhiwa kwa mtu yeyote. Na Roho wa Mungu atakuwa pamoja naye ikiwa atafuata maelekezo ya malaika.

Yohana alipaswa kuwaletea watu mwanga wa Mungu. Lazima awahakikishie haja yao ya kutaka haki ya Mungu. Mjumbe wa jinsi
[48] hiyo lazima awe mtakatifu, awe hekalu la Roho ya Mungu. Lazima

awe na afya kamili, yaani afya ya mwili, ya roho, na ya mawazo. Kwa hiyo itampasa kutawala uchu wa chakula na tamaa.

Siku za Yohana mbatizaji, choyo cha kutajirika, na hali ya kupenda raha, na kujionyesha, ilikuwa imeenea sana. Tamaa ya mwili, ulevi, na kujifurahisha kwa sikukuu, vilidhoofisha mwili, na kudumaza mawazo, na kuelekeza mwili katika ufisadi. Katika hali ya kawaida, na mavazi ya kawaida tu, angekemea anasa na ufisadi wakati wake. Hayo ndiyo maelekezo malaika aliyoleta kutoka mbinguni.

Katika utoto wake na ujana wake, lazima ajizoeze kujitawala, na kuwa na uwezo kamili. Mazoea yanayopatikana tangu utotoni, ndiyo yatakayokuwa wakati wa utu uzima, kama atashinda, au atalegealegea. Ujana ni wakati wa kupanda mbegu, baadaye itaonekana aina ya mavuno yatakayotokea, katika maisha ya sasa na yale yajayo.

Katika kutayarisha njia kwa ajili ya kuja kwa Kristo mara ya kwanza, Yohana alikuwa mjumbe na kielelezo cha watu wanaotayarisha watu kwa ajili ya kurudi kwake Kristo mara ya pili.

Ulimwengu umezama katika anasa. Makosa na hadithi ni tele. Wote wanaojiandaa katika kumcha Mungu lazima wajifunze kuwa na kiasi, na kujitawala. Soma 2 Wakorintho 7:1. Uchu wa chakula pamoja na tamaa, lazima vitekwe nyara, na kutawaliwa na uwezo mkuu. Mawazo yatiishwe. Kujitawala kuwa ni kwa lazima, ndiko kutatuwezesha kuelewa na kutenda mambo ambayo ni sawa na kweli ya Mungu; kama neno lake lilivyo.

## Elimu ya Yohana isiyo ya kawaida

Kwa kawaida mwana wa Zakaria angalipata elimu yake katika shule za walimu wa Kiyahudi yaani walimu wa kawaida wa Israeli. Lakini kwa vile elimu hiyo isingaifaa katika kazi atakayofanya, Mungu alimpeleka jangwani, ili apate kujifunza kazi ya Mungu ya uumbaji.

Yohana aliishi katika hali ya upweke katika vilima na vichaka na mapango, na miamba. Katika hali hii, alijiendeleza katika mazingira ya kawaida tu na ya kujinyima. Hapa ndipo angejifunza somo la viumbe na mafunuo, pamoja na mambo ya riziki. 'Tangu utoto wake alielekezwa juu ya kazi yake na wazazi wake waaminifu. Naye

alikubaliana na maelekezo hayo. Maisha ya jangwani katika hali ya upweke, yalimtenga mbali na jamii ya watu, ambako kuna ufedhuli
[49] na machafuko ya kila hali. Alikaa mbali na mashindano ya mivuto ya dhambi.

Lakini maisha ya Yohana hayakuwa ya kujitesa na kujinyima mambo ya lazima. Kila mara alikuwa katika makundi ya watu wengine, na kuona mambo yanavyoendelea ulimwenguni. Akifunzwa na Roho Mtakatifu alichungua maisha ya watu, ili ajue jinsi ya kuwafikia, na kuwapa ujumbe wa mbinguni. Mzigo wa kazi yake ulikuwa juu yake daima. Kwa njia ya maombi sana, alijitia kazini kamili.

Ingawa aliishi jangwani hakujiepusha na majaribu. Mwovu Shetani alimshambulia kwa majaribu ya kila nanma pia. Lakini hali yake ilikuwa safi tu. Na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu aliweza kung'amua na kushinda hila za Shetani.

Yohana alifungwa na kujazwa na kuwako kwa Mungu, kama Musa alivyokuwa katika milima ya Midiani. Katika makao yake ya upweke jangwani, na giza la mwituni, Yohana aliweza kuona hali ya maisha ya Waisraeli dhahiri. Shamba la Bwana la mzabibu limeharibika kabisa. Lakini hali hiyo ya matatizo, ahadi ya Mungu kama upindi wa mvua hutia tumaini. Akiwa peke yake katika giza la usiku, alisoma na kujikumbusha ahadi ya Mungu na Ibrahim, kwamba uzao wake utakuwa mwingi kama nyota za mbinguni. Mapambazuko ya asubuhi yalimwambia kuwa; ni nani atakayekuwa kama "mapamazuko ya asubuhi, wakati jua lichomozapo, na asubuhi bila mawingu." 2 Samweli 24:4. Na katika mng'ao wa mchana aliona utukufu wakati "utukufu wa Bwana utakapofunuliwa na wenye mwili wote watakapouona pamoja." Isaya 40:5. Kwa kicho na unyenyekevu alichunguza katika maandiko ya unabii kuhusu kuja kwa Masihi. Shilo ataonekana kabla mfalme hajakoma kutawala katika kiti cha enzi cha Daudi. Sasa wakati umefika. Mtawala wa Kirumi amekaa katika jumba la kifalme katika mlima wa Sayuni. Kwa neno la hakika la Bwana, Kristo alikuwa amezaliwa.

### Isaya afafanua maneno

Mafafanuzi ya Isaya kuhusu ufalme wa Masihi, ndiyo yalikuwa majifunzo yake aliyokuwa akichunguza mchana na usiku. Soma

Isaya 11:4; 32:2; 62:4. Moyo wa mtu aliyekaa katika hali ya upweke, uliyafurahia sana mafundisho ya ufunuo wa utukufu ujao. Alimtazama Mfalme katika uzuri wake, naye alijisahau mwenyewe. Aliuangalia utukufu wa utakatifu, naye alijiona kutofaa kitu. Alikuwa tayari kwenda kama mjumbe wa mbinguni na asiyefaa machoni pa [50]
mbingu. Aliweza kusimama mbele ya wafalme wa duniani bila hofu, kwa sababu ametumwa na Mfalme Mkuu. Mfalme wa wafalme.

Yohana hakufahamu kamili aina ya ufalme wa Masihi, lakini alitumaini kuwa atasimamisha ufalme wa haki kulikofanya taifa la Israeli kuwa taifa takatifu.

Aliwaona watu wake wakiridhika, na wakilala katika dhambi zao. Ujumbe aliopewa na Mungu ulipaswa kuwaamsha na kuwafanya kutaharuki. Kabla mbegu ya Injili haijapandwa kwao, lazima kwanza mioyo yao kulainishwa. Kabla ya kutafuta dawa ya kuponya kwa Yesu, lazima kwanza waamshwe na kuona hatari inayowakabili kutokana na majeraha ya dhambi.

Mungu hatumi wajumbe wake kupeleka ujumbe kwa watu, ili kuwatumbuiza, na kuwatuliza, wakae asiwasi, bali huwaonveshei utisho wa kuzidi kuishi dhambini. Malaika hudhihirisha adhabu za Mungu wazi, ili kuwafanya watu waone haja ya kutubu na kuepuka adhabu hizo. Kisha mkono ule uliotubisha watu, hutuliza tena.

## Ukingoni mwa Mapinduzi

Wakati huduma ya Yohana ilianza taifa la Israeli lilikuwa ukingoni mwa mapinduzi, yaani uasi mkuu. Arkelao mfalme, alipoondolewa, Uyahudi ilikuwa imewekwa katika utawala wa Kirumi moja kwa moja.

Udhalimu wa watawala wa Kirumi, na juhudi zao za kutaka kuingiza desturi za kishenzi katika Israel zilichochea chuki kubwa sana, iliyokuwa imenyamazishwa kwa njia ya kumwaga damu nyingi ya mashujaa wa Israeli.

Katika hali ya mvurugano na mashindano hayo, sauti ilisikika jangwani, ambayo ni kali, ya kushtusha, lakini imejaa tumaini, ikisema, “Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.” Sauti hiyo ilistua watu, maana ilikuwa na uwezo mpya. Hili lilikuwa tangazo kwamba, kuja kwa Kristo kumekaribia. Yohana alikemea dhambi kwa uwezo wa nguvu za Eliya. Maneno yake yalikuwa

dhahiri, yenye nguvu. Taifa lilitaharuki. Makundi ya watu walifurika kwenda jangwani.

Yohana aliwaita watu watubu. Waliwabatiza katika maji ya mto wa Yordani, kama dalili ya nje ya kutubu dhambi. Alisema kuwa watu wanaojiita kuwa wana wa Mungu, wana dhambi. Wasipotakaswa mioyoni mwao, hawatakuwa na sehemu katika ufalme wa Masihi.

Wakuu, askari, walimu wa Kiyahudi, watoza ushuru, na wakulima wote walikuja kumsikia nabii. Watu wengi walitubu
[51] na kubatizwa ili wapate kushiriki katika ufalme, na sasa siri za maovu yao zimefunuliwa. Lakini Yohana aliona kuwa watu wengi hawakuwa na maungamo ya kweli, bali walikuwa nusunusu. Walijipendekeza kwa nabii, ili washiriki katika ufalme wa Masihi. Na kwa kubatizwa kwao walidumu dhambini, huku wakiheshimiwa na watu.

### Maonyo makali ya Yohana kwa wanafiki

Yohana aliwakabili akiwa na maneno machungu haya: "Ninyi wazao wa nyoka, Nani aliyewaonya mwikimbie adhabu ijayo? Zaeni basi matunda yapasayo toba. Wayahudi wamejitenga mbali na Mungu, walikuwa wakiteseka na adhabu zake. Hii ndiyo ilisababisha watekwe na mataifa ya kishenzi. Kwa kuwa zamani Mungu aliwafanikisha, ndiyo sababu walidumu dhambini, huku wakidhani kuwa wangali Wapenzi wa Mungu. Walijivuna bure kwamba wao ni bora kuliko mataifa mengine; ndiyo sababu wanafanikiwa.

Yohana aliwaambia walimu wa Israeli kuwa kiburi chao, na uchoyo wao na ukatili wao, vimewafanya kuwa watu wa laana. Kufuatana na nuru yao, walikuwa bora kuliko wengine kama Mungu alivyowaagiza. Lakini sasa ni wabaya kuliko wengine. Mungu hawatumaini kutimiza kusudi lake tena. Mungu ataita wengine wafanye kazi yake.

Nabii alisema: "Sasa shoka limewekwa chini ya mti: kila mti usiozaa matunda mazuri, utakatwa na kutupwa motoni." Ikiwa matunda ni mabaya, jina la mti haliwezi kuuokoa usiharibiwe. Yohana aliwaambia. Wayahudi kuwa, kama tabia zao hazipatani na amri za Mungu, wao sio wa Mungu kamwe.

Alisema, "Watakaohesabiwa kuwa raia wa ufalme wa Kristo, wataonyesha imani yao kama ushahidi. Wema, na haki vitaonekana katika maisha yao, Watawahudumia wahitaji, watawakaribisha wasiokuwa na makao, na wataonyesha mfano mwema wa utawa na unyofu.

"Mimi nawabatiza kwa maji, kwa ajili ya toba, lakini yeye ajaye nyuma yangu, ni mkuu, kuliko mimi, ambaye mimi sistahili hata kulegeza kamba za viatu vyake. Yeye atawabatiza katika Roho na kwa moto." Isaya alikuwa amesema: "Bwana atawatakasa watu wake kwa Roho ya hukumu, na kwa Roho ya kuteketeza." Isaya 4:4. Kwa wote watakaokubali uwezo wake, roho wa Mungu atateketeza dhambi. Waebrania 12:29. Lakini watu wakiambatana na dhambi, Roho wa Mungu ateketezaye dhambi, atawateketeza wao. Wakati wa kurudi mara ya pili kwa Kristo, waovu wote watateketezwa na kuangarnizwa; kwa pumzi ya kinywa chake na kwa mng'ao wa kufunuliwa kwake. 2 Wathesalonike 2:8. Utukufu wa Mungu ulelao uzima kwa watakatifu, utawateketeza waovu. [52]

Siku za Yohana Mbatizaji, Kristo alikuwa karibu kutokea, ambaye ni sura ya Mungu, na tabia yake. Kuwako kwake kutadhihirisha dhambi za watu. Wasipokubali kuondolewa dhambi zao hawatakuwa washiriki wa ufalme wake. .

Hivyo ubatizo ulieleza ujumbe wa Mungu kwa Israeli. Watu wengi walitubu, wakaacha vyote ili wapate kutii. Watu wengi walimdhania kuwa ndiye Masihi. Lakini Yohana alipoona watu wengi wakimjia, alifanya kadiri awezavyo kuwaelekeza kwa yule ajaye.

[53] # 11 — Ubatizo wa Yesu

Ujumbe wa nabii wa jangwani ulifika mpaka milimani, wakaapo wakulima, na mpaka baharini kwenye wavuvi. Watu hawa wanyenyekevu waliamini. Katika Nazareti ilisemwa kwamba, Yusufu, Seremala na mmoja ambaye ndiye Yesu walimwamini ujumbe. Wakati wa Yesu umekuja. Alimwaga mamaye, akajiunga na wengine kwenda huko Yordani kwa nabii.

Yesu na Yohana mbatizaji walikuwa binamu, yaani ndugu kwa baba au kwa mama walakini walikuwa hawajaonana. Na sasa mambo yamewakutanisha. Muda ulikuwa haupo wa kukabiliana kama huu.

Yohana alikuwa na habari za kuzaliwa kwa Kristo, na hali yake ya maisha safi bila dhambi. Alimwamini kuwa ndiye Masihi. Lakini kwa kuwa Yesu hakujidhihirisha wazi, bali alikuwa katika hali ya ukimya, jambo hili lilitia wasiwasi na mashaka kumhusu. Walakini ubatizo ulingojea wenye imani. Ilijulishwa kwa Yohana kuwa Masihi atakuja kwake ili ambatize, na itakuwa ndiyo mwanzo wa kazi yake.

Yesu alipokuja kwa Yohana ili abatizwe, Yohana aliona utawa kwake, ambao hajawahi kuona hali kama hiyo kwa mtu yeyote. Kuwako kwake kulikuwa kwa hali ya kicho cha ajabu. jambo hili lilipatana jinsi alivyofunuliwa kabla, kumhusu Masihi. Sasa, inakuwaje yeye awe mwenye dhambi, hata ahitaji ubatizo? Inakuwaje kwake asiye dhambi ahitaji ubatizo wa kuoshwa dhambi?

Wakati Yesu alipotaka kubatizwa, Yohana alisema: Mimi ndiye ninahitaji kubatizwa na wewe, na wewe waja kwangu? Lakini Yesu alimjibu, Acha mambo hayo, maana hivyo ndivyo itakuwa kutimiza sheria. Basi akaacha. Kisha Yesu alipobatizwa, alitoka majini mara
[54] moja, na tazama, mbingu zilifunguliwa, akashuka Roho wa Mungu, kama njiwa, akamkalia.

### Kristo asiyekuwa na dhambi, abatizwa

Yesu hakubatizwa kwa kuungama makosa yake, kana kwamba anayo, bali alijifanya kama mwenye dhambi sawa na sisi, akichukua hatua zile zile tunazochukua sisi. Maisha yake ya taabu na uvumilivu wake, baada ya ubatizo, vilikuwa kielelezo kwetu.

Yesu alipotoka majini, alipiga magoti kuomba kando ya mto. Alikuwa sasa anaingia katika mapambano makubwa maishani mwake. Ingawa alikuwa Mkuu wa wakuu kuja kwake ni kama upanga uliochomolewa alani. Ufalme ambao atasimamisha, ni tofauti na ule Wayahudi wanaotamani. Ataonekana kana kwamba yeye ni mvunja sheria na mharibu wa mambo ya Israeli, ambaye atashutumiwa kama mwasi, na kutukanwa kama Belizebuli. Hakuna mtu aliyemwelewa, kwa hiyo itampasa aishi maisha ya upweke. Mamaye na nduguze hawakuelewa na kazi yake. Hata wanafunzi wake pia hawakuelewa.

Kama mmoja wetu, lazima achukue maovu yetu na matatizo yetu yote. Mtakatifu asiyekuwa na dhambi, lazima apate aibu ya dhambi. Mpenda amani lazima akae kwenye mashindano, mwenye ukweli lazima akae katika uongo na udanganyifu. Msafi, akae kwenye machukizo na uchafu, kila dhambi, kila ufedhuli, kila uchafu vyote viwe fungu lake, kana kwamba ni vyake hasa.

Lazima aitembelee na yeye mwenyewe. Kwake yeye aliyepokea hadhi ya kuwezesha ukombozi wa wanadamu, lazima autimize kikamilifu. Alijisikia kuwa na mzigo mzito mno, lakini alidumu kuwa imara.

Mwokozi alitoa moyo wake wote katika sala. Alijua jinsi dhambi ilivyokomaza mioyo ya watu, alijua jinsi ilivyo vigumu kwa watu kutambua kazi yake na kuikubali. Alimwomba Baba awalainishe wapate kuamini. Avunje pingu ambazo Shetani amewafunga, na apate kumshinda. Hakuna wakati ambao malaika walisikiliza sala yoyote kama hiyo. Baba mwenyewe ataijibu sala ya Mwanawe. Mbingu zilifunguka, nuru ya ajabu ikiwa mfano wa njiwa ikamshukia Yesu.

Waliokuwako hapo Yordani, ni wachache sana waliofahamu njozi hiyo, isipokuwa Yohana mbatizaji tu. Lakini hali ya kicho cha mbinguni iliwakalia wote waliokuwapo pale. Kristo aliyekuwa akielekeza uso mbinguni alitukuzwa kwa ajabu ambayo watu hawajaona, uso wa mtu uking'aa hivyo. Kutoka mbinguni, sauti ilisikika [55]

ikisema: "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye."

## Mbingu yatia Sahihi

Maneno hayo yalisemwa ili kuimarisha imani ya wale walioona jambo hilo, na kumtia moyo Mwokozi kwa kazi yake. Ingawa uovu wa dhambi ya ulimwengu uliwekwa juu ya Kristo, ingawa amejidhili kiasi hicho, sauti kutoka mbinguni ilimtaja kuwa Mwana wa Mungu wa milele.

Yohana alishangaa sana. Kwa vile utukufu wa Mungu ulivyomzunguka Yesu, na sauti kutoka mbinguni ilisikika. Yohana alijua kuwa huyu ndiye Mwokozi wa ulimwengu ambaye amembatiza. Halafu akinyosha mikono yake kuelekea kwa Yesu, alipaza sauti na kusema, "Tazama Mwana Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Hakuna mtu, hata msemaji mwenyewe, aliyefahamu umuhimu wa maneno hayo, yaani "Mwanakondoo wa Mungu. Watu wengi wa wana wa Israeli walihesabu kafara walizokuwa wakitoa, kama wakafiri wanavyozihesabu, yaani ni kafara za kumfurahisha Mungu ili awajalie. Mungu alikusudia kuwafundisha kuwa kutokana na kipaji chake cha upendo waweze kupatanishwa kwake.

Maneno yaliyosemwa kwa Yesu, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa, ninayependezwa naye," yaliwakumbatia watu wote kwa Mungu. Sote tukiwa na dhambi na takataka zote, Mungu hatutupi kama vitu ovyo. Ametupokea kwa njia ya Mwana wake. Waefeso 1:6.

Utukufu uliomwangukia Kristo, ilikuwa thibitisho la upendo wa Mungu kwetu. Hutuambia uwezo wa maombi, jinsi maombi ya wanadamu yanavyofika katika sikio la Mungu, na sala zetu zinavyokubalika katika mbingu. Nchi ilitengwa na mbingu kwa ajili ya dhambi, lakini Yesu ameiunganisha tena kwa njia ya sala, ya utukufu. Nuru iliyomwangukia Yesu, hata sisi itatuangukia tunapoomba ili tushinde majaribu. Sauti iliyosema kwa Yesu, husema kwa kila mwamini, kwamba, 'Huyu ni mtoto wangu mpendwa, ninayependezwa naye."

Mwokozi wetu amefungua njia, ili mtu mwenye dhambi hasa, maskini, adharauliwaye, apate kamfikia Baba. Wote waweze kupata makao katika yale ambayo Yesu amekwenda kuwaandalia.

## 12 — Majaribu [56]

"Ndipo Yesu alipoongozwa na Roho mpaka jangwani, ili apate kujaribiwa na shetani. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, baadaye aliona njaa."

Yesu hakujitia majaribuni mwenyewe. Alikwenda jangwani ili akae peke yake, apate kutafakari juu ya kazi yake Alikuwa akijifikiria na kujikaza kuhusu njia ngumu ya hatari, ambayo ataiendea. Lakini Shetani alidhani kuwa huo ndio wakati mzuri wa kumkabili.

Matokeo makubwa yalikuwa hatarini. Shetani alidai kuwa dunia hii ni mali yake, na yeye mwenyewe hujiita "Mtawala wa ulimwengu." Husema kuwa watu wamemchagua awe mtawala wao. Kwa ajili hiyo amepata utawala wa ulimwengu. Kristo alikuja ili kuyakanusha madai hayo. Kristo atadumu kuwa mwaminifu kwa Mungu, akiwa katika hali ya binadamu. Hivyo itaonyesha kuwa Shetani hakuutawala ulimwengu kamili, na madal yake kuwa ni mfalme wa ulimwengu, ni uongo. Wote wanaotamani kutolewa mikononi mwake watafunguliwa.

Shetani aliiua kuwa hakuutawala ulimwengu kamili. Ulionekana uwezo katika wanadamu unaoupinga utawala wake. Soma Mwanzo 3:15. Katika kafara iliyotolewa na Adamu na wazao wake, ilionekana alama ya kuongea kati ya dunia na mbingu. Shetani alijitia kati kuzuia mawasiliano haya. Alimtaja Mungu vibaya na kueleza kinyume juu ya mifano iliyokuwa ikimwelekeza mwokozi. Watu walimwogopa Mungu kama mwenye kufurahia maangamizi yao. Kafara ambazo zingalionyesha upendo wake, zilipotoshwa na kufanya kuwa kumfurahisha Mungu ili awahurumie. Sura hii imeandikwa katika Mathayo 4:1-ll; Marko 1:12, 13; Luka 4:1-13, Wakati Neno la Mungu lilipotolewa, Shetani alijifunza unabii. Toka kizazi mpaka kizazi, alijitahidi kuwapofusha watu ili wamkane Kristo na kuja kwake.

Wakati wa kuzaliwa kwa Kristo, Shetani alijua kuwa amekuja [57]
atakayepinga utawala wake. Kwamba Mwana wa Mungu angekuja ulimwenguni kama mtu mwenye uwezo wa kukamata na

kuangamiza. Roho yake ya ubinafsi isingeweza kufahamu upendo huo. Kwa kuwa mwenyewe amekosa kuishi mbinguni, aliazimia kuwapotosha wengine, ili washiriki ajali yake. Alitaka kuwafanya watu wadharau mambo ya mbinguni, ila wathamini mambo ya dunia tu.

### Shetani alikusudia kufaulu

Tangu wakati ule Amiri jeshi wa mbinguni alipokuwa angali mtoto mchanga katika Bethlehemu, alikuwa katika mashambulio ya Shetani, Katika kikao cha Shetani iliazimiwa kuwa, lazima washinde. Majeshi ya malaika waovu walipangwa katika njia zote za Yesu ili kumpinga, na ikiwezekana kumshinda.

Katika ubatizo wa Yesu Shetani alisikia sauti ikishuhudia Uungu wa Yesu, kutoka kwa Yehova. Na sasa Yesu amekuja katika umbo la mwili wa dhambi, (Warumi 8:3). Baba mwenyewe alizungumza. Kwanza alisema na watu katika Kristo, sasa anasema nao katika hali ya kibinadamu ndani ya Kristo. Sasa ilidhihirika wazi kuwa mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu yamekamilika. Sasa Shetani aliona kuwa lazima ashinde au ashindwe. Juhudi zote za uasi zilitumika kumpinga Kristo.

Watu wengi waliangalia mashindano haya baina ya Kristo na Shetani kuwa ni jambo lisilowahusu. Lakini katika kila moyo wa mwanadamu, mashindano hayo yanahusika. Mitego na majaribu ambayo Yesu alishinda, ndiyo yanayotushinda leo. Yesu akiwa na nzigo wa dhambi za ulimwengu juu yake, alishinda jaribu la tamaa ya chakula, na la upendo wa dunia, na la kujionyesha ambako ni majivuno na kiburi. Majaribu hayo ndiyo yaliyomshinda Adamu na Hawa na ndiyo yanayotushinda sisi.

Shetani huonyesha kushindwa kwa Adamu kuwa ndio ushahidi wa kuthibitisha kwamba sheria ya Mungu haiwezekani kutiiwa. Katika hali ya kibinadamu Kristo alikukomboa kuanguka kwa Adamu. Lakini Adamu aliposhambuliwa na mjaribu, hakukuwa na laana ya dhambi kwake. Alikuwa mtu mkamilifu kabisa, mwenye mawazo kamili na mwili wa nguvu. Akizungukwa na utukufu wa Mungu, alikuwa akiwasiliana na viumbe wa mbinguni.

Haikuwa hivyo kwa Yesu alipokwenda jangwani kupambana na Shetani. Kwa muda wa miaka 4000 watu walikuwa wamed-

hoofishwa na dhambi kimwili na kiroho pia. Kwa hiyo walikuwa katika hali mbaya mno. Na Kristo alichukua maovu yao yote. Kwa [58] njia hiyo aliweza kumwokoa mtu yeyote, hata yule aliyezama dhambini mno.

### Alichukua Hali zote za kibinadamu

Watu wengi hudai kuwa haikuwezekana kwa Yesu kushindwa na majaribu ya Shetani. Kwamba hakuwa katika hali aliyokuwamo Adamu, wala hakuweza kushinda katika hali kama hiyo. Tungejua hali ya kutisha aliyokuwamo Kristo ndipo tungefahamu kuwa anatupita. Alichukua hali zote za ubinadamu pamoja na hali ya kushindwa na majaribu. Sisi hatuna udhuru wa jambo lolote ambalo Kristo hakukutana nalo, na kufaulu.

Kama kwa Kristo sawa na kwa wazazi wetu katika Edeni, jaribu la uchu wa chakula, lilikuwa la kwanza kutajwa. "Alipokwisha kufunga siku arobaini mchana na usiku akaona njaa. Na mjaribu alipomjia, alisema, Kama wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mkate."

Maneno haya ya kwanza yaliisaliti tabia yake. "Kama wewe ni Mwana wa Mungu." Hilo lilikuwa neno la kutoamini lililopenyezwa hapo. Kama Yesu angefanya maneno aliyosema Shetani angelikubali neno la mashaka lililotolewa na Ibilisi. Shetani alifikiri kuingiza neno katika mawazo ya Hawa neno la shaka kuhusu tunda zuri, liwe kinyume cha vile Mungu alivyosema juu yake. Hivyo ndivyo mjaribu alivyofanya kuleta hila yake: akasema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu." Katika sauti yake kulikuwa na mashaka kabisa. Je, Mungu angemwacha Mwanawe akae katika jangwa kati ya wanyama, bila chakula, wala maji? Alipenyeza neno la mashaka kwamba Mungu asingalifanya namna hiyo, kwa hiyo alisema, "kama wewe ni Mwana wa Mungu", onyesha uwezo wako, kwa kuyaamuru mawe haya yawe mkate.

### Jaribu la kutia shaka

Neno lililotoka mbinguni, kwamba "Huyu ni Mwanangu mpendwa, lilikuwa lingali likisikika katika masikio ya Shetani. Lakini aliazimia kumpata Yesu asiliamini neno hilo. Neno la Mungu

lilikuwa thibitisho la kazi ya Kristo kuwa ni ya mbinguni, maana neno hilo lilionyesha ushikamano wake na mbinguni. Ushikamano wa Kristo na mbingu ulikuwa imara usio tikiswa. Shetan alijua kuwa hawezi kumshinda Kristo. Alidhani kuwa kwa njia ya njaa na kukata tamaa, Kristo atakubali kutia shaka juu ya Babaye, na kufanya miujiza yeye binafsi. Kama angalifanya hivyo mpango wa wokovu ungalivunjika kabisa.

[59] Shetani alitegemea silaha yake kuu, malaika aliyefukuzwa kutoka mbinguni. Kuonekana kwa Yesu kulikuwa kama malaika aliyefukuzwa mbinguni na kudharauliwa na wanadamu. Basi mwenye asili ya Uungu angeonyesha uwezo wake kwa kufanya miujiza. "Kama wewe ni Mwana wa Mungu amuru mawe haya yawe mkate." Shetani alisema kuwa kwa kutenda miujiza, kungekuwa uthibitisho wa Uungu wake. Basi mashaka yangekoma.

Lakini Mwana wa Mungu asingemhakikishia Shetani Uungu wake. Kama Kristo angekubali mashauri ya Shetani, angelimwambia amwonyeshe ishara ya kuthibitisha kuwa yeye ni Mwana wa Mungu. Kristo asingetumia uwezo wa Uungu kwa kujiagiza. Amekuja kukabili mambo tunayokabili sisi, ili awe kielelezo chetu. Kazi zake za ajabu zote zilikuwa kwa ajili ya wengine. Akitiwa nguvu na ile sauti ya mbinguni, Yesu alitegemea neno la Baba tu.

Yesu alikabiliana na Shetani kwa maandiko. "Imeandikwa". Silaha yake ilikuwa maandiko. Shetani alidai Yesu afanye mwujiza. Lakini mwujiza mkuu kuliko yote ni "Hivyo ndivyo asemavyo Bwana." Kristo aliposhikilia silaha hiyo, Shetani hakuwa na njia nyingine, ya kumweza.

Wakati wa udhaifu mkuu, Kristo alishambuliwa na majaribu makali mno. Hivyo ndivyo Shetani anavyowatendea watu. Hesabu 20:1-17; 1 Wafalme 19:114. Mtu anaposhindwa na wasiwasi, au matatizo mengine, au ufukara, Shetani huwa tayari kushambulia. Hutushambulia kwenye hali zetu za udhaifu. Hutumaini kutudhoofisha na kututenga na Mungu. Lakini tukikabiliana naye kama Yesu alivyofanya, tutaepukana na kuanguka kwingi.

Kristo alimwambia mjaribu, "Mtu haishi kwa mkate peke yake, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Katika jangwa kwa muda wa miaka elfu moja na mia nne iliyopita, Mungu alituma watu wake kuwalisha na chakula kutoka mbinguni. Jambo hili liliwafundisha kuwa kama wakimtumaini na kuenenda katika

maagizo yake, hawezi kuwaacha. Kwa neno la Bwana Waebrania walilishwa huko jangwani. Na kwa neno hilo hilo Yesu alilishwa. Alimgojea Mungu ampe mahitaji yake kwa wakati wake. Asingepata chakula kwa kushauriwa na Shetani. Ni vizuri kuteseka kwa vyo vyote kuliko kujitenga na neno la Mungu.

Mfuasi wa Mungu, mara kwa mara hufika mahali ambapo huonekana kuwa, kama akiambatana na mapenzi ya Mungu hatapata riziki yake. Shetani humfanya aamini kuwa kwa njia ya kujitenga na mapenzi ya Mungu kutamsaidia. Lakini jambo moja tu tuwezalo [60]
kutumaini ni uwezo wa neno la Mungu. Hatuwezi kufuata mashauri ya Shetani kuwa tukijenga neno la Mungu tutapungukiwa na riziki zetu. Lazima tushike amri yake na kuamini ahadi zake.

Katika mashindano makuu ya mwisho pamoja na Shetani, wale wanaomtegemea Mungu, wataona kuwa mahitaji yao yanaondolewa, kwa sababu wanakataa kuvunja amri za Mungu. Watakatazwa kuuza na kununua. Soma Ufanuo 13:11-17. Lakini kwa watiifu wa amri za Mungu wamepewa ahadi, "Huyu ndiye atakayekaa juu, majabali ni ngome yake, atapewa chakula chake, maji yake hayatakoma." Isaya 33:16. Wakati nchi itakapoangamizwa na njaa, yeye atalishwa. Zaburi 37-19

## Udhalimu bila Kiasi

Katika vizazi vyote, majaribu ya mwili humharibu mtu, hasa kwa kutokuwa na kiasi. Na Shetani hufanya kazi kwa njia ya kuleta udhalimu na kuharibu uwezo wa akili, na kuwafanya watu wawe kama wanyama. Na kwa hiyo watu hupumbaa hata wasiweze kuthamini mambo ya milele. Kwa njia ya uasherati Shetani hutaka kung'olea mbali kila wazo lielekezalo kwa Mungu.

Kristo alisema kuwa kabla ya kuja kwake mara ya pili, hali ya ulimwengu itafanana na ile iliyokuwako kabla ya gharika, na ile ya Sodoma na Gomora. Kwetu sisi, fundisho la kufunga kwa Yesu, lazima lizingatiwe kwa makini. Kwa njia ya maumivu yasiyosemekana ya Kristo, ndiyo tutaweza kutambua na kupambanua ubaya wa kutokuwa na kiasi. Tumaini letu tu ni kuteka nyara uchu wa chakula na tamaa na kuvileta chini ya Kristo, na kupatana na mapenzi ya Mungu.

Kwa nguvu zetu wenyewe hatuwezi kushinda hali ya uasi, ambayo ni asili yake. Lakini kwa njia yakupita katika njia ya Yesu aliyotuandalia tutaweza kushinda. Yesu hatatuacha tuwe wenye hofu na kukata tamaa. Asema, Jipeni moyo mimi nimeushinda ulimwengu." Yohana 16:33.

Hebu mtu yule anayeshindana na uchu wa chakula amtazame Mwokozi huko jangwani katika majaribu. Mwangalie huko msalabani katika maumivu makuu huku akilia na kusema, "Nina kiu" Ushindi wake ni wetu pia.

Yesu alisema, "Mkuu wa ulimwengu huu anakuja, wala hana kitu kwangu." Yohana 14:30. Hakuna kitu kilichomhusu Shetani, ambacho Yesu alikuwa nacho. Hakushiriki katika dhambi. Hakukubaliana na dhambi ingawa kwa mawazo tu. Hivyo ndivyo itupasavyo na
[61] sisi tuwe. Ubinadamu wa Kristo uliungana na Uungu; aliwezeshwa kushindana kwa Roho Mtakatifu aliyekuwa akikaa ndani yake. Naye alikuja ili kutushirikisha na Uungu. Mkono wa imani wa Mungu unatushika na kutuongoza katika Uungu ulioko kwa Kristo, ili tupate ukamilifu wa tabia.

Jinsi jambo hili linavyotimilika, Kristo ametuonyesha. Je, Kristo alimshinda Shetani kwa njia gani? Alimshinda kwa njia ya Neno la Mungu. Alisema, "Imeandikwa." Kila ahadi iliyomo katika Neno la Mun,gu ni yetu. Soma 2 Petro 1:4. Ukichambuliwa na majaribu, tazama uwezo wa Neno. Uwezo wote wa Neno ni wako. Zaburi 119:11; 17:4.

## 13 — Ushindi [62]

“Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, kisha akamwambia: “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini, maana imeandikwa: Atakuagizia malaika zake wakulinde, na mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.”

Shetani alikuwa bado anaonekana kama malaika wa nuru. Alijionyesha kuwa anajua maandiko. Jinsi Yesu alivyotumia maandiko kumsaidia, ndiyo mjaribu huyu alivyoyatumia pia kukamilisha ukamilifu wake. Shetani alimdai Mwokozi aonyeshe ushahidi zaidi kwamba ni Mwana wa Mungu.

Lakini tena jaribu hili liliambatana na mashaka ya kutoamini: “Kama wewe ni Mwana wa Mungu.” Kristo, alijaribiwa, “Kama”, lakini yeye aliepuka kuonyesha mashaka ya kutoamini.

Shetani alitaka kumtegatega na kumshinda, kwa kuwa ni mwanadamu. Akamtaka ajionyeshe, yaani ajivune. Lakini ajapokuwa Shetani hushawishi ili tu atende dhambi, hawezi kumlazimisha mtu. Alisema, “Jitupe chini”, hali akijua kuwa hawezi kumtupa chini, wala kumlazimisha ajitupe chini. Kristo asipokubaliana na jaribu hilo, hawezi kulitimiza, ila atashinda.

Mjaribu hawezi kamwe kutulazimisha tutende dhambi. Dhamiri lazima ikubali, imani lazima ianguke kwa Kristo, ndipo Shetani hurumia hila zake juu yetu. Lakini kila aina ya tamaa tunayopendelea, ndiyo mlango tunaofungua ili mjaribu atuingilie kutuharibu. Na kila kushindwa kwetu tunakoshindwa, humdhihaki Kristo. Wakati Shetani alipotumia neno lile kwamba, Atakuagizia malaika, aliacha maneno yasemayo, “akulinde katika mapito yako yote”. Maana yake, wakulinde katika mapito yale yaliyoamriwa na Mungu. Yesu [63]
alikataa kwenda kinyume na maagizo ya Mungu. Kama angeruka, asingalitazamia hifadhi kumjia. Na hivyo asingalikuwa kiele kwa wanadamu.

Yesu alimwambia Shetani, “Imeandikwa tena Usimjaribu Bwana Mungu wako.” Mungu alikuwa ametangaza wazi kuwa yeye ni

Mwanawe. Sasa kutaka kithibitisho ni kulijaribu Neno la Mungu, yaani kumjaribu Mungu. Tusitoe maombi yetu kwa Mungu kwa kujaribu kuona kuwa atafanya au namna gani. Atafanya kama alivyosema kwa sababu anatupenda. Soma Waebrania 11:6. Majivuno ni maigizo ya Shetani kwamba ndiyo imani. Imani ni ile inayodai ahadi za Mungu, na huleta matunda ya utiifu. Majivuno pia hudai ahadi za Mungu, lakini huzitumia katika kuasi. Imani ingewaongoza wazazi wetu wa kwanza kuutegemea upendo wa Mungu, na kutii sheria zake; wakiamini kuwa pendo lake kuu litawaokoa kutoka dhambini. Hakuna imani inayodai fadhili za Mungu, bila kuambatana na masharti ambayo rehema za Mungu hutolewa.

### Kuthubutu kuingia katika Uwanja wa Shetani

Kama Shetani akiweza kutushawishi ili tuwe mahali pa majaribu bila lazima, ajua kuwa atashinda bila shaka. Mungu atalinda watu wote wanaokwenda katika maagizo yake; lakini kutofanya hivyo ni kujiingiza katika kiwanja cha Shetat. Mwokozi ametuagiza akisema, “Kesheni na kuomba, msije mkaingia majaribuni ” Marko 14:38.

Kila mara tunapojiingiza mahali pa majaribu, huwa na wasiwasi, kwamba Roho wa Mungu ndiye anayetuogoza. Lakini Roho ndiye alimwongoza Yesu jangwani. Mungu akituingiza mahali pa majaribu, huwa na kusudi jema kwetu. Yesu hakwenda kulingana na ahadi za Mungu, kwenda mahali alipokatazwa pa, majaribu, wala hakukata tamaa, majaribu yalipomkabili. Hata sisi inatupasa kuwal hivyo. Soma 1 Wakorintho 10:13; Zaburi 50:14, 15.

Yesu alikuwa mshindi katika jaribu la pili, na sasa Shetani alijidhihirisha alivyo, ingawa alikuwa malaika aliyeanguka. Alikiri wazi kuwa yeye ndiye kiongozi wa maasi, na ndiye mungu wa ulimwengu huu. Akimpandisha Yesu juu ya mlima mrefu, alifanya falme zote za ulimwengu kupita mbele yake kama sinema. Akaona nuru ikimulika juu ya miji na majumba yake, akamwonyesha mashamba mazuri yenye rutuba, na miti yenye matunda. Hali ya laana na uovu ilifichika. Macho ya Yesu yaliona mambo hayo mazuri yenye ku-
[64] fanikiwa. Halafu sauti ya mjaribu ilisikika ikisema, “Haya yote nitakupa. . . . Kama wewe utanisujudia” Mbele ya Kristo kulikuwa na maisha ya huzuni, hali ngumu, na mapambano, na kifo cha aibu. Kristo angalijiokoa na hali hiyo mbaya kwa kukubali

uku alioahidiwa na Shetani. Lakini kufanya hivyo kungalimletea kushindwa katika mapambano hayo. Je, Shetani atafaulu sasa? Ushindi utakuwa wa mwasi?

## Kristo asingeweza kununuliwa

Wakati mjaribu alipotoa ufalme wa ulimwengu kwa hari zake, alikusudia kuwa Kristo ashikiliwe chini ya Shetani. Huu ulikuwa ufalme ule ambao ulitumainiwa na Wayahudi. Wao walitamani ufalme wa dunia hii. Lakini Kristo alimwambia mjarilbu. "Nenda nyuma yangu, Shetani: maana imeandikwa, "Utamsujudia Bwana Mungu wako, yeye peke yake utamwabudu." Kristo asingeweza kununuliwa. Amekuja kusimamisha ufalme wa haki, naye asingeliacha kutimiza kusudi lake.

Shetani huwafikia watu akiwajaribu na jaribu hilo hilo, naye hufaulu sana kuliko kwa Kristo. Huwapa ufalme wa dunia hii kwa sharti moja, yaani wauache unyofu wao kwa Mungu, na kuukiri ukuu wa Shetani. Husema, chochote cha kuendesha maisha haya yawe na mafanikio, kifanye, ndiko kunitumikia. Mimi nitawapa utajiri, anasa, heshima, na furaha. Msichukuliwe na hali ya unyofu na kujikana nafsi.

Hivyo makundi ya watu hupendelea maisha ya anasa na ubinafsi, na Shetani huridhika. Lakini huwapa kitu ambacho sicho chake, ambacho kitatoweka mara. Badala yake huwapotosha wakaacha haki ya kurithi na kuwa wana wa Mungu.

## Shetani huduma kuwa Adui Aliyeshindwa.

Mwishoni Shetani alitambua kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Uungu ulipita katika ubinadamu. Shetani alipaswa kuondoka mbele yake, ambaye ni Mkombozi wa ulimwengu. Ushindi wa Yesu ulikuwa kamili, kama kushindwa kwa Adamu kulivyokuwa kamili.

Vivyo hivyo na sisi twapaswa kuyapinga majaribu, na kumdhalilisha Shetani atuache. Yesu alipata ushindi kwa njia ya utii kwa sheria ya Mungu, na imani imara kwa Mungu. Naye asema kwetu kwa njia ya mtume: 'Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atakimbia. Mkaribisheni Mungu, naye atawakaribia ninyi." Yakobo

4:7, 8. “Jina la Bwana ni mnara imara. Mwenye haki huukimbilia,
[65] akawa salama.” Mithali 10:10. Shetani hutetema wakati mtu dhaifu anapokimbilia kwenye jina hilo imara.

“Shetani alipoondo kwa Yesu, Yesu alianguka ameishiwa na nguvu zote, akiwa karibu kufa. Malaika walikuwa wakimtazama jemadari wao, alipokuwa akishindana na majaribu, ambayo ni makali mno, sisi hatuwezi kuyakabili. Sasa walimhudumia Mwana wa Mungu, alipokuwa akilala kama mtu anayekufa. Alitiwa nguvu na Mungu, akifarijiwa kuwa mbingu yote inashangilia ushindi wake. Alipozindukana tena, roho yake ikawaka kwa upendo, jinsi alivyowapenda watu; akaendelea kukamilisha kazi aliyokuja kuifanya, ambayo sasa ameianza, naye hatapumzika mpaka taifa la wanadamu limekombolewa.

Gharama ya ukombozi haitatambulikana kamwe, mpaka wakati waliokombolewa watakaposimama na Mwokozi mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Ndipo utukufu wa makao ya milele utakapofunuliwa katika akili zetu, na kushangaa kwa furaha, tutakumbuka ya kwamba Yesu aliacha yote kwa ajili yetu, na kwamba, kwa ajili yetu alijihatarisha hivyo kuwaokoa waliopotea milele, hapo tutapaza sauti tukiimba: “Anayestahili sifa na shukrani ni MwanaKondoo, aliyechinjwa, ndiye astahiliye kupokea uwezo, na utajiri, na hekima, na nguvu na heshima, na utukufu, na mibaraka.” Ufunuo 5:12.

## 14 — Tumemwona Masihi [66]

Wakati huu Yohana Mbatizaji alikuwa akihubiri huko Bethlehemu, kando ya mto wa Yordani. Mahubiri ya Yohana yalikuwa yamewaingia watu sana. Hakuwajali wakuu wa Sanhedrin wala hakutaka ruhusa kwao, walakini kazi yake ilipendeza sana, akaongeza kuifanya zaidi na zaidi.

Baraza la Sanhedrin lilihusika na makuhani, watawala na walimu. Wakati wa utawala wa Wayahudi, baraza la Sanhedrin ndilo lilikuwa baraza kuu la taifa, ingawa kwa wakati huu lilikuwa chini ya watawala wa Kirumi, lakini lilikuwa likihesabiwa kuwa ni baraza la mambo yahusuyo dini. Sanhedrin basi lisingeweza kuacha kuchunguza kazi ya Yohana. Wengine walitaja mafunuo yaliyokuja kwa Zakaria hekaluni, kuhusu mtoto wake kwamba ndiye Masihi aliyetangazwa. Mambo haya yaliwataharuki watu kuhusu kazi ya Yohana.

Muda ulikuwa umepita, tangu Waisraeli walipopata nabii. Madai ya kutaka watu watubu yalionekana kuwa mapya na ya kustusha. Waongozi wengi wasingekwenda kusikia ujumbe wa Yohana wasije wakafunuliwa siri za maisha yao. Walakini mahubiri yake yalikuwa ni matangazo ya Masihi.

Ilikuwa inaeleweka kuwa unabii wa Daniel wa majuma sabini, ulifunika na kuja kwa Masihi pia. Nao ulikuwa karibu kumalizika. Kwa hiyo walitazamiwa kushiriki katika ufalme wa utukufu kama walivyotazamia. Jambo hilo ndilo lililokuwa likiwatumainisha kwa uchangamfu. Na Sanhedrin ingepaswa kuukubali ujumbe wa Yohana au kuukataa. Mpaka wakati huo walikuwa na tatizo jinsi ya kuwatuliza watu, wasishughulike na mahubiri ya Yohana. Ili kufikia uamuzi fulani walituma wajumbe kutoka kwa makuhani na walawi wapate kwenda Yordani kwa Yohana, ambaye ni mwalimu mpya.

Wajumbe walipofika walikuta makutano wanasikiliza mahubiri [67]
ya Yohana. Walikuja wakijionyesha jinsi walivyokuwa maarufu, ili kusudi kufanya mvuto kwa watu, lakini watu waliwaona vivi hivi tu, ingawa walijionyesha jinsi walivyokuwa na fahari.

Watu wakuu wakiwa na mavazi rasmi., walisimama mbele ya Yohana na kusema: "Wewe ni nani?" Yohana akijua mambo yao, alisema: "Mimi siye Kristo." Nini basi, wewe ni Eliya?" "Mimi siye Eliya." "Je, wewe u nabii?" "La." Wewe u nani basi, ili tuwapelekee majibu waliotutuma?" "Wewe wajinena kuwa nani?" "Mimi ni sauti iliayo nyikani: Itengenezeni njia ya Bwana, yanyoosheni mapito yake," kama alivyosema Isaya.

Zamani mfalme alipotaka kutembelea nchi yake, watu walitumwa kwenda kutengeneza njia, mabonde yalijazwa, na kusawazisha mahali palipoharibika, ili mfalme apate kusafiri katila hali ya usalama. Hali hii imesemwa na nabii ' Isaya ili kuonyesha kazi ya Injili, "Kila bonde litajazwa na kila mahali palipoinuka patasawazishwa." Isaya 40:4. Roho wa Mungu anapomjaza mtu, kiburi chake hudhiliwa. Anasa za ulimwengu, cheo, na kujitukuza huonekana kuwa havina thamani yoyote. Kisha unyenyekevu, kujinyima, na upendo. Hayo ndiyo huonekana yenye thamani kwake. Hii ndiyo kazi ya Injili, ambayo Yohana alikuwa akifanya. Ndiyo ujumbe kwake.

Walimu wa Kiyahudi waliendelea kumwuliza: "Mbona unawabatiza watu, kama wewe siye Kristo, wala Eliya, au nabii?" Kusema nabii, kulimaanisha Musa. Wakati Yohana Mbatizaji alipoanza kazi yake, watu wengi walidhani kuwa ni Musa aliyefufuka toka ufuni. Iliaminiwa pia kwamba, kabla ya kuja kwa Masihi, Eliya ataonekana wazi kimwili kwanza. Yohana alilikanusha tazamio hilo. Lakini baadaye Yesu alisema, habari za Yohana: "Mkitaka kukubali, ndiye Eliya atakayekuja." Mathayo 11:14. Yohana alikuja katika nguvu na roho ya Eliya ili kufanya kazi ya aina ile Eliya aliyofanya. Lakini Wayahudi hawakukubali ujumbe wake. Kwao hakuwa Eliya.

### Wengi leo wanashindwa "kumwona" Kristo

Wengi katika hao waliokusanyika huko Yordani walikuwako wakati Yesu alipobatizwa. Lakini ishara iliyotolewa ilifahamika kwa watu wachache tu kati yao. Miezi iliyotangulia huduma ya Yohana Mbatizaji, watu wengi walikataa mwito wa kutubu. Hivyo wakati mbingu ilivyomshuhudia Yesu wakati wa ubatizo wake, hawakutam-
[68] bua. Watu ambao hawakuwa na imani kwake, hawakuuona ufunuo wa utukufu wa Mungu. Masikio ambayo hayakusikiliza sauti yake,

hayakutambua ushuhuda huo. Hivyo ndivyo ilivyo na sasa. Kila mara kuwako kwa Yesu, na malaika wahudumu hudhihirika katika mikutano ya watu, lakini wengi huwa hawana habari. Hawasikii kitu kigeni. Lakini kwa wengine kuwako kwa Mwokozi hudhihirika kwao. Wao hufarijika, na kutiwa nguvu, na kubarikiwa.

Wakuu waliotoka Yerusalemu walimwuliza Yohana: "Kwa nini unabatiza?" Nao walikuwa wakingojea jawabu lake. Ghafla, alipowaangalia makutano uso wake ulingaa na mwili mzima ukabadilika. Mara akinyosha mikono yake, alisema, "Nawabatiza katika maji lakini kati yenu anasimama msiyemjua yule ajaye nyuma yangu, ambaye sistahili hata kulegeza gidamu za viatu vyake." Ujumbe uliwekwa kando tu, kama usio na maana, wa kupelekwa kwa wazee wa baraza la Sanhedrin.

Wakati wa ubatizo wa Yesu mawazo ya Yohana yaliongozwa kwenye fungu la Isaya 53:7 lisemalo: "Kama Mwana Kondoo apelekwaye machinjioni." Katika majuma yaliyofuata, Yohana alijifunza sana unabii huu, na pamoja na matoleo ya kafara. Aliona kuwa kuja kwa Kristo kulikuwa muhimu sana kuliko makuhani na watu walivyodhani. Alipomwona Yesu yuko katika mkutano baada ya kutoka jangwani, alisubiri kwa subira asikie Mwokozi akitangaza kazi yake. Lakini hakusikia neno, wala hakuona ishara yoyote. Yesu hakujibu lolote kwenye ubatizo wake katika tangazo lililotolewa, bali aliunganika na wanafunzi wa Yohana, wala hakujionyesha.

Siku ya pili yake Yohana alimwona Yesu akimjia, akiwa na nuru ya utukufu wa Mungu iking'aa juu yake, nabii alinyosha mikono yake, akasema: "Tazama Mwana Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Huyu ndiye niliyesema kuwa, ajaye nyuma yangu ni mkuu .... Niliona Roho akishuka kama njiwa kutoka mbinguni juu yake. . . . Aliyenituma nibatize kwa maji, aliniambia,. . . Huyu ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu." Nami nimeona na kushuhudia kwamba huyu ni Mwana wa Mungu.'

## Sura ya Kristo Haikupambanuliwa

Huyu ndiye alikuwa Kristo? Watu walimtazama kwa mshangao mkubwa aliyekuwa akisemwa kuwa ndiye Mwana wa Mungu. Walikuwa wameshangazwa sana kwa maneno ya Yohana. Alikuwa amesema kwa jina la Mungu. Walikuwa wakimsikiliza siku kwa

[69] siku, kadiri alivyokuwa akikemea dhambi zao. Na uhakika wa maneno yake kama mtu aliyetumwa na mbingu aliwatia nguvu. Lakini ni nani huyu ambaye ni mkuu kuliko Yohana? Katika kuonekana kwake na sura yake hakuna kitu cha kuonyesha ukuu wake. Kwa kweli alikuwa mtu wa kawaida tu, akivaa nguo za kawaida tu za hali ya mtu maskini.

Wengine katika mkutano walikuwako katika ubatizo wa Kristo, na walisikia sauti ya Mungu. Lakini sura ya Mwokozi ilikuwa amebadilika sana. Wakati wa ubatizo wake walimwona aking'aa kwa nuru ya mbinguni, sasa amechoka na kudhoofika, anatambuliwa na Yohana peke yake.

Lakini watu waliona uso ambao ulikuwa na fadhili za Uungu na mchanganyiko wa uwezo. Kila hali yake sasa ilikuwa ya kibinadamu kamili, na usemi wa upendo. Aliwashangaza watu kwa uwezo uliofichika, lakini ukionekana kidogo. Je, huyu ndiye yule ambaye amekuwa akingojewa na Waisraeli?

Yesu alikuja katika hali ya kimaskini na katika hali ya unyenyekevu, ili apate kuwa kielelezo chetu na Mwokozi wetu. Kama angeonekana katika hali ya kifahari, angefundishaje unyenyekevu? je, kama Yesu angalikuja katika hali ya kifalme, yenye fahari, watu wanyonge na maskini wangepata wapi matumaini?

Lakini kwa watu wengi ilionekana kuwa mtu aliyetukuzwa hivi na Yohana, haiwezekani kuwa hafifu kama sisi tulivyo. Wengi waliona uchungu, na kutatanika.

Maneno yaliyotamaniwa ya kutamkwa na Yesu kuhusu kusimamishwa kwa ufalme, hayakutamkwa. Kama angalikuwa mtu wa fahari, makuhani na walimu wa Kiyahudi na wakuu wengine wangalikuwa tayari kumpokea. Lakini, mtu atakaye kusimamisha ufalme wa haki katika mioyo yao, wasingalimpokea.

### Yohana awaelekeza wanafunzi wake kwa Yesu

Siku ya pili yake, wanafunzi wawili wa Yohana walipokuwa karibu naye, Alimwona Yesu tena. Mara tena uso wake uliwaka, kwa nuru ya mbinguni, alipopaza sauti yake na kusema: "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, wanafunzi wake hawakufahamu sawasawa maana ya jina hilo Yohana analomwita, "Mwana Kondoo wa Mungu ni nini?"

Walipomwacha Yohana walikwenda kumtafuta Yesu. Mmojawapo alikuwa Andrea, nduguye Simoni; mwingine alikuwa Yohana mwinjilisti. Watu hawa ndio walikuwa wanafunzi wa Yesu wa kwanza. Walimfuata Yesu wakiwa na hamu ya kusema naye, [70]
walakini wakiogopa, wakanyamaza tu, hayo yakabaki mawazoni. Je huyu ndiye Masihi? Yesu alifahamu kuwa watu wawili hawa walikuwa wakimfuata. Wao ndio walikuwa matunda yake ya kwanza katika kazi yake. Walakini akiwageukia, aliwauliza: "Mnatafuta nini?" Wakasema "Rabi, (Maana yake mwalimu) . . . unakaa wapi?" Kwa mazungumzo mafupi wakiwa hapo njiani, waliridhika kabisa. Walitamani kuishi na Yesu, na kusikia maneno yake.

"Aliwaambia, njooni, mwone, Walikuja, wakaona anapoishi, wakakaa naye siku hiyo."

Kama Yohana na Andrea wangalikuwa na mioyo isiyoamini, kama walivyokuwa makuhani na wakuu, wasingalikuwa wanafunzi, bali wangalikuwa wapimaji wa kuhukumu maneno yake. Lakini kwa kuwa walitikia mwito wa Roho kwa njia ya mahubiri ya Yohana Mbatizaji sasa walimfahamu mwalimu wa mbinguni. Kwao, maneno ya Yesu yalikuwa dhahiri na mapya. Nuru ya mbinguni uliangaza katika Agano la Kale na kuwaelimisha maneno yake. Ukweli ukadhihika nuruni.

Mwanafunzi Yohana alikuwa na juhudi na upendo wa halisi, na mwalimu mwenye kutafakari sana mambo. Alikuwa ameanza kupambanua "utukufu wa Mwana wa pekee wa Baba, amejaa neema na kweli." Yoh. 1:14.

Andrea alitaka kushirikisha furaha iliyomjaa. Alipokwenda kumtafuta nduguye, alisema, "Tumemwona Masihi." Simoni pia alikuwa amesikia mahubiri ya Yohana mbatizaji, na kwa hiyo akaharakisha kwenda kwa Mwokozi. Macho ya Kristo yalisoma tabia yake na maisha yake. Haraka haraka yake, upendo wake, na fadhili zake, hali yake ya kimbelembele na ya kujitegemea; anguko lake, na kazi yake na kifo chake cha kusulubishwa. Mwokozi alisoma hayo yote. Ndipo alisema, "Wewe ni Simoni mwana wa Yona, utaitwa Kefa, maana yake jiwe"

Siku ya pili yake . . . Yesu . . . allmfuata Filipo, akamwambia, 'Nifuate Filipo alitii amri hiyo mara moja, naye akawa mmojawapo wa wafuasi wa Kristo."Filipo akamwita Nathanieli, aliyekuwa katika mkutano, wakati Yohana Mbatizaji alipomwonyesha Yesu kuwa

ndiye Mwana Kondoo wa Mungu. Nathanaeli alipomwangalia Yesu, alikata tamaa. Je, mtu huyu aonekanaye kuwa mtu fukara na mwenye wasiwasi, aweza kuwa ndiye Masihi? Walakini ujumbe wa Yohana ulikuwa umemwaminisha Nathanaeli.

[71] **Maombi ya siri ya Nathanael yalisikiwa**

Filipo alipomwita, Nathanael alikuwa ametoka kuomba katika kichaka, na kutafakari juu ya unabii, unaohusu kuja kwa Masihi . . . aliomba kwamba, kama huyo anayehubiriwa na Yohana Mbatizaji ndiye Mkombozi, basi afahamishwe. Roho Mtakatifu akamjilia, akamhakikishia kuwa, Mungu alikuwa amewajilia watu wake. Filipo alifahamu kuwa rafiki yake alikuwa akichunguza unabii, na wakati Nathanaeli alipokuwa akiomba kichakani, Filipo alimwona. Kila mara walikuwa wakiomba pamoja kwa siri mahali pa maficho,

Ujumbe kwamba, "Tumemwona Masihi," ambaye alinenwa na Musa na kuandikwa katika sheria yake, na manabii, kwa Nathanaeli ilionekana kwamba, ndilo jawabu wazi la sala yake. Lakini Filipo alipoongeza na kusema, "Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu,' Nathanael alichukizwa, na kusema, "je, kitu chema chaweza kutoka Nazareti?"

Filipo akasema, 'Njoo, uone." Yesu alimwona Nathanael akimjia, akasema, "Tazama, huyu ndiye Mwisraeli halisi asiye na ila! Nathanael akasema kwa mshangao, "Ulinifahamu lini?" Yesu akajibu, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Ilitosha Roho wa Mungu aliyeshuhudia kwa Nathanael alipokuwa akiomba mahali pa siri chini ya mti, alimzungumzia katika maneno ya Yesu. Nathanaeli alikuja kwa Yesu akiwa na shauku ya ukweli, na sasa ametosheka, na shauku yake imekwisha. Alisema, "Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe u Mfalme wa Israeli!"

Kama Nathanaeli angaliwategemea walimu wa Kiyahudi ili wamwongoze, asingalimwona Yesu kamwe. Alikuwa mfuasi kwa ajili ya kuona na kuamua yeye mwenyewe. Na leo ni vivyo hivyo. Watu wengi huwategemea wanadamu walio waongozi. Inatupasa tusome neno la Mungu sisi wenyewe kama Nathanaeli alivyofanya, na kuomba ili tupate uvuvio wa Roho Mtakatifu. Aliyemwona Nathanaeli akiomba chini ya mti hutuona sisi pia tunapokuwa

tukiomba mahali pa siri. Malaika huwa karibu na wale wanaomtafuta Mungu kwa unyenyekevu, ili awaongoze.

Katika kuitwa kwa Yohana, Andrea, Simoni, Filipo na Nathanaeli, ndipo ulianzishwa msingi wa kanisa la Kristo. Yohuna Mbatizaji aliwapeleka wanafunzi wake wawili kwa Kristo. Halafu mmojawapo wa wanafunzi hao, yaani Andrea, alimpata ndugu yake. Kisha Filipo aliitwa, naye akaenda kumtafuta Nathanaeli.
Mfano huu unatufundisha fundisho muhimu sana, kuhusu jinsi ya [72]
kuwaita jamaa zetu, marafiki zetu, na majirani zetu. Wako watu ambao hawajajaribu kamwe kufanya bidii kuleta hata mtu mmoja kwa Kristo.

Wengi wamepotea bila tumaini, ambao wangaliokolewa kama majirani zao, watu wa kawaida tu wangalijitahidi kuwashughulikia. Katika jamaa, ujirani, na katika miji tunapoishi, kuna kazi inayotupasa kufanya. Mara mtu unayemshughulikia akiongoka, naye hutamani kuwashughulikia wengine. Akimpata mtu huwa rafiki yake wa thamani katika Kristo.

## Hoja yenye nguvu zaidi

Filipo hakumwambia Nathanaeli akubali ushahidi wa Mtu mwingine, ila amwone Kristo yeye mwenyewe. Njia moja muhimu ya kuongoa roho kwa Kristo, ni kudhihirisha tabia ya Kristo ndani yetu katika maisha yetu ya kila siku. Watu hupinga wengine wasikubali ujumbe kwa ajili ya tabia zisizo za Kikristo. Lakini maisha ya upendo bila kuwa ubinafsi, ndiyo hotuba yenye kuaminisha watu na kuwaleta kwa Kristo.

Neno la Mungu, likisemwa na mtu ambaye ametakaswa kwalo, huwa na uwezo wa kuleta uzima, na huingia katika roho za watu. Mtu akilipokea neno kwa upendo, atatamani kulieneza kwa wengine. Ataeneza kile ambacho amepata. Ushuhuda wake huwa kamili wa kuwaongoza wengine kwa Kristo.

Mtu anayetaka kuangaza nuru ya Yesu, lazima kwanza yeye mwenyewe awe nuru. "Anyweshaye, atanyweshwa mwenyewe." Mithali 13:25. Ili kusudi tuingie furaha ya utukufu wa Kristo, yaani furaha ya kuona waliookoka kwa damu yake, inatulazimu tushirikiane naye katika kazi yake pia.

Ungamo la imani la Nathanael lilikuwa katika masikio ya Yesu sawa na wimbo mtamu: "Kwa sababu nilikuambia kuwa, nilikuona chini ya mti. Unaamini? Utaona mambo makuu kuliko haya." Mwokozi alitazamia kazi yake ya kuhubiri habari njema za wokovu, akiwaganga waliovunjika, na kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao kutoka kwa Shetani. Yesu akaongeza tena, "Amin, amin nakuambia, tangu sasa utaona mbingu zikifunguka, malaika wa Mungu wakipanda na kushuka juu ya Mwana wa Adamu."

Hapa Kristo alikuwa akisema kuwa, kando ya Yordani mbingu zilifunguka, Roho akashuka. Lakini ukaniamini, imani yako itaimar-
[73] ishwa. Utaona kuwa mbingu zimefunguka, wala hazitafungwa. Nimezifungua kwa ajili yako. Malaika wa Mungu wanashuka wakichukua maombi ya wahitaji na wenye dhiki kwa Baba, na kushuka kuleta tumaini, na shime, na uzima kwa wanadamu.

Wakati wote malaika hupitapita kutoka duniani kwenda mbinguni, na kutoka mbingum kwenda duniani. Kwa niia ya Kristo, na kwa njia ya watumishi wake huleta mibaraka ya Mungu kwetu. Mwokozi alipotwaa hali ya binadamu alichukua fadhaa zetu zote ambao ni wana wa Adamu Na kwa Uungu wake hutufikisha katika kiti cha Mungu.

## 15 — Yesu Ahudhuria Harusi [74]

Katika kijiji kidogo cha Galilaya walipokusanyika watu kwa karamu Ya arusi, Yesu alifanya mwujiza ili kuongeza furaha zaidi katika arusi. Hivyo ndivyo alivyoonyesha fadhali zake kwa watu, na jinsi alivyowahudumia. Katika jangwa yeye mwenyewe alikinywea kikombe cha masumbuko, sasa alikuja kuwanywesha watu kikombe cha baraka.

Kulikuwa na arusi huko Kana na Yusufu na Mariamu walihusika katika arusi hiyo, maana ni ya jamaa yao; na Yesu pia alihudhuria pamoja na wanafunzi wake.

Mariamu, mama yake, alikuwa amesikia habari za mafunuo yaliyotokea huko Yordani, wakati wa ubatizo wa Yesu. Habari hizi zilimfikirisha upya juu ya mambo aliyokuwa akiwaza kwa muda mrefu. Kazi ya Yohana Mbatizaji ilimchangamsha sana Mariamu. Alikuwa akiona hali ya Yesu, na kuamini kuwa ndiye Masihi, lakini alikuwa na mashaka pia. Alitamani siku ambayo atajidhihirisha wazi kuwa ndiye Masihi hasa.

Kifo kilikuwa kimewatenga Yusufu na Mariamu tayari; Yusufu alikuwa na mawazo sawa na Mariamu kabla ya kufa kwake. Sasa hakuna mtu ambaye Mariamu atamweleza mawazo yake ya matumaini, na mashaka pia. Aliyatafakari maneno ya Simioni, yaliyosema: "Nawe mwenyewe, upanga utaingia moyoni mwako." Luka 2:35. Kwa hamu, alingoja Yesu arudi.

Kwenye arusi ya Kana alikutana na Yesu; mwenye upendo ule ule. Lakini alikuwa umebadilika. Uso wake ulikuwa hali ya mashindano aliyokuwa nayo jangwani. Na hali ya utukufu ilionyesha kuwa yeye anafanya mambo ya mbinguni. Alikuwa na kikundi cha watu waliokuwa wakimwita Bwana. Kikundi hiki kilimweleza Mariamu mambo waliyosikia na kuona kwenye ubatizo, na kwingineko. Watu [75]
walipokusanyika, ikawa hoihoi ya karamu. Na Mariamu alipoona kuwa macho ya watu yanamwangalia Yesu, alitaka sana ajionyeshe kuwa yeye ni mpendwa wa Mungu.

Ilikuwa desturi kuwa sikukuu ya ndoa huendelea siku kadha wa kadha. Katika mfulizo huo kabla sikukuu haijamalizika, divai iliwaishia. Mariamu alikuwa akihudumia kama jamaa, sasa alimwambia Yesu, “Hawana divai.” Maneno haya yalimaanisha kuwa Yesu atengeneze nyingine. Lakini Yesu alisema, mwanamke, nina nini nawe? Saa yangu haijaja bado”

Usemi huu sio wa kudharau, au kutokuwa na adabu. Katika desturi za watu wa mashariki, huo ndio usemi wa heshima na adabu. Kristo mwenyewe alitoa amri isemayo: “Mheshimu baba yako na mama yako.” Kutoka 20:12. Pote, katika arusi na katika msalaba, maneno ya mwisho ya Kristo kwa mama yake yalionyesha heshima na adabu na upendo.

Wakati wa ujana wake, alipokwenda hekaluni, Kristo alisema kwa.Mariamu: “Hamkujua ya kuwa inanipasa kuwa katika nyumba ya Baba yangu?” Luka 2:49. Sasa anarudia fundisho lile lile. Ilikuwa hatari kwa Mariamu kudhani kuwa uhusiano wake na Yesu, unampa haki ya kumfanya mwana wake, wala si Mwokozi wa ulimwengu. Kwa muda wa miaka thelathini alikuwa mwana wake akimtii, lakini sasa yapasa awe kwa kazi ya Baba, yaani kazi ya ukombozi. Kama Mwokozi wa ulimwengu, hapaswi kufungwa na uhusiano wa jamaa kiasi cha kumzuia asitimize kazi yake. Fundisho hili linatuhusu na sisi pia. Mvuto ya duniani, ushikamano wa jamaa, wala kitu kinginecho, visituvute tutoke katika mapito tuliyoagizwa na Mungu kupita.

Mariamu angepata wokovu kupitia kwa Kondoo wa Mungu peke yake. Uhusiano wake na Yesu haukuwa tofauti na uhusiano wa watu wengine na Yesu. Maneno ya Mwokozi yalipambanua wazi uhusiano wake na yeye, na uhusiano wake na Mungu. Uhusiano wa kuzaliwa tu hautaleta uhusiano upasao wokovu.

“Saa yangu bado haijaja.” Yesu alipotembea kati ya wanadamu, alikuwa akiongozwa hatua kwa hatua na mapenzi ya Baba. Kule kusema kwa Mariamu kuwa saa yangu haijaja bado, alisema maneno ambayo bado ni mawazo tu, ni mawazo yale aliyokuwa na matazamio ya kujidhihirisha wazi kuwa ni Masihi. Lakini saa haijaja bado.
[76] Sio kuwa mfalme, ila ni kama mtu mweye masikitiko na huzuni tu, ajuaye sikitiko.” Yesu alikubali kuchukua fadhaa za wanadamu.

## Imani ya Mariamu yapata thawabu

Ingawa Mariamu hakufahamu vizuri kazi ya Kristo, alimtegemea. Kwa hiyo Yesu alikubali imani hii kwa ajili ya kuheshimu imani yake na kwa ajili ya kuimarisha imani ya wanafunzi wake, alifanya mwujiza wa kwanza. Kwa wanafunzi ilidhihirika kabisa kuwa yeye ni Masihi, lakini walisikitika sana kwa kutoamini kwa makuhani na walimu wa Kiyahudi kwamba Yesu ndiye Masihi. Mwujiza huu uliwaimarisha wanafunzi wake katika mashindano yao ya upinzani.

Mariamu aliwaambia waliokuwa wakihudumu katika meza, "Lolote atakalowaambia, lifanyeni."

Kando ya mlango kulikuwako na mabalasi makubwa sita Yesu aliwaambia watumishi wayajaze maji. Kisha akasema, "Choteni sasa maji hayo mkampelekee mkuu wa karamu." Badala ya kuwa maji tu, yakageuka kuwa divai tamu.

Walipoyaonja maji hayo yaliyoletwa na watumishi, mkuu wa karamu akaona kuwa ni matamu kuliko yote aliyopata kunywa. Akimgeukia mkuu wa meza, alisema, "Kila mtu hutanguliza kuleta divai nzuri, na watu wakisha kushiba, huleta ile mbaya, lakini wewe umengoja na divai nzuri mpaka sasa.

Zawadi zinazotolewa na ulimwengu zinaweza kupendeza macho na kuleta utamu, lakini hazitoshelezi chochote. Mvinyo hugeuka kuwa uchungu, shangwe hugeuka kuwa majonzi, kilichoanza kwa shangwe na furaha huishia katika uchungu na ghasia. Bali zawadi ya Yesu ni ya kudumu daima. Karamu anayoandaa ni ya kudumu, na huleta furaha. Hakuna upungufu wowote. Kama ukiishi ndani yake, zawadi nzuri ya leo, hukukaribisha katika zawadi bora ya kesho.

Zawadi ya Kristo katika arusi, ilikuwa mfano tu. Maji yaliyojaza mabalasi yaliletwa na wanadamu, lakini Neno la Mungu peke yake ndilo liliweza kutia uhai na ladha. Neno la Kristo lilitoa ladha ya kuwaridhisha watu karamuni. Hivyo wingi wake ndio unaondoa udhalimu na kusafisha moyo. Divai iliyofanywa na Yesu karamuni na ile aliyowapa wanafunzi, ambayo ilikuwa mfano wa haya Isaya husema, wakati akitaja divai mpya: "Kama vile divai mpya ipatikanavyo katika kichala, na mtu mmoja husema, "Usikiharibu, maana mna baraka ndani yake. Isaya 65:8.

Kristo alionya katika Agano la Kale, akisema: “Mvinyo
[77] hudhihaki, kileo huleta ugomvi; akosaye juu ya hayo hana hekima” Mithali 20:1. Yesu kamwe hakufanya kitu kama hicho. Shetani huwapa kitu kama hicho ili kuvuruga akili zao na kupumbazika wasiweze kupambanua kitu. Lakini Kristo hufundisha kuwa inatubidi tuvitiishe viungo vyetu ndani ya amri. Yesu ndiye alifundisha kwamba Yohana Mbatizaji asinywe mvinyo wala kileo chochote. Alisema mambo hayo kwa mke wa Manoa, mamaye Samsoni. Naye alilaam mtu ambaye atampa jirani yake kileo. Kristo hakukanusha mafundisho yake. Divai aliyofanya katika karamu ya arusi ni matunda yasiyochacha ya mzabibu.

Wageni walipokunywa walitaharuki, na kuulizauliza habari za divai hii tamu, watumishi waliwaeleza kuwa huu ni mwujiza. Makutano walipomtafuta Yesu, alikuwa ameenda zake.

Sasa waliwageukia wanafunzi, waliokuwa na nafasi ya kuonyesha imaru yao kwa Yesu. Walisema mambo waliyoona na kusikia juu ya Kristo, kule kando ya mto wa Yordani. Habari ya mwujiza huo ilifika mpaka Yerusalemu. Makuhani na wazee wakaamka kwa upinzani kuchungua unabii unaohusu kuja kwa Mashihi.

### Kristo alivunja mtengano wa matabaka

Yesu alianza kazi yake kwa njia ya kuwahurumia watu Wakati alikuwa mtiifu wa amri za Mungu, alikemea unafiki wa Mafarisayo; naye alijaribu kuwatoa katika vifungo vya sheria walivyofugiwa na Mafarisayo. Alikuwa akitaka kuvunja mtengano wa matabaka ya watu tofauti katika jamii. Alitaka awalete watu katika hali ya umoja kama watu wa jamaa moja.

Yesu alishambulia hali ya ubinafsi, walakini yeye alikuwa mtu wa kushirikiana na watu wote. Alikuwa mkarimu kwa watu wa hali zote, akiwazuru watu nyumbani kwao, matajiri na masikini pia, wasomi na wasio wasomi, akitaka kuwafikisha juu ya mambo ya milele, wala siyo mambo hafifu tu ya dunia. Yeye hakuchafuliwa na mambo ya dunia hii walakini akapata furaha katika kuangalia mambo ya asili na viumbe vyake. Furaha ya arusi ya Wayahudi haikuwa chukizo kwake. Kule kuhudhuria kwake kwenye arusi kulikuwa kuiheshimu ndoa, kwamba ni jambo takatifu lililoanzishwa na Mungu mwenyewe.

Katika Agano la Kale na Agano Jipya pia, ndoa ni mfano wa mwungano mtakatifu ulioko baina ya Yesu na watu wake. Katika mawazo ya Yesu, furaha ya arusi ni mfano wa furaha ya siku ile ambayo kanisa la Mungu, likiwa kama bibi arusi litakapokaribishwa [78]
nyumbani mbinguni, yaani watu waliookolewa.

"Kama bwana arusi anavyomfurahia bibi arusi, ndivyo nitakavyokufurahia wewe. Atakushangilia kwa shangwe; . . . . Atakufuahia kwa kuimba." Isaya 62:6, 7; Sefania 3:17. Yohana mtume aliandika: "Nilisikia kama sauti ya watu wengi . . . ikisema. ... Na tufurahi, tushangilie, na tumtukuze; kwa maana arusi ya Mwana-kondoo imekuja, na bibi arusi amekwisha kuwa tayari." Ufunuo 19:6, 7.

Yesu aliwafikia watu katika roho zao kwa kuwa alijichanganya kati yao, kama mtu anayewatakia heri. Aliwatafuta popote, njiani, nyumbani, baharini, kwenye mashua, sinagogini, katika karamu ya arusi, na mahali popote. Alionyesha fadhili zake katika mambo yao yote. Huruma zake ziliwavuta kwake. Maombi yake ya pekee katika milima, yalikuwa ndiyo matayarisho kwa kazi yake ya kukutana na watu katika shughuli zao. Kutoka katika maombi hayo alikuja akiwa tayari kuwasaidia wagonjwa, na kuzivunja pingu za Shetani alizofunga watu.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwa njia ya kuishi na kushirikiana nao. Wakati mwingine wakiwa kando ya mlima, wakati mwingine wakiwa pwani ya bahari, au wakiwa wanatembea njiani, hapo ndipo aliwafundisha siri ya ufalme wa Mungu. Hakuhubiri, bali alifundisha; wala hakuwaamuru wanafunzi wake wafanye hili au lile, ila alisema: "Nifuateni." Rafiki zake alifuatana nao ili wapate kuona jinsi anavyofundisha watu.

Kielelezo cha Kristo kinapaswa kuigwa na wote wanaofundisha Neno lake. Haitupasi kujitenga na watu, bali kushirikiana na watu wa hali mbali mbali, mahali popote walipo. Roho za watu haziguswi kwa njia ya mahubiri mimbarani peke yake. Njia nyingine ya kuwafikia watu, ambayo inafaulu sana ni katika nyumba za watu wa hali ya chini, na nyumba za watu wa hali ya juu, na katika makusanyiko halali.

Haitupasi kuunganika na watu wa ulimwengu katika mambo yao ya ufedhuli. Tusiihalalishe dhambi kwa na yoyote, kwa maneno yetu, au kwa matendo yetu, au kwa kukaa kimya kwetu, au kwa

kuhudhuria mahali pa dhambi. Popote tuendapo lazima twende na Yesu. Lazima tuwe mashahidi wa Yesu popote. Katika mikusanyiko yote, inayotakaswa na neema ya Yesu, lazima iwe ya kuongoa watu. Watu waone kuwa dini yetu si dini ya udhalimu bali ni ya kweli iliyojaa utu wema na baraka, hata watu watuone kuwa tunataka hata wao washiriki baraka hizo. Wote waliomwamini Kristo
[79] wawe wahudumu wa mambo mema kwa wengine, sawa kama yeye alivyokuwa mhudumu kwa watu.

Tusiupotoshe ulimwengu kwa kutudhania kuwa, Ukristo umetufanya kuwa watu hafifu wasio na faida yoyote. Watu wa Kristo hawaishi kama wenye masikitiko, wasio na furaha, watu baridi, bali wenye furaha, wachangamfu, waliojaa upendo na matendo mema, watu wa Mungu hasa. Nuru yao iwamulikie wengine kuwa na kazi njema za upendo wa Kristo.

# 16 — Kristo Akabili Machafuko Hekaluni [80]

Pasaka ya Wayahudi ilikuwa karibu, na Yesu alipanda kwenda Yerusalemu. Yesu alikuwa bado kutangaza kazi yake waziwazi; kwa hiyo alijichanganya na kundi la watu bila kutambulikana. Nyakati kama hizi neno kuu la mazungumzo lilihusu kuja kwa Masihi. Yesu alijua kuwa tumaini la fahari ya taifa la Israeli litakatishwa tamaa, maana tumaini hili lilikuwa limejengwa kwenye tafsiri potofu ya Maandiko. Kwa juhudi kubwa alieleza jinsi unabii usemavyo, na akajaribu kuwafikirisha zaidi juu ya kuchunguza Neno la Mungu.

Wakati wa pasaka, watu wengi sana walikusanyika kutoka pande zote za Palestina, na nchi za kando yake. Sebule ya hekalu ikajaa tale kwa wingi wa watu. Wengi hawakuweza kuleta sadaka zilizotakiwa kutolewa kuwakilisha yule, ambaye ni sadaka halisi. Kwa ajili ya nafuu ya kupata sadaka za wanyama, wanyama wengi walikuwa wakiuzwa na kununuliwa hapo katika uwanja wa nje wa hekalu.

Kila mwaka, Myahudi alitakiwa kutoa sadaka kwa ajili ya roho yake. Fedha zilikusanywa kutengeneza hekalu. Soma Kutoka 30:1,2-16. Zaidi ya fedha hizi, jumla kubwa ya fedha zililetwa kama mchango, na kutiwa katika hazina. Uvunjaji wa fedha hizo uliimarisha udanganyifu na utozaji gharama isiokuwa halali, ambao ulihesabiwa kuwa ni fungu la makuhani.

Wenye kuabudu walifundishwa kuwa, wasipotoa fedha hizo kama sadaka, mibaraka ya Mungu haitawakalia katika ibada yao na wala nchi yao haitabarikiwa pia. Wenye biashara waliuza wanyama wao kwa bei ya juu sana, na faida wakagawana na makuhani na wakuu wengine. Hivyo walijitajirisha kwa ajili ya kuwatoza watu bure.

### Udhalimu wa kifedha kazini mwa Mungu [81]

Makelele ya mnada, milio ya ng'ombe na kondoo, makelele ya njiwa pamoja na milio ya fedha, jinsi zilivyokuwa zikibadilishwa, vilikuwa ghasia kubwa. Ilikuwa fujo, kwamba maneno yaliyokuwa

yakisemwa kwa Mwenyezi Mungu yalizimwa katika makelele hayo. Wayahudi walifurahia hekalu lao, nao waliyahesabu maneno yaliyosemwa kwa mzaha hekaluni kuwa ni makufuru. Lakini upendo wa fedha umewapumbaza. Wametangatanga, wakaacha utakatifu wa ibada iliyoanzishwa na Mungu mwenyewe. Popote Mungu anapoabudiwa huwa ni mahali patakatifu. Soma Kutoka 19:12, 13. Mzunguko wa hekalu la Mungu ungehesabiwa kuwa ni mahali patakatifu, penye kuheshimiwa. Lakini katika kushindania mapato ya udhalimu, yote hayo hayakujaliwa. Makuhani na wakuu wengine, wangekuwa wamenyamazisha makelele yaliyokuwa hekaluni; na kuwapa watu kielelezo cha uchaji wa kweli, badala ya kukaa na kutafuta mapato yao, wangewasaidia wale wanaotafuta sadaka. Lakini choyo kimewafanya kuwa wagumu wasiojali.

Katika sikukuu hii, walikuja watu, ambao walikuwa na upungufu wa vitu, na wenye dhiki vipofu, na vilema na viziwi walikuja. Wengine walikuwa wamechukuliwa katika vitanda, kama machela. Wengine wao hawakuweza kupata hata sadaka ndogo sana ya kuleta kwa Bwana. Hata hawakuweza kujinunulia chakula. Watu kama hawa walikatishwa tamaa kwa usemi wa makuhani. Makuhani walijivunia fahari yao, lakini hawakuwa na fadhili yoyote, wala huruma. Maskini, na wagonjwa, na wenye shida, hawakuonyeshwa huruma hata kidogo.

Yesu alipoingia hekaluni, aliona biashara haramu humo. Aliona taabu ya maskini ambao walikuwa wakifikiri kuwa, pasipo kumwaga damu, hakuna ondoleo la dhambi. Aliona uwanja wa hekalu, ambao ni mtakatifu, ukifanyiwa biashara haramu. Jambo fulani lapaswa kufanywa. Wenye kuabudu wanatoa sadaka zao bila kuelewa, kuwa wanawakilisha sadaka halisi itakayotolewa kwa kutosheleza. Kati yao alisimama yule ambaye anawakilishwa na sadaka hizi, lakini bila kutambulikana, wala kuheshimika. Aliona kuwa sadaka zinatolewa kwa njia ya kupotoshwa. Makuhani na wakuu hawakuwa na uhusiano wowote kati yao na Mungu. Kazi ya Kristo italeta tofauti kamili katika ibada.

Katika kuangalia, Kristo aliangalia mambo ya nyakati na vizazi
[82] na karne, aliona jinsi Makuhani na wakuu walivyokataza Injili isihubiriwe kwa maskini, na jinsi upendo wa Mungu ungalizuiwa usiwafikie watu, na namna watu wangalifanyia neema yake biashara. Kwa mambo kama haya, alibadilika sura, akaonekana kuwa mwenye

chuki na hasira. Watu wakamwangalia. Macho ya wale waliokuwa wakifanya biashara haramu yakakazwa juu yake. Wakaona kuwa mtu huyu amesoma mawazo yao, na kugundua siri za mioyo yao. Wengine walijaribu kuficha nyuso zao.

Makelele ya wafanya biashara yalinyamaza. Ukimya ukawa mzito sana. Ikaonekana kama watu wamesimama mbele ya mahakarna ya Mungu. Wakimtazama Kristo waliona Uungu ukifunuliwa katika ubinadamu. Mtukufu wa mbinguni akasimama mbele yao kama Hakimu, jinsi atakavyosimama siku ya mwisho, bila kufunikwa na utukufu utakavyomfunika siku hiyo, lakini akiwa na uwezo ule ule wa kusoma siri za mioyo. Macho yake yakamkazia kila mtu. Sura yake ikaonekana kuwa juu ya wote, aking'aa kwa mng'ao wa Uungu, kama mwenye amri. Sauti yake wazi kama ilivyokuwa katika mlima wa Sinai, alipotangaza sheria, sauti hiyo ilisikika hekaluni, ikisema: "Ondoeni hapa mmeifanya nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara."

Yesu akiinua mjeledi wa kamba kwa hao waliokusanyika hapo, akaamuru wafanya biashara watoke hekaluni. Kwa ushujaa, kutumia mkono, alizipindua pindua meza za wabadilisha fedha. Fedha zikamwagika sakafuni. Hakuna aliyethubutu kumwuliza. Hakuna aliyeshughulika na habari za biashara tena. Yesu hakuwachapa na mjeledi wa kamba, lakini mjeledi uliokuwa mkononi mwake ulionekana kana kwamba ni upanga mkali unaometameta. Wakuu wa hekalu, makuhani, wabadili fedha, na wauza ng'ombe na kondoo, walikimbia pamoja na vitu vyao kutoka mahali hapo, wakiepuka kutoka mbele yake, kama wanaoepuka hukumu.

### Hekalu latakaswa kwa kuwako kwake Bwana

Watu wote walioona uwezo huu walitaharuki. Hata wanafunzi wake walitetemeka. Hali ya maneno ya Yesu vilitia hofu sana, na watu wakawa na uchaji kamili. Walikumbuka kuwa iliandikwa kuhusiana na hili kwamba, "Wivu wa nyumba yako, umenila." Zaburi 69:9. Baadaye uwanja wa hekalu haukufanyiwa biashara tena. Watu walitulia kabisa. Kuwako kwake Bwana kumeleta utakaso wa hekalu, na heshima ipasayo kuonyeshwa.

Katika kutakasa hekalu, Yesu alitangaza kazi yake, ya kuwa [83]
ndiye Masihi, na akaingia katika kazi mara moja kwa dhahiri.

Hekalu lilikusudiwa kuwa fundisho kwa Waisraeli na kwa ulimwengu pia. Mungu alikusudia ya kuwa kila kiumbe kiwe hekalu la kiroho la makao ya Mwumbaji. Kwa ajili ya kuchafuliwa na dhambi, mioyo ya watu haikuwa makao ya Mwenyezi Mungu tena. Lakini wa kule kufanyika mwili kwa Mwana wa Mungu, Mungu huishi katika ubinadamu, na kwa ajili ya neema yake, mioyo ya watu huwa makao yake tena. Mungu alikusudia kuwa hekalu la Yerusalemu, lingeendelea kushuhudia ukuu uliofunguliwa kwa ajili ya watu wote. Lakini Wayahudi hawakujitolea kuwa hekalu takatifu la kuwa makao ya Mungu. Uwanja wa hekalu ulitumika kama mahali pa biashara haramu, ukiwakilisha mahekalu yote machafu, ambayo ni mioyo ya watu yenye tamaa na mawazo machafu, isiyofaa kuwa makao ya Roho Mtakatifu.

Katika kutakasa hekalu, Yesu alitangaza kazi yake ya kutakasa mioyo ya watu. Kutokana na dhambi; yaani tamaa ya mwili, na kuupenda ulimwengu, na kupenda mazoea mabaya yanayoharibu roho. "'Bwana mnayemtafuta atakuja ghafla katika hekalu lake; M jumbe wa agano ambaye mnampenda. . . . Lakini nani atastahili siku ya kuja kwake, na ni nani atasimama atakapoonekana? Maana ni kama moto utakasao. . . . Ataketi kama mtakasaji wa fedha, naye atawatakasa wana wa Lawi, kama atakasaye dhahabu na fedha." Malaki 3:1-3.

"Hamjui kuwa ninyi ni hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu hukaa ndani yenu? Mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu pia atamharibu mtu huyo; maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ni ninyi." 1 Wakorintho 3:16, 17.

Mtu hawezi kuondoa maovu yaliyomo moyoni mwake, kwa nguvu zake mwenyewe. Kristo peke yake aweza kutakasa hekalu la roho. Lakini hawezi kumlazimisha mtu ili apate kuingia. Yeye husema: "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango, nitaingia kwake." Ufunuo 3:20. Kuwako kwake kutatakasa moyo, upate kuwa safi, mtakatifu kwa Bwana, "makao ya Mungu, kwa Roho." Waefeso 2:22.

### Kabla ya Hukumu ya Mwisho

[84] Wakishikwa na hofu, makuhani na wakuu walikimbia kutoka hekaluni, wakiukimbia uso wa Yesu na macho yake yaliyoweza

kusoma siri za mioyo yao. Katika hali hiyo Kristo aliona jinsi taifa zima la Wayahudi lilivyojitenga na Mungu kwa ajili ya uovu wao, na kutotubu kwao. Kwa nini makuhani walikimbia? Kwa nini hawakusimama? Aliyewaamrisha alikuwa mwana wa seremala, mtu wa Galilaya. Kwa nini hawakumpinga? Kwa nini waliacha faida zao wakakimbia nje kwa agizo lake yule aliyekuwa akionekana kuwa mtu wa kawaida tu?

Kristo alinena kwa mamlaka ya kifalme, na katika kuonekana kwake, na usemi wake, kulikuwako na uwezo ambao hawakuweza kuuvumilia. Katika maneno ya kuamuru waliona hali yao jinsi ilivyo hasa, yaani hali ya unafiki na unyang'anyi. Wakati Uungu ulipomulika katika ubinadamu; walifanana kama wako mbele ya hakimu, wakihukumiwa kifo cha milele. Kwa muda watu wengi walimwamini kuwa ndiye Masihi. Roho Mtakatifu aliwafunulia mioyoni mwao kuhusu usemi wa manabii juu ya Kristo je, watashikilia imani hiyo?

Hawakutubu. Walijua kuwa wamekuwa na hatia ya kutoza watu bure. Kwa kuwa Kristo aligundua siri zao, kwa hiyo walimchukia. Makemeo yake ya wazi mbele ya watu, yaliwaaibisha. Hivyo waliona wivu kwa jinsi alivyozidi kuwa na mvuto mkubwa. Walikusudia kukanushia mbali uwezo uliowafanya wakimbie.

Walirudi hekaluni polepole, huku wakiwa na chuki mioyoni mwao, wakatafakari sana juu ya haya yote. Wamepata badiliko kiasi gani! Walipokimbia, maskini walibaki nyuma, hekaluni, na hawa walikuwa wakimwangalia Yesu, ambaye uso wake ulikuwa na tabasamu na upendo.

Watu walisongamana kuja kwa Yesu, wakimwomba awabariki. Sikio lake lilisikia kila aina ya kilio au lalamiko. Kila mtu alisikilizwa. Kila mtu aliponywa maradhi yalikuwa yakimsumbua.

Makuhani na mkuu wa hekalu walipokuwa wakiangalia kazi kubwa hii, walipata mafunuo mapya kiasi gani. Watu walikuwa wakisimuliana maradhi waliyokuwa nayo, na jinsi walivyokuwa na matumaini ya bure, na jinsi walivyoishi kwa shida sana na masumbuko bure. Walipokata tamaa kabisa, Kristo aliwaponya wote. Mmoja alisema, "Lo, nilisumbuka sana, lakini nimepata msaidizi. Yeye ni Kristo Mwana wa Mungu, nitaandamana naye maisha yangu yote." Wazazi walisema kwa watoto wao, "Ameokoa maisha yenu, msifuni yeye kwa shangwe." Furaha na vicheko viliwajaza watoto,

[85] vijana, akina mama, na akina baba, na wote waliokuwa wakiangalia hayo. Walijazwa na furaha wakarudi nyumbani wakitangaza habari hizo; za upendo wa Yesu.

Wakati Yesu aliposulubishwa, watu walioponywa hawakujiunga na mkutano kumzomea, na kusema, "Msulubishe, msulubishe." Wao walimsikitikia Yesu, maana wameona upendo wake wa ajabu, na uwezo wake. Walijua kuwa yeye ni Mwokozi wao. Waliwasikia mitume, nao wakawa wajumbe wa Mungu kwa ajili ya wokovu wa watu.

Watu waliokimbia kutoka hekaluni, walirudi pole pole baadaye, lakini walikuwa na aibu kubwa. Waliamini kuwa unabii unaomhusu Masihi unakamilika kwa Yesu. Dhambi ya kuchafua hekalu ilikuwa kwa makuhani kwa sehemu kubwa. Kwa ajili ya mpango wao, uwanja wa hekalu uligeuka kuwa soko. Watu hawakuwa na hatia. Lakini makuhani na wakuu, walihesabu kazi ya Kristo kuwa ni mapinduzi ya sheria, wakamwuliza kuwa, ana haki gani kuingia katika mambo yaliyoruhusiwa na wenye mamlaka.

Walichukizwa kwa sababu ya kuingilia habari za biashara na kwa hiyo waliendelea kufanya shingo zao kuwa ngumu, wasijali mvuto wa Roho Mtakatifu.

## Mwanzo wa Kumkataa Kabisa Kristo

Makuhani na wakuu, wangalimwona Yesu kuwa ni mpakwa mafuta wa Mungu, maana walikuwa na maandiko ya unabii uliokuwa ukiieleza kazi ya Kristo. Walijua kuwa kutakaswa kwa hekalu kulifanywa kwa uwezo unaozidi wa kibinadamu. Ijapokuwa walimchukia Yesu, wasingalikimbia, isipokuwa walikuwa na wazo kuwa, labda ni nabii aliyetumwa na Mungu ili kulitakasa hekalu. Wakiwa na wazo la jinsi hiyo walimwendea na neno, kwamba, "Unatuonyesha ishara gani kwamba unafanya mambo haya?"

Yesu alikuwa amewaonyesha ishara. Katika kufanya kazi ambayo Masihi atakuja kufanya, alikuwa amewaonyesha tabia yake jinsi ilivyo. Sasa aliwajibu kwa mfano, akiwaonyesha kuwa anasoma mawazo yao, ambayo ni mabaya. Alisema: "Livunjeni hekalu hili, nami nitalilenga kwa muda wa siku tatu."

Kwa kusema hivyo hakumaanisha kujivunia hekalu la Wayahudi na ibada yao, bali kwa kifo chake, yaani kulivunja hekalu la

mwili wake. Jambo hili la kumwua Wayahudi walikuwa wamelilia njama. Wakati makuhani na wakuu waliporudi hekaluni, walikuwa wamekusudia kumwua Yesu ili kuondoa ghasia. Walakini waliyachukua maneno yake, kana kwamba yalihusu kuvunja hekalu [86] lililokuwa Yerusalemu. Na kwa chuki walisema, "Hekalu hili lilijengwa kwa muda wa miaka arubaini na sita, nawe utalijenga kwa siku tatu tu?" Sasa waliona kuwa Yesu ameitia kasoro imani yao, kwa hiyo walithibitisha msimamo wao wa kumkataa.

Kristo alijua kuwa maneno yake yangaliwakera vibaya, na kumdhania vingine. Wakati wa mashitaka yake ya mwisho, katika kusulibishwa kwake, wangalimtupia maneno hayo. Lakini kuyafafanua wakati huu kungewajulisha wanafunzi wake juu ya mateso yatakayompata, na kungeleta huzuni kubwa na kusononeka. Wakati huu hawajawa tayari kupokea mambo kama hayo. Kuyafafanua mambo hayo, kungefanya Wayahudi wafunike unafiki wao na kujifanya kuwa waaminifu kabisa. Maana wamekwisha kukanyaga katika njia itakayowaongoza kwenye mwisho wa kumchinja Yesu kama Mwana Kondoo apelekwaye machinjioni.

Kristo alijua kuwa maneno haya yatakaririwa. Ingawa yamesemwa kwa watu wachache katika pasaka, yatachukuliwa na kutangazwa kwa watu maelfu ulimwenguni. Baada ya kufufuka kwake kutoka ufuni, maneno haya yatafahamika wazi. Kwa wengi wao yatakuwa ni ushahidi wa Uungu wake, uliofichika.

Maneno ya Mwokozi kwamba: "Livunjeni hekalu hili nami nitalisimamisha kwa siku tatu, yalikuwa na maana kubwa sana, kiasi cha kukaririwa na wasikilizaji wake. Huduma za hekaluni zilikuwa mfano wa dhabihu ya Mwana wa Mungu. Mpango mzima wa matoleo ya kafara na huduma zake, ulikuwa unaelekeza juu ya kifo cha Mwokozi cha kuwaokoa wakosaji. Kanuni ya uwekevu wa mali haukuwa na faida yoyote mbali na yeye. Wakati Wayahudi walipobadilisha kusudi lao la kumkataa Yesu, na kumtoa ili auawe, walikataa mambo yote ya utulivu hekaluni pamoja na huduma zake. Utakatifu ndio ulioondokana nao. Sasa walipaswa kuangamizwa. Tangu siku hiyo dhabihu zote zilizokuwa zikitolewa hazikuwa na maana yoyote. Katika kumwua Kristo, kwa kweli Wayahudi walilivunja hekalu. Kristo aliposubishwa pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili toka juu mpaka chini kuonyesha

kuwa dhabihu halisi iliyo ya mwisho imetolewa. Kawaida ya kutoa dhabihu za wanyama, ilikoma kabisa.

“Nitalisimamisha kwa siku tatu.” Kutoka katika kaburi la Yusufu lililopasuka, Yesu alitoka akiwa mshindi hasa. Kwa kilo chake na kufufuka, Kristo alikuwa “mhudumu wa hema ya kweli, ambayo
[87] Bwana ndiye mjenzi wake, wala si mwanadamu.” Wagalatia 8:2. Watu walisimarnisha hema au hekalu la Wayahudi, lakini hekalu la juu, halikujengwa na fundi wa kibinadamu. “Mtu ambaye jina lake ni Chipukizi . . . atalijenga hekalu la bwana . . . naye atauchukua huo utukufu, naye ataketi na kutawala katika kiti cha enzi.” Zekaria 6:12, 13.

Huduma ya dhabihu ambayo ilikuwa ikimwonyesha Kristo ilipita. Lakini macho ya watu yaligeukia dhabihu halisi ambayo ni dhabihu ya dhambi ya ulimwengu. Makuhani na ukuhani ulikoma, lakini tunamwangalia Yesu mhudumu wa agano mpya. “Njia iendayo katika utakatifu ilikuwa haijadhihirika, wakati hema ya kwanza ilipokuwa ingalipo . . . lakini Kristo ajapo yeye aliye kuhani mkuu wa mambo mema yajayo, ni hudumu bora katika hema bora zaidi isiyofanywa kwa mikono, bali kwa damu yake mwenyewe, aliingia mara moja katika patakatifu, akafanya ukombozi kwa ajili yetu.’ Waebrania 9:1-12.

“Naye kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye, maana yu hai siku zote ili awaokoe.” Waebrania 7:25. Ingawa hekalu la mbinguni na kuhani wetu mkuu huonekana wazi, wanafunzi hawangeona kuwa kuna mavunjiko kati yao na mbingu, na hakuna uwezo walio nao kwa ukosefu wa kuwako kwa Yesu kati yao. Yesu alipojidhihirisha hekaluni mbinguni, huendelea kwa Roho yake, kujionyesha katika kanisa lake duniani. Neno lake la kuagia watu wake lilitimia, “Tazama, mimi niko pamoja nanyi siku zote, mpaka mwisho wa dunia. Mathayo 2:20

“Kwa kuwa hatuna Kuhani Mkuu asiyeweza kuchukuliana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupate rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji. Waebrania 4:15, 16.

## 17 — Nikodemo Amwendea Yesu Wakati wa Usiku [88]

Nikodemo, mtu mwenye elimu kubwa, mheshimiwa sana, ambaye ni mbunge wa laifa la Kiyahudi, alikuwa ametatanishwa kwa mafundisho ya Yesu. Ingawa ni mtu tajiri, na mwenye elimu kubwa, alikuwa amevutiwa na tabia nyenyekevu ya mtu wa Nazareti. Mafundisho ya Mwokozi yalikuwa yamemwingia sana Nikodemo, naye aiitaka kujifunza zaidi mambo hayo.

Tendo la Kristo la kutakasa hekalu kwa nguvu, lilikuwa limeanzisha chuki kwake toka kwa makuhani na wakuu wa Kiyahudi. Kule kuamuru kwa mtu huyu wa Galilaya, na kufukuza watu hekaluni, kusingaliweza kuachwa hivi hivi, bila kushughulikiwa. Lakini sio wote waliokubaliana kumshughulikia Yesu. Wengine waliogopa kumpinga mtu ambaye anaonekana wazi kuwa anaongozwa na Roho wa Mungu. Walifahamu kuwa mateso wanayopatiwa na watu wa mataifa, yanakuja kwa ajili ya uasi wao na ugumu wao, maana hawayakubali maonyo ya Mungu. Waliogopa kuwa, kufanya njama juu ya Yesu, ni kufuata njia ya uasi kama baba zao walivyofanya. Hayo ndiyo mashauri ya makuhani na wakuu. Na kukubali mambo hayo kutawaletea ajali kubwa zaidi.

Nikodemo, alikubaliana na watu waliojisikia hivyo. Katika baraza la Sanhedrin, Nikodemo aliwaonya kuwa waangalifu. Alisema kuwa, kama Yesu alikuwa na mamlaka ya Mungu, itakuwa hatari kumkanusha. Makuhani hawakulijali shauri hilo.

Nikodemo alikuwa amechunguza kwa bidii na kwa hamu kubwa, unabii unaomhusu Masihi. Kadiri alivyochunguza ndivyo aliyozidi kuamini kuwa Yesu ndiye yule atakayekuja, kama unabii unavyosema. Alikuwa amesikitishwa sana na kufuru za watu. Alikuwako wakati Yesu alipowafukuza wenye biashara hekaluni. [89] Aliona Mwokozi akiwaponya wagonjwa; aliona walivyomshangilia kwa shangwe, na kusikiza maneno ya kumtukuza. Hakuwa na shaka kwamba Yesu wa Nazareti in Mwana wa Mungu. Alitamani wakutane na Yesu na kuongea naye. Lakini alisita kukutana naye waziwazi. Maana kama angeonekana na wana baraza wa Sanhedrin

ngalijiletea lawama bure na kudhihakiwa. Alikusudia kukutana naye kwa siri. Alipojua kuwa Mwokozi huenda kulala katika mlima wa Mizeituni, alingoja mpaka watu wamelala, ndipo akaenda kumwona Yesu.

Akiwa mbele ya Yesu, Nikodemo aliona haya, lakini alijitahidi kujikaza, akasema: "Rabi, tunajua ya kuwa wewe ni mwalimu, atokaye kwa Mungu; maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe; isipokuwa Mungu awe pamoja naye." Maneno yake yalionyesha kuwa anataka mazungumzo. Walakini yalionyesha hali ya kutoamini. Hakumkiri Yesu kuwa ndiye Masihi, ila alisema kuwa ni mwalimu atokaye kwa Mungu.

Yesu alimwangalia Nikodemo, kama mtu asomaye moyo wake. Alimwona kuwa ni mtafuta ukweli. Yesu alitaka kuimarisha imani yake, alisema: "Amini, amini nakuambia, Mtu asipozaliwa kutoka juu, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Yohana 3:3.

Nikodemo amekuja ili wajadiliane na Yesu, lakini sasa amefunua wazi kanuni za ukweli wote. Alimwambia unachohitaji si kuelewa mambo yalivyo, ila unahitaji kuwa na moyo mpya. Inakupasa upokee hali mpya kutoka juu kwanza, ndipo utafurahia mambo ya mbinguni. Usipokuwa na hali hiyo, haitakuwa na maana yoyote, kujadiliana na mimi kuhusu uwezo wangu na kazi yangu.

Nikodemo alikuwa amesikia mahubiri ya Yohana Mbatizaji kuhusu kutubu. Walakini mahubiri hayo, ambayo ni ya kufikirisha sana, yalikuwa yameshindwa kumtubisha Nikodemo. Alishikilia hali ya Ufarisayo kamili, na alijivunia matendo yake mema. Alihesabiwa kuwa mtu mtawa sana, hivyo alijisikia kuwa yu salama, mkamilifu wa Mungu. Alishituka kusikia kuwa katika hali hiyo aliyo nayo sasa hawezi kuuona ufalme wa Mungu.

Namna ya kuzaliwa mara ya pili haikufahamika kwake. Kuongoka rohoni, kulifananishwa na mtoto aliyezaliwa. Kwa hiyo Nikodemo hakuyaelewa maneno ya Kristo. Lakini sawa kama Waisrael wengine, hakuona kuwa anahitaji badiliko lolote. Kwa hiyo alishitushwa kwa maneno ya Mwokozi. Kiburi na majivuno ya Mfarisayo huyu vilitiwa wasiwasi sana, maana anatamani kupata
[90] ukweli wote. Nikodemo akiwa na mshangao kwa ajili ya maneno hayo alijibu kwa mzaha, akasema: "Awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee?" Kama watu wengine walivyo, alieleza kuwa kitu cha kiroho

kinacholinganishwa na kitu cha asili, maana mambo ya kiroho ni mambo ya kiroho tu, hujulikana kwa hao yenyewe.

Mwokozi akinyosha mikono yake juu, aliusema ukweli kamili: "Amin, amini nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu." Hapa Nikodemo alijua kuwa Kristo anasema juu ya ubatizo wa maji, na kufanywa upya kwa uwezo wa Roho wa Mungu. Alifahamu kwamba, anasimama mbele ya yule aliyesemwa na Yohana kuwa atakuja nyuma yangu.

### Siri ya kuzaliwa upya inaelezwa

Yesu akaendelea kusema: "Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaliwa kwa Roho ni Roho." Kwa asili hali ya mwili ni uovu. Tazama Ayubu 14:4. Hakuna uvumbuzi wa kibinadamu unaoweza kupata dawa ya moyo wa mtu wa dhambi, "Moyo wa asili ni uadui na Mungu." Katika moyo hutoka "mawazo mabaya, uuaji, uasherati, uzinzi, wizi, uongo, makufuru." Warumi 8:7; Mathayo 15:19. Chemchemi ya moyo lazima iwe safi; kabla ya maji yake kuwa safi. Yule anayejaribu kuingia mbinguni kwa matendo yake, kwa kushika sheria, hufanya jambo lisilowezekana. Maisha ya Ukristo siyo kutengeneza maisha ya zamani yawe bora, ila ni mabadiliko ya hali ya asili, ya mwili. Kufa kwa ubinafsi, na hali ya dhambi, na kuishi maisha mapya kabisa. Mabadiliko ya namna hiyo huletwa na Roho Mtakatifu peke yake.

Nikodemo, alikuwa angali akitatanika. Ndipo Yesu akatumia mfano wa upepo kama kielelezo. Akasema: "Upepo huvuma utakapo, na sauti yake waisikia, lakini huwezi kujua utokako, wala uendako. Kadhalika na mtu aliyezaliwa wa Roho."

Upepo husikiwa ukitikisa majani na maua, walakini hauonekani. Hali kadhalika na Roho Mtakatifu katika moyo wa mtu. Mtu hawezi kusema kwa hakika ni lini, au wapi alipata kuongoka, lakini jambo kama hili siyo kusema kuwa bado hajaongoka, ati kwa sababu hajui ni lini au wapi. Kwa njia ya uwezo usioonekana kama upepo, Kristo hufanya hivyo kwa moyo wa mtu, kidogo kidogo hali ya mvuto wa kuelekea kwa Kristo hufanyika kwa mtu. Mambo haya hufanyika kwa ajili ya kusoma maandiko matakatifu, au kwa ajili ya kusikia mahubiri ya mhubiri. Ghafla kiasi cha msukumo wa Roho Mtakatifu, mtu hujitoa kwa Kristo. Watu wengi huita hali hii [91]

kwamba ni kuongoka kwa ghafla. Lakini sivyo, ni kazi ya Roho Mtakatifu ya wakati mrefu.

Upepo hufanya vitu vionekane na kusikia. Vivyo hivyo na kazi ya Roho Mtakatifu itajidhihirisha kwa matendo bora kwa mtu anayesukumwa naye. Roho Mtakatifu hubadilisha maisha ya mtu. Mawazo maovu huachwa, matendo ya dhambi hukanushwa. Upendo, unyenyekevu, amani huja badala ya hasira, wivu, na mashindano. Furaha huja badala ya huzuni. Mtu anapojitoa kwa Yesu kwa imani, uwezo ambao hauonekani kwa macho, huumba utu mpya kwa mfano wa Mungu. Mwanzo wa ukombozi tunaweza kuufahamu hapa duniani, kwa njia ya maisha; matokeo yake hufikia umilele.

## Nikodemo aanza kuona mwanga

Wakati Yesu alipokuwa akizungumza, nuru ya ukweli ilipenya na kuingia moyoni mwa mkuu huyu. Walakini alikuwa bado kuelewa vizuri maneno ya Mwokozi. Akauliza, huku akishangaa mambo haya yanawezaje kuwa?" Yesu akajibu: "Wewe uliye mwalimu wa Israeli, hujui mambo haya?" Badala ya kuchangamka, Nikodemo angalipaswa kunyenyekea na kujidhili kwa ajili ya ujinga wake wa kutojua mambo. Walakini Yesu alimzungumzia kwa ufasaha sana ili asichukizwe. Lakini Yesu alipomweleza kuwa kazi yake ni kusimamisha ufalme wa kiroho, wala si wa dunia, Nikodemo alitiwa wasiwasi. Yesu alipoona hivyo, aliongeza kusema: "Kama nimekuambia mambo ya dunia, nawe hukuamini, utaaminije nikikuambia mambo ya mbinguni?" Ikiwa hakufahamu kazi ya Yesu duniani, atafahamuje kazi yake mbinguni?

Wayahudi walifukuzwa na Yesu hekaluni, walikuwa na juhudi ya kujionyesha kuwa ni watakatifu kijuujuu, lakini hawakuwa watakatifu mioyoni. Walikuwa na juhudi kukariri sheria, huku wakiziasi mioyoni mwao. Haja yao kubwa ilikuwa kubadilika katika maisha kama Yesu alivyomwambia Nikodemo, yaani kuzaliwa upya kiroho, kutakasika kutokana na dhambi, na kufanywa upya katika utakatifu.

Hapakuwa na udhuru kwa Waisraeli kuhusu mabadiliko ya mioyo. Daudi alikuwa ameomba: "Ee Mungu uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu." Ahadi ilitolewa kwa njia ya Ezekieli: "Nitawapa roho mpya, nitawawekea moyo mpya, nitawondolea moyo wa jiwe, nitawapa moyo wa nyama. Nami nita-

tia ndani yenu Roho yangu, ili mwenende katika amri zangu." Zaburi 51:10; Ezekieli 36:26, 27. Nikodemo sasa alianza kufahamu maana [92] ya fungu hili. Akaona kuwa kung'ang'ania kushika na kukariri kariri sheria hakutaweza kamwe kumpeleka mtu mbinguni.

Nikodemo alivutwa kwa Kristo sasa. Mwokozi alipomweleza habari ya kuzaliwa upya, alitamani hali hiyo ionekane kwake mwenyewe. Itafanyikaje? Yesu akasema: "Kama Musa alivyomwinua nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuli wa, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

Mfano wa kuinuliwa kwa nyoka kulimfanya Nikodemo aelewe kazi ya Mwokozi. Wakati Waisraeli walipokuwa wakifa kwa kumwa na majoka, Mungu alimwambia Musa atengeneze nyoka wa shaba, na kumwinua katikati ya mkutano. Wote watakaomwangalia wangeliishi. Nyoka wa shaba alikuwa mfano wa Kristo. Kama mfano ulivyofanywa wa nyoka aharibuye, aliinuliwa kwa ukombozi wao. Vivyo hivyo aliyetwaa hali ya binadamu mwenye dhambi, ndiye atakuwa Mwokozi wao. Warumi 8:3. Mungu alitamani kuwaongoza Waisraeli wamwone Mwokozi. Wamwone kwa kuponywa majeraha yao au kwa kusamehewa dhambi zao. Wasingeweza kufanya lolote kwa nguvu zao, ila wamwamini Yesu, ambaye ni kipawa cha Mungu, Iliwapasa kumwangalia na kuishi.

Wale walioumwa na nyoka, wangelidai wafahamu kwa njia ya kitaalam. Lakini hakuna maelezo yoyote yaliyotolewa kuhusu kupona kwao. Waliokataa kuangalia waliangamia. Nikodemo alilipokea fundisho hilo akalikubali. Alichunguza maandiko ili apate uzima kwa kuamini na kujitoa zaidi. Roho Mtakatifu akamwongoza, naye akakubaliana na uongozi huo.

Leo watu maelfu wanahitaji kujifunza fundisho lile la kuinuliwa kwa nyoka, alilojifunza Nikodemo. "Hakuna jina jingine chini ya mbingu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Matendo 4:12. Tunapokea neema ya Mungu kwa imani, lakini imani siyo wokovu wetu. Haileti chochote. Ni mkono tu unaoweza kumshika Kristo, ambaye ndiye dawa ya dhambi. Hatuwezi hata kutubu bila msaada wa Roho wa Mungu. Maandiko husema juu ya Kristo Mtu huyu Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisrael toba na msamaha wa dhambi." Matendo 5:31. Toba hutoka kwa Kristo, kama vile msamaha wa dhambi.

Sisi basi tutaokolewaje? “Tazama Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Yohana 1:29. Nuru inayong’aa kutoka msalabani huufunua upendo wa Mungu. Upendo wake hutu-
[93] vuta kwake. Tusipokaidi upendo huu tutaongozwa mpaka chini ya msalaba kwa kutubu dhambi zile zilizomsulubisha Mwokozi. Halafu Roho wa Mungu huleta uzima mpya kwa imani. Ndipo mawazo, na hamu ya mtu humtii Kristo. Moyo na nia huumbika upya kwa mfano wake atendaye kazi ndani yetu, ambaye huvihisha vyote chini yake. Halafu sheria ya Mungu huandikwa katika dhamiri zetu na roho zetu, nasi tunaweza kusema pamoja na Kristo, kwamba: “Kuyafanya mapenzi yako, ee Mungu, ndiyo furaha yangu.” Zaburi 40:8

Katika mazungumzo ya Yesu na Nikodemo, Yesu aliufunua mpango wa wokovu. Katika hotuba zake zote, hakuna hata moja ambayo alieleza mpango wa wokovu kwa ukamilifu hatua kwa hatua kazi inayopaswa kutendwa katika moyo wa mtu yeyote atakayeurithi ufalme wa mbinguni. Tangu mwanzo wa kazi yake, alieleza ukweli kamili kwa mbunge huyu wa Sanhedrin, ambaye ni mwalimu wa watu wa Israeli. Lakini viongozi wa Israel hawakuikubali nuru. Nikodemo alihifadhi kweli ya Mungu moyoni mwake, na kwa muda wa miaka mitatu matunda yalikuwa kidogo sana.

Lakini maneno yaliyosemwa usiku katika mlima hayakupotea. Katika baraza la Sanhedrin Nikodemo alikazia kuuvunja mpango wa kumwangamiza Yesu. Mwishoni Yesu aliposulubishwa Nikodemo alikumbuka maneno ya Yesu kwamba “Kama Musa alivyomwinua nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali apate uzima wa milele.” Nuru kutokana na maongezi ya usiku ilimulika msalabani pale Kalwari, na Nikodemo akamwona Yesu kuwa ndiye Mwokozi wa ulimwengu.

Baada ya kufufuka kwake Bwana, wakati wanafunzi wametawanyika kwa ajili ya mateso. Nikodemo alijitokeza mbele. Alitumia mali yake kulisaidia kanisa, changa ambalo Wayahudi walikusudia kuliangamiza wakati wa kifo cha Kristo. Wakati wa hatari, Nikodemo aliyekuwa mwenye maswali na wasiwasi, alisimama imara kama mwamba, akiitetea imani na kulisaidia kahisa lipate kueneza Injili. Alitoa mali yote, akabaki kuwa maskini, lakini aliimarika katika imani aliyoipata wakati wa mazungunzo ya usiku.

Nikodemo alihusiana na Yohana kwa damu kwa historia iliyosemwa, na kwa kalamu ya kuwafundisha watu mamilioni. Ukweli wanaofundisha leo ni muhimu kama ulivyokuwa wakati wa maongezi ya usiku, wakati mtu mkuu alipokuja kujifunza kwa mnyenyekevu wa Galilaya.

## [94] 18 — Yeye Hana Budi Kuzidi Bali Mimi Kupungua’

Kama Yohana Mbatizaji angalijitangaza mwenyewe kuwa ni yeye Masihi, na afanye upinzani kwa senkali ya Kirumi, makuhani na watu wangalimfuata. Kila aina ya upinzani na kutaka heshima ya dunia hii, Shetani huunga mkono. Lakini Yohana alikataa kabisa heshima hiyo. Heshima iliyomwelekea, yeye aliielekeza kwa mwingine.

Sasa aliona makundi ya watu yakigeuka kutoka kwake na kumwelekea Mwokozi. Kila siku kundi la watu waliomjia lilizidi kupungua, maana walikwenda kumsikiliza Yesu. Jumla ya watu waliomfuata Yesu walizidi kuongezeka kila siku.

Lakini wanafunzi wa Yohana waliangalia jambo hilo kwa wivu. Wakawa tayari kumlaumu Yesu, na kazi yake. Mara swali likatokea baina ya wanafunzi wa Yohana na makuhani, kuhusu ubatizo, kwamba ubatizo hutakasa moyo wa mtu kutokana na dhambi. Walisema kuwa ubatizo wa Yesu unatofautiana na wa Yohana. Mara yakatokea mabishano kati ya wanafunzi wa Yesu na wa Yohana, kuhusu maneno yafaayo kutumiwa wakati wa ubatizo; na haki yao ya kubatiza watu. Wanafunzi wa Yohana walimjia wakiwa na masikitiko, wakisema: “Mwalimu, yule mliyekuwa naye huko Yordani, ambaye alisikia sauti ya uthibitisho, anabatiza watu pia, na watu wote wanamfuata.”

Kwa maneno haya, Shetani alileta jaribu kwa Yohana. Kama Yohana angalilalamika kwa kuwa amedharauliwa, na kuingiliwa, angekuwa amepanda mbegu za fitina, za mashaka na za wivu, katikati ya maendeleo ya Injili.

Yohana alikuwa na upungufu na kasoro za kibinadamu kama kawaida ya wote. Lakini upendo wa Mungu umembadilisha. Alikuwa katika hali ambayo si rahisi kuchafuliwa na ubinafsi, na tamaa kutaka makuu. Hakuonyesha hali ya kukubaliana na wana-
[95] funzi wake, ila alionyesha kuwa alimfurahia yule ambaye yeye anamtengenezea njia.

Alisema: “Hakuna mtu apokeaye kitu, isipokuwa amepata kutoka mbinguni. Ninyi wenyewe mnanishuhudia kuwa nimesema

kuwa mimi siye Kristo, ila nimemtangulia. Aliye na bibi arusi ndiye Bwana arusi, rafiki wa bwana arusi, anayesimama karibu naye na kumsikiliza, huifurahia sana sauti yake.” Yohana huwakilisha kama rafiki anayetumwa kati ya watu wawili wonaochumbiana; wakijitayarisha kwa ndoa. Bwana arusi anapokwisha kumpokea Bibi arusi, kazi ya rafiki, au msindikizaji, huwa imetimilika. Hufurahia katika shangwe ya maarusi. Ndivyo ilikuwa kwa Yohana pia kushuhudia jinsi kazi ya Mwokozi inavyofaulu. Kwa hiyo alisema: “Shangwe yangu imetimilika. Lazima azidi, na mimi nipungue.”

Akimwangalia Mwokozi kwa njia ya imani, Yohana alikuwa ameinuka juu ya kujikana nafsi. Yeye alikuwa ni sauti tu, iliayo nyikani. Na sasa anafurahi kukaa kimya, ili macho ya watu wote yaelekee kwenye Nuru ya uzima.

Moyo wa nabii Yohana usiokuwa na kiburi wala majivuno, ulijazwa na mwanga wa Mungu. Kwa hiyo alisema: “Ashukaye kutoka juu, yu juu ya yote .... Maana aliyetumwa na Mungu hunena maneno ya Mungu, maana Mungu hampi Roho ya kumpima, ila humpa tele.” Kristo aliweza kusema: “Sitafuti kufanya mapenzi yangu mwenyewe, bali mapenzi ya Baba aliyenituma.” Yohana 5:30.

Vivyo hivyo na wafuasi wa Kristo. Tunaweza kupokea nuru ya mbinguni tu, tunapokuwa tayari kuondoa ubinafsi ndani yetu, na kukubali kuleta kila wazo limtii Kristo. Wote wafanyao hivyo, Roho Mtakatifu hutolewa kwao bila kipimo.

Kufaulu kwa kazi ya Kristo, ambayo Yohana alikuwa akiifurahia, ilijulikana hata kwa wakuu huko Yerusalemi. Makuhani na walimu wakuu, yaani marabi, walikuwa na wivu kwa maendeleo ya Yohana, kwa vile walivyoona watu wengi wakitoka katika masinagogi na kwenda jangwani kwa Yohana. Lakini sasa yuko mwenye uwezo mkuu anayewavuta watu wengi kumwendea. Waongozi wa Waisraeli hawakuwa tayari kusema kwa Yohana kwamba, “lazima azidi, na mimi nipungue.”

## Kielelezo cha Yesu cha kuepuka kutokuelewana

Yesu alifahamu ya kuwa dhoruba ilikuwa ikijikusanya itakayomfurikia nabii mkuu, ambaye hajatokea kama yeye ulimwenguni. Yesu alitaka kuepukana na fujo ya namna hiyo, aliondoka akaenda [96]
Galilaya. Hata sisi pia tunapoishika kweli kabisa, yatupasa tuepuke

hali yoyote iletayo machafuko. Mahali popote hali ya mambo inapoelekea kuleta mtengano kati yetu, lazima tufuate kielelezo cha Yesu na Yohana Mbatizaji.

Yohana alikuwa ameitwa awe mtengenezaji wa mambo yaliyoharibika. Lakini kazi yake haikutosha kuweka msingi wa kanisa la Kikristo. Kazi nyingine zaidi ilipaswa kutendwa; ambayo itazidi ushuhuda wa Yohana. Wanafunzi wake hawafahamu hili. Walipomwona Kristo akifanya kazi pia, Waliona wivu.

Hatari ya aina ile ile ipo hata leo. Mungu humwita mtu afanye kazi fulani. Anapoiendesha kwa kadri ya ujuzi wake, Bwana huleta wengine ili kuiendeleza zaidi. Lakin wengi hujisikia kuwa mafanikio ya kazi ni juu ya yule wa kwanza. Wivu hutokea, na kazi ya Mungu hutiwa madoa. Mtu yule anayepewa sifa zisizompasa, huanza kujidhania kufaa. Watu humtegemea mtu bila kumtegemea Mungu.

Wana heri wanaojinyenyekeza, bila kuwa na ubinafsi, wakisema kama Yohana: “Lizima azidi, na mimi nipungue.”

## 19 — Yesu na Mwanawke Mwenye Waume Watano [97]

Yesu alipokuwa njiani kwenda Galilaya, alipitia Samaria. Alipofika katika kisima cha Yakobo, ilikuwa adhuhuri. Akiwa amechoka kwa safari hiyo, aliketi chini kando ya kisima, wakati wanafunzi wake walikwenda kutafuta chakula.

Wayahudi na Wasamaria walikuwa maadui. Wakati wa shida waliweza kuuziana vitu, hasa marabi. Lakini Myahudi hakuweza kukopa au kukopesha Msamaria. Hawakuhusiana kwa vyovyote. Wanafunzi katika kununua chakula, walifuata kanuni inavyotumiwa na taifa lao. Lakini kwa aina nyingine haikuwezekana hata kwa wanafunzi wa Yesu.

Yesu alipokuwa akiketi pale kisimani, alikuwa na njaa na kiu. Safari ilikuwa ndefu sana, na jua la saa sita za mchana lilimchoma sana. Kiu yake iliongezeka kwa vile alivyokuwa karibu na maji baridi yenye kuzima kiu, na hali yeye hana njia ya kuchotea maji katika kisima, kirefu jinsi hiyo.

Mara mwanamke wa Kisamaria alitokea, akiwa hana habari kuwa Yesu yuko. Akajaza chombo chake na maji. Alipokuwa akiondoka kurudi, Yesu alimwomba maji. Katika nchi za mashariki ombi la namna hiyo lisingefanyika. Kumpa maji msafiri ilikuwa huduma takatifu kwa Waarabu, ambao wangekuwa tayari kuifanya.

Mwokozi alikuwa akitafuta njia ya kuongea na mwanamke huyu ili amwambie Neno la Mungu. Kwa njia ya werevu wa upendo wa Mungu, alimwomba maji akitumaini kumvuta aamini. Mfalme wa mbinguni alikuja katika ulimwengu huu, akiomba huduma ya wanadamu. Yeye aliyeumba bahari, na kutawala vilindi vya maji, yeye anayefungua chemchemi za nchi, aliyetegemea fadhili za mgeni huyu ili ampatie maji.

Mwanamke alimwona Yesu kuwa ni Myahudi. Kwe mshangao [98]
wake, alisahau kumpatia alichoomba, ila alitaka kujua maana yake. Akasema, "Imekuwaje, wewe Myahudi kuniomba maji mimi Msamaria, ambavyo haiwi hivi?" Yesu akajibu: "Kama ungejua karama ya Mungu, na ni nani akuombaye maji, ungalimwomba

yeye, naye angekupa maji ya uzima.” Kama ungeniomba mimi ningelikupa maji ya uzima wa milele.

### Usikizi wa Mwanamke Umeamshwa

Hali ya mwanamke ikaanza kubadilika kiusemi, akasema: “Bwana, huna kitu cha kuchotea maji, na hali kisima ni kirefu sana; nawe umepata wapi maji yaliyo hai? Je, wewe ni mkuu kuliko baba yetu Yakobo, aliyetupa kisima hiki, naye alikunywa maji haya?” Mbele yake mwanamke huyu alimwona na kumfikiri msafiri huyu mchovu tu, anayetaka maji. Mwanamke huyu alimfananisha Yesu na Yakobo. Alikuwa akififikiria nyuma juu ya baba zake, na kumtazama Masihi ajaye, kumbe Masihi mwenyewe alikuwa pamoja naye, wala hakumjua. Watu wangapi leo walio na kiu ya haki huwa karibu na chemchemi, huku wakitafuta kwa mbali wapate kisima cha uzima!

Yesu alisema kwa makini: “Anywaye haya huona kiu tena: bali atakayekunywa maji nitakayompa hataona kiu kabisa: lakini maji nitakayompa yatakuwa chemchemi ibubujikayo hata uzima wa milele.”

Kila mahali watu hutafuta kitu kitakachowaridhisha katika haja zao. Mtu mmoja tu awezaye kuridhisha kila mwenye haja, yaanikn-sto. Yeyendiye “Tunu ya mataifa yote.” Neema ya Mungu anayoitoa ni kama maji yenye uhai, yatakasayo, na kuimarisha mtu.

Yesu hakusema kuwa kila mtu achotaye maji haya tu ataridhishwa haja yake. Yule atakayeonja upendo wa Yesu atazidi kuutaka zaidi, wala hatataka kitu kingine zaidi. Utajiri, cheo na anasa za dunia havitamvutia kamwe. Kilio chake cha daima kitakuwa zaidi kwa Bwana. Mwokozi wetu ni chemchemi isiyokauka. Tunaweza kunywa kwake zaidi na zaidi bila upungufu wowote.

Yesu alikuwa ameamsha usikizi wa mwanamke huyu na shauku yake kwa kipawa alichotaka. Akasema, “Bwana, nipe maji hayo, ili nisione kiu tena, wala nisije hapa kuchota maji.”

### Siri ya mambo yake ya nyuma

[99] Sasa Yesu aligeuza maongezi yake ghafla. Mwanamke huyu apaswa kupokea karama ambayo Yesu anatamani kuitoa, yaani lazima afahamu makosa yake na amfahamu Mwokozi wake pia.

Yesu alimwambia, “Nenda ukamwite mume wako, mje naye hapa.” Mwanamke akajibu, “Sina mume.” Lakini Mwokozi akaendelea kusema, “Umesema vema kwamba sina mume, maana una waume watano, na yule uliye naye siye mume wako. Umesema kweli.”

Mwanamke alitetemeka. Mkono wa siri ulikuwa unafunua kurasa za maisha yake. Ni nani huyu anayeweza kugundua siri ya maisha yake? Mawazo yakamjia ya mambo ya milele, na hukumu ya mwisho, wakati siri zote zitakapofichuliwa. Alijaribu kupiga chenga, lakini alishindwa. Basi akasema: “Bwana naona kwamba wewe u nabii.” Halafu akitaka kukomesha mazungumzo, aligeukia mambo ya dini.

Kwa uvumilivu Yesu alingojea nafasi ya kumweleza ukweli kamili. Mwanamke alisema, “Baba zetu waliabudu katika mlima huu, nanyi mwasema kuwa, Yerusalemu ndipo mahali pa kuabudu.” mlima wa Gerizimu ulikuwa unaonekana, ambao ndio uliokuwa ukishindaniwa baina ya Wayahudi na Wasamaria. Kwa muda wa miaka mingi Wasamaria walijichanganya na waabudu sanamu, kwa hiyo dini yao ikapotoshwa na kuharibika kabisa; watu wote wakaharibika.

Wakati hekalu la Yerusalemu lilipojengwa na Ezra, Wasamaria walitaka kuungana na Wayahudi ili wajenge mji. Jambo hili lilikataliwa, kwa hiyo uadui ukaibuka kati ya mataifa hayo mawili. Wasamaria walijenga hekalu juu ya mlima wa Gerizimu kwa kushindana na Wayahudi. Lakini hekalu lao liliharibiwa na maadui, wakaonekana kama wamelaaniwa. Walakini hawakuliamini au kulikubali hekalu lililokuwa Yerusalemu; kama ni nyumba ya Mungu, wala hawakukubali kuwa dini ya Wayahudi ilikuwa dini bora.

Yesu akimjibu mwanamke, alisema: “Saa inakuja ambayo hamtaabudu katika mlima huu, wala Yerusalemu. Mnaabudu msichojua, sisi tunaabudu maana wokovu unatoka kwa Wayahudi.” Sasa Yesu alitaka kuondoa uhasama huu baina ya Wasamaria na Wayahudi. Ukweli mkuu wa wokovu ulikuwa umekabidhiwa kwa Wayahudi, na kutokana na wao Masihi atatokea.

Yesu alitaka kuinua mawazo ya mwanamke huyu yaondoke katika mambo ya ushindani. Akasema: “Saa inakuja, na sasa ipo, ambayo wamwabuduo Baba halisi watamwabudu katika roho na kweli, maana Baba atafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni
Roho, na watu wamwabuduo yeye inawapasa kumwabudu katika [100]
roho na kweli.”

Watu hawaletwi mbnguni kwa njia ya mlima mtakatifu, au kwa hekalu takatifu. Ili tupate kumwabudu Mungu sawasawa, hatuna budi kuzaliwa kiroho kutoka juu. Jambo hili litatakasa moyo na kuimarisha dhamiri, na kutuwezesha sisi tutembee katika utii wa maagizo yake. Hii ndiyo ibada ya kweli. Haya ndiyo matunda ya utendaji wa Roho ndani yetu. Mtu yeyote anapomtafuta Mungu kikweli, utendaji wa Roho Mtakatifu huonekana, na Mungu hujidhihirisha kwa mtu huyo.

Mwanamke alipokuwa akizungumza naye, maneno ya Yesu yalimwingia. Maisha yake ya zamani yalipofunuliwa wazi, akaona kiu ya haki moyoni mwake, ambavyo maji ya kisima cha watu hayawezi kumaliza. Hakuna kilichovuta usikivu wake kuliko hiki. Ingawa Yesu alimtobolea siri zake, walakini alimhesabu kuwa rafiki yake, anayemhurumia na kumpenda. Ijapokuwa utakatifu wa Yesu umefunua dhambi zake, lakini Yesu hakutamka neno lolote la kumlaumu kwa ajili ya dhambi hiyo, Yesu amekuwa akiongea juu ya neema iwezayo kutakasa moyo wake. Swali alilouliza kuhusu Masihi lilisahauliwa, vile alihisi kuwa ni yeye. Alisema: "Najua kuwa Masihi, ambaye ni Kristo, akija atatueleza yote." Yesu akasema "Mimi nizungumzaye na wewe ndimi Masihi."

Mwanamke aliposika maneno hayo imani ilichemka rohoni mwake. Akakubaliana na usemi wote uliosemwa na Mwalimu wa mbinguni.

Moyoni mwa mwanamke huyu kulikuwa na furaha sana. Alipendezwa na maandiko matakatifu. Roho Mtakatifu alikuwa akimtayarisha kupokea ukweli mwingi zaidi. Unabii wa Agano la Kale ulikuwa ukimulika moyoni mwake. Maji ya uzima ambayo Kristo humpa kila mwenye kiu, yalikuwa yakianza kububujika moyoni mwake.

Maelezo ya wazi yaliyoelezwa na Kristo kwa mwanamke huyu, yasingalielezwa na Wayahudi wanaojiona kuwa haki machoni pao. Mambo hayo yamefichika kwao, na wanafunzi wanayachuchumilia. Hayo yamefunuliwa kwa mwanamke huyu. Yesu akamwona kuwa atashirikiana na wengine furaha hii pia.

Wanafunzi wake waliporudi, walishangaa kumwona Mwalimu wao anazungumza na mwanamke. Hakungoja kula chakula kilicholetwa na wanafunzi. Mwanamke alipokwisha kwenda, wanafunzi walimsihi Yesu ale chakula. Walimwona akiwa kimya na uso wake

ukingaa. Waliogopa kumwingilia, huku wakifikiri kuwa si vema [101]
kunyamaza bila kumpa chakula. Yesu akielewa watakavyo, alisema, “Nina chakula ambacho ninyi hamkijui.

Wanafunzi wakawa na wasiwasi, kuwa ni nani aliyemletea chakula! Halafu Yeye alisema: “Chakula changu ndicho hiki, kuyafanya mapenzi yake yeye aliyenipeleka, na kuimaliza kazi yake.” Kumhudumia mtu aliyekuwa na njaa na kiu ya ukweli wa Mungu, ulikuwa muhimu yake kuliko kula chakula; au kunywa maji.

Mwokozi wetu alitamani kuwashughulikia na kuwafadhili watu ambao aliwanunua kwa damu yake. Kama vile mama anavyofurahia kicheko cha mtoto wake anayekua, ndivyo Kristo anavyofurahia yule anayekua kiroho.

Mwanamake yule alijazwa na furaha alipokuwa akiyasikiliza maneno ya Kristo. Aliuacha mtungiwake pale, akarudi mjini ili kupasha habari hizi kwa wengine. Alisahau mambo ya kuchota maji, na kiu ya Kristo aliyotaka kushughulikia. Kwa furaha iliyojaa moyoni mwake aliharakisha kwenda kuwapasha wengine juu ya nuru aliyopokea.

Alipaaza sauti akisema: “Njooni mwone mtu aliyeniambia mambo yangu niliyofanya.” “Je huyu siye Kristo?’ Alikuwa na mabadiliko usoni pake, na hali yake ilichangamka sana. Wakatoka mjini wakamwendea.

Yesu alipokuwa angali akiketi pale kisimani, aliangalia uwanda ulioenea mbele yake umejaa nafaka pevu iliyokomaa. Akinyosha mikono yake kuuelekea, alisema kwa mfano: “Hamsemi ninyi, Imebaki miezi minne ndipo yaje mavuno? Angalieni nawaambia, Inueni macho yenu, mkayatazame mashamba, kwa maana yamekuwa meupe tayari kwa mavuno. Hapa yalikuwako mavuno tayari kwa kuvunwa.

## Mzunguko wa Mavuno ya Injili

“Avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda katika uzima wa milele, ili wote, yeye apandaye naye avunaye wafurahi pamoja.” Huu ni usemi wa kweli kwamba mmoja hupanda na mwingine huvuna. Wale wanaopokea Injili huwa wajumbe wake walio hai. Mmoja hupanda mbegu; mwingine hukusanya mavuno; wote hufurahia pamoja thawabu ambayo ni malipo ya kazi.

Yesu alisema kwa wanafunzi wake. "Niliwatuma ninyi mkavune pale ambapo hamkupashughulikia. Watu wengine walipashughulikia, na ninyi mkaingia katika kazi yao. Wanafunzi walikuwa
[102] wanaingia katika kazi za watu wengine. Mjumbe asiyeonekana alifanya kazi kimya kimya, lakini mavuno yalipatikana. Kristo alikuwa karibu kuzimwagilia mbegu kwa damu yake mwenyewe. Wanafunzi walikuwa wenzake Kristo katika kazi pamoja na watakatifu wa zamani. Kwa njia ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste, watu maelfu waliongolewa kwa siku moja. Hii ilkuwa kazi ya kupanda ya Kristo, na mavuno ni ya kazi yake.

Wasamaria walikuja wakamsikiliza Yesu, wakaamini. Kundi kubwa la watu waliomzunguka kisimani, walimsikiliza kwa makini, na kuuliza mambo mengi ambayo hayakujulikana kwao zamani. Mashaka ya kila namna waliyokuwa nayo yalianza kutoweka. Wakitamani kumsikiliza zaidi, wakamkaribisha katika mji wao kwa muda wa siku mbili alikaa na Wasamaria hao, na matokeo yalikuwa makubwa, maana watu wengi waliamini.

Yesu hakutenda mwujiza wowote kwao, isipokuwa kule kumwambia yule mwanamke siri yake katika maisha yake ya zamani. Walakini watu wengi walimpokea. Kwa ajili ya furaha yao walimwambia yule mwanamke: "Sasa tumeamini siyo kwa maneno yako, maana tumemsikia sisi wenyewe, na tunajua kuwa huyu ndiye Kristo hakika, Mwokozi wa ulimwengu.

## Kristo avunja ukuta wa chuki

Yesu alikuwa ameanza kuvunja kuta za chuki baina ya Wayahudi na watu wa mataifa, na kuhubiri Injili kwa ulimwengu wote. Alijichanganya kamili na Wasamaria, na kuwafanyia fadhili watu hawa waliodharauliwa. Alilala nyumbani mwao, akala pamoja nao, akafundisha katika njia zao, na akawatendea kwa wema kamili

Katika hekalu la Yerusalemu katika ukuta mfupi uliotenganisha sehemu nyingine, palikuwapo na maandishi yakisema kwamba, hakuna mtu anayeruhusiwa kupita hapa isipokuwa Myahudi peke yake. Mtu wa mataifa kama angalipita sehemu hii, angalilipa maisha yake, yaani angaliuawa. Lakini Yesu asili ya hekalu hilo, aliwaletea watu wa mataifa wokovu walionyimwa na Wayahudi.

Wanafunzi walishangaa kwa vile Yesu alivyokuwa. Siku mbili walizokaa Samaria waaminifu kwake, walijizuia wasionyeshe hali ya ubaguzi, lakini mioyoni walikuwa na hali hiyo. Walikuwa wagumu kujifunza namna hiyo iliyowafanya wakose fadhili na huruma kwa watu. Lakini baada ya kupaa kwa Bwana, fundisho hili liliwajia kwa uwezo mpya. Walikumbuka hali bora ya Yesu, kuhusu usemi [103]
wake, fadhili zake, na jinsi alivyowahesabu watu waliodharauliwa. Petro alipokwenda kuhubiri Samaria alikuwa na roho ile ile. Yohana alipoitwa huko Efeso na Smirna, alikumbuka mambo ya Shekemu, na hali ya Bwana Yesu alivyokuwa.

Watu wanaojiita kuwa wafuasi wa Mwokozi, wanaweza kudharau na kutenga watu, lakini hakuna kutenga mtu kwa ajili ya mahali alikozaliwa, wala kabila, wala kitu chochote kisichomfanya mtu asimfadhili mtu, hata akiwa mwenye dhambi kiasi gani. Mwito wa injili hutolewa kwa wote katika kisima cha Yakobo Yesu, hakuacha kusema na mwanamke, ingawa alikuwa mwenye dhambi kiasi gani.

Kila mara alianza fundisho lake kwa watu wachache waliokuwa wakimzunguka, lakini watu waliopita njiani walizidi kuongezeka na kusikiliza, mpaka ukawa mkutano mkubwa ukawa ukimsikiliza Mwalimu wa mbinguni kwa mshangao mkubwa. Leo, anaweza kuwa na mtu mmoja tu, anamsikiliza mtenda kazi wa Bwana, lakini nani aweza kujua jinsi mvuto huo utakavyokwenda mbali?

Mwanamke wa Kisamaria alithibitisha jinsi alivyokuwa mtendakazi anayefaa, kuliko wanafunzi wa Yesu. Kwa njia ya mwanamke huyu, mji mzima ulileta kwa Bwana. Kila mfuasi wa Bwana anayezaliwa upya ni mtendakazi. Anayekunywa maji ya uhai, huwa chemchemi ya kunywesha wengine, maji ya uzima. Anayepokea, huwa mtoaji. Neema ya Yesu inapokuwa moyoni mwa mtu, ni kama chemchemi jangwani, huwanywesha wote waliokuwa karibu kupotea, wapate burudiko la uzima.

[104] ## 20 — “Msipoona Ishara na Maajabu”

Wagalilaya waliorudi kutoka Yerusalemu kwa pasaka, walileta habari za mambo ya ajabu waliyoona kwa Yesu. Watu wengi walilalamika kwa ajili ya kuchafua hekalu, na kwa ajli ya uchoyo na ufidhuli wa makuhani. Walitumaini kuwa mtu huyu aliyewafukuza wakuu hekaluni anaweza kuwa ndiye Mkombozi wao, waliyemtazamia kwa muda mrefu. IIisemekana kuwa nabii Yohana Mbatizaji amejitangaza kuwa ndiye Masihi. Habari za kurudi kwa Kristo kutoka Kana pia, zilienea pote, katika Galilaya. Katika Kapernaumu habari hizi zilimvutia Myahudi mmoja aliyekuwa katika utumishi wa utawala. Mwana wa mtu huyu alikuwa na ugonjwa unaosemekana kuwa hauponyeki. Baba yake aliposikia habari za Yesu, alikusudia kutafuta msaada kwake. Alitumaini kuwa, akimsihi atamhurumia.

Alipofika huko Kana, baba huyu alipenyapenya katika mkutano mpaka akamfikia Mwokozi. Imani yake iliweweseka, kwanza alipomwona Yesu akiwa mtu wa kawaida tu, mwenye mavazi ya kawaida, hali amechoka kwa ajili ya safari. Basi alimzungumzia, akamweleza jambo lililomleta kwake. Akamwomba Mwokozi afuatane naye kwenda kwake.

Yesu alijua kwamba, moyoni mwake alikuwa akimtakia mwanawe uzima, maana alikuwa akimwamini. Na kama haja yake ikikataliwa hawezi kumwamini kuwa ndiye Masihi. Wakati mtu yule alipokuwa akingoja kwa uchungu, Yesu alisema, “Msipoona dalili na maajabu, hamwezi kuamini.”

Mwokozi alitofautisha swali la mwombaji na mashaka na imani kamili ya mwananike wa Samaria ambaye hakuomba ishara wala mwujiza. Maneno yake yalikuwa na uwezo uliowagusa mioyo.
[105] Alisikitika kwamba watu wake hasa walishindwa kutambua sauti ya Mungu ikisema ndani ya Mwanawe.

Hata hivyo diwani huyo alikuwa na imani kiasi fulani, maana alikuja kuomba msaada, ambao ni jambo muhimu kwake. Yesu alikusudia, si kumponya kijana wake peke yake, ila kuwaongoa watu wote wa nyumba hiyo, na kuwasha mwanga katika Kapernaumu

nzima. Lakini diwani huyu lazima atambue haja yake kuu, kabla ya kupata neema ya Kristo. Watu wengi katika taifa lake walimpenda Kristo kwa nia ya ubinafsi. Imani yao kwake ilikuwa kwa ajili ya kupata misaada ya muda tu, lakini hawakuona haja ya neema ya Mungu.

Kama kimuli cha nuru, maneno ya Kristo yaliufunua moyo wake ukawa wazi. Akaona kuwa nia yake ilikuwa ya ubinafsi. Haja yake ikafunuliwa kuwa ilikuwa imejifunika katika ganda, kumbe sivyo ilivyo. Akatambua kwa masikitiko kuwa kusitasita kwake kungeweza kugharimu maisha ya mwanawe. Akalia kwa uchungu: "Bwana, shuka nyumbani kwangu, mtoto wangu yumo kufani." Imani yake ikamshikilia Kristo kama Yakobo alipokuwa akishindana na malaika, alisema: "Sikuachi, usiponibariki." Mwanzo 32:26 Alishinda sawa na Yakobo. Yesu akasema, Enenda zako, mtoto wako amepona." Diwani akatoka kwa Yesu akifurahi sana, huku akiwa na amani kamili.

Wakati ule ule watu waliokuwa wakimwuguza mtoto waliona mabadiliko ya ghafla kwake. Hali ya homa ikageuka kuwa uzima wa afya safi. Nguvu za mwili zikatokea badala ya udhaifu katika mwili wake. Hakuna dalili yoyote ya ugonjwa iliyosalia kwake. Akapona kabisa, mwili wake ukawa safi, na akaendelea kulala tu. Jamaa yake wakashangaa, ikawa furaha kubwa.

Yule diwani angalifika nyumbani wakati wa jioni ile, baada ya kuongea na Yesu, lakini hakuwa na haraka ya kuja nyumbani, mpaka kesho yake ndipo akafika Kapernaumu. Ilikuwa hamu kubwa kiasi gani kwa wote wa nyumbani.

Alipomwendea Yesu alikuwa na huzuni kubwa. Sasa hali yake ni tofauti kiasi gani! Aliposafiri katika utulivu wa asubuhi, hali ya nchi ilionekana kuwa inamsifu Mungu, yeye akiwa mmoja wao. Alipokuwa angali kitambo kufika kwake, watumishi walimlaki ili kumtuliza, maana walijua kuwa hali yake ni ya wasiwasi. Hakushtuka kusikia habari walizomletea, ila aliwauliza tu, muda ambao homa ilmwacha. Wakamjibu: "Jana, muda wa saa saba, ndipo homa
ilimwacha." Wakati ule ule imani ya mzee ilipoimarika kwa Yesu; [106]
na Yesu akasema: "Mwanao yu hai," ndipo upendo wa Mungu ulipomgusa kijana aliyekuwa katika kufa.

Baba akaharakisha kwenda kumpa pole mwanawe. Alimkumbatia, kama mtu atokaye Kifoni, akamshukuru Mungu tena na tena kwa ajili ya kuponywa kwa ajabu.

Baadaye diwani alipozidi kujifunza neno la Mungu, ndipo mji wake wote wakawa wafuasi wa Kristo. Habari za mwujiza huu zikaenea pote, na mji wa Kapernaumu ukatayarishwa kwa kazi ya Kristo.

Sisi nasi sawa na baba yule, mara kwa mara humtafuta Yesu ili atusaidie katika mambo ya duniani, na kwa kutupatia haja zetu, humtegemea. Mwokozi anatamani kutupatia mibaraka zaidi kuliko ile tuombayo, naye hukawia kutujibu, ili apate kujua dhambi zetu, na kuona haja zetu kubwa za neema yake. Anataka tuondoe ubinafsi unaotufanya tumwendee.

Diwani alitaka kuona utimilifu wa haja yake kwanza kabla hajamwamini lakini inampasa aliamini neno la Mungu kwamba maombi yake yamesikiwa, na haja yake itatolewa. Siyo kujisikia au kuona kuwa Mungu atusikia ndipo tuamini. Yatupasa kuziamini ahadi zake. Tunapomwomba, lazima tuamini kuwa tunapokea tuliyoomba, na tushukuru ya kuwa tumepokea. Kisha tuendelee katika shughuli zetu tukijua kuwa haja zetu zitatujia wakati tuzihitajipo zaidi.

## 21 — Bethzatha na Sanhedrin [107]

“Sasa katika Yerusalemu, penye mlango wa kondoo pana birika iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha ina matao matano. Ndani ya hayo jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, viwete, nao waliopooza, wakingoja maji yachemke.”

Wakati fulani maji hutibuliwa katika birika, na iliaminiwa kuwa kuna uwezo usiokuwa wa kibinadamu, na kwamba mtu yeyote atakayetumbukia humo mara ya kwanza, ataponyeka ugonjwa wake. Watu wengi walikuwa wakingoja maji hayo; lakini watu walizidi sana, hata waliokuwa na nguvu walikuwa wakiwakanyaga wadhaifu, wakikimbilia kuponywa. Wengi waliweza kufika hapo walifia kwenye kingo zake kwa kukosa uwezo wa kuingia ndani. Kambi zilijengwa kando kando yake na kuwahifadhi wagonjwa. Baadhi ya wagonjwa walilala kando ya matao hayo wakingoja maji yatibuliwe.

Yesu alikuwako Yerusalemu tena. Akitembeatembea huko mwenyewe, akiwa na kusudi la kuomba, walifika kwenye dimbwi hilo. Akiwaona wagonjwa hao, alitamani kutumia uwezo wake wa kuponyesha, na kumponya kila mgonjwa. Lakini ilikuwa siku ya Sabato, naye alijua kuwa akitenda tendo la kuwaponya watu, ataleta fujo sana kwa Wayahudi, na atakatiza kazi yake kabla ya wakati.

Walakini Mwokozi alimwona mtu mmoja aliyekuwa mgonjwa zaidi ya wote, mtu ambaye amekuwa hawezi, kwa muda wa miaka thelathini na minane. Ugonjwa wake ulihesabiwa kana kwamba ni adhabu kutoka kwa Mungu. Akiwa peke yake, bila msaada wowote, ni kana kwamba ametengwa mbali na huruma za Mungu. Mgonjwa huyu ameugua muda wa miaka thelathini na minane bila kuhurumiwa na mtu yeyote. Wakati maji yalipotibuliwa, watu waliomhurumia walimchukua kuelekea kwenye dimbwi. Lakini wakati huo [108]
inavyoelekea kutibuliwa kwa maji, hukosa mtu wa kumwingiza dimbwini. Kwa muda wote hakuweza kufika mbali zaidi ya ukingo wa dimbwi, Juhudi yake ya kuingia dimbwini na uchungu wa kukosa kuingia, vilimdhoofisha sana.

Mgonjwa alikuwa amelela katika kirago chake, wakati alipofikiwa na mtu mwenye uso wa huruma. Maneno yenye tumaini, kwamba: "Unataka kuwa mzima?" yalimsisimua. Alitumaini kuwa inawezekana kupata msaada. Lakini tumaini lake lilififia mara. Alikumbuka jinsi alivyokuwa akijaribu kila mara, na kushindwa. Akasema: "Bwana sina mtu wa kunisaidia, wakati maji yanapotibuliwa, kunitupa dimbwini, lakini wakati ninapojikakamua, mtu mwingine hutangulia mbele yangu kutumbukia dimbwini."

Yesu hakumwambia mgonjwa huyu amwamini, ila tu alisema: "Inuka ujitwike kitanda chako uende." Lakini imani ya mtu huyu ikamshikilia Yesu. Kila mshipa wake, na misuli yote ikapata uhai mpya. Akayaamini maneno ya Kristo, na kutii maagizo yake, kwa hiyo mishipa yote ikapata nguvu. Akaruka kwa miguu yake, akawa mtu mzima.

### Siri ya kuponywa kiroho

Mtu huyo lazima alikuwa amepoteza tumaini la kupona. Lakini aliyaamini maneno ya Kristo na alipofuata yale aliyoambiwa alipata baraka ya kupona. Sisi pia tunaweza kupata kuponywa kiroho kwa imani ile ile. Dhambi imetutenga na uzima wa Mungu, na tumekufa ganzi. Hatuwezi kwa nguvu zetu kuishi maisha matakatifu kama mtu yule alivyoshindwa kutembea. Watu wengi wanaotambua kushindwa kwao, nao hujaribu kufaulu kwa nguvu zao hufanya kazi bure. Mwokozi huwainamia watu hao wasumbukao bure, na kusema: "Mwataka kuwa wazima?' Msingoje kujisikia kuwa mnapona. Yaamini maneno yake na wekeni nia zenu kando ya Kristo. Mkitii maneno yake mtapokea nguvu. Maovu yoyote yaufungao mwili na roho Kristo anaweza kukuokoa. Atatia uzima rohoni, ambayo ni "mfu katika uasi." Waefeso 2:1

Mwenye kupooza aliinama akachukua blanketi yake na virago vyake vingine, alipoinuka akamtafuta Mponyaji wake. Lakini Yesu alikuwa amechanganyika ndani ya mkutano. Alipoondoka akienda zake basi amepona kamili, hali akishangilia kupata nguvu mpya, aliwaeleza Mafarisayo kadhaa juu ya kupona kwake. Alishangazwa
[109] na hali yao, jinsi walivyosikiliza habari hizo kwa ubaridi sana.

Pole pole walimkata kauli wakimwuliza, kuwa kwa nini anajitwika kitanda siku ya Bwana. Kwa furaha yule mtu aliyokuwa

nayo, alisahau kuwa ilikuwa siku ya sabato. Alijibu kishujaa: “Aliyeniponya ndiye aliyeniambia kuwa “jitwike kitanda chako uende.” Walimwuliza kuwa, ni nani aliyefanya haya, lakini yeye hakuweza kusema. Wakuu hawa walitaka thibitisho dhahiri, ili waweze kumhukumu Yesu kuwa ni mvunja Sobato. Hakuvunja Sabato tu, bali amefanya kosa pia la kumwambia mtu yule abebe kitanda siku ya Sabato.

## Kanuni zisizokuwa na maana

Wayahudi walipotosha sheria kabisa, hata ikageuka kuwa mzigo mzito kwa watu, na wakafanya kuishika kuwe jambo lisilovumiliwa. Myahudi hakuruhusiwa kuwasha moto, au kuwasha mshumaa siku ya Sabato. Hivyo watu waliwategemea watu wa mataifa kuwafanyia mambo yale waliyokatazwa kufanya wao wenyewe. Walidhani kuwa wokovu ulikusudiwa kwa Wayahudi tu, na kanuni za watu wengine zilikuwa ovyo tu. Lakini Mungu hakutoa sheria ambayo haiwezi kutiiwa na watu wote.

Katika hekalu, Yesu alikutana na mtu aliyekuwa ameponywa. Alikuja kutoa sadaka ya dhambi, na sadaka ya shukrani kwa rehema alizopata. Yesu aliwajulisha kwake. Mtu yule alishangilia kwa kukutana na Mponyaji wake. Bila kujali uhasama wanaomfanyia Yesu, aliwaeleza Mafarisayo kuwa huyu ndiye aliyeniponya. Kwa hiyo walimsumbua Yesu, wakakusudia kumwua, kwa sababu anavunja Sabato.

Yesu alifikishwa katika bunge la Sanhedrin ili kujibu mashtaka hayo. Kama Wayahudi wangekuwa wanajitawala, mashitaka hayo ya kuvunja Sabato yangalileta kifo kwa Yesu. Lakini mashitaka ya jinsi hiyo hayana uzito wowote katika mahakama ya Kirumi. Mambo mengine walitumaini kuwa yatawasaidia. Kristo alikuwa na mvuto mkubwa kwa watu, kuliko Mafarisayo. Makundi ya watu hayakupenda hotuba za Marabi kama zile za Yesu. Alikuwa akinena maneno ya kweli ya Mungu, wala si kama mlaumuji na msutaji mwenye kuhukumu. Kwa njia ya mafundisho yake na matendo yake ya huruma alivunja nguvu za kanuni za wanadamu, alitoa neno dhahiri, na kuudhihirisha upendo wa Mungu.

[110] **Watu wamkusanyikia Yesu**

Katika mojawapo ya unabii unaomhusu Yesu, iliandikwa: “Fimbo ya enzi haitaondoka kutoka kwa Yuda, wala mtoa sheria katikati ya miguu yake, mpaka Shilo ajapo, na kwake mataifa yatakusanyika.” Mwanzo 49:10. Watu walikuwa wanakusanyika kwa Kristo. Kama makuhani na marabi wasingekuwa wanaingilia, mafundisho yake yangalileta mabadiliko ya ajabu ambayo hayajaonekana. Lakini wakuu hawa walikusudia kuharibu mvuto wa Yesu. Mipango waliyokuwa wakipanga katika Sanhedrini, na malaumu ya waziwazi juu yake, vingesaidia kuvunja mvuto wake. Mtu yeyote aliyethubutu kumlaumu Rabi, alihesabiwa kama mhaini. Kwa jambo hili marabi walitumaini kuchochea fitina juu ya Yesu alipokuwa akijaribu kuzikanusha desturi za marabi, na hivi wakaleta mgawanyiko katika watu, na kuandaa njia ya kuwa chini ya utisho wa Warumi.

Baada ya Shetani kushindwa kumwangusha Yesu jangwani, alijikusanya tena apate kumdhoofisha Yesu na kazi yake. Aliwapofusha Wayahudi wasimtambue Yesu kuwa ndiye Mwokozi, wakaungana na waongozi wao, wakimhesabu mkuu wa ukweli kuwa ni adui yao. Akawafanya wamkane Kristo, na kumwudhi daima. Kwa njia hiyo wangalimkatisha tamaa na kuvuruga kazi yake.

Yesu alikuja kuitukuza sheria, na kuifanya iheshimiwe. Isaya 42:21. Alikuja kuifungua Sabato kutokana na mambo ya kiutumwa watu waliyoiwekea, mpaka” ikaonekana kuwa ni laana badala ya kuwa baraka. Kwa ajili ya hayo aliamua kuponya mgonjwa siku ya Sabato, huko Bethzatha. Angeweza kuponya mgonjwa siku nyinginezo, au angemponya bila kumwagiza ajitwike kitanda chake. Lakini alichagua njia hiyo na kumwambia mtu ajitwike kitanda apite wazi akionwa na kila mtu katika siku hiyo. Jambo hili lingeonyesha kuwa anakanusha mambo ya marabi na sheria mbaya juu ya Sabato, ambayo ni siku ya Bwana.

Yesu alitangaza kuwa kumponya tu mwenye dhiki siku ya Sabato ni tendo halali kabisa kufanywa siku ya Bwana. Malaika wa Mungu daima huwahudumia wanadamu. “Baba yangu hufanya kazi siku zote, vivyo hivyo na mimi nafanya kazi.” Siku zote ni za Mungu za kuendeshea mpango wa wokovu kwa ajili ya wanadamu. Kama Wayahudi wangetafsiri na kuieleza sheria kikamili, ndipo

aliyeiumba sabato angefanya nafasi katika kazi yake, na angekomesha mzunguko wa ulimwengu ambao hauna mwisho.

Je, Mungu angekataza jua lisifanye kazi yake siku ya Sabato? [111]
Je, azuie vijito vya maji visifurike kunywesha nchi siku ya Sabato? Je, azuie ngano na mahindi kukua siku ya sabato? Je, miti na maua visichanue siku ya Sabato?

Mungu asingeweza kuzuia mkono wake usifanye kazi hata nukta moja, ama sivyo, watu na viumbe hai vingezimia na kufa. Mwanadamu pia anayo kazi impasayo kufanya siku ya Sabato. Wagonjwa lazima wahudumiwe, mahitaji ya lazima budi yatolewe. Siku takatifu ya Mungu ya kupumzika ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu. Mungu hataki viumbe vyake viwe na taabu hata saa moja, ila lazima vishughulikiwe, siku ya Sabato.

Amri ya Sabato hukataza kufanya kazi za kawaida siku hiyo, kazi za kujishughulikia ili upate riziki, lazima zikome. Hakuna kazi za kujipatia mapato zinazokuwa halali kufanyika. Lakini kama vile Mungu alivyoacha kufanya kazi siku hiyo, na kustarehe katika Sabato, vivyo hivyo mtu pia afanye kazi siku sita, na kustarehe siku ya Sabato. Sabato ni ya kuabudu, na kutenda matendo matakatifu.

Lakini Mafarisayo walikuwa wakichukiza zaidi. Yesu hakuvunja sheria tu, jinsi wao walivyodhani, lakini kwa kumwita Mungu ni "Baba yake", alijitangaza kuwa sawa na Mungu. Walimlaumu kuwa anakufuru. Maadui hawa wa Kristo, waliziita kanuni zao na desturi zao kuwa ni mambo ya dini. Hizi zilionekana kuwa hazifai kitu kulinganisha na maelezo ya Yesu ya kutoka katika Neno la Mungu, na kufuatana na hali ya ulimwengu katika mzunguko wake usiokuwa na mwisho. Lakini Marabi walipotosha maelezo yake, wakawachochea watu wamchukie kwa kuwa anajifananisha na Mungu. Kama makuhani na marabi wasingekuwa wanaogopa watu wangalimwua mara moja. Lakini mvuto wake kwa makutano ulikuwa mkubwa sana. Wengi waliona kuwa kumponya mgonjwa wa Bethzatha ilikuwa sawa kabisa.

### Yesu alitegemea uwezo wa Baba

Yesu aliyakanusha malaumu kuwa, anakufuru. Alisema: "Mamlaka yangu kuwa mimi Mwana wa Mungu; ambaye kwa hali niko pamoja na ninyi, yaani ninafanana na ninyi. Ninashiriki pamoja na

Mungu. Mwana hawezi kufanya kitu kwa mapenzi yake mwenyewe, ila kwa yale aliyoona kwa Baba.” makuhani na Marabi walikuwa wakizungumza, Mwana wa Mungu kufanya kazi aliyotumwa na kufanya ulimwenguni. Basi kwa mambo hayo waliona kuwa wana
[112] ushahidi wa kutosha, wala hawana haja zaidi. Lakini Mwana wa Mungu alikuwa anamtegemea Baba katika uwezo wake, na hekima yake. Kristo hakujitungia mambo. Kila siku Baba alikuwa anampangia mambo. Sisi pia inatupasa tumtegemee Mungu, ili maisha yetu yapatane na mapenzi ya Mungu.

Maneno ya Kristo hutufundisha kwamba, sisi tusingejitenga mbali na Mungu, aliye Baba yetu katika mambo yetu yote, hata kama ni jambo gani, lazima tumtegemee Mungu tu. Yeye ametuweka katika kazi yoyote ile, na anatukubali kuifanya. Kadiri tunavyojitoa kwake na kuomba hekima kwake, na kumtegemea kabisa, tutaongozwa katika mapito ya usalama, na kutimiza kazi ile tuliyopewa. Lakini mtu yeyote anayejitegemea kwa akili zake, hutengana na Mungu na kusimama upande wa adui wa Mungu.

Masadukayo waliamini kuwa hakuna ufufuo wa wafu, lakini Yesu aliwaambia kuwa, kazi kubwa ya Baba yake ni kuamsha watu waliokufa. Na yeye mwenyewe anao uwezo wa kufanya hivyo pia. “Jinsi Baba awafufuavyo wafu, na kuwafanya waishi, vivyo hivyo na Mwana vile vile, kwa wale anaotaka. “Saa inakuja, na saa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu nao watatoka.” Kristo alisema kuwa uwezo wenye kufufua wafu ulikuwa kati yao, nao wangeutazama jinsi ulivyo. Uwezo ule ule huwapa watu uzima na kuwaweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti. Warumi 8:2. Kwa njia ya imani mtu hulindwa kutoka dhambini. Yeyote afunguaye moyo wake kwa Kristo, huwa mshiriki wa uwezo huo ambao utamfufua toka kaburini.

Mnazareti mnyenyekevu aliinuka juu ya wanadamu, akaitupilia mbali sura ya dhambi na aibu, akasimama ameonekana kuwa Mwana wa Mungu, ambaye ni umoja na Mungu. Mwumbaji wa ulimwengu. Wasikilizaji wake walipagawa kwa utamu wa maneno. Hakuna mtu hata mmoja aliyesema maneno kama Yeye au kuonekana kifahari kama Yeye. Matamshi yake yalikuwa dhahiri na wazi kabisa. “Baba hamhukumu mtu yeyote, lakini amekabidhi hukumu yote kwa mwana . . . Baba . . . amempa Mwana mamlaka ya kuhukumu, kwa sababu Yeye ni Mwana wa Adamu.”

Makuhani na wakuu wa watu walijifanya ndio waamuzi wa kazi ya Kristo, lakini Kristo alijitangaza mwenyewe kuwa ndiye mwamuzi wao na wa nchi yote. Kutoka kwa Mungu mafanikio yote ya watu huwajia kwa njia ya Kristo. Kwa kadiri dhambi inapokuwapo, huwapo Mwokozi pia. Aliyetoa mwanga kuwamu- [113]
likia watu, ndiye anayewatafuta watu watoke dhambini waje katika utakatifu, na ndiye atayekuwa Hakimu wa wote. Yule ambaye amewasihi watu kwa vizazi na vizazi watoke katika utumwa wa dhambi, ndiye atakayewahukumu, watu wote.

Kwa kuwa Yeye ameyaonja. mavurugiko na majaribu ya wanadamu, na kufahamu dhiki ya wanadamu, na kwa kuwa aliyashinda majaribu ya Shetani, atawatendea watu mambo ya haki. Maana amewanunua kwa damu yake mwenyewe. Kwa ajili hii Mwana wa Adamu amewekwa awe Mhukumu wao.

Lakini "Mungu hakumtuma Mwanawe ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe kwa njia yake Yeye." Yohana 3:17. Katika Sanhedrin, Yesu alisema: "Yeye alisikiaye neno langu, na kumwamini aliyenituma, anao uzima wa milele, wala haji hukumuni, bali amepita toka mauti hata uzima wa milele."

## Ufufuo wa Uzima

"Saa inakuja ambayo wote waliomo makaburini watakapoisikia sauti yake, nao watatoka. Waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, nao waliofanya maovu kwa ufufuo wa hukumu."

Nuru ambayo ingewaangazia Waisraeli, ndiyo itaangazia makaburi. Lakini watu hawa walikuwa vipofu tu. Yesu alikuwa anazivunja kanuni za marabi wala hawakuamini.

Wakati, na mahali na hali ya kujisikia kwa watu, viliyafanya maneno ya Yesu katika Sanhedrin yawe yenye kupendeza. Wakuu wa dini wa Israeli walikuwa wakimtafuta yule aliyejitangaza kuwa msimamizi wa Israeli. Bwana wa sabato alikuwa anapanga kujibu malaumu ya kuvunja sabato. Washitaki wake walimwangalia kwa ghadhabu, lakini maneno yake yalikuwa hayajibiwi. Alikataa kuingiliwa katika kazi yake na makuhani na marabi. Hakukubali kuwa alikosa.

Badala yaYesu kuomba msamaha, aliwakemea kwa kutojua maandiko. Aliwalaumu kwa kulikataa Neno la Mungu; pamoja

na kumkataa Yeye pia. Alisema: "Mwayachunguza maandiko kwa sababu mnadhani kuwa mna uzima wa milele ndani yake; hayo ndiyo yanishuhudiayo."

Agano la Kale huangaza utukufu wa Mwana wa Mungu. Mpango mzima wa Yuda ulikuwa wa unabii wa Injili. Tangu wazee wote na mpango wa utoaji wa mali ilikuwa nuru ya mbinguni ikiangaza
[114] miguu ya watu kumwelekea Mwokozi. Katika matoleo yote ya sadaka kifo cha Kristo kilikuwa kinaonyeshwa katika uvumba uliokuwa ukitolewa haki ya Kristo ilionyeshwa. Katika siri ya patakatifu na patakatifu mno, utukufu wake ulikuwako.

### Mahakama yashindwa kumtisha Yesu

Wayahudi walidhani kuwa, hali yao ya kuwa na dini ya nje tu wanao uzima wa milele. Lakini kwa kuwa wamemkataa Kristo katika neno lake, wamemkataa Yeye hasa. Alisema: "Hamji kwangu ili mpate uzima."

Viongozi wa Wayahudi walijifunza unabii, si kwa kutaka kufahamu, ila kwa kutafuta mambo yenye kuwasaidia katika mipango yao. Kristo alipokuja kwa njia tofauti na matazamio yao hawakumpokea, ila walijaribu kuona kuwa ni mwongo. Kadiri Mwokozi alivyowasuta katika kawaida zao, ndivyo walivyozidi kuikataa nuru.

Yesu alisema: "Siupokei utukufu wa wanadamu." Yeye hakutafuta ukubali wa Sanhedrin. Yeye alivikwa na utukufu wa mbinguni. Kama angeliutamani utukufu huo, malaika wangalimpa. Lakini kwa ajili ya faida yao alitaka Wayahudi wafahamu tabia yake.

Alisema: "Nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamkunipokea." Wengine wakija wakitaja kuwa na tabia yangu, ila wakitafuta mambo yao, hao huwapokea. Kwa nini? Kwa sababu watafutao mambo yao hukubaliana na ninyi. Wayahudi huwakubali walimu wa uongo, kwa sababu huwasifu. Kwa kuwa mafundisho ya Kristo ni ya kiroho, hutaka kajinyima nafsi, kwa hiyo hayakubaliwi. Kwao sauti yake ni sauti ngeni.

Je, siku hizi hawako walimu wa dini wanaolikataa, neno la Mungu, na kufuata mapokeo yao?

"Kama mngalimwamini Musa mnganiamini na mimi, maana aliandika mambo yanayonihusu. Lakini kwa kuwa hamwamini

maneno yake, mtayaaminije maneno yangu?" Kama wangeliyaamini maneno ya Mungu yaliyosemwa kwa njia ya kiongozi wao mkuu, wangefahamu mafundisho ya Kristo. Makuhani na marabi waliona kuwa upinzani wao kwa Kristo hauna maana, walakini chuki yao ya uuaji ilizidi tu kuwachochea. Waliogopa walipoona kuwa kuna uwezo mkuu katika kazi yake, lakini walizidi kujifungia gizani.

Walikuwa wameshindwa kuupindua uwezo wa Yesu, wala kuzuia watu wasimfuate. Wengi walikuwa wameongolewa kwa maneno yake. Wakuu hao walishindwa kabisa kumhukumu Kristo, walakini walikusudia tu kumwulia mbali. Walituma watu ili wawahadhari watu juu ya Yesu, kuwa mtu mlaghai tu, siye mtu [115]
wa kweli. Walituma wapelelezi kuona anachofanya na mambo anayosema. Mwokozi wa thamani, alikuwa sasa katika uvuli wa mauti ya msalaba.

[116] # 22 — Kifungo na Kifo cha Yohana

Yohana Mbatizaji alikuwa mtu wa kwanza kutangaza habari za ufalme wa Kristo, pia alikuwa mtu wa kwanza kupata mateso. Kutoka mahali peupe huko jangwani aliletwa gerezani, katika ngome ya Herode, kama mfungwa. Herode Antipa mwenyewe alisikia mahubiri ya Yohana yakamtetemesha sana. Herode alimwogopa Yohana, akifahamu kuwa ni mtu mtakatifu, mtu wa haki. Yohana alikemea kule kuchukuliana na Herodias, mke wa ndugu yake, ambaye ni shemeji yake. Kwa muda kitambo Herode alitaka kuvunja mawazo hayo ya uasherati, lakini Herodias alimng'angania kwa nguvu, hata akamshawishi Herode amtupe Yohana gerezani.

Hali ya gereza ilikuwa mbaya sana, nayo ilimtaabisha sana Yohana. Muda ulipopita mwingi hali, ya mashaka ikamjia. Wanafunzi wake walimletea habari za kazi ya Yesu, na jinsi makundi ya watu yanavyomfuata. Lakini kwa nini mwalimu huyu, akiwa ndiye Masihi, anisaidie katika kufungwa huku? Mashaka ambayo yasiligalimjia, yakaanza, kumjia. Shetani alifurahi kwa maneno ya wanafunzi hao ambayo yamemjeruhi roho ya mjumbe wa Mungu. Mara ngapi rafiki mkuu wa mtu hugeuka kuwa adui yake?

Yohana Mbatizaji alimtazamia Yesu kukitwaa kiti cha utawala cha Daudi. Wakati ulipopita, wala Yesu hakuonyesha dalili yoyote ya kuwa mfalme wa dunia hii, Yohana aliingiwa na wasiwasi. Alikuwa ametazamia cheo kikubwa cha kibinadamu, na uwezo. Masihi angesafisha sakafu kabisa, na kukusanya ngano ghalani., na kuyachoma makapi katika moto usiozimika. Soma Isaya 40; Mathayo 3. Sawa kama Eliya, alitazamia kuja kwa Masihi kutokee kama Mungu atajibu kwa moto.

[117] Yohana Mbatizaji alisimama bila hofu akikemea maovu mahali pote. Alithubutu hata kumkabili mfalme Herode akimkemea kwa dhambi zake. Na alingojea Simba wa Yuda aingilie kati na kumwokoa. Lakini Yesu alionekana akitulia tu, akifanya kazi ya kuponya watu na kufundisha. Alikuwa akila na watu huku mzigo wa Warumi ulizidi kuwakandamiza watu, ambavyo mfalme Herode na wenzake

waliendelea kufanya wapendavyo, na kilio cha maskini na wenye dhiki kikipanda mbinguni.

### Uchungu mkali

Mambo hayo yote yalionekana kuwa maajabu. Manong'onezo ya Shetani yaliusumbua moyo wa Yohana na kivuli cha hofu kilimwingilia. Je, inawezekana kuwa Mwokozi aliyengojewa kwa muda mrefu bado kufika? Yohana alikata tamaa vibaya kuhusu kazi yake. Alitumaini kuwa ujumbe kutoka kwa Mungu utawasisimua watu kama ule wa siku za Yosia na Ezra. (2 Mambo ya Nyakati 34; Nehemia 8), kwamba watu watatubu. Je, maisha yake ya kujitolea yamekuwa kazi bure? Je, kazi kwa wanafunzi wake imekuwa ya bure, bila matunda? Je, hakuwa mwa-minifu kazini, ndiyo sababu amekomeshwa? Je, kama Mwokozi aliyeahidiwa angekuwa amekuja, na Yohana amekuwa mwaminifu Yesu asingaliwatoa katika utumwa wa Warumi na Yohana kufunguliwa?

Walakini Yohana Mbatizaji hakuacha imani yake kwa Kristo ianguke. Sauti aliyosikia kutoka mbinguni, kushuka kwa mfano wa hua, maisha manyofu ya Kristo, Roho Mtakatifu aliyemjilia Yohana alipomjia Mwokozi, ushuhuda wa maandiko matakatifu, yote hushuhudia kuwa Yesu ndiye Mwokozi aliyeahidiwa.

Yohana aliazimu kutuma ujumbe kwa Yesu. Alituma wanafunzi wake wawili, akiamini kuwa kukutana na Yesu kutawaimarisha. Na yeye alitamani kusikia maneno kutoka kwa Yesu. Wale wanafunzi walimjia Yesu wakisema: "Je wewe ndiye yule ajae, au tumtazame mwingine?' Swali hilo lilikuwa la kuonyesha uchungu na kukata tamaa. Kama Yohana ambaye ndiye mtangulizi wa Yesu, alishindwa kutambua kazi ya Yesu, je, ingetazamiwa nini kwa watu wapendao mambo ya ubinafsi?

Mwokozi hakulijibu swali hilo la wanafunzi mara moja. Walipokuwa wakisimama katika hali ya ukimya, wagonjwa na wenye maradhi walikuwa wanamjia Yesu ili awaponye. Vipofu, wenye maradhi mbalimbali walikuwa wakisongamana kumjia Yesu. Sauti ya Mponyaji mkuu ilipenya mpaka ndani ya kiziwi. Neno lake, mguso wa mkono wake, ulifungua macho ya kipofu. Yesu alikemea homa na maradhi yote. Sauti yake ilifika mpaka kwa [118]
mtu anayekufa, na wote wakachangamka, wakasimama. Alipokuwa

akiwaponya wenye maradhi, watu maskini na wakulima ambao walikuwa wamepigwa marufuku na marabi, kama watu wasiotakiwa, walikuwa wakisongamana kuja kwake, naye akawazungumzia maneno ya uzima wa milele.

### Yesu atoa vithibitisho

Siku iliendelea kumalizika, na wanafunzi wa Yohana waliona na kusikia mambo yote. Halafu Yesu aliwataka wanafunzi hao wa Yohana, akawaambia waende wamweleza Yohana yote waliyoona na kusikia. Akaongeza kusema: "Heri mtu yule asiyechukizwa nami." Uthibitisho wa Mungu wake ulikuwa umeonekana wazi, utukufu wake ulionekana dhahiri hata kwetu sisi watu wa hali ya chini.

Wanafunzi walichukua ujumbe huo, ikatosha. Yohana akakumbuka unabii uliomhusu Masihi. "Bwana amenitia mafuta, niwahubiri wanyenyekevu habari njema. Amenituma niwagange waliovunjika moyo, kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao." Isaya 6:1. Kazi ya Kristo ilijidhihirisha kuwa yeye ni Masihi. Yesu alifanya kazi yake, si kama mwenye kupindua wafalme, isipokuwa kusema na watu kuhusu uzima wa milele, kwa njia ya fadhili na kujinyima.

Kanuni ya maisha ya Yohana Mbatizaji ilikuwa ndiyo kanuni ya ufalme wa Masihi. Lakini kile kilichomthibitishia Kristo Uungu wake sicho ambacho kingekuwa thibitisho kwa Viongozi wa Israeli. Yohana aliona kuwa matokeo ya kazi ya Mwokozi yalikuwa chuki na malaumu. Yohana kama mtangulizi wa Kristo alikuwa akinywea kikombe kichungu ambacho Kristo mwenyewe atakinywea baadaye.

Maonyo ya Mwokozi ya upole hayakuwa ya bure kwa Yohana. Ufahamu kamili kwamba ndiye Masihi ulimfanya Yohana kujitoa kamili kwa Mungu kufa na kupona, na kufanya kazi yake kamili.

Moyo wa Mwokozi ulinihurumia mtumishi mwaminifu akiwamo gerezani kwa Herode. Hakutaka watu wadhani kuwa, Mungu amemsahau, au kwamba amekata tamaa na kuacha imani yake, wakati wa majaribu. Yesu alisema, "Mlikwenda jangwani kuona nini? Majani yakitikiswa na upepo?"

Marabi wakiwa kama majani marefu kando ya mto wa Yordani, walisimama wakipeperushwa huku na huko katika mawazo
[119] ya watu wenye kutangatanga. Lakini kwa kuwaogopa watu waliogopa kuikanusha kazi ya Kristo, waziwazi. Lakini mjumbe wa

Mungu hakuwa na roho ya woga jinsi hiyo, Yohana alinena ukweli wa namna moja kwa Mafarisayo, Masadukayo, mfalme Herode, wakuu wote, watoza ushuru na wakulima. Hakuwa kama majani yaliyokuwa yakitikiswa na upepo. Alikuwa mwaminifu kwa Mungu hata ndani ya gereza. Alikuwa na kanuni thabiti kama mwamba.

## Hakuna mtu mkuu zaidi

Yesu aliongeza kusema: "Mlikwenda jangwani kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? Tazameni wenye kupendeza, wavaao mavazi mazuri wamo katika nyumba za wafalme." Watu matajiri wenye kujipamba, waishio kianasa, katika fahari, hawamo katika kundi la watenda kazi wa Mungu. Makuhani na wakuu wa Wayahudi walijipamba kwa fahari kubwa; kwa mavazi ya fahari. Walitafuta kuheshimiwa na watu, kuliko kutafuta upendeleo wa Mungu. Utii wao haukumwelekea Mungu, bali ulielekea kwa wafalme wa dunia hii.

Yesu aliwauliza: "Lakini mlikwenda kuona nini" Nabii . . . Huyu ndiye aliyeandikiwa.

"Angalieni namtuma mtumishi wangu mbele ya uso wako. Atakayetengeneza njia mbele yako.

Nawaambia, katika watu waliozaliwa na wanawake, hakuna mtu mkuu kuliko Yohana Mbatizaji." Yesu aliendelea kusema, "Walakini aliye mdogo katika ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko yeye." Tangazo lililotolewa kwa Zakaria kabla ya kuzaliwa kwa Yohana, malaika alisema: "Atakuwa mkuu machoni pa Bwana." Luka 1:15. Machoni pa mbingu, ni nini kinachofanya mtu kuwa mkuu? Sicho kile kinachohesabiwa na ulimwengu. Ukuu mbele ya macho ya Mungu ni kule kuwa mnyofu. Unyofu ndio Mungu huhesabu kuwa ukuu. Mungu huheshimu upendo na usafi wa maisha. Yohana alikuwa mkuu machoni pa Mungu, alipokataa kujitukuza yeye mwenyewe, ila heshima yote akaielekeza kwa Yesu, ambaye ni yeye aliyeahidiwa. Kutokuwa na ubinafsi kwake na kufurahia na kutukuza kazi ya Yesu, kulimfanya aonekane kuwa ni kielelezo halisi cha ukuu umpasao mtu.

## Zaidi ya Nabii

Yohana alikuwa "Zaidi ya nabii". Wakati manabii walikuwa wakiona mbali kuhusu kuja kwa Kristo, lakini kwa Yohana alipewa kumwona na kumkabidhi kwa Israel; kama mtu aliyetumwa na
[120] Mungu. Yohana alikuwa nuru ndogo ambaye atafuatwa na nuru kuu. Hakuna nuru kuu zaidi itakayomulikia wanadamu kuliko nuru ya Yesu.

Mbali na furaha Yohana aliyokuwa nayo katika kazi yake, lakini maisha yake yamekuwa yenye masikitiko kabisa. Alikuwa mtu wa huzuni, akikaa katika hali ya upweke. wala hakuweza kuishi na kuona matokeo ya kazi yake. Hakuwa na nafasi ya kuishi pamoja na Kristo, na kusikia maneno yake, ambayo ni nuru halisi, yenye kung'aa katika unabii.

Herode aliamini kuwa Yohana ni nabii wa Mungu, naye alikusudia kumfungulia. Lakini alimwogopa Herodias. Alijua kuwa asipochukua hatua thabiti hawezi kumwua Yohana, ambaye anamchukia, kwa hiyo alitaka kukamilisha kusudi lake kwa njia ya hila. Siku ya kuzaliwa kwa mfalme ilifanywa sikukuu, na ulevi wa kila namna. Herode angesifiwa na kutukuzwa kama apendavyo.

Sikukuu ilipofika, mfalme na wakuu wake walifanya anasa na kulewa. Herodias akamtuma bintiye katika jumba la sikukuu ili akawatumbuize wageni kwa nyimbo na michezo. Binti wa Herodias ambaye ni Salome, alikuwa katika kilele cha ujana wake. Akacheza kwa madaha na maringo sana, akawapendeza na kuwafurahisha wakuu wote. Wakamsifu Herode na kumtukuza kwa ajili yake.

Mfalme alikuwa amelewa kwa mvinyo. Akapumbaa. Hakuweza kufikri kitu zaidi, ila karamu, jumba la karamu, mvinyo, taa na msichana akicheza mbele yao. Wakati ule bila kufikiri sawa, alitaka kutenda kitu kitakachomletea fahari na kutukuka zaidi mbele ya wakuu wake, walioko kwenye karamu hiyo. Alitoa ahadi kwa binti huyo wa Herodias kwamba aombe kitu chochote atapewa, hata nusu ya ufalme wake.

Salome akakimbia kwa mama yake, na kumwuliza kuwa aombe kitu gani? Jawabu lilikuwa tayari, kichwa cha Yohana Mbatizaji. Salome alisita kuomba kitu hicho, lakini sisitizo la Herodias lilifaulu. Binti alirudi na haja ya kutisha. "Nataka unipe kichwa cha Yohana Mbatizaji katika sahani, sasa hivi."

Herode alishangaa na kuchanganyikiwa. Aliogopa na kushangaa kukata kichwa cha Yohana Walakini hakupenda kuonekana kuwa mwongo na, mfedhuli. Ameapa mbele ya wageni wake, na kama mtu mmoja katika wageni angelipinga jambo hilo, Herode angefurahi kumwacha hai nabii.

Aliwapa nafasi kuzungumza kuhusu Yohana, ambaye ni mfungwa. Walifahamu kwamba Yohana ni mjumbe wa Mungu. Lakini waliogopa kwa ajili ya matakwa ya msichana, na kwa kulewa [121] kwingi hawakuweza kutoa shauri lolote. Hakuna mtu aliyesema neno la kumponya mjumbe wa mbinguni. Kwa watu hawa wenye madaraka makubwa wajibu mkubwa ulikuwa juu yao, walakini walijitolea kulewa tu. Vichwa vyao vilikuwa na kizunguzungu kwa ajili ya kelele za michezo. Kwa ajili ya ukimya wao, walikubali nabii wa Mungu auawe ili kutimiza matakwa ya mwanamke mwasherati.

Herode alisita kuamuru kumkata kichwa nabii. Baadaye kichwa cha Yohana kililetwa katika sahani. Sauti hiyo ya Yohana haitasikika tena ikiwaita watu watubu. Karamu ya siku moja tu iligharimu kichwa cha mtu mkuu sana, ambaye ni nabii.

Mara nyingi watu watawa wasiokuwa na kosa wameangamizwa na walevi ambao wangalikuwa wahifadhi wao, kwa kutetea haki Yeye awekaye kileo kinywani mwake ajitia katika hatia ya kudhulumu chochote katika uwezo wake. Wale walio waamuzi katika mambo ya maisha ya wengine, watakuwa hatia wanapojitolea kuwa walevi. Wanahitaji kuwa watu wenye mawazo kamili, afya kamili, na unyofu kamili, ili wawe na hali kamili ya kutenda mambo ya haki.

Herodias alifurahia mauaji hayo ya kikatili, hali akizidi kujidai kuwa Herode atatulia, bila kuwa na wasiwasi. Lakiri matokeo yake hayatakuwa na utulivu. Jina lake lilikuwa shutuma kuu, wakati Herode alipokuwa akihangaishwa na dhamiri yake. Kila mara alikuwa akitafuta utulivu wa dhamiri. Herode hakuweza kuwa na utulivu, alipokumbuka jinsi Yohana alivyokuwa mtu mtawa, mwenye kujikana nafsi, maonyo yake ya kweli na mashauri yake safi. Alionekana kana kwamba anachangamka, lakini kwa ndani alikuwa mwenye taabu.. Alikuwa na hakika kuwa Mungu aliona mambo ya karamu yake, akaona maazimio ya Herodias, na kukiona kichwa cha Yohana, ambaye alikuwa mwonyaji wake.

Herode alipoisikia kazi ya Kristo, alidhani kuwa Mungu amemfufua Yohana kutoka ufuni. Alihofu na kufikiri kuwa Yohana atalipa kisasi kwa kumwadhibu yeye na nyumba yake. Herode alikuwa akivuna mavuno ya dhambi zake; yaani kuwa na wasiwasi moyoni, kupofuka macho, na kutetemeka daima moyoni mwake. Asubuhi itasema: "Heri jioni, na jioni utasema, Heri asubuhi, kwa ajli ya hofu ya moyo wako." Torati 28:65-67. Hakuna masumbuko makuu kuliko kuwa na wasiwasi moyoni, ambayo hakuna kupumzika mchana wala usiku.

[122] **Sababu ambayo Kristo hakumwokoa Yohana**

Watu wengi huwaza kuwa kwa nini Yohana Mbatizaji aliachwa asumbuke na kufia gerezani. Lakini jambo hili la giza haliwezi kutikisa imani yetu kwa Mungu, tunapokumbuka kuwa Yohana alikuwa mtumishi wa Mungu, na mshiriki wa mateso ya Kristo. Wote wanaomfuata Kristo watavaa taji ya kujikana nafsi. Shetani atafanya vita na kanuni hii ya kujikana nafsi popote inapoonekana.

Shetani amekuwa akishughulika kumfanya Yohana Mbatizaji awe mtu wa kujipenda nafsi, akashindwa. Katika majaribu ya jangwani Shetani alishindwa. Na sasa alikusudia kumhuzunisha Kristo kwa njia ya kumshambulia Yohana kiajabu. Mtu yule aliyeshindwa kumvuta dhambini, alimletea mateso.

Yesu hakuingilia kati na kumwokoa mtumishi wake. Alijua kuwa Yohana atavumilia jaribu hilo. Mwokozi angemfariji katika gereza ili asiwe na wasiwasi. Lakini hakutaka kuhatarisha kazi yake mwenyewe. Yohana ilimpasa anywee kikombe cha namna hiyo, kwa ajili ya watu maelfu watakaofuatana, na kunywea kikombe cha mauti. Sisi kama wafuasi wa Kristo, tulalamike tunapotiwa gerezani, na kukabili mauti? Inapoonekana kuwa kana kwamba tumeachwa na Mungu mawazo Yohana aliyokuwa nayo gerezani, hatuwezi kuyakumbuka,?

Yohana hakuachwa na Mungu. Malaika wa mbinguni walikuwa wenzake, waliomufunulia unabii kumhusu Kristo na maandiko matakatifu. Kwa Yohana, na kwa wengine watakaofuata ahadi husema: "Tazama mimi nipo pamoja nanyi mpaka mwisho, wa dunia.' Mathayo 28:20.

Mungu hawaongozi watu wake kinyume cha matakwa yao. Kama wangaliona mwanzo mpaka mwisho, kwamba wanatimiza jambo liwapasalo watenda kazi pamoja naye. Si Enoka aliyehamishiwa mbinguni, si Eliya aliyepazwa mbinguni bila kufa, kwamba walimzidi Yohana, aliyefia gerezani. "Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, siyo kuamini tu, bali hata na kuteseka pia." Wafilipi 1:29. Wote wapewao vipawa vya mbinguni, kuteswa na Kristo ni thamani kubwa.

## [123] 23 — Jinsi Danieli Alivyomtambua Yesu kuwa ni Kristo

Kuja kwa Masihi kulitangazwa mara ya kwanza katika Yuda. Juu ya milima ya Bethlehemu malaika walitangaza kuzaliwa kwa Yesu. Katika Yerusalemu mamajusi walikuja kumtafuta.

Kama waongozi wa Israeli wangelimpokea Kristo, angaliwatuma kama wajumbe wake kuitangaza Injili duniani pote. Lakini hawakufahamu majira ya kujiliwa kwao. Wivu na kutoamini kwa viongozi wa Israeli vilitokeza chuki, na roho za watu ziligeukia mbali kutoka kwa Yesu. Baraza la Sanhedrin liliidhinisha kuuawa kwake. Kwa hiyo Yesu aliondoka kutoka Yerusalemu; kwa watu waliofundishwa sheria ya Mungu, akaligeukia taifa jingine kutangaza ujumbe wake.

Kwa kila kizazi, historia ya Kristo kujitenga na Yuda zilitangazwa. Wakati watengenezaji wa dini walipohubiri neno la Mungu, hawakuwa na wazo la kujitenga na kanisa, lakini viongozi wa kanisa hawakukubaliana na nuru hiyo mpya, na hao waliokuwa na nuru hiyo, walipaswa kutafuta watu wanaokubaliana na ukweli huo. Siku zetu hizi ni watu wachache tu baina ya wafuasi watengenezaji wa kanisa, yaani Reformers, husikia sauti ya Mungu, na kuwa tayari kukubaliana na neno linalohubiriwa. Kila mara wale wanaofuata hatua za watengenezaji hulazimishwa kutengana na makanisa yao, ili waweze kuhubiri neno la Mungu. Wengi hutoka na kutengana na makanisa ya baba zao, ili wapate kumtii Mungu.

Watu wa Galilaya walikuwa waelekevu sana kwa kazi ya Mwokozi. Waliokuwa na uhuru kutokana na wazazi wao, walilipokea neno la Mungu kamili. Huko Galilaya kulikuwa na mchanganyiko wa watu zaidi kuliko ilivyokuwa Uyahudi.

Yesu alipozunguka zunguka Galilaya, akifundisha na kuponya watu wengi walimfuata hata kutoka Uyahudi pia. Watu walisisimka
[124] kwa nguvu sana, hata ikabidi kujihadhari wasije wakaamsha wasiwasi kwa Warumi, wakidhani kuwa kutatokea mapinduzi. Wenye njaa na kiu ya haki, walilishwa neema ya Mwokozi mwenye huruma.

## Nabii Danieli Alitabiri Kazi ya Kristo

Mzigo wa mahubiri ya Kristo ulikuwa: "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni mkaiamini Injili." Marko 1:1 5. Ujumbe wa Injili kama ulivyosemwa na Mwokozi, ulijengwa juu ya unabii. "Wakati" ambao alisema kuwa umetimia, ulikuwa muda ule aliofunuliwa Danieli. "Majuma sabini yamekusudiwa juu ya watu wako na juu ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha uasi, na kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho wa maovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri njozi na unabii, na kumtia mafuta Mtakatifu." Danieli 9:24. Kwa unabii siku inasimama badala ya mwaka. Ezekiel 4:6. Majuma sabini au siku 490 ni sawa na miaka 490.

Mwanzo wa muda huu umeelezwa: "Ujue basi na kufahamu, kuwa tangu kutolewa amri ya kuujenga Yerusalemu hata Masihi Mkuu, utakuwa muda wa majuma saba na muda wa majuma sitini na mawili. Majuma sitini na tisa au miaka 483. Danieli 9:25.

Amri ya kuurudisha na kuujenga Yerusalemu, kama ilivyotimizwa kwa amri ya Artashashta Longimanus (Tazama Ezra 6:14; 7:1-9) iliyotolewa mwaka B.C. 457. Tangu wakati huo miaka 483 iliendelea mpaka A.D. 27, kama unabii usemavyo. Muda huu utafika mpaka kwa Masihi, ambaye ni mtiwa mafuta: Mwaka A.D. 27 Yesu alipobatizwa alitiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, na baadaye akaanza kazi yake. Kisha ujumbe ulitangazwa kwamba: "Wakati umetimia."

Kisha malaika alisema: "Kwa juma moja atathibitisha agano kwa wengi (miaka saba). Kwa muda wa miaka saba baada ya Mwokozi kuingia kazini, Injili itatangazwa hasa kwa Wayahudi. Kristo mwenyewe atatangaza injili miaka mitatu na nusu, na mitume miaka iliyobaki.

"Kati ya juma atakomesha kafara ya dhabihu." Danieli 9:27. Katika mwaka A.D. 31 Kristo ambaye ni kafara halisi alitolewa huko Kalwari. Kisha pazia la hekalu lilipasuka sehemu mbili kuonyesha kuwa umuhimu wa huduma na kafara za kawaida umeondoka. Wakati umefika wa kukomesha kafara na dhabihu.

Juma moja, yaani siku au miaka saba ilimalizika katika mwaka A.D. 34. Ndipo kwa kumpiga Stefano kwa mawe, Wayahudi walitia muhuri kukataa kwao injili. Mitume waliotawanyika kwa ajili ya [125]

mateso. “Walienda huko na huko wakilihubiri lile neno.” Matendo 8:4. Baadaye Sauli mtesaji aliongoka, akawa Paulo, mtume kwa watu wa mataifa.

Muda wa kuja kwa Kristo, kufa kwake, na kuhubiri injili kwa mataifa vilionyeshwa dhahiri. Iliwapasa Wayahudi waufahamu unabii huu na jinsi ulivyotimia katika kazi ya Yesu. Kufuatana na unabii wa Danieli, Yesu alisema: “Asomaye afahamu.” Mathayo 24:15. Alisema hayo kuhusu wakati wao. Baada ya kufufuka kwake, alieleza kwa wanafunzi wake: “Unabii wote unaomhusu yeye.” Luka 24:27. Mwokozi alikuwa amesema kwa njia ya manabii, akishuhudia kabla na mateso yake na utukufu utakaofunuliwa baadaye. 1 Petro 1:11. Alikuwa Gabrieli, malaika mkuu, aliyekuja kumfunulia Danieli. Malaika huyu huyu ndiye alitumwa na Kristo kwenda kumfunulia Yohana mambo ya Ufunuo. Uheri umesemwa kwa wale wenye kusoma maneno ya unabii na kuyashika mambo yaliyoandikwa humo, Ufunuo 1:3. Mungu atawabariki wenye kutii, wakisoma unabii kwa unyenyekevu kwa roho ya maombi.

Kwa ujumbe kwa kuzaliwa kwa Kristo ulivyotangazwa, ambao ulikuwa ni ujumbe wa neema, ndivyo na ujumbe wa kurudi kwake kwa utukufu utakavyotangazwa. Ujumbe huu wa pili, sawa na ule wa kwanza, umejengwa juu ya unabii. Mwokozi mwenyewe ametoa unabii kuhusu kurudi kwake kwa kuonyesha dalili nyingi. Amesema: “Jiangalieni mioyo yenu isije ikalemewa na ulevi na ulafi, na masumbuko ya dunia hii, hata siku ile iwaghafilishe kama mtego unasavyo.” “Kesheni basi, na kuomba daima, ili mhesabiwe kuwa mnastahili, mambo haya yatakapotokea, mpate kusimama mbele ya Mwana wa Adamu ajapo.” Luka 21:34, 36.

Wayahudi waliutafsiri unabii kimakosa, na wala hawakujua wakati wa kujiliwa kwao. Miaka ya kazi ya Kristo na ya mitume Wayahudi walishughulika kupanga namna ya kuwaangamiza tu wajumbe wa Mungu. Anasa za dunia na kutafuta makuu ya dunia hii kumewapumbaza watu wengi, hata hawaoni mambo yanayotimiza unabii yatokeayo kwa haraka sana, na dalili za kuja kwake zinazoharakisha mno, zikitangaza kuja kwa ufalme wa Mungu. Ingawa hatujui siku kamili ya kuja kwa Bwana, tunaweza kujua jinsi ilivyokaribia sana. “Kwa hiyo tusilale usingizi kama wengine; ila tukeshe na kuwa na kiasi.” 1 Wathesalonike 5:6.

## 24 — “Je, Huyu Siye Mwana wa Seremala?” [126]

Kuvuka ng’ambo ya kazi ya furaha na siku za mafanikio za Kristo huko Galilaya, kulikuwa na wasiwasi kama kivuli katikati ya mwanga, yaani ni watu wa Nazareti walimkataa. Walisema: “Je, huyu siye mwana wa seremala?” Mathayo 13:55.

Wakati wa ujana wake, Yesu alikuwa akishiriki kuabudu pamoja na ndugu zake katika sinagogi la Nazareti. Wakati alipoanza kazi yake, alikuwa haonekani hapo tena, lakini alipoonekana, matazamio yao yalikuwa tofauti. Hapo palikuwa na watu waliofahamiana tangu utoto wake. Mama yake, ndugu zake na dada zake wote wapo. Alipoingia katika sinagogi na kutafuta mahali pake kama kawaida, wote walimtazama ikiwa ni siku ya Sabato.

Katika ibada, mzee wa kanisa aliwasisitizia watu wadumu kuwa na tumaini la kumtazamia Masihi ajaye; ambaye ataleta utawala wa fahari, na kuondoa udhia wa kusumbuliwa na Warumi. Aliwakazia wasikihzaji wake wazidi kumtazamia Masihi, ambaye kuja kwake kunakaribia. Aliwaambia kuwa atakuja na mamlaka ili kuwakomboa Waisraeli.

Wakati Rabi alipokuja, alikuwa akitazamiwa kuhubiri na Mwisraeli fulani asome maandiko ya unabii. Kwenye Sabato hii Yesu alikuwa ndiye mhubiri. “Alisimama ili asome, naye alipewa chuo cha Nabii Isaya” Fungu alilosoma lilieleweka kuwa linamhusu Masihi:

“Roho ya Bwana ni juu yangu. Kwa sababu amenitia mafuta ili niwahubiri maskini Injili.

Amenituma niwaponye waliovunjika moyo; kuhubiri kufunguliwa kwa wafungwa; kuponya macho ya vipofu, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubalika.”

Akakifunga chuo akampa msimamizi akaketi chini, macho [127]
ya watu wote waliokuwa katika sinagogi yakamtazama.... Wakamshuhudia wote, wakiyasta-ajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwake.”

Yesu akiyaeleza maneno aliyosoma, akanena kuhusu Masihi kama msaidizi wa wenye dhiki, mponyaji wa wenye kuteswa, mponyaji wa vipofu, na mfunua nuru ya Kweli, Uwezo wa maneno yake uliowasisimua, ambavyo hawajaona. Mawimbi ya mvuto wake wa kimungu ulivunja kila kipingamizi. Kadiri walivyosisimuka kwa ajabu, waliitikia, amina, na kumsifu Bwana.

Wakati Yesu aliposema kwamba: "Andiko hili leo limetimizwa masikioni mwenu, mara moja kwa ghafla walikumbuka madai anayodai huyu aliyewahubiri. Wao wakiwa watoto wa Ibrahim wamesemwa kuwa wamo utumwani, kwamba ni wafungwa wanaohitaji kufunguliwa kutoka katika nguvu za Shetani, kwamba wamo gizani wakihitaji nuru ya kweli ya Mungu. Kiburi chao kiliguswa. Kazi ya Yesu kwao ilikuwa kinyume cha matazamio yao. Matendo yao lazima yachunguzwe kikamilifu. Walijikunyata kutoka katika macho yao dhahiri yanayochunguza.

Waliuliza wakisema: "Yeye huyo ni nani?" Huyu anayedai utukufu wa Masihi alikuwa mwana wa seremala. Walikuwa wanafahamiana na ndugu zake na dada zake. Walimwona akipanda na kushuka milimani akiwa katika shughuli za kazi ya useremala. Walijua maisha yake na kazi yake, wamemwona na kufahamu alivyokua toka utotoni mpaka ukubwani. Ijapokuwa maisha yake yalikuwa matakatifu, wasingalikubali kuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa. walifungulia mlango wa mashaka, na mioyo yao ikawa migumu zaidi, na Shetani akajitahidi kuwafunga wasiweze kuamini.

Dhamiri zao ziliwasadikisha kuwa, ni yeye Mwokozi aliyehubiri. Lakini Yesu aliwathibitishia kuwa ni yeye wa kurungua mioyo yao. "Hakuna nabii anayekubaliwa kwao na katika nchi yake mwenyewe. Lakini nawaambia yaliyo ya kweli kuwa, kulikuwa na vijana wengi katika Israeli katika siku za nabii Eliya, wakati mbingu ilipofungwa miaka mitatu na miezi sita, kulipokuwa na njaa kuu katika nchi, na Eliya hakutumwa kwa mmoja wao, ila huko Zerefath katika nchi ya Sidoni kwa mmoja aliyekuwa mjane. Na kulikuwa na wenye ukoma wengi katika Israeli, katika siku za nabii Elisha, wala hakuna aliyetakasika, ila Naamani mtu wa Shamu."

Watumishi waliotumwa na Mungu hawakuruhusiwa kufanya
[128] kazi kwa watu wagumu wasioamini. Katika siku za Eliya, Waisraeli walikuwa wamewakataa watumishi wa Bwana kabisa. Kwa hiyo Mungu aliwapatia watu wake maficho katika nchi za watu wa

mataifa, kwa mwanamke mshenzi ambaye hakuwa katika hesabu ya watu wa Mungu. Lakini moyo wa mwanamke huyu ulifunguka ili apokee nuru kuu kutoka kwa nabii wa Bwana, ambayo ililetwa na nabii wake.

Kwa njia ile ile, katika siku za Elisha, wenye ukoma katika Israeli walipitwa. Lakini Naaman, jemadari wa Shamu, mtu wa mataifa ya kishenzi, alipokea neema ya Mungu.

Hakuponywa ukoma peke yake, ila alipata baraka ya kufahamu Mungu wa kweli. Watu wa mataifa waliochagua njia njema kadiri ya ujuzi wao, huwa katika upendeleo wa Mungu zaidi ya watu wanaojidai kuwa ni watumishi wa Mungu, bali hawajali kufuata njia ya nuru, na katika maisha yao ya kila siku wakienda kinyume na maungamo yao.

### Yesu alifunua hali yao halisi mbele yao

Maneno ya Yesu yalipiga kwenye shina la hali yao ya kujifanya kuwa wenye haki machoni pao wenyewe. Kila neno liliwakata kama kisu kikali kikatavyo, maana hali yao ya kujipa haki wenyewe ilifunuliwa wazi mbele yao. Sasa wakadharau imani ambayo ilielezwa na Yesu dhahiri. Hawakuweza kukubali kuwa mtoto aliyezaliwa katika hali ya nchi ya kimaskini, angaliweza kuwa Masihi, ila ni mtu wa kawaida tu. Wakashupaza mioyo yao wasiamini. Wakapiga makelele kwa hasira, wakimkataa Mwokozi. Ghadhabu yao ikaamsha kiburi chao cha kitaifa, na maneno yake yakazama katika makelele. Ghadhabu yao ikawaka wakawa tayari kuua.

Mkutano ukavurugika, wakamkamata Yesu, wakamtoa nje ya Sinagogi na kumtupa nje ya mji wao. Wakitaka kumwangamiza, walimtupa katika genge ili aanguke na kuangamia humo. Makelele yalijaa hewani. Wengine walikuwa wakimtupia mawe, wakati alipotoweka kwao kwa ghafla. Wajumbe wa mbinguni walikuwa pamoja naye katika fujo hizo, wakamtoa humo salama salmini.

Ndivyo ilivyo katika vizazi vyote, majeshi ya Shetani yako tayari kuwashambulia wafuasi waaminifu wa Kristo; lakini majeshi ya mbinguni huwazunguka wote wanaompenda Mungu na kuwakinga na fujo hizo. Katika umilele ndipo tutaelewa kuwa wajumbe wa

mbinguni kutoka kwa Mungu walifuatana na sisi kila siku hatua kwa hatua.

[129] Yesu hakuacha kuwatia watu watubu katika sinagogi. Karibu na mwisho wa kazi yake huko Galilaya, alikwenda tena katika kijiji cha kwao alikozaliwa. Sifa za mahubiri yake na miujiza yake, zilikuwa zimeenea katika nchi yote. Katika Nazareti sasa hakuna mtu ambaye hakukubali kuwa anao uwezo unaozidi wa kibinadamu. Kati yao kulikuwa na watu waliowaponya wagonjwa wao.

Sasa mara tena walipoyasikia maneno yake, watu wa Nazareti waliingiwa na Roho wa Mungu. Lakini hawakukubali habari za mtu huyu aliyezaliwa na kukulia hapa kwetu, na mkuu kuliko sisi. Kumbukumbu ya madai yake kuwa ni Masihi, ilikuwa inawakasirisha. Amesema kuwa wao kama Waisraeli wanapitwa na watu wa mataifa. Kwamba Mungu anawaona watu wa mataifa afadhali kuliko wao. Ingawa waliuliza kuwa, "Mtu huyu amepata hekima hii wapi na uwezo huu wa kutenda mambo makuu?' Mathayo 13:54, walikuwa hawako tayari kumkubali kama Kristo Mwana wa Mungu. Kwa sababu, ya kutoamini kwao, Kristo hakufanya miujiza mingi huko kwao, na zaidi aliondoka kwao, wala hakurudi tena.

Kutokuamini kulikoshikiliwa na watu wa Nazareti, kuliendelea hata katika Sanhedrini, na taifa lote likawa katika hali hiyo. Hali hiyo iliongoza mpaka kwenye msalaba wa Kalwari, na mpaka kuharibiwa kwa mji wao, mpaka kutawanywa kwa taifa lao katika mataifa ya kishenzi.

Kristo alitamani kuwafunulia Waisraeli hazina za ukweli wenye thamani. Lakini wao waling'ang'ania mambo yao yasiyofaa, na maadhimisho yao ya dini bandia. Walitumia fedha zao kununua makapi na takataka tu, wakati mkate wa uzima ulikuwako. Kristo alitaja mara nyingi mambo ya unabii, na kusema; "Maneno haya leo yametimia masikioni mwenu." Kama wangelichunguza maandiko kwa makini, wakilinganisha mambo yao na Neno la Mungu, Yesu asingelikuwa na sababu ya kusema: "Angalieni nyumba yenu imeachwa ukiwa." Luka 13:35. Ajali iliyowaangukia na kuuteketeza mji wao, ingeliepukwa, kama wangejali maonyo.

Lakini mafundisho ya Kristo yaliyotaka watu Watubu hayakufuatwa. Kama wangefuata mafundisho yake, mambo yao lazima yangegeuka, na matumaini yangekuja wima. Lazima waende kinyume na wataalamu wao na walimu wao.

Viongozi wa Wayahudi walikuwa na kiburi na majivuno. Walipenda kuketi katika viti vya mbele ndani ya masinagogi. Walipenda kutajwatajwa kwa majina ya heshima na watu. Na [130]
kama hawakuheshimiwa hivyo walikuwa wachungu wenye wivu. Mawazo yao yakawa giza tupu kwa ajili ya ubinafsi, na chuki, wala hawakuweza kupatanisha hali yao na uwezo wa Kristo mwenye kuongoa na maisha yake matakatifu. Maisha ya Kristo ya kimaskini hayakuafikiana na madai yake ya kuwa Masihi. Mbona anajifanya namna hii? Kama ndivyo anavyodai kuwa Masihi, mbona hana jeshi lenye silaha? Anawezaje kuwokoa Wayahudi kwa njia hii?

Lakini Wayahudi hawakumkataa kwa ajili ya kutokuwa na mambo hayo, ila walimkataa kwa kuwa alikuwa kikwazo kwao kwa ajili ya maisha yake matakatifu, na maisha yao ni machafu. Utawa wake ulifunua hali yao ya uchafu, wakaonekana jinsi tabia zao zilivyo chafu. Nuru kama hiyo haikutakiwa kabisa. Wangeishi na hali hiyo ya uchafu, kuliko kuwa na hali Safi ya Yesu inayodhihirisha aibu yao. Wala hawakutaka hata kuwa mbele yake.

[131]

## 25 — Mwito Kando ya Bahari

Siku ilikuwa inakucha huko katika bahari ya Galilaya Wanafunzi walikuwa wamechoka kwa kazi ya usiku isiyokuwa na matokeo yoyote yaliyo mazuri, nao walikuwa wangali katika mashua zao katika ziwa la Galilaya. Yesu alikuwa amekuja kupunga hewa baharini asubuhi. Alitaka ajipumzishe kidogo kutokana na makutano yaliyokuwa yakimfuata siku kwa siku. Lakini watu walianza kukutanika, na mara akawa amezungukwa pande zote.

Kwa kuepuka msongamano wa watu, Yesu aliingia ndani ya mashua ya Petro, akamwambia aisogeze baharini kidogo. Mahali hapo aliweza kuonekana na kusikika vizuri na watu wote. Kutoka baharini hapo ndani ya mtumbwi, aliwafundisha watu waliokuwa wakisimama pwani. Aliyetukuzwa na mbingu alikuwa akiutangaza ufalme wake katika hewa, mbele ya watu. Ziwa, milima, uwanda mweupe, mwangaza wa jua, vyote hivyo vilikuwa vielelezo vya mafundisho yake, navyo viliwaingia watu kabisa. Hakuna fundisho lililopotea bure. Kila ujumbe ulipokelewa na watu kama neno la uzima wa milele.

Mambo kama haya ndiyo nabii alisema: "Nchi ya Zabloni na nchi ya Naftali, kuelekea bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa, Watu waliokaa gizani wameona mwanga mkuu na waliokaa katika uvuli wa mauti, Nuru kuu imewazukia."

Yesu akiangalia vizazi, aliwaona watu wake waaminifu wakiwa gerezani na katika majumba ya hukumu, na katika majaribu, na dhiki na mateso. Maneno yaliyonenwa kwa watu waliokusanyika pwani ya ziwa la Genesareti, yalikuwa yakizungumzwa pia kwa watu wote watakaokuwa katika giza, majaribu, dhiki na mateso.
[132] Maneno yaliyonenwa ndani ya mtumbwi yataendelea kusikika kwa watu, yakiwapa tumaini mpaka mwisho wa dunia.

Mahubiri yalipomalizika, Yesu alimwambia Petro asogeze mtumbwi majini zaidi, apate kuvua. Lakini Petro alikata tamaa. Usiku kucha alikuwa akivua, asipate chochote. Wakati wa saa za upweke, alikuwa akifikiri habari za Yohana Mbatizaji, akiteseka

gerezani, na habari za matazamio ya Yesu ya baadaye, habari za wafuasi wake, habari za kufaulu mgeuza Yuda, na habari za ukorofi wa makuhani na marabi. Alipoona kuwa hakupata kitu chochote katika nyavu zake, alikata tamaa kabisa. Akasema: "Bwana, tumesumbuka usiku wote, mpaka kumekucha; wala hatukupata kitu, walakini kwa ajili ya neno lako, nitatupa nyavu majini."

Baada ya kusumbuka usiku kucha bila kupata kitu, ilionekana kuwa ni kazi bure kutupa nyavu baharini. Lakini kwa kuwa walimpenda Bwana wao, walitii. Simoni na ndugu yake walitupa nyavu majini. Walipojaribu kuzivuta, zilikuwa zimejaa samaki tele, mpaka akamwomba Yakobo na Yohana kusaidia. Waliposhusha samaki mitumbwi yote ilikuwa imejaa kabisa karibu kuzama.

## Uovu ulifunuliwa

Mwujiza huu zaidi ya mingine, kwa Petro yalikuwa maonyesho dhahiri ya uwezo wa Mungu. Ndani, ya Yesu aliona uwezo wote wa kutawala mambo yote. Aibu ikampata kwa kutokuamini kwake. Shukrani kwa wema wa Yesu, zaidi ya yote, akijiona kuwa yu mwenye dhambi akiwa mbele ya Mungu aliye mtakatifu, akashangaa sana. Akaanguka miguuni mwa Mwokozi akilia: "Ondoka kwangu, maana mimi ni mwenye dhambi Bwana."

Hali hiyo hiyo ya kuwa mbele ya utakatifu, ndiyo iliyompata nabii Danieli, alipoanguka mbele ya malaika akawa kama mfu. Soma Danieli 10:8. Isaya naye alilia: "Ole wangu kwani nimepotea, kwa kuwa mimi ni mwenye midomo michafu . . . kwa kuwa macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi." Isaya 6:5. Hivyo imekuwa hali hiyo kwa wote waliopata kuuona utukufu wa Mungu.

Mwokozi alimjia Petro akasema: "Usiogope, tangu sasa utakuwa mvuvi wa watu." Baada ya Isaya kuona, utakatifu wa Mungu, na kujiona jinsi asivyofaa yeye mwenyewe, alikabidhiwa ujumbe wa mbinguni ili autangaze, Baada ya Petro kuona kuwa mwenye dhambi, asiyefaa kitu, alipata mwito wa kufanya kazi ya Kristo.

Wanafunzi walikuwa wameona miujiza mingi ya Kristo, na wa- [133]
likuwa wamesikiliza mafundisho mengi ya Kristo pia, lakini hakuna hata mtu mmoja aliyekuwa ameacha mambo yake, au shughuli zake za kwanza. Kifungo cha Yohana Mbatizaji kimekuwa cha kusikitisha sana. Kama hayo ndiyo matokeo ya kazi ya Yohana, walikuwa

na matumaini madogo sana kwa Bwana wao, na kwa vile waongozi wa dini walivyokuwa wakimpinga. Kwao ilikuwa nafuu kurudi katika kazi zao za uvuvi kwanza. Lakini sasa Yesu anawaita waache mambo yao ya zamani, na washrikiane naye kazini. Petro alikuwa amekubali. Walipofika pwani, Yesu aliwaambia wengine watatu: "Nifuateni, nami nitawafanya wavuvi wa watu.' Mara wakaacha vyote wakamfuata.

## Thawabu ya Kujitolea

Yesu kabla hajawauliza wanafunzi kuacha mashua zao za kuvulia, alikuwa amewaambia kuwa Mungu atawapatia mahitaji yao yote. Matumizi ya mashua ya Petro ilikuwa ikimpatia mapato mengi sana. Yeye aliye tajiri wa kila kitu alikuwa amesema: "toeni, nanyi mtapewa, kipimo cha kujaa, na kushindiliwa, na kusukwasukwa hata kujaa." Warumi 10:12; Luka 6:38. Katika kipimo cha namna hii ndicho Bwana alichomzawadisha Petro katika kazi yake. Na kila aina ya kujitolea katika kazi yake, italipwa sana. Soma Waefeso 3:20; 2:7.

Usiku huo wa wasiwasi katika ziwa, wanafunzi wakiwa peke yao, walikuwa na mashaka makuu. Lakini akiwapo pamoja nao, huburudika na kufurahi: Ndivyo ilivyo na kwetu pia. Tukiwa peke yetu bila Kristo, kazi yetu huwa kazi bure, na ni rahisi kunung'unika. Lakini tunapofanya kazi chini ya uongozi wake, hufurahi kwa uwezo wake. Hutuimarisha katika imani na tumaini. Yeye anayeweza kukusanya samaki baharini, kama alivyofanya kwa Petro na wenzake, huweza pia kuwavuta watu, ili watumishi wake waweze kuwa, "wavuvi wa watu."

Kristo alikuwa anao uwezo wa kuwawezesha watu wasio na elimu, kama wavuvi, ili wawe hodari na kuwa na madaraka kama hayo waliyokuwa nayo. Mwokozi hadharau elimu, ambayo hutawaliwa na upendo wa Mungu. Uwezo wa elimu ni baraka. Lakini wenye akili wa wakati wake walikuwa watu wenye kujitegemea wenyewe, hata hawakuweza kuafikiana na' mtu wa Nazareti. Walidharau kufundishwa na Kristo. Kitu cha kwanza ambacho wote wanapaswa kujifunza ni kutokujitegemea, hivyo hujiandaa kuvikwa
[134] tabia ya Kristo. Hali hii haipatikani kwa elimu ya sayansi inayofundishwa katika shule.

### Jinsi Watumishi halisi wanavyofundishwa

Yesu aliwachagua wavuvi ambao siyo wasomi waliofundishwa katika shule zenye makosa na desturi za wakati huo. Walikuwa watu wenye nguvu, wanyenyekevu, wenye nia ya kufundishwa. Katika hali ya kawaida, wengi walikuwa katika shughuli zao bila kutazamia mambo makuu ya ulimwengu. Wanahitaji mtaalamu awaamshe na kuwapa mambo yatakiwayo duniani. Watu wa jinsi hiyo ndio waliitwa na Yesu wawe watendakazi pamoja naye. Wanafunzi walipotoka kwa mafundisho ya Mwokozi, walikuwa sawa na Yeye katika nia, na katika tabia.

Kazi ya juu zaidi katika kufundisha ni ile ya kuzoeza nia kutafakari mambo ya juu, inayokutanishwa na nia kwa nia, na moyo kwa moyo. Maisha huhuika kwa njia hiyo tu. Basi ilikuwa bahati gani, kwa watu hao, kukaa na Kristo miaka mitatu kila siku. Yohana alisema: "Kutokana na ukamilifu wake, tumepokea neema kwa neema." Yohana 1:16. Maisha ya watu hawa, pamoja na kujenga tabia zao, na kazi kubwa iliyofanywa kwa ajili yao, ni kithibitisho cha vile Mungu anavyofanya kwa wote wanaokubali kufundishwa na kutii. Hakuna kikomo kwa kutumika, kwa mtu ambaye anaweka kando ubinafsi, na kumkaribisha Roho Mtakatifu afanye kazi moyoni mwake, na kuweka maisha yake wakfu kwa kazi ya Mungu. Kama watu watakubali kujiweka wakfu kwa Mungu, atawafundisha saa kwa saa wapate kufaulu. Mungu huwachukua watu jinsi walivyo, naye huwafundisha wafae kufanya kazi yake. Roho Mtakatifu akikaa ndani yao, atawarekebisha wafae kutumiwa naye. Nia inayojitoa kwa Mungu kamili, itakuzwa na kurekebishwa, halafu kutimiza matakwa ya Mungu. Tabia mbaya itatengenezwa kuwa kamili.

Ushirika wa kuendelea baina ya Yesu na wanafunzi wake, ulifanya maisha yao ya Kikristo yafanane naye katika hali zote. Atazidi kupata uwezo wa Yesu ukimwezesha kutambua hali halisi ya Kikristo. Naye atazaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Wakristo katika maisha yao ya kawaida, watakuwa wamepata elimu ya juu sana katika shule ya Kristo. Maana wameketi chini ya mtu ambaye hakuna mtu "aliyenena kama yeye."

[135] ## 26 — Siku za Shughuli na Raha katika Kapernaumu

Katika vipindi vya mapumziko ya Yesu kwa safari zake, alikaa Kapernaumu katika pwani ya bahari ya Galilaya, pakajulikana kana kwamba ndio "kwao". Mathayo 9:1. Pwani ya ziwa na vilima vilivyozunguka, kulikuwa na miji na vijiji vingi. Ziwani kulikuwa na mashua nyingi za wavuvi. Popote watu walikuwa na shughuli nyingi za maisha.

Mji wa kapernaumu ulikuwa kwenye njia kuu ya kutoka Dameski kwenda Yerusalemu, na Misri, pia kwenda upande wa bahari ya Mediterranean. Watu wengi walipitia katika mji wa Kapernaumu. Hapo Yesu aliweza kukutana na watu wa makabila na mataifa mbalimbali, na watu wa kila hali. Mafundisho yake yaliweza kuenezwa mahali mbalimbali na watu walioyasikia. Uchunguzi wa unabii uliwataharukisha wote waliohusika. Wakaanza kumfikiria Mwokozi. Malaika walikuwa wakitayarisha njia kwa ajili ya kazi yake. Mioyo yao iliguswa, na kumwelekea Mwokozi.

Katika Kapernaumu, yule mwana wa diwani ambaye aliponywa na Yesu, alikuwa shahidi wa uwezo wake. Mkuu wa mahakama na wenzake waliamini. Ilipojulikana kuwa Mwalimu alikuwako kati yao, mji mzima ulitaharuki. Siku ya Sabato mkutano mkubwa ulikusanyika, hata wakakosa nafasi.

Wote waliomsikia Mwokozi walishangaa kwa mafundisho yake, maana maneno yake yalikuwa na uwezo mwingi. Aliwafundisha kama wenye mamlaka, wala si kama waandishi. Luka 4:32; Mathayo 7:29. Mafundisho ya waandishi na wazee yalikuwa ya baridi sana wala hayana nguvu. Walikuwa wakisema kuwa wanaieleza she-
[136] ria, lakini hakuna mafunuo yoyote yaliyotoka kwa Mungu,, yenye kusisimua mioyo yao, na mioyo ya wasikilizaji wao.

Kazi ya Yesu ilikuwa kuifundisha kweli. Maneno yake yalimulika nuru katika mafundisho ya manabii, watu wakaona ukweli uliomo. Watu walikuwa hawajatambua maana ya maneno ya Mungu kama walivyotambua kwa mafundisho ya Yesu.

Yesu aliupamba ukweli wa neno la Mungu kwa njia ya kuulinganisha na hali halisi ya watu, kwa njia fupi. Watu wakaona wazi bila matatizo. Lugha yake ilikuwa safi, dhahiri, kama maji yatiririkayo. Sauti yake ilikuwa sawa na wimbo mtamu, ikilinganishwa na ya marabi.

## Hakuna Mashaka wala kusitasita

Alinena kama mwenye mamlaka. Marabi walinena kwa kusitasita, wakiwa na mashaka, na maana ya maandiko. Lakini Yesu alifundisha ukweli bila shaka yoyote. Fundisho lolote alilofundisha, alilinena kwa mamlaka.

Walakini alinena kwa juhudi na kwa moyo, si kwa magombano. Kwa kila hali, Mungu alidhihirishwa. Yesu alitaka kuvunja hali ya kupumbaza, inayowang'ang'ania watu katika mambo ya ulimwengu. Aliweka mambo ya ulimwengu kuwa, ni hafifu kulinganisha na ya milele. Lakini hakusahau umuhimu wake. Alifundisha kuwa, kufahamu mambo ya Mungu vema, humtayarisha mtu kutekeleza mambo ya dunia kwa uzuri zaidi, katika maisha ya kila siku. Akifahamu uhusiano wake na Mungu, alitambua nia mwungano wake na kila mtu katika ujamaa wa kibinadamu.

Alijua jinsi ya kunena kwa mtu mchovu, kwa wakati unaofaa. Isaya 50:4. Alikuwa na busara na jinsi ya kukutana na wenye chuki, na kuwaambia mifano itakayowavuta. Mifano yake alitumia mambo ya kila siku katika maisha. Ingawa huwa vielelezo rahisi sana, walakini huwaingia wasikilizaji wake kabisa. Ndege, maua, mbegu, mchungaji kondoo wa vielelezo hivi vyepesi, alifundisha ukweli. Na baadaye walipovikumbuka na kuviona, walikumbuka fundisho lake, au mafundisho yake.

Kristo hakuwasifusifu watu kamwe, wala kuwatukuza kwa ajili ya mambo yao mazuri. Lakini bila chuki wasikilizaji wake waliona kuwa maneno yake, kwa kweli ni ya busara, nayo yanapima ujuzi wao. Wasomi wakubwa waliburudishwa kwa maneno yake, na wasiokuwa na elimu walifaidika. Aliwafanya hata watu wa mataifa waone kuwa ujumbe wake unawahusu pia.

Hata katikati ya uhasama mkali, ulikaa katika hali ya salama. [137]
Tabia yake ya upendo, usemi wake na hali yake ya upendo, viliwavuta wote kwake, wale ambao hawakuharibiwa roho zao na hali

ya kutoamini. Watu wenye dhiki na mateso walimhesabu kuwa rafiki mfadhili mkuu, nao walitaka kujua zaidi ukweli anaoufundisha. Walitamani kukaa kwenye fadhili zake siku zote.

Yesu aliziangalia nyuso za wasikilizaji wake. Alipoziona jinsi zinavyong'aa kwa kuchangamka, zilimtia nguvu, na utoshelevu mkubwa. Mishale ya ukweli ilipokuwa ikipenya katika roho za watu wapendao ubinafsi, wakigeuka kuwa wema, Mwokozi alifurahi. Macho yake yalipowaona watu, ambao walikutana naye siku zilizopita, aling'aa kwa furaha. Aliposema maneno ya ukweli kwa wenye kushikilia sanamu, yaani anasa ya dunia, hali yake ilionyesha kuwa ujumbe wake haukukubalia na watu hao. Alipoona kuwa watu wameukataa ujumbe wa amani, roho yake ilisonononeka vikubwa mno.

Katika sinagogi Yesu alipokuwa akifundisha alikomeshwa, ili amweke huru mtu aliyefungwa na Shetani, yaani mwenda wazimu aliruka kutoka katika mkutano, huku akipiga makelele na kusema: "Tuache, tuna nini nawe, Ee Yesu wa Nazareti? Je umekuja kutuangamiza? Najua kuwa wewe mtakatifu wa Mungu." Mambo yalichafuka na kuvurugika. Watu waliangalia mambo ya mtu huyu, wakaacha mambo ya Yesu. Lakini Yesu alimkemea pepo, akisema: "Nyamaza, mtoke." Wakati pepo alipomwangusha kati ya watu, alimtoka asimzuru.

Mtu huyu aliyesumbuliwa hivyo, mawazo yake yalikuwa yameharibiwa na Sheteni lakini alipofika kwa Yesu aliamka kutaka afunguliwe kutokana na kifungo hicho cha Shetani. Lakini pepo mchafu alishindana ili amng'ang'anie. Mtu huyu alipotaka kuomba msaada kwa Yesu, pepo mchafu alitia maneno kinywani mwake, akapiga makelele kwa masumbuko na hofu.

Mwenye pepo mchafu alifahamu kidogo kuwa alikuwa mbele ya mwenye uwezo wa kumponya, lakini alipojaribu kumsogelea yule mwenye uwezo wa kuponya, alizuiliwa na uwezo fulani, uwezo huo ukaweka maneno fulani kinywani mwake. Mashindano baina ya Shetani na yeye yalikuwa makubwa.

Pepo mchafu alitumia uwezo wake wote ili amshikilie mtu huyu. Ilionekana kuwa mtu huyu atapoteza maisha yake, katika mashindano haya na adui huyu aliyeharibu hali yake. Lakini Mwokozi aliamuru na mtu akafunguliwa. Mtu huyu alisimama katika kundi
[138] la watu, hali wakishangaa, lakini wakifurahi kwa kuponywa kwake.

Hata pepo mchafu alishuhudia mamlaka ya Mwokozi. Macho ya mtu huyo yaliyokuwa yakitisha sana kuangalia, yalionekaria matulivu yakishukuru nguvu ya Yesu. Watu wakasema: "Jambo gani hili? Hili ni fundisho jipya! Kwa amri huwaamuru hata pepo wachafu nao humtii."

Mtu huyu amekuwa ameharibiwa na anasa za dhambi naye alidhani kuwa maisha yake yatakuwa yenye furaha na sikukuu. Hakufikiri kuwa atakuwa kitisho kwa watu, na shutumu kwa jamaa yake. Alidhani kuwa maisha yake yatakuwa katika hali safi ya upuzi wa anasa. Lakini pasipokuwa na kiasi na upuzi viliyaongoza maisha yake vibaya, na Shetani akamteka. Wakati alipotaka kujiokoa katika mtego huo, hakuweza. Alikuwa ameshikiliwa katika uwezo wa mwovu. Shetani alikuwa ametawala viungo vyake vyote. Mtu huyu alipokwisha kuwa katika utawala wake, Shetani akamtendea mambo ambayo hayana huruma. Ndivyo ilivyo kwa watu wanaojiweka katika mikono ya Shetani. Mtu anayejitumbukiza katika maisha ya anasa katika maisha yake ya ujana, huishia katika hali ya wazimu.

Roho ile iliwatawala Wayahudi wasioamini, lakini kulikuwako na Yesu ambaye alikuwa mtawa. Hali ya Wayahudi wasioamini ilikuwa mbaya kuliko ya mtu aliyepagawa na pepo mchafu. Maana wao hawakumhitaji Kristo. Kwa hiyo walikuwa katika uwezo wa Shetani zaidi.

Kuwako kwa Kristo, akifanya kazi kati ya watu, kulikuwa na juhudi kuu na msukosuko mkuu wa ufalme wa giza. Kwa vizazi na vizazi Shetani amewakandamiza watu katika masumbuko na maradhi ya namna namna. Amewatumbukiza dhambini na matatizoni. Halafu amemsingizia Mungu kuwa ndiye amesababisha hayo yote. Yesu alikuwa akiwafunulia watu tabia ya Mungu jinsi ilivyo. Alikuwa akivunja uwezo wa Shetani na kuwaweka watu huru kutokana na mambo ya Shetani. Upendo na uwezo wa mbinguni ulikuwa ukiwachangamsha watu, na mkuu wa giza alichukizwa sana. Alipinga kazi ya Kristo kwa kila hatua.

## Shetani atenda kazi kwa kujificha

Ndivyo itakavyokuwa katika wakati wa mapambano ya mwisho, baina ya haki na uovu. Wakati wanafunzi wa Yesu watakapopata nguvu mpya na maisha mapya, Shetani naye atawavuvia wafuasi

wake nguvu mpya na juhudi mpya. Kwa hila na ujanja wa muda mrefu alivyopata katika mapambano haya, Shetani atajigeuza hali
[139] katika mapigano haya, aonekane kana kwamba ni malaika wa nuru. Watu wengi hutega masikio kusikiliza mafundisho ya Shetani, na roho zenye kudanganya. 1 Timotheo 4:1.

Viongozi na walimu wa Israeli walidharau njia ambazo wangetumia ili washinde roho zidanganyazo za kishetani. Njia hizo ni kulifuata Neno la Mungu, ambalo lilimshindisha Kristo huko jangwani. Kwa kulitafsiri vibaya neno hilo, likaeleweka kinyume cha maongozi ya Mungu. Wakati ufafanuzi wa kinyume cha ukweli ulivyo hasa. Kwa hiyo neno la Mungu likapotoshwa, lisiwe na uwezo wake, na badala yake udanganyifu wa Shetani ukakubaliwa kana kwamba ndiyo ukweli.

Historia inajirudia. wakati wetu huu, waongozi wa dini huharibu imani yao na hali wanalo neno la Mungu mikononi mwao. Hukatakata vipande na kutia mawazo yao, badala ya neno la Mungu. Hii ndiyo sababu ushenzi umezidi na maovu yamejaa popote.

Wale wanaoacha kufuata maandiko matakatifu yaliyo dhahiri, ambayo ni uwezo wa Mungu, hukaribisha roho za mashetani. Tuhuma na kupapasapapasa maandiko wazi ya neno la Mungu, hufungua mlango wa kuingiza ibada ya roho chafu, hata kwa wale wanaojiita kuwa ni wakristo. Wajumbe wa Shetani huenda bega kwa bega na mahubiri ya injili. Watu wengi hujitia kuchunguza roho hizi za mashetani, na wakiisha kuona kuwa kuna nguvu isiyo ya kibinadamu, huendelea kudumu hapo mpaka hata wao wakapata hali hiyo pia. Mwisho uwezo wa mtu hushindwa, na mtu hutekwa nyara bila habari, huwa kama mwenye pepo wa Kapernaumu. Walakini hali yake si kama ya yule.

Anaweza kushinda kwa nguvu za Neno la Mungu. Tunapotamani kujua neno la Mungu na kulifuata, na kufanya mapenzi yake, ahadi yake kwetu ni "Mtaifahamu kweli, na kweli itawaweka huru." "Kama tu atataka kufanya mapenzi ya Mungu, atajua kama mafundisho haya ni ya Mungu." Yohana 8:32; 7:17. Kwa njia ya kuziamini ahadi hizi, kila mtu aweza kuokolewa na mitego hii na makosa yenye kushikilia mtu dhambini.

Saa kwa saa walifurika kuja na kwenda, maana hakuna ajuaye kuwa Mponyaji atakuwa bado yuko hapo. Kapernaumu ilikuwa haijaona siku yenye shughuli kama hii. Anga ilijazwa na sauti za

shangwe na shukrani kwa ajili ya kuponywa. Mwokozi alifurahia uwezo wake wa kuwaponya wenye dhiki.

Watu walipoondoka, usiku ulikuwa umeendelea sana, na ukimya [140]
wa usiku uliobaki ukawa wa kupumzika, nyumbani kwa Simoni. Mchana wa hoihoi ulikuwa umepita, na wakati wa kimya cha usiku kiliendelea. Lakini katikati ya kimya hicho, watu wakiwa wamelala .... Mwokozi alitoka akaenda mahali pa kimya kuomba.

Kila mara Yesu aliwaruhusu wanafunzi wake, ili akawasalimu katika miji yao, na kupumzika. Lakini ilikuwa vigumu kuacha kazi kwa ajili ya makutano ya watu. Mchana kutwa alishughulika na jioni, au asubuhi mapema alikwenda mlimani kuongea na Baba yake. Mara nyingi aliomba usiku kucha, ndipo akaja kufanya kazi yake kwa watu.

Asubuhi mapema Petro na wenzake walikula kwa Yesu wakisema kuwa watu wanamtafuta. Wakuu wa Yerusalemu wanamtafuta kumwua, hata watu wa kwao pia wanataka kumwua, lakini huko Kapernaumu alikaribishwa kwa furaha. Ndipo matumaini ya wanafunzi yakapata nguvu, maana walikuwa na wasiwasi. Ilikuwa, kwamba wapenda uhuru katika Kapemaumu ndio walikuwa watetezi wa ufalme mpya. Kwa mshangao walisikia maneno ya Kristo yakisema: "Twende tu katika miji mingine, ili nipate kuhubiri huko pia. Maana nilikuja kwa ajili hiyo." Marko 1:38.

Yesu hakuridhika kusifiwa kama mtenda miujiza. Watu walipokuwa na matumaini kuwa amekuja kama mfalme ili kuusimamisha ufalme duniani, alitaka kugeuza mawazo yao kuyaelekeza mbinguni, yaani mambo ya kiroho.

Mashangilio ya watu hawa wapuuzi yalimchukiza sana. Heshima na sifa wanazopewa watu wa dunia, kwa Kristo zilikuwa ngeni tu. Yesu hakutumia njia za watu ili kujulikana. Yesu hakupiga kelele, wala kujionyesha kwa njia yoyote. Alitoa haki kwa uaminifu tu. Isaya 42:2, 3.

Katika maisha ya Yesu hakikuwako kitu cha kujionyesha wala hali ya kutaka pato. Kristo alijificha ndani ya Mungu; na Mungu alijidhihirisha katika Mwana wake. Jua la Haki halikung'aa ulimwenguni kwa fahari ili kufanya nuru kwa utukufu wake, jua la Haki hilo lilitokea kimya, polepole, likang'aa gizani, likaleta uhai duniani. Ndivyo jua la haki hung'aa kwa mabawa ya kuponya. Malaki 4:2.

[141] # 27 — Mwenye Ukoma wa Kwanza Kuponywa na Kristo

Katika magonjwa yote yaliyojulikana huko Mashariki, ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya mno. Hali yake ya kutoponyeka, na jinsi unavyoambukiza, na matokeo yake kwa mgonjwa, yote huufanya uwe wa kutisha sana. Kwa Wayahudi ukoma ulikuwa unahesabiwa kuwa ni adhabu ya kutenda dhambi, yaani adhabu ya Mungu; kwa ajili ya dhambi.

Mwenye ukoma alifungiwa nje ya makao ya watu, akawa sawa-sawa na mtu aliyekufa. Kila kitu alichogusa kilichohesabiwa kuwa kichafu. Pumzi yake iliichafua hewa. Mtu yeyote aliyetuhumiwa kuwa ana ugonjwa wa ukoma, alipaswa kujionyesha kwa kuhani. Kama kuhani akiona kuwa ni ukoma, basi hutoka kwa watu wazima, akaenda kuishi na wenye ukoma. Sheria hiyo ilikuwa ya lazima, kwa kila mtu mtawala na raia pia.

Mwenye ukoma alipaswa kubeba laana hiyo, akitengwa mbali, na jamaa zake na rafiki zake pia. Ilimpasa kutangaza habari za ugonjwa ili kuwahadhari watu wengine kwa kupiga makelele na kusema: "Mchafu! mchafu!" Kelele za kilio cha huzuni cha kuwaonya watu, kilikuwa ndicho kionyesho kwamba kuna hatari.

Habari za Kristo na kazi yake zilienea mahali pengi pa matuo ya wagonjwa hawa, na kuwaletea matumaini. Lakini tangu siku za Elisha jambo la kutakasa wenye ukoma halikusikika tena, wala kujulikana. Kulikuwa na mtu mmoja ambaye alianza kuwa na imani. Walakini angalimfikiaje Mponyaji huyo? Je, Kristo angeweza kumponya? Je, kama akiona kuwa ugonjwa wake ni adhabu kutoka kwa Mungu, asingalimlaani?

Mwenye ukoma akafikiri mambo yote aliyosikia juu ya Yesu.
[142] Hakuna mtu aliyemtaka amsaidie, akafukuzwa. Mgonjwa huyu alikusudia kutafuta mponyaji. Labda wataweza kukutana naye njiani, au akiwa katika kufundisha watu, au uwandani nje ya mji. Hilo ndilo lilikuwa tumaini lake tu.

Mwenye ukoma aliongozwa kwa Yesu, akamkuta akifundisha watu, kando ya ziwa. Mwenye ukoma akiwa anasimama mbali, aliweza kusikia maneno machache ya Kristo. Alimwona akinyosha mikono yake juu ya mgonjwa fulani, aliyekuwa kilema. Akaona tena kipofu, na mwenye kupooza. Akaona na wafu wakifufuka, na kusimama, hali wakimsifu Mungu, kwa ajili ya kuponywa. Akapata imani, akasogea karibu. Akazuiliwa asimwendee akijisahau alivyo, alitazamia kupona tu.

Alionekana kuwa kioja; mtu wa kuchukiza. Watu walipomwona walitawanyika kumpisha, huku wakipiga makelele. Wengine walijaribu kumzuia asimfikie Yesu. Lakini hakuwajali. Alimwona Mwana wa Mungu peke yake. Akimsogelea Yesu, alijitupa miguuni mwake, huku akipaza sauti na kueema: "Bwana ukitaka waweza kunitakasa." Yesu akajibu: "Nataka, takasika." Akaweka mkono wake juu yake.

Mara moja badiliko likatokea kwenye ukoma. Mwili wake ukatakasika, akawa mwenye afya, mishipa yake na misuli ikaimarika. Makovu katika uso wake yakatoweka. Ngozi nyororo kama ya mtoto mchanga ikatokea.

Kristo akamwagiza asimwambie mtu jambo hilo. Yesu akamwambia: "Angalia, usimwambie mtu yeyote, ila nenda ukajionyeshe kwa kuhani, ukatoe vitu vile Musa alivyoagiza kutolewa, ili kuwa ushuhuda kwako." Kama kuhani angalijua maana yake, chuki yao kwa Kristo ingelitulia. Yesu alitaka mtu huyu afike hekaluni kabla uvumi wa kumponya haujawafikia. Hivyo uamuzi wa kawaida ungefikiwa, na mtu huyu angeruhusiwa kurudi katika jamaa yake. Mwokozi pia alijua kuwa kumponya mwenye ukoma kulikuwa kukizunguzwa popote na kwamba wenye ukoma wengine watakuja, na kelele zitapigwa kwamba watu wanatiwa unajisi kwa ajili ya wakoma wengi wanavyokuja. Wakoma wengi wasingaliona kuwa huu ni baraka mkubwa kwao na kwa wengine. Na kwa kuwa wakoma wengi wangemjia bila kushika utaratibu waliopewa angeshitakiwa kuwa anavunja sheria ya kuzuia wakoma. Na mahubiri yake yangevurugwa.

Makutano waliona kuponywa kwa mwenye ukoma, nao walitaka kujua jinsi makuhani watakavyosema juu ya jambo hilo. Mtu huyu aliporudi kwa jamaa zake, kulikuwa na furaha na hoihoi kubwa sana. [143]
Hakuzidi kunyamaza kuhusu kuponywa kwake. Maana hakuelewa

kuwa kutangaza jambo hilo kungefanya makuhani na wazee wakaze nia juu ya kumwangamiza Yesu. Mtu aliyeponywa alifurahi kwa ajili ya kupona na kurudi katika jamii ya wengine, na ilikuwa vigumu kuacha kumsifu Tabibu aliyemponya. Lakini kitendo chake hicho, kilisababisha watu waendelee kumjia Yesu, hata ikamlazimu kukomesha kazi yake kwa muda.

Kila kitendo cha Kristo katika kazi yake kilikuwa na kusudi lake. Alitumia kila njia ya kuwanyamazisha makuhani na wazee wasimlaumu kama mvunja sheria au kawaida. Alipomtuma mwenye ukoma kwa makuhani alitaka kuwaziba vinywa wasiseme kuwa hafuati kanuni. Mafarisayo walidai kuwa Kristo ni mvunja sheria, lakini alivyomwagiza wenye ukoma kwenda kujionyesha kwa kuhani na kutoa sadaka, vilionyesha kuwa madai ya Mafarisayo siyo ya kweli. Kristo alionyesha kuwa aliwapenda watu na kuheshimu sheria, na ana uwezo juu ya dhambi, magonjwa, na mauti.

Makuhani hao hao walimtenga mwenye ukoma na jamii, ndiyo waliomthibitishia kuwa amepona kabisa, akarudishwa katika jamii. Alilitukuza jina la Yesu kwa shangwe kuu. Makuhani walipewa nafasi ya kuujua ukweli. Wakati wa kazi ya Kristo, makuhani walijali kidogo sana, lakini baada ya kupaa kwake mbinguni, "hesabu kubwa ya makuhani waliitii kweli." Matendo 6:7.

### Jinsi Kristo anavyo safisha moyo kutokana na dhambi

Kazi ya Kristo ya kumtakasa mwenye ukoma ni kielelezo cha jinsi anavyosafisha moyo wenye dhambi. Mtu yule aliyemjia Kristo alikuwa amejaa "ukoma mwili mzima." Wanafunzi walitaka kumzuia Mwalimu wao asimguse. Lakini alipomwekea mikono yake kwenye ukoma, hakunajisika. Kule kumgusa kulileta uwezo wa kupona.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa ukoma wa dhambi. Haiwezekani kuponyesha kwa uwezo wa kibinadamu. Kutoka katika nyayo za miguu mpaka kichwani, hakuna uzima, ila ni vidonda, na majeraha, yatokayo usaha." Isaya 1:6. Lakini Yesu anao uwezo wa kuponya. Mtu yeyote atakayeanguka miguuni mwake na kusema", kwa imani, "Bwana ukitaka waweza kuni takasa", ataweza kusikia jibu, "Nataka takasika."

[144] Nyakati nyingine, Yesu hakutoa uwezo wa kuponya mara moja.

Katika habari za mwenye ukoma huyu, ombi lake lilishughulikiwa mara moja.

Tunapoomba vitu vya dunia jawabu pengine hutupatia kitu kingine badala ya kile tulichoomba. Lakini haitakuwa hivyo tunapoomba kuokolewa, kutokana na dhambi. Ni mapenzi yake kututakasa na kutufanya wana wake kamili, tuishi bila dhambi. Kristo alijitoa kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na maovu yaliyomo duniani, kwa kadiri ya mapenzi ya Mungu Baba yetu. Wagalatia 1:4. Tukiomba kitu kwa kadiri ya mapenzi yake atusikia. Na tukijua kuwa atusikia, kwa yote tuombayo, hujua ya kuwa tunayapokea yale tuombayo. Yohana 5:14, 15.

Katika kumponya mtu aliye huko Kapernaumu, Kristo alifundisha fundisho lile lile tena., Alidhihirisha uwezo wake wa kusamehe dhambi, ndipo alipofaya mwujiza. Sawa na mwenye ukoma, huyo wa kupooza naye hakuwa na tumaini lolote. Ugonjwa wake ulisababishwa na maisha yake mabaya. Na ugonjwa wake ulikuwa wa kuchukiza sana. Alikuwa amewataka Mafarisayo na waganga, lakini hawakuweza kumponya, walimwacha tu katika masumbuko yake.

Alipoona kuwa hakuna tumaini lolote mahali popote alikata tamaa kabisa. Kisha alisikia habari za Yesu. Rafiki zake walimtia moyo kuwa kama akimwendea Yesu kwa imani ataweza kuponywa. Watamchukua na kumpeleka kwake.

## Mzigo wa dhambi

Yesu hakufurahia kuponya watu miili tu, bali alifurahia kumwondoa mtu katika wasiwasi wa kulemewa na dhambi. Kama mtu angepata hakikisho la kusamehewa dhambi, angeridhika hata ikiwa ni kufa angekufa kwa tumaini. Mtu anayekufa hana wakati wa kupoteza. Aliwasihi rafiki zake wampeleke kwa Yesu hata kama ni kumbeba juu ya kitanda. Lakini pale Mwokozi alipokuwa palikuwa na watu wengi sana, hata haikuwezekana kwa mgonjwa na rafiki zake kufika karibu, au kiasi cha kusikia sauti yake.

Yesu alikuwa akifundisha nyumbani kwa Petro, Wanafunzi wake walikuwa karibu naye. Palikuwa na Mafarisayo na wataalam wakiketi karibu naye, nao walitoka katika miji yote ya Galilaya, na Uyahudi na Yerusalemu, kama wapelelezi. Huko nje walikusanyika

watu wengi, wenye kutaka kusikia, wanyenyekevu, wachunguzi wa mambo, na wasiamini. Uwezo wa Bwana wa kuponya ulikuwa
[145] unafanya kazi. Lakini Mafarisayo na Walimu wakuu hawakukutambua kuwako kwa Roho wa Bwana. Hakuwa na haja yoyote maana hawakuhusika na uponyaji huo. Aliwashibisha wenye njaa ya haki na mambo mazuri, ila matajiri, ambao hawakuwa na haja yoyote, walikwenda zao watupu. Luka 1:53.

Waliomchukua mwenye kupooza walijaribu kuwasukuma watu ili wapate nafasi ya kupita, lakini hawakufaulu. Mgonjwa atakata tamaa? Akawashauri waliomchukua wampitishe juu ya paa la nyumba, wavunje mahali na kumtelemsha chini katika miguu ya Yesu.

Mwokozi aliona macho yenye machozi akaelewa maana yake. Wakati mgonjwa huyu alipokuwa angali nyumbani, alikirishwa moyoni juu ya uwezo wa Yesu wa kuponya. Alipoungama dhambi zake, rehema za kuponya za Mwokozi zilimtia changamko rohoni.

Sasa maneno ya Mwokozi yalisema kwake: "Mwana . . . dhambi zako zimesamehewa." Hali yake ya kukata tamaa ikatoweka, hali ya kusamehewa na tumaini lake ikang'aa moyoni mwake. Maumivu yake yakatoweka, hali yake ya afya ikamrudia. Mgonjwa wa kupooza akaponywa, mzigo wa dhambi zake ukasamehewa.

Kwa maneno machache ya imani aliyaamini maneno ya Yesu. Wala hakutaka kuomba kitu zaidi. Akajazwa na furaha kuu aliondoka watu wakimwangalia kwa hofu.

Marabi walikumbuka jinsi mtu huyu alivyowafikia akitaka msaada, nao hawakuweza kumpa msaada wowote, akasema kuwa alikuwa akiugua ugonjwa wa laana ya dhambi. Wakaona mambo muhimu yanayotendwa na Yesu, na ya kwamba mvuto wake unazidi kuwa mkubwa kwa watu. Wakatazamana kwa mshangao. Wakaona kuwa ni lazima kufanya jambo fulani ili kuzuia mambo haya. Yesu ametangaza wazi kuwa mwenye kupooza amesamehewa dhambi zake Mafarisayo waliweza kusema kuwa, jambo hilo ni kufuru, ni kosa linalostahili kufa. Wakasema "Ni kufuru! Ni nani awezaye kusamehe dhambi, isipokuwa ni Mungu mwenyewe."

Yesu akiwakazia macho, alisema: "Kwa nini mnawazawaza mioyoni mwenu? Ni jambo gani jepesi kumwambia mwenye kupooza, Dhambi zako zimesamehewa, au kusema, Ondoka ujitwike kitanda uende zako? Lakini mjue kuwa Mwana wa Adamu anao

uwezo wa kusamehe dhambi. Akamwambia mwenye kupooza, Nakuambia ondoka, ujitwike kitanda chako uende zako nyumbani."

Ndipo mtu aliyekuwa amechukuliwa kwa machela, akasimama [146]
kwa miguu yake, akiwa na nguvu kamili kama kijana.

Kila kiungu mwilini mwake kikawa imara. Hali ya afya kamili ikawa badala ya hali ya unyonge na kifo. Mara moja akaondoka, akachukua kitanda akaenda zake mbele ya watu wote. Basi wote wakashangaa, wakamtukuza Mungu wakisema, Hatujaona jambo kama hili katika kizazi hiki.

Uwezo wa kuumba ulitia nguvu katika mwili uliooza. Uwezo ule ule uliosema kwa mtu wa kwanza aliyeumbwa kwa mavumbi ya nchi, ndio huo huo uliosema kwa mwenye kupooza . Uwezo uliotia uzima mwilini mwake, ndio uliotakasa moyo wake. Kristo alimwamuru mwenye kupooza, aondoke na kwenda ili watu wajue kuwa Mwana wa Adamu anao uwezo wa kusamehe dhambi duniani.

### Kuponya kiroho kila mara hutangulia kuponya kimwili

Leo watu maelfu huugua maradhi ya mwili kama yule mgonjwa kupooza, hutamani kupata ujumbe unaosema: "Dhambi zako zimesamehewa." Dhambi ndiyo asili ya maradhi yao. Mponya wa roho peke yake ndiye awezaye kutia afya ya mwili.

Yesu bado angali na uwezo wa kuponya kama alivyokuwa akiponya wagonjwa na kuwatangazia kusamehewa dhambi zao. "Yeye husamehe maovu yote." "Hukuponya maradhi yote." Zaburi 103:3; 1 Yohana 3:8; Yohana 1:4-10; 10:10; 1 Kor. 15:45.

Kama vile mtu aliyeponywa alivyopita kati ya watu akibeba mzigo wake kama kwamba ni mzigo wa manyoya, watu walimpisha. Kwa mshangao mkubwa walinong' onezana wakisema: "Leo umeona jambo jipya."

Mafarisayo walishangaa, wakawa kimya, wakashindwa la kusema, ila hawakukiri kuwa uwezo huo ni mkuu zaidi kuliko uwezo wa kibinadamu. Kutoka katika nyumba ya Petro, walikomwona mwenye kupooza akiponywa, walikwenda zao katika upotofu wao, wakitafuta njia ya kumnyamazisha Mwana wa Mungu.

Nyumbani kwa yule aliyeponywa kulikuwa na shangwe kuu. Jamaa zake walimkusanyikia wakilia kwa furaha, wakishangaa wakidhani ni ndoto. Mwili uliokuwa umenyong'onyea sana ulikuwa safi

kabisa. Alitembea sawasawa. Usafi na amani ilikuwa katika uso wake. Mtu huyu na jamaa yake walikuwa tayari kumwandama Yesu daima. Hakuna shaka yoyote iliyozima imani yao na nuru yao na kutia giza kamwe.

# 28 — Mathayo: Kutoka Kutoza Ushuru Mpaka Mwanafunzi [147]

Wakuu wa Kirumi katika Palestina walikuwa wamechukiwa sana. Na kwa kuwa kodi ilitozwa na watawala wa kigeni, lilikuwa chukizo la daima, linalowakumbusha kuwa kujitawala kwao kumekoma. Watoza kodi hawakuwa vyombo vya Warumi tu, bali walikuwa wenye uchu wa kujitajirisha kwa njia ya kidhalimu, na kuwatoza watu isivyo haki. Myahudi aliyefanya kazi hii alidharauliwa sana na kutiwa katika fungu la watu waovu.

Lawi Mathayo alikuwa wa namna hii, ambaye aliitwa kufanya kazi ya Kristo. Mathayo alikuwa amesikia mahubiri ya Kristo, na kwa kadiri Roho wa Mungu alivyomdhihirishia dhambi zake alitamani kwenda kwa Kristo, ili apate msaada, lakini alivyokuwa amezoea kutengwa na Marabi, na kuhesabiwa kuwa mtu mwovu hakuwa na atumaini kuwa Mwalimu Mkuu huyu angemjali.

Siku moja akiwa ameketi katika chumba chake cha kutozea kodi, mtoza ushuru huyu alimwona Yesu akitokea. Alishangaa mno aliposikia maneno yakimwambia, “Nifuate”.

Mathayo “akaacha vyote, akainuka, akamfuata.” Mathayo hakukawia, wala hakuuliza swali lolote kuhusu kazi au mali au ufukara wake kama akifuata kazi hiyo. Ilimtosheleza kuwa pamoja na Yesu, ili aweze kusikiliza maneno yake, na kushirikiana naye katika kazi yake.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika wakati Yesu alipowaita akina Petro na wenzake, ili wamfuate. Waliacha mashua zao na nyavu zao mara moja wakamfuata. Wengine walikuwa na watu waliowategemea ili wawape mahitaji yao, lakini walipokubali mwaliko wa Mwokozi, hawakuuliza kuwa, “Tutaishije na kusaidia watu wanaotutegemea?” Baadaye Yesu alipowauliza: “Je, hapo nilipowatuma hamna mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlipungukiwa na kitu? Wakasema.” Luka 22:35.

[148] **Jaribio la Kufarakisha wanafunzi**

Marabi walishikilia nafasi ya kumshitaki Yesu, lakini walitafuta kutimiza jambo hilo kupitia kwa wanafunzi wake. Kwa njia ya kuwachochoea wawe na chuki, walitumaini kuwafarakanisha na Bwana wao. Walisema: "Kwa nini Bwana wenu hula na watoza ushuru, na wenye dhambi?"

Yesu hakungoja wanafunzi wake wawajibu, ila Yeye mwenyewe aliwajibu, akisema:.... Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi wapate kutubu." Mafarisayo walijidai kuwa wenye haki, kwa hiyo hawakuhitaji tabibu, lakini waliwahesabu watoza ushuru na watu wa mataifa kuwa wapotevu. Basi haikuwa kazi yake kama tabibu kuwaendea watu wasiomhitaji, ila wanaomhitaji.

Yesu akawaaambia Marabi: "Nendeni mkajifunze maana ya maneno haya. Nataka rehema wala si sadaka." walijidai kulielewa neno la Mungu, lakini kamwe hawakuifahamu tafsiri yake kiroho.

Mafarisayo walinyamazishwa kwa muda, lakini walikusudia kamili kuendeleza uadui wao juu ya Yesu. Mara tena walijaribu kuwachochea wanafunzi wa Yohana Mbatizaji juu ya Yesu. Mafarisayo hao walikuwa wamemdharau Yohana mbatizaji kwa ajili ya maisha yake ya kutotaka makuu, na mavazi yake hafifu. Walimwita kuwa mtu aliyepungukiwa na akili. Walikuwa wamejaribu kuwachochoea watu wasimjali. Roho wa Mungu alikuwa amewaingia watu hawa wenye kudharau, wakatubu na kuungama dhambi zao, lakini walitangaza kwaamba Yohana ana roho wa mashetani.

Sasa Yesu alipokuja akichanganyikana na watu, na kula pamoja nao, na kunywa nao, wakamshitaki kuwa mlafi na mlevi. Hawakudhani kuwa Yesu alikula na wenye dhambi ili awalete nuruni, awatoe gizani. Hawakudhani kuwa kila neno lililonenwa na Mwalimu wa mbinguni, ilikuwa mbegu iliyopandwa, ambayo itaota na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Wao hawakukusudia kuipokea nuru hiyo, na ijapokuwa walimdhihaki Yohana Mbatizaji, sasa hawakutaka kufanya urafiki na wanafunzi wake ili kumpinga Yesu. Walisema kuwa Yesu alikuwa anadharau mapokeo yao ya kale, walitofautisha hali ya Yohana na kuona kuwa ilikuwa nafuu kuliko hii ya Yesu ya kula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi.

Kwa wakati huu wanafunzi wa Yohana walikuwa na huzuni sana. Siku zao zilikuwa za maombolezo kwa vile Mwalimu wao mpendwa

alikuwa gerezani. Na Yesu hakufanya chochote ili kumsaidia. Kama Yohana alitumwa na Mungu, kwa nini Yesu na wanafunzi wake [149] wanatofautiana basi?

Wanafunzi wa Yohana walidhani kuwa, huenda kuna haki katika maneno ya mafarisayo. Waliona kanuni nyingi zilizoshikwa na Marabi. Kufunga kulikuwa tendo linaloenea kwa Wayahudi, nalo lilionyesha wema, ambalo lilitendwa mara mbili kila juma. Mafarisayo na wanafunzi wa Yohana walikuwa wakifunga, wakati wanafunzi wa Yohana walipomjia Yesu na swali: "Kwa nini sisi na Mafarisayo hufunga kila mara, bali wanafunzi wako hawafungi?"

Yesu alijibu kwa upole. Hakutaka kukanusha kawaida yao juu ya kufunga, ila kuwaelekeza vizuri, kuhusu kazi yake. Yohana mwenyewe alikuwa amesema: "Aliye na bibi arusi ndiye bwana arusi, asimamaye na kumsikia akifurahia sauti ya bwana arusi; kwa hiyo furaha yangu ni kubwa." Yohana 3:29. Wanafunzi wa Yohana hawakusahau maneno ya Mwalimu wao. Kwa kutoa kielelezo Yesu alisema: "Mwaweza kuwafanya watoto wa bibi arusi wafunge wakati bwana arusi yuko pamoja nao?"

Mkuu wa mbinguni alikuwa pamoja na watu. Zawadi kuu ya Mungu imetolewa kwa ulimwengu. Furaha kwa maskini kwa sababu amekuja kuwafanya warithi katika ufalme wake. Furaha kwa matajiri, kwa sababu atawafundisha kusalimisha mali yao; ya milele. Furaha kwa wajinga, kwa sababu ataelimisha hata wapate wokovu. Furaha kwa wenye elimu, kwa sababu atawafungulia kina kipana zaidi cha mambo ambayo hawajayaona. Huu sio wakati wa kulia kwa wanafunzi na kufunga. Lazima wafungue mioyo yao wapokee utukufu wake, ili nao wapitishe nuru hiyo kwa wale wanaoishi gizani na katika uvuli wa mauti.

## Uvuli Mzito

Picha ilionekana kuwa ni safi, lakini mbele yake kulikuwa na uvuli mzito kabisa, ambao ulifahamiwa na Yesu peke yake. "Siku zitakuja ambazo, bwana arusi ataondolewa kutoka kwao, ndipo hapo watafunga." Watakapomwona Bwana wao akisalitiwa na kusulibishwa, ndipo wanafunzi watalia na kufunga.

Atakapotoka kaburini, huzuni yao itageuka kuwa furaha. Baada ya kupaa kwake kwenda mbinguni, ataendelea kukaa pamoja

nao kwa njia ya Mfariji, yaani Roho Mtakatifu, hapo hawatalia tena. Shetani anapenda kuwakatisha tamaa na kuwaambia kuwa wamedanganyika kabisa. Lakini kwa njia ya imani, watatazama
[150] katika patakatifu pa mbinguni, ambapo Yesu anapowahudumia. Lazima wafungue mioyo yao kwa Roho Mtakatifu, na kufurahi kwa ajili ya kuwako kwake. Walakini siku za kujaribiwa zitakuja. Wakati ambao Kristo hatakuwako kimwili, nao watashindwa kumtambua Mfariji, hapa basi itawafaa kufunga.

Maandiko Matakatifu huonyesha aina ya kufunga ambayo hutakiwa na Mungu; ni kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kuvunja kila nira." "Je siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta masikini waliotupwa nyumbani kwako?" Isaya 58:6, 10. Hapa ndipo inapoonyeshwa kazi ya Kristo.

Yesu akiendelea kuwajibu wanafunzi wa Yohana, alitoa mfano: "Hakuna mtu atiaye kiraka kipya kwa nguo kuukuu, maana kiraka hicho kitaipasua nguo." Mathayo 9:16. Majaribio ya kuafikanisha mapokeo na ushirikina wa Mafarisayo pamoja na dini halisi ya Yohana kungethibitisha matengano makubwa zaidi.

Wala kanuni za mafundisho ya Kristo zisingalipatana na dini ya nje ya Mafarisayo. Kristo angetofautisha wazi baina ya dini ya zamani na ile mpya." Wala watu hawaweki divai mpya katika viriba vikuukuu, maana wakifanya hivyo viriba vitapasuka na divai itamwagika; lakini divai mpya huwekwa katika viriba vipya, vikahifadhika vyote. Mathayo 9:17. Viriba vilitumiwa kuwekea divai mpya, lakini baada ya wakati kupita, hukauka, na kupasuka, na hivyo huwa havifai kutumika tena. Viongozi wa wayahudi walikazana kushika mapokeo tu na ibada za nje nje, bali roho zilifanana na viriba vilivyokauka. Kwa vile walivyoridhika na dini yao, hawakutaka kuona mambo mapya yakiingizwa katika dini yao. Dini ya kweli, ifanyayo kazi kwa upendo, haikupata nafasi katika dini ya Mafarisayo. Hii hutakasa mioyo na kuipa uzima mpya. Mafarisayo walikuwa na dini ya mfano tu ya kanuni za wanadamu. Kuunganika na dini ya kweli ya Kristo ingekuwa kazi bure. Ukweli wa Mungu, usingaliingia katika viriba vya mapokeo ya Mafarisayo.

### Viriba vipya kwa divai mpya

Mwokozi aligeukia mbali kutoka kwa Mafarisayo, akatafuta watu wengine ambao watasikiliza ujumbe wake wa mbinguni. Akapata wavuvi, watoza ushuru, katika soko, mwanamke wa Samaria, na kwa watu wa kawaida tu, ambao watasikiliza ujumbe wake, kwa watu wa namna hii alipata viriba vyake vya kuwekea divai. Watu hao waliupokea mwanga wake kwa furaha, ambao Mungu aliwatuma [151] wajumbe wake wautangaze.

Mafundisho ya Kristo yanayofananishwa na divai mpya hayakuwa mafundisho mapya, ila ni yale yaliyofundishwa tangu mwanzo. Lakini kwa Mafarisayo, mafundisho ya Kristo yalikuwa mapya kwa kila hali nayo hayakutambuliwa, wala kukubaliwa.

"Hakuna mtu anywaye divai kuu kuu, anayetamani divai mpya, maana husema, Divai kuu kuu ni bora." Ukweli uliotolewa kwa wazee wa zamani na manabii uling'aa kwa uzuri wa neno la Kristo. Lakini waandishi na Mafarisayo hawakuwa na haja ya divai mpya. Hawana haja ya mafundisho ya Kristo, mpaka kwanza mapokeo na kawaida zote za ovyo, viondoke katika mioyo yao.

### Hatari ya kushikilia mawazo

Hali hii ilithibitisha maanguko ya Wayahudi, nayo itathibitisha maanguko katika siku zetu. Watu wengi hukataa nuru itokayo kwa Baba wa nuru zote, kuliko kuyakataa mawazo yao wanayoshikilia. Hushikilia kusema kuwa wameokoka kwa njia fulani na kukamilisha jambo muhimu. Wasipoona njia yoyote, hukanusha wokovu uliomo.

Dini ya mfano haina upendo. Dini isiyo ya Kristo. Kufunga na kuomba kwa kujipendekeza ni chukizo mbele za Mungu. Matendo yetu wenyewe hayawezi kutuletea wokovu. Kwa watu wasioelewa hali yao ya kiroho jinsi ilivyo, ujumbe huwajia; "Maana wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja na kitu, nawe hujui kuwa u mnyonge, mtu wa kuhurumiwa, kipofu, na uko uchi. Kwa hiyo nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane." Ufunuo 3:17, 18. Imani na upendo ni dhahabu. Lakini kwa wengi wao dhahabu imefifia, utajiri wake umepotea. Haki ya Kristo ni vazi na chemchemi isiyoguswa.

"Dhabihu ya Mungu ni roho iliyovunjika, moyo iliyovunjika na kupondeka ee, Mungu hutaidharua." Zaburi 51:17. Ubinafsi unapoachwa, Bwana humfanya mtu kuwa kiumbe kipya. Kiriba kipya chaweza kuhifadhi divai mpya. Upendo wa Kristo unaweza kumpa mwamini maisha mapya. Ndani yake tabia ya Kristo itaonekana.

# 29 — Yesu Aiokoa Sabato [152]

Sabato ilitukuzwa tangu kuumbwa kwa dunia. Kama jinsi ilivyowekwa kwa ajili ya watu, mwanzo wake ni "wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu waliposhangilia kwa furaha." Ayubu 38:7. Nchi iliafikiana na mbingu." Mungu aliona kila kitu alichoumba, na tazama ni chema sana." Akastarehe siku ya furaha ya kumaliza kazi yake. Mwanzo 1:31.

Kwa kuwa Mungu alipumzika siku ya Sabato, aliitakasa, akaibariki." Mwanzo 2:3. Akaitenga kwa ajili ya kutumika kwa mambo matakatifu. Ilikuwa ukumbusho wa kuumba, na ukumbusho wa uwezo wake, na upendo wake.

Vitu vyote viliumbwa na Mwana wa Mungu. "Vitu vyote vilifanywa naye; na pasipo yeye hakikuumbwa kitu chochote kilichoumbwa." Yohana 1:3. Kwa kuwa Sabato ni ukumbusho wa uumbaji, hivyo ni ishara ya upendo wa uwezo wa Kristo.

Sabato huleta katika ushirika pamoja na Muumbaji. Katika nyimbo za ndege, katika kuhema kwa miti, na katika nyinbo za bahari, tunaweza kusikia sauti yake aliyenena na Adamu na Hawa katika Edeni. Nasi tunapoona uwezo wake ukionekana katika viumbe, tunapata farijiko, maana sauti iliyonena katika uumbaji na vitu vikaumbwa, ingali ikinena uhai katika roho zetu. "Aliyeamuru nuru kung'aa gizani, ili kutoa elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo."2 Wakorintho 4:6.

"Niangalieni wote, ncha zote za dunia mpate kuokoka, kwa maana ni Mimi Bwana, wala hakuna mwingine." Isaya 45:22. Huu ni ujumbe ulioandikwa katika viumbe ambavyo Sabato iliwekwa kuwa ukumbusho wake. Wakati Bwana alipowaambia Waisraeli kutunza Sabato, alisema: "Nazo zitakuwa ishara kati yangu na ninyi, ili mjue kuwa mimi ni Bwana Mungu wenu." Ezekiel 20:20.

Waisrael walijua Sabato kabla ya kufika Sinai. Njiani huko [153]
Sabato ilitunzwa. Sabato ilipovunjwa, Bwana alisema: "Mtakataa kushika sheria mpaka lini?" Kutoka 16:28. Sabato haikutolewa kwa ajili ya Waisraeli tu, bali kwa watu wote wa ulimwengu. Kama

sheria yote ya amri kumi ilivyo, haibadiliki wala kufutika. Kristo alisema kuhusu sheria hiyo. “Mpaka mbingu na nchi zitakapopita, nukta moja ya torati haitapita.” Mathayo 5:18. Kwa hiyo kadiri mbingu na nchi zitakavyodumu, Sabato itaendelea kuwa ishara ya uwezo wa Mungu wa kuumba. Edeni itakapotokea tena duniani, Sabato, itatukuzwa na wote walioko chini ya jua, maana ni siku ya Mungu ya kupumzika. “Toka Sabato hata Sabato, wenye mwili wote watakuja kuabudu mbele za Bwana.” Isaya 66:23.

### Ishara ya Mwongofu wa kweli

Ili kusudi kutunza Sabato kamili, watu hawana budi kuwa watakatifu wao wenyewe. Kwa imani lazima wawe wenye kushiriki haki ya Kristo. Sheria ilipotolewa kwa Waisraeli kwamba “Ikumbube siku ya Sabato uitakase.” Kutoka 20:6. Bwana alisema pia kuwa, “nanyi mtakuwa watakatifu kwangu.” Kutoka 22:31.

Jinsi Wayahudi walivyofarakana na Mungu, wala hawakupata haki ya Kristo kwa imani, Sabato ilipoteza umuhimu wake kwao. Shetani aliwaongoza kupotosha Sabato, kwa kuwa ni ishara ya uwezo wa Mungu. Viongozi wa Wayahudi waliiwekea Sabato mizigo mingi wakaifanya kuwa mzingo mzito kwa watu. Katika siku zile za Kristo ilionyesha tabia ya ufedhuli na ubinafsi kwa watunzaji wake badala ya tabia ya upendo wa baba wa mbinguni. Marabi walimwonyesha Mungu kama aliyewapa sheria isiyowezekana kushikwa, au kutiiwa. Waliwaongoza watu kumdhania Mungu kuwa asiyekuwa na huruma, na kuona kuwa Sabato ni ya ukatili. Ilikuwa kazi ya Yesu kusahihisha makosa haya. Kwa hiyo Yesu hakukubaliana na maongozi ya Marabi, ila aliendelea kuishika Sabato ya Mungu kwa kadiri ilivyo hasa.

### Fundisho la Sabato

Sabato moja Yesu na wanafunzi wake walipopita katika shamba la nafaka iliyoiva, wanafunzi walianza kuvunja masuke yake, na kuyapukuchua na kuyala. Katika siku nyingine ya juma jambo hili lisingekuwa kitu, maana ilikuwa kawaida kwa mtu yeyote anayepita katika shamba la matunda au shamba la ngano kula kitu cho chote
[154] atakacho. Soma Torati 23:23, 25. Lakini kufanya hivyo siku ya

Sabato ilikuwa haramu. Kupukuchua masuke ilihesabika kama kuvuna au kupura.

Wapelelezi mara moja walilalamika kwa Yesu wakisema: "Tazama wanafunzi wako wanatenda tendo lisilo halali kutenda siku ya Sabato." Marko 2:24.

Wakati Yesu aliposhitakiwa huko Bethesda kuwa amevunja Sabato, alijitetea kwa kujithibitishia kuwa yeye ni Mwana wa Mungu, akisema kuwa anatenda kazi kufuatana na mapenzi ya Mungu. Na sasa kwa kuwa wanafunzi wake wameshambuliwa, alitaja mfano katika Agano la Kale, katika siku ya Sabato wakati wale waliokuwa wakihudumu mbele za Mungu. Katika majibu ya Mwokozi, aliwakemea kwa kutojua maandiko: "Hamjasoma jinsi Daudi alivyofanya alipokuwa na njaa yeye na wale aliokuwa nao, jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu akatwaa mikate ya onyesho akala, ambayo si halali kwa mtu yeyote kuila isipokuwa kwa makuhani pake yao?" Akawaambia, Sabato ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato." Au hamjasoma katika sheria jinsi makuhani walivyo najinsi Sabato na wanajiona kuwa hawana hatia?" Nawaambia kuwa kitu kikuu zaidi kuliko hekalu. "Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato." Luka 6:3, 4; Marko 2:27, 28; Mathayo 12:5, 6, 8.

Kama ilikuwa haki kwa Daudi kula mikate iliyotengwa kwa ajili ya matumizi matakatifu, ilikuwa haki pia kwa wanafunzi kuvunja masuke ya ngano na kuyala siku ya Sabato. Makuhani pia walitenda kazi kubwa sana hekalu siku ya Sabato, kuliko siku nyingine. Kazi ya aina hiyo ikihusu biashara huwa dhambi, lakini walikuwa wakitenda mambo yanayohusu uwezo wa kuokoa Wakaristo, kwa hiyo kazi yao iliafikiana na Sabato.

Kusudi la kazi ya Mungu ulimwenguni ni kumwokoa mwanadamu. Kwa hiyo kitu ambacho kingefanywa kuhusiana na kazi hiyo ya ukombozi, kinapatana na sheria ya Mungu, na Sabato, wala si uvunjaji wa Sabato. Hivyo Yesu alikomesha majadiliano hayo kwa kutangaza kwamba, yeye ndiye "Bwana wa Sabato", yaani ndiye aliye juu ya yote na juu ya sheria. Mhukumu Mkuu huyu aliwaondolea wanafunzi lawama, kwamba wamevunja Sabato.

Yesu alisema kuwa, katika upofu wao, adui zake walikosea kujua makusudi ya Sabato. Yesu alisema: "Kama mngejua maana ya maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka, msingemhesabia

[155] makosa, mtu asiyekuwa na makosa.” Mathayo 12:7. Dini yao ya mfano tu, haiwezi kuleta uchaji kamili na upendo wa kweli, ambao huwa katika tabia za wenye kumwabudu Mungu kikweli.

### Yesu aliponya kwa makusudi siku ya Sabato

Dhabihu zenyewe kama zilivyo hazikuwa na maana yoyote. Zilikuwa njia tu sio mwisho. Kusudi la dhabihu ilikuwa ni kuwaelekeza watu kwa Mwokozi, ili kuwaleta watu wapatane na Mungu. Ni huduma ipendezayo kwa Mungu hasa. Huduma hii inapokosa kuwa na umuhimu wake, huwa machukizo kwa Mungu. Ndivyo ilivyo na Sabato pia. Mawazo ya watu yanapojawa na wasiwasi na mizigo yenye kuleta mashaka kunabaki tu kuishika kisheria makusudi ya Sabato hupotoshwa. Kuishika tu kisheria ilikuwa kukufuru.

Siku nyingine ya Sabato, Yesu aliona katika sinagogi mtu mmoja mwenye mkono umepooza. Mafarisayo walitazama kwa makini waone jinsi Yesu atakavyofanya. Mwokozi hakusita kuondoa ukuta wa mapokeo yao ya kuifanya Sabaato kuwa mwiko usiofaa.

Yesu alimwamuru yule mwenye dhiki kusimama, halafu aliuliza swali: “je ni halali kutenda mema siku ya Sabato, au kutenda mabaya, kuokoa maisha au kuangamiza?” Marko 3:4. Ilikuwa kawaida kwa Wayahudi kwamba, mtu anaposhindwa kutenda mema anapokuwa na nafasi ya kutenda hivyo, ilikuwa vibaya, kutojali kuokoa katika hali yao hasa. “Lakini wao walinyamaza kimya katika swali lake. Naye aliwaangalia kwa ghadhabu, hali akisikitika kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao, akasema: “Nyosha mkono wako.” Akanyosha mkono wake, akawa mzima” Fungu 5. Yesu alipoulizwa kuwa: “Ni halali kuponya siku ya Sabato?” Alijibu: “Ni mtu gani wa kwenu akiwa na kondoo aliyetumbukia shimoni siku ya Sabato asiyemwinua na kumtoa humo? Mtu ana thamani kubwa kiasi gani kuliko kondoo! Basi ni halali kutenda mema siku ya Sabato.” Mathayo 12:10-12.

### Wanyama walitunzwa sana

Wapelelezi hawakuthubutu kumjibu Kristo. Walijua kuwa alikuwa akinena yaliyo ya kweli. Wao badala ya kuvunja mapokeo,

walihiari kumwacha mtu ateseke ili kumsaidia mnyama awapo katika shida. Mnyama alitunzwa zaidi ya binadamu. Hiki ni kielelezo cha dini zote za uwongo. Huwa zina asili ya kibinadamu ambayo hujitukuza zaidi ya Mungu, lakini matokeo yake humdhili mtu zaidi ya mnyama. Kila mwalimu wa dini ya uongo na watu [156]
wake hudharau mahitaji ya wanadamu, masumbuko yao na haki zao. Injili humwinua binadamu juu zaidi kama mtu aliyenunuliwa kwa thamani kuu, yaani damu ya Kristo, nayo huwafundisha watu kuwajali binadamu na kuwashughulikia katika mahitaji yao na katika dhiki zao. Soma Isaya 13:12.

Mafarisayo walikuwa wakimwinda Kristo kwa chuki nyingi, wakati yeye alikuwa akiokoa maisha, na kuwaletea wafu furaha na burudiko. Je, ilikuwa halali kuua siku ya Sabato kama walivyokuwa wakipanga kufanya kuliko Yesu alivyoponya siku ya Sabato?

Katika kumponya mtu mwenye mkono uliopooza, Yesu aliilaumu kawaida ya Wayahudi, na kuiacha amri ya Mungu ikisimama kama Mungu alivyoamuru. Kristo alisema: "Ni halali kutenda mema siku ya Sabato." Yesu aliitukuza Sabato kwa njia ya kufyagilia mbali mapokeo yote, wakati wale waliokuwa wakilalamika kwa Yesu kuwa anavunja Sabato, wao wenyewe walikuwa wavunja Sabato ya Mungu.

Wale wanaosema kuwa Kristo aliiondoa Sabato, hudai kwamba alivunja Sabato na kuwahalalisha wanafunzi wake kuvunja pia. Hivyo hushika njia ya Wayahudi walianguka. Kufanya hivyo kutia tofauti kwa maneno ya Kristo, aliyesema, "Nimezishika amri za Baba yangu, na kukaa katika pendo lake." Yohana 15:10. Mwokozi, wala wafuasi wake hawakuivunja Sabato. Akiangalia watu ambao watamshitaki, alisema: "Nani kwenu anishuhudiaye kwamba nina dhambi?" Yohana 8:46.

"Sabato ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato." Amri kumi za Mungu, ambazo Sabato ni moja yao, Mungu aliwapa watu wake ili wapate mibaraka. Soma Torati 6:24. Wote wanaotunza "Sabato wasiinajisi", Bwana asema, "Watu hao nitawaleta katika mlima wangu mtakatifu. nitawafurahisha katika nyumba yangu ya sala." Isaya 56:6, 7.

"Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato." maana yote hii ilifanywa naye na pasipo Yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika." Yohana 1:3. Kwa kuwa Kristo alifanya vitu vyote,

alifanya na Sabato pia. Kwa ajili yake ilitengwa kando iwe ukumbusho wa uumbaji. Humtaja kuwa ni Mwumbaji na Mtakasaji. Sabato hueleza kuwa aliyeumba vyote ndiye Mkuu wa kanisa, na kwa ajili yake na uwezo wake twapatanishwa na Mungu. Asema: "Niliwapa Sabato zangu kuwa ishara kati yangu na wao, wapate kujua kuwa mimi Bwana Mungu niwatakasaye kuwafanya watakat-
[157] ifu." Ezekiel 20:12. Sabato ni ishara ya uwezo wa Kristo ututakasao. Nayo ni ishara kwa wote wanaotakaswa na Kristo.

Wote wanaopokea Sabato ni ishara ya uwezo wa uumbaji na ukombozi, itapendeza. Isaya 58:13, 14. Angalia Kristo ndani yake. Hupendeza kwake. Inapomkumbusha mpotevu Edeni iliyopotea, amani hiyo itarudishwa kwa njia ya Mwokozi. Kila kiumbe kitakariri mwito: "Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao, na wenye mzigo mizito, nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28.

# 30 — Awekea Mikono Mitume Kumi na Wawili [158]

"Ndipo alipanda mlimani, akawaita wale aliowataka, nao wakamjia. Naye akaweka kumi na wawili wawe pamoja naye, ili awatume waende kuhubiri."

Chini ya vivuli vya miti ya milimani, mbali kidogo na pwani ya ziwa la Galilaya, watu kumi na wawili waliitwa ili wapate kuwa mitume, na hapo ndipo tangazo la mlimani lilipotolewa. Katika kuwafunza wanafunzi wake Yesu aliamua kutoka katika ghasia na fujo ya mjini, akaenda mahali pa kimya, katika milima penye utulivu, ili apate kuwafundisha. na katika kazi yake yote, alikuwa akiwakusanya watu mahali pa wazi, katika majani kando ya milima, au kando ya ziwa mahali penye utulivu. Mahali kama hapo ndipo alikuwa akiwaongoza wasikilizaji kwenye viumbe vya asili, hapa angewageuza watu kwa yale mambo yaliyofanywa kwa mikono ya watu kwa yale ya asili. Watu waliweza kujifunza kukua na kuendelea kwa viumbe, na hapo walipata mafundisho ya hakika ya ukweli wa Mwenyezi.

Sasa hatua ya kwanza ilikuwa ikichukuliwa kupanga kanisa ambalo baada ya kuondoka kwa Kristo, litakuwa likimwakilisha katika ulimwengu. Hakuna mambo yenye gharama kubwa yaliyohitajika. Bali uzuri na utakatifu wa hali, ambayo watakuwa nayo milele wakiangalia uzuri wa uumbaji katika milima, mabonde, na bahari.

Yesu aliwaita wanafunzi wake ili awazoeze na kuwafunza ili baadaye awatume ulimwenguni kutangaza mambo yale waliyoyaona na kusikia kwake. Madaraka waliyopewa yalikuwa muhimu sana ambayo watu hawajapewa kama hayo. Madaraka yao yalikuwa ya pili kwa yale ya Kristo mwenyewe. Kazi yao ilikuwa kushirikiana na Mungu ili kuuokoa ulimwengu.

Kristo alijua tabia za watu ambao amewawekea mikono wawe [159]
mitume wake; udhaifu wao na makasoro yao yalikuwa wazi machoni mwake. Alijua hatari zilakazowakabili, kwa hiyo aliwahurumia sana. Kila mara aliwaombea wakiwa peke yao juu mlimani usiku kucha;

wakati wao walikuwa wamelala chini ya mlima. Asubuhi mapema alikuwa amewaendea tayari.

Yohana na Yakobo na Petro, pamoja na Filipo, Nathanael na Mathayo, walikuwa washiriki wa Kristo wa karibu sana, wakiwa watenda kazi wenye juhudi. Petro na Yakobo na Yohana walikuwa washiriki wa karibu zaidi kwa Kristo, wakiona miujiza yake na kusikia maneno yake. Mwokozi aliwapenda wote, lakini Yohana alikuwa mpendwa hasa. Alikuwa kijana zaidi na alikuwa na matumaini ya ujana zaidi. Alifungua moyo wake kwa Yesu kabisa. Hivyo alifadhiliwa sana na Yesu na kupokea mafundisho ya Mwokozi.

## Mwenye imani Haba

Filipo alikuwa mtu wa kwanza aliyepewa agizo na Yesu kusema, "Nifuate." Alikuwa amesikia Yohana akimtaja Yesu kuwa ni Mwana Kondoo wa Mungu. Alikuwa mtafuta ukweli hasa; ila alikuwa mwenye imani haba, kama imani yake ilivyoonyesha wakati alipomwita Nathanaeli. Ijapokuwa Kristo alitangazwa kwa sauti iliyotoka mbinguni kuwa ni Mwana wa Mungu, lakini kwa Filipo alikuwa "Yesu mwana wa Yusufu mtu wa Nazareti." Yohana 1:45. Tena wakati watu 5,000 walipolishwa, Filipo alionyesha imani haba. Swali Yesu alilomwuliza kwamba,

". . . Tununue mikate wapi, ili kuwalisha watu hawa ... ?" Lilikuwa la kumjaribu. Jibu la Filipo la kuonyesha imani haba, lilimsikitisha Kristo. Filipo alisema, "Mikate ya dinari mia mbili haitoshi kila mtu apate kidogo tu." Yohana 6:5, 7. Filipo alikuwa amemwona Yesu akifanya kazi, na kuona uwezo wake, walakini hakuwa na imani.

Wakati Wayunani walipomwuliza Filipo kuhusu Yesu, hakujishughulisha kuwaonyesha Mwokozi na kueleza habari zake kwao, ila alikwenda kumweleza Andrea. Tena wakati ule kabla ya kusulibishwa kwa Yesu maneno ya Filipo yalionyesha imani haba. Wakati Toma aliposema, "Bwana ... tutajuaje njia?" Mwokozi alijibu, "Mimi ndimi njia .... Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba yangu pia." Filipo alisema maneno yenye imani haba, kwamba "Bwana tuonyeshe Baba, yatutosha." Yohana 14:5-8.

Kinyume cha imani haba ya Filipo kulikuwa na imani kamili ya
[160] Nathanaeli. Nathanaeli alikuwa na imani ya kweli, siyo ya kuona

kwanza mambo, bali imani kwa mambo yasiyoonekana. Walakini Filipo alikuwa mwanafunzi katika shule ya Kristo, na Mwalimu ambaye ni wa mbinguni alivumiliana na kutoamini kwa Filipo. Roho Mtakatifu alipomwagwa kwa wanafunzi Filipo alifundisha kwa hakika kabisa kiasi cha kutubisha watu wasioamnini; ambao walimsikiliza.

Yesu alipokuwa akiwatayarisha wanafunzi ili wawekewe mikono ya uchungaji, mmoja ambaye hakuitwa alidai ili awe mmoja wao pia. Yuda Iskariote aliyejidai kuwa mmoja wa wafuasi wa Yesu, alikuja ili awe mmoja wao wa hawa wanaotayarishwa kuwekwa mikono. Kwa kujiunga na wanafunzi alikuwa akitamani kupata madaraka makubwa katika ufalme huo mpya. Alikuwa mtu mtaalamu sana, mwenye uwezo na akili sana. Wanafunzi walimshuhudia kwa Yesu, na kumtaka amkubali kuwa mwenzao, ambaye atamsaidia sana kazini. Kama Yesu angalimkataa Yuda wanafunzi wangalikuwa na mashaka juu ya Yesu. Walakini hali ya Yuda ingeonyesha hatari katika kazi ya Mungu, maana ingeleta kanuni za kidunia ambazo hazitakiwi katika kazi ya Mungu.

Walakini Yuda alijisikia kuwa katika hali ya kuongoa roho za watu kwa Mwokozi. Yesu asingalimkataa mtu huyu aliyejiingiza kuongoa roho. Mwokozi alisoma moyo wa Yuda; aliona uovu umo ndani yake, kama hatasaidiwa na Mungu, atazama. Katika kuunganika na mtu huyu, Yesu alimweka mahali panapofaa, siku kwa siku alimshirikisha na huduma yake isiyokuwa ya ubinafsi. Kama Yuda angefungua moyo wake kwa Kristo, angaliweza kuwa raia wa mbinguni.

[161] # 31 — Mahubiri Mlimani

Mara chache Kristo aliwafundisha wanafunzi wake peke yao. Kusudi lake lilikuwa kuwafundisha makutano ya watu wengi, maneno ya kuonya ya kusihi na ya kutia moyo, akitafuta kuwafaidia wale watakaokubaliana naye.

Mahubiri ya mlimani ijapokuwa yalitolewa kwa wanafunzi wake, yaliwafaa makutano. Baada ya kuwatia mikono wanafunzi, ambao ni mitume, Yesu alikwenda kando ya bahari. Asubuhi sana watu walianza kukusanyika. Waliposikia mambo makuu aliyotenda, walikuja kumsikiliza na kuponywa maradhi yao... uwezo ulikuwa ukimtoka wa kuwaponya wote. Marko 3:8; Luka 6:17-19.

Pwani nyembamba haikutosha watu wote hata kama wangalisimama, kwa hiyo Yesu aliketi chini kwenye majani, na watu wote pia waliketi chini kwenye majani.

Wanafunzi wake waliketi karibu naye wakitamani kusikiliza mafundisho yake, ambayo watawapelekea watu wa nchi zote ili kuwafundisha. Waliamini kuwa ufalme ulikuwa karibu kusimamishwa.

Makutano pia walijisikia hali hiyo hiyo. Watu walipokuwa wameketi majanini kando ya mlima, mawazo yao yalikuwa yakiwaza juu ya utukufu wa baadaye. Waandishi na Mafarisayo walikuwa wakitazamia wakati watakapojitawala na kuachana na Warumi ambao wanawachukia, na kufurahia fahari ya kujitawala katika enzi tukufu katika ulimwengu.

Wakulima na wavuvi masikini walitumaini kusikia kuwa watapata starehe mahali pengine kuliko wakati huu wanapoishi katika hali ya dhiki, katika vibanda vyao na kula chakula cha wasiwasi. Walitumaini kuwa Waisraeli watatukuzwa kuliko mataifa mengine
[162] ya dunia, maana wao ni taifa teule lililoteuliwa na Bwana, na Yerusalemu utainuliwa juu ya miji yote.

**Kristo alikatisha tamaa tumaini la ukuu wa duniani**

Katika mahubiri mlimani Kristo alitaka kufuta kazi iliyofanywa na walimu wa uongo, na kuonyesha ukweli wa ufalme wake. Bila kueleza jinsi ufalme wa mbinguni ulivyo, hakuwaambia wasikilizaji wake masharti ya kuuingia, akiwaacha wafikiri wenyewe jinsi ufalme huo ulivyo. Alisema: "Wa heri wanaofahamu umaskini wao wa kiroho, na wanatafuta kuponywa katika hali hiyo." Injili haisemi juu ya kiburi cha kiroho, bali kwa wanyenyekevu, wenye roho iliyopondeka.

Wenye moyo wa kiburi hushindana kuingia katika ufalme kwa nguvu na kwa matendo yao, lakini haki yetu na kufaa kwetu kuingia mbinguni hutokana na haki ya Kristo. Bwana hawezi kumfanyia mtu kitu cha kumsaidia, mpaka amejitolea kamili kwa Mungu, na kutawaliwa naye kamili. Ndipo anaweza kupokea kipawa ambacho Mungu huwapa watu. Mtu anayejisikia kuwa na haja, hatanyimwa chochote. Angalia Isaya 57:15.

"Wa heri wenye huzuni: maana watafarijika." Huzuni anayozungumzia sio ile ya kuhuzunikia jambo lililotukia kwa mtu, na kumfanya aomboleze. Mara nyingi sisi huhuzunika kwa ajili ya matokeo ya matendo maovu tuliyotenda. Lakini huzuni ya kweli huja kwa njia ya kazi ya Roho Mtakatifu afanyaye kazi ndani yetu, na kutudhihirishia ubaya wa dhambi hasa. Roho Mtakatifu hutufikisha chini ya msalaba. Hapo huona kuwa kila dhambi tutendayo humsulibisha Yesu kwa upya. Tunapomwangalia akiteseka msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, huhuzunika na kuacha kufuata njia za dhambi hizo. Huzuni hii humfunga mwenye huzuni na Mungu. Na machozi ya mwenye huzuni huwa kama matone ya mvua yanayotangulia nuru ya jua kuleta utakatifu. Na huo hutangaza furaha ya kudumu, itakayokuwa kama chemchemi katika moyo wa mtu. tazama Yeremia 3:12, 13; Isaya 61:3.

Wale wanaohuzunika kwa njia hiyo watafarijika. Kwa njia ya mateso na dhiki Mungu hutufunulia madahra yaliyomo katika tabia zetu, ambazo zapaswa kushindwa kwa neema yake. Mambo mabaya yaliyo katika tabia zetu, ambayo hatuyafahamu, Mungu hutufunulia. Na hapo sisi hupata mtihani kama tutafuata njia ya Mungu, au tutang'ang'ania tabia zetu ambazo ni za madhara. Tupatapo jaribu tusipoasi au kunung'unika tukiwa mikononi mwa Yesu, tutapita. [163]

Njia ya Mungu machoni mwa wanadamu huonekana kuwa giza, na isiyokuwa ya kupendeza. Lakini njia hiyo ndiyo ya huruma, na mayokwenda wokovuni.

Neno la Mungu kwa wenye huzuni ni: “Nitageuza huzuni zao kuwa furaha, nami nitawafariji.” Yeremia 31:13.

## Roho tulivu humtukuza Mungu

“Wa heri wenye upole”. Mambo magumu tunayopata yanaweza kupunguzwa kwa ajili ya upole uliofichika ndani ya Kristo. Tukiwa na unyenyekevu wa Bwana wetu, tutashinda, mapingamizi yote, na uchokozi wote. Mambo kama hayo hayataweza kuleta wasiwasi na giza katika moyo. Mtu anayeshindwa na mapingamizi ya kila namna hawezi kuwa na utulivu wa moyo, naye humwibia Mungu haki yake ya kudhihirisha tabia yake ndani ya mtu. Upole wa roho ni uwezo unaoleta ushindi kwa wafuasi wa Kristo.

Wale wanaoonesha roho ya upole ya Kristo, wanaweza kuonekana kwa watu wa dunia kama watu duni, wanaodharauliwa lakini mbele za Mungu ni wenye thamani sana. Maskini wa roho, wanyenyekevu wa roho, ambao kusudi lao kubwa ni kufanya mapenzi ya Mungu, watahesabika katika kundi ambalo limefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana Kondoo.

“Wa heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa” kule kujisikia kutofaa kwa mtu kutamfanya mtu awe na njaa kwa ajili ya haki. Wote wanaotamani kupata tabia sawa na ya Mungu watatosheka. Upendo utaufanya moyo wa mtu uchuchumilie mambo ya juu, na wala mtu hatakoma wala kuridhika na mambo hafifu yasiyotimilika.

Wenye rehema watarehemiwa, na wenye moyo safi watamwona Mungu.. Kila mawazo machafu hutia hali ya tamaa mbaya na kumfukuza Roho Mtakatifu. Bwana anaweza kumsamehe mwenye kutubu, walakini ingawa amesamehewa, roho yake imeharibiwa. Usemi wote mchafu, na mawazo yote machafu, lazima viepukwe na mtu anayetamani kufahamu mambo ya mbinguni, ambayo ni ukweli kamili.

Lakini maneno ya Kristo, yanaenda zaidi ya kuacha mawazo machafu tu, au kawaida nyingine zisizo safi, ambazo Wayahudu waliziepuka. Ubinafsi hutuzuia tusimwangalie Mungu. Tusipouacha

ubinafsi na kutafuta mambo ya ubinafsi, hatuwezi kumwelewa Mungu ambaye ni Pendo. Moyo usiokuwa na ubinafsi peke yake, na moyo mnyenyekevu unaotegemea maongezi ya Mungu, na moyo [164] wenye rehema, ndio utamwona Mungu. Kutoka 34:6.

“Wa heri wasuluhishi” Ulimwengu ni adui wa sheria ya Mungu. Wenye dhambi ni maadui wa Mwumbaji wao. Kwa hiyo matokeo yake huwa adui wao kwa wao. Mipango ya wanadamu itashindwa kuleta amani, kwa sababu mipango hiyo haitoki mioyoni. Uwezo peke yake unaoweza kuleta amani ni neema ya Kristo tu. Neema hii inapokaa moyoni, itafukuza maovu yote ya tamaa ya mambo ya ulimwengu inayochipuza mashindano na vita.

## Makutano walishangaa

Watu walikuwa wakidhani kuwa furaha huja kwa kuwa na vitu vingi vya dunia hii. Furaha hiyo hufuatana na heshima na fahari pia. Kwa hiyo ilipendeza sana mtu kuitwa “Rabi”, na kuheshimiwa kama mtaalamu na mwalimu wa dini. Lakini Yesu alisema kuwa heshima ya ulimwengu ndiyo yote mtu awezayo kupata. Uwezo ulikuwa katika maneno yake. Wengi walikirishwa kwamba hakika Mwalimu huyu aliongozwa na Roho wa Mungu.

Baada ya kueleza jinsi furaha ya kweli inayopatikana, Yesu alieleza wajibu wa wanafunzi wake, kama mitume. Alijua kuwa watashambuliwa na ujumbe wao utakataliwa. Wanyenyekevu na wapole walioyapokea maneno yake walitazamiwa kusingiziwa, kuteswa, kufungwa, na kuuawa, lakini iliwapasa kuvumilia mpaka mwisho, na kuendelea mbele.

“Wa heri wateswao kwa ajili ya haki, kwa maana ufalme wa mbinuni ni wao”. “Mheri ninyi watu watakapowashutumu na kuwaudhi, na kuwanenea kila neno baya kwa uongo kwa ajili yangu. Furahini na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kubwa mbinuni, maana ndiyo walivyowatesa manabii waliokuwa kabla yenu”

Ulimwengu hupenda dhambi na kuchukia haki, na ndiyo iliyokuwa sababu ya fujo waliyomfanyia Yesu. Nuru ya Kristo ilimulika mahali pote na kuondoa giza lote lililofunika dhambi zao, na matengenezo ya hakika yalionekana jinsi yanavyotakiwa. Wale waliomhitaji Roho Mtakatifu vita ilianza mioyoni mwao; na wale

waliong'ang'ania dhambi walianza kushindana na ukweli na walioufuata.

Hivyo wafuasi wa Kristo walishitakiwa kuwa ni wenye kuleta fujo kwa watu. Lakini ni kushirikiana na Mungu ndiko kulileta uadui kwa ulimwengu. Wao wanafuata njia ile iliyofuatwa na watu
[165] wema katika nchi. Kila aina ya jaribu wanalopata ni njia ya Mungu ya kuwatakasa. Kila shindano wanaloshindana huongeza furaha katika ushindi wao wa mwisho. Wakielewa mambo haya, majaribu yote wanayopata kwa ajili ya imani yao watayapokea kwa furaha, sio kwa malalamiko.

"Ninyi ni chumvi ya dunia" Hamwezi kuondoka katika nchi, ili kuepuka mateso. Hamna budi kuishi kati ya watu ili utamu wa upendo wa Mungu ndani yenu uweze kuwa kwao kama vile chumvi inavyohifadhi nchi isioze. Kama watumishi wa Mungu wangelihami-shwa kutoka nchini, dunia ingeachwa katika uharibifu. Waovu wanawiwa hapa duniani kwa mibaraka ya watu wa Mungu, ambao wanawadharau na kuwatesa. Lakini Wakristo wakiwa ni kwa jina tu, wala si kwa hakika, hufanana na chumvi iliyoharibika. Kwa kutomwakilisha Mungu vilivyo, huwa wabaya kuliko wasioamini.

"Ninyi ni nuru ya ulimwengu" Wokovu ni kama mwanga wa jua, unaenea katika ulimwengu wote.

Dini ya Biblia siyo ya kufunikwa ndani ya kitabu, au kufungiwa katika jengo la kanisa. Dini ni ya kutakasa maisha ya kila siku, na kujidhihirisha katika hali zote za kushirikiana na watu. Kanuni za haki lazima zihifadhiwe mioyoni mwa watu wote. Maisha ya unyofu, hali kamilifu na moyo mkarimu, ndiyo yanayoangazia ulimwengu, kama nuru ya ulimwengu.

Yesu alijua kuwa wapelelezi wako tayari kuchukua kila neno lake ambalo litawafaa kutimilizia kusudi lao. Hakusema jambo lolote kuhusu maagizo ya Mungu, ambalo linahusu imani. Kristo mwenyewe ameeleza mambo yahusuyo sheria ya Mungu, na sheria yakawaida. Hakuja kuharibu mafundisho yake mwenyewe. Wakati alipokataa mambo muhimu yaliyotolewa kwa Waebrania.

Maneno ya Mwokozu yalikuwa kama ni ya uzushi kwa Mafarisayo. Alipofagilia mbali takataka zilizochanganyikana na na ukweli, walidhani kuwa alikuwa akifagia ukweli wenyewe. Alisoma mawazo yao, na kuwajibu kwamba "Msidhani kuwa nalikuja kuondoa sheria, au manabii. Sikuja kutangua, bali kutimiza" Kazi yake

ilikuwa kuonyesha utakatifu wa sheria ambayo wao walisema kuwa ameivunja. Kama sheria ya Mungu imevunjwa au imetanguliwa, basi Kristo asingeliteseka kwa ajili ya maasi yetu. Alikuja kueleza uhusiano wa sheria na binadamu, na kuifikiliza katika maisha yake ya kuitii.

Utii huleta furaha. [166]

Mungu huwapenda wanadamu. Ili kusudi kutukingia tusikumbwe na matokeo ya uasi, amedhihirisha kanuni ya haki. Sheria inapopokewa katika Kristo, hutuinua juu ya uwezo wa tamaa ya asili na maelekeo yake, na hutuinua juu ya majaribu yaletayo dhambi. Mungu alitupa amri zake, ili tunapozitii tupate furaha.

Katika mlima wa Sinai Mungu alijijulisha mwenyewe jinsi utakatifu wake na tabia yake vilivyo, ili kwa kuona tofauti ilivyo wapate kuona jinsi walivyo wenye dhambi sheria ilitolewa ili kuwathibitishia dhambi, na kufunua haja yao ya kuhitaji Mwokozi. Kazi hii ingali ikifanyika vile vile. Roho Mtakatifu anapowafunulia wanadamu hitaji lao la damu ya Kristo yenye kutakasa na kuwahesabia haki, sheria bado ndiyo inatuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani. "Sheria ya Bwana ni kamilifu huiburudisha nafsi." Zaburi 19:7.

"Mpaka mbingu na nchi zitakapopita, yodi moja au nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie." Jua liwakalo, na nchi isimamayo imara ni mashahidi wa Mungu kwamba sheria yake ni ya milele. Hata kama mbingu na nchi zitapita, lakini sheria ya Mungu itadumu. Kawaida ya mfano, kwamba Yesu ni Mwana Kondoo wa Mungu, itapita wakati wa kifo cha Yesu, lakini amri za Mungu zitadumu kama kiti chake cha enzi kidumuvyo.

Maisha ya Mwokozi ya utii yalithibitisha kwamba sheria inaweza kushikwa na wanadamu, na ilionyesha uzuri wa tabia itakayokuzwa. Kwa upande mwingine, wale wanaovunja amri za Mungu, humsaidia Shetani anayedai kuwa sheria ya Mungu haiwezekani kushikwa. Kama wakikaribishwa huko mbinguni, wataleta manung uniko na uasi, na kuharibu uzuri wa ulimwengu. Hakuna mtu yeyote atakayevunja kanuni yoyote ya sheria atakayeingia katika ufalme wa mbinguni.

Siku zile Kristo alipokuwapo ulimwenguni udanganyifu mkuu wa watu ulikuwa kwamba, ukikubali tu dini kwa juu juu, utapata haki. Katika maisha yote ya kibinadamu kukubali dini ya juu juu tu

na kukariri kanuni za kweli hakukuleta wokovu kwa mtu yeyote, wa kuzaa matunda ya pasayo toba.

Matokeo ya kujua tu maneno ya dini peke yake huleta chuki kwa wale walio na imani ya kweli. Sura yenye giza zaidi katika historia ni ile inayohusu maasi makuu yaliyotokana na wenye dini. Mafarisayo walidhani kuwa wao ndio wakuu wa dini kuliko wengine wote ulimwenguni, lakini kujidai kwao kuliwaongoza mpaka wakamsulu-
[167] bisha Bwana wa utukufu. Watu wengi hujidai kuwa ni wenye dini, lakini dini yao hiyo isipowafanya kuwa waaminifu hasa, wenye utu wema, wavumilivu, wastahimili, wenye mawazo ya kimungu, huwa laana kwao tu, na kwa mivuto yao huwa balaa kwa ulimwengu.

## Kina na Upana wa Sheria ya Mungu

Yesu alizichukua amri moja moja na kuelezea kanuni zake jinsi zilivyo. Alisema kwamba mawazo mabaya, au mtazamo wa kutamani ni kuvunja amri ya Mungu. Kutenda jambo dogo tu ambalo si la haki ni kuvunja sheria. Mtu anayeruhusu chuki katika moyo wake, huwa ameweka miguu yake katika njia ya kuua.

Wayahudi walitunza roho za kulipa kisasi, yaani ovu kwa ovu. Katika hali yao ya kuwachukia Warumi, walikuwa wakitoa matusi ovyo ovyo, hali wamejizoeza kutenda amtendo maovu. Kuna mambo ya kutia uchungu ambayo huhalalishwa hata kwa wafuasi wa Kristo. Wanapoona kuwa jina la Mungu linadharauliwa, au wenye haki wakitendewa ukatili, hasira yao huchochewa. Hasira kama hizo si dhambi. Lakini uchungu na hasira za kawaida, lazima ziondolewe katika watu wanaoelekea mbinguni.

Mawazo ya Mungu kwa watoto wake ni ya juu mno kuliko mawazo ya kibinadamu yaliyo bora mno. "Mwe wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. Amri hii ni ahadi. Mpango wa ukombozi hutaka kuondolewa kabisa mikononi mwa Shetani. Kila mara Kristo humtenga kabisa mtu yule anayetubia dhambi zake. Amepanga kwamba Roho Mtakatifu atamjia kila mtu anayetubu, na kumtunza asifanye dhambi tena.

## Hakuna udhuru kwa majaribu

Majaribu ya Shetani hayawezi kufanyiwa udhuru. Hakuna udhuru kwa kutenda dhambi. Kila mtoto wa Mungu mwenye kutubu, lazima achuchumilie kuwa na hali ya kufanana na mtoto wa Mungu, akijivika hali ya hasira njema katika mambo yote.

Yesu aliishi maisha makamilifu alipokuwa hapa duniani kama mwanadamu, hivyo wafuasi wake nao wapaswa kuwa kama alivyokuwa. Yesu alifananishwa na ndugu zake katika mambo yote. Alikuwa na hali ya namna ilivyo kwetu sisi. Alishiriki mambo yetu ya kibinadamu, walakini bila kasoro yoyote. Alikuwa Mungu katika mwili, akiwa na tabia kama zetu. Kristo ndiye ile ngazi Yokobo aliyoiona katika ndoto ambayo kitako kilifika chini, na kilele chake kikifika juu mbinguni. Kama ngazi hiyo ingalishindwa kufika chini, tungalipotea. Lakini Kristo alitufikia mahali tulipo. Alitwaa hali [168]
yetu, akashinda, ili sisi tukitwaa hali yake tushinde pia. Akafanywa kuwa "mwili wa dhambi" (Warumi 8:3) lakini akaishi bila dhambi. Sasa anatuagiza kwa njia ya imani, tushike utukufu wa tabia ya Mungu, twapasa kuwa "wakamilifu kama Baba aliye mbinguni alivyo mkamilifu."

Yesu alikuwa ameonyesha kile ambacho ndiyo haki na alikuwa ameonyesha kuwa Mungu ndiye asili ya haki. Sasa aligeukia upande wa wajibu na shughuli zipasazo haki. Kitu cho chote kisifanyike chenye kuleta mvuto wa ubinafsi. Wasaidie maskini kwa stahili yao, wala si kujivutia hali ya ubinafsi, yaani kukusifu wewe. Katika maombi, zungumza na Mungu. Katika kufunga usiwe na roho ya kujionyesa kuwa wewe ni mtawa, umefunga, huo ni ubinafsi.

Huduma yo yote inayotendwa bila kuwa na ubinafsi ndani huwa na sifa kubwa mbele za Mungu. "Baba yenu wa mbinguni atakujaza kwa dhahiri." Katika maisha yetu tuishiyo tabia zetu hujengeka kwa neema ya Kristo. Hali ya Ukristo wa Yesu hupatikana ndani yetu, na sura ya Mungu huanza kuonekana kwetu. Watu wanaoenenda na kutenda kazi pamoja na Mungu hali ya mbinguni huwazunguka. Watu hawa ufalme wa Mungu umeanza ndani yao.

"Hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili." Dini ya Biblia haina mivuto mingi katika mchanganyiko; inaingia katika sehemu zote za maisha.

"Jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa nuru lakini jicho lako likiwa ovu, mwili wako wote utakuwa giza." Anayetamani kuijua kweli lazima awe tayari kuikubali kweli yote inayofunuliwa kwake. Kutangatanga na kushika kweli nusu nusu ni kuchagua njia ya makosa ni udanganyifu wa Shetani.

Kanuni za ulimwengu na kanuni za dini ya Mungu haziafikiani hata kidogo; ni kama rangi za upindi wa mvua. Kati ya kanuni hizo mbili, kanuni ya Mungu ni dhahiri kabisa. Sura ya Kristo hutofautiana na ya Shetani. Kanuni hizo hutofautiana kama mchana na usiku. Watu wale wanaoishi maisha ya Kristo, ndio watu wake.

Wote waliochagua kazi ya Mungu hustarehe katika ulinzi wake. Kristo alitaja juu ya ndege warukao na maua yaotayo na kusema: "Ninyi je, si bora kuliko vitu hivyo?" Ndege wadogo kama shorwe hutunzwa. Maua na majani hutunzwa na kulindwa na Baba wa mbinguni. Mwenyezi, ambaye ni Muumbaji, hujishughulisha na mambo madogo kama haya, na kuyafanya yatoe maua kama ya Sulemani. Je atamtunza mtu kiasi gani, ambaye alimwumba kwa sura yake, na
[169] utukufu wake. Kama vile jua hutoa nuru yake na kuing'azia maua madogo, ndivyo Mungu hutoa uzuri wake na kuwang'arizia watu, na kuwapa tabia yake.

Katika kitabu cha Mungu, maisha tunayoishi huwa na ukurasa wake wa pekee. Katika ukurasa huo huandikwa kila jambo la maisha yetu yote. Jambo kwa jambo, kubwa au dogo. Wana wa Mungu hawawezi kusahauliwa hata katika mawazo yake. "Kwa hiyo msisumbukie mambo ya kesho." Mungu hakuwafunulia watoto wake mambo yote ya maisha ya safari yao. Huwambia yale wanayoweza kukumbuka na kufanya. Yale wanayofunuliwa huhusu wakati huo tu.

"Msihukumu msije mkahukumiwa." Msijidhanie kuwa ninyi ni bora kuliko watu wengine, na kujifanya mahakimu wao. Hamwezi kuona makusudi ya matendo yao. Katika kuwalaumu, huwahukumu. Kwa njia hiyo hujiunga na Shetani; ambaye ni mshitaki wa ndugu. Tazama 2 Wakorintho 13:5; 1 Wakorintho 11:31.

Mti mwema huzaa matunda yaliyo mema. Vivyo hivyo matunda yanayozaliwa katika maisha hudhihirisha tabia ya mtu. Matendo mema hayawezi kununua wokovu, lakini huonyesha kuwa kuna imani ifanyayo kazi kwa upendo, nayo hutakasa moyo. Zawadi

haitolewi kwa ajili ya kazi bora tuliyofanya, walakini kwa kadiri ya kazi ya uaminifu iliyofanywa kwa neema ya Mungu.

Kristo aliweka kanuni ya ufalme wake. Ili kukaza' kufundisha aliongeza kielelezo. Haitoshi kusikiliza tu maneno yangu, kwa kuyatii mtayafanya kuwa asili ya tabia zenu. Mkijenga juu ya hadithi za wanadamu, nyumba zenu zitaanguka. Zitaangushwa na upepo wa majaribu, na matatizo vitazibomolea mbali. Lakini kanuni hii niliyowaonyesha itadumu, na nyumba zenu hazitaanguka. Nikuba lini, jengeni katika maneno yangu.

"Kila mtu asikiaye maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye hekima aliyejenga nyumba yake katika mwamba; mvua ikanyesha mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyumba hiyo isianguke, kwa sababu misingi yake imewekwa katika mwamba."

[170] ## 32 — Afisa wa Jeshi Aomba Msaada Kwa Ajili Mtumishi Wake

Kristo alikuwa na masikitiko kwa vile taifa lake mwenyewe lilikuwa likitaka kuona ishara ndipo likiri kuwa alikuwa Masihi Lakini alishangaa kwa kuwona akida akija kwake, wala si0 kumwomba aende nyumbani kwake ili akafanye mwujiza wa kuponya, ila alisema “Sema neno tu, na mtumishi wangu atapona.”

Mtumishi wa akida alikuwa na ugonjwa wa kupooza. naye alikuwa katika hali ya kufa. Baadhi ya watumishi wa Warumi walikuwa watumwa, ambao walikuwa wakinunuliwa na kuuzwa, na kutendewa ukatili mkubwa, hali wakidharauliwa. Lakini Akida huyu alikuwa akimtendea mtumishi wake kwa fadhili sana, kwa hiyo alikuwa akitamani apone. Aliamini kuwa Yesu aliweza kumponya Habari za Yesu alizosikia zilimpa tumaini Mrumi huyu alikubali kuwa dini ya Wayahudi ilikuwa bora zaidi kuhko dini yake. Alikuwa ameacha chuki iliyokuwapo kati ya Wayahudi na Warumi; naye aliwapenda Wayahudi. Katika mafundisho ya Kristo alipata kuu ambacho mtu huhitaji. Mambo vote ya kiroho aliyokuwa nayo yalikubaliana na maneno ya Mwokozi Lakini alijiona kuwa hastahili kufika mbele zake. Kwa hiyo aliwauhza wazee wa Kiyahudi wamwombee kuhusu mtumishi wake. Walikuwa wamezoeana na Mwalimu huyu Mkuu, kwa hiyo wangaliweza kujua iinsi ya kumfikia, na kumvutia. Yesu alipoingia Kapernaumu alikutana na kikundi cha wazee. Wakaeleza kuwa wanamjua, na wakasema kuwa yeye anastahili kutendewa fadhili; maana anaPenda taifa letu, naye ametujengea sinagogi.

Mara moja Yesu aliondoka kwenda kwa akida huyo. lakini kwa kusongwa na makutano ya watu, mwendo wake ulikuwa wa
[171] pole ppole. Akida akiwa na wasiwasi alimtumia ujumbe kwamba: “Bwana . . . sistahili wewe uingie nyumbani mwangu ” Lakini Mwokozi aliendelea na safari yake tu. Akida baadaye akimkaribia, alisema. Wala sistahili kuja mbele yako.” “Sema neno lako tu na mtumishi wangu atapona. Maana mimi pia ni mtu niliyewekwa chini

ya mamlaka, nina askan chini yangu, nikimwambia huyu "Nenda huenda. na huyu njoo, huja, na kwa mtumishi wangu, fanya hivi hufanya. Kama ninavyowakilisha serikali ya Kirumi, ndivyo hata wewe huwakiliksha uwezo wa Mwenyezi Mungu; na viumbe wote hutii amri zako. Unaweza kuag a ugonjwa ukaondoka, na utatii neno lako. Unaweza kuamuru watumishi wa mbinguni wakaleta nguvu za kuponya. "Sema neno tu, na mtumishi wangu atapona.

Yesu aliposikia hivyo, alistaajabu, akawageukia watu waliomfuata, akawaambia: "Amin nawaambieni, sijaona imani kubwa, katika Israeli." na kwa akida alisema, "Kama ulivyoamini, iwe hivyo kwako. Mtumishi wake akapona saa ile ile."

Katika upofu wao wa kuwa na haki yao wenyewe. Waahudi walimsifu akida kwa ajili ya wema aliowafanyia kama taifa. Lakini akida alijisema mwenyewe kuwa "hastahili." Hakutumainia wema wake. Alimwamini Kristo tu ambaye ni rafiki na Mwokozi wa wanadamu.

Wakati Shetani anakuambia ya kuwa u mwenye dhambi, mwambie kuwa Kristo alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi. Maombi tunayomwomba sasa huonyesha hali yetu ya kutoweza chochote, ambayo hufanya atusaidie kutoweza kwetu.

Mkononi mwangu hakuna bei ninayoleta
Msalabani mwako nashikilia

Wayahudi hawakuona kitu chochote cha kumtamani Yesu Lakini akida, ambaye alifundishwa kat a shule za kimizimu za Rumi, ambaye alionekana kutengwa na hali ya dini ya Kiyahudi mtu huyu alipata ni kamili, ambayo watoto wa Ibrahim hawakuijua. Nuru iwamulikiayo watu wanaokuja ulimwenguni (Soma Yohana 1:9) imeng'aria mtu huyu, naye ameuona utukutu wa Mwana wa Mungu. Kwa Yesu mtu huyu alikuwa mavuno maalum ya watu kutoka katika mataifa, kuja katika ufalme wake.

### Mtu mfu amefufuliwa

Zaidi ya maili ishirini kutoka Kapernaumu palikuwako na mji
wa Naimi, hapo Yesu alipumzika. watu walikuja kutoka katika njia [172]
yote, wakileta wagonjwa wao ili waponywe, na hapo wakitumaini kuwa Yesu atajidhihirisha kuwa ndiye Mfalme wa Israeli. Kundi

lenye furaha lilimfuata katika njia yote ipitayo miambani mpaka kwenye mji wa mlimani.

Walipokaribia waliona jeneza linachukua maiti kwenda makaburini. Katika jeneza mlikuwamo maiti. Watu walikuwa wakilia sana, kuonyesha masikitiko yao kwa mtu aliyekufa.

Maiti alikuwa mwana pekee wa mama yake, na mama huyo alikuwa mjane. Mama aliyefiwa alikuwa akifuatana na maiti mpaka makaburini. "Bwana alipomwona alimhurumia." Alipoendelea alimsogelea, akamwambia, "Usilie."

"Akaenda, akalishika jeneza." Kwa Yesu kugusa mtu mfu hakutamtia unajisi wowote. Waliolichukua jeneza wakasimama na kundi lote lililokuwa likilia likakusanyika likitumaini jambo fulani. Aliyekuwa akifukuza pepo alikuwako, je hata kifo pia kinashindwa na uwezo wake?

Alitamka maneno kwa sauti ya mamlaka, akisema: "Kijana, nakuagiza, Ondoka." Sauti hiyo ilipenya masikioni mwa mfu. Kijana akafungua macho. Yesu akamshika mkono, akamwinua, mama yake akamkumbatia kwa furaha. Makutano wakaangalia kwa mshangao, kana kwamba wako mbele za Mungu. Kisha wakamhimidi Mungu, wakisema: "Nabii Mkuu ametujia, na Mungu amewajia watu wake." Waliokuwa wakichukua jeneza wakarudi Naini kwa furaha kuu.

Aliyekuwa akisimama kwa mama aliyekuwa akilia huko Naini, huguswa na masikitiko yetu leo. Maneno yake leo yanafaa sana kama yalivyofaa kwa kijana wa Naini. Tazama Mathayo 28:18. Kwa watu wote wanaomwamini yeye ni Mwokozi yule yule aliye hai.

Kijana yule alirudishwa kuwa mzima katika nchi hii, akishindana na matatizo ya dunia na kupitia katika nguvu za mauti. Lakini Yesu hutufariji katika matatizo na huzuni za mauti kwa maneno haya: "Mimi ndimi aliyekuwa amekufa, nami sasa ni hai. tazama Mimi ni hai milele hata milele nami.. ninazo funguo za kuzimu na za mauti. Ufunuo 1:18.

Shetani hawezi kumshikilia mtu katika mauti ya kiroho, yule anayemshikilia Kristo kwa imani, na maneno yake yenye uwezo yakiwa moyoni mwake. "Amka wewe usinziaye, ufufuke katika wafu ..." Waefeso 5:14. Maneno ya Kristo yaliyomwamuru mtu wa kwanza akawa hai, yangali yanatoa uzima. Maneno ya Kristo kwa
[173] kijana yule, kwamba: "Kijana nakuagiza ondoka", yakampa kijana

wa Naini uzima, ndivyo ilivyo kwa maneno kwamba Inuka kutoka katika ufu, hutoa uzima kwa mtu anayeyapokea.

Roho wa yule aliyemfufua Yesu kutoka ufuni akikaa ndani yenu, yule aliyemfufua Kristo kutoka ufuni ataifufua miili yenu. Soma Warumi 8:11; 1 Wathesalonike 4:16, 17. Hayo ndiyo maneno yenye kutufariji sisi kwa

[174] # 33 — Jinsi Yesu Alivyojihusisha na Matatizo ya Jamaa

Watoto wa Yusufu walikuwa mbali sana na kazi ya Yesu, wala hawakumhurumia hata kidogo, wala kumsaidia. Habari za maisha yake na kazi yake viliwachukiza. Walisikia kuwa alikuwa akikesha usiku kucha akiomba, na kwamba wakati wa mchana alizungukwa na makutano ya watu, hata hakuwa na nafasi hata ya kupumzika, wala kula. Rafiki zake waliona kuwa atajichakaza mwenyewe kwa jinsi hiyo, wala hawakuweza kugeuza hali yake mbele ya Mafarisayo; na wengine waliona kuwa mambo yake yamezidi.

Ndungu zake waliona haya kwa ajili ya mashutumu yatokanayo na hali yake, akiwa jamaa yao. Waliona uchungu sana kwake kwa ajili ya masuto ya Mafarisayo. Lazima atakuwa amekoma kufanya kazi kwa jinsi hiyo. Walimshawishi Mariamu awaunge mkono kumlaumu, wakidhani kuwa upendo wake kwake utafaulu kumgeuza. Mafarisayo wamemlaumu mara nyingi kuwa:” .... Kwa nguvu za mkuu wa pepo atoa pepo” Mathayo 9:34. Kristo aliwaambia kuwa wale wanaompinga hawaelewi na tabia yake ya Uungu; kwa hiyo hawana budi kusamehewa. Kwa Msaada wa Roho Mtakatifu wataona makosa yao na kutubu. Lakini mtu anayekataa kazi ya Roho Mtakatifu hujiweka katika hali ambayo kutubu hakutamfikia. Watu wakimkataa Roho Mtakatifu kwa ukaidi, na kumtaja kuwa ni Shetani, huwa wamekata kiungo cha kuongea na Mungu.

Mafarisayo wenyewe hawakuyaamini malaumu waliyomlaumu Yesu. Wakuu hao walisikia sauti ya Roho mioyoni mwao ikiwashuhudia kuwa Yesu ndiye Mpakwa Mafuta wa Israeli. Mbele yake walijitambua kuwa wao si watakatifu, na walitamani haki ya kweli. Lakini baada ya kumkataa, ilionekana kuwa ni kujishusha
[175] kukubwa sana kumkubali kuwa ndiye Masihi. Kwa hiyo walishindana na kuyabishia mafundisho ya Mwokozi ili kuepukana na kumkiri kuwa ndiye Masihi. Hawakuweza kumzuia asitenda miujiza, ila walijitahidi kumnena vibaya isivyo haki. Hata hivyo Roho

wa Mungu wa kuwakirisha kwamba ni yeye Masihi, ilikuwa kati yao. Lakini wao walijaribu wawezavyo kujenga ukuta wa kutoamini.

Mungu hawezi kuwaacha watu wawe vipofu, na kuwafanya kuwa wagumu wa mioyo kiasi cha kutoweza kuona ukweli. Huwatumia nuru ili kuwaangaza waone makosa yao. Lakini wasipojali nuru hiyo macho yao hupofuka na mioyo yao huwa migumu kiasi cha kutatanika. Nuru moja isipojaliwa huleta giza fulani katika hali ya kiroho, na mtataniko wa hali ya kiroho huzidishwa. Giza la kiroho huongezeka, mpaka huwa giza kamili katika roho. Ndivyo ilivyokuwa kwa viongozi wa Mafarisayo katika taifa la Wayahudi. Wakaihesabu kazi ya Roho Mtakatifu kuwa ni kazi ya Shetani. Kwa kufanya hivyo walichagua njia ya udanganyifu, na hivyo wakajitia katika utawala wa Shetani.

Maneno yanayokaribiana na onyo la Kristo kuhusu kumtukana Roho Mtakatifu, ni yale ya usemi mbaya. Maneno ndiyo yanayoonyesha tabia ya mtu ilivyo. "Kinywa cha mtu huyanena yale yaujazayo moyo wake." Maneno yana uwezo wa kuonyesha tabia ya mtu. Mtu hupimwa kwa maneno anenayo. Mara nyingi maneno ya ubishi huongozwa na Shetani, husemwa tu bila kufikiriwa, lakini matokeo huonyesha mambo ya moyoni. Maneno yasemwayo katika utani hupitia hivyo bila kusahihishwa. Husemwa tu kwa namna hiyo.

Ni hatari kusema maneno ya mashaka, na kubishia maneno ya kweli, ya nuru. Maneno hafifu na yasiyo na adabu huhusiana na tabia ya mtu, nayo huonyesha mashaka na kutoamini. Mtu huendelea hivyo mpaka mwisho hukanusha hata yaliyo ya kweli. Yesu alisema: "Kila neno lisilo maana watu watakalonena, watatoa hesabu yake siku ya hukumu. Maana kwa maneno yako utapewa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa."

Kisha Yesu alitoa onyo kwa wale walioguswa na maneno yake, lakini hawakuchukua hatua yoyote. Pepo mchafu akimtoka mtu, huenda huko na huko, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate. Kisha husema, Nitarudi katika nyumba yangu ya zamani nilikotoka. Hurudi huko na kuikuta nyumba yako safi imefagiliwa. Halafu huchukua mashetani wengine saba walio waovu kuliko yeye nao huingia na kuishi humo."

Wengi katika siku za Kristo, kama walivyo leo, huwekwa huru [176]
kwa neema ya Mungu, kutokana na nguvu za mwovu. Hufurahia

upendo wa Mungu, kwamba Kristo atakaa ndani yao. Wakati roho wa mashetani akiwarudia pamoja na wengine saba walio waovu kuliko yeye, basi hutawaliwa na roho ya mashetani.

## Uwezo Mpya watawala

Wakati roho inapojitoa kwa Kristo, uwezo mpya hutawala moyo wake. Badiliko hupatikana ambalo mtu hawezi kulileta. Mtu anapojitoa kwa Kristo, Kristo huwa ngome yake hasa, iliyomsaidia kati fujo za ulimwengu; akiazimu kwamba hakuna mamlaka yatakajulikana kwake ila yake mwenyewe, yaani hakuna mtawala, ila yeye tu. Hivyo mtu anapolindwa na mbingu namna hiyo, huwa asiyewezekana kushindwa na mashambulio ya Shetani. Lakini tusipojitolea kamili kutawaliwa na Kristo, tutashindwa na mwovu. Sio lazima kwamba tuchague njia za Shetani ndipo atutawale, ila tu tusipojali kuunganika kabisa na utawala wa nuru, na kushiriki kikamilifu na wajumbe wa mbinguni, Shetani atafanya makao yake katika mioyo yetu. Ulinzi peke yake kwa majeshi maovu ni kumfanya Kristo awe na makao ya kudumu katika mioyo yetu, kwa njia ya imani ya kutaka haki yake. Tusipoambatanisha uhai wetu kwa Mungu hatutaweza kuzuia hali ya ubinafsi na majaribu ya kutenda dhambi. Kwa muda kitambo tunaweza kuacha mazoea yetu mabaya, lakini bila kujitoa kwa Kristo dakika kwa dakika, na kuendelea kushirikiana na Kristo, tutakuwa katika hali ya kushindwa na Shetani, na mwisho tutatenda apendavyo yeye. Hali ya mwisho ya mtu huyo itakuwa mbaya kuliko kwanza." Hivyo ndivyo itakuwa kwa kizazi hiki kiovu. Hakuna waliokuwa wakaidi zaidi ya wale waliokaidi mwito wa rehema. Onekano la kawaida la dhambi ya kumtukana Roho Mtakatifu ni kule kuzidi kukaidi mwito wa mbinguni wenye rehema wa kutubu.

Katika kumkataa Kristo, Wayahudi walitenda dhambi isiyosamehewa, na kwa kukataa mwito wa rehema, tunaweza kutenda dhambi ya namna ile ile. Tunamweka Bwana Yesu katika aibu mbele ya Shetani na mbele ya viumbe wote wa mbinguni; na katika malimwengu yote wakati tunapokataa ujumbe wake wa rehema badala yake hutega masikio yetu kusikiliza mambo yanayowavuta watu mbali na Kristo. Mtu yeyote afanyaye mambo kama hayo, hawezi

kupata msamaha wa dhambi zake, na mwisho hupoteza nia yote ya kupatanishwa na Mungu.

### Ndugu halisi wa Kristo [177]

Yesu alipokuwa akiwafundisha watu, wanafunzi wake walileta habari kwamba, mama yake na ndugu zake walikuwa huko nje, wakitaka kumwona. Lakini alimjibu mtu yule aliyempa habari: Mama yangu ni nani, na ndugu zangu ni nani? Akiwanyoshea mikono wanafunzi wake, alisema: "Hawa ndio mama zangu na ndugu zangu! Mtu yeyote afanyaye mapenzi ya Baba aliye mbinguni, ndiye ndugu yangu, na dada yangu na mama yangu."

Wote wanaompokea Yesu kwa imani huunganika naye kwa kiungo kinachozidi kile cha mwungano wa kijamaa cha kibinadamu. Waamini na watendaji wa mapenzi yake, yaani washikao neno lake, huwa na uhusiano zaidi kuliko mama wa kawaida wa hali ya kibinadamu. Ndugu zake wasingepata kitu zaidi kwake, isipokuwa wampokee Kristo kuwa Mwokozi wao.

Kutoamini kwao kutakuwa ni uchungu mkali sana unaowekwa kikombeni ukiandaliwa kwetu.

Uadui unaoandaliwa kwa wanadamu kwa ajili ya kupinga injili ulikuwa mchungu mkali katika maisha ya Yesu katika maisha ya kwao nyumbani. Ndugu zake walimtazamia kuwa mshauri wao. Waliona kuwa kama angalisema maneno yanayokubalika kwa Mafarisayo, angaliepukana na mabishano yasiyo ya lazima. Walifikiri kuwa alirukwa na akili kwa kujiweka katika haIi ya Uungu. Walijua kuwa Mafarisiyo walikuwa wakitafuta njia za kumshitaki, nao walidhani kuwa amewapatia njia za kutosha kumshitaki.

Hawakupima kazi aliyokuwa akifanya, wala hawakumhurumia katika matatizo yake. Mambo yake hayakujaliwa, wala yeye na maneno yake hayakujaliwa hata kidogo. Kwa hiyo alisikitishwa sana na hali yao; maana alieleweka vibaya, na kuumia vibaya sana.

Ndugu zake walithubutu kudhani kwamba wataweza kumfundisha ajue mambo ya kweli, Walimlaumu wazi katika mambo wasiyoyajua. Walidhani kuwa wanafanya mapenzi ya Mungu, kumbe hawakumwelewa hata.

Mambo haya yalifanya njia ya Yesu kuwa yenye miiba. Kwa hiyo maisha ya Yesu yalikuwa machungu huko kwao kwa watu wa

kwao; na ilikuwa afadhali kwenda mahali pengine ambapo mambo hayo hayakuonekana. Alipenda kwenda kwao Lazaro, Maria na Martha, mahali ambapo palikuwa na utulivu na upendo alipata burudiko. Walakini alipata burudiko mara nyingi alipokuwa peke yake akiongea na Baba yake.

[178] Watu walioitwa kufanya kazi kama ile ya Yesu ya matatizo, na kunenwa vibaya kwa ajili ya Kristo, katika nchi ya kwao wenyewe, watafarijika kwa kuwa Yesu naye alipambana na mambo ya jinsi hiyo. Anawaagiza wajiburudishe kwake na kwa Baba wa mbinguni.

Wanaompokea Kristo, hawawezi kuachwa kana kwamba ni yatima, wakabiliane na matatizo peke yao. Wao kama jamaa ya mbinguni, Yesu anawaagiza kumwita Baba yake kuwa Baba yao. Baba Mungu ana fadhili kubwa sana juu yao kuliko fadhili za baba wa dunia wanazoonyesha kwa watoto wao.

Wakati Mwebrania alipolazimika kujiuza kwa ajili ya umaskini, na kuwa mtumwa, jamaa wa karibu alipaswa kumkomboa. Tazama Mambo ya Walawi 25:25, 47-49; Ruth 2:20. Vivyo hivyo kazi ya kutukomboa humwangukia aliye wa jamaa yetu ya karibu. Kristo ndiye alikuwa jamaa yetu wa karibu. Amekuwa wa karibu zaidi kuliko baba, mama, ndugu, rafiki mpendwa yeyote. Bwana Yesu ni Mwokozi wetu. Sisi hatuwezi kufahamu upendo huo, lakini twaweza kujua kuwa ni wa kweli kwa njia ya maisha.

## 34 — Nira Yake ni Laini na Mzigo Wake ni Mwepesi [179]

“Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.” Mwokozi hakumwacha mtu yeyote nje bila kumshughulikia, kwa upendo na uangalizi. Huwaangalia wenye dhiki na wenye wasiwasi, watu ambao hawana matumaini yoyote, wala utulivu katika mioyo yao, naye huwaalika wamjie ili wapate pumziko kwake.

Huwaambia wenye kusumbuka kwamba: “Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu, maana mimi ni mpole, na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata pumziko mioyoni mwenu.”

Kwa maneno haya Kristo huwazungumzia watu wote wenye kujua na wasiojua pia, wote wenye kulemewa na mizigo, ambayo ni Kristo peke yake awezaye kuwatua. Mizigo mizito zaidi ni ile ya dhambi. Kama tukiachwa kuichukua sisi wenyewe, itatukandamiza na kutuseta na kutupondaponda. Lakini Kristo ambaye hana dhambi ametuchukulia. “Bwana ametwika maovu yetu sisi sote.” Isaya 53:6. Amechukua mizigo ya maovu yetu. Mizigo ya masikitiko yetu na maafa yetu pia amechukua.

Ndugu mkubwa wa jamaa yetu huishi milele katika kiti chake cha enzi. Anajua kabisa udhaifu wa wanadamu, maana aliupitia; mahitaji yetu, na haja zetu zote. Pia anajua uwezo wa majaribu, maana alijaribiwa katika mambo yote bila kutenda dhambi. Je, unajaribiwa? Atakuokoa. je, wewe ni dhaifu? Atakutia nguvu. Je, wewe hujui lolote? Atakuelimisha. Je, una majeraha? Atakuponya. “Atawaponya waliovunjika mioyo, na kuwaganga wenye majeraha.” Zaburi 147:3.

Kwamba matatizo yako ni makubwa kadiri gani, mwambie Bwana. Roho yako itatakasika kiasi cha kudumu. Njia itafunguliwa kwako kwa matatizo na matisho yote. Mzigo wako mzito utakuwa [180]
mwepesi zaidi wa kufurahisha. Pumziko Kristo ambalo hutolewa na Yesu, lina masharti, lakini limetajwa dhahiri. Wote waweza kulipata.

“Jitieni nira yangu.” Nira ni kitu cha huduma. Ng ombe hutiwa nira ili kutumika na ili watumike kwa urahisi na ufanisi. Kwa

kielelezo hicho Yesu hufundisha kuwa tumeitwa kwa utumishi. Kwa hiyo tunapaswa kuchukua nira yake.

Nira hiyo ni sheria za Mungu, ambazo zimeandikwa ndani ya mioyo. Humwunganisha mtenda kazi wa Mungu na mapenzi ya Mungu. Kama tungaliachwa kuenenda jinsi tupendavyo, tungelitumbukia katika mashimo ya Shetani. Kwa hiyo Mungu hutufunga katika mapenzi yake.

Nira ya kazi Kristo amekwisha kuichukua badala ya wanadamu. Alisema, "Nalishuka kutoka mbinguni siyo kufanya mapenzi yangu, ila kufanya mapenzi yake aliyenipeleka." Yoh. 6:38. Upendo kwa Mungu, juhudi kufanya mapenzi yake, na utukufu wake, na upendo kwa wanadamu waliopotea, ndivyo vilimleta Yesu duniani. Jambo hili ndilo lilikuwa likimlazimisha, katika maisha yake yote hapa duniani. Kanuni hii alituachia pia tuwe nayo.

## Kile Kinachotuchosha

Watu wengi wenye kuelemewa na mizigo ya masumbufu ya kila namna, huwa wanafanya kazi ya ulimwengu na kukubaliana na kanuni zake na njia zake. Hivyo maisha yao huwa ya matatizo tu wakati wote. Kwa kutamani mambo ya ulimwengu, hujeruhi hali zao, na kujiletea mizigo isiyo ya lazima; ambayo ni mizigo ya matatizo tu. Bwana wetu hutaka waondoe mizigo hii, ambayo ni kongwa la utumwa. Husema: "Nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi." Huwashauri kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki yake. Wasiwasi ni kipofu hauwezi kutambua mambo ya wakati ujao. Lakini kwa kila tatizo Yesu huwa ameandaa njia tayari ya unafuu. Baba yetu wa mbinguni anazo njia maelfu za kutusaidia; ambazo sisi hatuzijui. Wale wanaoifanya kazi ya Mungu na heshima yake kuwa kitu cha kwanza, wataona kuwa wasiwasi wao umetoweka, na kuna njia wazi safi iko mbele yao.

"Jifunzeni kwangu." Huo ndio usemi wa Yesu. Kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha." Tunapaswa kuingia katika skuli ya Kristo na kujifunza kwake. Wokovu
[181] ni mfululizo wa kujifunza mambo ya mbinguni; yaani mambo ya kiroho. Mafundisho haya ni kujikabidhi kwa Kristo kamili, kimawazo, kimazoea na kimatendo; yaani kuachana na kanuni za giza, ambazo huongozwa na Shetani.

Moyoni mwa Kristo kulikuwa na amani kamili. Hakupotoshwa na kusifiwa wala kudharauliwa. Kunenwa vema au kunenwa vibaya. Kutendwa vema au kutendwa vibaya. Katika mambo hayo yote, Yesu alikuwa na hali ile ile. Lakini wengi wa wafuasi wake huwa na hali ya wasiwasi na msukosuko moyoni, kwa sababu huogopa kumtegemea Mungu. Huwayawaya kwani hawajitoi kamili kwa Mungu. Walakini wasipojitoa kamili kwa Mungu hawawezi kupata utulivu na amani kamili.

Wakati tunapozaliwa kutoka juu, tutakuwa na nia ile ile iliyokuwa kwa Yesu. Ndipo hatutatafuta vyeo vya juu. Tutatamani kuketi miguuni mwa Yesu, na kujifunza kwake. Tutafahamu kuwa thamani ya kazi yetu, ni kadiri ya kumwagiza Roho Mtakatifu kwetu. Kumtegemea Mungu huleta utakatifu katika nia, ili kwamba katika uvumilivu tuokoe roho zetu.

## Jinsi Nira yake inavyorahisisha kazi

Nira huwekwa shingoni mwa dume la ng'ombe ili kurahisisha kazi ya kukokota mzigo. Ndivyo ilivyo na nira ya Kristo. Wakati mapenzi yetu yanapomezwa katika mapenzi ya Mungu, tutaona kuwa mzigo wa maisha huwa rahisi kubebeka. Mtu anayetembea katika njia ya Mungu na katika sheria zake, hutembea na Kristo, na katika upendo wake, roho kupata pumziko. Wakati Musa alipoomba kwamba, nionyeshe njia yako, ili nikujue wewe, Baba alimjibu, "Kuwako kwangu kutaenda pamoja nawe, na mimi nitakupa pumziko." Kutoka 33:14.

Watu wanaomchukua Kristo katika neno iake, na kujitoa kufuata anavyoagiza, watapata amani na burudiko. Hakuna kitu duniani kitakacho wahuzunisha, wakati Yesu atakapowafurahisha kwa kuwako kwake, "utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea;' katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini." Isaya 26:3.

Maisha yetu yaweza kuonekana kana wamba yana matatizo, lakini kadiri tunavyojitoa kwa Bwana mwenye hekima zote, atayarekebisha maisha yetu katika hali ifaayo, ambayo ni ya utukufu wake. Hali hiyo iliyo ya tabia yake ya utukufu, ndiyo itakayopokewa katika Paradiso ya Mungu.

Kwa njia ya Yesu tutakapoingia katika pumziko, mbingu huanzia hapa. Tunaitikia mwito wake, kwamba: "Njoni, mjifunze kwangu," [182]

na kwa njia hiyo tunaanza maisha ya umilele. Mbingu haikomi kuonekana kwa njia ya Kristo. Tunapomjua Mungu zaidi na zaidi, ndivyo tutazidi kuwa na furaha kuu. Kadiri tunavyotembea na Yesu katika maisha haya, tunaweza kujazwa na upendo wake, na kuridhika kwa kuwako kwake pamoja nasi. Mambo yote ˆawezayo kupokelewa na binadamu hapa, tutayapokea.

# 35 — Kutuliza Dhoruba [183]

Ilikuwa siku yenye shughuli nyingi siku hiyo. Kando ya bahari ya Galilaya, Yesu alikuwa amenena mfano wake wa kwanza, akieleza aina ya ufalme wake, na kusimamishwa kwake. Kazi yake aliifananisha na ile ya mpanzi wa mbegu. Maendeleo yake yakifanana na punje ya haradali, na pia matokeo ya chachu ndani ya unga. Mwisho wa kutengana baina ya wenye haki na waovu, aliwafananisha sawa na ngano na magugu, pamoja na juya la samaki. Fundisho muhimu pia alilifananisha sawa na hazina iliyositirika ndani ya shamba.

Wakati jioni ilipofika, makutano walikuwa bado yako pamoja naye, wakimsikiliza. Alikuwa amewahudumia kila siku bila kupata nafasi ya kula, na kupumzika. Na sasa jioni ilipofika alitafuta mahali pa faragha ili apumzike, maana alikuwa amechoka sana. Aliwaagiza wanafunzi wake wamfuate ng'ambo ya ziwa.

Baada ya kuwaaga makutano walimwingiza mashuani wakatweka. Lakini watu wengine, baadhi ya makutano, waliingia katika mashua ya kuvulia samaki iliyokuwa hapo pwani, wakamfuata, wakiwa na shauri ya. kumsikiliza.

Mwokozi akiwa amechoka na njaa pia, aliingia ndani ya mashua, chini akalala. Ziwa lilikuwa tulivu na bila upepo, lakini kwa ghafla mambo yalibadilika. Kukawa na giza, na mawingu, na tufani kubwa ikatokea, juu ya ziwa.

Mawimbi yalinguruma yakisukumwa na upepo mkali yakaingia ndani ya mashua, ikawa kivumbi. Hapo wavuvi mashujaa walipata taabu sana kukiongoza chombo chao. Juhudi yao haikufaulu. Wakakata tamaa ya kuokoa, maana waliona kuwa mashua yao inazidi kudidimia chini.

### Yesu alijali [184]

Wanafunzi wakishughulika katika kujitahidi kujiokoa, walisahau kuwa Yesu alikuwamo mashuani. Sasa wakiona kuwa kifo kinawa-

jia, walimkumbuka yule ambaye ndiye wokovu wao, ambaye ndiye aliyewaagiza kuvuka ng'ambo ya ziwa. Yeye ndilo tumaini lao tu. Wakaita: Bwana, Bwana! Lakini sauti zao zilififia kwa ajili ya ngurumo kuu ya tufani, na hawakusikia mtu akiwajibu. Wakashikwa na hofu na wasiwasi sana. Je, huyu anayefukuza pepo na magonjwa, hata na kifo, hana uwezo iuu ya tufani hii yenye hatari, wala hawezi kuwaokoa wanafunzi wake katika balaa hili? Je, ni kusema kuwa haiali?

Mara tena waliita, bila kujibiwa, ila tu ngurumo ya tufani. Ilivyoonekana ni kuwa wataangamia katika maji.

Ghafla umeme ukamulika katika giza, wakamwona Yesu akilala kwa utulivu, wala hana wasiwasi na kelele za tufani. Kwa mshangao wakasema: "Bwana, huom kuwa tuko katika kuangamia?"

Sauti za kilio chao zilimwamsha Yesu. Umeme ulipomulika walimwona, akiwa na utulivu wa mbinguni katika uso wake, na utulivu wa upendo ulionekana kwake, ndipo wakasema: "Bwana, tuokoe tunaangamia.

Hakuna kilio cha moyoni kilitolewa kisijibiwe kamwe. Wanafunzi waliposhika makasia yao kujaribu tena kuiisogeza, Yesu alisimama. Tufani ilipozidi hata kuwamwagia maji, aliinua mkono wake, akasema kwa bahari yenye fujo, "Tulia".

Mawimbi yalizama, mawingu mazito yalitoweka, na nyota zikaonekana ziking'aa. Mashua ikatulia juu ya maji ya bahari. Kisha Yesu aliuliza swali kwa masikitiko, "Mbona mliogopa? Hamna imani"? Wanafunzi wakawa kimya. Hofu na aibu ikawashika wenye mashua waliofuatana na Yesu. Tufani ilikuwa imeisukuma mashua karibu na pwani, na wote waliokuwemo mashuani waliona kuwa ni mwujiza. Watu wakanong'onezana, "Huyu ni mtu wa namna gani, hata upepo na bahari humtii?"

Yesu alipoamka kukabiliana na dhoruba, hakuwa na alama ya hofu, wala hakuwa na alama ya wasiwasi kwake. Lakini hakuwa katika mikono ya Mwenyezi. Hakuwa Bwana wa nchi na bahari na mbingu, aliyepumzika kwa utulivu Uwezo huo aliuacha. "Siwezi kufanya kufanya neno mwenyewe." Yohana 5:30. Alitegemea uwezo wa Baba Ilikuwa imani, imani kwa Mungu na upendo wake na uangalizi wake. Hapo ndipo Yesu alitulia. Uwezo wa neno lililotuliza
[185] bahari na dhoruba ulikuwa uwezo wa Mungu.

Vivyo hivyo na sisi yatulazimu kuegemea kwa uwezo wa Mwokozi wetu. Hofu ya wanafunzi ilitokana na kutokuwa na imani, walimsahau Yesu, na wakati walipomrudia na kumkumbuka, ndipo aliwasaidia.

Ni mara ngapi wakati tufani ya majaribu inapotukusanyikia hupigana nayo tukiwa peke yetu? Huzitegemea nguvu zetu mpaka tunapokuwa tayari kupotea, ndipo humkumbuka Yesu. Tunapomwita ili atuokoe, mwito wetu hauwezi kuwa kitu cha bure. Hawezi kushindwa kutupa msaada tunaouhitaji. Tunapokuwa na Mwokozi katika roho zetu, hatuwezi kuhofu kitu. Mwokozi atatutoa hatarini kwa njia anayoona kuwa inafaa.

Wokovu ni kama bahari iliyochafuka. soma Isaya 57:20. Dhambi imeharibu amani yetu. Tamaa mbaya katika roho zetu hakuna uwezo wa kibinadamu unaoweza kuzitawala. Hatuwezi kufanya chochote ili kuzishinda Ni sawa na wanalunzi walipokuwa wakisshindana na dhoruba, bila matumaini yoyote. Walakini hata kama tufam ya majaribu ni kubwa kiasi gani, wale wanaomlilia Yesu kwamba: "Bwana, tuokoe" watapata ukombozi Neema yake hunyamazisha tamaa zote, na katika upendo wake roho zetu hupumzika kwa utulivu. "Hutuliza dhoruba, ikiwa shwari, mawimbi yake yakanyamaza. Ndipo walipofurahi kwa kuwa yametulia, Zaburi 107:2930." "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia va Bwana wetu Yesu Kristo." Warumi 5:1.

Asubuhi na mapema mwokozi na rafiki zake, walilika Pwani. Miali ya jua ikamulika na kuleta uhai duniani Wahpofika pwam waliona kitu cha kutisha kuliko dhoruba ya usiku. Wenda wazimu wawili waliwakimbilia kana kwamba wanataka kuwararulia mbali. Watu hawa walikuwa na vipande vya minyororo vikining'inia mikononi mwao ambavyo walifungwa navyo, nao wamevikatia mbali. Miili yao ilikuwa imekatwa katwa, na ilikuwa ikitoka damu. Walikuwa wamekodoa macho yao, karibu kutoka mahali pake. Nywele zao zilikuwa matimutimu. Walikuwa na roho za mashetani, nao walionekana katika hali ya kutisha sana, kama wanyama wa mwituni wala si kama watu.

Wanafunzi walikimbia kwa hofu iliyowapata; lakini wao walimkabili Yesu. Yeye alikuwa akisimama pale wanafunzi wake walipomwacha. Yeye aliyetuliza dhoruba hakukimbia. Watu wale [186]
walikuwa wakitoa povu midomoni, nao walimkabili Yesu. Kristo

aliinua mkono ule ulioituliza dhoruba, na watu wale walisimama kitambo kidogo kutoka kwa Yesu. Kwa uwezo mkuu, yesu aliwaamuru mashetani wale watoke ndani ya watu hao. Maneno yake yalipenya mpaka katika akili za watu hao, ambazo zilikuwa zimevurugwa vibaya na mashetani. Walitambua kuwa yuko mtu awezaye kuwafungua kutoka katika janga hili la mashetani. Lakini walipofungua vinywa vyao ili kuomba msaada, mashetani ndio walisema ndani yao, nao walisema kwa nguvu: "Tuna nini nawe Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakusihi usinitese.

Yesu aliuliza, "Jina lako nani?" Jibu likaja: "Jina langu ni Legion, maana tu wengi." Mashetani walimsihi Yesu asiwatoe nchini. Kando ya mlima kulikuwako na kundi la nguruwe likijilisha. Mashetani walimwomba Yesu awaruhusu wawaingilie. Kwa ghafla kundi lote likakimbia kiwazimu mpaka ziwasni wakafa majini.

Mara moja mabadiliko yalitokea lwa watu waliokuwa wenye kichaa. Nuru ya kweli imemulika katika akili zao.Wakaona kama wenye akili kamili. Wakamtukuza Mungu kwa kuponywa kwao.

Kule gengeni walisha nguruwe waliona yote yaliyotokea, kwa hiyo wakakimbia mjini kueleza habari hizi kwa wenye nguruwe. Kwa hofu na kwa mshangao mji wote ukatoka kumjia Yesu. Wenye wazimu hao walikuwa tishio katika nchi. Hakuna mtu aliyepita mahali pao kwa usalama. Sasa watu hawa wamepona, wanamsikiliza Yesu, na kumtukuza Mungu kwa furaha. Kupotea kwa nguruwe kulionekana kuwa ni jambo muhimu kuliko kuponywa kwa watu hawa.

Wenye nguruwe walikuwa wakitaka mali za ddunia tu kuliko mali ya mbinguni. Yesu alitaka kuvunja choyo na upendo wa mali ili waweze kusikiliza maneno yake yenye uzima.

## Ushirikina ulikuza hofu

Maonekano ya ushirikina na matendo yake huleta hofu kwa watu. Madhara zaidi hutokea kwa watu hawa wakiwa miongoni mwao. Waliovuka ziwa pamoja na Yesu walisimulia jinsi dhoruba ilivyokuwa, na jinsi mawimbi yalivyotulizwa. Lakini maneno yao hayakuwa na hatari. Ila kwa kushikwa na hofu ya washirikina, walimwomba Yesu aende zake; naye aliingia mashuani akaondo mara moja, akaenda ng'ambo.

Watu wa Gergasa waliogopa sana wasipoteze mali yao ya kidunia, kwamba yule alilyemwangamiza mkuu wa giza, alionekana machoni pao kama ni jasusi. Kipawa cha mbinguni kilipigwa marufuku kwao. Kulikuwa na wengi ambao hawakulipokea neno la Yesu kwa kuogopa kufilisika katika mali zao. Maana kulitii, kungehitaji kuacha mali zao. Walikataa kumkaribisha kwa kuogopa kuwa kutahitajika gharama zaidi za kuwakaribisha. Walikataa neema yake, wakamfukuza, atoke kwao. [187]

Lakini wenye kuponywa mashetani walitaka kufuatana na Yesu, Mponya wao. Waliona kuwa kukaa na Yesu kutawaepusha na mashetani yaliyowasumbua. Yesu alipotaka kuingia mashuani wao waliandamana naye. Lakini Yesu aliwaambia waende nyumbani kwao, wakawaeleze watu wa kwao mambo makuu Bwana aliyowatendea.

Hapa walipewa kazi ya kufanya. Kwenda katika miji yao ya kimataifa wakawaeleze mibaraka waliyopata kutoka kwa Bwana. Ilikuwa vigumu sana kutengana na Yesu, ambaye ni Mponya wao. Kwa kuwa wametengana na watu wa kwao kwa siku nyingi sana, ilionekana kwao kuwa vigumu kutimiza kazi Yesu aliyowapa. Lakini mara ile Yesu alipotaja kazi yao, walikuwa tayaari kutii. Walikwenda katika Dekapoli yote, wakieleza mambo makuu Yesu aliyowafanyia, kwa kuwafungua kwa nguvu za mashetani. Katika k;klufanya kazi hiyo walipokea mibaraka mingi kuliko vile wangalikaa pamoja na Yesu. Kufanya kazi ya kueneza habari njema ya wokovu, hutuleta karibu na Mwokozi zaidi na zaidi.

Watu wawili walioondolewa mashetani walikuwa ndio wamisionari wa kwanza waliotumwa na Yesu kwenda kuhubiri injili huko Dekapoli. Watu hawa walimsikia Yesu akifundisha kwa muda mfupi sana. Lakini walikuwa na ushuhuda wa kuwaambia watu kuwa Yesu ndiye Masihi. Walisema kile walichojua, na kile walichoona, na kusikia; kuhusu uwezo wa Kristo. Haya ndiyo kila mtu anaweza kuyafanya kama ameguswa na upendo wa Mungu. Tazama 1 Yohana 1:1-3.

Tunapomfuata yesu hatua kwa hatua, tutakuwa na jambo la kusimulia katika maongozi yake maishani mwetu. Jinsi tulivyojaribu ahadi zake na kuziona ni za kweli. Huu ndio ushuhuda Bwana anatutaka tuutoe.

Ijapokuwa watu wa Gergesa hawakumpokea Yesu, hakuwaacha gizani. Hawakusikia maneno yake. Hawakujua lolote juu yake, kwa hiyo aliwatumia nuru kwa njia ya wale waliomkubali.

[188] Kuangamia kwa nguruwe kuliwaamsha watu wote kuliko kitu kinginecho, kumwelekea Kristo. Watu walioponywa walikubali kuwa mashahidi wa uwezo wake, wakiwa mfereji wa nuru yake, na wajumbe wa Mwana wa Mungu. Milango ilifunguka katika nchi nzima. Yesu aliporudi Dekapoli watu maelfu walisikia neno lake. Hata watenda maovu pia hutumika kutenda mema.

Wenda wazimu wa Gergesa, waliokuwa wakiishi mapangoni, katika kifungo; katika tamaa zisizozuilika, huonyesha mambo ambayo Shetani huwatendea watu wanaojitolea katika njia zake. Mivuto ya Shetani kila mara huelekea kutawala nia na mawazo ya watu ili watende mambo yasiyosemeka. Hutia giza katika fahamu na kuvuruga nia ya mtu. Watu wanapokataa mwaliko wa Mwokozi, huwa wamejitolea katika mambo ya Shetani Watu maelfu katika miji yao, kazini, kwenye biashara, na popote pale, hufanya mambo kama haya siku hizi. Kwa ajili ya mambo haya, leo uasi umezidi duniani, na ufedhuli wa kila namna unawakumba watu. Shetani huwapeleka watu katika ubaya zaidi na zaidi, mpaka wameharibika kabisa kabisa. Usalama wa pekee ni kukaa pamoja na Yesu. Shetani amejionyesha mbele za malaika kuwa ni adui wa wanadamu, na mharibu wao. Na Yesu ni rafiki na Mwokozi wao.

Mungu ametuita tuwe, washiriki wa sura ya Mwana wake. Waarumi 8:29. Hata mtu aliyeazama na kuharibiwa na Shetani, katika Kristo, anaweza kuwa mtumishi wa haki, na aweza kutumiwa kwenda "Kutangaza mambo makuu ambayo Bwana amekufanyia."

# 36 — Mguso wa Imani [189]

Yesu aliporudi upande wa Magharibi wa ziwa kutoka Gergesa, aliwakuta makutano yamekusanyika wakimngojea. Alikaa pwani muda kitambo, akiwafundisha watu na kuponya maradhi yao. Kisha akaenda nyumbani kwa Lawi Mathayo ili kuhudhuria katika karamu. Hapo Yairo mkuu wa sinagogi alikutana na Yesu. Akiwa na masikitiko makubwa, alimwambia, "Binti yangu yumo katika hali ya kufa. Nakuomba uje uweke mkono wako juu yake ili apone; naye aishi."

Yesu akaondoka mara moja kwenda kwa Yairo. Wanafunzi wake walistaajabu kwa ukubali wake wa kwenda kwa Rabi huyu, walakini walifuatana na Mwalimu wao, na kundi la watu pia. Yesu na wanafunzi wake waliendelea pole pole sana, maana makutano walikuwa wakimsonga pande zote. Baba wa mgonjwa alikuwa na wasiwasi kwa kusimama mara kwa mara kwa Yesu ili kuwasaidia wenye dhiki, au kuwafariji wenye mashaka.

Wakati walipokuwa wangali njiani, mjumbe alifika na kutoa habari kuwa binti wa Yairo amekwisha kufariki. Yesu alisikia hivyo, akasema: "Usiogope, amini tu, binti yako atapona."

Basi wakaenda kwa haraka mpaka nyumbani kwa mkuu huyo. Waombolezaji walikuwako tayari wamgjaza mji na makelel. Yesu alijaribu kuwayama-zisha, akisema: "Mbona mnafanya ghasia hiVi? Msichana hakufa, ila amelala." Walichukizwa kwa maneno ya mgeni huyu. Wamemwona kijana akifa wazi. Yesu alipotaka waondoke wote, aliwachukua babaye na mamaye, pamoja na Petro, Yakobo na Yohana, wakaingia pamoja katika chumba alimolala marehemu.

Yesu alikaribia kitanda cha maiti, akaukumbatia mkono wake kama deaturi yao, akasema: "Msichana, nakauagiza ondoka." [190]

Akaondoka mara moja kwa kutetemeka, akapita katika watu wenye kushangaa, macho yake yamekodolewa sawa na mtu atokaye usingizini, akiangaliwa kwa mshangao mkubwa na watu wote waliokuwa hapo. Wazazi wake wakamkumbatia kwa furaha isiyosemeka.

Walipokuwa njiani wakienda kwa mkuu huyu, Yesu alikutana na mwanamke maskini, ambaye alikuwa amesumbuliwa na ugonjwa kwa muda wa miaka kumi na miwili. Alikuwa ametumia mali yake yote kwa waganga bila kupona. Lakini aliposikia kuwa kristo yuko, akawa na matumaini. Kama angemfikia tu angepona. Kwa shida akajikokota pole polae mpaka pwana. Yesu alipokuwa akifundisha watu, akajaribu kumsogelea, asiweze. Akamfuata katika nyumba ya Lawi Mathayo, lakini hata huko hakuweza kumfikia kwa asababu ya makutano. Alikuwa katika kukata tamaa, wakati Yesu aliposogea karibu naye.

Alikuwa karibu na Mganga Mkuu! Lakini kwa ajili ya ghasia nyingi na fujo kubwa, hakuweza kusema naye, wala kutazamana naye. Akiwa na hofu na wasiwasi wa kutokubaliana naye na kumweleza hali ya matatizo yake, alijisogeza kuelekea kwake, huku akijisemea mwenyewa: “Nikimgusa pindo la vazi lake, nitapona.” Yesu alipokuwa akipita, mwanamke huyu alinyosha mkono wake, akaweza kugusa upindo wa vazi lake. Katika mguso huo, ndipo alipoweka tumaini lake lote. Wakati huo huo udhaifu wake na ugonjwa wake ukapona kabisa.

Akajaribu kuondoka katika mkutano huo kwa furaha ya moyo wake, lakini wakati huo huo Yesu alisimama. Akiangalia huku na huku, aliuliza kwa sauti ya kusikika: “Nani amenigusa?” Swali hilo lilionekana kuwa ni swali la kigeni, maana alikuwa akisongwa-songwa na makutano pande zote.

Petro aliyekuwa tayari kusema, alisema: “Bwana makutano yanakusonga-songa, nawe wauliza: “Nani amenigusa?” Yesu alisema, “Maana naona nguvu zimenitoka”. Mwokozi aliweza kutambua mguso wa imani, na miguso-guso tu ya kawaida. Mguso wa imani hauwezi kupita ovyo tu. Angesema mwanamke huyu maneno ya faraja yataka yodumu mpaka mwisho wa dunia.

Akiwaangalia watu, Yesu aliweza kutambua yule aliyemgusa. Alipoona kuwa amefahamiwa, mwanamke alijitokeza wazi, akaja akitetemeka, akaeleza habari za ugonjwa wake, na jinsi alivyopata waokovu kwa Yesu. Ndipo Yesu akasema. “Binti.... Imani yako
[191] imekupnya, nenda zako kwa amani.” Hakumpa nafasi ya kueleza kwamba kuponywa kwake kumetokana na mambo ya ushirikina ya kugusa nguo na kupata uwezo wa kupona kimwujiza. Imani kamili ya kutegemea uwezo wa Mungu ndiyo imemponya.

## Imani hai huponya

Kuzungumzia dini kwa njia ya bahati nasibu tu, kuomba vivi hivi bila kusikia haja rohoni, ni kazi bure. Imani ya juu juu ambayo ni ya jina tu, inayomtaja kristo kuwa ni Mwokozi wa ulimwengu basi, haiwezi kuleta uhai wa roho ya mtu. Imani siyo elimu ya kujua kawaida za dini tu, wala haitoshi kusema kuwa namwamini Yesu Kristo. Yatupasa tumwamini na kumtegemea. Imani ya kweli ni hali ya kazi ya maagano ya lweli ya muungano kati ya Mungu na mtu. Kuwa na uhusiano halisi kati ya Mungu na sisi. Imani ya kweli ni kutumaini kwa kweli, kunakofanya ushindi katika maisha ya mtu.

Baada ya kumponya mwanamke yule, Yesu alitaka akiri mibaraka aliyopokea. Kipaji kinachotolewa na injili si cha siri. Ungamo letu la uaminifu wake ni chombo cha mbinguni cha kumdhihirisha Kristo ulimwenguni. Mambo muhimu katika dini yetu ni ule uaminifu wetu wa kweli katika kanuni za Mungu. Isaya 43:12. Ukubali wa neema yake unapoungwa na hali yetu ya kikristo katika maisha yetu, huwa uwezo unaoleta wokovu kwa watu.

Watu wenye ukoma kumi walipomjia Yesu wakitaka kuponywa, waliponywa. Lakini ni mtu mmoja tu aliyerudi kushukuru. Ni watu wangapi leo hufanya mambo kama hayo? Bwana humponya mgonjwa, huwatoa watu katika hatari, huwaagiza malaika zake wawaepushe watu na hali za lika namna, na kuwalinda na uharibifu wa maradhi, (Zaburi 91:6); ni hivyo hawajali upendo huo ulio mkuu. Kwa kutokuwa na shukrani hufunga mioyo yao isiione neema ya Mungu. Ni kwa ajili ya faida yetu tu, kulinda vipawa vya Mungu anavyotupatia. Hivyo imani ni nguvu inayoimarishwa. Basi tukumbuke upendo wa Mungu na fadhili zake kwetu. Tunapojikumbusha fadhili za Mungu, na jinsi anavyotntendea, husema: “Nimrudishie Bwana nini, kwa ukarimu wake wote alionitendea?” Zaburi 116:1.

[192] ## 37 — Wainjilisti wa Kwanza

Mitume walifuatana na Yesu wakitembea kwa miguu katika nchi yote ya Galilaya. Walikuwa wakiongea na kufanya kazi pamoja na Mwana wa Mungu, huku wakijizoeza jinsi ya kuwahudumia wanadamu. Yesu alipokuwa akiwashughulikia mkutano, wanafunzi nao walikuwa wakisaidia kumpunguzia Yesu mzigo wa kazi. Waliwasaidia walemavu kuwaleta kwa Yesu, na kuwafariji wote. Waliona watu wenye kupenda maneno ya Mungu, na wakawasaidia kutatua matatizo waliyokuwa nayo kuhusu maandiko matakatifu.

Walakini walihitaji mazoea ya kufanya kazi peke yao. Pia walihitaji mafundisho zaidi kutoka kwa Yesu. Sasa badala ya kukaa pamoja nao na kuwaongoza katika mambo mbalimbali, Yesu aliwatuma ili wakajizoeze kufanya kazi peke yao kama wajumbe wa Injili.

Kila mara wanafunzi waliona matatizo ya kukabiliana na Mafarisayo na makuhani, wakati walipowafundisha, na mara nyingi walimletea Yesu matatizo hayo. Yesu alikuwa amewaimarisha katika neno la Mungu, na alikuwa amewaweka mbali na mambo ya mapokeo yasiyokuwa na msingi. Alipowatenga mbali na yeye iliwapasa kujitegemea katika mambo yote, wakisimama katika ukweli wa neno la Mungu peke yake.

Aliwatuma waende katika miji yote, wakiwa wawili wawili. Hivyo walitiana nguvu na kuomba pamoja katika mambo yote.

Kazi ya Uinjilisti ingefaulu zaidi kama mpango huu ungalifuatwa.

Wanafunzi hawakupaswa kuingia katika mabishano kwamba Yesu ni Masihi, au la. Lakini kwa jina lake wataponya wagonjwa,
[193] watatakasa wenye ukoma, watafufua wafu, watafukuza pepo. Waliagizwa: "Mmepata bure, toeni bure."

Yesu alitumia wakati mwingi kuponya awagonjwa kuliko kuhubiri. Popote alipoenda furaha yake ilikuwa afya. Sauti yake ndiyo iliyotakiwa kusikiwa zaidi ya yote. Jina lake ndilo lililotakiwa ulimwenguni Uso wake ndio uliofurahiwa zaidi. Alipokuwa akipita

katika miji na vijijini alikuwa sawa na mkondo wa maji yenye kuleta furaha na uhai.

Wafuasi wa Kristo wapaswa kufanya kama vile yeye alivyofanya. Inatupasa kuwalisha wenye njaa, kuwafariji wenye dhiki, na kuwapa matumaini wale wasiokuwa na matumaini. Upendo wa Kristo ukionekana katika kazi yetu isiyokuwa na ubinafsi, itafaulu kabisa kuwaongoa wenye dhambi kuliko upanga, au mahakama ya hakimu yanavyoweza kufanya. Roho zitakuwa tayari chini ya upendo wa kikristo kuliko kitu kinginecho. Mungu anataka kuwa Mfariji Mkuu kwa watu kwa njia ya watumishi wake; ili ulimwengu uone upya ambavyo haujaona hivyo.

Katika safari ya kwanza ya wanafunzi kwenda kama wahubiri, walikwenda kwa "Kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." Kama wayahudi wanagalilipokea neno la Mungu, angaliwafanya kuwa wajumbe wake kati ya watu wa mataifa. Kwa hiyo wao ndio walikuwa watu wa kwanza kupelekewa ujumbe huu.

Katika safari hii ya kwanza wanafunzi walikwenda pale ambapo Yesu alikuwa ameshafika; na kufanya urafiki na watu. Kwa hiyo matayarisho kwa safari hiyo yalikuwa rahisi tu. Hawakupaswa kuwa na mavazi raswmi yanayovaliwa na walimu wa dini, wala hawakupaswa kuwa na mavazi ya pekee ya kuwapambanua kati ya watu wa kawaida. Wala haikuwapsa kukusanya watu kwa ajili ya mikutano yao. Kazi yao ilikuwa kuingia nyumba kwa nyumba. Kila mahali iliwapasa kupokea makaribisho ya wenyeji kama Kristo angalikuwako na kukubali. Watatoa salamu ya kawaida inayotolewa kwamba." . . . Amani iwemo nyumbani humu." Luka 10:5. Nyumba hii itabarikiwa kwa njia ya maombi, na nyimbo zao za kusifu, pamoja na kufungua neno la Mungu na kulisoma humo. Ujumbe wao, ambao watauchukua ni neno la uzima, na matokeo ya watu wa nyumba hiyo, hutegemea kulipokea au kulikataa neno hilo. Soma Mathayo 10:14, 15.

Yesu alisema: "Angalieni nawatuma kama kondoo kati ya mbwa wa mwiatu; kwa hiyo iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua." Kristo hakuondoa hata neno moja la kweli, ila [194]
alisema neno la ukweli katika upendo. Hakuwa mkaidi hata kidogo; wala hakumkasirisha mtu yeyote. Hakuulaumu udhaifu wa mtu yeyote. Aliukemea unafiki na uovu bila kuogopa. Lakini alikemea uovu kwa machozi. Kila mtu alikuwa wa thamani kwaka.

Watumishi wa Kristo wanahitajika kumkaribia Mungu sana, wasije wakatoa maneno yasiyotakiwa wakati wanapokemea uovu, yakaleta madhara. Watumishi wa Mungu inawapasa kukaza macho yao kwa upendo wa Kristo. Ndipo atatoa injili kwa hekima ya Mungu. Roho ya mtu ambayo inahifadhika na kutunzwa kwa hekima itatoa maneno yenye busara, ambayo hayawezi kubishiwa.

### Lazima tukabiliane na upinzani

Yesu akiendelea na mafundisho kwa wanafunzi wake, alisema: "Jihadharini na wanadamu." Wasingaliwategemea watu ambao hawamjui Mungu, na kutafuta mashauri kwao, maana kufanya hivi kungewapa watumishi wa Shetani nafasi ya kuwaingilia. Mavumbuzi ya wanadamu kila mara huwa kunyume cha kazi ya Mungu, na mipango yake. Watumishi wa Mungu wanapotegemea mashahauri ya watu na mipango yao, humdharau Mungu kabisa, na kuisaliti kazi ya Injili, wasipomtegemea roho Mtakatifu awaongoze.

"Watawapeleka mabarazani, . . . nao watawakokota mbele ya maliwali na mbele ya wafalme, kwa ajili yangu, ili kuwa ushuhuda wangu, na mbele ya watu wa mataifa. Watumishi wa Kristo wataletwa mbele ya wakuu wa dunia hii, ambao pasipo mambo haya wasingalisikia neno la Mungu. Wanaposikia mambo ya uongo kuhusu kazi ya watumishi wa Mungu, na imani ya wanafunzi wa Kristo, njia ya pekee ya kujua uhakika wa mambo, ni kuwatia majaribuni wafuasi wa Mungu kwa ajili ya imani yao. Yesu alisema. "Mtapewa katika saa hiyo mambo mtakayosema. Maana si ninyi msemao, bali roho wa Baba yenu ndiye asemaye ndani yenu." Wale wanaoikataa kweli ya Mungu watainuka na kuwashitaki wanafunzi wa Yesu. Lakini watu wa Mungu wanapasea kuwa na roho ya upole kama Bwana wao alivyokuwa. Hivyo watawala wataona tofauti baina ya watumishi wa Shetani, na wajumbe wa kristo.

Wafuasi wa Kristo wasingetayarisha usemi wao watakaosema, wanapofikishwa katika majaribu. Robo Mtakatifu atawaongoza jinsi ya kusema ukweli utakiwao. maarifa yaliyopatikana kwa kujifunza
[195] ukweli halisi katika maandili matakatifu, utawaka na kukumbukwa katika mawazo yao. Lakini kama mtu yeyote ambaye hakujali kujishughulisha na maneno ya Kristo, asidhani kuwa Roho Mtakatifu atamletea kumbukumbu yoyote katika mawazo yake.

## Tutafanyaje majaribu yatujiapo

Wanafunzi wa Kristo wangesalitiwa hata na watu wajamaa zao. “Mtachukiwa na watu waote kwa ajii ya jina langu; lakini atakayestahimili mpaka mwisho, ndiye atakayeokoka.” Lakini aliwaagiza kwamba wasijiweke wenyewe katika mateso bila sababu. Yeye mwenyewe kila mara aliacha kazi katika sehemu moja ili ifanywe na wengine, kwa kuepuka watu wanaotaka kumwangamiza. Vivyo hivyo watumishi wake, wasingevunjwa moyo na mateso, ila wangetafuta mahali pengine pa usalama ili waendelee kufanya kazi ya injili.

Lakini katika mateso yoyote, watumishi wa Kristo, lazima wadharau hali ya kujificha na kuepa mateso iwapo ni lazima. Hawawezi kuiacha kweli ili kuepa mateso. Yesu aliseema, “Niwaambiayo katika giza, yatangazeni katika nuru, na yale mnayosikia kwa siri ninyi yatangazeni juu ya nyumba.”

Yesu kamwe hakutaka usalama kwa njia ya kukubaliana na mambo yasiyokuwa ya kweli. Roho yake iliwahurumia wanadamu wote na kuwafadhili, lakini hakukubaliana na matendo yao ya dhambi, alinyamaza tu wakati walipoendesha mambo yatakayowaharibu. aliwafundisha ili wawe watu wa kweli, wanaochuchumilia faida ya juu. Watumishi wa Kristo wametiwa kazi ya jinsi hiyo. Hivyo lazima wajihadhari sana wasije wakashusha kanuni za kweli wakati wanapojaribu kuleta amani. Amani ya kweli haiwezi kupatikana kwa kutelemsha kanuni za unyofu. “Msiwaogope wenye kuua mwili, wasiweze kuua roho.” Hofu yao ingekuwa kuisaliti kweli ambayo kwayo, Mungu hutukuzwa, kwa njia yao.

Shetani hujitahidi kuwatilia watu mashaka. Huwashawishi watende dhambi, halafu waonekane kuwa ni wachafu mno. hawawezi kuonekana mbele ya Mungu mtakatifu, ambaye ni Baba wa mbinguni, bwana anafahamu haya yote. Yesu aliwathibitishia wanafunzi wake huruma za Mungu, kwamba hakuna kitu hata kidogo kisichojaliwa mbele zake.

Biblia hutuonyesha kwamba Mungu yuko juu, mahali patakatifu
(Isaya 57:15) wala hakai tu bila shughuli, akinyamaza kimya ila
anazungukwa na viumbe maelfu vyenye maarifa, ambao ni watakat- [196]
ifu, wanaofanya mapenzi yake. Sisi hatuwezi kuelewa na maajabu
yake. Huunganika na sehemu zote za utawala wake na kuwasil-

iana nao, pamoja na dunia yetu pia. Mungu huinama na kusikiliza malalamiko ya mwenye dhiki, ingawa anakaa kwenye kiti chake cha enzi. Hujibu kila ombi la mtu mwenye haja, na kusema: "Mimi hapa." Huwainua watu waliodidimia na wenye dhiki. Malaika kutoka mbele yake huenda kumwokoa kila mtu aliye katika majaribu na mateso.

Yesu alisema: "Jinsi mnavyonikiri mbele ya watu, ndivyo nami nitakavyowakiri mbele za Baba yangu na mbele ya malaika zake." Mtakuwa mashahidi wangu duniani, nami nitawawakilisha mbinguni. Baba haangalii tabia zenu chafu, ila huwaangalia mmevikwa haki yangu ambayo ni ukamilifu wa tabia yangu. Na kila mtu anayeshiriki dhabihu ya kujitolea kwangu, atakuwa mshiriki wa utukufu na furaha ya ukombozi.

Mtu ambaye atamwungama Kristo, lazima Kristo awe anaishi ndani yake. Mitume wake lazima wawe wakinena kwa ufasaha mafundisho yake. Lakini wasipokuwa nayo tabia ya kikristo halisi, tabia ya unyenyekevu na upendo, hawawezi kumwungamia. Roho ambayo ni kinyume cha roho yake humkana. Watu humkana Kristo kwa kusema misemo mibaya, kwa maongezi ya kijinga, kwa maneno ya ovyo ambayo siyo ya kweli, au kwa maneno yasiyo mema. Wanaweza kumkana kwa kutosaidia mzigo wa maisha ya watu, na kwa kujiunganisha na kawaida za dunia, na kwa hali isiyokuwa ya utu mwema, na kwa njia ya kukuza hali ya ubinafsi, na kwa kuwa na mashaka, na kuwa na uchokozi. "Mtu yeyote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni."

Mwokozi alisema: "Sikuja kuleta amani duniani, ila kuleta upanga." mashindano siyo mambo yafaayo kwa injili, bali ni kinyume cha injili. Katika mateso yote, yaliyo magumu ni ya nyumbani. Mfarakano wa watu wa nyumbani na marafiki. Lakini Yesu alisema: "Apendaye baba au binti kuliko mimi hanifai. Na mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata hanifai."

"Awapokeaye ninyi, hunipokea mimi, na yeye anipokeaye mimi humpokea aliyenituma." Hakuna tendo la wema litendwalo kwa jina lake, lisilopewa thawabu. Huongeza wana walio wadhaifu wa jamaa ya Mungu. Atakayemnywesha mmojawapo wa wadogo hawa kikombe cha maji baridi, amini nawambieni, hatakosa kupata thawabu yake."

[197] Hivyo ndivyo Mwokozi alimaliza mafundisho yake. Wanafunzi

kumi na wawili waliochaguliwa wakaenda nje, kama alivyokwenda kuhubiri injili kwa miaskini ... na kuwaponya waliovunjika mioyo, kuhubiri uhuru kwa wafungwa, na kuwafanya vipofu kuona. Luka 4:18.

[198] ## 38 — Kristo na Wanafunzi Wapumzika

Waliporudi kutoka katika safari yao ya mahubiri, wanafunzi walikuja kwa Yesu kumsimulia mambo ya safari yao, jinsi walivyofanya, na mafundisho waliyofundisha. Yesu aliwaambia: "Njooni peke yenu mahali pasipokuwa na watu mpumzike kidogo."

Uhusiano wa wanafunzi na Yesu ulikuwa mkubwa sana. Walimweleza mambo yote ya kazi yao ya kuhubiri, mafanikio yao na matatizo yao pia. Kwa jinsi walivyomweleza mambo kwa wazi, aliona kuwa wanahitaji mafundisho zaidi.

Lakini mahali walipokuwapo hapakufaa, maana watu wengi walikuwa wakiingia na kutoka mfululizo, wala hakuna nafasi ya kula. Watu walikuwa wakimfuata Kristo, ili awaponye maradhi yao, na kutaka kumsikiliza. Kwa wengi alionekana kuwa ni asili ya mibaraka yote.

Lakini sasa Kristo alitamani mahali pa kupumzika; maana alikuwa na mambo mengi yaliyowahusu wanafunzi wake wenyewe. Katika kazi yao mara nyingi wametatanika, hawakujua jinsi ya kusema. Sasa walitaka kwenda mahali pa upweke, ambapo Yesu angawaelimisha zaidi kuhusu kazi yao ya baadaye. Walikuwa wamejitumbukiza katika kazi kamili, hivyo nguvu zao za kimwili na za kiroho zimelegea. Iliwapasa wapumzike.

Kwa kuwa wanafunzi walifanikiwa kazini, kulikuwa na hatari ya kujisifu na kujichukulia utukufu, na kuangukia katika shimo la Shetani. Iliwapasa wajifunze kuwa uwezo wa kufaulu hautokani na wao wenyewe. Iliwapasa kuongea na Kristo, kuchunguza viumbe vya asili na kujichunguza wao wenyewe.

Wakati huo ndipo Yesu alipata habari za kifo cha Yohana Mbatizaji. Jambo hili lilimthibitishia mwisho wake pia, kwa kadiri
[199] alivyokuwa akienenda na mafundisho yake. Makuhani na Marabi walikuwa nyumba yake, kwa kuweka majasusi ili wapate kumnasa na kumshitaki.

Habari za kazi ya Yesu zilimfikia Herode . Basi Herode alisema: "Huyu ni Yohana Mbatizaji, amefufuka katika wafu." Naye alieleza

kuwa na hamu ya kumwona Yesu. Herode alikuwa na hofu ya daima kwa ajili ya mapinduzi yanayoweza kutokea ya Wayahudi kuasi serikali ya Warumi. Roho ya chuki na uasi ilienea pote kwa wayahudi. Ilikuwa wazi kwamba kazi ya Kristo huko Galilaya isingedumu muda mrefu, naye alitamani kuwa mbali na makutano ya watu kwa muda kidogo.

Kwa huzuni wanafunzi wa Yohana walikuwa wameuchukua mwili wa Yohana mpaka mahali pa makaburi. Kisha walikwenda na kumwarifu Yesu. Wanafunzi hawa walikuwa na wivu na Yesu, hata walikuwa na mashaka ya Uungu wake, maana hakumwokoa Yohana. Lakini sasa walitaka faraja katika huzuni yao, na maongozi kuhusu kazi yao ya siku zajazo. Walikuja na kuunganika na Yesu.

Huko nga'mbo ya ziwa, upande wa kasikazini kulikuwa na semu ya nafasi, isiyokuwa na watu. Ilikuwa sehemu nzuri yenye maji mengi na majani. Waliingia katika mashua kuiendea. Ilikuwa sehemu ya kupendeza. Mahali hapo wangemsikiliza Yesu bila fujo. na ghasia za Waandishi na Mafarisayo.

### Pumziko liliwaburudisha

Wakati ambao Yesu na wanafunzi wake walitumia katika mapumziko haukuwa wakati wa anasa. Waliongea pamoja kuhusu kazi ya Mungu na mambo yatakiwayo kufaulisha. Kristo aliwasahihisha makasoro yao, na kuwaonyesha jinsi ifaayo ya kukutana na watu. Walitiwa nguvu na uwezo wa Uungu na wakawa na ushujaa na moyo mkuu.

Yesu aliposema kwamba, "Mavuno ni mengi lakini watendakazi ni wachache", hakuwa na maana ya kufanya kazi wakati wote bila kukoma, bali "Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watendakazi katika mavuno yake." Mathayo 9:38. Mungu hapendi watu wachache tu wabebe mzigo mzito wa kuwalemea katika kazi yake, wakati huo huo wengine hawataabiki kwa lolote, kuhusu roho za watu.

Maneno ya Kristo ya huruma, yanawahusu watenda kazi wake leo pia. "Njooni peke yenu hapa . . . mpumzike kidogo." Sio hekima kufanya kazi ya kuwahudumia watu kwa mambo ya kiroho [200]
bila kupumzika, maana kwa jinsi hii utawa wa mtu huachwa bila kushughulikiwa, na nguvu za mwili huchoshwa sana. Kujitoa nafsi

kunahitajika, lakini hadhari lazima iwepo, ama sivyo Shetani atapata nafasi ya kupenya na kumdhoofisha mtu, na kazi ya Mungu itakuwa na madoa.

Shughuli zinapozidi za kazi ya Mungu, na watu wakifanikiwa katika kazi ya Mungu, kuna hatari ya kuwa na maombi machache na imani chache pia. Mambo hayo huelekea kuwa hivyo. Huelekea kuwa na kumtegemea Mungu kidogo, na kutegemea shughuli hizo. Uwezo wa Kristo ndio unaowezesha kazi kufanyika. Inatupasa tupate wakati wa kutafakari, kuomba, na kujifunza neno la Mungu. Kazi inbayotimilika kwa njia ya maombi mengi, na kwa uthibitisho wa Ksristo, ndiyo itakayofaulu mpaka mwisho kupata sifa bora.

## Usikose kuongea na Mungu kwa sababu ya shughuli nyingi mno

Hakuna mtu aliyekuwa na kazi nyingi maishani kama Yesu; walakini alikutwa akiomba mara ngapi! Mara kwa mara imesemwa kwake hivi: ". . . akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko." "Lakini habari zake .... Lakini yeye alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba." "Ikawa siku zile aliondoka alienda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu," Marko 1:35; Luka 5:15, 16; 6:12.

Mwokozi aliona kuwa ni lazima aache shughuli za maisha na kujitenga kwa maombi; ili kiungo kinachowaunganisha na Baba yake kisivunjike. Kama mmoja wetu, alikuwa akimtegemea Mungu kamili. Katika sala za siri alitafuta uwezo wa Uungu ili apate kufanya kazi yake akiwa na silaha na nguvu za kutendea mambo.

Yesu alivumilia uchungu wa maisha na matizo yake. Katika kushirikiana na Mungu aliweza kuvumilia mzigo wa dhambi uliomlemea. Yesu kama binadamu alikabiliana na kiti cha enzi cha enzi cha Baba, mpaka akapta moto upya, kama betri ya gari. Hiyo ilimvunganisha binadamu na Mungu ikamwezesha. Alipokea uzima kutoka kwa Mungu ili apate kuutoa uzima huuo ulimwenguni. Hali yake hiyo lazima iwe yetu.

Leo kama tungepata wakati wa kwenda kwa Yesu na kumweleza mahitaji yetu, angetutimizia. Yeye ni Mshauri wa Ajabu. Tunaambiwa kumwomba hekima, huwapa watu wote kwa ukarimu, wala hazuii. Isaya 9:6; Yakobo 1:5

Kila mtu anahitaji apate ujuzi kamili wa kumjua Mungu; na [201]
mapenzi yake. Lazima tumsikie akisema, sisi binafsi, sauti zote zikinyamaza, lazima tumsikie akituzungumzia mioyoni mwetu. Tunaponya-mazisha sauti zote, ndipo tunapoweza kuisikia sauti ya Mungu akinena nasi. Zaburi 46:10. Hapa ndipo pumziko la hakika linaweza kupataikana. Mtu anayepumzika kwa jinsi hii ndiye atakuwa na uwezo na nguvu za kuwaongoa wanadamu wenzake.

[202] 
## 39 — "Wapeni Ninyi Chakula"

Wanafunzi wa Yesu walifikiri kuwa hawatavurugwa na mtu yeyote, lakini wakati makutano walipomkosa Mwalimu wa mbinguni mda huo, walianza kuulizana: Amekwenda wapi?" Baadhi yao waliona upande alikoelekea pamoja na wanafunzi wke. Watu wengi walikwenda upande huo, wakitembea kwa miguu, na wengine katika mashua ili kumtafuta. Pasaka ilikuwa karibu, na wasafiri wa kwenda Yesusalem, walikuwa na hamu ya kumwona yesu. Watu wengi walikusanyika kiasi cha wanaume 5,000, mbali ya wanawake na watoto.

Kutoka kando ya mlima Yesu aliwaangalia makutano waliokusanyika, akawahurumia, kwa sababu walikuwa kama kondoo wasiokuwa na mchungaji. Akiachilia mbali shughuli yake kwa wanafunzi wake, alitafuta mahali pafaapo ili apate kuwahudumia.

Watu wakalisikiliza neno la neema kutoka kwa Mwana wa mungu, neno ambalo ni faraja katika mioyo yao. Mikono yenye kuponya ya Kimungu, iliwahuisha wenye dhiki, na wenye maradhi ya kila aina. Siku ilipita kama kivuli, hata wakasahau wakati wa mwisho walipokula chakula.

Wakati jua lilipokuwa likichwa wa walikuwa bado wanamzunguka. Yesu alikuwa ameshughulika siku nzima bila pumziko, wala kula; walakini asingeliweza kuwaacha watu wakimzunguka hivyo.

Mwisho wanafunzi wake walisema kuwa, ni afadhali watu wawapishe ili nao wapate kula. Watu wengi walikuwa hawajala chochote tangu asubuhi. Katika vijiji na miji inayowazunguka wanaweza kununua chakula wapeni ninyi chakula." Yesu akimgeukia Filipo, aliuliza: "Tutanunua wapi chakula cha kuwalisha watu hawa? Aliyasema haya ili kujaribu imani ya wanafunzi. Filipo
[203] akatazama utitiri wa watu, akasema: "Mikate ya dinari* mia mbili haitatosha kila mtu apate kipande kidogo tu."

Yesu akauliza kuwa wanacho chakula kiasi gani. Andrea akasema: "Yuko kijana hapa ana mikate mitano na samaki wawili;

* 'Dinara ni sawasawa na malipo ya siku, kwa kima cha chini. Angalia Mathayo: 1,2

na hivi vinafaa nini kwa makutano haya?" Yesu akaagiza wamletee vitu hivi, na wanafunzi wawaketishe watu makundi makundi ya hamsini na mia mia, ili wote washuhudie atakavyofanya. Mambo haya yalipokwisha kutendeka, yesu akatazama mbinguni, akavibariki, na kuvivunja vipande vipande, akawapa wanafunzi wawagawie watu, na akagawanya samaki wawili kwa watu wote. Wakala waote wakashiba. Wakakusanya makapu kumi na mawili ya vipande vya mikate na samaki vilivyobaki. Aliyekuwa akifundisha watu kuwa na amani na furaha alikuwa na uangalifu pia kwa mambo ya kawaida, ya mahitaji yao ya kila siku, kama mambo ya kiroho pia.

Kristo kamwe hakufanya miujiza, isipokuwa ilikuwa ni kwa kuimarisha mambo ya lazima tu, na hata hivyo kila mwujiza aliofanya ulikuwa ni kuwapeleka watu kwenye mti wa uzima. Chakula chepesi kilichotolewa na wanafunzi kwa makutano kilikuwa kimejaa mafunisho ya thamani. Maandalizi mepesi yaliandaliwa, ambayo ni samaki wawili na mikate mitano vilivyokuwa chakula cha kuliwa kila siku na wavuvi.

Kristo angeweza kuwaandalia chakula kilichokuwa bora zaidi, lakini chakula kinachotolewa ili kutimiza uchu na hamu ya wwatu tu, hakingeweza kutoa fundisho lolote kwa binadamu. Watu haawajafurahia karamu nzuri sawa sawa na watu wale walivyofurahia karamu hiyo iliyotolewa kwao na Kristo, kutokana na chakula chepesi jinsi hiyo.

Kama watu wangekuwa na mazoea ya kufanya mambo rahisi na mepesi leo, wakiishi kufuatana na sheria za asili, kungelikuwa na vitu vya kuwatosheleza wa wote, bila wengine kukosa chochote. Kungalikuwa na uhaba wa vitu vichance mno, ambao ni wa kukisia tu kimawazo. Lakini ubinafsi na choyo vimeleta dhambi na umaskini ulimwenguni. Kwa kutano kubwa namna hiyo njaa na uchovu wao, chukula chepesi hicho hakikuwaonyesha uwezo wa utunzaji wake kwa watu wote katika maisha yao. Mwokozi hakuwaahidi wafuasi wake kupata anasa na sikukuu. Chakula chao kinaweza kuwa chepesi tu; haIi yao inaweza kuwa ya kumasikini. Lakini neno lake lasema kuwa, chakula chao hakitakoma, na haja zao zitatimizwa siku zote. Ameahidi kuwa, zaidi ya yote yeye atawafariji kwa kuwako kwake yeye mwenyewe kwao.

Katika mavuno ya nchi, Mungu hufanya miujiza kila siku. Ku- [204]
tokana na mambo ya asili na uwezo wake, hutendeka mambo sawa

na yale ya kuwalisha makutano. Watu hulima na kupanda mbegu, lakini uzima wa Mungu huzimeesha. Ni Mungu anayewalisha watu mamilioni kila siku kwa njia ya mavumo ya mashambani. Watu wamepewa kazi ya kuendeleza uwezo wake katika mamo ya asili. Mtu hutukuzwa mahali pa Mungu, na vipaji vyake vya thamani hugeuka kuwa laana badala ya mibaraka. Mungu ataka tumtambue kwa ajili ya vipaji vyake. Kufikilisha jambo hili, miujiza ya Kristo ili fanyika.

## Fundisho muhimu la utunzaji

Baada ya kuwalisha makutano, byakula vingi vilibaki. Lakini Yesu alisema: "Kusanyeni mabaki, kitu kisipotee." Kila kitu kinachoweza kumsaidia mtu mwenye njaa, kisitupwe bure. Pia pangekuwa na uangalifu katika mambo ya kiaroho. Watu wangetaka rafiki zao wa nyumbani washiriki kuala mikate hii iliyobarikiwa na yesu. Vivyo hivyo wale waliokuwa karamuni wangetaka rafiki zao waliokuwa nyumbani washiriki kula mkate ule ulioshuka kutoka mbinguni, ili kushibisha mioyo ya watu. Walikariri tena mambo waliyosikia, ambayo ni ya ajabu, ambayo ni maneno ya Mungu. Kitu kisipotee.

Mwujiza wa mikate unafundisha fundisho la kumtegemea Mungu. Kristo alipowalisha watu 5,000 hakikuwepo chakula mkononi. Alikuwa msituni hapa, mahali pasipokuwa na chakula. Lakini alijua kuwa kundi hili la watu litachoka na kuona njaa, na yeye alikuwa pamoja nao, nao walihitaji chakula. Walikuwa mbali na miji yao, na wengine wao hawakuwa na fedha za kununulia chakula. Mungu alimweka Yesu mahali hapo, naye alimtegemea Baba yake wa mbinguni ili awasaidie na kuwapatia mahitaji yao.

Sisi pia yatupasa kumtumaini Mungu. Hatuwezikuingia katika matatizo na kutumia ovyo uwezo Mungu aliotupatia. Lakini baada ya kufuata maongozi yake, tukapata kufika mahali sawa, tunaweza kutafuta msaada wake aliye na hekima na vitu vyote. Yeye ataangalia kila mtu aliye katika matatizo akijaribu kutunza njia ya Bwana.

## Namna tunavyorudia kutoamini kwa Adrea

Kristo ametuagiza akisema: "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe." Marko 16:15. Lakini ni mara ngapi sisi tunakata tamaa, tunapoona ukubwa wa kazi, na udogo wetu wa kuweza kuikamilisha. Sawa kama Andrea, hata sisi husita- [205]
sita, na hatuwei tayari kutoa vyote tulivyo navyo ili kuwapa wengine chakula. Lakini yesu hutuagiza na kusema: "Wapeni ninyi chakula." Nyuma ya agizo lako kuna uwezo wa kuwalisha makutano ya watu.

Katika tendo la Kristo kumefungwa fundisho kwa ajili ya waatendakazi wakee. Kristo alipokea kutoka kwa Baba, akawapa wanafunzi wake; nao wakawagawanyia makutano, na kwa watu, kila mtu. wote wanaounganika na Kristo watapokea kwake mkate wa uzima, na kuwagawanyia wengine. Yesu alitwaa mikate midogo, na ingawa ilikuwa sehemu ndogo aliyoawapa wanafunzi wake, hakutaka waile; ila waigawanye kwa makutano. Chakula kilichoongezeka mikononi mwake, na mikononi mwa wanafunzi wake kiliyotoka kwa Kristo, hakikuwa kidogo. Baada ya watu kula, Kristo na wanafunzi wake nao wakala pamoja chakula kilichoongezeka kwa nguvu za mbinguni.

Wanafunzi ndio walikuwa njia ya mawasiliano, kati ya watu na Kristo, jambo hili ni la kutia moyo sana kwa wanafunzi wa Yesu siku hizi. Sisi tunaweza kutoa kile tulichopokea kutoka kwa Kristo, na sisi tunaweza kupokea tu kadiri lunavyotoa kwa wengine. Kadiari tunavyotoa sana ndivyo tutakavyopokea zaidi.

Mara nyingi mtendakazi wa Kristo hushindwa kufahamu madaraka yake. Huwa na hatari kuelekeza na kutoa wajibu wake na kulitwika shirika, badala ya kumtegemea mwenye uwezo wote. Kazi yenye kufaulu, ambayo ni kazi ya Kristo, haitegemei talanta mtu aliyojifunza na njia za kufanyia kazi mtu alizojifunza, ila hutegemea imani. Badala ya kutupa wajibu unaokupasa kwa mtu mwingine unayedhani kuwa anao uwezo zaidi yako, fanya kazi kwa kadiri ya uwezo wako. Unapopata swali moyoni mwako kuwa, "Tunanunua wapi mikate ya kuwatosha watu waote hawa?" Jibu lako lisiwe la kutoamini, ila lenye imani. Wakati watu wanapokosa kuwa na mkate wa uzima, je tumtume mtu kutoka mbali aende kuwalisha? Kristo alisema: "Waketisheni watu, mkawalishe." Vivyo hivyo, unapuzungukwa na watu wenye njaa, fahamu kuwa Kristo yuko hapo. Leta

vipande vyako kwa Yesu. Vichache vinavyotumiwa katika kazi ya Yesu kwa hekima, vitaongezeka wakati wa kuwapa watu.

Bwana husema, "Toeni, nanyi mtapewa." Yule anayezidisha mbegu za manzi, na mikate kwa walaji, ndiye atazidisha uwezo wako, nawe utapata mavuno ya haki. Utatajirishwa kwa kila njia wakati unapokuwa mkarimu. Tazama Luka 9:10, 11.

# 40 — Usiku Ziwani [206]

Watu walikuwa wameketi katika majani ya uwanda, walipokuwa wakila chakula kile yesu alichowaandalia wakati wa machweo ya jua. Mwujiza wa kuzidisha mikate kuwa chakula kingi, uliwaingia wote mioyoni mwao. Mungu alikuwa amewalisha Waisraeli jangwani, na sasa ni nani huyu aliyewalisha hawa, isipokuwa ni yule aliyenenwa na Musa? Hivyo ndivyo walivyosemezana wao kwa wao. "Kwa kweli huyu ndiye nabii ambaye atakuja ulimwenguni."

Tendo hilo mashuhuri lilikuwa ushuhuda wa Mkombozi aliyekuwa amengojewa kwa muda mrefu alikuwa kati yao. Huyu ndiye aliyefanya Uyahudi kuwa Paradiso ya duniani, nchi iliyojaa asali na maziwa. Anaweza kuvunja nguvu za Kirumi, ambao huchukiwa sana. Anaweza kuonya majeraha ya askari vitani. Anaweza kuwapatia jeshi zima la askari chakula. Anaweza kuwapatia Waisraeli dola inayotamaniwa kwa muda mrefu.

Watu walikuwa tayari kumtawaza awe mfalme. Walimwona kuwa hana bidii ya kujikweza, nao waliona mashaka kwamba hawezi kujishughulisha na mambo ya kutaka ufalme. Wakizungumza pamoja waliazimu kumtawaza kwa nguvu, ili awe mfalme wa israeli. Wanafunzi wake nao waliunga mkono kuwa mtu anayestahili kurithi kiti cha enzi cha Daudi ni mwalimu wao. iwe hivyo ili makuhani na wakuu ambao ni wenye majivuno makubwa, walazimike kumtii aliyekuja akiwa na uwezo wa Mungu.

Lakini Yesu aliona jinsi mambo yanavyokwenda. Kitakachofuata ni maasi na utumiaji wa nguvu, ambavyo vingeharibu mpango wa ufalme wa Mungu. Akaona kuwa hali hii ni lazima izuilike mara moja. Akawaita wanafunzi wake akawaagiza wapande mashua na kurudi Kapernaumu, na yeye abaki akiwaaga makutano. [207]

Wakati wowote agizo la Yesu halijawa gumu la kutiwa kama hili. Hii ilionekana kuwa ndiyo nafasi hasa ya kumtawaza mpendwa wao, awe mfalme wa Israeli. Ilikuwa vigumu kwa wanafunzi kwenda peke yao na kumwacha mwalimu wao mahali hapo. Walipinga

kwenda wenyewe, lakini sasa Yesu alitumia madaraka, ambayo haikuwa kawaida yake kufanya hivyo. Basi wakaondoka kimya.

Sasa Yesu akawaamuru watu waondoke, waende zao. Hali yake ilibadilika sana, wala hakuna mtu aliyesema neno lolote, wala kubisha. Wakati ule walipotaka kumshika ili wamtawaze, hatua zao zilishindwa kuondoka. Hali tukufu ya kuonekana kwa yesu, na maneno machache aliyosema kama mwenye mamlaka, yalibatilisha maazimio yao. Waliona kuwa alikuwa na mamlaka kupita watu wote, kwa hiyo hawakuwa na neno la kusema.

Walipoondoka na kumwacha yesu peke yake, alipanda mlimani akaomba. Aliomba muda mrefu, akiomba apate nguvu za kuwadhihirihia watu tabia ya Kimungu inayofanana na kazi yake, na kwamba Shetani asiwapofushe watu na kuwapotosha. Alijua kuwa siku zake duniani ziko karibu kumalizika, na watu wanaomwamini ni wachache tu. Wanafunzi wake watajaribiwa vikali sana, na matumaini yao yatatoweka. Badala ya kumwona akitawazwa kuwa mfalme, watamwona akisulubishwa msalabani Huku ndiko kulawazwa kwake; lakini hawakufahamu hayo, na pasipo msaada wa Roho Mtakatifu, imani yao itufifia. Kwa ajili ya wanafunzi wake aliwaombea kwa uchungu mkali na kulia.

Wanafunzi wake walikuwa hawajaenda mbali sana kutoka pwani, kwa kutumaini kuwa yesu atakuja. Lakini kadiri giza la usiku lilivyozidi kuongezeka, walisonga mbele, wakavuka bahari wakaenda kapernaumu. Walilalamika kwa sababu hawakupata nafasi ya kumtawaza kuwa mfalme. Walijilaumu kwa kutoka walipoambiwa. Kama wangesisitiza kukataa maazimio yao yangetimia.

Mashaka ya kutoamini yaliwajaa. Kutaka ukuu na heshima viliwapofusha. Walitamani kumwona Yesu akitawazwa kama walivyokusudia. Je, watadumu kuhesabika tu kuwa wafuasi wa nabii wa uongo? Kwa nini mwenye uwezo mkuu namna hii asijidhihirishe kwa wazi? na kwa nini hakumwokoa Yohana na mauti? Wanafunzi walitafakari mambo hayo mpaka wakajiletea giza mioy-
[208] oni mwao. Wakajiuliza, inawezekana Yesu awe mtu laghai kama Mafarisayo wanavyodai?

## Dhoruba mioyoni mwa wanafunzi

Siku hiyo tukufu sana ilikuwa imewajaza wanafunzi matumaini makuu, lakini walikuwa wameisahau kabisa. Mafikara yao yalikuwa ya mashaka tu na hoja zisizokuwa na sababu, kuwa Bwana angewapa kitu kingine cha kuwatuliza. Mungu mara nyingi hufanya hivi wakati watu wanapojisumbua na kujitia wenyewe kubeba mizigo isiyokuwa ya lazima. Wanafunzi haikuwapasa kujisumbua. Hatari ilikuwa ikiwajia karibuni.

Tufani ilikuwa ikiwakabili, lakini hawakuwa tayari kukutana nayo. Hatari hiyo ilikuwa jambo la tofauti kinyume cha mawazo yao, nayo ilikuwa tufani, ambayo ilipowatukia waliogopa. Hapo walisahau chuki yao, kutoamini kwao na kutosubiri kwao. Wakajitahidi, ili wasizame. Katika wakati wa kawaida safari hiyo ilikuwa ikichukua masaa machache tu, lakini sasa waliokotwa na kupelekwa mbali na kivuko chao. Mpaka kwenye kesha la nne walikuwa wakihangaika tu na makasia. Ndipo wachovu hawa walikata tamaa ya kuokoka. Walitamani Mwalimu wao, angekuwako.

Watu waliokuwa pwani waliwaona watu hao wakishindana na tufani. kwa macho yenye huruma sana Yesu aliiangalia mashua hii isumbukayo katika tufani, na watu waliomo humo, maana watakuwa nuru ya ulimwengu, waliomo humo, maana watakuwa nuru ya ulimwengu. Roho zao zilipotulia na mawazo mabovu yalipowatoka, ndipo waliomba msaada, nao wakapata.

Walipoona kuwa sasa wameangamia, ndipo umeme uliopomulika, waliona kitu kigeni, cha ajabu, kikitembea juu ya maji kinawakaribia. Aliyekuja kuwasaidia, wao walimhesabu kama adui wao. Hofu ikawajaa. Mikono yao yenye nguvu ikalegea. Mashua ikayumba kwa mawimbi. Macho yote yakamwelekea kiumbe huyu anayetembea juu ya maji.

Walifikiri kuwa ni pepo ambaye anakuja kuwaangamiza. Kwa hiyo walipiga kelele kwa hofu. Yesu aliendelea kama kwamba anataka kuwapita, lakini walimtambua, hivyo wakataka msaada kwake. Sauti yake ikawatuliza. Alisema: “Ni mimi, msiogope.”

Mara moja walipohakikisha kuwa ni yeye, Petro alisema, “Bwana, ukiwa ni wewe, niamuru nije kwako nikitembea majini.” Yesu akasema, “Njoo.”

[209]

## Kujiinua na kuanguka kwa Petro

Petro alitembea majini salama alipokuwa akimwangalia Yesu; lakini alipogeuza macho yake na kuwatazama wenzake katika mashua, macho yake yalitoka kwa Yesu ambaye ndiye Mwokozi wake. Mawimbi yaliinuka juu sana, naye aliogopa. Kwa kitambo kidogo Kristo alitoweka katika macho yake, na imani yake ikatatanika, akaanza kudidimia. Lakini mawimbi yalipozungumza na mauti, Petro aliinua macho yake katika maji yenye hasira, akalia na kusema, "Bwana, niokoe." Yesu akanyosha mkono wake, akisema, "Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka?"

Petro na Bwana wake walitembea wakishikana mikono wakaingia mashuani. Sasa Petro alitulia. Alikuwa karibu kupoteza maisha yake kwa ajili ya kutoamini kwake, na kwa ajili ya kujivuna.

Matatizo yanapotokea ni mara ngapi huangalia juu ya mawimbi badala ya kumwangalia mwokozi! Maji ya kiburi huingia katika roho zetu. Yesu hawezi kutuita tumfuate, kisha akatuacha. Asema, "msiogope." " . . Upitapo majini, mimi nitakuwa pamoja nawe; Upitapo katika mito, haitakugharikisha . . . Mimi ni Bwana Mungu wako, Mtakatifu wa Israeli, Mungu wako, na Mwokozi wako . . . " Isaya 43:1-3.

Katika msukosuko huu wa maji Yesu alitaka kumfundisha Petro kwamba usalama wake ulitegemea uaminifu wake na mng'ang'anio wake juu ya Mungu. Katika majaribu yafananayo na dhoruba usalama wake ni kumtazama Mwokozi peke yake. Alipojidhani kuwa ana uwezo, Petro alikuwa dhaifu kabisa. Kama angelijifunza fundisho lile la baharini, asingalishindwa wakati jaribu kubwa lilipomjia.

Mungu huwafundisha watoto wake siku kwa siku. Katika matukio mbalimbali ya kila siku, huwatayarisha ili waweze kufanya sehemu yao katika mambo makuu anayowaandalia. Tunaweza kudhani kuwa tunasimama imara sasa, wala hatutatikisika. Tunaweza kusema kwa uthabiti kuwa hakuna kitakachobabaisha imani yangu kwa Mungu na kwa neno lake. Lakini Shetani anapanga kupata njia katika hali ya mazoea yetu ili kutushambulia na kutubabaisha. Tunapofahamu makasoro yetu, na kutazamisha kwa Mwokozi hali zetu ili atusaidie, ndipo tutatembea katika usalama.

Mara moja tu Yesu alipozungumza mashuani, dhoruba ilikoma, na mashua ikafika pwani salama, wakafika mahali walipokusudia. Wanafunzi wake na watu wengine waliokuwa mashuani, walimsujudia Yesu kwa shukrani kubwa, huku wakisema, "Kwa kweli wewe [210]
ni Mwana wa Mungu."

[211] ## 41 — Hatari Katika Galilaya

Kristo alijua ya kuwa wakati wa kazi yake ulimwenguni ulikuwa ukingoni kumalizika, makundi ya watu wanamtukuza leo na kumtaka awe mfalme, kesho watamgeuka. Hoihoi za kibinafsi zinazoonekana leo, kesho zitageuka kuwa chuki isiyotaka kuona kazi hiyo.

Walakini hakuchukua hatua yoyote ya kuepukana na hatari hiyo. Tangu mwanzo hakuwa na tumaini lolote la kupata thawabu duniani, katika wale wanaoungana naye sasa, walikuwa wamevutiwa na utukufu wa duniani, yaani kutumaini kupata chochote katika ufalme wa duniani. Hawa lazima wamefahamu kuwa Yesu hana nia ya ufalme.

Kesho yake asubuhi na mapema watu walikusanyika wengi sana huko Bethsaida. Wale waliomwacha yesu ng'ambo kule, walienda huko tena wakitumaini kumkuta huko, maana haikuwapo mashua yoyote ambayo ingalimchukua. Lakini tumaini lao lilikuwa bure.

Wakati huo alikuwa amefika, Genesareti baada ya kutokuwapo siku moja. Wale waliotoka Bethsaida walipata habari kwa wanafunzi wake kuwa alivuka bahari kwa miguu. Walieleza jinsi tufani ilivyokuwa kubwa, jinsi walivyosumbuka kwa masaa mengi ndani ya upepo mkali, na jinsi Kristo alivyokuwa akitembea majini, na jinsi Yesu alivyotuliza tufani kwa neno lake, watu walitaka maelezo zaidi juu ya miujiza hiyo kutoka katika kinywa cha Yesu mwenyewe.

Yesu hakuwaambia maneno ili kuwaridhisha. Alisema tu kwa masikitiko: "Mnanitafuta, si kwa sababu mliona ishara, ila kwa kuwa mlikula mikate mkashiba. Msikitendee kazi chakula kiharibikacho, ila kile kidumucho hata uzima wa milele." Msitafute faida isiyodumu, bali tafuteni chakula cha kiroho kidumucho.

[212] Usikizi wa watu uliamshwa kwa muda kitambo, kwa hiyo wakauliza wakisema: "Tutafanyaje ili tutende kazi za Mungu?" Maswali yao yalihusu kwamba: Tufanyeje ili tufike mbinguni? Tutahitajika kulipa gharama gani ili tupate uzima ujao?

Kwa maswali haya yesu alijibu akisema: “hii ndiyo kazi ya Mungu, Mwaminini yule aliyetumwa naye.” Gharama ya kufika mbinguni ni Yesu. Njia ya kufika mbinguni ni kuwa na imani, au ni kumwamini Mwana Kondoo wa Mungu.

### Matumaini ya ubinafsi hayakutimiz.wa

Yesu alifanya kazi ile unabii ulivyosema kuwa Masihi ataifanya, lakini watu hawakuona kazi ambayo matumaini yao ya ubinafsi yalitazamia kuona. Siku zile za Musa Waisraeli walikula mana miaka arobaini, ambayo ilikuwa mibaraka ya Masihi. Kwa nini Yesu hangeweza kuwapa watu wake afya, nguvu, na utajiri, na kuwafungua watoke katika utumwa na kuwainua wawe watawala? Anadai kuwa alitumwa kutoka kwa Mungu, huku anakataa kuwa mfalme wa Waisraeli. Jambo hili lilikuwa fumbo, ambalo hawakulielewa. Je, hawezi kuthibitisha madai yake kwa sababu anaona mashaka kuhusu Uungu wake na kazi yake? Nusu ya watu walidhihaki swali la Marabi, kwamba “unatuonyesha ishara gani ili tuone na kukuamini Unafanya nini? Baba zetu waliila mana jangwani, kama ilivyoandikwa: Aliwapa chakula kutoka mbinguni wakala.”

“Kisha Yesu akasema: Amini, Amim nawaambiem, Musa hakuwapa mkate ule kutoka mbinguni.” Mtoaji wa mkate huo alikuwa anasimama katikati yao. Kristo mwenyewe ndiye aliyekuwa akiwaongoza Waisraeli jangwani na kuwalisha mkate huo kila siku kutoka mbinguni. Chakula kile kilikuwa mfano wa chakula cha kweli cha mbinguni. Chakula cha kweli ni ile mana iliayo uzima, ambayo ni chakula cha kiroho. Maana chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.

Hata hivyo wangali wakidhani kuwa ni chakula cna kawaida, kwa hiyo wengine waliuliza: “Bwana, utupatie chakula hicho. Ndipo Yesu akasema dhahiri: “Mimi ndimi mkate wa uzima.”

Musa alikuwa amesema: “Mtu hataishi kwa mkate peke yake, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Bwana.” Torati 8:3. Na Yeremia alikuwa ameandika: “Maneno yako yalionekana kwangu nikayala, na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu maana nimeitwa kwa jina lako, Ee Bwana, Mungu [213]
wa majeshi.” Yeremia 15:16. Mafundisho ya manabii yalidhihirisha mambo ya kiroho kuhusu mwujiza wa mikate. kama wasikilizaj:

wa kristo katika sinagogi wangalifahamu maandiko, wangalifahamu maneno yake pia. “Mimi ni chakula cha uzima.” Kama vile makutano walivyopokea chakula alichowapa siku nyingine, ndivyo wangalipokea kwa Kristo maneno ya uzima, yawezayo kuwapa uwezo wa kupata uzima. Yesu alisema: “Yeye ajaye kwangu hataona kiu kamwe,” Tena aliongeza kusema: “Ninyi mmeniona, wala hamkuniamini.”

Wamemwona kristo kwa kushuhudiwa na Roho mtakatifu, na kwa mafunuo ya Mungu katika mioyo yao. Ushahidi wa kweli zaidi ni ule wa kuwa kati yao siku kwa siku na kuona uwezo na nguvu zake, walakini bado wakawa wanataka ishara yake. Kama hawakuaminishwa kwa yale waliyoona na kusikia, ilikuwa kazi bure kuzidi kuwaonyesha mambo zaidi, wangalipata udhuru zaidi wa kutokuamini, na hata kama wangepata uthibitisho mkubwa kadiri gani, wangalidumu kutokuamini.

Mara nyingine tena Kristo aliwasihi watu hao wenye shingo ngumu: “Ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.” Wote wanaompokea Kristo kwa imani, asema, watapata uzima wa milele. Hakuna tena watu kulalamika katika mashaka na kutokuwa na matumaini. Yesu alisema: “Mapenzi yake aliyenipeleka ni haya: Mtu akimwona Mwana, na kumwamini anao uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho.”

Lakini viongozi walichukizwa, wakasema: “je, huyu siye Yesu mwana wa Yususu, ambavyo tunawafahamu baba yake na mama yake? Anawezaje kusema kuwa, nimeshuka kutoka mbinguni?” Wakasema kwa dhihaka kuwa ni mtu aliyezaliwa katika hali ya kimaskini tu, wakisema kuwa ni mwana wa seremala, asiyekuwa na elimu. Walipoona uzazi wake ni wa ajali wakamtilia shaka.

Yesu hakujaribu kuelezea kuhusu uzazi wake wa ajabu, wala hakuwajibu swali lao juu ya jinsi alivyovuka bahari. Alijifanya kuwa hana utukufu, akawa kama mtumwa. Lakini maneno yake yalidhihirisha tabia yake ya kweli.

Udhalimu wa Mafarisayo ulitokana na ukaidi wa mioyo yao. Kila neno na tendo la Yesu liliamsha upinzani kwao, maana roho waliyopendelea kuwa nayo haikuwa roho safi!

Yesu alisema: “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba yangu .... Imeandikwa katika manabii, wote watafundishwa na Mungu. Kila mtu aliyesikia na kujifunza kwa

Baba, huja kwangu." Hakuna watakaokuja kwa Kristo isipokuwa [214] ni wale waliokubali mvuto wa Baba wa upendo. Lakini Mungu huwavuta watu wote, isipokuwa ni wale wanaopinga mvuto wake ndio hawatakuja kwake. Waliojifunza kwa Mungu huja kwa Mwana wake, na kwa Yesu wa Nazareti watamtambua yule ambaye Yesu humwita kuwa Baba.

## Mbingu zinapoanza

"Amin, amin, nawaambieni, yeye aniaminiye ana uzima wa milele." Huo ndio usemi wa Yesu. "Nami nitamfufua siku ya mwisho." kristo alikuwa katika hali moja na sisi, katika mwili, ili sisi tuwe katika hali moja naye katika roho. Kwa njia ya mwungano huu wa uwezo, tunaweza kufufuka kutoka kaburini, maana kwa imani maisha yake yamekua maisha yetu. Wanaomwona Kristo na kumpokea mioyoni wanao uzima wa milele. Kwa njia ya Roho Kristo huishi ndani yetu; na Roho wa Mungu akipokelewa kwa imani, huanza uzima wa milele.

Mana ambayo ililiwa na baba zetu huko jangwani haikuweza kuzuia kifo, wala kuleta hali ya kutokufa kwa watu, lakini mkate wa mbinguni utawezesha mtu kuufikia uzima wa milele. Mwokozi alisema: "Huu ni mkate ushukao kutoka mbinguni, ili mtu akiula asife." Kwa kifo cha Kristo tu ndipo watu watapata uzima. Alionyesha katika kifo chake kuwa ndipo penye ukombozi. "Chakula nitakachowapa ni mwili wangu nitakaotoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu."

Katika mfano wa kondoo wa pasaka, Wayahudi hawakuelewa mwili wa Bwana. Ukweli ule ule ulifundishwa kwa maneno ya Kristo, lakini haukufahamika hata hivyo. Sasa Marabi waliuliza, huku wakikasirika, "Anawezaje mtu huyu kutupa mwili wake tuule?" Walifahamu maneno ya Yesu, kwa sehemu fulani, lakini kwa jeuri tu walitumaini kuwakoroga watu wampinge Yesu.

Kristo aliikariri kweli kwa nguvu zaidi, akisema: "Amin, amin, nawaambieni, Msipokula mwili wa Mwana wa Adamu na kunywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. Mtu atakayekula mwili wangu na kunywa damu anao uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho. Maana mwili wangu ni chakula cha kweli; na damu yangu

ni kinywaji cha kweli. Mtu yeyote aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu, hukaa ndani yangu na mimi ndani yake."

Chakula ni nini kwa mwili? Kristo lazima akae ndani ya mtu.
[215] Chakula hakitusaidii kitu kisipokuwa kinaingia ndani yetu na kuwa sehemu yetu. Hivyo basi kuwa na elimu juu ya dini na tarativu zake bila kuzitekeleza hakutufai loloe. Lazima tumle Kristo, maisha yake, upendo wake, neema yake lazima viwe sehemu yetu.

"Kama Ba ba alivyonituma, nami naishi kwa amri zake, ndivyo alivyo yeye aulaye mwili wangu, naye ataishi ndani yangu" Ndivyo yesu alivyojitoa kamili kwa mapenzi ya Baba, kwamba Baba peke yake ndiye alidhihirika katika maisha yake. Ingawa alijaribiwa katika mambo yote, kama sisi, lakini aliishi bila kutenda dhambi zilizomzunguka. Ndivyo hata sisi inatupasa kushinda kama Kristo alivyoshinda. Je, wewe ni mfuasi wa Kristo? Basi yote yaliyoandikwa kuhusu mambo ya kiroho ya yesu, yanaweza kuonekana ndani yako kwa ajili ya kuunganika naye. Je, upendo wako wa kwanza umepoa? Pokea tena upendo wa Kristo. Kula tena mwili wake na kuinywa damu yake; ndipo utakuwa mmojawao wa Baba na Mwana.

Kwa sheria Wayahudi walikatazwa kuonja damu, na sasa wao wameelewa lugha ya Yesu juu ya mwili na damu. Wengi hata katika wanalunzi wake walisema kuwa neno hilo ni gumu. Nani ataliweza?

Mwokozi aliwajibu akisema, "Neno hili limewakwaza? Itakuwaje mtakapomwona Mwana wa Adamu akipanda kwenda huko alikokuwa hapo kwanza? Roho ndiyo itiayo uhai, mwili haufai kitu, neno ninalowaambia ni roho tena ni uzima"

## Uzima katika Neno

Uzima wa Kristo, unaoufanya ulimwengu upate uzima umo katika neno lake, kwa neno lake tu, Yesu aliponya magonjwa ya kila namna na kulukuza pepo; kwa neno lake alituliza bahari, na kufutua watu. Biblia yote humdhihirisha Kristo, naye alitamani kukaza imani ya wasikilizaji wake na wafuasi wake juu ya neno lake, yaani Biblia. Wakati yeye asipokuwapo neno lake litakuwao lenye uwezo ule ule.

Jinsi maisha yetu ya kimwili yanavyosaidiwa na chakula tulacho, hali kadhalika maisha yetu ya kiroho husaidiwa na neno la Mungu.

Jinsi itupasavyo kula sisi wenyewe chakul;a cha mwili, ndivyo itupasavyo kulipokea neno la Mungu. Inatupasa kujifunza neno la Mungu kwa uangalifu sana, tukimwomba Mungu atusaidie kwa roho Mtakatifu, ili tuelewe neno lake bila makosa. Inatupsa kutafakari fungu kwa fungu na kutamhua mawazo ya Mungu anayotuwazia kuhusu fungu hilo. Tulitafakari fungu hilo mpaka litukae vizuri. [216]

Ahadi za Mungu na maonyo anayotoa, hunihusu mimi. Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili mimi nikiamini nisipotee, bali niwe na uzima wa milele. Maneno yote yanayotumiwa katika neno la Mungu kuhusu wokovu, hunihusu mimi. Maombi na ahadi ni vyangu. "Nimesulibishwa pamoja na Kristo, walakini ni hai; wala si mimi tena, ila Kristo huishi ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, nao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" Walatia 2:20. Jinsi imani inavyorekebisha kanuni za kweli, hufanyika kuwa sehemu yetu ya maisha na nguvu, neno hutengeneza maisha na kukuza tabia za unyofu.

Mungu atajidhihirisha kwa mtu mwenye njaa ya haki na kuchuchumilia unyofu. kwa kadiri watu wanavyojilisha kwa neno la Mungu huharibu tabia ya asilli, ambavyo ni potofu, na hutia hali ya kikristo, ambayo ni maisha ya yesu. Roho Mtakatifu huja kama mfariji. Kwa neema ya Mungu mwanafunzi wa Biblia huwa kiumbe kipya. Upendo huwa badala ya chuki, na moyo hupata uamsho wa kimungu. Hivi ndivyo kula ule mkate utokao mbinguni. Kristo alijua tabia za wale wanaojidai kuwa watu wake, na neno lake liliwapima kama ni kweli au sivyo. Alisema kuwa ni lazima waamini na kutenda kama inavyotakiwa na kugeuzwa nia zao ili kuambatana na tabia yake. Jambo hili linahusu kuacha tamaa zote na majivuno. Ni lazima kujitoa kamili kwa Kristo. Wanaotakiwa wawe wenye kujinyima, wanyenyekevu wa mioyo, wenye kutembea katika njia nyembamba iliyopitwa na mtu wa Kalwari.

### Maneno ya Kristo yafarakisha wengi

Jaribio lilikuwa zito sana. Hoi hoi na makusudi ya watu waliofikiri kumtawaza yesu kwa nguvu awe mfalme wao vilizimika. Maongezi hayo yalifunua macho yao. Wakaona kuwa kwa kushikamana naye hawataambulia chochote cha dunia hii. Wamekubaliana

na uwezo wake wa kutenda miujiza, lakini hawawezi kukubaliana maisha yake ya kujinyima. Kama hataweza kuwaondoa katika utawala wa Kirumi, hawatashughulika naye kwa vyovyote.

Yesu aliwaambia dhahiri; "Baadhi yenu hamwamini" Akaongeza kusema, "Kwa hiyo nawaambieni, hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba yangu" Wasipovutwa kumjia ni kwa sababu mioyo yao haikumkubali Roho Mtakatifu awaongoze.

[217] Kwa maonyo ya wazi hivi, hata sasa mioyo ya wanafunzi wake ilikuwa bado mbali; wanafarakana na Yesu kiroho. Watu wakitaka kumwumiza yesu, na kuambatana na udhalimu wa Mafarisayo, walimgeuzia mgongo, na kumwacha. Wameonyesha uamuzi wao, hawakuandamana na Yesu tena.

Maneno ya kweli ya yesu yametenganisha makapi na ngano Mathayo 3:13. maana walijiona kuwa wenye haki, kiasi ambacho hawakukubali kutiwa kasoro. Wengi waliondoka, wakaenda zao. Watu hujaribiwa siku hizi kama wafuasi wa yesu walivyojaribiwa katika sinagogi huko Kapernauamu. Ukweli unaposemwa na kuingia moyoni watu huona makasoro yote waliyo nayo, ila huwa hawakubali kujinyima, huenda zao hali wakichukizwa, na huku wakilalamika, kwamba "Huu ni usemi mzito, nani atausikia"?

## Kweli haikukubalika

Wakati makutano yalipofuata mambo ya Yesu, na kulishwa chakula, sauti zao zilisikika zikiimba na kumsifu Yesu kwa hayo aliyowatendea, lakini ukweli uliposemwa na kudhihirisha kasoro zao na dhambi zao, walimgeuzia migongo yao, na kuisukumia kweli mbali.

Watu hao walipokwenda zao na kuiacha kweli, hali nyingine ya tofauti na ile ya kwanza iliwaongoza. Hawakuona faida yoyote juu ya yesu, ambaye kwanza alikuwa akiwapendeza sana. Waliyatafsiri maneno yake kinyume cha yalivyokuwa. Wakagombana kuhusu hali yake, wakikusanya mambo mbalimbali ya kumwendea kinyume. Mambo hayo ya uongo yalishindiliwa sana, hata akaonekana kuwa hafai kuishi.

Maneno yalienea kwa haraka sana, hata ikasemwa kuwa ametamka mwenyewe kuwa siye Masihi. Hivyo katika Galilaya habari kama hizo zikawa kikwazo kikuu kwake, kama ilivyokuwa

katika Uyahudi. Waisraeli walimkataa Mwokozi wao kwa sababu walitamani chakula kiharibikacho, sicho kidumucho hata uzima wa milele.

Kwa masikitiko makubwa, Yesu aliona kuwa wale waliokuwa wanafuzi wake wakirudi nyuma. Huruma zake hazikujaliwa, upendo wake umedharauliwa, wokovu wake umekataliwa. Jambo hili lilimsikitisha mno. hali kama hii ijimfanya kuwa, mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko. "Isaya

Bila kujaribu kuwazuia wale waliokuwa wakiondoka, yesu aliwageukia wale mitume kumi na wawili, akasema, "Ninyi pia mantaka kuongoka".

Petro alijibu akimwuliza hivi, "Bwana twende kwa nani? Wewe [218]
ndiwe una uzima wa milele. Nasi tumeamini kwa hakika kuwa wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai".

"Twende kwa nani? "Wanafunzi wamepata amani na utulivu wa kweli, tangu walipomwamnini Kristo, kuliko walivyokuwa hapo mwanzo. Watawezaje kwenda kwenye mizaha, watu watendao mabaya?

"Twende kwa nani" Katika giza la kutokuamini, katika uovu wa dunia? Petro alieleza imani ya wanafunzi wote waliyokuwa nayo. "Wewe ndiwe Kristo" Kuachana katika bahari yenye dhoruba.

Kila neno tendo la Yesu lilikuwa na kusudi maalumu, katika mpango wa wokovu. Wakati sisi tusipofahamu njia za Mungu, ni vigumu kufahamu mema yote Mungu anayoyaweka kwa ajili ya watu wake. Mtu anayeishi karibu na Yesu atafahamu huruma zake na kuona makusudi ya moyo wake.

## Upendo katika mambo yote

Yesu alijua kitakachotokea kwa maneno yake. Aliona kuwa maumivu yake katika Gethsemane, kuteseka kwake na kusulibiwa, mambo hayo yatawaumiza mno wanafunzi wake. Kama mambo magumu ya kujaribu, yasingalitokea, watu wengi wanaotukuza ubinafsi wangaliungana nao. Wakati Bwana angeteswa wengi waliokuwa wakimtukuza wangetiririka na kwenda zao, wakati makutano wangalisema "Msulibishe, msulubishem watu hawa wangalichomoka na kwenda zao. Mfano wa wale waliomwacha lazima

wamekumba na wengine pamoja nao. Lakini Yesu aliwafariji kwa wale waliosima imara kwake.

Mwokozi mwenye fadhili, ambaye akijua mambo yanayomngoja, bado analainisha njia ya wanafunzi wake, akiwaandaa kwa mtihani mzito ujao, na kuwatayarisha kwa majaribu ya mwisho.

## 42 — Kristo Atabiri Juu ya Maanguko [219]

Kazi ya wale mitume kumi na wawili ikiongezeka na kupanuka kwa kazi ya Yesu ilileta mwamko mpya wa wivu kwa waongozi wa Yerusalemu. Makuhani waliotumwa Kapernaumu hapo mapema mwanzoni mwa kazi ya Kristo, walitatanika vikubwa, lakini sasa wajumbe wengine walipelekwa huko ili kuchungua mwenedo wake na kazi yake wapate cha kumshitakia.

Kama ilivyokuwa hapo kwanza, ni kwamba makosa yake ni ya kutojali kushika mapokeo waliyofundishwa yanayolinda sheria. Kati ya mapokeo muhimu ambayo Yesu hakuyajali yalihusu sheria ya kawaida inayoelekeza kuja kwa Masihi, ambayo itafutika akija na kutimiza yote. Kutofuata sheria ya kunawa mikono kabla ya kula ilihesabiwa kuwa ni dhambi mbaya sana.

Maisha ya wale walioishika sheria ya Marabi, yalikuwa maisha ya matatizo matupu. Watu walipokuwa wakishughulika na kushika sheria hizo, maisha yao yalikuwa mbali sana na kanuni za sheria za Mungu.

Kristo na wanafunzi wake hawakuzijali sheria hizo za kunawa. Wale wapelelezi waliotumwa hawakuweza kumshambulia Yesu wazi, ila walipitia kwa njia ya wanafunzi wake. Walisema: "kwa nini wanafunzi wako wanavunja sheria za wazee? maana hula bila kunawa mikono yao."

Yesu hakujaribu kujitetea au kutetea wanafunzi wake. Aliwaonyesha tu, maana ya sheria hizo. Aliwapa mfano wa kuzikariri kwao; alisema: "ninyi mnaacha sheria ya Mungu, ilimshike sheria ya wanadamu. Maana Musa alisema Mheshimu baba yako na mama yako; amlaaniye baba yake au mama yake, na afe; lakini ninyi husema, mtu asemaye kwa babaye au kwa mamaye kuwa, mali hii ni wakfu, wala asimsaidie baba au mama, atakuwa huru, asimsaidie baba au mama mtu kutamka kuwa mali yake ni wakfu, [220]
wala isitumike siku zote za maisha yake, na akifa isitumike hekaluni, huko ni kumdhulumu babaye na mamaye, huku wakijisingizia kuwa ni wakfu.

Yesu alimsifu mjane maskini aliyetoa vyote kwa hekalu kuwa sadaka. Juhudi kubwa ya makuhani na marabi kwa kazi ya Mungu na uchaji wao, ilikuwa ni kujionyesha kwa nje kwamba wao ni watakatifu na watawa kamili. Hata wanafunzi wa Yesu pia hawakuachana kamili na hali ya mafarisayo na marabi. Yesu alijitahidi kuwaondolea hali hiyo mbaya watu wote wanaofanya kazi ya Mungu.

"Ninyi manafiki, ni vema Isaya alivyowatabiria ninyi akisema, "Watu hawa huniheshimu kwa vinywa vyao, na kwa midomo yao hufanya mapenzi mengi; lakini mioyo iko mbali nami. Nao huniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu." Kristo alisema kuwa kuweka maagizo yao yawe juu ya amri za Mungu, marabi walikuwa wakijitukuza juu ya Mungu, marabi walikuwa wakijitukuza juu ya Mungu, yesu alitamka kwamba unajisi hautokani na mambo ya nje, bali hutokana na mambo ya ndani. Usafi au uchafu hutoka moyoni.

## Ghadhabu ya Majasusi

Wanafunzi waliona ghadhabu ya majasusi na kusikia maneno yao ya chuki. Walimwambia Kristo wakitumaini kuwa atapatana nao. Walisema: "Hujui kuwa Mafarisayo walichukizwa, waliposikia usemi huu?"

Yesu aliwajibu: "Kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni, litang'olewa." Kila aina ya desturi na mapokeo ambayo hutukuzwa sana na Marabi, hayataweza kufaulu mtihani wa Mungu. Kila aina ya uvumbuzi wa kibinadamu uliowekwa kuwa badala ya sheria ya Mungu, "kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." Soma Mhubiri 12:14.

Hata katika wakristo kuna desturi zinazotumika, ambazo hazina msingi wa kweli, ni mapokeo tu ya wazee. Watu hung'ang'ania mapokeo na kuwachukia wale wanaowanyesha makosa. Leo tunapoambiwa kuziangalia amri za Mungu na imani ya Yesu, huona uhasama sawa na ule uliokuwako nyakati za Kristo. Kwa masalio wa Mungu imeandikwa: "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo ..." Ufunuo 12:17.

[221] Lakini "kila pando lisilipandwa na Baba yangu wa mbinguni

litang'olewa." Badala ya wale waitwao kuwa ni baba wa kanisa, Mungu hutuamuru tushike neno la Baba yetu wa mbinguni, Bwana wa mbingu na nchi. Hapa ndio kweli ilipo isiyochanganyika na uongo, "huniabudu bure, wakifundisha mafundisho ambayo ni maagizo va wanadamu."

[222] # 43 — Kristo Avunja Ubaguzi wa Mataifa

Baada ya mapambano yao na Mafarisayo, Yesu alitoka Kapernaumu, akavuka bahari ya Galilaya, akaenda pande za kaskazini kwenye mipaka ya Foeniki. Akiangalia upande wa kaskazini aliweza kuona miji ya zamani ya tiro na Sidoni; na mahekalu yao ya kimizimu. Ng'ambo yake kulikuwa na bahari ya mediteranean ambako wajumbe wa Injili watakwenda kuhubiri katika miji yake iliyo mikubwa ya ulimwengu. Akiona kazi iliyokuwa mbele yake, ilimlazimu kuwatayarisha wanafunzi wake watakaochukua kazi hiyo mpaka huko.

"Tazama mwanamke wa Kikanani kutoka katika sehemu hizo, alikuja akilia na kusema, Ee Bwana, mwana wa Daudi nihurumie; binti wangu anasumbuliwa na pepo mchafu." Watu wa sehemu hii walikuwa waabudu sanamu, ambao walikuwa wakidharauliwa na kuchukiwa na Wayahudi. Mwanamke aliyekuja kwa Yesu alikuwa mmizimu, kwa hiyo alikuwa ametengwa kwa fadhili zilizowastahili Wayahudi.

Kazi ya Kristo ilikuwa imeenea mpaka katika sehemu hiyo. Mwanamke huyu alikuwa amesikia habari za nabii, ambaye huponya magonjwa ya kila namna. Akiwa na tumaini hata kwa kuponywa binti yake, Akisukumwa na upendo wa mama, alikusudia kupeleka tatizo hilo kwa Yesu . Akaamini kuwa atamsaidia. kwa muda alijaribiwa kuona shaka, kwa kuwa huyu ni Myahudi. Lakini alisikia kuwa Yesu hajali, wala hashindwi na ugonjwa wowote. Watu wote humwendea akawaponya, matajiri kwa masikini.

Yesu alijua kuwa mwanamke huyu alitamani kumwona, kwa hiyo alijitenga katika njia yake. Kwa kumhudumia tatizo lake, alimpa fundisho alilokusudia. Kwa ajili ya hili aliwaleta wanafunzi katika sehemu hii. alitaka waone ujinga uliojaa katika miji
[223] na vijiji vilivyokuwa karibu na Israeli. Watu waliopewa nuru ya kweli, hawashughuliki kuwasaidia walio gizani. Ukuta wa ubaguzi uliojengwa na Wayahudi kwa kiburi chao, hata wanafunzi wa Yesu pia walizuiwa wasiwahudumie wenye shida kwa ajili ya ukuta wa

utengano. Kuta hizi za matengano, au ubaguzi lazima zivunjwe kabisa.

Kristo alipata wajumbe wake katika taifa lililodharauliwa, ambalo lilikuwa na hali dhaifu kabisa, ambayo ilionekana katika Wayahudi. Lakini mwanamke huyu hakuwa wa hali ya namna hiyo, alikuwa na imani. Wakati Yesu alipopita kana kwamba hasikii tatizo lake, yeye alimfuata akiendelea kuomba ombi lake, akiwaudhi wanafunzi kwa ombi lake, walimwambia Yesu amfukuze. Waliona kuwa Bwana wao anamfanyia uzembe, na kwamba hali ya ubaguzi baina ya Wayahudi na Wakanani ilikuwa ikimpendeza.

Lakini Mwokozi mwenye fadhili ndiye alijibu akisema: "Sikutumwa, ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." ijapokuwa jawabu hili lilionekana kana kwamba linaunga mkono hali ya ubaguzi waliokuwa nayo Wayahudi, lakini lilikuwa laumu kwa wanafunzi ambao baadaye walielewa na kukumbuka mambo aliyokuwa akiwaeleza kuwa alikuja ulimwenguni kuwaokoa wote watakaomwamini.

Mwanamke aliongeza kuomba, hali ameanguka miguuni mwake, na kusema: "Bwana nisaidie." Yesu akionekana kana kwamba anakataa ombi lake, alimjibu akisema: "Haifai kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa." Maana yake hasa ilikuwa kwamba, si vema kushughulikia wageni na kuwanyang'anya Waisraeli mibaraka waliyopewa na Mungu. Jibu hili lingalimkatisha tamaa mwombaji. Lakini mwanamke aliona kuwa hii ndiyo nafasi yake.

Katika hali iliyoonekana kana kwamba ni ya kukataa kwa Yesu, aliona fadhili kwake, ambazo hazikuweza kufichika, akasema: "Kweli, Bwana, hata mbwa hurambaramba makombo yaliyoanguka chini ya meza za bwana zao." hata mbwa hawaachwi bila kulishwa! Hivyo hata kama kuna mibraka mingi waliyopewa Waisraeli, je, haukuwapo mibaraka unaonistahili hata mimi? Aliangalia kama mbwa angaliavyo. Je mbwa hawezi kutazamia makombo? kama anahesabiwa kama mbwa, basi aliridhika kuwa kama mbwa, naye mara moja alimkiri Yesu kuwa Mwokozi awezaye kumfanyia yote aliyomwomba.

[224] **Imani katika Kristo ilimpatia hoja ya ajabu**

Mwokozi alitosheka na imani ya mwanamke huyu. Alikuwa ameijaribu imani yake. Aliona kuwa mtu aliyetengwa na kuhesabiwa kwamba ni mmizimu na Wayahudi, hakuwa jinsi hiyo, bali alikuwa mwana wa ufalme wa Mungu. Akiwa kama mtoto wa nyumbani, ilikuwa ni haki yake kushiriki mibaraka na zawadi zote za Mungu. Sasa Kristo alimpa haja yake akifunga fundisho lake kwa wanafunzi. akimgeukia mwanamke kwa uso wenye kung'aa na upendo mwingi, alisema: "Ee mwanamke, imani yako ni kuu, iwe kwako kama ulivyotaka." Tangu saa ile binti yake akapona. Mwanamke aliondoka akimtukuza Mwokozi wake, na kufurahi kwa ajili ya kupatiwa haja yake.

Yesu alikwenda pande za Tiro na Sidoni kwa ajili ya kufanya mwujiza huu. Alipenda kumsaidia mwanamke huyu, na wakati huo huo kuwapa wanafunzi wake kielelezo cha fadhili zake wakati atakapoondoka. Alitaka kuwazoeza namna ya kuwahudumia watu wasiokuwa wa kabila lao.

Yesu alipenda kushindilia ukweli halisi, kwamba watu wa mataifa pia wana haki ya kuwa warithi pamoja na Wayahudi, na washiriki wenzao katika ahadi za Mungu katika Kristo kwa njia ya Injili. Waefeso 3:6. Katika kumponya mtumishi wa akida, na kuhubiri huko Sikar, Kristo alithibitisha kuwa hakuna kitu kinachowahusu Wayahudi peke yao, bila wengine, na sasa Yesu aliwaleta wanafunzi wake wakutane na wamizimu ambao walidhaniwa kuwa hawana haki kutendewa mema yale wanayotendewa Wayahudi. Aliwaonyesha kwamba upendo wake hauna upendeleo kwa kabila au kwa taifa fulani tu.

Wakati aliposema kuwa, "Sikutumwa, ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli, alisema kweli. Mwanamke huyu alikuwa mmoja wao wa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli, ambaye alistahili kuokolewa. Kristo alikuwa akifanya kazi ile ambayo wao waliipuzia.

Kitendo hiki kilifungua fahamu za wanafunzi zaidi sana, kuhusu kazi iliyowahusu kuwafanyia watu wa mataifa. Waliona watu ambao hawashughulikiwi, ambao wanamhitaji Mwokozi, na kutaka neno la kweli. Baadaye ukuta huu wa ubaguzi ulipovunjika wakati Kristo

alipokufa, fundisho hili lilifahamika zaidi na zaidi, na wajumbe wa kristo walifanya kazi kubwa huko.

Kufika kwa Kristo huko Foeniki na mwujiza aliofanya huko [225] ulifanya mvuto mkubwa, na ulikuwa na makusudi maalum. Leo, hali ile ile ya majivuno na chuki vimejenga kuta kubwa sana za ubaguzi kati ya Watu wa namna mbalimbali. watu wengi wametengwa mbali na injili. Lakini wao wasijione kuwa wametengwa mbali na Kristo.

Kwa imani mwanamke wa Kifoeniki alivunja ukuta huo na kujitupa miguuni mwa Kristo bila kujali utengano ulioko kati ya Wayahudi na mataifa. Bila kujali chochote alijitupa katika upendo wa Mwokozi. Kristo anatutaka tumtumaini hivyo. Baraka za wokovu na kwa kila mtu. Hakuna kitu kinachomzuia mtu asishiriki baraka hizi, isipokuwa mtu mwenyewe achague kuzikataa.

Ubaguzi ni chukizo kwa Mungu. Machoni pa Mungu watu wote wanalingana kabisa. "Naye alifanya kila taifa la wanadamu . . . akiisha kuwawekea nyakati alizoamuru . . . " "Kwa maana hakuna tofauti ya Myahudi na Myunani; maana yeye yule ni Bwana wa wote, . . . kwa kuwa kila atakayeliitia Jina la bwana ataokoka." Matendo 17:26, 27; Warumi 10:12, 13.

[226] # 44 — Ishara ya Kweli

Huko Dekapoli mahali ambao mwenye pepo aliponywa, na wenyeji wakamlazimisha Yesu aondoke kwao. Lakini walikuwa wamewasikiliza wajumbe aliowaacha huko. Yesu alipokwenda katika sehemu hiyo tena, kundi kubwa lilikusanyika kwake, na mtu bubu na kiziwi aliletwa kwake. Yesu akimtenga kando, aliweka vidole vyake katika masikio yake, na kuugusa ulimi wake. Alipiga kite kana kwamba masikio hayo hayatafunguka ili kuisikia kweli, na ulimi umeikataa kweli; na kumkataa Mwokozi. Aliposema, "Funguka", mtu akapona.

Yesu akapanda mlimani, na huko makutano walimkusanyikia, wakiwaleta wagonjwa wao na vilema, akawaponya wote. Watu walimtukuza Mungu ingawa walikuwa wamizimu. kwa muda wa siku tatu walikuwa na Mwokozi, huku wakilala nje mbugani tu, wakiwa na hamu ya kuyasikiliza maneno ya Mwokozi, na kuziona kazi zake.

Baada ya siku tatu kupita chakula walichokuwa nacho, kiliwaishia. yesu asingaliwaaga waende zao, na njaa, kwahiyo akawaambia wanafunzi wake wawapatie chakula. Huko Bethsaida waliona jinsi chakula kidogo kilivyotosha kuwalisha makutano mengi, walakini sasa hawakuweza kukumbuka mambo hayo na kutoa chochote walichokuwa nacho, ili kwa uwezo wake kitoshe kuwalisha watu. Lakini hata wakati huu wanafunzi walionyesha imani haba. Watu waliolishwa huko Bethsaida walikuwa Wayahudi, lakini hawa ni watu wa mataifa. Hali ya ubaguzi ilikuwa bado kali kwa wanafunzi. Kwa hiyo walisema: "Tutapata wapi chakula cha kutosha watu wote hawa nyikani hapa?"

Lakini kwa kutii neno lake, walileta walichokuwa nacho, ambacho ni mikate saba na samaki wawili. Basi hivi viliwalisha makutano, na kubakiza makapu saba. Jumla ya watu walikuwa wanaume elfu nne, bila kuhesabu wanawake na watoto.

[227] Kisha Yesu na wanafunzi wake walivuka ziwa mpaka Magdala. Sehemu hii ya Tiro na Sidoni roho yake iliburudika kwa habari ya

mwanamke wa Kifoeniki. Watu wa mataifa wa Nikapoli wamempokea kristo kwa furaha. Sasa walipofika tena Galilaya, ambako kazi zake nyingi zilifanyika, alipokewa kwa unyonge sasa.

## Ukoo wa utawala watoa changamoto kwa Kristo

Madhehebu mawili, yaani Mafarisayo na Masadukayo, walikuwa maadui wakubwa sana wa Kristo. Wao walikuwa wakitaka kuona ishara kutoka mbinguni. Wakati Waisraeli walipopigana na wakanaani huko Bethhoroni, jua lilisimama wakati Yoshua alipomwomba Mungu iwe hivyo. Ishara ya aina hiyo ilitakiwa pia wakati wa Yesu, lakini hakuna ishara yoyote ingaliwafaa, kama ushahidi wa Yesu kwamba ni Masihi.

Yesu alisema: "Enyi wanafiki, mnaweza kutambua nyakati, za majira." Kwa kuchunguza wanaweza kutabiri nyakati. "Lakini hamwezi kutambua ishara za wakati?" Maneno ya kristo yalinenwa kwa nguvu na uwezo wa Roho Mtakatifu, hayo ndiyo ishara iliyotolewa na Mungu, wimbo ulioimbwa na malaika kwa wachungaji, nyota iliyowaongoza mamajusi, sauti iliyotoka mbinguni wakati wa ubatizo wake, ulikuwa ushahidi kamili wa kumshuhudia Yesu kuwa ni Masihi.

Yesu akahuzunika rohoni mwake, akasema, akasema, "Kwa nini kizazi hiki chataka ishara?" "Hakitapata ishara, ila ni ile ishara ya nabii yona." Jinsi mahubiri ya Yona yalivyokuwa ishara kwa watu wa Ninawi, vivyo hivyo mahubiri ya Kristo yalikuwa ishara kwa kizazi chake. Lakini ni tofauti kiasi gani ya mapokeo ya neno la Mungu! Watu wa mataifa katika mji mkuu wa Ninawi walijinyenyekeza mbele za Mungu, wakubwa na wadogo walimlilia Mungu wa mbinguni wakahurumiwa.

"Watu wa Ninawi watasima siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki", asema Yesu, "nao watawahukumu, kuwa wamekosa kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona." Mathayo 12:41.

Kila mwujiza uliofanywa na Kristo, ulikuwa ishara ya Uungu wake, lakini kwa Mafarisayo ilikuwa machukizo. Viongozi wa Wayahudi waliangalia dhiki ya watu kwa mioyo ya kutojali. Kwa hiyo katika kazi nyingi za Kristo za kuwasaidia wenye dhiki hao

zilikuwa kikwazo kwao. Hivyo miujiza yote ya Yesu ya kuponya watu, kwao ilikuwa kazi bure tu.

[228] **Ushahidi wa kweli, kwamba Kristo alitoka kwa Mungu**

Kilichosababisha Wayahudi wamkatae Kristo ni ule uthibitisho wa tabia yake ya Uungu; na miujiza yake ambayo ilihusu msaada wa watu wenye dhiki. Maisha yake yalidhihirisha tabia ya Mungu, alifanya kazi ya mungu na kunena maneno ya Mungu, maisha ya jinsi hiyo mwujiza mkuu kuliko miujiza yote.

Siku zetu hizi, watu wengi hupiga kelele na kusema, 'Tuonyeshe ishara,' au fanya miujiza sawa na watu wa kale, yaani Wayahudi. Kristo hatupi uwezo wa kujionyesha jinsi tulivyo, au kufanya mambo ya kuridhisha watu na kutufanya tujivune. Je, miujiza mikuu siyo ile ya kuvunja nguvu za Shetani zisitutawale? Uadui wetu na Shetani sio wa kuumbika, ila ni wa kuondoleka kwa neema ya Mungu. Mtu anayetawaliwa na hali ya upotovu, anapojitoa kwa Mungu hutawaliwa na hali ya unyofu, huo ni mwujiza umefanyika. Ndivyo ilivyo pia kwa mtu anayeishi katika hali ya udanganyifu, azindukapo na kuifahamu kweli. Mabadiliko ya moyo na kurekebika kwa tabia ya mtu ni mwujiza unaodhihirisha kuwa Mwokozi anaishi ndani yake. Katika kuhubiri neno la Mungu ishara inayodhihirika hapo ni kuwako kwa Roho Mtakatifu, ili kuotesha neno hilo na kulikuza; katika maisha ya walioliamini.

Wale wanaotamani ishara kutoka kwa Yesu walikuwa wameshupaza mioyo yao. Walikuwa hawaoni kuwa kazi yake ilikuwa imetabiriwa na Biblia, na ilikuwa ikitimizwa. "Akawaambia, Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu." Luka 16:31.

Yesu akiwaacha wapinzani wake, aliingia mashuani pamoja na wanafunzi wake, wakavuka ziwa wakiwa na masikitiko makubwa. Walipofika ng'ambo, yesu alisema: "Jihadharini na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo." Wayahudi wamefundisha kwamba chachu ni mfano wa dhambi. Katika kuondoka kwa ghafla kutoka Mgdala, wanafunzi walisahau kuchukua mikate. Walidhani kuwa Yesu alikuwa akiwaonya wasinunue mikate ya Mafarisayo, au Masadukayo. Hali yao ya upungufu wa kiroho ulikuwa ukiwafanya kila mara kutoelewa maana ya maneno ya Yesu.

Sasa Yesu alithibitisha jinsi alivyowalisha watu maelfu kwa mikate michache na samaki wachache. Akawaambia kuwa hakumaanisha chakula cha mwili. Kulikuwa na hatari ya udanganyifu wa Mafarisayo na Masadukayo, ambao ungewadhuru wanafunzi katika imani yao. Wanafunzi walizidi kudhani kuwa Bwana wao angewapa ishara ya mbinguni kama ilivyotakiwa. Alikuwa na uwezo kufanya hivyo, na ishara hiyo ingewanyamazisha wabishi wake. Wanafunzi [229]
hawakufahamu unafiki wa wapinzani hao. Baada ya miezi mingi kupita, kristo alirudia kufundisha fundisho hilo. . . Jilindeni na chachu ya Mafarisayo, ambayo ni unafiki." Luka 12:1

## Kujidanganya kwa ubinafsi

Chachu hufanya kazi yake bila kuonekana, ikichachua chakula kwa jinsi yake. Vivyo hivyo hali ya unafiki ikikubalika huchachua tabia na kuharibu mtu. Waandishi na mafarisayo walifunika hali halisi ya mafundisho ya Biblia, wakatia polepole mambo mengine na kuyatia katika nia zao. Mfumo huu wa udanganyifu husababisha ugumu wa kuamini mameno ya Kristo.

Hali hiyo hiyo huwadanganya watu wale wanaojaribu kuitafsiri sheria ya Mungu ifuate mawazo yao, na matendo yao. Watu hawa hawaishambulii sheria ya Mungu waziwazi, ila hufiriri mawazo yaliyo ya hatari kuwa kama kanuni ya hali yao. Hueleza hivyo ili kuharibu maana yake.

Unafiki wa Mafarisayo ulikuwa matokeo ya kujitafutia ubwana. Hivyo waliongozwa kupotosha Maandiko Matakatifu. Uovu huu wa kijanja hata wanafunzi pia waliupendelea. Wafuasi wa Yesu, kwa sehemu kubwa walivutwa na madhumuni ya Mafarisayo, kuhusu kuamini au kutoakuamini. Hata wanafunzi pia walikuwa wakipenda kujitafutia umaarufu. Roho ya namna hii ilisabaabisha mashindano, kwamba, ni nani atakuwa mkuu zaidi. Jambo hili liliwafanya kuwa wadogo sana machoni pa Kristo ambaye ni mwenye maisha ya kuinyima. Jinsi chachu ilivyoharibu, ndivyo hivyo, kujitafutia umaarufu, kunapopendelewa, huchafua, na kuharibu mtu.

Leo, kama ilivyokuwa zamani, dhambi hii ya kujitakia ukubwa, imeenea kiasi gani! Watu wao tayari kiasi gani kuandamia hali ya kutaka umaarufu na upendeleo wa watu! Upendo wa ubinafsi, kutamani anasa na kupingana na kusudi la Mungu, na njia alizoweka,

mambo hayo husababisha kuhafifisha neno la Mungu na kutukuza mawazo ya binadamu zaidi ya mpango wa Mungu.

Dini ya Kristo ndiyo inayoelekezwa na Roho Mtakatifu, uwezo wa Mungu peke yake ndio unaoweza kuondoa ubaya wote, na unafiki. Badiliko hili huja kwa mtu kwa ajili ya kazi yake, yaani kwa njia ya Roho wake Mtakatifu, wakati imani tunayoamini inapokuwa ya hakika, haharibu upendo wa ubinafsi na kujipendekeza ambako si kweli. Hivyo sisi hutafuta utukufu wa Mungu, wala sio mapenzi
[230] yetu. Hali hiyo ikitokea tunaweza kujua kuwa tuko katika njia ya kweli. Kusudi la Kristo lilikuwa, "Baba, ulitukuze jina lako ..." Yohana 12:28. Na sisi tunapomfuata Yeye, hili Utakuwa kusudi letu pia.

## 45 — Kuonyeshwa Mbele Fumbo la Msalaba [231]

Hata kabla Kristo hajafanyika kuwa binadamu, aliona njia nzima atakayopitia ili kuwaokoa waliopotea. Kila aina ya kichomi kitakacho-mwumiza, kila aina ya ghasia atakayosukumiwa, kila aina ya dhiki atakayopitia vyote hivyo aliviona kabla hajakumbana navyo. Wakati huo alikuwa angali hajavua utukufu wa Enzi yake, na kujitwalia hali ya kibinadamu pamoja. Wakati huo alisema: "Tazama nimekuja, (Katika gomho la chuo nimeandikiwa,) Kufanya mapenzi yako Ee, Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam sheria yako imo moyoni mwangu." Zaburi 40:7, 8.

Maisha yake katika ulimwengu huu yaliyojazwa na hali ya kazi ngumu, na kujinyima, yaliburudishwa na jambo hili, kwamba kwa kujitoa maisha yake hivyo atarudisha ulimwengu katika umoja na Mungu. Ingawa ni lazima ipitie kwenye ubatizo wa damu, ingawa ni lazima abebe mzigo mzima wa dhambi za ulimwengu wote, ingawa atapita katika ole usiosemeka; walakini kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake, aliustahili msalaba.

Wakati ulikaribia alipowachagua wenzi wake katika kazi lazima wamwone yule wampendaye akiangikwa msalabani huko Kalwari. Karibuni atawaacha wakikabiliana na ulimwengu bila yeye kuwapo pamoja nao. Watateswa na watu wanaowachukia, ambao hawataki kuamini kwa hiyo alitamani kuwatayarisha vizuri kukabiliana na majaribu.

Sasa Yesu na wanafunzi wake walifika katika mji wa Kaisaria-Filipi. Walikuwa ng'ambo ya Galilaya, mahali umizimu ulikuwa ukistawi sana. Kuwazunguka kulikuwa na hali ya ukafiri na ushirikina unaoenea ulimwenguni pote. Yesu alitaka mambo ya namna hii yawatie moyo wa kuuhurumia ulimwengu, na kujitia kikamilifu katika kazi ya kuhudumia watu wa mataifa.

Alikuwa karibu kuwaeleza kuhusu mateso yanayomkabili. Lanili [232]
kwanza aliwaombea ili mioyo yao iweze kuyapokea maneno hayo. Hakuanza kuwaeleza mambo hayo mara moja, ila aliwapa nafasi kwanza ya kuthibitisha imani yao kwake. Kea hiyo aliwauliza

akisema: "Watu huninenaje mimi, Mwana wa Adamu, kwamba ni nani?"

Wanafunzi walisema kwa masikitiko kuwa Waisraeli wameshindwa kumtambua Masihi. Makutano huko Bethsaida walitamani wamtawaze awe mfalme wa Israeli. Watu wengi walikuwa tayari kumkubali kwamba ni nabii, lakini hawakumkubali kwamba ni Masihi.

Sasa Yesu aliuliza swali la pili, linalowahusu wao: "Na ninyi huninena mimi kuwa ni nani?" Petro alijibu, "Wewe ni Kristo Mwana wa Mungu aliye hai."

Tangu mwanzo Petro alikuwa amemwamini Yesu kuwa ni Masihi. Wengi wa waliomwamini yesu kuwa ni Masihi. Wengi wa waliomwamini walianza kuwa na mashaka kwa kazi ya Yohana Mbatizaji wakati alipotiwa gerezani, na kuhukumiwa kifo. Wakawa na mashaka kuwa yesu siye masihi. Wengi waliomdhania kuwa atatawala katika kiti cha Daudi, walianza kuondoka walipoona kuwa hana kusudi hilo. Lakini kusitasita kwa wale waliokuwa wakitangatanga hakukuweza kuharibu imani ya watu wa kweli. Petro alitamka: "Wewe ni Kristo Mwana wa Mungu aliye hai." Hakungojea mpaka atawazwe kwanza, ila alimwamini katika unyenyekevu wake.

Petro alikuwa ameeleza imani badala ya wanafunzi wote, kwamba wanamkiri Yesu kuwa ndiye Masihi. Walakini upinzani wa Makuhani na wakuu wa Kiyahudi uliwapa wasiwasi sana. Hata hawakujua mahali pa kuendea. Mafundisho waliyofundishwa na Marabi hapo kwanza, na msisitizo wa kufuata mapokeo vilipingana na ukweli. Nuru ya kweli ilikuwa imeng'aa mioyoni mwao walakini walifanana kama watu wanaopapasa-papasa gizani. Lakini siku hiyo Roho Mtakatifu aliwavuvia mioyoni mwao. Badala ya kubahatisha kibinadamu, walifunuliwa dhahiri na utukufu wa Mwana wa Mungu.

Yesu alimjibu Petro akisema: "Heri wewe simon Bar Yona; maana mwili na damu havikukufunulia, ila Baba yangu aliye mbinguni."

Ukweli uliosemwa na petro ndio msingi wa imani ya kila mwongofu. Lakini hakufunuliwa kwa ajili ya hekima yake, wala wema wake. Kwa kuwa Petro alitambua utukufu wa kristo, hilo lilithibitisha kuwa amefundishwa na Mungu. Soma Zaburi 25:14; Yohana 6:45.

Yesu aliendelea kusema: "Nakuambia tena, wewe ndiwe Petro, na juu ya Mwamba huu, nitalijenga kanisa langu, na milango ya kuzimu haitalishmda." Neno Petro linamaanisha ji we linalovingirika. Petro hakuwa Mwamba ambao Yesu atajenga kanisa lake. Milango ya kuzimu ilimshinda wakati alipomkana Bwana wake kwa kulaani na kuapa. Kanisa lilijengwa kwa yule ambaye milango ya kuzimu haikumshinda. [233]

## Kristo ndiye Mwamba

Musa alikuwa ameonyesha mwamba wa wokovu wa Israeli. Tazama Torati 32:4. Zaburi imeimba juu ya "Mwamba wa nguvu zangu." Zaburi 62:7. Isaya alikuwa ameandika: ". . . Tazama naweka katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, . . . Isaya 28:16. Petro mwenyewe aliutaja unabii huu kumhusu Yesu. Maana ninyi mmeonja wema wa Bwana. Njooni kwake, ambaye ndiye jiwe lililo hai, lililokataliwa na watu, lakini kwa Mungu ni jiwe teule, lenye thamani. Na ninyi kama mawe yaliyo hai, mmejengwa katika hekalu la kiroho. Soma 1 Petro 2:3-5.

"Maana msingi mwingine hakuna awezaye kuuweka isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo." 1 Wakorintho 3:11. Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu, nitalijenga kanisa langu." Kristo alijenga kanisa lake juu ya mwamba yaani juu yake mwenyewe, mwili watte, umevunjwa kwa ajili yetu. Juu ya kanisa lililojengwa juu ya msingi wake mwenyewe, milango ya kuzimu haitalishinda.

Wakati Kristo aliposema maneno haya kanisa lilionekana kuwa dhaifu kiasi gani ulimwenguni! Kulikuwa na wafuasi wachache sana, ambao watakabiliana na nguvu za Shetani na wanadamu pia. Walakini hawataogopa, hakuna kitu kitakachowashinda.

Petro alikuwa amesema ukweli ambao ni msingi wa kanisa na imani yake, na Yesu alimsifu kama mjumbe wa kweli badala ya kundi la waamini wote. "Nami nitakupa funguo za ufalme wa mbinguni: Lolote utakaolifunga duniani Utakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni."

"Funguo za ufalme wa mbinguni, ni maneno ya Kristo. Maneno yote ya Biblia ni yake. Maneno haya yana nguvu za kufungua na kufunga mbingu. Kazi ya wale wanaohubiri neno la Mungu huleta uzima au mauti.

[234] Mwokozi hakumkabidhi kazi Petro, kama mtu binafsi, yaani kazi ya kuhubiri Injili. Baadaye aliporudia kusema maneno hayo tena yaliyosemwa kwa Petro, Mwokozi aliyasema kwa kanisa zima, na kwa mitume kumi na wawili ambao walikuwa wawakilishi wa kundi zima la kanisa. Kama Yesu angalimkabidhi mtu mmoja ujumbe maalum zaidi ya wengine wote, tusingeona wakibishania ukubwa. Wangalimheshimu mtu aliyekabidhiwa tu. Badala ya kumteua mtu mmoja kuwa mkuu wao, Kristo alisema: "Msiitwe Rabi, . . . wala msiitwe mabwana, maana Bwana wenu ni mmoja tu, ndiye Kristo." Mathayo 23:8, 10.

Kichwa cha kila mtu ni Kristo. Mungu aliweka vitu vyote chini ya miguu ya Mwokozi, akamweka awe kichwa cha mambo yote kanisani, ambalo ni mwili wake, ambaye ni utimilifu wake katika mambo yote. Soma 1 Wakorintho 11:3; Waefeso 1:22, 23. Kanisa limejengwa kwa Kristo, aliye msingi wake. Kanisa haliwezi kumtegemea mtu, au haliwezi kutawaliwa na mtu. Watu wengi hudhani kuwa cheo walicho nacho kanisani, huwafanya wawe wenye uwezo wa kuwaamuru washiriki jinsi ya kufanya. Mwokozi alisema, Ninyi nyote ni ndugu, tazama Mathayo 23:8. Hakuna mtu yeyote au kiumbe chochote tunachoweza kutegemea ili kituongoze. Mwamba wa imani ni kuwako kwa Kristo kanisani. Wanaojidhania kuwa wana nguvu, wataonekana kuwa ni wanyonge mno, wasipomweka Kristo kuwa nguvu zao. Soma Yeremia 17:5; Zaburi 2:12.

Yesu aliwagiza wanafunzi wake kwamba wasimwambie mtu yeyote kuwa wao ndio Kristo. Watu walikuwa na mawazo ya makosa kumhusu Masihi. Hata wanafunzi wake pia hawakuwa na ufahamu wa wazi. Mawazo ya watu na usemi wao ungewakosesha wasitambue tabia yake, na kazi yake.

## Wanafunzi hawakutazamia juu ya kuja kwa msalaba

Wanafunzi walikuwa bado wanamtazamia kuwa Yesu atatawazwa kuwa mfalme wa nchini. Waliamini ila walitazamia wakati atakaosimamisha ufalme wake. Wazo ya kwamba, Kristo atakataliwa na

watu, na kushitakiwa kama mhaini na kuuawa juu ya msalaba, wazo kama hili halikuingia katika mioyo ya wanafunzi. Basi Yesu lazima awadhihirishie wanafunzi wake mambo hayo ijapokuwa ni ya huzuni.

Mpaka sasa alikuwa hajawafunulia wanafunzi wake kuhusu mateso na kifo chake. Katika maongezi yake na Nikodemo alikuwa amesema: "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, [235]
vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa, ili kila mtu amwaminiye awe na uzima wa milele katika yeye. Yohana 3:14. Lakini wanafunzi hawakuyasikia hayo. Sasa muda umefika, ambao pazia lililofunika mambo ya usoni litafunuliwa. "Tangu wakati huo na kuendelea Yesu alianza kuwafunulia wanafunzi wake, jinsi atakavyokwenda Yerusalemu, na kutesemka kwa mambo mengi mikononi mwa wazee na wakuu wa makuhani na waandishi, na halafu kufa, baadaye kufufuka katika siku ya tatu".

Wanafunzi wake walisikiliza kwa mshangao bila kusema neno. Yesu alikuwa amekubaliana na usemi wa Petro kuwa ni Mwana wa Mungu, na sasa kufuatana na maneno yake kuhusu mateso, yalionekana kutofahamika. Petro hakuweza kunyamaza, alimvuta Bwana wake kando akasema kuhusu Mambo haya yapitie mbali Bwana yasiwe karibu nawe".

Petro alampenda Bwana wake, lakini Yesu hakumsifu kwa ajili ya kumtakia mema, asipatwe na mateso. Maneno ya Petro hayakuwa na msaada wowote wala ufumbuzi wataabu inayomkabili. Maneno hayo hayakupatana na kujitoa ambako yesu alikuja kuwafundisha watu kwa kielelezo chake mwenyewe. Maneno Petro aliyosema yalikuwa kinyume cha mambo ambayo Kristo alikusudia kuwaonyesha wafuasi wake. Kwa hiyo Mwokozi alipaswa kutamka maneno makali ya kukemea ambayo yalikuwa hayajatoka kinywani mwake. "Nenda nyuma yangu, Shetani! kwani u kinyu;me changu. Maana huko upande wa Mungu, ila upande wa watu".

### Shetani alikuwa akijaribu kumfikia Kristo

Shetani alikuwa akijaribu kunikatisha Yesu tamaa na kumfanya aache kazi yake, na Petro alikuwa akitoa sauti ya jaribu. Mkuu wa maovu , aliyekuwa mwenye wazo hilo lililotamkwa na Petro, ndiye alikuwa mwenye kusudi hilo. Shetani alikuwa amemwambia Kristo

kuwa atampa milki zote za dunia kwa sharti la kuacha njia yake ya kujinyima na kujidhili. Sasa alitaka Petro akaze macho yake juu ya utukufu wa ulimwengu, ili asiutazame msalaba. Alimjaribu Yesu kwa njia ya Petro.

Lakini Mwokozi hakulijali jambo hilo, mawazo yake yalikuwa juu ya wanafunzi wake. Shetani alijiingiza kati ya Petro na Bwana wake. Maneno ya Kristo yalisemwa kwa mtu anayejaribu kutenda mtu na Mwokozi wake. "Nenda nyuma yangu, Shetani." Wacha nikabiliane na Petro, nipate kumdhihirishia upendo wangu.

[236] Hilo lilikuwa fundisho chungu ambalo Petro alifundishwa, lakini pote pote. Njia ya Kristo ni ya maumivu na unyenyekevu. Lakini ni katika tanuru la moto, ndipo wanafunzi wataona mibaraka yake. Zamani alikuwa ameandika: "Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe" 1 Petro 4:13.

Sasa Yesu aliwaeleza wanafunzi wake kuwa maisha yake ya kujinyima,, na ya kimaskini, ni kielelezo cha maisha ambayo lazima waishi. Alisema: "Mtu yeyote atakaye kunifuata lazima ajikane nafsi yake, ajitwike msalaba wake kila siku anifuate." Msalaba ulikuwa ukitumika katika utawala wa Kirumi. Ulikuwa kitu cha uchungu sana, na kifo chake kilikuwa cha ukatili kuliko vyote. Wahalifu waliohusika kwa kifo cha msalaba, iliwapasa kujichukulia msalaba mpaka mahali pa kusulubiwa. Kila mara walipobebeshwa misalaba walifurukuta sana na kutaka kujiokoa. Maneno ya Kristo kwa wanafuzi wake ingawa waliyafahamu kigizagiza, yaliwaonyesha mauti ya Kristo.

Maneno ya Kristo hayakuonyesha zaidi ya hali ya kujitoa kuliko hayo. Lakini hayo yote yalimpasa kwa ajili yao. Aliacha maisha ya mbinguni , akaja kuishi katika hali hafifu na ya matatizo, na mwisho kufa kifo cha aibu. Aliyekuwa wa fahari zote za mbinguni akawa maskini, ili kwa umaskini wake, tupate kuwa matajiri. yatupasa kufuata hatua alizopitia.

Upendo wa aroho za watu, maana yake ni kuisulubisha nafsi. Mtu aliye mtoto wa Mungu, angejiona kuwa yeye ni kiungo katika mnyororo wa kuongoa roho zilizopotea. Mkristo amejitoa nafsi yake kwa Mungu, na katika tabia yake humdhihirisha Kristo ulimwenguni.

"Mtu atakayejitahidi kujiokoa mwenyewe atajipoteza, na atakayejitoa nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili atajiokoa" Ubinafsi ni mauti. Moyo ukishindwa kusukuma damu mpaka mikononi au kichwani, utapoteza nguvu zake upesi. Hivyo ndivyo ilivyo na upendo wa Kristo huenea katika mwili mzima. Sisi tu viungo kila mtu kwa mwenzake, na mtu anayekataa kushirikisha imani yake atapotea. "Itamfaidia nini mtu, kuupata ulimwengu wote, na kupoteza nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?"

Kristo alionyesha kuja kwake katika utukufu kwa wanafunzi wake, akija na majeshi ya mbinguni, halafu Yesu alisema" Atakuja kumlipa kila mtu kadiri ya kazi yake ilivyo." Kwa kuwatia moyo alisema:"Amini nawaambieni, kuna watu wasimamao hapa ambao [237]
hawataonja mauti mpaka watakapomwona Mwana wa Adamu akija kaatika ufalme wake."

Lakini wanafunzi wake hawakuelewa maneno yake, mambo yao yalikuwa yakiuangalia umaskini wake, unyenyekevu wake, na mateso yake. Je, hawatamwona BWANA wao akitawazwa katika kiti cha enzi cha Daudi? Je, badala ya kutawazwa, inawezekana kwa Kristo kukataliwa na watu, na kuuawa? Huzuni iliwajaa mioyoni mwao; maana ilionekana kitu acha ajabu kuwa Mwana wa Mungu kupita katika matatizo ya namna hiyo. Kwa nini ajihatarishe kwenda Yerusalemu kukabiliana na mambo kama hayo? Kwa nini ajitolee kuingia katika hali hiyo, na kuwaacha wanafunzi wake gizani, wakihangaika katika mashaka kama vile walivyokuwa kabla ya kujua?

Katika mkoa wa Kaisaria Filipi wanafuzi waliongea kwamba, Kristo hana la kuongopa juu ya Wayahudi, au juu ya Warumi. Mbona asifanye kazi hapo tu? Mbona ajitolee mwenyewe kwenda kufa? Ilakuwaje kuwa atausimamisha ufalme ambao milango ya kuzimu haitaushinda? Jambo hili ni fumbo.

Sasa walikuwa safarini wakienda katika mji ule ambako wataona masikitiko makuu. Walikuwa wakizungumza polepole, kwa mioyo mizito kuhusu mambo yaliyo mbele yao. Labda jambo fulani litatokea la kuzuia mambo haya. Hivyo walikuwa na wasiwasi, wakiogopa mambo yatakayotokea katika siku sita za giza zijazo.

## [238] 46 — Yesu Ageuka Sura

Jioni ilikuwa imesogea wakati Yesu alipowaita Petro, Yakobo na Yohana, akapanda nao juu mlimani. Mchana kutwa walikuwa wakisafiri na kufundisha watu, kwa hiyo kupanda mlimani kulizidi kuwaongezea uchovu wao. Muda kitambo jua likachwa; wakaingia gizani. Hali ya giza na ukiwa ikafanana na jinsi maisha yao yalivyo. Mawingu yalikuwa yakikusanyika.

Wanafunzi hawakuthubutu kumwuliza Kristo mahali alipokuwa akienda, au kwa nini wamepanda mlimani. Kila mara alikuwa akienda mlimani kuomba, wakati mwingine akikesha huko usiku kucha. Huko mlimani na msituni alifurahishwa sana na hali ya utulivu huo. Lakini wanafunzi walishangaa kuwa kwa nini wanasumbuka kupanda mlimani na hali walikuwa wamechoka katika safari.

Mara Yesu aliwaambia kuwa safari yao imefika mwisho wake. Akijitenga kidogo nao; mtu wa huzuni akajibwaga katika maombi. Aliomba sana kwa machozi, akiomba uwezo wa kuvumilia katika hali yake ya kibinadamu. Ilimpasa aambatane na Mwenyezi, ndipo aweze kukabiliana na mambo ya siku za usoni. Aliwaombea Sana wanafunzi wake, ili imani yao isitikisike. Alipata umande mwingi usoni mwake, lakini hakujali. Hivyo saa zilipita taratibu.

Mara ya kwanza wanafunzi wake walishirikiana naye maombini, lakini baada ya kupita muda kidogo walilala. Yesu alikuwa amewaeleza kuhusu mateso yanayomkabili, naye aliwatia moyo kwamba imani yao siyo ya bure. Sio wote hata kati ya wanafunzi wake kumi na wawili, watakaopata njozi ya hakika kuhusu mambo yake. Ni wale walioona na kushuhudia huzuni yake katika Gethsemane
[239] tu, ndio aliopanda nao mlimani. Na sasa maombi yake yalikuwa kwamba washuhudie maonekano yake ya baadaye kabla ya matatizo makuu yanayomjia, ili wajue kwamba yeye kweli ni Mwana wa Mungu, na kwamba kifo cha aibu atakachokufa ni mpango wa wokovu.

Sala yake ilisikiwa. Ghafla mbingu zilifunguka, na mng'ao mtukufu uling'aa mlimani. Mwokozi akazungukwa na utukufu uliong'aa kwa ajabu. Uso wake ukang'aa. Uungu ukaangaza katika ubinadamu, na utukufu wa mbinguni ukaangaza kwake. Alipoondoka kutoka katika hali ya kuomba, Kristo alisirnama katika hali ya Uungu kamili katika fahari yake. Uso wake ulifanana kama jua, na mavazi yake yakawa kama nuru kwa weupe wake.

Wanafunzi walipoamka, na kumtazama Bwana wao anavyong'aa waliogopa. Walishikwa na mshangao usiosemeka. Walipozoeana na utukufu huo na nuru hiyo ya ajabu, waliona watu wawili wa mbinguni, yaani Musa na Eliya. Musa aliyezungumza na Mungu katika mlima wa Sinai. Eliya aliyepewa hadhi ya kutoonja mauti, akachukuliwa mbinguni bila kufa.

Musa hakuweza kuingia Kanani kwa ajili ya dhambi aliyofanya huko Meriba. Safari ya kuwaongoza Waisraeli kwenda katika nchi ya urithi wa baba zao, haikuwa yake. Kufia jangwani kulikuwa ni shabaha ya miaka arobaini ya safari ya matatizo, na uangalizi. Musa alipitia mauti, lakini hakubakia ndani ya kaburi, Kristo mwenyewe ndiye aliyemwita kutoka kaburini. Tazama Yuda 9.

Musa katika mlima ule waliomtokea Yesu, aliwakilisha watu wenye haki, watakaofufuka katika ufufuo wa kwanza. Eliya aliyechukuliwa kwenda mbinguni bila kuonja mauti, anawakilisha watakatifu watakaotwaliwa wakati wa kurudi kwake Yesu mara ya pili bila kuonja mauti; watakaobadililishwa kufumba na kufumbua, wakati wa tarumbeta ya mwisho. I Wakorintho 15:51, 52. Yesu alikuwa na utukufu ule atakaokuwa nao atakapokuja mara ya pili. Utukufu wa Baba yake na wa malaika watakatifu. Marko 8:38; Waebrania 9:28. Katika mlima, kulionyeshwa mfano wa ufalme utakaokuja, lakini kwa kifupi, Kristo Mfalme, Musa, mfano wa watakatifu watakaofufuliwa, na Eliya badala ya watakaochukuhwa bila kuonja mauti.

## Petro alichanganyikiwa

Wanafunzi walifurahi kwamba Bwana wao aliyekuwa kama mtu aliyepotea, mpole, akitangatanga tu katika hali ya ufukara, sasa ametukuzwa na utukufu wa mbinguni. Waliamini kuwa Eliya amekuja kutangaza kusimamishwa kwa, ufalme hapa duniani. Kwa [240]

hiyo walitaka kukaa hapa. Petro alitamka, "Bwana, ni vizuri sisi kukaa hapa, na tujenge nyumba tatu; moja yako, moja ya Musa na moja ya Eliya.' Wanafunzi waliamini kwamba Musa na Eliya wametumwa kuja kumlinda Bwana wao na kumsaidia kuimarisha ufalme wake.

Lakini ni kwamba, kabla ufalme haujasimamishwa, kwanza lazima uje msalaba. Yesu akivaa ubinadamu, akibeba mzigo wa huzuni zote na dhambi zote za wanadamu alitembeatembea kati ya wanadamu. Kadiri giza la mateso lililokuwa likimkabili, alikuwa na sikitiko kuu la rohoni, hasa akiwa katika ulimwengu usiomjua, hata wanafunzi wake wapendwa hawakuelewa kazi yake ulimwenguni. Katika ulimwengu aliouumba alikuwa mgeni kabisa asiyejulikana. Sasa mbingu ilikuwa imetuma wajumbe ambao si malaika, ila wanadamu waliovumilia na kupitia katika matatizo ya ulimwengu, yaani masikitiko ya kila aina, mateso, ambao ndio wanaomsikitikia Mwokozi.

Musa na Eliya wamekuwa wenzi wake Kristo. Wameshiriki kazi ya wokovu wa wanadamu. Musa aliwaombea Waisraeli akisema, "Walakini sasa ikiwa utawasamehe dhambi yao na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitaabu chako ulichoandika.' Kutoka 32:32. Eliya alikuwa amejua sikitiko la moyo, jinsi alivyokuwa katika miaka mitatu na miezi sita ya njaa jinsi alivyochukuliana mashutumu na chuki ya taifa zima. Alikimbilia jangwani akiwa peke yake mwenye masikitiko makuu na kukata tamaa. Mzigo wao ulikuwa kuhusu wokovu wa binadamu.

Wanafunzi waliokuwa wamelala walisikia mambo machache tu ya maongezi ya wajumbe hao. Hawakusikia mambo Mungu aliyokusudia wasikie; yaani mateso ya Kristo na utukufu wa baadaye. Walipoteza mibaraka kabisa. Walakini walijua kwa hakika kuwa dhambi za Waisraeli za kumkataa Mwokozi zilikuwa dhahiri mbele za Mungu. Walipewa ujuzi kuhusu kazi ya Mkombozi. Walikuwa mashahidi wake, na kuona yote. 2 Petro 1:16. Walifahamu kwa dhahiri kuwa Yesu ndiye Masihi, kwamba ni Mfalme wa ulimwengu.

Walipokuwa wangali wakiangalia mambo hayo, wingu jeupe liliwafunikiza, tazama sauti ilitokea winguni ikisema: "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye; msikieni yeye.' Waliposikia sauti ya Mungu ikisema kwa ngurumo iliyotetemesha mil-

ima, wanafunzi waliangukia mbali katika nchi, hali wamefunika nyuso zao, mpaka Yesu alipowasogelea, na kutuliza hofu yao kwa [241]
kusikia sauti yake ambayo wameizoea. Akasema, “Simameni, msiogope.” Utukufu wa mbinguni umekwisha kupita. Sura za Musa na Eliya zimekwenda. Sasa walibaki peke yao na Yesu.

[242] # 47 — Kupingana na Roho za Mashetani

Jua lilipochomoza Yesu na wanafunzi wake, walitelemka kutoka mlimani. Wanafunzi walikuwa kimya kwa ajili ya maajabu waliyoona. Wangalikaa mahali hapo patakatifu kwa furaha, lakini kulikuwa na kazi iliyowapasa kufanya.

Chini ya mlima kulikuwa na mkusanyiko mkubwa wa watu. Mwokozi alipowasogelea, aliwaagiza wale wanafunzi watatu kuwa wasimwambie mtu kuhusu mambo waliyoona. Alisema, "Msimwambie mtu habari ya njozi hii, mpaka Mwana wa Adamu atakapofufuka katika wafu." Kusimulia njozi hii kwa watu kungaliwashangaza tu, bila kitu cha zaidi. Walielewa kiasi gani hata kwa wale watatu, kwamba kufufuka katika wafu maana yake ni nini. Walakini hawakumwuliza Yesu awafafanulie zaidi.

Watu waliokuwa uwandani walipomwona Yesu akija, walimkimbilia ili kumsalimu walakini alipoangaza macho yake, alitambua kuwa kuna jambo lililotukia hapo, ambalo liliwakatisha tamaa wanafunzi. Baba mmoja alikuwa amemleta mwanawe ambaye alikuwa akisumbuliwa na pepo wachafu ili apate kuponywa. Yesu alikuwa amewapa wanafunzi uwezo wa kufukuza pepo na kuponya magonjwa, alipowatuma kwenda kuhubiri injili huko Galilaya. Walipokwenda kwa imani, mapepo waliwatii na kufukuzwa kutoka kwa watu. Sasa wanafunzi walisema kwa jina la Yesu kwamba pepo watoke kwa kijana huyu, lakini pepo waliwadhihaki tu wala hawakutoka. Wanafunzi bila kuona sababu ya kushindwa kwao, walijisikia kuaibika tu na kumwaibisha Bwana wao. Katika mkutano huo walikuwapo waandishi waliokuwa wakisema kuwa wamethibitisha kwamba wanafunzi na Bwana wao ni wadanganyifu. Hapo yuko pepo mchafu asiyeweza kushindwa na wanafunzi wala Bwana wao! Kundi lote liliona kuwa kushindwa kwao kumeleta aibu kubwa.

[243] Lakini ghafla Yesu na wanafunzi wake watatu walionekana wakija. Kushirikiana walikoshiriki pamoja na wajumbe wa mbinguni usiku uliopita, kuliwaachia utukufu katika nyuso zao, kulikofanya nyuso zing'ae kwa watazamaji. Mwokozi alifika katika mku-

tano wenye ghasia. Akiwatazama waandishi, aliuliza, akisema, "Mnajadiliana kitu gani?" Lakini sauti zilizokuwa kali, zilizojaa ubishi zilinyamaa kimya. Sasa baba mwenye shida akanyosha njia kumwelekea Yesu. Akianguka miguuni mwa Yesu alisimulia hadithi yake ya shida ya mwanawe, akasema, 'Bwana, nimemleta mwanangu kwako, ambaye ana pepo, na kumrarua . . . nilimleta kwa wanafunzi wako wasiweze kumponya."

Yesu akaona hali ya kutokuamini mioyoni mwao, akasema, "Enyi kizazi kisichoamini, nichukuliane nanyi mpaka lini? Kisha akamwambia baba mwenye mtoto mgonjwa, 'Mlete hapa mtoto wako."

Mtoto aliletwa, na roho mchafu alimtupa chini. Akifurukuta kwa maumivu, alilala na kugaagaa na kukoroma.

Mara tena Mkuu wa uzima na mkuu wa giza walikutana Katika vita. Kristo, kutangaza kufunguliwa kwa wafungwa, kuwaweka huru waliojeruhiwa (Luka 4:18). Shetani, kutaka kuwashikilia wafungwa wake. Kwa muda kidogo Kristo aliruhusu pepo mchafu kuonyesha nguvu zake.

Yesu aliuliza, "Kijana huyu amesumbuliwa na pepo huyu kwa muda gani?' Baba wa kijana alieleza muda mrefu wa mateso ya kijana. Kisha asipoweza kuvumilia zaidi, alisema, "Ukiweza fanya kitu. Tuhurumie utusaidie." "Ukiweza" Mpaka sasa baba huyu angali akitia shaka kuhusu uweza wa Yesu. Kristo alijibu akasema, "Mambo yote huwezekana kwake aaminiye." Baba akajibwaga miguuni pa Yesu, huku akiona hali yake ya kutokuamini, huku akilia na kusema, "Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu."

Yesu akamgeukia mgonjwa akasema, "Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala, usimwingie tena." Kukawa kilio cha maumivu, na mashindano makuu. Halafu kijana akalala kama mfu. Kukawa na mnong'ono katika mkutano wakisema, 'Amekufa". Lakini Yesu alimshika mkono, akamwinua, akamweka kwa baba yake mzima. Baba na mwanawe wakamsifu Mwokozi wao, wakati huo waandishi wameaibika, na kuondoka.

## Imani Hutuunganisha na Mbingu [244]

"Ukiweza kufanya jambo lolote, fanya, utuhurumie, na kutusaidia." Ni watu wangapi wenye kulemewa na mizigo ya dhambi

huomba ombi hilo. Kwa vyovyote vile, jawabu ni kwamba, "Mambo yote huwezekana kwake aaminiye." Mungu ameandaa mambo kwa njia ya Kristo, ili kushinda kila aina ya dhambi na majaribu yanayowajia watu wa Mungu. Lakini wengi huwa na upungufu wa imani, kwa hiyo huwambali na Kristo. Watu kama hawa wasijitegemee na kujiangalia wenyewe, bali wamtegemee Kisto.

Imani huja kwa ajili ya neno la Mungu. Wakashikilia ahadi ya Kristo kwamba "Yeye ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe." Yohana 6:37. Jitupe miguuni pake, ukilia, "Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu." Ufanyapo hivyo, hutapotea kamwe! Kwa muda mfupi, wanafunzi waliopata bahati, waliona mwanadamu akigeuka sura kufanana na hali ya Uungu, na pia kushushwa mfano wa kishetani Walimwona Yesu akitangazwa kuwa Mwana wa Mungu na kumwona akikutana na kijana mwenye pepo, akisaga meno kwa uchungu. Huyu Mkombozi mkuu ambaye muda uliopita, alionekana akiwa na utukufu, aliinama kumwinua mtu aliyefungwa na Shetani na kutiwa chini ardhini, akamleta kwa babaye na nyumbani.

Hili lilikuwa somo kuu la ukombozi. Mwana wa Mungu alishuka chini ili kusudi awaokoe waliopotea. Hali hiyo ndiyo itawahusu wanafunzi wake wawe hivyo pia. Maisha ya wanafunzi wa Yesu hayatazamiwi kuwa ya kuishi juu ya mlima pamoja na Yesu peke yake, ila hata chini uwandani pia wanatakiwa kuwahudumia watu walioko, ambao wamefungwa na Shetani, na kuwaweka huru.

Wakati Yesu alipokuwa na wale wanafunzi tisa peke yao, walimwuliza wakisema, "Mbona sisi hatukuweza kumtoa yule pepo?" Yesu aliwajibu na kusema, "Kwa sababu ya kutokuamini kwenu. Maana amini nawaambieni, mkiwa na imani kama punje ya mbegu ya haradali, mtaweza kuuambia mlima huu, ondoka hapa hata kule, nao utaondoka, wala hakuna kitu kisichowezekana kwenu. Walakini kwa namna hii, haiwezekani, ila kwa kufunga na kuomba.' Kutokuamini kwao kulikowatenga na Kristo, na kutojali wajibu mtakatifu waliokabidhiwa, vil-iwafanya washindwe kuponya. Wivu kwa wanafunzi waliochaguliwa kupanda mlimani na Kristo, ulikuwa ndio maongezi yao maalum, kwa hiyo walipokuwa katika hali hiyo
[245] ya giza walijiingiza katika mashauri ya Shetani.

Ili kushinda katika mashindano hayo iliwapasa kuwa katika maombi ya juhudi, wakifunga na kujinyenyekesha mbele za Mungu. Iliwapasa kuondoa ubinafsi kabisa, na kujazwa na nguvu za Roho

Mtakatifu na uweza wa Mungu. Imani inayomtegemea Mungu kabisa bila kubakiza sehemu yoyote, na kujiweka wakfu hasa katika kazi yake, hali hiyo peke yake ndiyo inaweza kumletea uwezo wa Roho Mtakatifu atakayewawezesha kushinda nguvu za roho za mashetani.

Shika neno la Mungu, na kufuata misaada yote Mungu aliyoweka kusaidia. Ndivyo roho yako itakuwa hodari Mitego na vizuizi vyote Shetani anavyoweka mbele yako, kama milima ya milele, vitatoweka kwa njia ya imani' "Hakuna jambo lisilowezekana kwenu."

[246]

## 48 — Nani Aliye Mkubwa Zaidi?

Yesu aliporudi Kapernaumu, alitafuta nyumba atakayoishi kwa muda. Siku zilizobaki za kuishi Galilaya alizitumia kuwafundisha wanafunzi wake kuliko kuhubiria makutano.

Kristo alikuwa amewaambia kuwa atauawa na kufufuka tena. Alisema kuwa atasalitiwa na maadui zake. Mpaka sasa wanafunzi walikuwa hawakuelewa kwa maneno yake. Ijapokuwa kivuli cha huzuni kilikuwa kikiwajia, wao walikuwa na mashindano tu ya kwamba ni nani atakuwa mkuu katika ufalme wa Mungu. Walijaribu kuficha mabishano hayo, ili Yesu asiyafahamu, lakini Yesu alingoja kwa uvumilivu wakati watakapofahamu dhahiri mambo haya.

Mara walipofika mjini, mtoza ushuru wa hekaluni aliuliza swali kwa Petro: “Je, mwalimu wenu hulipa kodi?” Kodi hii iliyoulizwa iliwahusu watu wa dini waliopaswa kulipa fungu fulani kila mwaka. Mtu asipolipa mchango huu alihesabika kwa marabi kuwa ni kosa baya. Sasa adui zake walitafuta makasoro juu ya Yesu. Katika mchango huo waliona sababu ya kumpata.

Ili kumkinga na laumu Bwana wao Petro alijibu kwa haraka kuwa Yesu atalipa kodi. Lakini baadhi ya watu walikuwa wakiachwa wasilipe mchango huo. Makuhani na Walawi, walihesabiwa kuwa wahudumu hekaluni, kwa hiyo hawakupaswa kutoa mchango huo. Manabii pia hawakupaswa kutoa mchango huo. Kwa kumdai Yesu kutoa mchango, marabi, walimhesabu kuwa si nabii, ila ni mtu wa kawaida tu. Kukosa kutoa mchango, kungehesabiwa kama kutojali mambo ya hekalu, au kwa upande mwingine, kama Yesu akilipa fungu hilo ingedhihirisha kuwa yeye si nabii. Jibu la Petro kwa jumla liliruhusu madai ya uongo ya Mafarisayo na wakuu juu ya Yesu.

[247] Petro alipoingia ndani Mwokozi hakumwuliza juu ya mambo yaliyotokea ila alisema; “Wafikirije Simoni, wafalme wa nchi huwatoza kodi akina nani, wana wao, au wageni?” Akajibu: “Wageni”. Yesu akasema: ‘Basi wana wako huru.” Watu wanapotozwa kodi kwa ajili ya kuimarisha mambo ya wafalme, watoto wa wafalme

hawatozwi kodi hiyo. Hivyo Waisraeli, watu wa Mungu walipotoa michango kwa ajili ya kutengeneza mambo ya Mungu Yesu aliye Mwana wa Mungu hakujaliwa hali hiyo.

Kama Yesu angalilipa kodi hiyo bila upinzani wowote, angekuwa karibu kukubaliana na madai yao, na wakati ule ule kuukana Uungu.

Lakini aliyakanusha madai yaliyokusudiwa. Alipotayarisha malipo kwa njia ya kimuujiza, alidhihirisha labia ya Uungu wake, kwa hiyo hakuwa mlipa kodi wa kawaida kama watu wengine, wa ufalme.

Akamwambia Petro: "Nenda baharini, ukatupe ndoana, na samaki atakayenaswa mara ya kwanza, ukifunua kinywa chake utaona ndani yake kipande cha fedha, ulipe kwa ajili yangu na kwa ajili yako."

Yesu alipoeleza kwamba hapaswi kulipa kodi ya jinsi hiyo, hakuna mtu aliyembishia. Alilipa mchango huo ili asiwachukize, ingawa hakupaswa kufanya hivyo. Fundisho hili lingekuwa muhimu kwa wanafunzi wake. Wasingejitia katika ushindani usio wa lazima, ili kushikilia haki na kutengeneza mambo. Wakristo wasingepaswa kuacha kanuni yoyote, ila inawapasa kuepukana na matatizo yoyote kadiri iwezekanavyo.

Wakati Petro alipokwenda baharini, Yesu aliwaita wanafunzi wengine, akawauliza: "Mbona mlikuwa mkihojiana na kubishana huko njiani?" Wakanyamaza kwa ajili ya kuona aibu. Yesu akawakumbushia kuwa alikuwa amewaambia kuwa, atakufa kwa ajili yao, na hali yao ya kutaka ukuu ilikuwa kinyume cha hali yake ya upendo usiokuwa wa binafsi. Lakini ijapokuwa amewaambia wazi kuhusu mambo yanayomkabili, usemi wake wa kwenda Yerusalemu, uliamsha matumaini yao ya kwamba anaenda kutawazwa kwa kuwa mfalme. Jambo hili lilileta maswali kwamba ni nani atakuwa mwenye cheo cha juu katika utawala huo. Mwishowe mmoja alithubutu kumwuliza Yesu: "Nani atakuwa mkuu katika ufalme wa mbinguni?"

## Mashindano ya Kushindania Ukuu

Mwokozi aliwaambia, "Mtu yeyote atakaye kuwa wa kwanza kwenu, na awe mdogo kuliko wote, na kuwa miumishi wa wote." Hawakufahamu aina ya ufalme wa Kristo, bila shaka hili ndilo

[248] lililokuwa asili ya mabishano yao. Lakini sababu hasa ilikuwa kubwa zaidi kuliko hilo. Hata walipokwisha kufahamu kabisa, swali lolote la mambo yaliyotangulia lingeweza kuamsha matatizo. Hivyo msukosuko ungeweza kuletwa kanisani, baada ya Kristo kuondoka. Kushindania ukuu, ulikuwa kazi ya juu juu ya nia ile ya ushindani mkuu ulioanzia mbinguni, uliosababisha Yesu kuja na kufa. Mbele yake ilitokea njozi ya Shetani aliyesema, "Nitafanana naye aliye juu." Isaya 14:14. Tamaa ya ukuu ilileta mashindano katika baraza la mbinguni. Lusifa alitamani kupata uwezo wa Mungu, sio tabia ya Mungu. Alitafuta kupata ukuu, na kila mtu au kila kiumbe chenye nia hiyo, hutenda mambo kama hayo. Utawala wa Shetani ni wa mabavu. Kila mtu humhesabu mwingine kuwa ni ngazi yake ya kupandia kwenda kwenye ukuu.

Wakati Lusifa alipotafuta kulingana na Mungu, "kristo alijifanya kuwa hana utukufu, akajitwalia namna ya mtumwa, akawa mfano wa mwanadamu, na alipokuwa na umbo la mwanadamu akajinyenyekeza, akawa mtii mpaka mauti, nayo mauti ya msalaba." Wafilipi 2:7, 8. Sasa msalaba ulikuwa mbele yake, na wanafunzi wake walikuwa wakijitafutia ukuu, wala hawakushughulikia na hali ya unyenyekevu aliokuwa nayo Bwana wao, wala hawakuelewa na maneno yake kuhusu unyenyekevu kwa ajili yao.

Yesu alijaribu kusahihisha maovu haya. Aliwaonyesha ni kanuni gani inayotakiwa katika ufalme wa mbinguni, na ukuu wa kweli ni upi. Wale waliojawa na kiburi na kujiona walikuwa wakijifikiria na zawadi watakayopata. Watu kama hao hawakufaa katika ufalme wa mbinguni, maana walionekana kuwa katika jamii ya Shetani. Kabla ya kupata heshima, kwanza kunyenyekea. Kupata cheo mbele ya wanadamu, mbingu huchagua watendakazi walio katika sehemu ya chini machoni pa Mungu. Mwanafunzi wafananaye na mtoto, ndiye afaaye zaidi katika kazi ya Mungu. Anayehitaji msaada wa mbinguni, atauomba kutoka katika kuongea na Kristo, ataondoka kwenda katika kazi yake, akiwa na msaada alioomba naye hufaulu pale watu wenye elimu zaidi wanaposhindwa.

Lakini watu wanaojitukuza wenyewe, wakijiona kuwa wanatosha kufaulu kazini na kuendesha mpango wa Mungu, Bwana huwaweka kando tu, wala hana haja nao. Kazi ya Mungu haisimami, bali huendelea kwa nguvu zaidi.

Haikutosha kuwafundisha wanafunzi wa Kristo namna ufalme wa Mungu ulivyo. Jambo kubwa walilohitaji ni kuongoka, na [249] kubadilika mioyo yao. Yesu akimwita mtoto, alimweka kati yao, akamkumbatia mikononi mwake, akasema, "Msipoongoka, mkawa kama' mtoto mdogo, hamtaingia katika ufalme wa mbinguni." Hali isiyokuwa ya kutaka makuu, kujisahau nafsi, na kuwa na upendo kama mtoto mdogo, ndiyo hali yenye thamani machoni pa mbingu, nayo ndiyo inayoonyesha ukuu wa kweli. Katika miguu ya Yesu, fahari ya ulimwengu na ukuu wake husahauliwa. Matajiri na maskini, wasomi na wasio wasomi, hukutana pamoja kama watu walionunuliwa kwa damu ya thamani bila ubaguzi wa aina yoyote.

Mungu huweka muhuri wake kwa watu, sio kwa ajili ya vyeo walivyo navyo, ila kwa ajili ya ungano waliloungana na Kristo. "Nawe umenipa ngao ya wokovu . . . wako." Kama mafao ya tabia ya mwanadamu, "Umenikuza." Zaburi 18:35.

Maneno ya Mwokozi yaliwafanya wanafunzi wake wasijitumainie. Yohana aliamshwa aulize, kama matendo yake ni ya sawa, au namna gani. Alisema: "Bwana, tulimwona mtu mmoja akifukuza pepo kwa jina lako . . . sisi tulimkataza kwa sababu hafuatani na sisi." Yakobo na Yohana walidhani kuwa kumkataza mtu huyo walikuwa wakimtetea Bwana wao; kumbe sivyo.

Walianza kufahamu kuwa kufanya hivyo walikuwa wakiona wivu kwa ajili yao wenyewe. Walikubali kosa lao, na kukubaliana na makemeo ya Yesu. Bwana aliwaambia: "Msimkataze, maana hakuna awezaye kufanya miujiza kwa jina langu, kisha akawa kinyume changu." Watu wengi walivutiwa na tabia pamoja na kazi ya Kristo, ambao walimwamini. Wanafunzi inawapasa kuwa waangalifu sana ili wasiwakatishe tamaa hawa watu. Lazima waonyeshe fadhili kama zile walizoona Bwana wao.

Kristo ni Mwalimu Mkuu; nasi twapaswa kukaa miguuni mwake na kujifunza kwake. Kila mtu aliyevutwa na Mungu ni mfereji wa kupitishia upendo wa Yesu na kuwafikia wengine. Ingelupasa kuwa waangalifu kadiri gani ili kusudi tusije tukawakatisha wachukuzi nuru wa Mungu na kuvuruga nuru ambayo wangeangaza ulimwenguni!

Kitendo kama cha Yohana cha kumkataza afanyaye miujiza kwa jina la Yesu, kingeweza kupoteza mtu. Yesu alisema kuhusu jambo

hili. “Ni heri kama angefungiwa jiwe, shingoni mwake na kutupwa kilindini mwa bahari.”

Mbona kusema maneno haya magumu? Kwa sababu “Mwana
[250] wa Adamu alikuja kukiokoa kilicopotea.” Luka 19:10. Je, wanafunzi wake wataonyesha roho ya ubinafsi kwa wenzao, kuliko Bwana wa mbinguni alivyoonyesha roho ya fadhili kwa watu? Dhambi ya kumkosesha mtu ni kubwa kadiri gani? Kwa mtu huyu kilio na masumbuko ya Mwokozi yalikuwa bure. Ni dhambi kubwa mno!

Ole ni wa ulimwengu kwa ajili ya mambo ya kukosesha. Mambo ya kukosesha hayana budi kuja. Ulimwengu utawapinga wafuasi wa Kristo kwa hakika. Lakini ole wa mkristo afanyaye mambo haya. Watu wengi hudanganywa na kupotoshwa na wale wanaojidai kuwa ni wafuasi wa Kristo, hali wakipotosha tabia yake.

## Jambo lolote likoseshalo litupwe mbali

Dhambi moja ikipendelewa na kuhifadhiwa na mtu inatosha kupotosha tabia ya mtu na kuwakosesha wengine. Kama mguu au mkono ungekatwa au jicho kung’olewa ili kuuokoa mwili usiangamie, tungekuwa na juhudi kadiri gani kuacha dhambi zinazotuangamiza!

Katika huduma ya kafara, chumvi ilitiwa katika kila sadaka iliyotolewa. Kama iliyokuwa sadaka ya manukato hii ilionyesba kuwa haki ya Kristo peke yake ndiyo iliyofanya huduma yoyote ikubalike mbele za Mungu. Kuhusu jambo hili Yesu alisema: “Mwe na chumvi ndani yenu, na mwe na amani ninyi kwa ninyi.’ Wote lazima wawe na chumvi yenye kuokoa, yaani haki ya Mwokozi wetu. Hapo ndipo watakuwa chumvi ya ulimwengu”, wakizuia maovu yasitendwe na watu, sawa kama chumvi inavyozuia kuharibika.” Mathayo 5:13. Lakini kama chumvi imeharibika, maisha ya mtu hayawezi kuwavuta watu kuelekea katika uzima. Yesu alisema: ‘Inawapasa ninyi kuwa washiriki wa neema yangu, ili mpate kuwa wenye mvuto uelekeao kwenye uzima. Ndipo hapatakuwapo naushindani, au ubinafsi, wala kutamani ukuu.’ Tunapomwona Yesu kama Mtu wa Huzuni, ajuaye sikitiko, akifanya kazi kuokoa ulimwengu uliopotea, akidharauliwa na kudhihakiwa, akifukuzwa toka mji hata mji mpaka kazi yake imalizike, tunapomwangalia katika Gethsemane akitoka jasho la damu, na katika msalaba akifa kifo cha uchungu mzito,

tuyaonapo haya, ubinafsi hautatusogelea, tutabeba msalaba kwa furaha kumfuata Yesu, na kustahimili yote, majaribu, aibu, mateso kwa ajili yake.

Hakuna mtu anayemwamini Kristo atakayehesabiwa kuwa hana thamani. Wote tuliopewa elimu, uwezo, uzuri wa tabia, utawa, tunalo deni kwa wale wasiopewa nafasi kama yetu. Lazima tuinue mikono ya watu kama hao. Malaika huwajia watu wale wanaopigana [251]
na hali ya ubinafsi, wenye makasoro ya tabia, ambao hupigana sana ili kurekebisha tabia hiyo ambao mazingara yao ni mazito sana. Hata hivyo watu hawa hujitia hivyo katika huduma ya Kristo.

Yesu alisema: "Mwaonaje, mtu akiwa na kondoo mia, mmoja akipotea, hawaachi wale tisini na lisa, akaenda milimani na kumtafuta yule aliyepotea, hata amwone? Na akimwona, nawaambieni, hufurahi sana kuliko wale tisini na tisa ambao hawakupotea. Vivyo hivyo na Baba yangu aliye mbinguni hufurahi kwa ajili ya mmoja wapo wa watoto hao, asipotee."

## Haja ya uangalifu wa huruma

Usimwaibishe mkosaji kwa ajili ya kutangaza makosa yake kwa watu wengine, wala usiliaibishe jina la Kristo kwa ajili ya kutangaza makosa ya mkristo waziwazi. Mkosaji lazima aonyeshwe makosa yake, ili ayaache. Lakini usihukumu au kulaumu. Katika kupo-nya mgonjwa wa moyo wa mtu kunahitaka kutumia uangalifu mwingi wa huruma. Upendo wa yule mtu wa Kalwari peke yake ndio unatosha kulishughulikia jambo hili. Kama ukifaulu katika jambo hili, "Utampo-nya mtu kutokana na mauti", na "Utaufunika wingi wa dhambi." Yakobo 5:20.

Lakini hata bidii hii inaweza kushindwa. Kisha Yesu alisema, "Chukua mtu mwingine au watu wawili mwende nao." Kama hatawasikia wao pia, ndipo sasa shauri hili litaletwa mbele ya kundi lote la washiriki. Hebu washiriki wa kanisa wote waungane katika maombi wakirnsihi ndugu huyu apate kurudi. Roho Mtakatifu atazungumza naye kwa njia ya watumishi wake, wawasihi kwa ili ya Kristo, mpatanishwe na Mungu." 2 Wakorintho 5:20. Mtu anayekataa maneno haya ya upatanisho huwa amejiondoa mwenyewe kutoka kwa Kristo, na hivyo hujifuta kutoka katika ushirika wa kanisa. Kwa hiyo Kristo alisema, 'Na awe kwako kama

mtu wa mataifa, na mtoza ushuru." Lakini asidharauliwe na kutojaliwa na ndugu zake wa kwanza, mtendee kwa fadhili wala si kwa uhasama.

Mtu anayedharau njia zilizowekwa na Kristo, kwa ajili ya kuwarudisha wakosaji, husetiriki dhambi zile yeye mwenyewe. Soma Mambo ya Walawi 19:17. Dhambi ambazo tungezisahihisha, hutukalia sisi kama sisi ndio watendaji wake.

Haitupasi kuhesabu makosa kana kwamba ni maelezo ya mafafanuzi, kati yetu, kuyasema kwa wengine. Tunapotaka kureke-
[252] bisha makosa ya ndugu zetu, inatupasa kuyafanya kisiri yasijulikane kwa watu hasa wale wasioamini. Jinsi tunavyo taka Kristo kutu-tendea ndivyo anavyotuamrisha kuwatendea wengine. "Mtakayoyafunga duniani, yatafungwa pia huko mbinguni, na mtakayoyafunga duniani, yatafunguliwa pia huko mbinguni." Mathayo 16:19. Matokeo yenu ni ya milele.

Lakini haitupasi kubeba madaraka haya peke yetu. Maneno haya yakifuatwa kikamilifu Kristo hukubaliana nayo katika nikusanyiko wa kanisa, wanafunzi wakusanyikapo, kwamba ni wachache, au wengi, wakusanyikapo kwa jina la Yesu, atakuwa pamoja nao. Asema "Wawili wenu wakipatana katika jambo lolote duniani, wakiomba, litafanywa na Baba yangu aliye mbinguni.'Wakati Yesu akiwa katika mwili, alishiriki na wanafunzi wake, katika majanbu yao na kuwahurumia katika matatizo yao, na katika Uungu wake huwaunganisha katika kiti cha enzi cha Mungu.

Ahadi ya ajabu. Uwezo wote wambinguni hujiunga na ubinadamu ili kuvuta watu kwa Kristo.

## 49 — “Mtu Akiwa na Kiu, na Aje” [253]

Wayahudi walipaswa kukutanika huko Yerusalemu mara tatu kwa mwaka kwa makusudi ya dini. Kusanyiko la Siku kuu ya Vibanda lilikuwa la mwisho kwa mwaka. Mavuno yalikusanywa katika mbuga na mabonde. Matunda ya kutoa divai yalikuwa yanachumwa.

Sikukuu iliendelea muda wa siku saba. Watu wengi wa Palestina na kutoka sehemu nyingine walikusanyika huko Yerusalemu. Wakubwa kwa wadogo, matajiri kwa masikini, wote walikuja wakiwa na vipaji vyao vya shukrani kwa Mungu aliyewabarikia katika mwaka, kwa ajili ya wema wake. Kila jambo lililoleta furaha lilitendeka, ili kuonyesha wema wake. Mji ulipambwa kwa mapambo yote.

Sikukuu haikuwa kwa ajili ya shukrani ya mavuno peke yake, ila ya ukumbusho wa ulinzi wa Mungu kwa wana wa Israeli jangwani. Katika maadhimisho ya maisha yao ya kuishi mahemani katika sikukuu ya vibanda vilivyojengwa kando ya hekalu. Vilima na mabonde vilivyojengwa vinazunguka Yerusalemu ilienezwa na vibanda hivi vya majani. Wenye kuabudu waliimba nyimbo takatifu walipokuwa wakisherehekea sikukuu hii.

Kitambo kabla ya sikukuu hii ilikuwa Siku ya Upatanisho, ambaya iliwalazimu watu kurekebisha maisha yao kama mbingu inavyotaka. “Mshukuruni Bwana... kwa kuwa rehema zake zakaa milele.”(Zaburi 106:1). Ilikuwa shangwe kuu, na watu wote walishirikiana katika kuimba na kusifu.

Hekalu ndiyo ilikuwa kiini cha furaha. Pande zote za ngazi za hekaluni ambazo ni zenye mawe yang’aayo waimbaji wana wa Lawi ndio walioongoza huduma, ya nyimbo. Sauti ilisikika kwa mbali sana, hata sifa za kusifu zikaenea mahali popote.

Wakati wa usiku hekalu liliangazwa kwa mwanga wa mishumaa [254]
na vimuli vilivyotengenezwa, nyimbo, kuyumba kwa matawi ya mitende na umati wa watu uliowasha taa na mienge, pamoja na maadhimisho ya sikukuu, ilifanya hali ya mambo iwe ya kupendeza

mno. Lakini jambo la kuvutia zaidi lilikuwa ni ule ukumbusho wa safari ya jangwani.

Wakati kunapambazuka, makuhani walipiga tarumbeta zao, na watu wote vibandani waliitikia kwa shangwe kuu. Kisha makuhani wakachovya maji ya kijito cha Kedron yaliyokuwa yakitiririka na kuyanyunyiza kwenye ngazi za hekalu, wakifuatisha mlio wa wimbo, na kufanya jambo lionekane kuwa la kupendeza mno.

Katika kibweta cha Makuhani kulikuwako na mabeseni mawili ya fedha. Mojawapo lilijazwa maji, na gudulia la mvinyo kwa jingine. Na yote mawili mawili yalifunika kabisa na kutiririka mpaka mtoni na baharini. Maji haya matakatifu yalifananishwa na ile chemchemi ya maji iliyofurika kutoka mwambani na kuwanywesha Waisraeli jangwani, ambayo iliamuriwa na Mungu.

Wana wa Yusufu walipojiandaa kuhudhuria katika sikukuu waliona kuwa Kristo hakuondoka, au kutoka toka wakati wa kuhudhuria. Tangu alipomponya mgonjwa huko Bethsaida, hakuhudhuria tena katika sikukuu za kitaifa. Aliendelea kufanya kazi yake huko Galilaya ili kuepukana na mashindano na Wayahudi huko Yerusalemu. Kule kuonekana kwake kana kwamba hajali mikusanyiko ya dini kama wengine, kuliwafanya makuhani na marabi wamchukie na kumfanyia uhasama, jambo hili lilileta wasiwasi hata kwa jamaa yake pia. Katika mafundisho yake alisisitiza juu ya utii, lakini yeye mwenyewe alionekana kana kwamba hajali mambo yaliyoamuriwa na Mungu, kuhusu huduma za mikusanyiko.

Hali yake ya kushirikiana na watoza ushuru na kutofuata maagizo ya marabi; na kutojali mapokeo ya wazee kuhusu kutunza Sabato, yote hayo yalimfanyia uhasama mkubwa kwa waongozi wa dini. Ndugu zake walisema kuwa ni kosa sana kuwapinga wakuu jinsi hii, hali ni watu waliojifunza sana, na kuheshimiwa na wote. Waliona kuwa watu hawa walikuwa sawa, Yesu ndiye mwenye makosa. Lakini walikuwa na matataniko, walipomwona Yesu jinsi anavyoishi bila makosa kama watu wengine, na kazi yake ya ajabu. Walitumaini kuwa atawaaminisha Wayahudi kuwa yeye ndiye Masihi, Mkuu wa Israeli. Walijivunia wazo hili.

Hiyo ndiyo ilikuwa haja yao, kwa hiyo walimkazania Yesu aende Yerusalemu. Walisema: "Ondoka hapa". Uende Uyahudi, ili wana-
[255] funzi wako nao wapate kuziona kazi zako. Maana hakuna mtu atendaye jambo kwa siri, na yeye pia alitaka kujulikana. Ukifanya

mambo haya, yafanye waziwazi ulimwenguni. Akijua kuwa ni yeye Masihi kwa nini kujificha? Kwa nini haendi huko Yerusalemu kijasiri na kutenda matendo haya yanayosemwa huko Galilaya? Walis-ema, “Usijifiche huku katika jimbo la Galilaya, mahali pasipojulikana wazi. Jidhihirishe huko katika makao makuu, ukaungwe mkono na Makuhani na wakuu, ili upate kuusimamisha utawala wako.

## Nia ya ubinafsi yadhihirishwa

Ndugu hawa wa Yesu walisema hayo kutokana na nia yao ya ubinafsi na kutaka makuu. Kisha Yesu aliwaambia: “Saa yangu haijafika bado, lakini saa zenu siku zote zipo. Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi, ila hunichukia mimi, kwa sababu mimi huushuhudia ya kwamba kazi zake ni mbovu. Ninyi nendeni katika sikukuu hiyo. Mimi siendi sasa katika siku kuu, maana saa yangu haijafika. Alipokwisha kuwaambia maneno haya, alizidi kukaa huko Galilaya zaidi.” Ndugu zake walisema naye kama watu wenye mamlaka. Aliyakanusha maneno yao, akiwahesabu kuwa sio wafuasi wake, ila ni watu wa ulimwengu tu. Ulimwengu hauwezi kuwachukia, kwa sababu wanafanana nao, ila huwapenda kama wenzao.

Yesu hakupaswa kuwa mwenye kiburi, wala hakujitia hatarini, ovyo, ovyo au kuharakisha matatizo yamjie. Alijua kuwa atachukiwa na ulimwengu, na kazi yake itaishia katika mauti, lakini kuharakisha na kujitia hatarini bila sababu, siyo mapenzi ya Mungu, ambaye ni Baba.

Watu wengi walikuja katika sikukuu kutoka pande zote, wakiwa na kusudi la kumwona Yesu. Mafarisayo na wakuu walimtazamia na kumtafuta wakitumaini kuwa wakati umefika wa kumshitaki. Waliuliza kwa makini wakisema: “Yuko wapi?” Lakini hakuna mtu aliyejua mahali alipo. Hakuna mtu aliyethubutu kumtaja kuwa Masihi, lakini kila mahali watu walikuwa wakiongea habari zake. Wengi waliamini kuwa alitumwa kutoka mbinguni kwa Mungu, wakati wengine wakimwita kuwa ni mdanganyifu.

Wakati ule ule Yesu alifika Yerusalemu kwa ghafla. Kama angalifuatana na msafara wa watu angejulikana na watu, na hoihoi kwa ajili yake zingezidi, na chuki ya wakuu ingechochewa juu yake.

Katikati ya sikukuu, Yesu aliingia hekaluni katika mkutano. Ilisemekana kwamba hawezi kujiingiza mwenyewe katika hatari ya makuhani na wakuu wa Kiyahudi wanaomchukia. Watu wote walis-
[256] taajabia kutokea kwake wakati huu. Watu wakanyamaza kimya.

Akasimama katikati huku akitazamwa na watu wote, aliwahutubia kwa namna ambayo mtu hajafanya hivyo. Maneno yake yalionyesha ujuzi kamili wa kujitoa na kufanya huduma ya kicho hasa, akafundisha mafundisho ya manabii, kuliko makuhani na marabi wanavyofundisha. Alinena kwa uwezo kama mtu aonaye mambo yasiyoonekana na alisema kama mtu mwenye mamlaka ya mbinguni na duniani. Watu walishangaa kwa mafundisho yake, kama watu wa Kapernaumu walivyoshangaa, maana maneno yake "yalikuwa na uwezo". Luka 4:32. Alifanya kila jambo liwaelekeze kutubu. Asingalikataliwa na watu wake, kama anawaokoa kutoka katika hatia ya dhambi.

Wakaulizana, 'Mtu huyu amepataje kujua mambo, naye hajajifunza katika shule?" Yesu na Yohana Mbatizaji wamekuwa wajumbe wa kweli kabisa, na hali hawakujifunza shuleni, mwa Marabi, ambao ndio wakufunzi maalumu. Watu waliowasikia walishangazwa kwa jinsi ujuzi wao wa maandiko ulivyo. Lakini Mungu wa mbinguni ndiye aliyewafundisha. Yesu alipohubiri hekaluni watu waliachama tu. Waliokuwa wakimchukia sana, hawakuwa na jambo la kusema, wala kutenda.

## Wasiwasi wa watu ulitulizwa

Asubuhi ya siku iliyofuata sikukuu, ilikuta watu wakiwa na uchovu wa sikukuu. Ghafla Yesu alipaza sauti yake na kusema: "Mtu akiwa na kiu na aje kwangu, kama maandiko yasemavyo, mito ya maji itabubujika tumboni mwake." Watu walikuwa katika kuhangaika na mambo mengi tu, na kusikiliza nyimbo tu, lakini mioyoni mwao walikuwa hawana kitu cha kuwaridhisha na kuwatuliza.

Asubuhi hiyo makuhani walikuwa wamefanya ukumbusho wa mwamba uliotoa maji jangwani. Mwamba huo ulikuwa mfano wa yule atakayekufa, na kifo chake kiwezeshe mito ya maji ibubujike matumboni mwao, ambao ni wokovu. Mbele ya mkutano huo Yesu alijidhihirisha kuwa ndiye mwamba utakaopigwa na kuuletea

ulimwengu wokovu. Yesu alipokuwa akisema haya watu walipata kicho cha namna ya ajabu. Wengi walikuwa tayari kusema kama mwanamke wa Kisamaria alivyosema: "Nipe na mimi maji haya, ili nisione kiu tena." Yohana 4:15.

Wengi waliomsikiliza Yesu walikuwa wakilia kwa kutokuwa na matumaini, wakihangaika tu na mambo ya ovyo, huku wakitamani mambo ya dunia, lakini kati ya masikitiko yao ilisimama furaha ya kuridhisha mahitaji yao. Lakini sauti ile iliyosema: "Kama mtu akiona kiu, na aje kwangu", na kusikiliza maneno yaliyofuata [257]
yalileta tumaini jipya. Waliona mfano uliokuwa mbele yao kuna toleo la mmoja asiye na kasoro la kupata wokovu.

Sauti ya Kristo kwa mtu aliye na kiu ingali inaendelea hata sasa. Sauti hiyo inatuita sisi kwa nguvu zaidi kuliko zamani, kwa watu waliosikia hekaluni ikinenwa na Yesu. "Mtu aliye na kiu na aje kwangu. Na yeyote atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure." Ufunuo 22:17.

[258] 

## 50 — Katikati ya Mitego

Katika muda wote wa sikukuu Yesu alikuwa akizungukwa na wapelelezi, kila siku mipango mipya ilipangwa jinsi ya kumwangamiza. Makuhani na wakuu walipanga namna ya kumkomesha kwa nguvu. Siku ya mwisho ya mkutano, walidai kutaka kujua kuwa alikuwa anafundisha kwa uwezo gani?

Yesu alijibu: "Mafundisho yangu hayatokani na mimi mwenyewe, ila yatokana na yeye aliyenituma. Mtu akitaka kufanya mapenzi yake, atajua kuwa mafundisho yangu hutoka kwa Mungu, au ni mawazo yangu tu. Yohana 7:16, 17. Alisema kuwa kuona ukweli na kuuelewa hutokana na dhamiri wala si mawazo tu. Ukweli hutaka utambuzi wake utoke katika dhamiri. Ni kazi ya neema ya moyoni. Ukubali wake hutaka mtu aamue kuachana na kila dhambi inayofunuliwa na Roho wa Mungu. Kunatakiwa kuacha vitu vyote na mazoea yote yanayopingana na kanuni za ukweli. Wanaojitoa kwa Mungu namna hiyo, watajua mtu asemaye mambo ya Mungu, na mtu asemaye mambo yake' mwenyewe. Mafarisayo walikuwa hawatafuti kweli, ila walikuwa wakitafuta sababu za kuukwepa ukweli, na hiyo ndiyo ilikuwa asili ya kutofahamu maneno ya Yesu, na mafundisho yake.

Yesu alisema: "Asemaye mambo yake mwenyewe, hutafuta utukufu wake, lakini atafutaye utukufu wake aliyemtuma huwa wa kweli, wala hana uwongo." Roho ya ubinafsi husaliti ukweli. Lakini Kristo alikuwa akitafuta utukufu wa Mungu. Huu ndio ulikuwa uthibitisho wake alipokuwa akiufundisha ukweli.

Yesu aliwathibitishia Marabi uungu wake kwa njia ya kusoma mioyo yao na kuona yaliyomo. Walikuwa wakipanga kumwangamiza, ambayo ni kuvunja sheria, ambayo wanajidai kuitetea. Yesu alisema: "Je, Musa hakuwapa sheria?" Na hivyo hakuna hata mmoja aishikaye. Kwa nini mnatafuta kuniua?" Ma-
[259] neno haya yalifanana kama kimuli kikali kilichomulika mioyoni mwao na kuyaona maovu waliyoficha humo. Maovu hayo walikuwa karibu kuyatenda, yaani kumwua Yesu. Kwa muda waliona

kuwa wanapingana na Mungu. Lakini walikaidi tu, huku wakificha kusudi lao la kuua na kufanya uzandiki kuwa hawana kusudi hilo, wakisema: "Una wazimu; nani anataka kukuua?"

Kwa kujifanya wazandiki, Kristo hakujali maneno hayo. Ila aliendelea kusema kuwa kazi yake ya kuponya aliyofanya huko Bethsaida siku ya sabato, ilishuhudia kuwa ni ya haki ingawa waliitafsiri vibaya, wala sivyo ilivyo. Ilidhihirika kwamba hawajui sabato inavyotunzwa. Kufuata sheria ni kwamba kila mtoto nwanamume lazima atahiriwe siku ya nane, lakini siku hiyo ikiangukia siku ya sabato, kitendo hicho lazima kitendeke. Je, hakuna uhalali wa kutuponya mtu siku ya sabato? Aliwaonya kwa kusema "Msihukumu hukumu ya macho, bali hukumu ya haki." Wakuu walinyamaza kimya.

## Mawazo yaliyopotoka kuhusu Masihi na kuja kwake

Watu wengi walioishi Yerusalemu walijisikia kuvutwa na nguvu isiyozuilika. Walijisikia kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu. Lakini Shetani alikuwa tayari kuwatilia mashaka. Iliaminika kwamba Yesu angezaliwa katika Bethlehemu, lakini baada ya muda angetoweka, na mara yake ya pili angekuja bila kujulikana atokako. Si watu wachache walioamini kuwa Masihi asingekuwa na uhusiano na binadamu.

Watu wengi walipokuwa wakitangatanga katika mashaka, Yesu alisema: "Mnanijua, na mnajua nilikotoka? Mimi sikuja kwa shauri langu, aliyenituma ni wa kweli naye hamumjui" Maneno ya Yesu yalikuwa marudio ya madai yake kwa baraza kuu la Sanhedrin, miezi mingi iliyopita, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu. Kati ya watu wengi walioamini walisema: "Je Kristo ajapo hatafanya miujiza mingi kuliko hii ifanywayo na mtu huyu?" Wakuu na Mafarisayo wakiangalia hali ya mambo yalivyo waliona hali fulani mkutanoni. Waliharakisha kwenda kwa makuhani wakuu ili kufanya mipango ya kumkamata akiwa peke yake, maana waliona kuwa watu wanamwunga mkono, kwa hiyo wasingeweza kumkamata wakiwapo watu.

Watu wengi walioamini kuwa ni Masihi, walipotoshwa na hoja za uongo za makuhani na marabi. Walimu hawa walikariri kuwa unabii unaomhusu Masihi atatawala katika Sayuni na Yerusalemu,

[260] naye atatukuzwa naye atatawala toka bahari mpaka bahari, na kutoka mtoni mpaka mwisho wa nchi. Isaya 24:23; Zaburi 72:8. Jambo hili liliwafanyia ulinganisho wa utukufu ujao na hali nyenyekevu ya Yesu. Kama watu wangalisoma maandiko na kujifunza wao wenyewe wasingalipotoshwa. Isaya 61 inathibitisha kuwa Kristo atatenda mambo yale yale aliyotenda. Sura ya 53 inaeleza jinsi atakavyokataliwa na watu. Na sura 59 inadhihirisha tabia ya makuhani na marabi.

### Uwezo wa kupambanua Wema na Ubaya

Mungu hawalazimishi watu kuamini. Amekusudia kuwa watu wasiamini kijuujuu tu, ila waamini kwa hakika hasa wakiwa na uthibitisho wa maandiko matakatifu. Kama Wayahudi wangalipima na kulinganisha unabii na matukio, wangalifahamu kamili wakati wao na kuja kwa mtu wa Galilaya aliye mpole na mnyenyekevu.

Watu wengi leo hujidanganya kama Wayahudi walivyojidanganya. Walimu wa dini husoma Biblia na kuitafsiri kufuata mawazo yao, sawa na mapokeo yao, wala hawasomi Biblia na kujipima walivyo ila hujitolea kufuata tu walimu wanavyowaongoza. Mtu yeyote anayejifunza Biblia kwa nia hasa na maombi, ili apate kuongozwa nayo, atapata ufahamu wa mbinguni. Ataifahamu Biblia, "Mtu yeyote apendaye kufanya mapenzi yake, atafahamu kama mafundisho haya yatoka kwa Mungu au ninanena mambo yangu mwenyewe."

Siku ya mwisho ya sikukuu, watu waliotumwa ili kumkamata Yesu, walirudi bila kuwa naye. Wakuu wao waliwauliza kwa hasira wakisema, "Mbona hamkumkamata?" Wao walijibu wakisema, "Kamwe mtu hajanena kama anenavyo mtu huyu."

Walipozwa mioyo yao migumu kwa maneno haya. Walakini Yesu alipokuwa akinena walimsogelea wapate kushika kitu katika maneno yake cha kumshitaki lakini walipomsikiliza, walimwamini. Waliona kile ambacho makuhani na wazee hawakukiona. Mioyo yao ilijaa na maarifa ya Mungu.

Makuhani na wakuu walipofika mbele ya Yesu walijisikia vile vile. Roho zao ziliwaka, nao wakakubali kuwa, "Kamwe mtu hajanena kama anenavyo mtu huyu." Lakini mara wakazidi kuwa wagumu wa mioyo, mpaka wakasema, "Je, hata ninyi mmedan-

ganyika? Ni nani katika makuhani au wazee waliomwamini? Lakini watu hawa wasiojua sheria wamelaaniwa, ndiyo sababu wanamwamini." Kwa wale ambao ukweli huhubiriwa kwao, mara chache huuliza, "Je, ni kweli? bali husema, "Unahubiriwa na nani?" [261]

Watu wengi huupima ukweli huu kwa kuona watu walioamini, lakini swali linabaki kuwa, "Je, kuna wasomi au wakuu walioamini?" Haidhuru kuwa ni wangapi walioamini, au wasomi wangapi Wanaamini au wakuu wa dini walioamini. Swala lilidumu kuwa, kama Yesu akiachwa vivi hivi, aendelee tu, atawapotosha watu waache dini iliyokwisha kusimama. Njia moja ya kufanya ni kumkomesha asiendelee na mambo haya, mara moja. Katika mazungumzo yao ya mipango walivurugika kwa njia ya swali lililoulizwa na Nikodemo kwamba: "Je, sheria yetu inaruhusu kumhukumu mtu kabla ya kumsikiliza na kumwona afanyavyo?" Wote walinyamaza kimya, maana hairuhusiwi kumhukumu mtu kabla ya kumsikiliza kwanza. Lakini walishupaza na kuona kwamba kuna mtu mmoja kati yao anayemtetea. Wakasema, "Je, na wewe ni mtu wa Galilaya pia?

Tafuta utaona kuwa hakuna nabii atokaye Galilaya. Walakini kwa ajili ya upinzani huo, wakuu walitulia kidogo, "Kila mtu akaenda nyumbani kwake."

## Yesu akishughulikia kesi ya uzinzi

Yesu aliondoka katika ghasia za mjini na fujo za Marabi akaenda mahali patulivu katika mlima wa mizeituni, mahali ambapo atakuwa na Mungu kwa upweke. Lakini asubuhi yake mapema alirudi hekaluni, na watu wakamkusanyikia.

Mara alitiwa fujo. Mafarisayo na Waandishi walifika kwake, huku wakimkokota mwanamke kwa hasira. Walipaza sauti wakisema kuwa wamemfumania mwanamke huyu katika uzinzi. Wakimsukumiza kwa Yesu, walisema: "Musa alituagiza kuwa watu wa namna hii wapigwe mawe. Nawe wasemaje?"

Walipata nafasi ya kupitia ili atakavyoamua, wapate sababu ya kumshitaki. Je, atamwachia huyu mwanamke, kama ndivyo watamshitaki kwamba anadharau amri za Musa. Kama akisema kuwa anastahili kupigwa mawe, watamshitaki kwa Warumi kuwa anachukulia sheria ya kuua watu badala ya serikali ya Kirumi.

Yesu alitazama mambo haya, mwanamke mbele yake, akitetemeka kwa aibu, wala hana la kujitetea. Akaangalia nyuso za washitaki wake, na kujua maisha yao yalivyo, bila kuonyesha dalili kuwa amesikia swali walilomuuliza, aliinama chini, akaanza kuandika mchangani.

Washitaki wale walianza kuwa na wasiwasi kwa ukimya wake, wakaanza kuchukia. Lakini walipotazama chini mahali
[262] alipoandika, nyuso zao zilibadilika, maana walisoma siri za maisha yao. Wakaaibika na kuwa na aibu.

Marabi hawa waliona kuwa ni wavunja sheria pamoja na heshima yao kama watu wa dini, llipasa mume wa mke huyu ndiye atoe hukumu iwapasayo. Walimtaka Yesu atoe uamuzi wake lakini Yesu alifunua siri za matendo yao maovu.

Sheria ilisema kuwa mtu aliyeshuhudia ndiye awe wa kwanza kumpiga jiwe. Yesu sasa alipoinua macho yake na kuwaangalia washitaki wale alisema: "Mtu asiye na dhambi kati yenu awe wa kwanza kumpiga jiwe." Akaendelea kuandika.

Sasa watu wale walifunuliwa vazi la utakatifu walilojifunika, wakaonekana wako wazi mbele za Mwenyezi wala hawakujificha kitu. Wakaondoka mmoja mmoja wakiwa na aibu, wakaenda zao, wakamwacha yule mwanamke na Yesu peke yake.

Yesu akiinua macho yake na kumtazama yule mwanamke, alisema: "Mwanamke, wako wapi washitaki wako? Hakuna aliyekuhukumu? Mwanamke alisema: "Hakuna Bwana." Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu: Nenda zako, usitende dhambi tena."

Mwanamke alikuwa amesimama mbele ya Yesu akiwa na hofu nyingi. Maneno ya Yesu kuwa "Mtu asiye na dhambi awe wa kwanza kumpiga jiwe", yalikuwa kama maneno mafu kwa mwanamke. Alingoja kusikia ajali itakayompata. Alishangaa kuwaona washitaki wake wakiondoka kimya kimya, wakifedheheka. Ndipo alisikia maneno yenye matumaini yakisema. "Wala mimi sikuhukumu, nenda zako usitende dhambi tena." Roho yake ilitulia na kujaa furaha kwa ajili va upendo huo. Aliungama dhambi zake kwa machozi.

Kwake huu ndio ulikuwa mwanzo wa maisha mapya; matakatifu ya amani. Kwa kumwinua mtu huyu kutoka dhambini Yesu alitenda mwujiza mkubwa, kwamba amemponya mwovu na kumwokoa na kifo. Mwanamke huyu alikuwa mfuasi wa Yesu mashuhuri.

Yesu hakuihalalisha dhambi, wala kuihafifisha, ila alitaka kuokoa. Mtu anamhurumia mdhambi na kumwinua toka matopeni ni bora. Sio kazi ya wafuasi wa Kristo kuwaacha wenye dhambi matopeni. Watu huwachukia wenye dhambi, wakati wanapoipenda dhambi. Kristo naye huchukia dhambi na kumpendelea mwenye dhambi. Watu wanaomfuata wangekuwa na roho kama ya Yesu. Wakristo wasipende dhambi, lakini wawapende wenye dhambi, wawe tayari kuwainua na kuwatoa dhambini, na kuwaweka kwa njia ya utakatifu.

[263]

# 51 — Nuru ya Uzima

"Mimi ni nuru ya ulimwengu: Anifuataye hataenda gizani, bali atakuwa na nuru ya uzima."

Ilikuwa asubuhi, jua lilikuwa limepanda juu ya mlima wa mizeituni, na miangaza yake ilikuwa iking'aa kwenye hekalu lenye mawe ya thamani, kuta za dhahabu, ndipo Yesu aliposema, 'Mimi ni nuru ya ulimwengu." Maneno haya baadaye yalisemwa na Mtume Yohana kama hivi: 'Ndani yake ulikuwamo uzima, na uzima ulikuwa nuru ya watu. Nuru iling'aa gizani wala giza halikuiweza." "Nuru ya kweli imwangazaye kila mtu ajaye ulimwenguni." Yohana 1:4, 5, 9. Mungu ni nuru; na katika maneno yale yasemayo kwamba: "Mimi ni nuru ya ulimwengu", Kristo husema kuhusu umoja wake na Mungu na uhusiano wake na ubinadamu. Ni yeye ambaye mwanzoni alifanya "nuru ing'ae gizani." 2 Kor. 4:6. Yesu nuru ya jua, na mwezi na nyota. Jinsi mishale ya jua inavyopenya katika pande zote za nchi, ndivyo ilivyo kwa jua la haki linavyong''aa kwa kila mtu.

"Hiyo ilikuwa nuru halisi iliyomulikia kila mtu ajaye ulimwenguni." Watu hodari, wenye uwezo mkubwa na akili nyingi sana ndio waliofungua fani mbalimbali za elimu, na uvumbuzi mwingi. Lakini mmoja huwapita wote. "Wote wale waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu " "Hakuna mtu aliyemwona Mungu, Mwana pekee, aliye katika kifua cha Baba ndiye alimwona." Yohana 1:12,18.

Tunaweza kufuata walimu wakuu wa uliwengu kwa kadiri ya kumbukumbu za watu zilivyo; lakini nuru ilikuwa kabla yao. Jinsi mwezi na nyota zinavyorudisha nuru ya jua, hali kadhalika walimu wakuu wa dunia kadiri ilivyo kweli hurudisha tu elimu ya jua la haki, yaani Yesu Kristo. Elimu ya kweli hutolewa naye, ambaye,
[264] 'Ndani yake zimesitirika hazina zote za maarifa yote." Wakolosai 2:3. 'Anifuataye hatakwenda gizani, bali atakuwa na nuru ya uzima."

Wakati Yesu aliposema kuwa, 'Mmi ni nuru ya ulimwengu", watu walifahamu kwamba ndiye Masihi aliyeahidiwa. Mafarisayo na wakuu waliona kuwa hayo ni majivuno. Waliona kuwa kwa mtu

kama wao kusema hivyo haiwezekani kumvumilia zaidi. Wakasema: "Wewe ni nani?" Walitaka awaambie kama yeye ni Kristo. Adui zake waliamini kuwa hali yake na kazi yake zilikuwa tofauti na tazamio la watu kiasi kwamba akiwaambia hivyo, angalikataliwa na watu kuwa ni mlaghai."

Lakini Yesu alijibu: "Hata nilivyowaambieni tangu mwanzo, ndivyo." Alikuwa mfano halisi wa ukweli aliofundisha. "Mimi sifanyi neno kwa shauri langu, ila nasema yale niliyofundishwa na Baba. Naye aliyenituma yu pamoja nami." Hakutaka kuthibitisha kwamba yeye ni Masihi, ila alionyesha kwamba yu umoja na Baba yake, Mungu. Kati ya wasikilizaji wake, wengi walimwamini. Kwa hiyo aliwaambia: "Mkishika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli, nanyi mtaifahamu kweli, na kweli itawaweka huru."

Maneno hayo yaliwachukiza Mafarisayo wakasema: "Sisi tu wana wa Ibrahim wala hatujawa watumwa wakati wowote, wasemaje kuwa mtakuwa huru?" Yesu akawaangalia watu hawa wakiwa watumwa wa uovu, akasema kwa masikitiko: "Amin nawaambieni yeye atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.' Walikuwa katika dhambi mbaya sana, wakitawaliwa na roho ya mwovu.

Kila mtu anayekataa kujitoa kwa Mungu, hutawaliwa na nguvu nyingine. Huwa katika utumwa mbaya sana, akili zake huongozwa na Shetani, Kristo alikuja kuzivunja nguvu za Shetani. "Kama Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli."

Katika kazi ya ukombozi hakuna lazima. Mtu hawezi kushurutishwa kuamini. Kila mtu huachwa achague atakayemtumikia kwa hiari yake. Mtu anapojitoa kwa Kristo huwa na uhuru kamili wa kuchagua. Kukataa dhambi ni kazi ya roho ya mtu. Tunapotamani kuwekwa huru mbali na dhambi, na tunapolia ili tupewe uwezo kutoka juu ili utuwezeshe, moyo hujazwa uwezo wa Roho Mtakaifu, ili uweze kutii maongozi ya Roho Mtakatifu ambayo ndiyo mapenzi ya Mungu.

Sharti moja tu la kuwezesha uhuru wa mwanadamu kukamilika ni kule kuambatana na Yesu, yaani umoja na Kristo. Dhambi hufaulu tu, umoja huo unapoharibika. Kujitoa kwa Mungu kikamihfu ndiyo
heshima ya binadamu. Sheria ya Mungu ambayo ndiyo inayotuleta [265]
kwa Mungu ni 'sheria ya uhuru". Yak. 2:12.

Mafarisayo walijitaja kuwa ni wana wa Ibrahim. Wana wa kweli hawawezi kujaribu kuua mtu ambaye hunena kweli itokayo kwa

Mungu. Kule kuwa wazao wa Ibrahim tu hakuna thamani yoyote. Pasipokuwa na nia ya Ibrahim na, kutenda matendo ya Ibrahim hawawezi kuwa wana wa Ibrahim.

## Swali kuhusu kurithi Utume

Jinsi uzao wa Ibrahim ulivyojulikana, si kwa majina tu ila kwa mfanano wa hali kadhalika kwa mitume, sio kwa vyeo na madaraka, ila kwa mfanano wa tabia na hali ya maisha ya kiroho. Maisha ya kiroho waliyokuwa nayo mitume na mafundisho waliyofundisha, ndiyo ushahidi kuwa mfanano wa mitume.

Yesu alisema: "Kazi ya baba yenu ndiyo mfanyayo.' Kwa dhihaka Wayahudi walijibu 'Hatukuzaliwa kwa zinaa, tunaye Baba mmoja ndiye Mungu." Maneno haya yalitajwa ili kuwafanya watu waliomwamini Kristo wababaike. Yesu hakuyajali hayo, bali alisema: "Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda maana nilitoka kwake"

Yesu akasema: 'Ninyi ni wa baba yenu Shetani", na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kufanya. Alikuwa mwuuaji tangu mwanzo, naye hakuwa katika kweli hata kidogo, maana hakuna kweli ndani yake . . . Nisemapo kweli mbona hamwezi kuniamini?' Ukweli ni kwamba Yesu alikuwa akinena kweli hasa ndiyo sababu waongozi wa Wayahudi hawakumtaka. Ukweli uliwafunua na kudhihirisha makosa yao, hivyo hawakuutaka. Wao hawakuipenda kweli.

## Yesu hakuwa na dhambi

"Nani anishuhudiaye kuwa nina dhambi" Ninaposema kweli mbona hamwamini?" Kwa muda wa miaka mitatu maadui wa Kristo walitafuta kasoro kwa Yesu wala hawakupata. Shetani alikuwa akitafuta njia ya kumshinda, lakini hakuweza kupata chochote juu yake cha kumshika. Hata mashetani pia walilazimika kuungama na kusema: '"Wewe ni mtakatifu wa Mungu." Marko 1:24. Yesu aliishi akishika sheria mbele ya mbingu, na mbele ya viumbe ambavyo havikuanguka dhambini, na mbele ya binadamu wenye dhambi. Alinena maneno yasiyokanushika na mtu yeyote, 'Siku zote natenda mambo yapendazayo mbele za Mungu.'"

[266] Wayahudi hawakuitambua sauti ya Mungu ndani ya Mwana

wake. Walijidhani kumhukumu, lakini waukuwa wakijihukumu wenyewe. Yesu alisema: "Aliye wa Mungu husikia sauti ya Mungu, ninyi basi hamsikii, kwa sababu ninyi si wa Mungu."

Wengi wanaotaka kulaghai, kulaumu, na kudadisidadisi neno la Mungu hudhani kuwa hiyo ndiyo njia ya maendeleo na ufasaha. Lakini ni kujidhuru na kusaliti njia ya Ukristo. Kama vile maua huelekea kwenye jua ili lipate kurembeshwa, hali kadhalika moyo wa mtu wapaswa kuelekea kwa jua la haki ili kurembesha tabia; kwa neema ya Kristo.

Yesu aliendelea kusema: "Baba yenu Ibrahim alishangilia kuona siku yangu, akaiona na kufurahi." Ibrahim aliomba kabla ya kufa kwake amwone Masihi. Alipewa ufahamu wa pekee. Alifahamishwa kuhusu kufa kwa Mwenyezi kwa ajili ya dhambi. Kwa jambo hili alifanya kielelezo chake mwenyewe. Aliagizwa: "Umchukue sasa mwana wako Isaka, umpendaye . . . ukamtoe sadaka ya kuteketezwa." Mwanzo 22:2. Juu ya madhabahu alimweka mwana wa ahadi, kisha akiinua kisu chake kumchinja, ili kumtii Mungu, alisikia sauti ya Mungu kutoka mbinguni ikisema: "Usimchinje mwanao, kwani sasa najua kuwa unamcha Mungu, ukiwa hukumzuilia mwanao Isaka, mwana wa pekee." Mwanzo 22:2,12. Amri kali hii ilitolewa kwa Ibrahim ili apate kuiona siku ya Kristo, na kutambua upendo wa Mungu kwa ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili apate kuuokoa.

Kwa kujitoa kikamilifu kwa Mungu, Ibrahim alionyesha kuwa kwa ajili ya kutoa Mwana wake wa pekee ili kuuokoa ulimwengu, Mungu alikuwa akitoa kipawa cha ajabu ambacho mtu hajawahi kutoa.

Katika kipawa cha Mungu badala ya Isaka, ilitangazwa kwamba hakuna mtu awezaye kujitolea, kafara ili ajiokoe. Kafara za watu wa mataifa wanazotoa ili kujifaidia, hazikubaliki mbele za Mungu. Hakuna mtu awezaye kumtoa mtoto wake awe kafara. Mwana wa Mungu peke yake ndiye awezaye kubeba dhambi zote za ulimwengu.

Maneno ya Kristo kuhusu Ibrahim hayakuwapa wasikilizaji wake maana kubwa zaidi. Mafarisayo waliona tu ni mambo ya utani. Waliendelea na hali yao tu ya kuona kuwa Yesu ana wazimu. Maana walisema: 'Hujapata bado hata miaka hamsini, nawe umemwona lbrahitnu?' Yesu alijibu kwa fahari: "Amin, amin nawaambieni kabla Ibrahim hajakuwapo, mimi nipo." Mkutano wote ukawa kimya. Jina

la Mungu lililopewa Musa ili alitangaze, mtu huyu Rabi wa Galilaya [267] anajitia kuwa ni yeye. Amejitangaza kuwa yeye ni wa milele kama Mungu, ambaye "matokeo yake yamekuwa tangu milele." Mika 5:2.

Makuhani na wakuu wakampigia kelele Yesu kwa kuwa anakufuru, maana anajitukuza mwenyewe. Watu wengi waliungana na makuhani na marabi wakachukua mawe ili kumpiga. Lakini Yesu akajificha akatoka hekaluni.

## Mtu aliyezaliwa akiwa kipofu

Yesu alipokuwa akipita alimwona mtu aliyezaliwa akiwa kipofu. Wanafunzi wake walimwuliza: 'Bwana, ni nani aliyetenda dhambi hata huyu akazaliwa akiwa kipofu, ni yeye au ni wazazi wake?' Yesu akajibu: "Mtu huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake, lakini kazi za Mungu zipate kuonekana ndani yake .... Aliposema hivi, alitema mate udongoni, akafanya tope, akampaka kipofu machoni, akamwambia, "Nenda ukanawe katika dimbwi la Siloam (tafsiri yake' aliyetumwa). Akaenda, akanawa akapata kuona."

Wayahudi walikuwa wakiamini kuwa, dhambi huadhibishwa katika maisha. Shetani ambaye ndiye asili ya dhambi amewaaminisha watu kuwa magonjwa na kifo ni adhabu ya Mungu anayowaadhibu watu. Mtu yeyote apatapo mambo haya huangaliwa kuwa kama mwenye dhambi mkuu. Hivyo njia iliandaliwa kwa Wayahudi ili kumkataa Yesu.

"Aliyechukua maafa yetu na kuchukua huzuni zote" aliangaliwa na Wayahudi kama aliyepigwa na Mungu na kuteswa, nao walimfichia nyuso zao." Isaya 53:4, 5.

Imani ya Wayahudi juu ya jambo hili ilishikwa pia na wanafunzi wa Yesu. Baada ya kumpaka tope la macho, Yesu alimpeleka kipofu kunawa dimbwini, na macho yake yakaona. Basi Yesu alilijibu swali la wanafunzi wake kwa njia ya tendo. Wanafunzi hawakushughulika na jambo la ni nani aliyetenda dhambi, au hakutenda; ila walifahamu rehema za Mungu kwa kuponya kipofu. Hapakuwa na dawa katika dimbwi alilokwenda kipofu huyu kunawa, ila dawa ilikuwa ndani ya Kristo.

## Muujiza siku ya sabato

Wayahudi walishangaa na kuchukizwa kwa kuponywa, ambako ni mwujiza uliofanyika siku ya Sabato.

Majirani walipomwona yule aliyekuwa kipofu akiona, waliingia shaka, maana alionekana kana kwamba ni mtu mwingine kabisa. Uso wake ulikuwa unang'aa wengine walisema: "Ndiye," wengine walisema "Amefanana naye." Lakini yeye alimaliza mambo kwa kusema kuwa ni yeye. Aliwasimulia habari za Yesu na jinsi alivyo- [268]
pony wa. Ndipo walimwuliza "Wapi aliko sasa? Alisema, "Sijui."

Katika baraza la Wayahudi, aliulizwa jinsi alivyoponywa. Aliwaambia: "Alifanya tope akanipaka machoni, nikanawa, na sasa naona. Mafarisayo walisema kuwa, huyu si mtu wa Mungu, kwa kuwa haitunzi Sabato. Mafarisayo walikazania utunzaji wa Sabato, na hali walikuwa wanapanga kuua mtu siku ya Sabato. Lakini watu wengi walisadiki kuwa aliyemponya kipofu ana uwezo zaidi ya binadamu. Walisema: "Mtu mwenye dhambi anaweza kufanya mwujiza?"

Mara tena Marabi walimwuliza kipofu: "Wewe wasemaje juu ya mtu huyu, aliyekuponya? Akasema: 'Ni nabii." Mafarisayo wakasema kuwa, hakuzaliwa akiwa kipofu. Wakawaita wazazi wake wakasema: "Je, huyu ni mwana wenu msemaye kuwa alizaliwa kipofu?"

Mtu mwenyewe yuko anayeeleza kuwa alizaliwa kipofu na sasa anaona. Mafarisayo waliona kuwa ni heri kukataa ushuhuda wake, kuliko kukubali kosa lao. Walishikilia ukaidi wao, na kujitumainia kuwa wao, Mafarisayo ni wenye haki kamili. Mafarisayo walikuwa na tumaini moja limebaki. Nalo ni kuwatisha wazazi wa mtu huyo waseme mengine. Waliuliza: "Sasa anaona kwa vipi?" Maana ilikuwa imetangazwa kwamba, mtu atakayemkiri Yesu kuwa ni Masihi, atatengwa mbali na ushirika, yaani atatengwa kwa siku thelathini. Hukumu hiyo ilihesabiwa kuwa ni msiba mkubwa, jambo kubwa alilotendewa mwana wao, liliwaaminisha, lakini kwa ajili ya hofu walisema: "Tunajua kuwa huyu ni mwana wetu, na alizaliwa kipofu, walakini jinsi alivyopata kuona hatujui. Yeye ni mtu mkubwa, mwulizeni yeye mwenyewe." Walitupa mambo yote kwa mwana wao.

## Mwujiza haukanushiki

Hoja za Mafarisayo na chuki yao, pamoja na hali yao ya kutoamini viliwazibua watu, wakaona hali halisi ilivyo. Walijiuliza wenyewe kwa wenyewe wakisema, Yawezekana kwamba Mungu afanye jambo kubwa kama hili kwa njia ya mtu asiyemwamini, jinsi Mafa:risayo wanavyosema kuwa Yesu si mtu wa Mungu?

Mafarisayo hawakuweza kukanusha mwujiza huo. Mtu aliyekuwa kipofu alisimulia kisa chake kwa furaha sana na shukrani kubwa. Mafarisayo walijaribu tena kumkatisha tamaa ili anyamaze. Walisema: "Msifu Mungu, kwani tunajua ya kuwa mtu huyu Yesu ni mwenye dhambi." Usiseme kuwa mtu huyu amekuponya, Mungu
[269] ndiye aliyekuponya. Kipofu akajibu: "Kwamba yu mwenye dhambi, au la, mimi sijui. Najua jambo moja tu, 'nilikuwa kipofu. na naona."

Wanafiki hawa walipojaribu kumkosesha mtu huyu asiamini, Mungu alimsaidia, akasimama imara, wala hakuyumbishwa yumbishwa. Aliwajibu akisema: "Niliwaambia tayari, hamkusikia?" Je, mnataka kuwa wanafunzi wake? Kisha walimtukana wakisema: "Wewe u mwanafunzi wake sisi tu wanafunzi wa Musa. Tunajua kuwa Mungu alizungumza na Musa, lakini mtu huyu hatujui atokako."

Bwana alimpa neema na usemi wa kukata na kukemea unafiki wa Mafarisayo hawa, naye akawa mashahidi wa Kristo. Hapa Yesu alifanya mwujiza, na Mafarisayo walikiri bila kujua uwezo wake wa kufanya hivyo. Yule mtu akasema: . "Hii ni ajabu! Hamjui atokako, naye amenifumbua macho! Twajua kuwa Mungu hawasikii waovu, lakini mtu akiwa mcha Mungu na kutenda yampendezayo humsikia. Tangu mwanzo wa ulimwengu hatujasikia kuwa mtu amemfungua kipofu macho. Kama mtu huyu Yesu angekuwa mwenye dhambi, asingeliweza, kutenda lolote."

Hoja ya mtu yule haikupata jawabu. Mafarisayo hawakupata la kujibu. Walinyamaa kwa muda. Kisha Makuhani na Marabi walimkemea kwa ghadhabu, wakisema: "Ulizaliwa katika dhambi, nawe sasa watufundisha sisi?" Wakamwondoa hapo.

Yesu aliposikia mambo waliyomfanyia, alipomwona, akamwambia: "Unamwamini mwana wa Mungu?" Kwa mara ya kwanza yule alimtazama Mwokozi uso kwa uso. Alikuwa amewaona wazazi wake, wakihangaika na kuwa na wisiwasi, alikuwa ameona nyuso

za Marabi zenye shari, sasa macho yake yaliona uso mtulivu, uliojaa upendo, ambao ni uso wa Yesu. Yeye aliyekuwa akimwuungamia kwa shida na wasiwasi mkuu, sasa amemwona uso kwa uso.

Kwa swali la Mwokozi, yule mtu "Ni nani Bwana nipate kumwamini?" Yesu akasema: "Umemwona na ndiye unayesema naye." Ndipo yule mtu akajitupa miguuni pake akamsujudia. Kristo alijidhihirisha kwa mtu huyu, na kumpokea kama aliyetumwa na Mungu.

Kundi la Mafarisayo lilikuwa limekusanyika hapo karibu, na Yesu akaona tofauti ya maneno yake na kazi yake ilivyo dhahiri. Yesu akasema: "Nimekuja ulimwenguni kwa hukumu, ili wanaoona wawe vipofu, na vipofu wapate kuona." Watu wa siku za Mwokozi walikuwa na bahati ya kumwona Mungu kwa ukamilifu. Lakini [270]
katika bahati hii ilipita bure tu. Tabia zao zilipimwa, na maelekeo yao yalionekana wazi.

Baadhi ya wasikilizaji wake waliona kuwa maneno yanawahusu, kwa hiyo waliuliza: Sisi nasi vipofu? Yesu akajibu, "Kama mngalikuwa vipofu msingelikuwa na dhambi." Kama Mungu amewawezesha kuona ukweli, kutojua kwenu kusingekuwa hatia. Lakini mwasema: "Tunaona." Mwadhani kuwa mnaona, na kuikataa kweli " Mafarisayo walikataa kuja kwa Kristo, wakaachwa gizani. Yesu alisema "Dhambi zenu zinakaa."

[271] ## 52 — Mchungaji, Mungu

“Mimi ndimi Mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. Yohana 10:11.

Yesu alipata usikizi kwa watu wake kwa njia ya kuwapa mambo wanayoyazoea kufanya. Kwa watu waliomwamini aliwatolea mfano wa Mchungaji mwema. Hakuna mfano uliojulikana kwa wasikilizaji wake zaidi ya huu. Wakikumbuka fundisho lake, wanafunzi wake wataweza kuona jinsi Kristo anavyofanana na kila mchungaji, mwaminifu na wao kama kondoo wasioweza kujisaidia.

Mafarisayo walikuwa wamemfukuza mtu mmoja, aliyemshuhudia Kristo. Walimwondoa mtu, ambaye Mchungaji halisi alikuwa akimtafuta kwa njia hii walijionyesha kuwa ni wachungaji wasiofaa kitu. Na sasa Yesu alijitambulisha kuwa mchungaji halisi wa kundi la Bwana.

“Asiyeingia kwa mlango, lakini akiingia kwa kupitia mahali pengine ni mwizi na mnyanganyi. Lakini aingiaye kwa mlango ni mchungaji wa kondoo.” Mafarisayo walipowaza mioyoni inwao maana yake, Yesu aliwaambia waziwazi: “Mimi ndiye mlango wa kondoo, mtu akiingia kwangu atakuwa salama, ataingia na kutoka na kupata malisho. Nimekuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.”

Kristo ndiye mlango wa zizi la Mungu. Watu wake tangu zamani wamepata kuingia. Mifano yake ikitiwa weusi, na mafundisho yake yakipotoshwa, hata hivyo wamemtazama Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Yohana 1:29. Ibada na kawaida vilikusudiwa kuwaletea watu matumaini na kuwapa watu haki na utulivu pamoja na Mungu. Lakini waliovumbua mambo mengine mbali na Kristo, ili kuwaingiza zizini, ni wezi na wanyang’anyi.

[272] Makuhani, wakuu, waandishi na mafarisayo, wameharibu mfano uliowekwa ili kuwaongoza, pamoja na uchungaji wa kweli na maji yaliyo hai. Maandiko huwataja hawa kuwa: “Wagonjwa hawakuwatia nguvu, wala hamkuwaponya wenye maradhi, wala hamkuwa-

funga waliovunjika, wala kuwarudisha waliofukuzwa, wala kutafuta waliopotea, bali kwa nguvu na ukali mmewatawala.” Ezekiel 34:4.

Kila taifa Umekuwa na walimu wake, na dini yake pamoja na matoleo yake ya dini, ambayo ni mbali kabisa na ukombozi wa Kristo, wamekuwa wakigeuza nyuso zao kinyume na Mungu na kuwajaza watu na hofu tu. Watu mamilioni wanazo dini za uongo, ambazo haziwaletei furaha, ila huwaletea giza na hofu za siku za usoni. Injili ya neema ya Mungu peke yake ndiyo huwainua watu na kuwaletea utulivu kuliko kitu kinginecho. Anayewageuzia watu mbali na Kristo, huwageuzia watu mbali na maendeleo yoyote na kuwaondoa katika njia ya kupata utukufu na uzima. Mtu kama huyu ni mwizi na mnyang’anyi.

## Wajibu wa Mchungaji Mwaminifu

Katika upande wa Mashariki kazi ya uchungaji ilikuwa kazi ya daima na ambayo haikomi Wanyang’anyi au wanyama wakali walikuwa tayari kutawanya kundi la kondoo. Ulinzi wa mchungaji ulihitajika katika maisha yake yote. Yakobo aliyechunga makundi ya kondoo za Labani alisema: “Mchana jua likanipata, na baridi usiku, usingizi, ukanitoka machoni mwangu.” Mwanzo 31:40. Kijana Daudi alipokuwa akilinda kondoo za Baba yake alikesha ili kuwalinda kondoo wasikamatwe na wanyama wa mwitu.

Mchungaji alijishughulisha na wale aliokabidhiwa. Kila kondoo alikuwa na jina lake, naye alimwitikia mchungaji. Ndivyo na Mchungaji anajua kondoo waliotawanyika ulimwenguni. Yesu alisema: ‘Nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu.” Isaya 43:1. Yesu atujua kama tulivyo, kila mmoja wetu, na anajisikia kuwa na hali yetu ya udhaifu wetu. Anafahamu nyumba tunazoishi ndani yake. Wakati fulani amewaagiza watumishi wake kwenda katika nyumba fulani katika mji fulani ili kumtafuta kondoo wake aliyepotea.

Kila mtu anajulikana kwaYesu kana kwamba ndiye mwenyewe aliyefiwa na Yesu. Masikitiko ya kila mtu hugusa moyo wa Yesu. Alikuja kuwavuta watu wote kwake. Anajua mtu anayemsikia kwa furaha, na yuko tayari kuja chini ya ulinzi wake. Yeye husema: [273]
“Kondoo wangu husikia sauti yangu, nami nawajua, nao hunifuata.”

## Kwa nini Kondoo wake humfuata kwa furaha

Mchungaji wa nchi za mashariki hakuwa akifukuza kondoo kwa kutumia fimbo yake. Hakuwatisha kondoo kwa kuwasukuma, ila yeye alikuwa akiwatangulia kondoo, nao humfuata nyuma yake. Ndivyo hivyo na Mchungaji ambaye ni Mwokozi. Husema: "Nimekupenda upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu." Yeremia 31:3.

Wanafunzi wa Yesu hawamfuati kwa kuogopa adhabu yake, au kwa kutamani zawadi yake. Humfuata kwa ajili ya upendo wake uliodhihirishwa kwake, tangu kuzaliwa katika Bethlehemu, ndani ya hori, mpaka kufa kwake Kalwari juu ya msalaba. Onekano lake huvutia watu na kuwaburudisha kabisa. Upendo huamshwa moyoni mwa mtu, naye husikia sauti yake na kumfuata.

Mchungaji hutangulia mbele ya kondoo zake, na kukumbana kwanza na hatari zilizoko mbele. Hivyo ndivyo Yesu anavyofanya kwa watu wake. Njia ya mbinguni hutakaswa na nyayo za Mwokozi.

Ingawa sasa anaishi katika utukufu wa mbinguni, Yesu hakupoteza hali yake ya fadhili. Leo mikono ile iliyopigiliwa na misumari, huonyeshwa ili kuwabariki watu wake waliomo ulimwenguni. Asema: "Hawatapotea kamwe, wala hakuna mtu atakayewapokonya toka mikononi mwangu." Mtu yeyote atakayejitolea kwa Kristo huwa wa thamani kabisa kuliko ulimwengu wote. Yesu hatamwacha mtu yeyote aliyemfia. Atawashikilia kabisa, isipokuwa watu wake wamwache wenyewe.

## Kristo bado ni Mchutigaji wetu binafsi

Msaidizi wetu ambaye hatuachi kamwe, hawezi kutuacha tupigane na majaribu sisi wenyewe, mpaka tushindwe. Ingawa sasa hatumwoni uso kwa uso, sikio la imani humsikia akisema: "Usiogope, mimi nipo pamoja nawe. Nimejitwika huzuni zako, nimejitia katika mashindano yako nimejikinga katika majaribu yako. Ninajua machozi yako, na mimi pia nimelia. Masikitiko makuu kabisa ya wanadamu ninayafahamu. Wewe hukuachwa kamwe. Ingawa masikitiko yako hayasikiwi mahali popote duniani, nitazame mimi upate kuishi angalia." Isaya 54:10.

Kwa kuwa sisi ni kipawa cha Baba yake, na zawadi ya kazi yake, Yesu hutupenda kama watoto wake. Anakupenda wewe. [274] Mbingu haiwezi kutoa kitu kikubwa zaidi kuliko hiki kwa hiyo amini tu. Yesu aliwafikiri watu wote wa ulimwengu waliokoseshwa na wachungaji wanyonge. Yeye asema: "Ninao kondoo wasiokuwa wa zizi hili, inanipasa niwalete hao nao. Wataisikia sauti yangu kwa hiyo kutakuwa kundi moja na mchungaji mmoja."

Kwa hiyo Baba anipenda, kwa kuwa nautoa uzima wangu, na nitautwaa tena .... Nina uwezo wa kuutoa, na nina uwezo wa kuutwaa tena. Yesu akiwa wa jamii ya wanadamu, alikuwa mtu wa mwili. Akiwa kama Mungu alikuwa ndiye asili ya uzima wa ulimwengu. Alishinda mauti. Lakini alitoa maisha yake, ih apate kuyatwaa tena. "Aliyejeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa makovu yetu .... kwa kupigwa kwake tumepona. Sisi sote kama kondoo waliopotea, kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe na Bwana ameweka maovu yetu sisi sote." Isaya 53-5, 6.

[275] # 53 — Safari ya Mwisho Kutoka Galilaya

Kadiri huduma yake ya duniani ilipokaribia kumalizika, Yesu alibadili kazi yake yaani aligeuza namna ya kufanya kazi. Pale na pale alikuwa akiepuka makutano ya watu wasimsifu, na aliwaagiza watu wasimtajetaje.

Wakati wa Sikukuu ya Vibanda alikuwa amefika Yerusalemu, bila kujidhihirisha yaani kwa siri. Lakini katika safari yake ya mwisho haikuwa kwa siri. Alisafiri waziwazi, akitangazika huko na huko, ambavyo haikuwa kawaida yake. Sasa alikuwa akienda mahali pa kujitolea kwake wakfu, na kwa hiyo lazima watu wafahamu sana.

“Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu naye hana budi kuinuliwa. Yohana 3:14. Macho yote lazima yamwangalie, ili kuona kafara iliyotolewa kuleta wokovu katika ulimwengu uliopotea.

Wanafunzi wangalimkataza kwenda Yerusalemu. Walikuwa Wanajua uhasama mkubwa wa waongozi wa dini waliokuwa nao huko Yerusalemu. Kwa Yesu ilikuwa safari nzito sana kupeleka wanafunzi wake mahali pa namna hiyo, wakaone mambo ya kukatisha tamaa na huzuni vilivyomngojea Yesu huko Yerusalemu. Shetani alikuwa tayari kuhimiza majaribu hayo yampate Kristo. Kwa nini aende huko Yerusalemu kwenye hali kama hiyo? Kila upande kulikuwako na wenye dhiki wengi waliokuwa wakitaka kuponywa. Kwa nini asiende katika ulimwengu mpana, mahali anapoweza kunena neno lake na kuponya watu? Kwa nini asiende kuwaangazia watu mamilioni wanaokaa gizani? Adui za Kristo walimshambulia kwa ukali na majaribu ya hila. Kama Yesu angalibadili kusudi lake, na kufanya vinginevyo ulimwengu ungaliangamia kabisa.

[276] Lakini Yesu amenuia kabisa kwenda Yerusalemu kwa vyovyote vile. Sheria yake imara ni kutenda mapenzi ya Baba yake peke yake. Tangu utoto wake, alimwambia Mariamu mama yake, “Hamjui ya kuwa inanipasa kuwa katika shughuli ya Baba yangu?” Luka 2:49.

Lakini katika mpango mkuu wa Baba, kuhusu saa ya kujitoa kwa ajili ya kuwa kafara ya ulimwengu, ilikuwa karibu kufika.

Hamwezi kukosea, wala Baba pia hawezi. Adui zake wamepanga kumwua kwa muda mrefu, sasa muda umefika wa kutoa maisha yake.

Alituma wajumbe wamtangulie. Nao wakaenda, wakaingia mjini huko Samaria ili kumtayarishia. Lakini watu wa Samaria walikataa kumkaribisha, kwa sababu alikuwa akienda Yerusalemu; hawakufahamu kuwa walikuwa wakikikataa kipaji cha mbinguni. Lakini Wasamaria walipoteza yote kwa ajili ya chuki na ushindani wao.

Yakobo na Yohana waliokuwa wajumbe wa Kristo, waliudhika sana kwa jambo hilo. Walighadhabika kwa kuwa Yesu ametendwa vibaya kwa kukataliwa hivi, na Wasamaria. Walimwambia Kristo kuwa watu hao wamekataa hata kuwapa nafasi ya kulala usiku mmoja tu. Wakiuona mlima wa Karmeli ambako Eliya aliwateketeza manabii wa Baali ambao ni waongo, walisema: "Huwezi kuamuru moto utoke mbinguni na kuwateketeza wabaya hawa?" Halafu jibu la Yesu liliwashangaza aliposema, "Hamjui roho mliyo nayo, kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuangamiza watu, ila kuwaokoa." Kisha akaenda katika kijiji kingine.

Siyo kazi ya Kristo kuwalazimisha watu wamwamini. Yeye hutaka watu wamwamini kwa hiari yao wenyewe kumfuata wakivutwa na upendo wao. Hakuna ushahidi mkubwa zaidi wa roho ya kishetani kuliko huu iwapo tunawachukia wale wasiokubaliana na sisi katika imani yetu, na kutupinga. Hakuna kitu kinachomchukiza Mungu zaidi kuliko wakristo kuwasumbua wale waliotiliwa na Kristo na kununuliwa kwa damu yake.

Miezi ya mwisho mwisho wa kufunga kazi ya Kristo, ilitumika zaidi katika sehemu ya Perea, wilaya ya ng'ambo ya Yordani kutoka Uyahudi. Tazama Marko 10:1. Hapo watu wengi walimfuata, na kazi yake ya kwanza ilirudiwa.

Kama alivyowatuma wale mitume kumi na wawili, ndivyo sasa alituma wengine sabini, akawaagiza wamtangulie, naye atafuata nyuma. Akawatuma waende wawili wawili katika kila mji. Watu hawa walikuwa katika mafundisho kuhusu kazi hiyo. Walikuwa na bahati ya kukaa pamoja naye na kusikiliza mafundisho yake.

Maagizo aliowaagiza wale kumi na wawili, yalikuwa kwamba, [277]
wapite kwa watu wa mataifa, au kwa Wasamaria. Lakini wale

sabini hawakuagizwa hivyo. Ingawa Yesu alifukuzwa na Wasamaria, lakini upendo kwao hakupunguzwa. Aliwapenda kamili. Wale watu sabini kwa mara ya kwanza walikwenda katika miji ya Samaria wakalihubiri neno kwa jina lake.

### Wasamaria waliamini upendo wa Yesu

Katika agizo la Yesu kwa wanafunzi wake kabla ya kupaa kwenda mbinguni, alitaja Samaria pamoja na Yerusalemu na Uyahudi mahali alipokuwa akifanyia kazi, ya kuhubiri Injili. Walipofika Samaria walikuta watu wako tayari kuamini. Wasamaria waliona kwamba ijapokuwa hawakumtendea Yesu vizuri, lakini alikuwa akiwafikiria mambo ya heri, kwa hiyo waliamini neno la Mungu. Baada ya kupaa kwake kwenda mbinguni, wanafunzi wake walipata mavuno makubwa ya waongofu kwa watu waliokuwa na uhasama kwao. "Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima, hukumu duniani." Isaya 42:3.

Katika kuwatuma watu sabini, Yesu aliwaagiza kuwa wasiwalazimishe watu ili wawakaribishe. "Katika mji wowote mwingiamo, wasipowakaribisha tokeni humo na kukung'uta mavumbi ya miguu yenu, na kusema kuwa mavumbi haya yatawashuhudia mbele za Mungu" Haikuwapasa kufanya hivyo kwa hasira, ila kwa masikitiko ya kuwakataa wajumbe wa Bwana. Kuwakataa wajumbe wa Bwana ni sawa na kumkataa Kristo mwenyewe.

### Waongon wa Dini waliwapotosha watu wengi kumkataa Kristo

Yesu alisema: "Nawaambieni itakuwa heri kwa Sodoma siku ile kuliko mji ule." Halafu mawazo yake yaligeukia miji ya Galilaya ambako amefanya kazi nyingi zaidi. Kila siku Mkuu wa uzima alikuwa akiingia na kutoka katika miji hiyo. Utukufu wa Mungu umekuwa ukiangaza kwao na walikuwa wakimfuata Mwokozi hatua kwa hatua. Hata hivyo wameukataa ujumbe wa kipawa cha mbinguni. Marabi walikuwa wamewaonya watu wasije kupokea mafundisho ya mwalimu mpya huyu. Badala ya kulipata neno la Mungu na kujisomea wenyewe, watu walifuata tu mambo waliyoelekezwa na makuhani na waongozi wa dini, na kumkataa mkuu wa uzima na ukweli anaoufundisha. Wakachagua kufuata mapokeo na kukataa

kweli. Wengi walikuwa kama waongofu, lakini hawakushika kamili njia ya uongofu halisi. Kwa hiyo waliukataa ukweli ambao ungewaletea wokovu. [278]

Shahidi wa kweli husema: "Tazama nasimama mlangoni, nabisha." Ufu. 3:20. Kila neno la kuingilia katika uongofu lisemwalo na wajumbe wa Mungu ni mbisho katika mlango wa moyo wa mtu. Ni sauti ya Yesu akibisha ili afunguliwe. Kila kubisha kusikoitikiwa, humfanya mtu kuwa mgumu zaidi na zaidi. Moyo huzoea ufedhuli na kutojali. Hukumu ya Mungu haitakuja kwa sababu tumekuwa tukiishi katika makosa, ila kwa sababu tumekataa kujali njia za Mungu za kutusaidia tuifikie kweli.

Kazi yao ilipomalizika, wale sabini walirudi kwa furaha wakisema: "Nilimwona Shetani kama umeme akianguka kutoka mbinguni." Yesu alitazama kupita kwenye msalaba wa Kalwari na mateso yake na aibu akaona shindano kuu la mwisho, wakati Shetani atakapoangamizwa ndani ya dunia iliyokuwa imechafuliwa vibaya na udanganyifu wake, na uasi.

Tangu hapo wafuasi wa Yesu lazima wamwangalie Shetani kama adui ambaye ameshindwa tayari. Katika msalaba alipata ushindi kwa ajili ya wafuasi wake. Ushindi huo ndio Kristo anawatakia wafuasi wake wote,waupate uwe wao. Asema, "Tazama, nimewapa uwezo wa kuwakanyaga nyoka, na nge, na nguvu zote za yule mwovu, wala hakuna kitu kitakachowashinda." Nguvu za Mwenyezi na Roho Mtakatifu ni ngome ya kila mfuasi wa kweli wa Kristo. Hakuna mfuasi wa kweli mwenye kutubu kikweli anayedai ulinzi kwa Kristo, atakayepitwa tu na kuachwa katika uwezo wa mwovu Shetani. Majaribu na matatizo yanapokuja, tumtazame Yesu, ambaye ndiye msaada wetu. Tumshukuru Mungu, kwa kuwa tunaye Mwokozi hodari, aliyemfukuza mwovu kutoka mbinguni. Kwa nini tusizungumze juu yake na ushindi wake? Mungu hatawaacha kamwe watu wake washindane wenyewe na yule mwovu Shetani.

### Siri ya Uwezo wa Binafsi

Yesu aliongeza kusema; "Msifurahi kwa kuwa pepo wanawatii kwa jina langu, ila furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni." Angalieni ubinafsi usiwaingilie mkafanya kazi kwa nguvu zitokanazo na ninyi wenyewe. Ubinafsi uko tayari

kuwaingilia, mkadhani kuwa kufaulu kazi ni kutokana na nguvu zenu wenyewe. Tunapotambua udhaifu wetu, hatuna budi kutegemea nguvu ambazo sio zetu. Tazama 2 Wakorintho 12:10. Hakuna
[279] kitu kinachotusukuma katika utendaji wetu kwa hakika kama upendo wa Kristo. Lazima tushirikiane na Mungu, ndipo atatuvuvia Roho wake atakayetuwezesha kuwafikia wanadamu wenzetu. Kadiri utakavyoambatana na asili ya uwezo wote na nuru, ndipo utakuwa na uwezo zaidi wa kufanya kazi ya Mungu.

Jinsi wale sabini walivyomsikiliza Kristo, Roho Mtakatifu alivyoandika ukweli mioyoni mwao. Na kadiri makutano ya watu walivyokuwa wakiwazunguka, walikuwa kama wamefungwa ndani ya Mungu.

Yesu akijua ya kuwa wamevuviwa na uwezo wa juu, alisema: "Nakushukuru Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa umewaficha mambo haya wenye hekima, ukawafunulia watoto wachanga, maana ndivyo ilivyokupendeza wewe."

Wenye heshima na wakuu wa dunia hii, hawakuweza kutambua tabia ya Kristo. Ila wavuvi na watoza ushuru ndio waliofunuliwa mambo yasiyoonekana. Kila mara walipojitolea kwa Roho Mtakatifu na uwezo wake, mioyo ya wanafunzi iling'arishwa na uwezo wa mbingu. Wakatambua kuwa Mwenyezi Mungu aliyejivika katika ubinadamu, yuko pamoja nao. Kila mara alipoeleza mambo ya Agano la Kale na kutaja mambo yanayomhusu Yeye, walikuwa wakijisikia kuwa katika hali ya mbinguni. Walikuwa na ufahamu wazi kuliko walioyaandika. Hivyo waliweza kusoma maandiko ya Agano la Kale kama ni mafunuo mapya kutoka kwa Mungu. Walimwona yule ambaye ulimwengu haumjui." Yohana 14:17.

Njia moja tu ambayo tutaweza kufaulu kupata ujuzi kamili wa ukweli ni kunyenyekeza mioyo yetu na kujiweka chini ya Roho ya Kristo. Elimu ya sayansi ya wanadamu ni ndogo nno kuweza kufahamu mpango wa ukombozi. Filosofia haiwezi kuueleza mpango wa ukombozi. Lakini sayansi ya ukombozi yaweza kujulikana kwa maisha yenvewe. Mtu anayeona maisha yake ya dhambi ndiye atafahamu thamani ya Mwokozi.

Yesu alikuwa akifundisha mafundisho kamili alipokuwa akienda Yerusalemu. Katika sehemu ya Perea watu hawakushikwa sana na mambo ya makuhani, kwa hiyo mafundisho ya Yesu yaliwaingia zaidi mioyoni.

Katika miezi ya mwisho, ndipo mifano mingi ya Yesu ilinenwa. Makuhani na Marabi hawakuweza kuipotosha. Walakini haikuwafaidia ipasavyo, ila waliendelea na mpango wa uhasama. Kristo aliutoa mfano safi wa kondoo aliyepotea na akautafsiri wazi na kusoma juu ya fedha na mwana mpotevu. Baada ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu wanafunzi, walipokwenda kazini, wakikabil- [280]
iana na mashutumu na umaskini, na mateso, kila mara walijipa moyo walipokuwa wakikumbuka mafundisho hayo ya safari ya mwisho. "Msiogope enyi kundi dogo, kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapeni ufalme. Viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Jifanyieni mifuko isiyochakaa akiba isiyopungua katika mbingu mahali pasipokaribia mwizi, wala nondo haharibu. Kwa kuwa hazina yenu ilipo ndipo itakapokuwa na mioyo yenu." Luka 12:32-34.

[281]

# 54 — Msamaria Mwema

Wakati Kristo alipokuwa akifundisha watu, Mwanasheria mmoja alisimama, akamjaribu na kusema: "Bwana nitafanya nini ili niurithi uzima wa milele?" Makuhani na Marabi walikuwa wakitaka kumtatanisha Kristo, kwa kutaka Mwanasheria, amwuliza swali la namna hiyo. Lakini Mwokozi hakutaka mabishano. Kwa hiyo alisema: "Kumeandikwa nini katika sheria? Unasomaje humo?' Aliligeuza swali hilo la wokovu kuwa mambo yahusuyo amri za Mungu.

Mwanasheria akasema: "Mpende Bwana Mungu kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa nia yako yote, na jirani yako kama nafsi yako." Yesu akasema: "Umesema vema, enenda ukafanye hivyo ndipo utaishi "

Mwanasheria alikuwa akijifunza maandiko mtakatifu apate kujua maana yake. Katika jibu lake kuhusu matakwa ya sheria, alisema kuwa hakuna faida ya kukariri-kariri tu maandiko ya sheria bila vitendo. Lakini kuna matendo mawili hasa ambayo hutegemewa na sheria yote na manabii pia. Jibu lililosifiwa na Kristo lilifanya Marabi na Mwokozi wakabiliane uso kwa uso.

Yesu aliposema "Fanya hivyo, ndipo utaishi", aliiweka sheria katika mwungano wa Mungu. Haiwezekani kushika sheria moja na kuvunja nyingine. Kanuni ile ile huhusu zote, yaani kumpenda Mungu na mwanadamu; ndivyo vitakiwavyo katika maisha.

Mwanasheria alikubaliana na usemi wa Kristo. Hakuwa akionyesha upendo kwa wenzake. Lakini badala ya kutubu, alijaribu kujitakasa kwa kusema: "Jirani yangu ni nani?" Katika Wayahudi swali hili lilikuwa na msukosuko. Watu wa mataifa na Wasamaria walihesabiwa kama wageni, na maadui, lakini ni wapi ubaguzi wa
[282] makabila na utengano wa watu unapotoka? Je, watawahesabu wajinga na watu duni katika jamii moja kuwa 'wachafu' nao ni jirani pia?"

## Ondoa Giza kwa kuruhusu Nuru

Yesu hakuwakanusha wapinzani wa dini, waliokuwa wanatafuta nafasi ya kumshambulia. Lakini kwa njia ya kisa kidogo rahisi aliwapa kitu kilichowaeleza upendo wa kimbingu ulivyo. Kisa hicho kilitosheleza, hata yule mwanasheria akaungama. Njia bora ya kushughulikia makosa ni kueleza ukweli ulivyo. Yesu akasema: "Kulikuwa na mtu aliyekuwa akisafiri toka Yerusalemu kwenda Yeriko. Akaangukia katika kundi la maharamia, waliomnyang'anya mali yake, na kumpiga sana, wakamwacha nusu ya kufa. Kwa bahati Kuhani alikuwa akienda katika njia hiyo hiyo, alipomwona, akapitia kando upande mwingine akaenda zake. Hali kadhalika na Mlawi pia akapita, alipomwona akapita upande. Mfano huu haukuwa jambo la kubuni, ila lilitokea hakika. Kuhani na Mlawi walikuwako katika kundi lililokuwa likimsikiliza.

Njia ya kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko ilikuwa ikipitia katika msitu wa mawe mawe uliokuwa ukikaliwa na maharamia. Kila mara mahali hapo palikuwa penye matendo ya ujangili. Hapo ndipo yule msafiri aliposhambuliwa, akaachwa nusura kufa. Kuhani alimtazama tu akapita upande. Mlawi alijisikia kuwa anapaswa kumsaidia, lakini aliona kuwa jambo hilo halimhusu. Watu hawa wote walikuwa wateule waliopaswa kutenda mambo kama hayo. Wote walitazamiwa na watu kuwa ni wajumbe wanaoaminiwa, kuwaonea huruma walio kando ya njia. Waebrania 5:2.

Malaika wa mbinguni huangalia kwa wenye dhiki walioko duniani, nao huwa tayari kushirikiana na wanadamu ili kuwasaidia. Mbinguni hutazama kama Kuhani na Mlawi watawahurumia wenye dhiki na shida. Mwokozi alikuwa amewafundisha Waebrania jangwani mafundisho yote muhimu kuhusu mahitaji ya wanadamu na mambo yote ambayo watu wangalipata kwa makuhani na walimu wao. Ujumbe kamili ulitolewa kwa Musa na Bwana Mungu kwamba wawaangalie wasiokuwa na wazazi na maskini, na wageni "wapendeni basi wageni." "Mtawapenda kama nafsi zenu." Torati 10:18, 19; Mambo ya Walawi 19:34.

Lakini watu hao walifundishwa katika skuli za kidini ya taifa ambayo ni ya ushindani, Kuhani na Mlawi wamekuwa wenye ubinafsi, watu wenye mawazo hafifu sana wenye kujipenda kama si watu wa [283]
dini. Wakati walipomwangalia yule mtu aliyejeruhiwa hawakuweza

kutambua kama ni mtu wa kwao au mwingine. Walidhani ya kuwa ni Msamaria tu wakageukia mbali.

Sasa akaja Msamaria akamwona yule aliyejeruhiwa akamhurumia. Msamaria alijua wazi kwamba, hali yao ya kubezwa na Wayahudi, wasingalifadhiliwa, wangalipitwa tu. Yeye pia aliliofia hali yake asije akawa hatarini kwa kukawia mahali hapo. Ilitosha kuwa, yupo binadamu anayehitaji msaada. Alitwaa vazi lake na kumfunika. Mafuta ya divai alivyochukua kwa safari yake alivitumia kumgangia. Alimpandisha juu ya mnyama wake, akamchukua taratibu akampeleka mpaka nyumba ya wageni apate kulala hapo na kutunzwa.

Asubuhi yake Msamaria, kabla ya kwenda zake alimkabidhi katika mikono ya mwenye nyumba, baada ya kulipa gharama, na kutoa fedha za zaidi kwa ajili ya kumtunza, akaenda zake. Akatoa na ahadi kuwa kama akigharimiwa zaidi, arudipo, atalipa.

Habari ikaishia hapo. Yesu akamkazia mwanasheria macho, akasema, "Katika watu hawa watatu, ni nani aliyekuwa jirani yake?" Mwanasheria akajibu, 'Ni yule aliyemhurumia." Yesu akasema: "Nenda ukafanye mambo kama hayo."

Swali kwamba "Jirani yangu ni nani", lilijibiwa kabisa. Jirani zetu ni kila binadamu anayehitaji msaada wetu. Kila mtu aliyejeruhiwa na kuumizwa na mwovu Shetani, kila aliye mali ya Mungu ni jirani yangu.

Katika kisa cha Msamaria mwema, Yesu alieleza mambo yanayomhusu Yeye na kazi yake. Mtu alikuwa amejeruhiwa na kuumizwa na kuachwa nusura ya kufa, ameachwa katika mikono ya Shetani. Lakini Mwokozi aliacha fahari yake na utukufu wake akaja kutuokoa. Aliponya majeraha yetu, akatufunika na vazi lake la haki. Alitoa gharama yetu yote kabisa. Akieleza kielelezo chake, aliwaambia wasikizi wake: "Kama nilivyowapenda ninyi . . . mpendane vivyo hivyo." Yohana 13:34.

Msamaria alitii na kufuata kanuni ya wema na upendo wa moyoni, na kwa jinsi hii alijionyesha kuwa yeye ni mtendaji wa sheria. Kristo alimwagiza mwana sheria akisema: "Enenda ukatende hivyo."

Fundisho hilo si kama halitakiwi leo. Ubinafsi na hali ya ubaridi maishani imezimisha moto wa upendo katika maisha ya wakristo, na kuondoa hali ya uchangamfu katika tabia ya wengi.

Watu wanaolitaja jina lake wamesahau kuwa ukristo ni kufanana na Kristo mwenyewe. Isipokuwa maisha yetu yamfuatishe Kristo [284] popote tulipo, hata kama tuwe na cheo gani kanisani, hatuwi watu wa Kristo.

Kristo atuambia tuwe kama yeye katika kuwahudumia watu. "Mmepata bure, toeni bure." Mathayo 10:8. Huo ndio usemi wa Kristo. Wengi hushindwa na kuona aibu na upotevu katika hali yao mbaya. Wanaishi kwa njaa na kiu. Watu kama hawa wanahitaji huduma halisi kwa wakristo. Huangalia makosa yao mpaka wakakata tamaa. Kama sisi ni wakristo, tuwaonapo wanadamu kwa hali hiyo, kwamba ni katika dhiki au, katika dhambi, tusiseme kuwa, mambo hayo hayanihusu.

Habari ya Msamaria mwema, na tabia ya Kristo, hudhihirisha maana ya sheria na kutenda kwake, jinsi isemavyo kumpenda jirani kama nafsi yako. Wakati wana wa Mungu wakidhihirisha tabia hiyo kwa watu wote, huwa mashahidi kamili wa sheria ya mbinguni. "Tukipendana Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake hukamilika kwetu." 1 Yohana 4:12.

[285] ## 55 — Si Kujionyesha kwa Nje

Tangu Yohana Mbatizaji alipohubiri, ilikuwa imepita miaka mitatu. Hubiri lake kuu lilikuwa: “Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.” Mathayo 3:2. Wengi katika wale waliokataa ujumbe wa Yohana, na ambao walikuwa wakimpinga Yesu kwa kila hatua, walikuwa wakijipenyeza kidogo kidogo wakisema kuwa kazi yake imeanguka.

Yesu alijibu: “Ufalme wa Mungu hauji kwa kuji-onyesha kwa nje, (kwa kuonyesha ishara) maana hawatasema: Tazama yuko hapa. Au yuko kulel Maana ufalme wa Mungu uko ndani yenu.” Ufalme wa Mungu huanza moyoni. Wala hautatangazwa kama ufalme wa dunia utangazwavyo.

“Siku zitakuja ambazo mtatamani kuona moja ya siku za Mwana wa Adamu, nanyi hamtaona.” Hamfahamu bahati mliyo nayo ya kuwa pamoja na mwenye asili ya uzima na nuru ya watu. Mtatazama nyuma na kuona bahati mliyokuwa nayo ya kuishi na kuongea pamoja na Mwana wa Mungu.

Wanafunzi hawakuelewa hayo mpaka baada ya kupaa kwake mbinguni na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu, ndipo wanafunzi walifahamu kwa ukamilifu juu ya kazi ya Mwokozi na tabia yake. Walifahamu kuwa walikuwa mbele ya Bwana wa utukufu. Tazama Yohana 1:14. Mawazo yao yalifunguliwa waelewe unabii pamoja na miujiza aliyofanya. Walifanana sawa na mtu anayeamka kutoka katika ndoto. Wanafunzi hawakuwa na wasiwasi kuhusu Maneno yake na kazi yake. Mafundisho yake yalifunguwa wazi katika mawazo kana kwamba ni mafunuo mapya. Biblia ikawa kana kwamba ni kitabu kipya kwao.

Basi kiasi wanafunzi walivyokuwa wakichunguza unabii
[286] unaomshuhudia Kristo, walivutwa wakawa katika umoja na Mungu na kujifunza kwake yeye aliyepanda mbinguni ili kukamilisha kazi aliyoianzisha hapa duniani. Wakasema unabii unaohusiana na tabia yake na kazi yake. Wakaona jinsi walivyoelewa unabii kidogo mno! Walipomwona akitembeatembea kati ya wanadamu,

hawakuelewa jinsi alivyofanyika kuwa mwili. Hawakuweza kufahamu jinsi alivyokuwa, kwamba Uungu uwe ubinadamu. Lakini baada ya kuvuviwa na Roho Mtakatifu, walitamani namna gani kumwona tena, na jinsi gani walivyopenda afundishe ukweli ule kwao tena! Kristo alikuwa na maana gani aliposema: "Ninayo mengi ya kusema, kwenu, lakini hamwezi kiiyashika yote?" Yohana 16:12. Wakasikitika kwamba imani yao ilikuwa hafifu sana, hata hawakuweza kuelewa lolote.

Mwanadamu aliyesemwa na Yohana kuwa atakuja, alikaa nao muda wa miaka zaidi ya thelathini bila kuelewa kuwa ndiye aliyetumwa na Mungu. Wanafunzi waliruhusu hali ya kutokuamini iwazibe mioyo wasielewe kitu. Kila mara walisema: Kwa nini tuliruhusu mashaka na kukubali upinzani wa Marabi utuchafue mawazo, kiasi kwamba hatukutambua kuwa mkuu zaidi ya Musa Alikuwa kati yetu, ambaye ni mwenye hekima kuliko Sulemani, ndiye anayetufundisha? Masikio yetu yalikuwa mazito kiasi gani?

Wanafunzi wa Kristo walipofikishwa mabarazan., na kutupwa magerezani, walifurahi kwa kuhesabiwa kuwa wakosaji kwa ajili ya jina lake. Matendo 5:41.

Waliutambua utukufu wa Kristo, na wakachagua kumfuata na kuacha vitu vyote.

Ufalme wa Mungu hauwi kwa kujionyesha kwa mambo ya nje tu. Injili iliyo ya kweli haiwezi kufuatana na mfumo wa ulimwengu. Lakini leo makutano wanataka kumtawaza Bwana wetu awe mfalme wa duniani. Atawale katika mahakama ya ulimwengu, na katika mabunge, na kutawala masoko. Wataka awatawale akifuata kanuni za kibinadamu. Kwa kuwa sasa Kristo hayuko hapa kimwili, wataka wawe badala yake. Utawala wa jinsi hiyo ndiyo Wayahudi walitaka kuwa nao wakati wa Kristo. Lakini yeye alisema: "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu." Yohana 18:36.

Utawala wa siku zile ambazo Kristo alikuwako, ni utawala ulioharibika na kuoza, wenye dhuluma, na wenye kuonea watu. Kila upande kulikuwa na malalamiko ya ufedhuli wa kila aina.

Walakini Kristo alijaribu kufanya matengenezo ya utawala huo, ambao ni wa haki, usio na uhasama. Yesu hakujiingiza na mambo ya kuwasahihisha wenye mamalaka wa siku hizo. Yeye aliyekuwa kielelezo chetu alijitenga na mambo ya sasa, na mambo ya serikali. [287]
Si kwamba alikuwa hajali mambo ya wanadamu, ila kwa sababu

dawa yake haikutokana na mawazo ya wanadamu, wala kanuni za mambo ya nje nje. Dawa yake ni lazima iwe ile iponyayo mioyo ya watu kwanza.

Mambo ya kuponya mioyo ya watu hayategemei mahakama, wala mabaraza, wala mabunge. Utawala wa Yesu haujengwi juu ya mabunge, bali ni kuwa na hali ya ukristo na Kristo mwenyewe katika maisha ya mtu kwa kusaidiwa na Roho Mtakatifu. Hii ndiyo njia ya kuwa na uwezo wa kumwinua mwanadamu kutoka katika kudidimia kwake na kuwa hafifu kwake. Kumsaidia mtu katika kazi hii ni kusoma maandiko matakatifu, yaani neno la Mungu.

Sasa, kama ilivyokuwa siku za Kristo, kazi ya kujenga ufalme wa Mungu haitegemei msaada wa wakuu wa dunia hii, au sheria zilizotungwa na mabaraza ya duniani, bali hutegemea watu watawa wanaolitangaza neno la kweli la Mungu na kulifuata jinsi linavyosema, na kufuata mashauri ya Paulo: "Nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi niliye hai, ila Kristo yu hai ndani yangu." Wagalatia 2:20.

## 56 — Upendo wa Yesu kwa Watoto [288]

Yesu alikuwa mpenda watoto. Alipenda hali yao ya kitoto, kwa moyo wote. Shukrani yao ya kitoto ilimridhisha, naye alijisikia vibaya sana alipowaona wakitendewa mambo ya ufedhuli na watu manafiki. Popote alipokwenda hali yake ya wema na fadhili iliwavuta sana watoto.

Ilikuwa kawaida kuleta watoto kwa marabi ili wawabariki, kwa kuweka mikono juu yao. Lakini akina mama walipowaleta watoto kwa Yesu, wanafunzi wake waliona vibaya. Walidhani kuwa watoto hao wangali wadogo sana kuja kuongea na Yesu, kwa hiyo walidhani kuwa yeye atachukiwa. Lakini wanafunzi ndio waliochukizwa. Kwa Mwokozi aliona matatizo ya kina mama na mzigo walio nao wa kuwafundisha njia bora maishani. Yeye aliwakaribisha waje kwake.

Mara kadha wa kadha walikuja wakiwa na watoto wao wote pamoja, ili Yesu apate kuwabariki watoto wao. Yesu alisikia haja yao kwa moyo wa huruma. Lakini alingoja kwanza kuona wanafunzi watakavyowatendea. Alipoona kuwa wanafunzi waliwafukuza mama hao, aliwaonyesha kosa lao kwa kusema: "Msiwazuie watoto kunijia, hao ufalme wa mbinguni ni wao." Aliwachukua mikononi mwake akawabariki kama ilivyokusudiwa.

Wale akina mama walifarijika kwa maneno ya Yesu wakati wa nguvu ili kubeba kazi yao kwa furaha. Akina mama wa sasa wayapokee maneno ya Yesu kwa imani kama wale mama waliofanya. Kristo ni Mwokozi wa kila mtu binafsi, na leo ni hakika yu tayari kuwapokea kama alivyofanya kwa mama wa zamani, wa Uyahudi Yesu anajua mzigo kila mama walio nao. Alisafiri mwendo mrefu ili kumridhisha mama wa Kanaani. Alimfufua mwana wa mjane, ambaye alikuwa wa pekee kwake. Na katika msalaba wa uchungu alimkumbuka mama yake. Leo masikitiko ya mama yeyote [289]
humgusa. Atafariji mwenye masikitiko yeyote na kumsaidia.

Yeye aliyesema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwakataze", hata leo angali akiwangoja akina mama wamwendee pamoja na watoto wao ili awabariki. Hata mtoto anayekuwa an-

gali mdogo mikononi mwa mama, anaweza kukaa kivulini mwa Mwenyezi kwa ajili ya maombi ya mama ya imani. Yohana Mbatizaji alijazwa na Roho Mtakafifu tangu kuzaliwa. Tukiunganika na Mungu, tunaweza kutazamia watoto wetu kujazwa na Roho tangu utoto wao.

Yesu aliona kuwa baadhi ya watoto walioletwa kwake siku hiyo, watakuwa wafia dini, kwa ajili yake. Watu hawa watampokea kama Mwokozi wao, zaidi kuliko watu wazima leo. Bwana wa mbinguni hujibu maombi yao na kurahisisha mafundisho yao ili yaeleweke kafika hali yao ya kitoto.

## Kielelezo kwa akina Mama na Baba

Watoto ni wepesi sana kufundishwa injili, mioyo yao hupokea mafundiso kwa upesi sana. Watoto waweza kuwa wakristo kufuatana na umri wao. Wazazi wangehesabu watoto wao kuwa ni washiriki wao katika jamaa, wakiwaongoza kuelekea mbinguni. Nyumba ya kikristo ingekuwa shule ya kufundisha, wazazi wakiwa walimu wadogo, na Kristo akiwa mwalimu mkuu. Yatupasa kuwafundisha watoto wetu kuleta dhambi zao kwa Kristo, wakimwomba awasamehe, hali wakiamini kuwa watasamehewa na kupokelewa, kama alivyowapokea watoto zamani.

Jinsi mama anavyomfundisha mtoto wake kumtii, maana anampenda, huwa anamfundisha fundisho la kwanza la maisha katika ulimwengu. Upendo wa mama kwa mtoto wake huwa mfano wa upendo wa Kristo, na mtoto anavyojifunza kumtii na kumheshimu mama, huwa anajifunza kumtii Kristo, ambaye ni Mwokozi wake.

Yesu pia alikuwa kielelezo cha Baba. Maneno yake yalikuwa na uwezo, hata watu wakorofi, walimtii bila kutumia maneno makali. Neema katika maneno ya Kristo iliwalainisha hata watu wakaidi. Maneno hayo yatawafunza akina mama na baba kuwasamehe watoto wao kama wao wenyewe wanavyopenda kusamehewa.

Wazazi, katika kazi ya kuwafundisha watoto wenu, jifunzeni jinsi Mungu alivyosema kuhusu mambo ya asili, jinsi anavyofanya kwa viumbe. Kama mngezoeza maua ya waridi, mngefanyaje?
[290] Mwulize mtunza bustani akueleze namna anavyoyaongoza maua yaendelee kuslawi na kupendeza. Atakuambia kuwa, siko kuyashika kwa nguvu na kuyayumbishayumbisha wala siyo kuyavurumisha

huku na huko kutakakoyasaidia kuendelea vema na kupendeza, ila ni kutenda kidogo kidogo, na kurudia mara kwa mara, na kuyasamadi na kuyang'olea kwa taratibu magugu, na kuyashika kwa polepole. Kufundisha kwa upole, ndivyo utaweza kuongoza tabia zao kuelekea katika tabia ya Kristo.

Watie moyo kusema msemo wa upole na wema kumhusu Mungu na kusemezana wao kwa wao. Sababu ya kuwa na wakorofi wengi uliniwenguni leo ni kwa kuwa misemo ya upendo na fadhili imetoweka sana kwa watu. Mianzo ya watu hawa iliharibiwa na kufanywa migumu katika utoto wao. Upendo wa Mungu usipoingilia kati, maisha yao yataharibika kabisa. Kama tukitaka watoto wetu wawe na hali ya fadhili kama ya Yesu, yatupasa kukuza hali ya wema, ukarimu, upole na wema katika maisha yao ya tangu utoto.

Wafundishe watoto kujifunza na kumwona Yesu katika viumbe. Wachukue waende huko katika miti ya milima, na maua. Katika viumbe vyote vya asili, wafunze kumwona Yesu anavyotenda kwa fadhili. Hufanya sheria inayoongoza viumbe vilivyo hai. Naye amefanya sheria inayotuletea faida na furaha. Usiwasumbue na sala ndefu na mambo mengi, ila waelekeze kumtii Mungu na sheria yake.

Wakati unapojaribu kupanga ukweli wa wokovu, waelekeze watoto kwa Kristo aliye Mwokozi wa kila mtu peke yake. Malaika watakuzunguka ili kukusaidia. Mungu atawapa akina baba na mama neema ya kuwawezesha kuwaelekeza watoto wao kwa mtoto wa Bethlehemu.

Usiwapeleke watoto mbali na Yesu, kwa njia ya mambo ya ufisadi na ukorofi. Usiwafanye waone kuwa mbingu itakuwa mahali pabaya pa kuishi kama na wewe utafika, huko pia. Usiseme juu ya dini kana kwamba watoto hawawezi kuifahamu. Usiwakoseshe watoto kwa kudhani kuwa mbinguni ni mahali pasipokuwa na furaha, ila ni mahali pa ukiwa tu, na kudhani kuwa kumfuata Kristo ni kuacha kila kitu.

Roho Mtakatifu anapowavuvia watoto shirikiana nao katika kazi yao. Mwokozi huwaita. Hakuna kitu kinachompendeza kuliko kuona watoto wakitoa kwake katika miaka yao ya utotoni. Roho yake huwafikia, si watoto wema tu, ila hata wale wenye tabia mbaya waliyorithi kwa kufundishwa vibaya. Wazazi wengi hawana hekima [291]
ya kuwalea watoto wao kama ipasavyo. Lakini Yesu huwaangalia watoto hawa kwa huruma.

Uwe mjumbe wa Kristo wa kuwalea watoto hawa kwake. Uwaelekeze kwa utaatibu na kwa hekima mpaka kwa Kristo. Kwa neema ya Yesu watabadilika katika hali yao, ili isemwe kwao maneno haya: "Watoto wa namna hii ufalme wa Mungu ni wao."

## 57 — Kijana Tajiri Mtawala Amepungukiwa na jambo Moja [292]

“Alipokuwa njiani akienda mtu mmoja alimjia akikimbia, akamwuliza akisema: “Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?” Mtu huyu mtawala, alikuwa na mali nyingi na madaraka makubwa. Aliona upendo Yesu aliokuwa nao kwa watoto. Moyo wake uliwaka kwa ajili ya Mwokozi. Alivutiwa mno kiasi cha kumkimbilia Yesu, na kumpigia magoti kwa nia hasa, na kuuliza swali muhimu kwake na kwa watu wote.

Kristo alisema: “Kwa nini kuniita mwema?’ Hakuna mwema, ila mmoja tu ndiye Mungu.’ Je, alifahamu kuwa yule aliyekuwa akizungumza naye ndiye Mwana wa Mungu? Elezo lake lilikuwa la kweli kiasi gani?

Mtawala huyu alikuwa akijiona kuwa yu mwenye haki kabisa, walakini alijisikia kuwa hana kitu kimoja. Je, inawezekana Yesu kumbariki na kuuridhisha moyo wake? Katika majibu ya Yesu alimwambia kuwa utii kwa amri za Mungu ni lazima, kama mtu akitaka kuurithi uzima wa milele. Jibu la kijana huyu lilikuwa dhahiri. Alisema: “Yote hayo nimeyashika tangu utoto wangu, nimepungukiwa nini tena?”

Kristo alimtazama usoni, kama mtu anayesoma habari za maisha yake, na kuchunguza tabia yake. Alimpenda na akatamani kumpatia amani na furaha. , Alimwambia: “Umepungukiwa na kitu kimoja, nenda ukauze vyote ulivyo navyo, ukawape maskini nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo ujitwike msalaba wako unifuate.”

Kristo alivutiwa sana na kijana huyu. Mwokozi alitamani kumfunulia ibada halisi ya moyo. Alitamani kumwona akijinyenyekeza kikweli bila kujificha na kujifanya kwamba anashika dini ya kweli.

Yesu alirnwona mtu huyu kuwa anahitaji, msaada unaohusu
wokovu. Kama akijitoa kamili kwa Kristo atakuwa mwenye uwezo [293]
wa kutenda mema. Alipochungulia tabia yake alimpenda. Upendo wa Kristo ulimwamsha, akatamani kuwa mtu v ake. Yesu pia alitamani kumwongoa, na kuendeleza tabia yake hiyo bora, ipate kuwa

katika utumishi wa Bwana. Kama mtu huyu angalijitolea kwa Kristo, angalibadilika kadiri gani siku za usoni!

Yesu alisema: “Umepungukiwa na kitu kimoja.” Nenda ukauze vitu ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate.” Kristo aliona moyo wake. Alipungukiwa na kitu kimoja tu, ni hicho kilikuwa sharti kubwa lenye kanuni. Alihitaji upendo wa Mungu moyoni mwake. Jambo hili ndilo alilopungukiwa, na lisipopatikana atakuwa ameshindwa kabisa. Maisha yake yote ya usoni yatakuwa yameharibika kabisa. Ili kusudi apokee upendo wa Mungu, lazima upendo wa ubinafsi uachwe kabisa.

Kristo alimwambia achague kati ya hazina ya mbinguni na hazina ya duniani, na ukubwa wake. Ubinafsi lazima utupiliwe mbali, na mapenzi yake lazima yatolewe yote kwa Kristo. Kijana huyu alikuwa na bahati ya kuchagua hazina za mbinguni na kurithi pamoja na Kristo. Lakini hana budi kuchukua msalaba na kumfuata Yesu katika njia ya kujikana nafsi.

Uchaguzi uliachwa juu yake. Yesu alikuwa amemwonyesha maana ya amri kumi anazosema kuwa ameshika tangu utoto wake. Akitaka kumfuata Kristo, lazima akubali kuacha matazamio yake ya siku za usoni. Yesu alimtazama kijana huyu kwa makini, akitumaini kuwa atakubali kufuata njia ya Mungu ya kujikana nafsi, kama anavyoshauriwa na Roho Mtakatifu.

Maneno ya Kristo yalikuwa maneno ya hekima, na ijapokuwa yalionekana kana kwamba ni makali. Kuyakubali na kuyafuata, ndilo lilikuwa tumaini la mtu huyu la kupata wokovu. Cheo chake na mali zake vilikuwa vikibashiri mabaya tu, katika tabia yake. Kama vikiendekezwa vitamfukuza Mungu katika mawazo yake.

## Je, Yesu alidai yasiyowezekana?

Kijana tajiri mtawala alifahamu maana ya maneno ya Yesu, kwa sababu alikwenda zake kwa huzuni. Alikuwa mmojawapo wa wabunge wa Kiyahudi, na Shetani alikuwa akimjaribu apate kujivunia hali yake ya baadaye. Alitaka hazina ya mbinguni, lakini pia alitaka kile ambacho utajiri wake utakachomfanyia duniani. Alitamani uzima wa milele lakini pia aliona kuwa kuuza vitu vyake
[294] ni kujitolea kukubwa kabisa, kwa hiyo alikwenda zake kwa huzuni, kwa “kuwa alikuwa na mali nyingi.”

Kule kujigamba kwamba ameshika amri za Mungu tokea utoto wake, kulikuwa kwa uongo. Ilionyesha kwamba utajiri ndio uliokuwa sanamu yake. Alipenda kipawa cha Mungu zaidi kuliko kumpenda mwenye kumpa kipawa. Kristo alimwambia kijana huyu amfuate. Alisema: "Nifuate." Lakini Mwokozi hakuwa na thamani kwake, kuliko jina lake na mali zake vilivyokuwa na thamani mbele ya watu. Kukubali vitu visivyoonekana na kuacha vitu vinavyoonekana, kwake lilikuwa jambo zito. Alikataa uzima wa milele, akaenda zake. Hata ulimwengu kamwe haumkubali. Watu maelfu huchagua ulimwengu na mambo yake kuliko Kristo.

Jinsi Kristo alivyoshughulika na kijana huyo ni fundisho kubwa. Mungu ametupa kanuni, ambazo wafuasi wake lazima wazifuate. Ni kuzitii amri zake, sio kuzikariri tu. Ni utii unaoonekana katika maisha ya kubadili tabia. Bwana husema: Watakaosema kuwa vitu vyangu vyote na mimi ni wake, ndio watakaotambuliwa kama wana wa Mungu. Mwokozi hutaka tushirikiane naye kufanya kazi ya Mungu, kwa njia hii tu tutaokolewa.

Mungu amewapa watu mali, talanta, na nafasi ili wawe wajumbe wake wa kuwasaidia maskini na wahitaji. Anayetumia mali yake kama Mungu alivyotaka huwa mkazi pamoja naye.

Wale wenye mali na wakuu duniani, kama yule kijana huona kuwa Mungu huwadai mno kupita kiasi, kwa hiyo huenda zao kwa huzuni. Hakuna utii wa nusu nusu utakaokubaliwa mbele za Mungu. Hakuna njia ya kumwokoa mtu, ila kuacha yote yanayoleta laana.

Wafuasi wa Kristo wanapomtolea Bwana mali yake, huweka hazina mbinguni, ambayo watapewa watakaposikia sauti: "Vema .... Ingia katika furaha ya Bwana wako." Mathayo 25:23. "Furaha ya kuwaona waliokombolewa kwa wote waliojitia kazini mwa Bwana, aliyesema: 'Nifuate."

[295]

# 58 — Kufufuliwa kwa Lazaro

Miongoni mwa wanafunzi wa Yesu wa maana sana, mmojawapo alikuwa Lazaro wa Bethania, naye alikuwa mpendwa mkubwa wa Mwokozi. Kwa Lazaro ndiko mwujiza mkubwa wa Yesu ulifanyika. Mwokozi aliwapenda wanadamu wote, lakini kwa wengine aliwashiriki zaidi.

Nyumbani kwa Lazaro ndiko Yesu alilala mara nyingi. Mwokozi hakuwa na nyumba yake. Alipochoka, au kuwa na kiu au njaa, kama binadamu wote, kila mara alikwenda katika mji huo, ambapo alikaribishwa na kupafanya kana kwamba ni kwao.

Makutano walipomfuata Kristo mahali pa wazi aliwaeleza kuhusu uzuri wa viumbe hasa miti na mimea. Lakini makutano hawakuwa wepesi wa kuzingatia. Na katika Bethania, Yesu alipata mahali pa kupumzikia, baada ya shughuli za mchana. Hapa hapakuwa na haja ya kusema kwa njia ya mifano.

Kristo alipokuwa akitoa mafundisho yake ya ajabu, Mariamu alikuwa akipenda miguuni pake na kumsikiliza. Wakati fulani Kristo alipokwenda Bethania kama mgeni, mara ya kwanza, Martha aliyekuwa akipika, alimwendea Yesu, na kumwambia kuwa amwambie Mariamu ili amsaidie. Yesu alijibu, akasema: "Martha, Martha, unajisumbua na mambo mengi: Lakini kuna haja ya kitu kimoja tu, na Mariamu alichagua fungu lililo jema, ambalo halitaondolewa.' Martha asingalihangaika sana kwa mambo yanayo-pita, ila ahangaikie mambo ya milele. Martha anahitaji maneno ya Kristo, kama Mariamu, kabla ya kushughulika na mambo mengine. Kwanza apate mibaraka ya Kristo.

Huzuni ilianguka katika mji ambao ulikuwa mapumziko ya
[296] Yesu. Lazaro alishikwa na ugonjwa wa ghafla, na dada zake walituma habari kwa Yesu wakisema: "Bwana tazama yule umpendaye hawezi sana." Waliona ugonjwa uliomshika ndugu yao ulikuwa mkubwa sana, lakini walijua kuwa Yesu amejionyesha kuwa na uwezo wakuponya magonjwa ya kila namna. Hawakumwita kwa haraka sana, ila walitaka aende Bethania kwa upesi inavyowezekana.

Walingoja kwa subira kubwa kwa kadiri ya ugonjwa ulivyozidi kuwa mkubwa kwa ndugu yao. Walimwombea sana na kumsubiri Mwokozi. Lakini mtu aliyetumwa kwake alirudi mwenyewe, bila Kristo, lakini, alituma ujumbe akisema: “Ugonjwa huu sio wa mauti”, kwa hiyo walitumaini kuwa Lazaro atapona. Mgonjwa alipofariki walisikitika vikubwa sana, lakini” walijisikia kuwa na tumaini katika Kristo.

Yesu aliposikia habari hizo hakuonyesha huzuni, kama vile wanafunzi wake walivyotazamia kuona. Alisema tu kwamba: ‘Ugonjwa huu sio wa mauti, ila ni wa kumtukuza Mungu, ili Mwana wa Mungu atukuzwe.” Yesu alikawia muda wa siku mbili. Kukawia huku kulikuwa fumbo kwa wanafunzi wake, kwa kuwa waliwapenda watu wa jamaa hiyo ya Bethania.

Kule kukawia kwake kwa siku mbili wanafunzi wake walidhani kuwa amepuuza habari hizo. Wanafunzi walifikiri habari za Yohana Mbatizaji. Kwa nini Yesu hakumtoa gerezani wala kumfufua na hali alikuwa na uwezo wa kutenda miujiza? Mafarisayo walileta hoja hiyo, kama kanusho la kujidai kuwa Mwana wa Mungu. Kristo alikuwa amewaonya wanafunzi kuhusu majaribu, kupotea, na mateso. Je, atawaacha majaribuni? Mambo haya yote yaliwahangaisha mioyoni.

Baada ya kungoja siku mbili, Yesu alisema: “Twendeni huko Uyahudi tena.” Hawakuweza kuona kitu kingine, ila hatari tu. Walisema: “Bwana, juzijuzi Wayahudi walitaka kukupiga kwa mawe, nawe unataka kwenda huko tena?” Yesu akajibu na kusema, “Mchana hauna saa kumi na mbili? Mimi niko kwenye ulinzi wa Baba. Kadiri ninavyotenda mapenzi yake, maisha yangu yako salama. Nimefikia mwisho wa siku zangu, lakini wakati uliobaki niko salama.’ “Mtu akitembea mchana hajikwai, kwa kuwa kuna nuru ya mchana.” Mchana hajikwai, kwa kuwa kuna nuru ya mchana. Nuru ya uongozi wa Mungu humpa uhakika wa kazi yake. Nayo humwongoza mpaka mwisho wa kazi yake. Lakini mtu akitembea gizani hujikwaa kwa kuwa hakuna nuru ndani yake. Mtu atembeaye kama apendavyo hujikwaa. Maana hakuna usalama katika kutembea [297]
kama mtu apendavyo.

“Maneno haya aliyasema Yesu, baadaye aliwaambia, rafiki yetu Lazaro amelala, nami ninakwenda nipate kumwamsha.” Kuhusu hatari Bwana wao alipaswa kwenda Yerusalemu. Wanafunzi wa-

likuwa karibu kusahau kuhusu maafa ya Bethania, lakini Kristo hakusahau. Wanafunzi walikuwa wameshasahau juu ya fadhili Mwokozi alizokuwa nazo kuhusu Lazaro na dada zake. Lakini ahposema rafiki yetu Lazaro amelala, ndipo walishituka na kukumbuka mambo yalivyo. Kristo hakuwasahau rafiki zake.

Kisha wanafunzi wake wakasema: "Bwana, kama amelala, ataamka. Walakini Yesu alisema habari za kufa kwake. Wao walidhani kuwa anasema juu ya kulala usingizi."

Yesu alifananisha kifo na kulala usingizi, kwa waaminifu wake. Maisha yao yamefichika ndani yake katika Mungu. Na katika siku ya mwisho tarumbeta itawaamsha wote waliolala ndani yake. Tazama 1 Wakorintho 15:51-54.

Kisha Yesu akawaambia wazi wazi, "Lazaro amekufa. Nami nafurahi kwa ajili yenu kwamba sikuwako, ili ninyi mpate kuamini, walakini twende huko."

Wanafunzi walishangaa kwa maneno ya Kristo, kwamba: "Lazaro amekufa, Nami nafurahi . . . sikuwako huko." Je, Mwokozi alikosa kwenda kwa mgonjwa kwa mapenzi yake mwenyewe? Lakini Kristo aliona mpango wote, na kuwaona wale dada wenye kulia watafarijika kwake. Yesu aliona masikitiko yote ya hawa madada kwa ajili ya kifo hiki. Lakini Kristo hakuwafikiria watu wa jamaa hiyo tu katika Bethania. Aliwafikiria wanafunzi wake pia waliokuwa mafunzoni. Watakuwa wajumbe wake ulimwenguni. Kwa ajili yao Lazaro aliruhusiwa afe. Kama ungaliponywa ugonjwa tu, mwujiza muhimu ambao ni uthibifisho kamili wa Uungu wake usingelifanyika.

Kama Kristo angalimkuta mgonjwa, kifo kisingalimpata. Hiyo ndiyo sababu ya Yesu kutokuwako. Aliwaacha wale madada wamwone kaka yao akifa. Aliwaacha wavumilie huzuni yote bila kubakiza. Alijua kuwa Lazaro atafufuka sio kwa uwezo wake.

Kwa wote watakaotegemea uongozi wa Mungu, wakati wa huzuni kuu, ndipo wataona kuwa msaada na faraja iko karibu sana. Wataangalia nyuma wakati wa giza kuu kwa shukrani wakiona wakati ule wa giza. Kwa kila jaribu na shida atawatoa na kuwaleta
[298] katika hali ya utulivu na furaha tele, hali wakiwa na uthabiti na imani kamili.

Kristo alikawia ili kwa kumfufua Lazaro, apate kuwapa watu hawa wagumu na wasioamini uthibitisho kuwa hakika huyu ni "ufu-

fuo na uzima". Alitaka kuwapa watu hawa wasioamini, uhakika kuwa, yeye ndiye peke yake aletaye uzima na tumaini la Waisraeli. Ndiye asili ya uzima na nuru. Ndiyo sababu ya kukawia kwake.

Alipofika Bethania, Yesu aliwajulisha madada wale kwamba amekuja, lakini alibaki huko njiani muda kidogo. Kundi kubwa la waombolezaji kwa ajili ya kifo cha jamaa, hali kuafikiana na mipango ya Kristo. Alisikia maombolezo kwa mbali, naye hakutaka akutane na dada wale katika ghasia za jinsi hiyo. Katika baadhi ya waombolezaji, walikuwa maadui wa Kristo. Alijua kusudi lao, kwa hiyo hakutaka kukutana nao mara moja.

Martha alipashwa habari kimya kimya, watu wasisikie, hata Mariamu pia hakujua. Moyo wa Martha ulijaa huzuni. Alipofika kwa Kristo aliona huzuni ile ile vile vile, ila alimfikiria marehemu, na kusema: "Bwana kama ungalikuwa hapa ndugu yangu asingakufa." Dada huyu alirudia maneno haya tena na tena.

Martha hakuwa na mashaka juu ya kurudia mambo ya nyuma, lakini alipomwangalia uso wake wenye huruma alisema:" Najua kuwa lolote utakalo mwomba Mungu atakufanyia." Yesu alimfariji akisema: Ndugu yako ataishi." Jibu hilo lilimfikirisha Martha juu ya ufufuo wa mwisho. Martha akasema: "Najua kuwa atafufuka siku ya mwisho." Yesu akitaka kumhakikishia, alisema: "Mimi ndimi huo ufufuo na uzima." Katika Kristo ndipo asili ya uzima ulipo. "Aliye naye Mwana anao uzima." 1 Yohana 5:12. "Aniaminiye mimi, ijapokuwa amekufa, ataishi, naye mwenye kuishi, akiamini hatakufa. Je, wayaamini haya?" Hapa Kristo anaangalia wakati wa kurudi kwake. Wakati wa kurudi kwake wafu walio mwamini watafufuka, na walio hai watabadilika bila kuonja mauti. Kumfufua Lazaro kutakuwa mfano wa wenye haki waliokufa watakaofufuliwa. Kwa maneno na kazi za Yesu humfanya kuwa asili ya kuwapa watu uzima wa milele.

Maneno ya Mwokozi, kwamba: "Waamini?" Martha alijibu "Ndiyo Bwana, naamini kuwa wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu, atakayekuja ulimwenguni." Alikiri kuwa na imani kuhusu Uungu, na kuhusu uwezo wa kutenda apendavyo.

Alipokwisha kusema hivyo, aliondoka, akamwita dada yake Mariamu kisirisiri, akisema: "Bwana amekuja." Alisema polepole [299]
iwezekanavyo, maana Makuhani na wakuu walipanga kumkamata

Yesu ikiwezekana. Kilio cha waombolezaji kiliwazuia wasisikie maneno yake.

Mariamu aliposikia aliondoka mara moja akaenda. Waombolezaji walimfuata wakidhani kuwa anakwenda kaburini. Alipomfikia Yesu alisema, kwa masikitiko: “Bwana kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.” Vilio vya waombolezaji vilimwumiza, naye alitaka kusikia maneno ya faraja kidogo.

“Yesu alipomwona akilia, na Wayahudi pia wakilia pamoja naye, alihuzunika moyoni naye akalia.” Aliona wengi walikuwa wakijifanya tu kama wenye masikitiko. Baadhi ya waliokuwa wakijifanya, walikuwa na njama ya kuua. Yesu aliuliza: “Mmemweka wapi?” Wakasema: “Bwana, njoo uone.” Wakaenda wote pamoja kaburini. Lazaro alikuwa mpendwa sana, na dada zake walimlilia kwa uchungu mno, na wengineo walijiunga na Mwana wa Mungu alikuwa amechukua mwili wa kibinadamu, ndiyo sababu alipata masikitiko kama wao.

Yesu hakulia kwa sababu ya Martha na Mariamu, bali alilia kwa sababu ya masikitiko ya miaka yote ya binadamu yalikuwa juu yake. Aliona matokeo mabaya mno ya kuvunja sheria ya Mungu. Aliona kuwa mapambano ya haki na uovu yameongezeka zaidi na zaidi. Aliona masikitiko na vifo, ambavyo vingalikuwa mzigo wa watu wote siku zote. Ole wa wanadamu wenye dhambi wote ulikuwa unamkalia yeye, kwa hiyo machozi yake yalitoka kwa kuwahurumia.

Lazaro alikuwa amewekwa kaburini, na jiwe kubwa sana lilikuwa limewekwa mlangoni. Kristo alisema: “Liondoeni jiwe.’ Martha alikanusha, kwa kudhani kuwa Yesu anataka kuona alikolazwa. Alisema kuwa ananuka sasa kwa kuwa tangu kuzikwa sasa ni siku nne. Usemi huu, haukuwapa nafasi maadui zake kupenyeza hoja zao za kusema kuwa kuna udanganyifu uliofanyika. Kristo alipomfufua binti Yairo, alisema: “Msichana hakufa bali analala’” Marko 5:39. Kwa vile alivyofufuliwa mara moja, Mafarisayo walikanusha kwa kusema kwamba binti alikuwa hakufa, ila amelala. Walijaribu kusema kuwa hakuna mwujiza uliofanyika, ila ni udanganyifu tu. Lakini kwa habari za kufa kwa Lazaro hakuna mtu angalikanusha, kwa kuwa amekuwa kaburini siku nne.

Bwana anapokuwa tayari kufanya kazi yake, Shetani humwinua mtu fulani kupinga. Martha alipinga kwamba mwili umeoza sasa. Maneno yake hayakulingana na ukweli aliouamini, wa ahadi ya

ufufuo. Mwokozi alimsahihisha Martha kwa kusema: "Sikukuambia kwamba ukiamini utaona utukufu wa Bwana?" Unalo neno langu wala hakuna kitakacholipinga, na kuzuia kazi za Mwenyezi. Kutokuamini sio unyenyekevu, bali kuamini neno la Kristo ndio unyenyekevu na kujitoa kwa kweli. "Liondoeni jiwe." Kristo angaliweza kuwaagiza malaika waliokuwa wakiwazunguka kufanya hivyo, lakini alitaka wanadamu kushirikiana na wanadamu. Kile watu wanachoweza kufanya Mungu huwaacha wafanye. Wasichoweza, ndipo Mungu huingilia. [300]

Amri hiyo ilitiiwa. Jiwe liliondolewa. Kila kitu kilifanyika waziwazi. Wote waliona kuwa hakuna udanganyifu. Pale mwili wa Lazaro ulikuwa umelala, amekufa. Watu waliokuwako walingoja kwa hamu kitakachofuata. Watu walikuwa kimya. Kristo alisogea karibu na kaburi. Kristo akiinua macho yake mbinguni, alisema, "Baba, nakushukuru, kwa kuwa unanisikia." Adui za Kristo wamemshutumu, kwamba anakufuru na kujiita Mwana wa Mungu.

Kristo alijihadhari asifanye jambo kisirisiri, ila wazi. Alimtegemea Baba yake kabisa. Ni kwa imani na kwa maombi ndiyo aliweza kufanya miujiza. Alitaka watu wote wafahamu uhusiano wake na Baba yake. Kwa hiyo alisema: "Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nimejua ya kuwa hunisikia siku zote, lakini kwa ajili ya watu hawa nasema hayo, ili wapate kuamini kuwa ni Wewe uliyemtuma." Wanafunzi wake na watu wengine walijua ya kwamba madai ya Kristo siyo ya uongo.

Alipokwisha kusema hayo, alisema kwa sauti kuu: "Lazaro toka nje." Uungu ulimulika katika ubinadamu. Katika uso wake uliong'aa kwa utukufu wa Mungu, watu waliona uthibitisho wa uwezo wake. Kila mtu alitazama kaburini, kila sikio liliinama kusikia chochote. Wote walisikiliza kwa hamu sana, kuona madai ya Yesu kuwa Mwana wa Mungu yalivyo.

Kulikuwa na kujongezana kaburini, ndipo aliyekuwa amekufa alisimama mlangoni. Mwendo wake ulizuiwa na sanda alizofungwa. Kwa hiyo Kristo aliwaambia wenye kushangaa "Mfungueni sanda." Tena alionyesha kuwa binadamu ahudumie binadamu. Lazaro akasimama mbele ya wote, akiwa hana alama ya mauti. Mtu mzima kabisa. Macho yake yaling'aa kama kawaida, akampenda mponya wake sana na kumsujudia.

Watu walinyamaza kimya mara ya kwanza, kwa mshangao mkubwa. Halafu furaha ikafuatia na vifijo vyote. Madada
[301] zake wakampokea kaka yao kama zawadi kutoka kwa Mungu. Wakamshukuru Mwokozi kwa machozi ya furaha isiyosemaka. Wakati wa hoihoi za furaha, Yesu alitoweka. Walipomtafuta mwenye uzima hawakumwona.

# 59 — Makuhani na Wakuu Wanaendelea na Njama Yao [302]

Habari za kufufuliwa kwa Lazaro mara moja zilifikishwa Yerusalemu. Wakuu wa Yerusalemu walikuwa wakipashwa mambo yote ya matendo ya Yesu kwa njia ya wapelelzi. Baraza la Sanhedrini lilikusanyika mara moja ili kuamua mambo kuhusu jambo la Lazaro. Mwujiza mkubwa huo umefanywa na Mungu kuwa uthibitisho kuwa alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili kuleta wokovu kwa watu. Hicho kilikuwa kielelezo cha wazi cha Mungu cha kutosha kuwaaminisha watu, na kuwaondolea mashaka.

Lakini Makuhani walikasirishwa tu na mwujiza huu. Mtu aliyekufa amefufuliwa mchana kabisa, na mbele ya mashahidi wengi. Hakuna fumbo lolote lililokuwako. Kwa sababu hii Makuhani waliazimia kumkomesha Yesu kabisa asiendelee na kazi hii.

Masadukayo hawakuwa na nia mbaya sana kwa Yesu kama Mafarisayo walivyokuwa, lakini wakati huu hao wamejiingiza pia. Hawakuamini juu ya ufufuo wa wafu, wakisema kuwa haiwezekani kumfufua mtu. Lakini kwa mafundisho ya Kristo, walijionyesha kuwa hawajui maandiko wala ufufuo wa wafu, utokanao na uwezo wa Mungu. Mtu anawezaje kufufuka kutoka kaburini? Lakini sasa mwujiza huu wa Lazaro hauwezi kubishiwa. Baada ya ufufuo wa Lazaro ndipo Masadukayo waliamua kumkomesha kwa kumwua.

Mafarisayo waliamini juu ya ufufuo, wala hawakuona kuwa kumfufua mtu kulikuwa uthibitisho wa kuwa Masihi. Lakini tangu mwanzo aliwabomolea ukuta uliowaficha kwa hiyo walimchukia. Dini safi aliyofundisha iliwafunua wakawa uchi, hivi walitaka kulipiza kisasi. Mara kadhaa walitaka kumpiga kwa mawe, lakini yeye akatoweka.

Mafarisayo walimshitaki kwa Warumi kuwa ni mtu anayetaka kuingilia mamalaka yao, na hayo waliyasema ili kufanya serikali [303] imwangalie kwa makini. Walijaribu kwa kila njia kwamba anawashawishi watu wapate kuasi serikali. Lakini mambo yao yote yaliarrguka. Makutano walioona miujiza yake na kusikia ma-

fundisho yake safi sana, waliona kuwa mambo ya Mafarisayo siyo ya kweli hata kidogo. Yeye si mvunjaji wa Sabato wala siyo mwenye kukufuru. Majaribio ya Mafarisayo yaliposhindwa, mwisho wakapitisha kuwa mtu akimwamini Yesu, atatengwa katika sinagogi.

Kwa hiyo Mafarisayo na Masadukayo walikuwa karibu kukubaliana katika mipango yao. Walikubaliana katika kumpinga Kristo.

Wakati huu baraza la Sanhedrini halikuwa halali kisheria. Lilikuwa baraza la usuluhishi tu. Baadhi ya wajumbe waliuliza kama wana ruhusa kumwua Kristo. Waliogopa kwamba jambo hili litaleta fujo kuu. Masadukayo walijiunga na Mafarisayo kumchukia Kristo, waliogopa Warumi wasije wakawashusha vyeo vyao.

### Jinsi Roho Mtakatifu alivyojaribu kuwasaidia

Katika mkutano huu wa kupanga jinsi ya kumwua Kristo, shahidi aliyesikia majivuno ya mfalme Nebukadneza, na kusikia sikukuu ya sanamu ya Belshaza aliwasisitizia waone kazi zao na matokeo yake. Mambo katika maisha ya Kristo yamewatokea na kuwaonya kuhusu hali zao. Wanakumbuka wakati alipokuwa mtoto wa miaka kumi na miwili alisimama mbele ya walimu wakuu wa sheria, akiwauliza maswali yaliyowatatanisha. Mwujiza uliofanyika wa kumfufua Lazaro, unaonyesha kuwa Yesu si mtu wa kawaida, ila ni Mwana wa Mungu. Wazee wa baraza waliulizana kwa wasiwasi, wakisema: "Tufanyeje sasa?' Baraza liligawanyika.

Baraza lilipokuwa na wasiwasi mkubwa, Kayafa, ambaye ndiye kuhani mkuu alisimama, mwenye kiburi, na mkatili, alisema kwa ushujaa: "Hamjui kitu ninyi, inapasa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, kuliko taifa lote kupotea." Hata kama Yesu ni mtakatifu hivyo, lazima aondoke njiani. Alikuwa, akihafifisha mamlaka ya wazee, ikiwa watu wakipoteza imani yao kwa waongozi wao, uwezo wa taifa utaharibika. Baada ya mwujiza huo wafuasi wa Kristo walifanana kama wenye kutaka kupindua nchi. Warumi wangekuja na kufunga hekalu letu na kutuharibu kama taifa. Hivyo ndivyo alivyosema. Maisha, ya mtu huyu wa Galilaya, yana faida gani ukilinganisha na taifa zima? Je, kumwondolea mbali mtu huyu sio
[304] kufanya kazi ya Mungu? Ni afadhali mtu mmoja afe kuliko taifa zima kuangamia.

Kanuni ya Kayafa aliyofuata ilikuwa ni kanuni ya mataifa aliyoiga. Kanuni hiyo kwamba, mtu mmoja afie taifa, ndiyo iliyofuatwa ikiwafanya kutoa sadaka ya mtu. Kwa hiyo Kayafa akaazimia kumwua Yesu ili kuliokoa taifa lenye hatia, sio kutoka dhambini, ila kuendelea katika dhambi.

Katika baraza hili maadui wa Kristo walimthibitishia Kristo kuwa ana hatia kabisa. Roho Mtakatifu alikuwa amewachoma mioyo sana, lakini Shetani aliwavuta waone aibu waliyotiwa na Kristo. Jinsi alivyowadharau na kuwaona kuwa hawana dini. Akidharau ibada zao na kawaida zao za dini. Amewaambia wenye dhambi kuwa wamwendee Mungu moja kwa moja bila kupitia kwa wazee, kwa maana yeye ni Baba mwenye fadhili nyingi. Amedharau Shule ya Manabii, na kudharau huduma za Makuhani, kwa njia hii ametuvunjia heshima kabisa. Hivyo ndivyo walivyosema, kwa hiyo walimwona kuwa mwenye hatia kabisa.

Baraza la Sanhedrini lilikubaliana na shauri la Kayafa, kana kwamba ni neno la Mungu isipokuwa watu wachache sana, ambao hawakutoa maoni yao. Wasiwasi ukaisha na kutokubaliana kukamalizika. Wakaazimu kumwua Kristo, wakati utakapopatikana. Makuhani hawa na wakuu, wameingia katika mikono ya Shetani kamili walakini wao waliona kuwa wametenda tendo bora la kupendeza sana. Walijidhania kuwa wanatafutia taifa lao fanaka na baraka na wokovu.

Watu wasipotafakari sana juu ya Yesu, wataangukia kwao wao kwa wao, baraza lilichelewesha matimizo ya kile walichoamua. Mwokozi alijua kuwa mazimio yao yatatimizwa karibuni, lakini haikumpasa kujiweka katika shida pasipo sababu kwa hiyo aliondoka katika wilaya hiyo, pamoja na wanafunzi wake.

Yesu sasa alikuwa amefanya kazi muda wa miaka mitatu kamili, ulimwenguni. Hali yake ya kujikana nafsi, na ukarimu na upendo ilijulikana kwa wote.

Walakini muda mdogo huo, ulikuwa mrefu mno kwa walimu. Mwenye huruma zote za kila namna kwa wanadamu, alifukuzwa, kama asiyefaa watu. Aliyevunja nguvu za kaburi na kuwatoa waliokuwamo humo, aliyetoa mafundisho ya kutoa watu usingizini, alishindwa kufikia mioyo ya wale wenye chuki waliofishwa, na walioendelea kwa ukaidi kukataa nuru.

[305] ## 60 — Cheo Kikuu Ni Kipi?

Pasaka ilikuwa inakaribia, na Yesu alikuwa akielekea kwenda Yerusalemu tena. Moyoni mwake alikuwa na utulivu kamili wa kuwa na umoja na Baba yake. Alikuwa akielekea kwenda mahali pa kujitolea kuwa kafara. Lakini wanafunzi wake walikuwa na hali ya hofu, mashaka, wasiwasi na giza. Mwokozi alitangulia, nao walistaajabu, wakamfuata kwa hofu. Tena Kristo akawafunulia wale kumi na wawili habari za kusulubiwa kwake na kuteswa kwake, akasema:

"Angalieni tunapanda kwenda Yerusalemu, na mambo yote Mwana wa Adamu aliyoandikiwa yatatimizwa. Kwa maana atatiwa mikononi mwa mataifa, nao watamdhihaki, na kumpiga. Watamtemea mate na kumwua, na siku ya tatu atafufuka. Nao hawakufahamu na usemi huu.

Je, hawakuwa wakitangaza kuwa: "Ufalme wa mbinguni umekaribia?" Kristo mwenyewe hakuwapa wanafunzi wake ahadi ya cheo kikuu katika ufalme wake? Je, manabii hawakutabiri kuhusu utukufu wa ufalme wa Masihi? Katika nuru ya mawazo hayo, maneno yake kuhusu kusalitiwa kwake yalikuwa tatanisho, na kivuli.

Vyovyote vile vingetokea waliamini kuwa ufalme utasimamishwa karibuni.

Yohana naYakobo nduguye walikuwa katika kundi la kwanza la walioacha vyote wakamfuata Kristo. Mioyo yao iliunganika na moyo wake, hivyo walitamani kupata wakati wa kuwa katika ufalme wake mara moja. Kila mara Yohana alikaa karibu na Mwokozi, na Yakobo alitazamia kupata heshima hiyo.

Mama yao alikuwa akimhudumia Kristo kwa moyo wote. Kwa moyo wa upendo wa mama alitamani kuona watoto wake wakipata heshima katika ufalme huo. Siku moja walimjia Yesu, wote; mama
[306] na wanawe. Akasema, "Mnataka niwatendee nini?" Mama akasema: "Wape wanangu kuketi, mmoja mkono wako wa kulia, na mwingine mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako."

Yesu alisoma mioyo yao. Aliona ushirika walio nao kwake. Upendo wao kwake ulikuwa kama upendo wake wa kuokoa. Alisema: "Mnaweza kukinywea kikombe nitakachonywea na kubatizwa ubatizo nitakaobatizwa?" Walitafakari maneno yake ya fumbo, kisha wakasema: "Tunaweza". Maana yake taabu na majaribu yake. Yesu akasema: "Ndiyo, nmaweza kunywea kikombe changu, na kubatizwa ubatizo wangu. Yohana na Yakobo walikuwa tayari kushiriki katika mateso ya Kristo. Mmoja alikuwa wa kwanza kuuawa kwa upanga, na mwingine alikuwa wa kwanza kuteseka kwa muda mrefu kuliko wote.

Yesu akasema: "Lakini upande wangu wa kulia au upande wangu wa kushoto, sina amri, ila watapewa na Baba yangu wale walioandaliwa." Katika ufalme wa Mungu, vyeo havipewi kwa upendeleo au kwa sheria. Hupokewa kwa tabia ilivyokuwa. Taji na kiti cha enzi ni ishara ya hali ya ushikamano uliokuwapo baina ya mtu na Kristo. Atakayesimama karibu sana na Kristo, ni mtu yule aliyepata kukinywea kikombe kichungu zaidi duniani, yaani aliyejinyima sana na kuishi maisha ya kujikana nafsi yake, na kuwa na upendo kama ule uliofanya wanafunzi kuacha vyote, na kuishi na kufanya kazi kwa njia ya kujikana nafsi ili kuokoa wapotevu.

Wale kumi hawakufurahi. Kwao cheo cha juu katika ufalme ni kuishi kwa ubinafsi. Wakakasirika kwamba wale wawili wamewapita.

Yesu alisema kwa wenye kukasirika: Mnajua ya kuwa wakuu wao huwatawala na kuwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu."

Katika ufalme wa ulimwengu vyeo ni kujitwalia kila kitu watu huishi kwa kutawala watu wa chini. Utajiri wa elimu ndivyo vinavyowapa madaraka, ya kutawala watu wengine, na kuwakandamiza walio chini. Dini nayo ilikuwa namna hiyo.

## Ufalme wenye Kanuni Tofauti

Kristo alikuwa, akisimamisha ufalme wenye kanuni tofauti. Aliita watu, si wawe wakuu wa madaraka, ila wawe wahudumu, watu wenye nguvu za kuwategemeza wanyonge. Madaraka, vyeo, elimu, huwekwa chini ya huduma.

"Mwana wa Adamu hakuja kuhudumiwa, bali kuhudumu, na
[307] kutoa, maisha yake kuwa fidia ya wengi." Kanuni ambayo Kristo aliyoweka ni ya kuliongoza kanisa ambalo ni mwili wake katika ufalme wa Kristo, wale wenye kufuata kielelezo chake ndiyo wakuu, wenye cheo.

Maneno ya Paulo yanadhihirisha ukuu wa hakika ambao ndio ukristo halisi. Paulo asema: "Ijapokuwa mimi ni huru kwa watu wote, lakini nimekuwa mtumwa wa wote. Sitafuti faida yangu mwenyewe, ila faida ya wengi, ili wapate kuokolewa.' 1 Wakorintho 9:19; 10:33.

Kwa habari ya dhamiri hakuna mtu anayeweza kumtawala mwingine na kumpangia mambo yampasayo kutenda. Mungu amempa kila mtu uhuru wa kufikiri na kuamua. Kadiri ya uamuzi wake. Katika habari za kanuni, Paulo asema: "Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe." Warumi 14:5. Malaika wa mbinguni hawaji hapa duniani kutawala, au kudai heshima, ila huja kushirikiana na kuwainua wanadamu.

Kanuni na mafundisho ya Kristo yalikaa katika mawazo ya wanafunzi wake wapendwa mpaka siku zake za mwisho. Uzito wa mahubiri ya Yohana ulikuwa: "Mapana, hii ndiyo habari mliyosikia tangu mwanzo, kwamba tupendane sisi kwa sisi." "Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa Yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.' 1 Yohana 3:11, 16.

Roho ya namna hii ndiyo ilikuwako katika kanisa la kwanza baada ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu "Watu walioamini walikuwa na mojamoja na roho moja." Mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi kwa." Matendo 4:32, 33.

## 61 — Mtu Mfupi Aliyekuwa Mashuhuri [308]

Mji wa Yeriko ulijengwa katika uwanda wa katikati katika Tropiki, mahali pazuri sana penye majani mazuri, na kuzungukwa na chemchemi za maji na vilima vinavyong'aa kama chokaa. Mji ulikuwa kituo kikuu cha biashara. Wakuu wa Kirumi na askari; pamoja na wageni wengi kutoka kila mahali walipatikana hapa. Watoza kodi wengi walikuwa wanashughulika kutoza ushuru.

Mkuu wa watoza ushuru alikuwa Myahudi aitwaye Zakayo, alikuwa akichukiwa sana na watu wa kwao kwa kumfikiria alijitajirisha kwa njia za dhuluma. Walakini hata hivyo Zakayo hakuwa kama vile watu walivyomdhani. Zakayo alikuwa amemsikia Yesu. Habari za wema wake na fadhili zake kwa watu wote zilienea kila mahali. Yohana Mbatizaji alikuwa amehubiri Yordani na Zakayo alikuwa amesikia mwito wa kutubu. Na sasa aliposikia habari za Mwalimu Mkuu, alijiona kuwa mwenye dhambi mbele za Mungu. Walakini habari za Yesu alizosikia zilimchangamsha moyo.

Akaona kuwa ana haja ya kutubu na kujirekebisha. Je, mtoza ushuru mwingine hakuwa mfuasi mwaminifu wa Mwalimu, ingawa ni mtoza ushuru? Zakayo alianza kufanya mipango ya kutekeleza mchangamko wake. Habari ilipotangazwa kwamba Yesu anaingia Yeriko, Zakayo aliazimu kumwona.

Mtoza ushuru huyu alitamani kuona uso wa mtu mwenye maneno yaliyomletea tumaini moyoni mwake.

Njia zilikuwa zimejaa watu, na Zakayo ambaye alikuwa mtu mdogo na mfupi hangeweza kuona chochote kwenye watu warefu jinsi hiyo. Kwa hiyo Zakayo alitangulia mbele, akapanda juu ya mkuyu. Wakati mkutano ulipopita alikodoa macho yake kwa hamu ili apate kuona sura ya mtu huyu aliyemtamani.

Ghafla mkutano ulisimama chini ya mkuyu huo. Mtu ambaye [309]
aliweza kusoma mioyo ya watu, alitazama juu. Mtu huyu aliyekuwa juu ya mkuyu alisikia sauti ya mtu ikisema: "Zakayo, shuka upesi, kwa maana leo nitashinda nyumbani kwako."

Zakayo alishuka. Akitembea kama mtu yumo ndotoni aliongoza njia kwenda nyumbani kwake. Lakini marabi na watu wengine katika mkutano walinung'unika wakisema, Anakwenda kwa mtu mwenye dhambi.

Zakayo alikuwa na wasiwasi mwingi sana kwa Yesu kuingia kwake, maana alijiona kuwa hastahili hata kidogo. Sasa upendo kwa Bwana wake mpya na mgeni wake, ulimfanya asinyamaze. Ataungama wasiwasi mbele ya watu. Zakayo alisimama mbele ya mkutano akasema: "Bwana, tazama, nusu ya mali yangu nitawagawia maskini, na ikiwa kuna mtu yeyote niliyemdhulumu, nitamrudishia mara nne. Yesu akasema: "Leo wokovu umeingia nyumbani humu, kwa kuwa huyu naye ni mtoto wa Ibrahim."

Sasa wanafunzi walionyeshwa kielelezo dhahiri cha maneno ya Kristo jinsi yalivyo kweli kwamba; "Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu yawezekana" Luka 18:27. Waliona sasa kwa uwezo wa Mungu kwa tajiri anaweza kuingia ufalme wa Mungu.

Kabla Zakayo hajamwangalia Bwana uso wake, aliungama kwanza dhambi zake. Alianza kutekeleza maandiko yaliyoandikwa zamani, kwamba, "Ndugu yako akiwa maskini, na akawa hawezi kujisaidia, msaidie, awe kama mgeni au msafiri kwako. Usimtoze faida ya kitu chochote ila mche Mungu."

"Msitendeane ubaya ninyi kwa ninyi, bali mtamcha Mungu wenu, kwa maana mimi ni Bwana Mungu wenu." Mambo ya Walawi 25:35, 36, 17. Jambo la kwanza Zakayo alilosema kwa Kristo, kuonyesha toba yake lilikuwa kuwafadhili maskini na wenye dhiki. Kati ya watoza ushuru kulikuwa na umoja wa kuwadhulumu watu, na kusaidiana wao kwa wao. Lakini Zakayo alipoamini alitupilia mbali matendo yasiyokuwa ya adili.

Hakuna maungamo yaliyokamlika, isipokuwa yawe na matengenezo ya mambo yaliyokwenda upogo. Haki ya Kristo siyo koti la kuficha dhambi ambazo haziachi kutendwa na mtu. Utakatifu ni hali ya kutakaswa kwa Mungu, kwa njia ya kujitoa kamili kwake, na kufuatana na kanuni za mbinguni.

Mkristo katika shughuli zake ulimwenguni ni kumdhihirisha Kristo na kuonyesha namna ambayo. Kristo mwenyewe angekuwa.
[310] Kwa kila tendo atendalo angeonyesha kuwa Mungu ndiye mwalimu wake. Neno: "Utakatifu kwa Bwana" lingeandikwa katika mambo

yake yote atendayo. Kila muumini wa Kristo angeonyesha kuwa anaruhusu utakatifu umkalie, kwa njia ya kuachana na matendo yote yasiyokuwa ya kweli. Ataonyesha ukweli wake waziwazi kama Zakayo alivyofanya. Maandiko husema: "Kama mwovu akirudisha amana yake, na kumrudishia mtu mali aliyomwibia na kutembea katika njia ya haki, bila kutenda maovu ataishi hakika." Ezeldeli 33:15.

Kama tumewaumiza wengine, tumedanganya katika biashara, au tumemdhulumu mtu yeyote, hata kama tumeasi sheria yoyote, tutaungama dhambi zetu, na kufanya matengenezo na kurekebisha mambo yetu, kwa kadiri ya uwezo wetu. Si lazima turudishe vitu tulivyodhulumu tu, lakini hata vyote ambavyo havikutumika.

Mwokozi alisema kwa Zakayo: "Leo wokovu umeingia katika nyumba hii." Kristo alikwenda kwa Zakayo kumfundisha ukweli, na kufundisha nyumba yake mambo ya ufalme wa mbinguni. Waliokuwa wametengwa na marabi wasiingie katika masinagogi, sasa walikusanyika nyumbani wakiwa na mwalimu wa mbinguni, ili kusikia neno la uzima.

Kristo anapopokelewa kama Mwokozi wa pekee, wokovu huja kwa yule aliyempokea. Zakayo alimpokea Yesu si kama mgeni mpitaji, ila kama mgeni wa kudumu katika moyo siku zote. Waandishi na Mafarisayo walimshutumu kama mtu mwenye dhambi, lakini Mwokozi alimtambua kuwa kama mwana wa Ibrahim. Wagalatia 3:7, 29.

[311] ## 62 — Mariamu Ampaka Yesu Mafuta

Simoni wa Bethania alikuwa mmojawapo wa Mafarisayo wachache waliojiunga na wafuasi wa Yesu dhahiri. Alitumaini kuwa Yesu bila shaka ni Masihi, ila hakumwamini kuwa ni Mwokozi. Tabia yake haikubadilika, na kanuni zake zilikuwa zile zile.

Simoni alikuwa ameponywa ukoma, naye alitamani kuonyesha shukrani yake. Katika safari ya mwisho ya Kristo ya kutembelea Bethania, Simon alimfanyia makaribisho rasmi pamoja na wanafunzi wake. Makaribisho haya yalihudhuriwa na Wayahudi wengi waliotaka kuona mwenendo, wake, na wengine wasiokuwa rafiki zake.

Kama kawaida ya'Mwokozi ilivyokuwa, alikwenda kwa Lazaro kupata mapumziko. Watu wengi walikuja Bethania, wengine kumtaka Yesu, na wengine kumwona Lazaro aliyefufuliwa katika wafu. Lazaro alitangaza kwa uthabiti kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu.

Watu walikuwa na shauku kuona ikiwa Lazaro, ataambatana na Yesu mpaka Yerusalemu, na kama nabii atatawazwa kuwa mfalme wakati wa sikukuu ya Pasaka. Makuhani na wakuu wasingekuwa na subira ya kungoja wakati mwingine wa kumwondoa Yesu kutoka katika njia yao. Wakikumbuka jinsi alivyogutusha mipango yao ya mauaji na walikuwa na wasiwasi kuwa labda hatakuja. Waliulizana wenyewe: “Mnafikirije, hawezi kuja: katika sikukuu?”

Baraza ikaitwa. Tangu kufufuliwa Lazaro mawazo ya watu wengi yalimuunga mkono Kristo kiasi kwamba lisingekuwajambo la busara kumkamata Yesu waziwazi. Kwa hiyo wakuu waliazimia kumkamata kwa siri, na kumshitaki na kumhukumu kimya kimya. Walitumaini kuwa hukumu yake itakapojulikana msimamo genge
[312] wa makutano utawaunga mkono. Lakini kwa kuwa Lazaro anaishi, makuhani na marabi walijua kuwa hawangekuwa salama. Kuwepo kwa mtu aliyekuwa amekufa kwa siku nne, na kufufuliwa kwa neno la Yesu atasababisha upinzani mkubwa kwao. Watu wangelipiza kisasi dhidi ya wakuu wao kwa kumwua Mtu aliyefanya mwujiza

wa nanma hiyo. Baraza la Sanhedrini likaamua kuwa hata Lazaro pia lazima auawe.

Wakati mpango wa njama hii ulipokuwa ukipangwa huko Yerusalemu, Yesu na wanafunzi wake walikuwa katika makaribisho kwa Simoni. Katika makaribisho haya Simoni aliketi upande mmoja wa Mwokozi, na Lazaro upande wa pili. Martha alihudumu, lakini Mariamu alikuwa akisikiliza maneno ya Mwokozi, maana Yesu alikuwa amemsamehe dhambi zake, na kumfufua kaka yake, kwa hiyo moyo wa Mariamu ulikuwa umejaa shukrani tele. Alikuwa amemsikia Yesu akizungumza juu ya kukaribia kwa kifo chake, naye alitamani kumuonyesha heshima yake.

Alikuwa amegharamia kununua kisanduku cha marhamu ambacho ni cha ghali sana, ili kitumike kuupaka mwili wake. Lakini sasa uvumi ulienea kuwa atatawazwa kuwa mfalme. Huzuni ya Mariamu iligeuka kuwa furaha, naye alitaka awe mtu wa kwanza kumheshimia Bwana wake. Alikileta kichupa cha marhamu akikivunja na kummwagia Yesu mafuta kichwani na miguuni, na kisha akapiga magoti huku akilia, na kumlowesha kwa machozi yake, kisha kumfuta kwa nywele zake ndefu. Kushughulika kwake kungeweza kusijulikane na mtu, lakini harufu ya manukato ikajaa chumbani, na kutangaza kitendo chake kwa wote waliokaa humo.

### Kwa nini Yuda alichukizwa

Yuda hakuona kuwa kitendo hicho ni cha muhimu. Alianza kunung'unika, kwa kunong'onezea waliokuwa karibu naye, akimlaumu Yesu kwa kuruhusu kitendo hicho chenye hasara. Yuda aliyekuwa mtunza fedha wa wanafunzi alikuwa amechukua fedha kidogo kutoka katika akiba yao kwa matumizi yake binafsi, na kufanya mfuko wao kuwa hafifu. Alikuwa tayari kukusanya cho chote alichoweza kupata. Wakati akiona kuwa kitu fulani kikinunuliwa kisicho cha muhimu kwake, husema, kwa fedha hizo hazikuwekwa katika hazina yao aliyokuwa anaitunza ili kuwapa maskini?

Kitendo cha Mariamu kilitofautiana na kusudi lake la ubinafsi, kiasi kwamba aliaibika. Alitafuta kutoa sababu ya maana kwa ajili ya katazo lake kwa tunu hiyo; "Mbona marhamu hii haikuuzwa [313]
kwa dinari mia tatu, wakapewa maskini?" Naye alisema hayo, si kwa kuwahurumia maskini, bali kwa kuwa ni mwivi" Laiti kama

Marhamu ya Mariamu yangaliuzwa, na fedha kuwekwa mikononi mwake maskini wasingalipewa kitu.

Kwa kuwa Yuda alikuwa Bwana fedha alijidhani kuwa ni mkuu kuliko wanafunzi wenzake, na alikuwa na mvuto mkubwa sana kwao. Unafiki wake wa kuwapenda maskini uliwadanganya. Manung'uniko yalienea mezani yakisema: "Hasara yote hii ni ya nini? Marhamu hii ingaliuzwa na kuwagawia maskini." Mariamu alisikia alivyoshutumiwa, naye katetemeka moyoni. Alidhani kuwa hata dada yake atamshutumu kwa hasara hii. Hata Bwana pia atamwona kuwa ni mfujaji wa vitu. Akuwa karibu kushusha moyo, wakati Bwana aliposikika akisema: "Mwacheni; mbona mnamtaabisha?" Yesu alijua kuwa katika kutenda hivyo alionyesha shukrani yake kwa ajili ya kusamehewa dhambi zake. Akipaza sauti yake, alisema: "Ametenda kazi njema; alivyoweza maana siku zote maskini mnao lakini mimi hamnami siku zote. Ametenda alivyoweza; ametangulia kupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko."

Manukato ambayo Mariamu angeipaka maridhawa maiti ya Mwokozi aliyapaka mwili wake ulio hai. Kwa kuipaka maiti, manukato hiyo ungepenya na kuenea pote kaburini lakini sasa ikafurahisha moyo wake Kristo. Kuonyesha upendo, wakati Mwokozi akingali hai ulikuwa uthibitisho wa kujitoa kwake, maana alikuwa ana mpaka mafuta kwa ajili ya maziko yake. Kristo alipoingia katika giza kuu la masumbuko yake, alikwenda na kumbukumbu ya kitendo hicho cha upendo na uaminifu ambao utakuwa wake kutoka kwa watakaookolewa milele na milele.

## Mariamu alitii maongozi ya Roho Mtakatifu

Mariamu hakufahamu umuhimu wa kitendo chake cha upendo. Hakuweza kueleza sababu ya kuchagua wakati ule kuwa wa kumtia Yesu mafuta. Roho Mtakatifu alikuwa amempangia naye amefuata maongozi yake. Uvuvio wa Roho hautoi sababu. Nguvu isiyoonekana, huusukuma moyo kutenda. Inayo sababu yake yenyewe. Mtu hutenda tu bila maelezo.

Kristo alimfafanulia Mariamu maana ya kitendo chake: "Kwa kuwa amenipaka mafuta, amefanya hivyo kwa ajili ya maziko yangu." Kama vile kichupa cha marhamu kilivyovunjwa na kujaza nyumba kwa harufu nzuri, hivyo mwili wa Kristo ulikuwa uvun-

jwe lakini akitoka kaburini, ataijaza nchi yote na harufu yake nzuri. "Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, na [314] dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato" Waefeso 5:2.

Kristo akasema: "Amini, nawaambia, kila ihubiriwapo Injili katika ulimwenguni wote na hili alilotenda, huyu litatajwa kwa kumbukumbu lake." Mwokozi alisema kwa uhakika kuhusu injili itakavyohubiriwa ulimwenguni kote. Na kwa kadiri injili itakavyoenea ulimwenguni, tendo la Mariamu litaendelea kutoa harufu nzuri, na mioyo ya watu itaburudishwa kwa tendo lake hilo. Falme zitainuka na kuanguka na mashujaa watasahauliwa, lakini kitendo cha mwanamke huyu hakitafutika katika kumbukumbu za historia takatifu. Mpaka wakati utakapokoma, kichupa cha manukato kilichopasuliwa kitaendelea kueleza habari za upendo wa Mungu wa ajabu kwa wanadamu waliopotea.

Ni fundisho dhahiri kiasi gani Kristo angempatia Yuda! Yeye asomaye madhumuni ya kila moyo angeweza kufunua mbele ya waliohudhuria karamuni sura za siri katika maisha ya Yuda. Badala ya kuwahurumia maskini, alikuwa akiwaibia fedha zilizokusudiwa kuwasaidia. Lakini ikiwa Kristo angemuumbua Yuda, hili lingekazaniwa kama sababu ya kumsaliti. Hivyo Yuda angeweza kupata huruma, hata kutoka miongoni mwa wanafunzi. Mwokozi alijiepusha asimpe kisingizio cha usaliti wake.

## Yuda alitoka katika mwaliko huo kufanya njama ya kumsaliti Yesu

Lakini mtazamo wa Yesu aliomtazama Yuda ulimdhihirishia kuwa, Yesu alisoma unafiki wake wa kujifanya kuwa mfuasi wa Yesu, huku ni mlaghai tu. Na katika kumsifia Mariamu Kristo alimkemea Yuda. Kemeo hilo lilimwumiza Yuda, naye akatoka na kumwendea kuhani mkuu, ili kumsaliti Yesu.

Viongozi wa Israeli walikuwa wamepata fursa ya kumpokea Kristo kama Mwokozi wao, bila fedha na bila gharama. Lakini waliikataa karama yenye thamani na wakamununua Bwana wao kwa vipande thelathini vya fedha.

Yuda alionea husuda tuzo la Mariamu la marhamu ya thamani kwa Yesu. Moyo wake uliwaka kwa wivu vipi Mwokozi asitahili

kupokea tuzo waliyostahili wafalme wa dunia. Kwa gharama pungufu kuliko thamani ya marhamu, alimsaliti Bwana wake.

Wanafunzi hawakuwa kama Yuda. Wao walimpenda Mwokozi, ila hawakuifafanua kwa dhati tabia yake. Mamajusi kutoka
[315] Mashariki ambao walijua mambo machache sana kuhusu Yesu, walionyesha kutambua kwa dhati heshima iliyompasa.

Kristo huthamini vitendo vya ustahifu utokao moyoni. Hakulikataa ua la kawaida lililochumwa na kutolewa na mkono wa mtoto kwa upendo. Alizikubali sadaka za watoto, na kuwabariki watoaji. Katika Maandiko, kwa Mariamu kumpaka Yesu marhamu hutajwa katika kumtofautisha na Mariamu wengine. Matendo ya upendo na taadhima ni ushahidi wa imani katika Yesu kama Mwana wa Mungu.

Kristo aliukubali utajiri wa upendo safi wa Mariamu ambao wanafunzi wake hawakuweza, wasingeweza kuuelewa. Ulikuwa upendo wa Kristo uliomshurutisha. Yale marhamu yalikuwa mfano wa moyo wa mtoaji, uthibitisho wa nje wa upendo uliojazwa na vijito vya mbinguni hadi ukafururika. Upweke wa Kristo, kuishi kwake maisha ya kibinadamu, kamwe hayakufurahiwa na wanafunzi kama ilivyopaswa kuwa. Mara nyingi alihuzunishwa. Alifahamu kuwa ikiwa wangekuwa chini ya mvuto wa malaika wa mbinguni waliofuatana naye, na wao pia wasingefikiria sadaka yo yote ile kama yenye thamani tosha kuutangaza upendo wa moyoni.

## Yesu Kwa Kweli Hakuthaminiwa

Wakati Yesu alipokuwa hayupo pamoja nao tena na wakajiona kama kondoo wasio na mchungaji, ndipo wakaanza kuona, jinsi ambavyo walikuwa waufuraishe moyo wake. Hawakumsukumia lawama tena Mariamu, bali wakajilaumu wao wenyewe. Loo, kama ingeliwezekana kufutilia mbali shutuma zao za awali, kuwaona maskini kuwa waliostahili zaidi lile tunzo kuliko Kristo! Walihuzunishwa mno na lile karipio walipokuwa wakiuondoa msalabani mwili wenye majeraha wa Bwana wao. Leo, ni watu wachache wanaofurahia yale yote Kristo aliyowafanyia. Kama wangefanya hivyo basi ule upendo mkuu wa Mariamu ungedhihirishwa. Hakuna ambacho kingefikiriwa kuwa cha thamani nmo kumpa Kristo, hakuna kujikana nafsi au kujitoa mhanga ambako kungeonekana kama

kupita kiasi kwa ajili yake. Maneno yaliyosemwa kwa hasira, "Ni wa nini upotevu huu?" yalionyesha dhahiri kwa Kristo kafara kuu kuliko zote iliyowahi kutolewa karama yake Mwenyewe kuwa kipatanisho kwa ulimwengu uliopotea. Kwa mtazamo tu wa kibinadamu, mpango wa wokovu ni upotevu potovu waliseme zana. Hebu na jami ya mbinguni waiangalie kwa mshangao jamii ya wanadamu wanaokataa kutajirishwa kwa upendo usiyo na kifani [316] uliodhihirishwa katika Kristo. Hebu kwa mshangao na waseme, kwa nini upotevu huu mkuu?

Lakini sadaka ya upatanisho kwa ulimwengu mpotevu ilikuwa iwe kamili, tele, na timilifu. Kafara ya Kristo ilikuwa tele na zaidi ili kuifikia kila roho. Siyo wote wanaookolewa; hata hivyo mpango wa ukombozi siyo upotevu kwa sababu tu haukufaulu kutimiliza yote yale yaliyokusudiwa kupatikana kwa ukarimu wake. Ni sharti wokovu uwepo tosha nakusaza.

Simon mwenye kuwakaribisha alishangaa kwa maneno ya Yesu, akasema kimoyomoyo, "Mtu huyu angelikuwa nabii angelijua kuwa mwanamke huyu anayemgusagusa ni wa aina gani; maana ni mwenye dhambi."

Kwa sababu Kristo alimruhusu huyu mwanamke kumkaribia, na kwa vile tu hakumkatalia kwa hasira kuwa ni mwenye dhambi nyingi mno kiasi cha kutosameheka, na kwa sababu Kristo hakuonyesha kuwa alimtambua alivyoanguka. Simoni alishawishika kufikiri kuwa Kristo hakuwa nabii. Lakini ni kutokumjua Mungu na Kristo ndiko kulikomuongoza kufikiria kama alivyo waza.

## Jinsi Mungu anavyotenda

Simon hakung'amua kuwa Mwana wa Mungu sharti atende sawa sawa na Mungu, kwa huruma, wema, na msamaha. Fikira za Simoni zilikuwa za kutozingatia huduma ya toba ya Mariamu. Kitendo cha Mariamu kuibusu miguu ya Kristo na kuipaka mafuta kilichochea ugumu wa moyo wa Simoni. Alifikiri kuwa Kristo anapaswa kuwatambua wenye dhambi na kuwakemea.

Kwa mawazo hayo ya Simoni, Mwokozi alijibu "Simon, nina neno nitakalo kukuambia. Akasema, Mtu mmoja mkopeshaji alikuwa na wadeni wawili, mmoja amwia dinari mia tano, na wa pili hamsini. Na walipokuwa hawana cha kumlipa, aliwasamehe

wote wawili. Katika hao wawili ni yupi atakayempenda zaidi? Simon akajibu, akasema, “Nadhani ni yule aliyesamehewa nyingi.” Akamwambia “Umeamua haki.”

Kama alivyofanya Nathani kwa Daudi (2 Samweli 12:1-7), Kristo alimtupia mkaribishaji wake mzigo wa kujihukumu yeye mwenyewe. Simon ndiye aliyemuongoza kutenda dhambi mwanamke huyu anayemdharau sasa. Simon ndiye alimkosesha hasa. Mfano uliosemwa juu ya wadeni wawili, ulihusu Simon na Mariamu. Yesu hakutaka kufundisha kwamba tofauti za matakwa zingeonekana baina ya watu wawili, maana kila mtu alipaswa
[317] kushukuru kwa yale aliyosamehewa. Lakini Yesu alitaka kuonyesha kuwa Simon alikuwa na dhambi kubwa kuliko ya Mariamu, kama vile deni la dinari mia tano linavyozidi deni la hamsini. Simon sasa alinza kujiona katika nuru mpya. Aliona jinsi Mariamu alivyofikiriwa na yule aliyekuwa zaidi ya nabii. Akaaibika sana, akatambua kuwa alikuwa mbele ya Mtu mkuu kuliko yeye mwenyewe.

Kristo aliendelea kusema, “Niliingia nyumbani mwako, wala hukunipatia maji ya kuosha miguu yangu, lakini Mariamu kwa moyo wa kutubu ameniosha miguu yangu kwa machozi, na kuifuta kwa nywele za kichwa chake. “Hukunibusu, lakini mwanamke huyu, ambaye unamdharau, tangu nilipofika hakuacha kubusu miguu yangu.” Kristo alihesabu muda ambao Simon alioupata wa kuonyesha kuwa Bwana amemtendea mema kiasi gani. Mchunguza mioyo aliona kilichomfanya Mariamu atende kitendo hicho. Aliona pia kilichomfanya Simon aseme maneno ya jinsi hiyo. Yesu alisema, “Wamwona mwanamke huyu?” Nakuambia, “Dhambi zake ambazo ni nyingi zimesamehewa, kwa kuwa amependa sana. Lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo.”

Simon alidhani kuwa amemheshimu Yesu kwa vile alimkaribisha nyumbani kwake. Lakini sasa ameona ukweli wa mambo ulivyo. Aliona kuwa dini yake ilikuwa ni vazi la Kifarisayo tu. Alikuwa amedharau wema wa Yesu. Hakumtambua kama mjumbe wa Mungu. Mariamu alikuwa mwenye dhambi aliyesamehewa, lakini yeye alikuwa mwenye dhambi ambaye hakusamehewa.

### Jinsi kiburi cha Simon kilivyoshushwa

Simoni aliguswa na wema wa Yesu ambao uliomfanya asikemee wazi mbele ya wageni wake. Hakutendewa jinsi alivyotaka Mariamu atendewe. Aliona kuwa Yesu alitafuta kwa wema na huruma kuutiisha moyo wake. Kukemewa kwa ukali, kungalishupaza toba, lakini onyo la upole kulimsadikisha dhidi ya kosa lake. Aliona ukubwa wa deni analowiwa na Bwana wake. Farisayo huyu jeuri alitubu, akawa mnyenyekevu, na mwanafunzi aliyejikana nafsi. Kristo alijua hali iliyoongoza maisha ya Mariamu. Angaliweza kuzima kila cheche ya tumaini rohoni mwake, lakini hakufanya hivyo. Alikuwa amemnyanyua kutoka katika kukata tamaa na maangamizi. Mara saba alikuwa amesikia Yesu akikemea mashetani yaliyokuwa yakimtawala moyoni na akilini. Alikuwa amemsikia akimlilia Baba yake kwa nguvu zote kwa niaba yake. Mariamu alijua jinsi dhambi ilivyo kinyaa kwa weupe wa usafi wake Yesu, na kwa uwezo wa [318]
Yesu alikuwa ameshinda hali hiyo.

Wakati ilionekana kwa hali ya kibinadamu kuwa hali ya Mariamu ni isiyo na tumaini, lakini Kristo aliona ndani ya Mariamu uwezekano wa hali bora. Mpango wa ukombozi umempa mwanadamu uwezekano mkubwa, na katika maisha ya Mariamu mambo haya yangewezekana. Kwa njia ya neema yake Yesu, Mariamu akawa mshirika wa asili ya Uungu. Aliyekuwa ameanguka, ambaye moyo wake umekuwa makao ya mashetani, alifikishwa karibu na Mwokozi katika ushirika na utume. Mariamu aliketi miguuni pake, na akajifunza kwake' alimpaka mafuta, na kumnawisha miguu yake kwa machozi yake; Mariamu alisimama kando ya msalaba, na akanifuata mpaka ka-burini; Alikuwa wa kwanza kufika kaburini na kumtangaza Mwokozi aliyefufuka.

Yesu hujua hali zote za kila mtu. Unaweza kusema kuwa u mwenye dhambi sana, sana. Labda ndivyo; lakini jinsi ulivyo ovyo, ndivyo unavyonihitaji zaidi Yesu yeye hamzuii mwenye machozi na toba Yeye huwasamehe wale wote wanaomjia kupata msamaha na kufanywa upya.

Watu wanaomwendea, kama kimbilio, Kristo huwaunganisha katika asili ya Uungu wake. Hakuna mtu au malaika mwovu atakayewashutumu. Watasimama ubavuni mwake Mwondoa dhambi mkuu, katika nuru iangazayo kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu.

"Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; na zaidi ya hayo amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea." Warumi 8:33, 34.

## 63 — Yesu Atangazwa Kuwa Mfalme wa Israeli [319]

Miaka mia tano kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, nabii Zekaria alitabiri kuja kwake kama mfalme wa Israeli. Alisema: "Furahi sana, Ee binti Sayuni, Piga kelele, Ee binti Yerusalemu, tazama mfalme wako anakuja kwako; ni mwenye haki naye ana wokovu, Ni mnyenyekevu, amepanda punda Naam, mwana punda mtoto wa punda." Zekaria 9:9. Yeye aliyeukataa ufalme na heshima yake, sasa aliingia Yerusalemu kama mrithi aliyetabiriwa wa kiti cha ufalme wa Daudi.

Katika siku ya kwanza ya juma, Kristo aliingia kwa shangwe mjini: Watu wengi waliokuja Bethania ili kumwona walifuatana naye. Wengine waliokuwa wakienda katika Pasaka waliungana naye pia. Shangwe ilionekana mahali pote hata miti ilitoa maua, na mwamko wa kutawazwa kwa mfalme mpya ulionekana kwa watu.

Yesu alikuwa amewatuma wanafunzi wawili waende wakamletee punda na mwana punda. Ingawa ng'ombe walioko milimani elfu, elfu ni mali yake, (Zaburi 50:10) alimtegemea mgeni ili amfadhili, na mnyama wa kupanda ili aingie Yerusalemu kwa shangwe, kama Mfalme. Walakini hata hivyo Uungu wake ulidhihirishwa katika wakati uliotajwa. Kama alivyotabiri "Bwana ana haja nao," alipewa mara moja. Wanafunzi walitandika nguo zao juu ya punda, wakampandisha Bwana wao juu yake. Kila mara Yesu alikuwa akitembea kwa miguu, na sasa wanafunzi walishangaa kutaka kumpanda punda. Lakini hamu yao iliwaka kuwa ataingia mjini ajitangaze kuwa mfalme mwenye uwezo. Mashangilio ilijaa mji wote, na matazamio ya watu yaliamshwa kwa kiwango cha juu.

Kristo alifuata desturi ya Kiyahudi ya kuingia kwa heshima mjini, kama mfalme. Unabii ulitabiri kwamba Masihi ataingia hivyo kwa shangwe kama mfalme. Mara moja alipopanda punda watu [320]
wakamtukuza kama Masihi Mfalme wao. Wanafunzi na makutano waliona katika dhana zao majeshi ya Warumi yakifukuzwa kutoka katika nchi yao, na Waisraeli wanakuwa taifa huru tena. Wote walishindana katika kumtukuza kwa heshima kuu. Badala ya kumpa

zawadi za gharama, walitandika mavazi yao chini kama zulia njiani na kutawanya matawi ya mizeituni na mitende. Wakiwa hawana bendera ya kifalme kupeperusha, walikata matawi mapana ya mitende, kama nembo ya Asili ya ushindi, na kuyapeperusha juu.

Watazamaji waliochanganyikana na kundi, waliuliza: "Huyu ni nani? Hoi lioi hii yote ni ya nini? Walijua kuwa Yesu amekataa juhudi zote za kumtawaza kuwa mfalme, na walishangaa kugundua kuwa huyu ndiye. Ni kitu gani kilichombadilisha yeye aliyekuwa ametangaza kuwa ufalme wake siyo wa dunia hii?

Kutoka kwa makutano waliokuja kuhudhuria Pasaka, maelfu walimsalimu kwa kumpungia matawi ya mitende na kumwimbia nyimbo takatifu. Makuhani Hekaluni walipiga tarumbeta ya kuwaita watu kwenda katika ibada, ya jioni, lakini ni watu wachache tu ndio walioitikia kwenda. Wakuu wakasemezana: kwa hofu "Ulimwengu umekwenda nyuma yake."

### Kwa nini Yesu alikubali hoi hoi hizo

Kabla ya hapo Yesu alikuwa hajaruhusu hoi hoi kama hizo. Aliona mbele matokeo yake. Mambo hayo yangalisababisha kifo chake. Lakini alitamani kudhihirisha kujitoa kwake kafara ambako kungekuwa kilele cha utume wake kwa dunia iliyoanguka. Yeye aliye asili ya mfano wa Kondoo kwa tendo la hiari akajiweka, wakfu kama dhabihu. Kanisa lake katika vizazi vyote, lazima lihesabu kifo chake kuwa jambo muhimu la kutafakari na kujifunza kwa ndani. Kila jambo lihusulo kifo hicho lazima lithibitishe pasipo mashaka kabisa. Matukio yaliyotangulia kafara yake kuu lazima yaelekeze kwa kafara yenyewe. Baada ya thubuti kama ile ya maingilio yake Yerusalemu, macho ya watu wote yatafuata safari yake hadi kufikia mwisho wake. Maingilio hayo ya shangwe yatakuwa mazungumzo ya kila mtu na kumweka Yesu mawazoni mwa kila mtu. Baada ya kusulibishwa kwake, watu wengi watakumbuka mambo haya, na hivyo kuongozwa kuuchunguza unabii. Wengi watakirishwa kuwa hakika Yesu alikuwa ndiye Masihi.

Siku hii, iliyoonekana kwa wanafunzi kama siku ya ajabu katika
[321] maisha yao, ingetiwa giza la mawingu kama wangejua ilikuwa utangulizi wa kifo cha Bwana wao. Alikuwa amewaambia mara kwa

mara kuhusu kafara yake, lakini katika ile furaha kuingia Yerusalemu walisahau maneno yake ya huzuni.

Isipokuwa tofauti chache tu, wale wote waliojiunga na msafara ule walishikwa na uvuvio wa saa ile. Shangwe ziliendelea kupazwa: "Hosana kwa Mwana wa Daudi. Abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana. Hosana aliye juu mbinguni."

### Hakuna msururu wa maombolezo katika ushindi huu

Kamwe ulimwengu ulikuwa haujapata kuona maandamano ya ushindi jinsi hii. Mwokozi alizungukwa na nyara tukufu za kazi zake za upendo kwa mwanadamu mwenye dhambi. Hizi zilikuwa mateka waliokolewa kutoka kwa mamlaka ya Shetani. Vipofu waliokuwa wamepata kuona waliongoza maandamano. Bubu waliokuwa na ndimi huru walipiga kelele za Hosana. Viwete waliokuwa wame-ponywa nao waliruka ruka kwa furaha. Wenye ukoma aliowatakasa walitandika mavazi yaliyosafi katika njia yake. Lazaro aliyeamshwa kutoka katika usmgizi wa mauti alimuongoza punda aliyepandwa na Mwokozi.

Mafarisayo wengi wakiwaka kwa hasira ya wivu, walijaribu kuwanyamazisha watu, lakini vitisho vyao viliongeza tu kelele za hoihoi. Katika juhudi ya mwisho walimwambia Mwokozi: "Bwana wanyamazishe watu hawa. Wanapiga kelele na kuvuruga mambo ambavyo si sheria." Lakini Mafarisayo walinyamazishwa na jibu la Yesu, aliposema: "Nawaambieni, watu hawa wakinyamaza, mawe yatapiga kelele mara moja." Shangilio hili shangwe yalikuwa yametabiriwa na manabii. Watu wangeshindwa kutimiza mpango wa Mungu, mawe ambayo hayazungumzi, yangemshangilia Mwana wake. Mafarisayo waliponyamazishwa watu wakayatimiza maneno ya nabii Zekaria wakiimba:

Furahi sana, Ee binti Sayuni;
Piga kelele, Ee binti Yerusalemu;
Tazama, mfalme wako anakuja kwako;
Ni mwenye haki, naye ana wokovu;
Ni mnyenyekevu, amepanda punda,
Naam, mwanap-unda, mtoto wa punda.

Maandamano yalipofika kwenye ukingo wa kilima, Yesu na maandamano yote walisimama. Mbele yao mji wa Yerusalemu uli-

tanda na utukufu wake, uking'aa kwa mwangaza wa jua kuchwa.
[322] Hekalu maarufu liliinuka kuliko majengo yote, ambalo lilikuwa fahari na utukufu wa taifa la Wayahudi. Hata Warumi pia walijivunia fahari yake. Fahari yake na utajiri wake vililifanya kuwa ni mojawapo ya maajabu ya ulimwengu.

Wakati jua lilipokuwa likishuka upande wa magharibi, miali yake ilipiga katika mawe ya hekalu yenye thamani kuu, na kuling'aza. Kutoka pale Yesu alipokuwa akisimama, lilionekana likimetameta kama jengo la barafu, lenye minara ya dhahabu, liking'aa kwa utukufu kana kwamba ni utukufu wa mbinguni.

### Yesu Atokwa Na Machozi

Yesu alilikazia macho tamasha, na umati ukawa kimya, wakiwa wamepigwa na butwaa kwa uzuri. Macho yote yalielekezwa kwa Mwokozi' Wakashangazwa na kuhuzunishwa kuyaona macho yake yakilengwalengwa na machozi huku mwili wake ukisukasuka kama mti uliokumbwa na kimbunga. Kilio cha uchungu kilisikika ghafla kutoka katika midomo yake iliyokuwa inatetemeka, kama vile kutoka katika moyo uliovunjika. Ni shani ya jinsi gani kutazamwa na malaika! Ni shani ya jinsi gani kuangaliwa na makutano yenye furaha yaliyokuwa yanamsindikiza kuingia mji mtakatifu, ambapo walitegemea alikuwa karibu kutawala! Huzuni hii ya ghafula ilikuwa kama ishara ya kilio katika jamii inayoshangilia. Mfalme wa Israeli alikuwa analia; siyo machozi ya furaha ya kimya, bali ya uchungu usiozuilika. Kwa ghafla makutano wakapigwa na giza la huzuni. Wengi wakilia kwa huruma na huzuni wasiyoweza kuielewa.

Mbele ya Yesu kulikuwa Gethsemane, ambako muda si kitambo giza kuu la kutisha litamkabili. Lango la Kondoo pia lilikuwa likionekana, ambalo ndio kondoo wa kafara walipokuwa wakipitia kupelekwa machinjoni. Lango hii karibu lifunguliwe ili Yeye aingie ambaye ndiye Kondoo wa kafara wa kweli, na ambaye kondoo waliochinjwa walikuwa mfano wake. Karibu hapo kulikuwa na Kalwari, mahali hasa pa uchungu uliokuwa unamkaribia. Walakini huzuni yake siyo ya ubinafsi. Wazo la huzuni ya nafsi yake halikutisha roho yake. Kitu kilichomhuzunisha ni kule kuuona mji wa Yerusalemu, Yerusalemu uliokuwa umemkataa Mwana wa Mungu, na kuudhihaki upendo wake, na ulikuwa unapanga kumwua. Aliona

jinsi ambavyo ungekuwa ikiwa ungemkubali yeye pekee ambaye angeuponya jeraha lake. Angewezaje kuuachilia mbali?

Waisraeli walikuwa watu waliopendelewa sana; Mungu alikuwa amelifanya hekalu lake kuwa makazi yake; "Kuinuka kwake ni mzuri sana, ni furaha ya dunia yote." Zaburi 48:2. Kwake Yehova ameonyesha utukufu wake, makuhani wamehudumu, kawaida za dini na ibada zimefanyika miaka yote. Lakini haya yote lazima yakome. Yesu alipunga mkono wake juu ya mji ulikuwa unaijiliwa na ajali, na kwa huzuni alisema: "Laiti ungejua, hata wewe, katika siku hii yapasayo amani yako! "Mwokozi hakuyasema mambo jinsi yangelikuwa kama wangalitafuta msaada wa Mungu, na shukrani yao kwake kwa kumtoa Mwanawe kama zawadi. Yerusalemu ungalisimama katika majivuno ya mataifa na falme kwa msaada wa Mungu, wala Warumi wasingalikanyaga ndani yake. Mji ungalidumu kati ya miji mikuu ya dunia. [323]

Mwokozi aliacha kusema vile ambavyo hali ya Yerusalemu ingekuwa kama ungekuwa umekubali msaada ambao Mungu alitamani kuupatia tuzo la Mwana wake. Yerusalemu ungeendelea kutukuka kama fahari ya usitawi, malkia katika madola, ukiwa huru katika nguvu za enzi itokanayo na Mungu, na bendera za Warumi kamwe zisingepepea juu ya kula zake. Mwana wa Mungu aliona kuwa ungekuwa huru kutokana na utumwa na kusimamishwa kama mji mkuu wa dunia. Kutoka katika kuta zake njiwa wa amani mngeruka kuyaendea mataifa yote. Ungekuwa taji ya utukufu wa ulimwengu.

Lakini Mwokozi alijua kuwa sasa Yerusalemu uko chini ya utawala wa Warumi, ukikabiliwa na adhabu ya Mungu kama malipo yake, ila sasa mambo haya yamefichika kutoka machoni mwake. "Kwa kuwa siku zitakuja, adui zako watakuzingira na kukujengea maboma, kukuzunguka, nao watakubomoa kabisa, hata mawe ya msingi wake yatafukuliwa kabisa, jiwe lisibaki juu ya jiwe jingine kwa sababu hukujua majira ya kujiliwa kwako."

Yesu aliona mji wenye ajali, ukizingirwa na adui zake hata kuangamia kwa njaa na kwa upanga, mama wakila mizoga ya watoto wao, na wazazi wakinyang'anyana mizoga ya waliokufa kati yao wao kwa wao. Upendo wa mama kwa watoto wao utatoweka kabisa kwa sababu ya njaa. Yesu aliona kuwa ugumu wa Wayahudi utawafanya wasisalimu amri kwa washambuliaji wao na hivyo wajivutie mateso bila sababu. Aliona misalaba ikiwekwa

na watu wakiangikwa juu yao. Aliona jinsi majumba mazuri ya kifalme yatakavyoharibiwa, na hekalu lao wanalojivunia aliliona katika hali ya maangamizo yasiyosemekana, na katika kuta zake
[324] kuu hakuna jiwe litakalosalia juu ya jiwe jingine ambalo halikubomolewa. Aliona mji mashuhuri ukilimwa kama shamba.

Jinsi baba anavyomwombolezea mtoto wake, aliyekufa, ndivyo Yesu alivyouombolezea mji wa Yerusalemu. Alisema: "Nitawezaje kukuacha? Nitawezaje kukuona ukiwa ndani ya magofu? Jinsi jua litakavyopita juu yako likienda kutua upande wa magharibi, ndivyo Yerusalemu utakavyokoma." Wakati maandamano yalipokuwa yangali yakisimama penye mlima wa mizeituni nafasi ya kuokoka: kwa Yerusalemu ilikuwa bado iko.

Wakati mishale yajua ilipokuwa ikizama taratibu, upande wa magharibi, malaika hawawezi kuwatubisha watu hawa wapate kuuona upendo wa Mwokozi? Mji mzuri usio, mtakatifu uliowaua manabii na kuukataa upendo wa Mwokozi, siku yake ya mwisho ilikuwa inafikia mwisho, yaani mwisho wa rehema.

Hata hivyo Roho wa Mungu atasema na watu wa Yerusalemu tena. Kabla ya mwisho wa siku ushuhuda mwingine wa Yesu utatolewa. Kama Yerusalemu ungalimpokea Mwokozi alipoingia kwake kwa shangwe, ingeweza kuokolewa.

Lakini wakuu wa Yerusalemu hawakumtaka Mwana wa Mungu. Maandamano yalipokuwa karibu kupanda katika kilima cha mizeituni wakuu walizuia njia wakiuliza kuwa sababu ya ghasia hiyo ni nini? Walipouliza kuwa "Huyu ni nani?" Wanafunzi wakijaa na roho ya ujasiri, walikariri unabii unaomhusu Kristo.

Adamu atawaelezeni. Huu ni uzao wa mwanamke utakaoponda kichwa cha nyoka. (Tazama Mwanzo 3:15). Ibrahimu atawaambia: Ni Melkizedeki, Mfalme wa Salemu, Mfalme wa Amani. (Tazama Mwanzo 14:18) Yakobo atawambia: Ndiye Shilo wa kabila la Yuda, Isaya atawaelezeni, "Imanueli, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani." Isaya 7:,14; 9:6.

Yeremia atawaelezeni "Shina la Daudi. Bwana ni Haki yetu." Yer 23:6. Danieli atawaelezeni: "Yeye ni Masihi (Mtiwa mafuta)." (Tazama Dan 9:24-27). Yohana Mbatizaji atawaeleza: "Yeye ni Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29.

Yehova Mkuu ametangaza: “Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu.” Mathayo 3:17. Sisi wanafunzi wake tunatangaza: “Huyu ni Yesu, Masihi, Mkuu wa uzima, Mkombozi wa ulimwengu.”

[325] 
## 64 — Watu wa Kuangamia

Juhudi ya mwisho ya kuusihi Yerusalemu upate kutubu imekuwa kazi bure. Makuhani na wakuu wamesikia sauti ya unabii, wakati walipouliza kuwa, “Huyu ni nani?” Lakini hawakukubaliana nayo kuwa ni sauti ya unabii, inayowaita watubu. Walijaribu kuwanyamazisha watu kwa hasira. Kwa maofisa Warumi waliokuwa katika maandamano, ambao ni maadui wa Yesu, walimlaumu Yesu kuwa analeta fujo ya maasi. Walidhani kuwa atachukua uongozi wa hekaluni, na kutawala katika Yerusalemi kama mfalme wao.

Lakini kwa sauti ya upole, Yesu aliwajibu kwamba hakuja kusimamisha ufalme wa duniani. Karibuni atapanda kwenda kwa Babaye, na adui zake hawatamwona tena, mpaka atakapokuja tena katika utukufu. Hapo basi, wakiwa wamechelewa mno ndipo watakapomkiri.

Yesu aliyasema maneno haya kwa masikitiko sana. Wakuu wa Kirumi walinyamazishwa kimya. Mioyo yao iliwaka sana. Katika uso wa Yesu waliona hali ya upendo na Uungwana. Wakaona hali ya huruma katika mioyo yao, kwa jinsi wasivyoweza kuelewa; wakamheshimu sana. Walipowaona makuhani na wakuu, waliwaona kuwa watu wakaidi na wafedhuli sana.

Wakati ule ule Yesu alitoweka, akaenda hekaluni. Mahali hapo palikuwa kimya, kwa kuwa maandamano yaliyoelekea katika mlima wa mizeituni, yamevuta watu huko. Yesu alibaki mwenyewe kwa muda kitambo akiliangalia hekalu kwa masikitiko. Kisha alirudi kwenda Bethania. Watu walipomtafuta wamtawaze, hakuonekana.

Usiku kucha Yesu alikuwa akiomba. Kulipopa-mbazuka alirudi hekaluni tena. Alipokuwa njiani, aliona njaa, “naye aliuona mtini
[326] kwa mbali kidogo, umestawi sana. Akaujia akitazamia kupata matunda kwake. Alipoufikia hakupata cho chote kwake, maana wakati wa kuzaa tini haujafika”.

Katika nyanda za juu kuelekea Yerusalemu, ni kweli kuwa wakati wa kuzaa tini haujafika, lakini katika viunga ambako Yesu alitokea, mtini mmoja ulionekana kana kwamba umetangulia mingine.

Ulikuwa umetanda majani tayari kuweka maua na matunda. Lakini mwoonekano wake ulikuwa udanganyifu tu. Yesu hakuona kitu cho chote juu yake ila majani tu.

Kristo aliulaani kwa kusema, “Mtu ye yote asile matunda kwako.” Asubuhi yake Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakirudi njiani, waliona kuwa matawi na majani yake yamenyauka. Petro alisema: “Bwana, tazama mtini ulioulaani umenyauka.”

Kitendo cha Kristo kuhusu kulaani mtini kilionekana kwa wanafunzi wake kuwa si kawaida. Walikumbuka maneno yake yasemayo “Mwana wa Adamu hakuja kuangamiza watu, bali kuokoa.” Luka 9:56. Kazi zake hazikuwa za kuharibu, ila za kutengeneza. Kitendo hiki ni cha pekee. Makusudi yake yalikuwa nini? Wanafunzi waliuliza.

“Kama mimi niishivyo, asema Bwana Mungu, sikufurahii kufa kwake mwovu ...” Ezekieli 33:11. Kwake, maneno ya kutukana, na kulaani ni kazi ngeni, au nl “tendo la kigeni.” Isaya 28:21. Lakini kwa rehema na upendo huinua pazia linalofunika mambo mbele, ili laana ya dhambi ionekane.

Mtini uliokauka, uliojionyesha wazi mbele ya Kristo, ulikuwa mfano wa Wayahudi. Kristo alitaka kudhihirisha ajali ya Wayahudi kwa mfano huo wa mtini.

Wayahudi walijidai kuwa na haki kuliko mataifa yote. Lakini walikuwa wafedhuli sana na wenye kupenda mapato. Walitangaza madai yao ya udhalimu na kujionyesha kuwa taifa la Kiyahudi ni la haki hasa, lakini halikuwa na lo lote, ila majani tu. Dini ya Wayahudi na hekalu lao mashuhuri pamoja na mipango mizuri ya ibada zao, kwa kweli ilikuwa safi kwa nje tu, lakini unyenyekevu, upendo, na uongofu haukuwako.

## Kwa nini mtini huo ulilaaniwa

Mitini isiyokuwa na majani haikuamsha tegemeo wala kukatisha tamaa. Hii ilisimama badala ya wamataifa, waliokuwa fukara wa utauwa kama vile Wayahudi. Pamoja nao “wakati wa tiini” ulikuwa bado. Walikuwa bado wanasubiri nuru na tumaini. Wayahudi, waliokuwa wamepokea mibaraka mingi zaidi kutoka kwa Mungu, walipaswa kuwiwa kwa kukufuru karama hizi. Nafasi waliyojivunia [327]
iliongeza tu hatia yao.

Yesu alikuja kwa Waisraeli akitumaini kuona kwao matunda yapasayo toba. Kila aina ya baraka walipewa, naye alitumaini kuona kwao hali ya kujinyima, rehema na kuwashughulikia watu wenzao ili wapate wokovu. Lakini upendo wa Mungu na upendo wa watu wenzao ulikuwa umefunikwa na kiburi na ubinafsi. Ukweli wa thamani waliopewa hawakuutoa kwa watu wengine wa ulimwengu. Kwa mfano wa mtini usiozaa wangaliweza kutambua makosa yao na adhabu watakayopata. Mtini uliolaaniwa ulikauka mpaka shina lake. Mfano huo ulionyesha jinsi Waisraeli watakavyokuwa wakati neema ya Mungu itakapoondolewa kwao. Kutoshirikisha mibaraka yao kwa wengine wasinga-liweza kupata mingine. Bwana asema: "Haya ndiyo maangamizo yako, Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako," Hosea 13:9.

Tendo la Kristo la kuulaani mtini aliouumba yeye mwenyewe, husimama kama onyo kubwa kwa makanisa na kwa Wakristo wote. Kuna watu wengi ambao hawaishi maisha ya Kikristo yasiyo na unafiki wala ubinafsi. Wakati ni wa manufaa kwao tu, wanapoweza kujipatia faida. Katika mambo yote ya maisha yao, hili liwe ndilo kusudi lao. Mungu anakusudia kwamba wawasaidie wanadamu wenzao kwa hali zote iwezekanavyo. Lakini ubinafsi huwafanya wasione kitu hicho, ila kujitumikia wenyewe peke yao. Wale wanaoishi kwa njia hiyo ya ubinafsi hufanana na mtini ule. Huonekana kuwa na mfano wa dini, isiyokuwa na imani, wala toba ya kweli. Hukiri kwamba wanamjua Mungu, lakini wakikana nguvu zake. Maneno Kristo aliyotamka kwa mtini, alisema kuwa mtu anayetenda dhambi kiwazi ana heri kuliko mtu anayedai kuwa anamtumikia Mungu bila kuzaa matunda ya haki, yanayoonyesha utukufu wake.

Mfano wa mtini usiozaa uliosemwa na Yesu kabla ya kwenda Yerusalemu, unaofuatana na fundisho la kuulaani mti usiokuwa na matunda. Kwa ajili ya mti usiozaa, mkulima alisema: "Hebu, uuache mwaka huu nao niupalilie, na kuutilia samadi. Ukizaa matunda mwaka ujao vema, la usipozaa ndipo utaukata." Luka 13:8, 9. Mti huo utashughulikiwa. Katika mfano shughuli ya mtunza bustani haikuelezwa, ilitegemea watu ambao Kristo alisemea maneno hayo, ambao walifananishwa na mti usiozaa. Ilitegemea juu yao kuchagua mambo yao. Kila shughuli ilitolewa kwao lakini haikufaa kitu kwao.
[328] Katika tendo la Kristo la kuulaani mtini usiokuwa na matunda,

matokeo yake yalionekana. Wao waliamua juu ya mambo yao ya baadaye, yaani kuangamia.

Kwa muda wa zaidi ya miaka elfu moja Wayahudi walikuwa wamekataa maonyo ya Mungu, na kuwaua manabii wake. Kwa dhambi zile zile, watu wa siku za Kristo walijionyesha kufuata njia ile ile. Mali ile watu wa Israeli waliyokuwa nayo kwa miaka mingi sana, ndiyo na watu wa siku za Kristo walikuwa nayo.

Kunakuja wakati ambao rehema ya Mungu hukoma kuita. Ndipo sauti pole ya Roho Mtakatifu ya kuwasihi wenye dhambi watubu hukoma. Siku kama hiyo ilikuwa imekuja kwa wenyeji wa Yerusalemu. Yesu aliwalilia kwa huzuni kuu watu ambao wanakabiliwa na maangamizo. Lakini haikufaa kitu. Katika kukataa maonyo ya Mungu, Israeli ilikataa njia ya kuwasaidia.

Taifa la Wayahudi lilikuwa mfano wa watu wa karne zote wanaodhihaki wito wa Upendo Mkuu. Machozi ya Kristo alipoulilia Yerusalemu yalikuwa ni kwa ajili ya dhambi za nyakati zote.

Katika kizazi hiki watu wengi husafiri katika barabara ile Wayahudi waliyosafiri bila kujali. Roho Mtakatifu amewazungumzia, bila kujali. Wamekataa maonyo na wajumbe wa Mungu. Leo ukweli wa Biblia, dini ya Kristo, hushindana na mkondo mzito wa ufedhuli. Hali mbaya ya kuchukia neno la kweli, sasa inazidi kuliko wakati wa Kristo. Neno la Mungu linalopingana na mawazo yao linakataliwa wazi, na watu huchagua wapendavyo lakini kwa uangamivu wao.

Wale waliopinga neno la Kristo walipata sababu nyingi kuhusu upinzani wao, mpaka wakatengana na Kweli na Uzima. Mungu hakusudii kuondoa kila kitu watu wanachotoa kama udhuru. Wale wanaokataa nuru ya neno la Mungu watabaki gizani milele. Kwao neno la kweli limefichika.

Maneno ya Kristo humhusu kila mtu anayedharau mwito wa Mungu wa rehema. Kristo anatoa machozi kwa ajili yako, wewe usiyejililia mwenyewe. Kila aina ya uthibitisho wa Mungu, na kila mwali wa nuru ya Mungu hukung'arisha au hufifia na kukuacha katika giza la milele.

Kristo aliona kuwa Yerusalemu utadumu kuwa mkaidi hivyo, lakini maovu yote yanaukalia mlangoni. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa watu wote wanaofuata njia ya namna hiyo. Bwana anasema: "Ee Yerusalemu mwenye kuwaua Manabii ume-

jiharibu mwenyewe.” “Sikia ee nchi, tazama nitaleta maovu juu ya watu hawa, kuwapa matunda ya roho zao, kwa sababu hawakunisikia, wala maneno yangu, wala sheria yangu; lakini wameikataa.” Hosea 13:9; Yeremia 6:19.

## 65 — Hekalu Latakaswa Tena [329]

Mwanzoni mwa huduma yake, Kristo alikuwa amewafukuza hekaluni watu waliokuwa wakifanyia biashara yao batili hekaluni. Ujasiri na mwenendo wake mtakatifu viliwatia hofu wafanya biashara wenye hila.

Panapo mwisho wa huduma yake alikuja tena hekaluni akaona hali ya uchafuzi wa hekalu ingalipo kama hapo kwanza. Milio ya wanyama na kelele za ubadilishaji wa, fedha, na fujo ya kila aina vilifanyika humo. Wakuu wa hekalu ndio waliokuwa wenyewe, wakinunua na kuuza. Wao wenyewe ndio walikuwa wachoyo kabisa, wala mbele za Mungu hawakuwa na afadhali kupita watu wezi.

Kila wakati wa Pasaka na Sikukuu ya vibanda, wanyama maelfu walichinjwa, damu zao zilichukuliwa na makuhani na kumwagwa madhabahuni. Wayahudi walikuwa wamesahau umuhimu wa kuchinja wanyama hao kwamba ni kwa ajili ya dhambi. Hawakufahamu kwamba kuchinja wanyama ni mfano wa kumchinja Kristo kwa, ajili ya dhambi za ulimwengu.

Yesu aliona jinsi Wayahudi walivyofanya mikutano hii kuwa tamasha za kumwaga damu na ukatili. Walikuwa wamezidisha wanyama wa kafara kana kwamba Mungu hupendezwa na huduma za juu juu tu. Makuhani na watawala walizifanya kafara zinazoelekeza kwa Mwana Kondoo wa Mungu kuwa njia za kujipatia mapato. Kwa hiyo utakatifu wa kafara kwa kiasi kikubwa uliharibiwa kabisa. Yesu alijua kuwa damu yake ambayo karibu itamwagwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, nayo ingehafifishwa na makuhani na wazee kama walivyofanya damu ya wanyama!

Kristo alikuwa amepinga matendo ya jinsi hii kupitia kwa manabii. Isaya, akiona kwa njozi Wayahudi walioasi aliwaambia. “Huu [330] wingi wa sadaka zenu mnazonitolea una faida gani? asema Bwana. Nimejaa mafuta ya kafara ya kondoo waume, na mafuta ya wanyama walionona, mimi siifurahii damu ya ng’ombe wala ya wana kondoo wala ya mbuzi waume. Jiosheni, jitakaseni, ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu.” Isaya 1:11-16.

Yeye aliyetoa unabii huu, sasa kwa mara ya mwisho anarudia maonyo haya. Katika utimizo wa unabii huu watu walikuwa wamemtangaza Yesu kuwa mfalme wa Israeli. Alikuwa amekubali heshima yao, na kukubali uteuzi wa kuwa mfalme. Katika tabia hii lazima atende. Alifahamu kuwa katika kujitahidi kuwarekebisha makuhani itakuwa kazi bure; Hata hivyo ushahidi wa utume wake mtakatifu lazima utolewe kwa taifa lisiloamini.

Mara hii tena mtazamo wa kutisha wa Yesu ulieneza ukumbi wote wa hekalu. Watu wote walimtazama. Uungu uliwaka kama umeme katika ubinadamu na kumwangaza, Kristo, kwa utukufu na heshima, ambavyo hakupatwa kuwa navyo kabla ya hapo. Watu waliokuwa karibu naye walisogea mbali kadiri ilivyowezekana. Alisimama peke yake isipokuwa wanafunzi wake wachache. Kukawa kimya kabisa. Kristo alizungumza kwa uwezo mkuu uliotikisa watu kama tufani; Akisema: "Imeandikwa, Nyumba yangu itakuwa ya sala, lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi." Sauti yake ilitoka kama tarumbeta ndani ya hekalu. "Yaondoeni haya ..." Yohana 2:16.

Miaka mitatu iliyopita wakuu wa hekalu walikuwa wameaibishwa na kukimbia kwao mbele ya agizo la Yesu. Hawakutaka tena hali yao ya kudhalilishwa kurudiwa tena mara ya pili. Walakini hata hivyo wakati huu waliogofishwa zaidi kuliko hapo kwanza, na wakaharakisha kutii amri yake. Makuhani na wenye biashara walikimbia na wakiwaswaga ng'ombe wao.

Walipokuwa njiani kutoka hekaluni, walikutana na watu wengi wakileta wagonjwa wao kwa Mganga Mkuu. Habari walizoambiwa na watu waliokimbizwa hekaluni ziliwaogopesha, hata wengine wakarudi, lakini kundi kubwa zaidi walisonga mbele wakitamani kumfikia. Mara ukumbi wa hekalu ulijaa watu wenye maradhi, na waliokuwa karibu kufa na Yesu akawahudumia wote.

Baada ya muda, makuhani na wakuu walithubutu tena kurudi hekaluni. Walikuwa wakidhani kuwa Yesu atatawazwa kuwa mfalme na kuchukua kiti cha Daudi. Walipoingia hekaluni walisimama hali wakiduwaa. Waliwaona wagonjwa wa kila aina wakiponywa,
[331] vipofu wakiona, vilema wakiruka kwa furaha, viziwi wakisikia na kadhalika. Watoto ndio waliokuwa wakishangilia zaidi. Yesu alikuwa amewaponya maradhi yao; na kuwakumbatia mikononi mwake. Na sasa wanamsifu kwa sauti zao za shangwe. Walirudia

kuimba Hosana na kupunga matawi, kama walivyofanya siku ya jana yake.

Sauti za hawa wenye shangwe ziliwachukiza wakuu na waangalizi wa hekalu. Wakawaambia watu kuwa nyumba ya Mungu inadharauliwa sana kwa kelele za shangwe na mirukoruko ya furaha za watoto. Wakuu wakamwambia Kristo: "Husikii hayo yote?" Yesu akawaambia: "Je, hamjasoma kwamba: Kwa midomo ya watoto na kwa midomo ya wanyonyao utakamilisha sifa?" Unabii ulitabiri kuwa Kristo atatangazwa kama mfalme, na Mungu aliwainua watoto hawa wawe mashahidi wake. Kama sauti za watoto zingenyamaza kimya, nguzo za hekaluni zingemsifu Mwokozi.

Mafarisayo walifadhaishwa kabisa. Yesu alikuwa hajajichukulia mamlaka ya kifalme jinsi hivyo. Alikuwa ametenda maajabu, lakini kamwe, alikuwa hajatukuzwa kama wakati huo. Ingawa alikuwa amewachukiza na kuwafedhehesha makuhani na wakuu, lakini hawakufanya lo lote siku ile. Kesho yake tena baraza la Sanhedrin lilikutana ili lione nini cha kumtendea Yesu. Kwa miaka mitatu wakuu walishuhudia kuwa Yesu ni Masihi. Sasa hawakuwa na haja kutaka ishara, ila walitaka akiri au kutamka ili wapate sababu ya kumkamata na kumhukumu.

Ndani ya hekalu walimwuliza: "Unafanya haya yote kwa uwezo gani? Nani amekuruhusu?" Yesu aliwakabili na majibu yenye masharti ya kujibu swali lake: "Ubatizo wa Yohana ulitoka wapi, mbinguni au kwa wanadamu?"

Makuhani waliona kuwa wamo mtegoni. Kama wakisema kuwa ulitoka mbinguni, Yesu atawaambia: Mbona hamkumwamini? Yohana alishuhudia akisema: "Tazama Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Kama makuhani waliukubali ujumbe wa Yohana kwa hiyo wangewezaje kuukataa Umasihi wa Kristo?

Kama wangekubali kuwa ubatizo wa Yohana ulikuwa wa wanadamu, watajiamshia fujo na vita kutoka kwa makutano. Maana waliamini kuwa Yohana ni nabii. Watu walijua kuwa makuhani walimkiri Yohana kuwa nabii, na kukubali kuwa alitumwa na Mungu. Lakini baada ya kushauriana kwa siri, walikata shauri kujitosa wenyewe. Kwa unafiki wakidai hawafahamu, walisema "Hatujui." Kristo naye alisema: "Hata mimi siwaambii kwamba kwa uwezo [332]
gani ninatenda haya."

## Makuhani na wakuu wanyamazishwa

Wakisimama katika hali ya kutahayari, makuhani, wakuu na waandishi walikosa jambo la kusema mbele ya Kristo. Watu wengine walisimama kando wakiwacheka watu hawa wenye kiburi na majivuno wakiwa wameshindwa.

Mambo yote ya Kristo yalikuwa ya maana tupu na mvuto wake ulikuwa, uendelee kukumbukwa kwa kiasi kikubwa hata baada ya kusulubiwa kwake, na kupaa mbinguni. Watu wengi waliamini na kumfuata kwa ajili ya mambo ya siku hiyo. Tofauti baina ya Yesu na Kuhani Mkuu ilionekana wazi kwa jinsi walivyokuwa wakizungumza. Mkuu wa hekalu alijivika kwa heshima na fahari sana. Kichwani alivaa taji lililong'ara, nywele na ndevu zikiwa na mvi kutokana na umri wake. Mbele ya huyu mwenye majivuno, alisimama Mtukufu wa mbinguni bila mapambo yo yote, uso wake umefadhaika, wenye kuonyesha uvumilivu, na uaminifu. Huku akionyesha heshima na huruma. Watu wengi walioyasikia maneno yake na kuona matendo yake siku ile hekaluni walimwamini moyoni mwao kuwa ni nabii wa Mungu. Lakini kadiri watu walivyomfuata, ndivyo chuki ya Makuhani ilivyozidi juu yake.

Halikuwa kusudi la Kristo kuwaaibisha adui zake jinsi hiyo. Alikuwa na fundisho muhimu la kuwafundisha. Kule kudai kutotambua ubatizo wa Yohana Mbatizaji, kulimpa nafasi ya kusema mengi zaidi kwao na kuwadhihirishia hali zao, na kuongeza onyo jingine. "Mnafikiri nini?" Mtu mmoja alikuwa na wana wawili. Akamwambia mtoto wa kwanza: "Mtoto nenda leo shambani ukalime. Akajibu, nitakwenda, wala asiende. Akamwambia na mwingine: Mwanangu, nenda leo shambani ukalime, akakataa, lakini baadaye akajuta na kwenda. Ni yupi katika hao aliyefanya mapenzi ya babaye?"

Swala hili liliwatupa wasikilizaji wake kando ya ngome yao. Mara moja walijibu "Yule aliyekwenda kulima." Yesu akawakazia macho akawajibu kwa ujasiri na kusema: "Amini nawaambieni, watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu katika kuingia kwenye ufalme wa Mungu. Maana Yohana alikuja kwenu kwa njia ya haki, wala hamkumwamini, ila watoza ushuru na makahaba walimwamini, nanyi mlipoona hivyo hamkutubu, ili mmwamini baadaye."

Makuhani na wakuu hawakuweza kumjibu Kristo isipokuwa kama ipasavyo; na hivyo alipata jibu kuwa mwana aliyekataa kulima, walakini baadaye akaenda. Na ambaye alikuwa mfano wa watoza ushuru na makahaba. Yohana alipokuja na kuhubiri toba, watoza ushuru walimwamini na kubatizwa. [333]

Mwana wa pili asiyekwenda kulima ni mfano wa waongozi wa Wayahudi ambao hawakukiri kuwa Yohana alitumwa na Mungu. Walipinga "shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye." Luka 7:30. Wayahudi walikuwa sawa na mwana aliyekataa kulima, wakijidai kukubali, lakini wakitenda kinyume cha maungamo yao.

Makuhani na wakuu waliendelea kuwa kimya. Lakini Kristo alisema: "Sikieni mfano mwingine: Mkulima mmoja alifanya bustani yake, akaizungushia ugo, akachimba shinikizo ndani yake, akajenga mnara, akawakabidhi watunzaji wake, akasafiri katika nchi za mbali. Wakati wa matunda watunzaji wakawakamata watumishi wale, wakampiga mmoja, na kumwua mwingine, na kumpiga mawe mwingine. Tena akatuma watumishi wake zaidi ya wale wa kwanza, wakawatenda kama walivyowatenda wa kwaaza. Mwisho wa yote alimtuma mwanawe, akisema kuwa huyu watamjali. Lakini watunzaji walipomwona, waliambiana. Huyu ndiye mrithi wa yote, basi na tumwue na kutwaa urithi wake. Walimshika na kumtupa katika shinikizo na kumchinja. Je, Bwana wa shamba hili atawatendaje waangalizi wale?"

Makuhani na wazee wakajibu: "Atawaangamiza waovu hao, na kuwaweka watunzaji wengine, ambao watatoa matunda kwa wakati wake." Wasemaji hao waliona kuwa sasa wametoa hukumu inayowahusu wao wenyewe. Jinsi ambavyo watunza shamba walivyopaswa kutoa matunda kwa wakati wake, vivyo hivyo na watu wa Mungu walipaswa kuishi maisha ya kweli kufuatana na hadhi takatifu waliyo nayo. Lakini kama wale watunza shamba walivyowaua watumishi wa Bwana, ndivyo Wayahudi walivyowaua manabii waliotumwa kwao na Mungu ili kuwatubisha.

Hivyo maana ya mfano wa wakulima wale, haukuweza kubishiwa. Mwana mpendwa ambaye alitumwa na Mungu mwishowe, kwa watumishi wakaidi wakamkamata na kumwua, makuhani waliona wazi yaliyokuwa yanamkabili Yesu. Katika adhabu iliy-

owafika watumishi wasiyo na shukurani Kulidhihirika yaliyokuwa yanawasubiri wale ambao wangemwua Kristo.

[334] **Jiwe geni lilokuwa mfano wa Kristo**

Mwokozi akiwaangalia kwa masikitiko, alisema: "Hamkusoma kwamba jiwe lililokataliwa na waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni? Hii ni kazi ya Bwana, nayo imekuwa ajabu machoni mwetu?" Kwa hiyo nawaambieni, ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, litapewa taifa jingine lenye kuzaa matunda yake. Na ye yote aangukaye juu ya jiwe hili atavunjika vipande vipande; lakini yeye yule jiwe hili litakayemwangukia, litamsagasaga kuwa unga."

Unabii huu ulikaririwa na Wayahudi mara kwa mara masinagogini mwao, ukimhusu Masihi ajaye. Kristo alikuwa Jiwe kuu la pembeni katika itikadi ya Wayabudi, na katika mpango mzima wa wokovu. Jiwe hili la msingi sasa lilikuwa linakataliwa na wajenzi wa Kiyahudi. Kwa kila njia na kwa bidii yote, Mwokozi alijitahidi kuonyesha maana ya matendo waliyokuwa wanataka kutenda. Kama wakishindwa kutubu kutokana na maonyo hayo yote, basi hukumu itawakumba, ajali ya Mungu katika kuwanyang'anya nafasi ya taifa lao na kisa cha kuwaacha na siyo tu kuliacha hekalu lao liharibiwe lakini kwa taifa lao kutawanywa.

Wasikiaji wake walifahamu maonyo hayo, lakini ya hukumu waliyojikatia wenyewe, licha makuhani na wakuu walikuwa tayari kujaza kikombe chao kwa kusema: "Huyu ndiye mrithi wa yote, haya na tumwue; "Lakini walipotaka kumkamata, waliogopa makutano, maana walikuwa upande wa Kristo."

Kristo alipotaja juu ya unabii wa jiwe la msingi, lililokataliwa, alikuwa akisemea hekalu la kwanza. Jambo hili lilikuwa na maana kuhusu kuzaliwa kwake Yesu, lakini pia lina umuhimu na kwetu pia. Wakati hekalu la Sulemani lilipojengwa, mawe makubwa yaliandaliwa katika machimbo yake. Yalipoletwa mafundi waliyatia tu katika mahali pake. Kuhusu msingi, jiwe moja lilikuwa limeletwa na wajenzi hawakupata mahali pa kulitia. Jiwe hilo lililokosa mahali pake lilisumbua kuachwa tu pembeni. Hilo likabaki kama jiwe lililokataliwa.

Lakini wajenzi walipotafuta jiwe lifaalo katika hekalu la pili, iliwalazimu watafute na kuchagua jiwe lenye kufaa. Kama watatia

jiwe lisofaa wangalileta uharibifu katika jengo. Lakini mwishowe walilirudia jiwe la kwanza walilolikataa. Lilipigwa na jua na baridi bila kupata nyufa. Baada ya kulijaribu lilionekana kuwa ndilo lifaalo. Jiwe hilo ni mfano wa Kristo.

Isaya asema: "Naye atakuwa ni mahali patakatifu bali ni jiwe la [335] kujikwaza, na Mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili .... Na wengi watajikwaa juu yake, na kuanguka na kuvunjika, na kunaswa na kukamatwa." Kristo atachukua majaribu yote ambayo jiwe la pembeni katika hekalu la Sulemani alikuwa mfano wake. "Tazama naweka jiwe katika Sayuni liwe msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara, yeye aaminiye hatafanya haraka." Isaya 8:14, 15; 28:16.

Mungu alichagua jiwe kuu la pembeni akaliita, "Msingi ulio imara." Ulimwengu mzima unaweza kuweka juu yake uzito wake wote na matatizo yake yote. Vyote vya ulimwengu vitakaa juu yake bila kuuharibu. Wale wanaomtegemea hatawakatishwa tamaa. Yeye amejaribiwa katika mambo yote, akashinda. Amebeba kila mzigo uliowekwa juu yake na kila mtu atubuye. Wote wanaomtegemea yeye, hukaa salama kabisa. Kristo ndiye "Basi heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, Jiwe walilolikataa waashi, Limekuwa jiwe kuu la pembeni. Tena, Jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha. Kwa maana hujikwaza kwa neno lile, wasiliamini, nao waliwekwa kusudi wapate hayo" 1 Petro 2:7, 8.

### Jinsi ya kujengeka baada ya kuvunjika

Kwa wale wanaomwamini, Kristo ni msingi ulio imara. Wameanguka mwambani na "wamevunjika". Kuanguka mwambani na kuvunjika, maana yake ni kuacha hali ya kujiona kuwa mwenye haki, ni kumwendea Kristo kwa unyenyekevu, kama mtoto na kutubu makosa yetu yote, na kuamini upendo wake wa msamaha. Kwa imani na utii hujenga juu ya Kristo, ambaye ni msingi imara.

Juu ya msingi huu ambao jiwe hai kuu la pembeni ni Yesu watu wote hujenga kwake, yaani Wayahudi na watu wa mataifa pia. Unawatosha wote, na kuchukua uzito wa ulimwengu wote. Wote wanaojiunga naye na kujenga juu ya msingi huu huwa mawe yaliyo hai. (Soma 1 Petro 2:5).

Kwa wale wanaojikwaa kwa neno, huasi. Kristo ni mwamba wa kujikwaa. Kama jiwe lililokataliwa, alichukua aibu zote. "Alidharauliwa na kukataliwa na watu, wala hakuhesabiwa kuwa ni kitu." (Soma Isaya 53:3.) Lakini kwa kulufuka kutoka kwa wafu alihesabiwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu. (Tazama Warumi 1:4.) Atakaporudi ataonekana kuwa Bwana wa mbingu na nchi, jiwe lililokataliwa na waashi, sasa ni jiwe kuu la pembeni, mfalme wa ulimwengu.

[336] Mtu ambaye ataangukiwa na jiwe hili atasangwasagwa. Waliomkataa Kristo, walishuhudia maangamizo ya mji wao na nchi yao. Utukufu wao ukatawanyika kama mavumbi. Mwamba ambao wangalijengea ungekuwa usalama wao. Zilikuwa ni rehema za Mungu zilizodharauliwa na wema uliodhihakiwa. Watu walijiweka wenyewe kuwa kinyume na Mungu, na yote yale yaliyokuwa yawe wokovu wao yakawa maangamizi yao.

Kusulubishwa kwa Kristo na Wayahudi kulichanganyikana na kuangamizwa Yerusalemu. Damu ya Yesu waliyomwaga ndiyo iliyokuwa uzito uliowazamisha kwa maangamizi.

Hivyo katika siku ya mwisho wakati hukumu ya Mungu itakapowakalia walioikataa neema ya Mungu, Kristo ataonekana kama mlima wakulipiza kisasi. Utukufu wake, ambao kwa watakatifu ni uzima, kwa waovu utakuwa ni moto wa kuteketeza. Kwa ajili ya upendo uliokataliwa, neema iliyodharauliwa, wenye dhambi wataangamizwa. Hekalu lililochafuliwa, mwana mkaidi, wakulima waovu, wajenzi wakorofi, wote hupata mfano katika njia ya kila mwenye dhambi. Asipotubu hukumu iliyowakabili itakuwa yake.

## 66 — Kristo Akabiliana na Adui Zake [337]

Makuhani na wazee hawakuweza kukanusha madai ya Kristo, ila tu walinuia kumtega. Walimtumia mijasusi "waliojifanya kuwa waaminifu kwake, ili wapate kumka-mata katika maneno yake, na kumshitaki kwa watawala." Vijana hao wenye juhudi walifuatana na wafuasi wa Herode kusudi wasikie maneno yake wapate kumnasa na kumshitaki.

Mafarisayo waliudhiwa na kodi za Warumi wakidai kuwa kulipa kodi ni kinyume cha sheria ya Mungu. Sasa majasusi walimjia Yesu wakijifanya wanataka kujua wajibu wao, wakisema: "Bwana, twajua kuwa wewe hufundisha ukweli mtupu, wala hujali cheo cha mtu, ila hufundisha sheria ya Mungu tu: Je, ni halali kumlipa Kaisari kodi kwa Kaisari?"

Wale waliomwuliza Yesu swali hilo walidhani kuwa wameficha kusudi lao, lakini Yesu alisoma nia yao kana kwamba ni kitabu. Akasema: "Mbona mnanijaribu?" Alisema hayo kuonyesha kuwa anafahamu nia yao. Walikuwa bado wangali katika mtataniko, aliposema: "Nionyesheni dinari." Walimletea. Naye aliwauliza: "Sanamu hii ni ya nani?" Wakasema, "Ni ya Kaisari." Yesu akisonda dinari hiyo alisema: "Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu."

Wapelelezi walijiona kuwa duni katika mtego wao na kushindwa. Ufasaha wa majibu ya maswali yao uliwafanya wasiwe na la kusema zaidi. Majibu ya Kristo hayakuwa ya kupiga chenga, bali majibu adilifu kwa maswali yao. Akishikilia dinari ya Kirumi mkononi aliwaambia kuwa kwa kuwa wanaishi chini ya ulinzi wa Warumi, ni haki kabisa kulipa kodi kwao. Lakini wakiwa chini ya sheria ya Warumi lazima utii wao kwanza uwe kwa Mungu.

Kama Wayahudi kwa uaminifu wangalitimiza wajibu wao kwa [338]
Mungu, wasingalitawaliwa na watu wa mataifa mengine. Bendera ya Warumi isingalipepea katika Yerusalemu; wala mtawala wa Kirumi asingelitawala humo.

Mafarisayo walishangazwa na majibu ya Yesu. Hakuwakemea tu bali alieleza kanuni zinazohusu wajibu wa watu kwa Mungu wao na wajibu wao kwa serikali inayotawala. Ingawa wengi hawakuridhika, lakini waliona kanuni ilivyo kwa majibu ya maswaii yao. Walishangazwa kwa uwezo wa Kristo kwa kujibu.

Haukupita muda mara baada ya Mafarisayo kunyamazishwa Masadukayo nao wakajitokeza na maswali ya ujanja. Ingawa hawakumwamini Kristo kwa ujumla, lakini baadhi yao walikuwako waaminifu katika mafundisho ya Kristo. Masadukayo walikiri kuwa Wanaamini sehemu kubwa ya Maandiko Matakatifu, lakini kimaisha walikuwa wenye mashaka na wapenda utajiri.

### Ufufuo wa wafu, fundisho lenye utata

Baina ya Mafarisayo na Masadukayo, fundisho la ufufuo wa wafu lilikuwa jambo la utata mkubwa. Mafari-sayo waliamini kabisa fundisho la ufufuo wa wafu, lakini fikara zao kuhusu hali ya baadaye ya wafu zilikuwa na kasoro. Mauti ilikuwa siri isiyoelezeka. Mabishano baina ya makundi hayo mawili yalizusha ubishi wenye hasira.

Watu wa kawaida hawakuvutiwa na Masadukayo. Lakini wengi wa Masadukayo walikuwa na mvuto uletwao na utajiri wa mali. Katika hao ndio alichaguliwa kuhani mkuu. Kule kustahili kushika wadhifa huo kulitoa mvuto kwa mafundisho yao yenye makosa.

Masadukayo waliyakataa mafundisho ya Yesu; mafundisho yake kuhusu maisha ya baadaye yalikuwa kinyume na dhana zao. Waliamini kuwa baada ya kuumbwa na Mungu mwanadamu aliachwa tu ajitawale. Walichukulia kuwa mwanadamu alikuwa huru kumudu mambo yake duniani, na hali yake ya baadaye imo mikononi mwake.

### Mawazo ya Mungu yakalibisha tabia

Mawazo yao kuhusu Mungu ndiyo yaliyokalibisha tabia zao. Kwa kuwa hawakuona kuwa Mungu hushugulika na watu, hata wao hawakushughulika kuhusu mtu na mtu. Wakikataa mvuto wa Roho Mtakatifu, walipungukiwa na nguvu zake katika kuongoza maisha yao. Walijivunia tu kuwa wao ni wa uzao wa Ibrahim, lakini

hawakuwa na imani yake. Hawakuhangaika kuwafikiria wengine, ila waliishi maisha ya ubinafsi. Katika maneno na kazi zake Kristo [339] alishuhudia uwezo wa Mungu wa kushughulikia watu kwa maisha ya baadaye, Mungu kama Baba wa watu wote. Akiwatunza kwa kila hali. Alifundisha kuwa Mungu huwavuvia watu kwa Roho wake Mtakatifu. Alionyesha makosa ya kutegemea uwezo wa mwanadamu kuleta mabadiliko ya tabia, ambayo ni kazi ya Roho wa Mungu.

Katika kutafuta majadiliano na Yesu Masadukayo walitumaini kumletea sifa mbaya, kama si kumlaumu. Walichagua kumwuliza swali kuhusu ufufuo wa wafu. Kama akikubaliana nao, atawaletea Mafarisayo machukizo. Lakini asipokubaliana nao, watayahesabu mafundisho yake kuwa ya ovyo. Masadukayo walidhani kuwa ikiwa mwili wa marehemu huwa katika hali yake ya kutokufa katika hali ile ile ya mtu hai, basi uwe na nyama na damu na uendelee katika umilele na hali ile iliyokatishwa katika ulimwengu huu. Mume na mke wataungana tena, na kutimiliza ndoa mambo yao yataendelea kama yalivyokuwa kabla ya mauti.

Katika kuwajibu Yesu alifunua pazia ili waone mambo ya mbele. Alisema: "Kwa maana katika kiyama hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika mbinguni." Mathayo 22:30. Masadukayo walikuwa na makosa. Alisema: "Hamjui Maandiko, wala uwezo wa Mungu." Hakusema kuwa ni wanafiki, ila wanakosea katika imani yao.

Alisema kuwa kutojua kwao Maandiko, pamoja na kutojua uwezo wa Mungu ndizo sababu za kutatanika katika imani na kuchanganyikiwa kwao. Kristo aliwataka wafungue mioyo yao na kusoma Maandiko yatakayopanua hali yao finyu na kupanua kuelewa kwao. Watu wengi huwa makafiri kwa sababu hawawezi kufahamu siri na uwezo wa Mungu. Ufunguo pekee kwetu kwa siri zinazotuzunguka ni kuukiri kuweko na uwezo wa Mungu. Watu lazima wamtambue Mungu kuwa ni Mwumbaji wa ulimwengu. Anayeamuru kutendeka vitu vyote.

Kristo aliwatangazia wasikilizaji wake kwamba, kama pasingekuwako na ufufuo wa wafu, Maandiko wanayosema kuwa wanayafuata yasingalikuwa na maana yo yote. Akasema: "Lakini kuhusu wafu, hamkusoma alivyosema Mungu wenu: Mimi ni Mungu wa Ibrahim, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo?

Mungu si Mungu wa wafu, bali wa walio hai. Mungu huona kazi yake kana kwamba imekamilika. Wafu wenye thamani wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu nao watatoka makaburini wapate uzima wa milele. Hapo patakuwa na uhusiano wa karibu sana baina ya
[340] Mungu na wafu watakatifu waliofufuka. Yeye huchukulia uhusiano kana kwamba tayari upo sasa. Wafu huishi katika yeye.

Masadukayo walinyamazishwa. Hakuna neno lililonenwa ambalo lingetumiwa kumshutumu. Hata hivyo Mafarisayo hawakukata tamaa. Walimwomba Mwandishi fulani amwulize maswali, kuhusu amri kuu katika amri kumi za Mungu ni ipi. Walikuwa wakizitukuza amri nne za kwanza zinazoeleza wajibu wa mtu kwa Mungu kuwa ndizo kuu zaidi. Kuliko zile sita zilizohusu wajibu wa mtu kwa mwanadamu mwenzake lakini Yesu alikuwa ameshutumiwa kwa kuziwekea uzito zile amri sita za mwisho zinazoeleza wajibu wa mtu kwa mwenzake dhidi ya zile nne.

Mwandishi aliamka na swali: "Ni amri gani iliyo kuu kuliko zote?" Jibu la Kristo lilikuwa wazi. Kwamba, "Amri ya kwanza mpende Bwana Mungu kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nia yako yote, na kwa nguvu zako zote". Ya pilli hufanana nayo, nayo ni hii: "Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hukaa amri zote na manabii."

Amri hizi zote huonyesha kanuni ya upendo. Amri ya kwanza haiwezi kushikwa na ya pili kuvunjwa, wala ya pili kushikwa na ya kwanza kuvunjwa. Na pale tu tumpendavyo Mungu kadiri iwezekanavyo, ndivyo itakavyowezekana kumpenda jirani bila upendeleo.

Kristo aliwafundisha wasikilizaji wake kuwa amri za Mungu ni za muhimu zote, wala hazitengani. Hakuna ya muhimu kuliko nyingine. Kumpenda Mungu kutadhihirika katika kuzishika amri zake zote.

Mwanasheria aliyemuuliza Yesu swali hilo alishangaa. Mbele ya makuhani na wazee alikiri kwa dhati kuwa Yesu alikuwa amefafanua sheria kweli kabisa.

Yule mwandishi alikuwa anaelewa kutofaa kitu kwa ibada na sadaka za kuteketeza na umwagaji wa damu katika upatanisho wa dhambi. Kumpenda Mungu na kumtii na kumheshimu mwanadamu bila kuwa na ubinafsi, vilionekana kwake vya maana kuliko kufuata mapokeo haya ya bure. Majibu yake ya kweli yalikuwa tofauti

kuliko ya makuhani na wazee. Yesu alimhurumia mwandishi huyu aliyethubutu kumkiri Kristo wazi hivyo. Yesu akamwambia: "Hu mbali na ufalme wa Mungu."

Mafarisayo walikuwa wamemzunguka Yesu alipokuwa akimjibu mwandishi. Sasa aliwauliza: "Mnadhani Kristo ni nani? Ni mwana wa nani?" Swali hili ni la kujua wanavyomdhania, kuwa ni binadamu tu au kama Mwana wa Mungu. Walijibu: "Mwana wa Daudi." Yesu alipodhihirisha Uungu wake kwa njia ya miujiza, alipowaponya wag- [341]
onjwa na kuwafufua wafu, watu walikuwa wanajiuliza, "Huyu siye mwana wa Daudi." Lakini wengi waliomwita Yesu kuwa Mwana wa Daudi hawakuutambua Uungu wake, Mwana wa Daudi alikuwa pia Mwana wa Mungu.

Katika kujibu Yesu akasema: "Daudi mwenyewe alisema kwa uweza wa Roho Mtakatifu; "Bwana alimwambia Bwana wangu; Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako kuwa chini ya miguu yako.

Ikiwa Daudi basi alimwita Bwana, anakuwaje tena mwana wake? Hakuna mtu aliyeweza kumjibu neno, wala hakuna mtu aliyethubutu kumwuuliza swali tena."

[342] 
## 67 — Yesu Azuru Hekalu Mara ya Mwisho

Ilikuwa siku ya mwisho ya Yesu kufundisha hekaluni. Kijana wa Kigalilaya alisimama, akiwa hali ya kawaida tu. Akizungukwa na makuhani wenye hali ya kitajiri sana, na wakuu wenye mavazi ya fahari sana na mapambo ya kila hali, na Waandishi wakishikilia mkononi mwao magombo waliyoyafunua kila mara. Yesu alisimama kimya kama mwenye kuvikwa uwezo wa kimbingu. Aliwakodolea macho adui zake, waliokuwa na uchu wa uhai wake. Mitego yao ya kutaka kumnasa ikiwa imeshindwa. Alikuwa amekutana na maswali mbali mbali, akitoa majibu safi ya hakika, kinyume cha giza la makosa ya Mafarisayo na Makuhani. Maonyo yalitolewa kwa uaminifu. Walakini ilibakia kazi nyingine kwa Kristo, kufanya.

Watu walikuwa wamefurahishwa na mafundisho yake, ingawa walikuwa na wasiwasi. Walikuwa wakiwatumaini Makuhani na Waalimu, lakini sasa wanawaona watu hawa wakimwinda Yesu, kumdhalilisha ambaye maarifa yake yalitoa nuru ya kila shambulio. Walishangaa kwa kuwa Makuhani na Marabi hawakumwamini Yesu, ambaye mafundisho yake yalikuwa dhahiri na rahisi kueleweka. Wao wenyewe hawakujua njia ya wima ya kufuata.

Katika mifano, lilikuwa kusudi la Kristo kuwaonya wakuu na kuwafundisha watu ukweli. Lakini ilikuwa ni lazima kusema kwa wazi zaidi. Kutokana na imani yao duni kwa ukuhani, uliopotoshwa, watu walikuwa wametekwa. Kristo lazima akate minyororo hii. Alisema: "Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti cha Musa, basi yo yote watakayowaambieni myashike na kuyatenda, lakini msiwaige jinsi wanavyokuwa, maana kwao hunena tu, wala hawatendi hivyo wanavyonena."

Waandishi na Mafarisayo waliamua kukichukua kiti cha Musa,
[343] wakiwa kama ndio wenye kufundisha sheria, lakini hawakufanya kama sheria isemavyo. Na walifundisha mengi yaliyo kinyume cha Maandiko Matakatifu. Wao hufunga Mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitende wenyewe kugusa kwa kidole chao.

Hufundisha sheria, na kuwalazimisha watu wazishike, wao hujidai kusamehewa wasitenda hivyo.

"Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu; kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao; hupenda viti vya mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masinagogi, na kusalimiwa masokoni, na kuitwa na watu Rabi. Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoia, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo."

Katika maneno ya wazi kama hayo Mwokozi alidhihirisha tamaa ya ubinafsi iliyokuwa inajikweza kutaka makuu kila mahala, huku ikionyesha kejeli ya unyofu, na huku moyo umejaa wivu na choyo. Mafarisayo walikuwa wakitafuta kwa kila hali kujionyesha na kujipendelea. Mambo kama hayo yalikemewa na Yesu.

Alikemea ubatili uliyoonyeshwa katika kutamani kuitwa Rabi, au Bwana. Makuhani, Waandishi na Wazee, wote walikuwa ni ndugu, watoto wa Baba mmoja. Watu hawakupaswa kumpa mtu ye yote heshima ya kuwafanya watawaliwe nia zao, au imani yao.

Kama Kristo angelikuwako ulimwenguni leo, akizungukwa na watu wenye majina ya heshima kama vile Mstahiki (Reverend), au Mstahiki Sana (Right Reverend), je, asingaliurudia usemi wake kwamba Msiitwe bwana, kwa kuwa mnaye Bwana mmoja ndiye Kristo?" Maandiko Matakatifu humtaja Mungu kuwa, jina lake ni Takatifu na la kuogopwa." (Zaburi 119:9). Watu wangapi hujiita kwa jina hilo linalomhusu Mungu na huku wakiwakilisha vibaya jina na tabia yake. Mara ngapi tamaa za kidunia na dhambi mbaya kabisa zimefichwa ndani ya vazi la cheo cha juu na kitakatifu!

Mwokozi aliendelea kusema: "Atakaye kuwa mkubwa wenu, atakuwa mtumishi wenu. Atakaye-jikuza atashushwa, na atakayejidhili atakuzwa." Kristo alifundisha mara nyingi kwamba, ukuu wa kweli hupimwa katika hali ya unyofu. Mbele ya mbingu ukuu halisi hupimwa kwa jinsi mtu anavyowahudumia wanadamu wenzake. Kristo ambaye ni Mfalme wa utukufu alikuwa mtumishi wa wanadamu wenye dhambi.

"Mnawafungia watu wasiingie katika ufalme wa mbinguni, ninyi [344]
wenyewe hamwingii, na wanaotaka kuingia mnawazuia." Kwa njia

ya kuyapotosha Maandiko Matakatifu makuhani na wanasheria walizuia watu wasielewe njia ya kuingia katika ufalme wa mbinguni.

"Mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki mnaomba sala ndefu; kwa hiyo mtapokea hukumu iliyo kubwa zaidi." Mafarisayo walipata heshima ya wajane watauwa, na walifanya kuwa ni kawaida yao kuchukua vitu vyao kwa ajili ya makusudi ya dini. Baada ya kupata fedha zao walizitumia kwa faida yao. Ili kujificha na upotovu wao waliomba sala ndefu sana na kujionyesha kuwa ni watu wa dini kamili. Makaripio ya aina hiyo yanawahusu watu wa sasa pia. Maisha yao yamejaa ubinafsi na uovu, walakini hujifunika na vazi la dini, waonekane kana kwamba ni wenye dini halisi.

### Sadaka isiyo na Kifani ya Mjane Maskini

Kristo aliwakaripia wenye kuharibu mali, lakini alikuwa mwangalifu kwa watu wanaotmiza wajibu wao kuhusu kutumia mali. Matumizi mabaya ya matoleo ya Mungu yasingelizuia mibaraka ya Mungu kutoka kwa mtoaji.

Yesu alikuwa ukumbini, akiwatazama waliokuwa wakitoa sadaka zao. Matajiri walileta fedha nyingi kwa majivuno. Yesu aliwatazama kwa masikitiko ila hakusema neno kuhusu sadaka zao kubwa. Mara moja uso wake uling'aa alipomwona mjane mmoja maskini akija kwa kusitasita kana kwamba anawaogopa watoaji.

Aliangalia sadaka yake katika mikono yake. Ilikuwa ndogo sana kulinganisha na sadaka za wengine, walakini ilikuwa ndiyo yote aliyo nayo. Aliweka vipande viwili vya fedha kwa haraka, akaondoka. Alipofanya hivyo alikutanisha macho na Yesu aliyekuwa akimwangalia kwa makini.

Mwokozi aliwataka wanafunzi wake wamwangalie mjane huyu maskini. Kisha maneno yake ya sifa yakasikika masikioni mwa yule mjane. "Hakika nawaambia huyu mjane maskini: ametia zaidi kuliko wote." Machozi ya furaha yakamlengalenga, alipofahamu kuwa sadaka yake imekubalika. Watu wengi wangalimshauri kuwa aache kutoa, atumie tu maana isingelitambulikana miongoni mwa sadaka nyingi za thamani kubwa zilizoletwa katika hazina. Lakini aliamini kuwa huduma ya hekaluni imeamuriwa na Mungu, naye alitaka kuisaidia huduma hiyo kwa kadiri awezavyo. Alitenda alivyoweza, na sadaka yake ilikuwa ukumbusho wakati wote, na furaha

yake ya milele. “Ametia zaidi kuliko wote.” Sadaka kubwa ya matajiri haikuwa ya kujinyima, kwa hiyo haikuweza kuhesabika kwa thamani kama ile ya mjane maskini. [345]

Nia huongoza matendo yetu, ikiyafanya yawe mazuri au yawe mabaya. Matendo madogo yatendwayo kwa furaha, na sadaka zitolewazo bila majivuno, huwa ya thamani mbele za Mungu. Mjane maskini alijinyima chakula chake ili kutoa senti mbili hizo kwa kazi aliyoipenda sana. Alifanya hivyo kwa imani, akiamini kuwa Baba wa mbinguni hawezi kumnyima riziki yake. Huduma hii isiyokuwa ya ubinafsi, na imani kama ya mtoto mdogo, ilisifiwa na Mwokozi.

Watu wengi miongoni mwa katika maskini hutamani kuonyesha shukrani zao kwa Mungu kwa ajili ya neema yake na kweli yake. Watu kama hao hebu na wakusanye senti zao chache na kuziweka katika hazina ya mbinguni. Ikiwa watazitoa kwa moyo mkunjufu, uliyojaa upendo wa Munngu, vitu vidogo hivi vikitolewa sadaka, Mungu huvifurahia na kuvibariki.

Yesu aliposema kwa mjane yule kuwa, “Ametia zaidi kuliko wote”, maneno yake yalikuwa ya kweli, siyo kwa nia tu, bali pia kwa matokeo ya sadaka yake. Zile senti mbili hizo zilizoletwa hazinani, zilizidi matoleo ya Wayahudi matajiri. Sadaka ndogo hiyo imekuwa kijito kilicho panuka na kuzidi kima kwa karne zote. Kwa njia elfu elfu mbali mbali imekuwa msaada kwa wenye dhiki, na kuitegemeza injili. Kielelezo chake cha kutoa kwa kujinyima kimeigwa katika nchi zote na watu maelfu katika kila karne. Mbaraka wa Mungu kwa sadaka ile ya mjane umeifanya kuwa na matokeo makubwa sana. Ndiyo ilivyo na kwa sadaka zote zitolewazo kwa utukufu wa Mungu. Matokeo yake hayahesabiki na mwanadamu

“Ole wenu Waandishi na Mafarisayo, wanafiki, kwa kuwa maana mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani adili na rehema na imani, hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.” Yesu hakuacha kuhimiza mambo ya lazima. Kulipa zaka kuliamuriwa na Mungu nako kulitekelezwa tangu mwanzoni. Ibrahimu alilipa zaka katika mali zake zote. Mpango wa kulipa zaka jinsi Mungu alivyouweka ulikuwa safi na wa haki, lakini Makuhani na Walimu walikuwa wameufanya kuwa mzigo wa kusumbua.

Mafarisayo walikuwa wakilipa zaka kamili ya mazao ya bustani zao, kama bizari, jira na mboga. Vitu hivyo viligharimu kidogo

sana, na hivyo kuwapa sifa kwamba ni waaminifu kweli kweli.
[346] Lakini mambo makuu ya sheria, kama vile adili, rehema, na ukweli waliyaacha. Kristo alisema: "hayo imewapa kuyafanya wala yale mengine msiyaache."

Mambo mengine ya sheria yalikuwa yamepotoshwa kwa jinsi hiyo na Walimu. Maagizo aliyoagizwa Musa, kama kula nyama ya nguruwe, na wanyama wengineo waliokatazwa yalitolewa ili kuepukana na maradhi na hivyo kufupisha maisha. Lakini Mafarisayo walipita kiasi. Watu waliambiwa wachuje maji yote yasije yakawa na wadudu, ambao wangehesabiwa sawa na wanyama wachafu. Yesu akilinganisha haya mambo madogo madogo na dhambi zenyewe hasa aliwaambia Mafarisayo "Viongozi vipofu, wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia."

"Mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote." Makaburi meupe yaliyopambwa yalificha maozea yaliyomo ndani yao. Ndivyo ilivyokuwa kwa makuhani na wazee waliokuwa wakionekana kwa nje kama wanyofu, walificha uovu ndani yao.

Yesu aliendelea kusema: "Mnayajenga makaburi ya manabii, na kuyapamba maziara ya wenye haki, na kusema: Kama sisi tungalikuwepo zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika (kumwaga) damu ya manabii". Hivyo mwajishuhudia wenyewe kuwa ninyi ni wana wa wale waliowaua manabii".

Ushirikina wa kuheshimu makaburi ya watakatifu ulidumishwa na fedha nyingi zilitumika katika kuyapamba. Machoni pa Mungu hii ilikuwa ni ibada ya sanamu. Ilionyesha kuwa hawakumpcnda Mungu hata kidogo, wala jirani zao kama nafsi zao. Leo watu wengi hawawajali wajane, na yatima, wagonjwa na maskini, ili kutoa gharama ya kujenga minara ya kumbukumbu kwa ajili ya watu. Wajibu kwa waliohai,wajibu ambao Kristo ameuagiza kwa dhati umeachwa bila kutendeka.

Mafarisayo walisema wao kwa wao: Kama sisi tungaliishi siku za baba zetu, tusingalishirikiana nao kumwaga damu za watumishi wa Mungu. Lakini wakati ule ule walikuwa wakipanga kumwua Mwana wa Mungu. Jambo hili linapasa kumfunua macho yetu tuone jinsi Shetani anavyowadanganya watu na kuwatoa katika njia ya kweli. Wengi hushangaa kwa upofu wa Wayahudi wa kumkataa

Kristo. Husema: Kama sisi tungaliishi siku hizo za Kristo, tusingelishiriki katika hatia ya wale waliomkataa Mwokozi, lakini watu hawa wanapotakiwa kumtii Mungu na kuishi maisha yasiyokuwa [347] ya ubinafsi, hukataa kufanya hivyo. Hudhihirisha roho ile ile ya Mafarisayo.

Wayahudi hawakutambua hata kidogo matokeo ya kutisha ya kumkataa Kristo. Katika kila kizazi manabii walipaza sauti zao kuwaonya watawala, wakuu, na watu, na hivyo wakihatarisha maisha yao katika kumtii Mungu. Kumekuwako na kurundikana kwa adhabu ya kufisha wale walioikataa nuru na kweli. Kwa kunikataa kwao Mwokozi makuhani na watawala walijihusisha na damu ya watakatifu wote kutoka Habili mpaka hadi Yesu mwenyewe. Wayahudi walikuwa karibu kukijaza kikombe chao cha uovu. Na karibu kitamwagwa vichwani mwao katika kulipiza haki. Kwa ajili ya hayo Yesu aliwaonya akisema: "hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habili, yule mwenye haki hata damu ya Zakaria na bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu Amini nawaambieni, Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki."

Waandishi na Mafarisayo walijua jinsi nabii Zakaria alivyouawa. Wakati alipokuwa akinena onyo kutoka kwa Mungu, ghadhabu ya kishetani ilimchochoea mfalme mwovu na kwa amri yake nabii akauwawa. (Tazama 2 Nyakati 24:18-22). Damu yake ilikuwa imejigandisha katika mawe ya hekalu, na kuwa ushuhuda wa uasi wa Israeli. Kadiri hekalu litakavyodumu kuwako, doa la damu hiyo itakuwa ikilia mbele za Mungu ili ilipiziwe kisasi. Yesu alipozighusia dhambi hizi, hofu kuu iliwajaza watu.

Yesu alipoona ugumu wa mioyo ya Wayahudi, alisema kuwa hali yao ya ngumu wa moyo itakuwa sawa kama ilivyokuwa wakati uliopita.

"Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii, na wenye hekima, na Waandishi: na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulubisha; na wengine wao mtawapiga masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji. "Yesu alitamka maneno haya ya adhabu hali mikono yake ikiwa imeinuliwa mbinguni, na nuru ya Uungu ikimfunika, Kristo alinena hayo kama jaji katika kukemea na hukumu. Wasikilizaji wake walitetemeka sana. Hali ya mvuto na maneno yake ilikuwa nanma isiyoweza kufutika kabisa.

Chuki ya Kristo hasa iliekezwa kwa dhambi zinazotendwa na watu wakijiharibu wenyewe, na kuwadanganya wengine na kumdharau Mungu. Lakini hakunena maneno ya kulipiza kisasi. Hakudhihirisha hasira yo yote. Huruma ya kimbingu ilionekana usoni pa Mwana wa Mungu, alipolitazama mara moja hekalu na kisha
[348] wasikilizaji wake. Kwa sauti iliyojawa na huzuni na majonzi mazito alitamka, "'Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! ni mara ngapi nimetaka kuwa kusanya Pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabaya yake, lakini hamkutaka." Katika maombolezo ya Kristo, moyo wa Mungu uliguswa. Hivyo ilikuwa kwaheri ya kisirisiri ya uvumilivu wa. upendo wa Mungu.

Mafarisayo na Masadukayo walinyamazishwa kimya. Yesu aliwakusanya wanafunzi wake wakatoka hekaluni, akiwa siyo kama mtu aliyeshindwa, bali kama ambaye ametimiza kazi yake. Aliondoka akiwa mshindi kutoka katika pambano.

Katika siku hiyo yaajabu, katika mioyo mingi mawazo mapya yalichipuka, na, historia mpya ikaanza. Baada ya kusulubishwa na kufufuka, watu hawa walijitokeza mbele wakiwa na hekima na bidii. Walikuwa na ujurnbe uliowavutia watu. Mbele ya ushuhuda wao dhana na falsafa za wanadamu zilikuwa hadithi za kubuni.

Lakini Israeli kama taifa lilikuwa limejitenga kutoka kwa Mungu. Akiangalia ndani ya hekalu kwa mara ya mwisho, Yesu alisema kwa huruma na kuomboleza! "Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. Kwa maana nawambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana." Kama vile Mwana wa Mungu alivyozitoka zile kuta, Utukufu wa kuweko Mungu utaondolewa milele kutoka, katika hekalu lililojengwa kwa ajili ya utukufu wake. Tamasha zake hazitakuwa na maana, huduma zake zitakuwa dhihaka.

## 68 — Wayunani Walipotaka “Kumwona Yesu” [349]

“Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwenda kuabudu kwenye sikukuu. Basi hao walimwendea Filipo, wakamwomba wakisema Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu. “Andrea na Filipo wakamwambia Yesu.”

Kwa wakati huu kazi ya Kristo ilionekana kana kwamba itashindikana. Alikuwa ameshinda katika majadiliano na Mafarisayo na Makuhani, lakini ilikuwa dhahiri kuwa hangepokelewa, nao kama Masihi. Utengano wa mwisho ulikuwa umefikiwa. Ilionekana hakuna tumaini. Lakini jambo kubwa la kuhusu ulimwengu mzima lilikuwa karibu kutokea. Kristo aliposikia kwa hamu kwamba kuna watu “wanaotaka kumwona, Yesu” wakiwakilisha kilio cha ulimwengu, uso wake uling’aa kwa furaha, akasema: “Saa imefika, atukuzwe Mwana wa Adamu.”

Watu hawa walikuja kutoka Magharibi ili kumwona Mwokozi katika saa ya mwisho ya maisha yake. Mamajusi walikuja panapo mwanzo kutoka Mashariki. Wayunani hawa waliwakilisha mataifa, makabila na watu wa alimwengu mzima. Watu wa nchi zote na wa vizazi vyote watavutwa na msalaba wa Mwokozi.

Wayunani hao walitamani kujua ukweli kuhusu kazi ya Kristo. Wakati waliposema: “Tunataka kumwona Yesu,” Alikuwamo hekaluni, sehemu ile ambamo watu wengine wote isipokuwa Wayahudi hawakuruhusiwa, lakini Yesu aliwaendea Wayunani huko katika ukumbi wa nje akaongea nao binafsi.

Haja ya Wayunani ilimwonyesha Kristo kuwa dhabihu aliyekuwa anataka kutoa itawaleta wengi kuwa wana na binti za Mungu. Alifahamu kuwa muda si kitambo Wayunani watamwona wakiwa katika hali ambayo hawakudhania. Watamwona akiwekwa [350]
pamoja na Baraba, mnyang’anyi na muuaji. Kwa swali, “Basi, nimtendeeje Yesu?” Jibu litakuwa “Asulibishwe.”(Mathayo 27:22. Kristo alijua kuwa kwa kufanya, upatanisho ufalme wake utakamilika na kuenea katika ulimwenguni kote. Atakuwa Mtengenezaji, na Roho wake atashinda.

Kwa muda kitambo alisikia sauti zikitangaza katika sehemu zote za dunia "Tazama Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Katika wageni hawa aliona ahadi ya mavuno makubwa. Tegemeo la haya, utimilivu wa tumaini lake ulionekana katika maneno haya; "Saa imefika, atukuzwe Mwana wa Adamu." Lakini njia ya kufikia kutukuzwa huku haikuwa kujificha mawazoni mwa Kristo. Kwa kifo chake peke yake ndipo ulimwengu ungeokolewa. Kama punje ya ngano, Mwana wa Adamu hana budi kufukiwa ardhini afe na kuzikwa asionekane; lakini yapasa aishi tena.

"Amini, amin nawaambia chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa hutoa mazao mengi." Chembe ya ngano inapoanguka chini na kufa, huchipua na kuzaa mazao. Hivyo ndivyo na kifo cha Kristo kitazaa matunda mengi katika ufalme wa Mungu. Kufuatana na kawaida ya asili ya mbegu za mboga uhai ulikuwa uwe matokeo ya kufa kwake.

Mwaka hadi mwaka mwanadamu huhifadhi pato la mbegu zake kwa kuzimwaga chini mbegu bora. Kwa muda lazima zifunikwe ardhini kuangaliwa na Bwana. Kisha huonekana jani, halafu mche, kisha mmea kamili ndipo chembe.

Mbegu iliyofunikwa udongoni huzaa tunda, halafu tunda nalo hupandwa, na hivyo mavuno huongezeka. Ndivyo hivyo na kifo cha Kristo msalabani, kitazaa matunda ya uzima wa milele. Kuitafakari kafara hii utakuwa utukufu kwa wale ambao kama tunda lake wataishi milele zote.

Kristo angeweza kujiokoa na kifo kama angechagua. Lakini kufanya hivyo angalibakia mwenyewe. Kwa kuanguka ndani ya udongo ili kufa ndiko kungeweza kuzaa matunda, yaani kuokoa watu wengi na kuwaingiza katika ufalme wa Mungu.

Fundisho hili la kujitoa kafara lazima lifunzwe kwa wote. "Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele." Maisha lazima yazikwe katika mfereji wa haja za ulimwengu. Kujipenda nafsi,
[351] upendo wa nafsi lazima vipotee. Kanuni ya kujitoa ndiyo kanuni ya uzima. Kutoa ni kuishi. Maisha yatakayohifadhiwa ni yale yanayotumika katika kazi ya Mungu na kumhudumia mwanadamu.

Maisha yanayotumikia nafsi ni kama mbegu iliyoliwa. Hakuna ongezeko. Mtu anaweza kukusanya vitu vyote awezavyo; anaweza

kuishi na kufikiri, na kujipangia awezavyo; lakini maisha yake hutoweka na wala hana kitu cho chote. Maisha ya ubinafsi ni maisha ya kujiangamiza.

Yesu anasema: "Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu." Wale wote waliochukua msalaba wa kujikana pamoja na Yesu, watakuwa washiriki utukufu pamoja Naye. Wao ni watenda kazi pamoja na Kristo, na Baba atawaheshimu jinsi anavyomheshimu , Mwanaye.

Ujumbe wa Wayunani ulileta mawazoni mwa Yesu kazi ya ukombozi tangu ilivyopangwa mbinguni, hadi kifo ambacho sasa kilikuwa kinakaribia sasa. Wingu la siri lilionekana kumfunika Mwana wa Mungu. Alishikwa na mawazo mengi. Baadaye ukimya ukaondolewa kwa sauti ya kilio. "Sasa roho yangu imefadhaika nami nisemeje Baba, uniokoe katika saa hii? Ubinadamu wake Kristo ulijikunyata kutoka katika saa ya kuachwa, wakati ambapo wote watamwona akipigwa na kuteswa. Alijikunyata kutoka katika hali ya kutendewa kama mhalifu mkuu wa wote, kutoka katika mauti ya fedheha. Mzigo mkubwa wa makosa ya walimwengu na ghadhabu ya Baba kwa sababu ya dhambi za ulimwengu vilisababisha roho ya Yesu kuzimia, na hofu ya mauti kuutanda uso wake.

## Sauti ya Mungu Ilisikika

Ndipo ukaja utukufu wa uungu katika mapenzi ya Babaye, Akasema, "Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii. Baba, ulitukuze jina lako." Ni kwa kifo cha Kristo tu, ndio utawala wa Shetani ungeangushwa, mwanadamu akombolewe na Mungu atukuzwe. Yesu aliikubali dhabihu, akakubali kuteseka kama Mchukua Dhambi. Sauti ikatoka ndani ya wingu liliotanda juu ya kichwa chake; "Nimelitukuza nami nitalitukuza tena." Katika mateso ya kiungu kibinadamu yajayo Kristo, atalitukuza jina la Baba yake. Sauti iliposikika nuru ilimzunguka Kristo, kana kwamba mkono wa nguvu za Uungu uliomzungushia ukuta wa moto. Hakuna mtu aliyethubutu kusema kitu. Wote walisimama wakimwangalia Yesu. Ushuhuda wa Baba ukiwa umetolewa, wingu liliinuka na kutawanyika hewani. [352]

Wayunani waliokuwa wamekuja kumwulizia waliliona wimgu, wakaelewa maana yake na kumtambua

Kristo, hakika; kwao alidhihirishwa kama Aliyetumwa na Mungu. Sauti ya Mungu ilikuwa imesikika wakati wa Ubatizo wa Yesu, na wakati Yesu alipogeuka sura mlimani. Sasa kwa mara ya tatu ilisikika katika kundi la watu wengi. Yesu alikuwa ametoa wito wake mara ya mwisho, na kutamka maafa yatakayowapata Wayahudi. Na sasa Mungu anamtambua yule aliyekataliwa na Israeli. Yesu akasema: "Sauti hiyo haikuwako kwa ajili, yangu, bali kwa ajili yenu. " Ilikuwa ni ushuhuda kutoka kwa Mungu kwamba Yesu alikuwa amesema ukweli, na kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.

"Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa," Kristo aliendelea kusema, "mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje," "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu. Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa". Ikiwa mtakuwa kipatanisho kwa dhambi za wanadamu, ulimwengu utaangazwa. Uwezo wa Shetani kuwashikilia watu utavunjika. Sura ya Mungu iliyoharibiwa itarudishwa kwa wanadamu, na jamii ya wenye haki waaminio watayarithi makao ya mbinguni. Mwokozi aliuona msalaba, jinsi ulivyo wa ukatili na aibu yake pamoja taabu zake, ukiwaka kwa utukufu. Lakini ukombozi wa mwanadamu si yote yaliyomalizwa na msalaba. Upendo wa Mungu unadhihirishwa ulimwenguni. Doa lililotiwa mbinguni na Shetani linaondolewa kwa milele. Malaika na watu watavutwa kwa Kristo. "Nami nikiinuliwa juu ya nchi," Alisema "nitawavuta wote kwangu."

Watu wengi walikuwa wamemzunguka Kristo alipokuwa akisema maneno haya; "Walakini ajapokuwa amefanya ishara nyingi namna hiyo mbele yao, hawakumwamini."

Ishara zisizohesabika zilikuwa zimetolewa lakini watu walifumba macho yao na kufanya mioyo migumu. Kwa vile sasa Baba mwenyewe alikuwa amenena na hawakuwa na la zaidi kuuliza, bado walikataa kuamini.

"Walakini hata katika wakuu walikuwamo wengi waliomwamini; lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakumkiri, wasije wakatengwa na sinagogi". Katika kujikinga na fedheha na aibu walimkana Kristo na kukataa toleo la uzima wa milele. Ole kwa wale, ambao hawakutambua wakati wao uliowajilia! Taratibu na kwa huzuni Kristo aliondoka hekaluni milele.

## 69 — Dalili za Kuja Kwa Kristo Mara ya Pili [353]

Maneno ya Kristo kwa makuhani na wakuu “Angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa” (Mathayo 23:38), yaliwatiya hofu sana mioyoni. Swali likaendelea kuwa katika mawazo yao, kuhusu maana ya maneno hayo. Je, inawezekana hili hekalu kuu lililo tukufu wa taifa likabomolewa na kuwa maghofu?

Bashiri ya mabaya yatakayoujia Yerusalemu yalitafakariwa na wanafunzi wake pia. Walipokuwa wakitoka pamoja Naye hekaluni walimkumbusha juu ya uzuri wa hekalu na ngome yake. Mawe yaliyojengewa hekalu yalikuwa marumaru ya thamani kuu, na mengine makubwa mno. Sehemu moja ya ukuta ilistahimili shambulio la Nebukadneza, na majeshi yake. Jinsi mafundi walivyolijenga lilifanana kana kwamba mawe yote ni jiwe moja lililobandikwa hapo toka katika machimbo yake.

Mwonekano wake machoni pa Kristo ulikuwa mzuri sana, lakini alinena kwa huzuni, Naona hayo yote. Mnaonyesha kuta hizi kwamba ni ngome zisizoweza kubomolewa, lakini, sikilizeni: Siku zinakuja ambapo “halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.” Alipokuwa peke yake, Petro, Yohana, Yakobo na Andrea walimwendea, wakisema: “Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?” Mathayo 24:3. Yesu hakuwajibu kwa njia ya kutenganisha juu ya uharibifu wa Yerusalemu na siku kuu ya kurudi kwake. Alielezea akiyachanganya mambo yote mawili pamoja. Kama angaliwafunulia wanafunzi wake jinsi mambo yajayo yalivyo hasa, wasingaliweza kuyavumilia kuyasikia. Kwa huruma zake, alichanganya matukio hayo mawili, na kuwaacha wanafunzi wenyewe wachanganue maana yake wenyewe. Aliposema mambo kuhusu uharibifu wa Yerusalemu, maneno ya unabii wake yalikwenda mbele hadi siku kuu ile, Bwana [354]
atakapoondoka kuwaadhibu walimwengu kwa ajili ya maovu yao. Mazungumzo hayo yote yalitolewa, sio kwa wanafunzi peke yao, ila pia kwa watu wote watakaoishi katika nyakati za matukio ya historia ya mwisho wa ulimwengu.

Kristo akawaambia “Angalieni, mtu asiwadanganye. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watadanganya wengi”. Masihi wengi watatokea wakitangaza kuwa wakati wa, ukombozi wa taifa la Wayahudi umekaribia. Hawa watawapotosha watu wengi. Maneno ya Kristo yalitimia. Kati ya kifo cha Yesu na kuzingirwa kwa Yerusalemu masihi wengi walijitokeza. Udanganyifu wa jinsi hiyo utatokea tena.

“Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita, angalieni, msitishwe; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho wa taifa la Kiyahudi wenyewe bado. Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na njaa, na tauni, na matetemeko ya nchi mahali mahali. Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu”. Walimu watafundisha kwamba dalili hizo ni za kuja kwa Masihi. Msidanganyike; dalili watakazosema kuwa ni dalili za kukombolewa katoka utumwani zitakuwa ni za uharibifu wao.

“Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki nao watawauawa; nanyi mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu. Ndipo wengi watakapojikwaa nao watasalitiana, na kuchukiana.” Wakristo waliteseka katika hayo yote. Wakina Baba na wakina mama waliwasaliti watoto wao, watoto nao wazazi wao. Marafiki waliwapeleka rafiki zao katika baraza kuu la Sanhedrini. Watesaji waliwaua Stefano, Yakobo na Wakristo wengineo.

Kwa njia ya watumishi wake Mungu aliwapa, Wayahudi nafasi ya mwisho ya kutubu. Mungu alijidhihirisha mwenyewe kwa njia ya mashahidi wake katika kukamatwa na kuhukumiwa kwao; walakini ingawa ya hayo walihukumiwa kufa, na mahakimu. Kwa kuwaua hivyo Wayahudi walimsulubisha tena Mwana wa Mungu. Hali hiyo itarudiwa tena. Wakuu wataweka sheria ya kuondoa uhuru wa dini. Watadhani kuwa wanaweza kuilazimisha dhamiri ambayo ni Mungu pekee anayepaswa kuitawala Wataendelea na mipango hiyo mpaka watakapofikia ukingo wasioweza kuupita. Mungu ataingilia kati kwa ajili ya watu wake waaminifu wazishikao amri zake.

Mateso yatokeapo wengi hujikwaa na kuanguka wakikana imani
[355] ile waliyokuwa nayo zamani. Wale watakaoasi wakati wa mateso ili kujisalimisha nafsi: zao, watawashuhudia uongo na kuwasaliti ndugu zao. Kristo ametuonya kwa mambo hayo, tusishituzwe na hali ya ukatili usio kawaida wa wale watakaokataa kweli.

Kristo aliwaambia wanafunzi wake namna watakavyoepuka hatari itakayokuja juu ya Yerusalemu. "Lakini, hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia. Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani, na walio katikati yake wakimbilie nje, na walio katika mashamba wasiuingie." Onyo hili lilitolewa kusudi lizingatiwe miaka arobaini, baadaye wakati Yerusalemu utakapoharibiwa. Wakristo walikumbuka onyo hilo, na hakuna hata mmoja aliyeangamia mji ulipotekwa.

Kristo alisema: "Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya Sabato." Yeye aliyeifanya Sabato, hakuitangua. Sabato haikubatili-shwa au kufutwa na kifo chake. Miaka arobaini baada ya kusulibishwa kwake iliendelea kuwa takatifu.

### Karne za giza za mateso

Kutoka katika maangamizi ya Yerusalemu Kristo aliunganisha habari na historia inayomalizia mwisho wa ulimwengu, kurudi kwa Mwana wa Mungu katika nguvu na utukufu. Kati ya matukio mawili haya kutakuwa na karne nyingi za giza kuu, karne ambazo kanisa lake takumbwa na umwagaji wa damu, huzuni na mateso. Yesu alipitia matukio haya kwa muhtasari tu. "Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea nanma yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo".

Kwa muda zaidi ya miaka elfu moja wafuasi wa Kristo watapata mateso ambayo ulimwengu haujayaona. Mamilioni ya wafuasi wake waaminifu watauawa. Kama mkono wa Mungu usingalinyoshwa ili kuwalinda watu wake, wote wangalipotea kabisa.

Sasa, Bwana akazungumzia kurudi kwake kwa usemi wa wazi "Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule, msisadiki. Kwa maama watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele. Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki. Kwa maana kama vile umeme [356]
utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo ku-

takavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." Katika mikutano ya maelfu wanaodai kuongea na wafu, je hapasikiki wito wa, "Tazama, Kristo yumo nyumbani?" Haya ndiyo madai yanayofanywa na roho za mizimu. Lakini Kristo anasemaje? "Msisadiki"

## Ishara katika Mbingu

Mwokozi anatoa dalili za kurudi kwake, na kutaja wakati ambapo dalili za kwanza kati ya hizo zilakapoanza kutokea; "Lakini mara, baada ya dhiki ya siku zile, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka mbinguni, na nguvu za mbinguni zitatikisika; ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu walakapoombeleza; nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu".

Mwisho wa mateso makuu yaliyoendeshwa na upapa, Kristo alitamka, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake. Kukifuata nyota kuanguka mbinguni. Na anasema; "Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni." Mathayo 24:33. Kristo anasema kwa wale watakaoziona dalili hizi: "Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia." Dalili hizi zilikwisha kutokea. Sasa tunajua kuwa kurudi kwa Bwana kuko, karibu mlangoni.

Kristo anakuja na utukufu mwingi. Majeshi ya Malaika wenye utukufu watafuatana naye. Atakuja kuwafufua wafu na kuwabadilisha watakatifu walio hai; ili kuwatukuza watu wake waliompenda na kuzishika amri zake na kisha kuwapeleka kwake. Tunapowaangalia wafu wetu na tukumbuke asubuhi ile ambayo'"wafu waafufuliwa, wasiwe na uharibifu nasi tutabadilika." 1 Wakorintho 15.52. Mfalme atayafuta machozi yote kutoka katika macho yetu, na kutusimamisha "mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu" (Yuda 1:24). "Basi: mambo hayo yaanzapo kutokea changamkeni mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia." Lakini Kristo alisema wazi kuwa yeye mwenyewe hawezi kusema

siku au saa ya kurudi kwake. Siku: hasa ya kurudi kwake Yesu ni siri ya Mungu.

### Kuzidi kupita kiasi kwa uovu wa siku za mwisho. [357]

Kristo aliendelea kusema: "Na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika, Safina, wasitambue hata Gharika ikaja ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."

Siku za Nuhu zilikuwaje? "Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani, na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni haya tu siku zote," (Mwanzo 6:5). Watu wa siku za Nuhu walifuata dhana zao ovu na mawazo yaliyopotoka. Kwa sababu ya uovu wao waliangamia. Leo ulimwengu unashika njia ile ile.Waasi wa sheria ya Mungu wanaujaza ulimwengu na maovu. Uchezaji wa kamari, ufedhuli, tamaa mbaya na ahiki zisizozuilika, yote hayo yanaujaza ulimwengu kwa maasi.

Kristo alisema; "Kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa. Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka. Tena habari njema hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwenguni wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Kabla ya kuanguka Yerusalemu, Paulo aliishuhudia Injili "iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu," (Wakolosai 1:23). Na sasa, injili ya milele itahubiriwa kwa "kila taifa na kabila na lugha na jamaa," (Ufunuo 14:6). Kristo hakusema ulimwengu wote utaongolewa bali kwamba, "habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, ndipo ule mwisho utakapokuja." Kwa njia ya kuhubiri injili ulimwenguni, lutaharakisha kurudi kwake Yesu. Sisi litupasi tu kutazamia kuja kwa Yesu bali pia kuharakisha kuja kwa siku ya Mungu. (Tazama 2 Petro 3:12.) Kama kanisa lingefanya kazi liliyopewa na Bwana, ulimwengu wote ungekuwa umeonywa na Yesu angekuwa amerudi.

Jambo la kuishi kwalo! Kwa kuwa hatujui wakati kamili wa kurudi kwake Bwana, tumeagizwa kukesha. (Tazama Luka 12:37.)

Wale wanaokesha kwa kurudi kwa Bwana hawawezi kukesha katika hali ya uvivu. Watakuwa wakijitakasa roho zao, kwa kuitii ile kweli. Pamoja na bidii ya kukesha kutakuwepo na kufanya kazi kwa dhati. Juhudi yao itaamshwa ili kushirikiana na mbingu katika shughuli ya wokovu wa wanadamu. Wanatangaza ujumbe unaopasa kwa saa hii. Kama walivyokuwa akina Enoki, Nuhu, Ibrahimu na Musa kila
[358] mmoja alivyotangaza ujumbe kwa wakati wake, ndivyo watumishi wa Kristo watakavyolitangaza onyo maalum kwa kizazi chao.

Lakini Kristo analitaja kundi jingine pia: "Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia akaanza kuwapiga wajoli wake, na kula na kunywa pamoja na walevi Bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua;"

Mtumishi mwovu hasemi kuwa Bwana hawezi kuja. Ila katika matendo na maneno yake hutangaza kuwa kuja kwa Bwana kunakawia. Huondoa katika mawazo ya wengine kule kumtazamia Bwana aje karibu. Mvuto wake huwathibitisha wengine katika mambo ya ulimwengu na bumbuazi. Tamaa za ulimwengu humpumbazisha na kumtawala akili. Mtumishi mwovu huwapiga watumishi wenzake, akiwashitaki na kuwashutumu wale waliowaaminifu kwa Bwana wao. Hujichanganya na walimwengu, na kwa njia hiyo hunaswa mtegoni. "Bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhani, na saa asiyojua, atamkata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki."

Kurudi kwa Kristo kutawaghafdisha walimu wa uongo. Kwa wale wote wenye kuufanya ulimwengu huu kuwa makao yao siku ya Mungu itawapata kama mtego unasao, na kama mwizi ajaye usiku. Ulimwengu ukiwa umezama katika machafuko na anasa za ufedhuli, umelala katika utulivu wa mauti. Watu huyacheka maonyo; "Na kesho itakuwa kama leo, sikukuu kupita kiasi." Isaya 56:12. Tutatazama zaidi katika ya maisha ya anasa. Lakini Kristo asema: "Naja kama mwivi." Ufunuo 16:15. Wakati wenye dhihaka wanapoende-lea kwa kiburi wakati watafula mali wanaendelea katika kupata mali bila kujali kanuni, wakati mwanafunzi anajitahidi kutafuta kila elimu, isipokuwa Biblia, Kristo atakuja kama mwizi.

Kila kitu ulimwenguni kinachemka. Dalili za nyakati zinaogofya. Roho wa Mungu anaondolewa duniani taratibu, na ajali zinafuata moja baada ya nyingine katika nchi na bahari. Kuna tufani na tetemeko, mioto, mafuriko, mauaji ya kila namna. Nami awezaye

kuzisoma nyakati? Usalama uko wapi? Hakuna uhakika katika cho chote kile cha mwanadamu au ulimwengu.

Wako wale wanaongojea, wakikesha na kutenda kazi kwa ajili ya kurudi kwa Bwana wetu. Kundi jingine linasimama katika mstari wa yule mwasi mkuu wa kwanza.

Hatari inatujia pole pole. Jua linang'aa mbinguni, likiendelea na mzunguko wake wa kawaida juu mbi-nguni. Watu wanaendelea kula na kunywa, wakipanda na kujenga majumba. Wafanya biashara [359]
wanaendelea kuuza na kununua. Watu wanagombea madaraka. Wenye kupenda anasa wanajazana katika majumba ya starehe zao mashindano ya Farasi michezo yakamali. Ashiki kuu hutawala, na huku saa ya mlango wa rehema kufungwa inaharakisha na kila jambo karibu linakatwa kwa milele. Shetani amewaweka wakala wake wote shughulini ili wanadamu wadanganywe, na kupotoshwa, mpaka mlango wa rehema umefungwa milele.

"Basi, kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika hayo yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.

[360] # 70 — Kristo Ashirikiana na Wenye Dhiki na Masikini

"Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu . . . ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua. Hivyo ndivyo Kristo alivyoelezea picha ya siku kuu ya hukumu itakavyokuwa. Wakati mataifa yatakapo-kusanyika mbele zake, kutakuwapo na makundi mawili tu, na mwisho wao, utaamuliwa kutokana na yale ambayo walimtendea, au yale ambayo hawakumte-ndea, kwa njia ya kuwahudumia maskini na wenye dhiki.

Katika siku hiyo Kristo hatatoa mbele za watu kazi kuu aliyowatendea kwa kutoa uhai wake kwa ajili yao, ila ataweka hadharani kazi waliyomtumikia kwa uaminifu. Atasema: "Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia." Lakini wanaosifiwa hivyo na Kristo hawajui kuwa walimhudumia. Kwa maswali ya mshangao wao Anawajibu, "kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."

Yesu alisema: Katika wale wote wanaoudhiwa kwa ajili ya jina langu, mnapaswa kunitambua humo. Na kadiri ambavyo mgenihudumia, ndivyo mwahudumie wao. Wale wote waliozaliwa katika jamaa ya mbingu kwa namna maalum ni ndugu za Bwana wetu. Upendo wa Kristo huwafunga pamoja jamaa wote wa familia yake. "Na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu." 1 Yohana 4:7.

Wale wanaosifiwa na Kristo katika siku ya hukumu, inawezekana
[361] kuwa walikuwa Wanajua theolojia kidogo tu, lakini walizipenda kanuni za mbinguni. Hata miongoni mwa watu wasioamini wako wenye moyo wa ukarimu. Kabla maneno ya uzima hayajaingia katika masikio yao waliwafadhili wahubiri bila kujali hatari zili-

zowakabili. Wanaomwabudu Mungu bila kujua, ambao hawajapata nuru yo yote ile hawatapotea. Ingawa hawaijui sheria ya Mungu iliyoandikwa, wamefanya mambo yanayotakiwa na sheria. Matendo yao hudhihirisha kuwa Roho Mtakatifu ameyagusa maisha yao; nao wanatambuliwa kuwa ni wana wa Mungu.

Kutakuwa na mshangao kiasi gani kwa watu wanyonge kusikia, wakiambiwa na Mwokozi: "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."!

Lakini upendo wa Kristo hauna mpaka kwa watu wa kundi lo lote lile. Yeye ni Mwana wa Adamu, hivyo ndugu wa kila mwana na binti wa Adamu. Wafuasi wake wasijione kuwa wametengwa na ulimwengu uwazungukao na unaoangamia. Waoni sehemu ya utandu wajamaa kuu ya wanadamu, ni ndugu zao wenye dhambi na wenye haki pia. Upendo wa Kristo huwakumbatia wenye dhambi na walioangukia mbali; na kila kitendo kinachofanywa ili kumwinua mkosaji kutoka matopeni, hukubaliwa kana kwamba kimetendwa kwa Kristo.

Malaika wa mbinguni hutumwa ili kuwahudumia wale watakaourithi wokovu. Haijadhihirika bado kwamba ni nani watakaourithi wokovu, lakini malaika wanazungukazunguka duniani kote wakitafuta kuwafariji wenye huzuni na kuwalinda walio hatarini na kuwaleta watu kwa Kristo. Hakuna hata mmoja anayepitwa. Mungu hana upendeleo.

Unapofungua mlango wako kwa wenye dhiki na wasumbukao, unawakaribisha malaika wasioonekana. Huleta utulivu na furaha. Kila tendo la huruma hupeleka wimbo mzuri mbinguni. Baba katika kiti cha enzi huwahesabu wenye matendo yasiyo na ubinafsi kuwa hazina yake ya thamani kuu.

Wale watakaokuwa katika mkono wa kushoto wa Kristo, ambao hawakumshughulikia yeye katika wenye dhiki, ambao ni maskini na wenye dhiki, hawakutambua hatia yao. Waliishi katika hali ya ubinafsi wala hawakujali haja za wengine,

Mungu amewapa matajiri mali ili wawasaidie wenye dhiki ambao ni watoto wake, lakini mara nyingi hawajali dhiki na mahitaji ya watu wengine. Hawaelewi majaribu na matatizo ya maskini, na hivyo huruma hufifia katika mioyo yao. Mali waliyopewa na [362]
Mungu, ili wawasaidie wenye dhiki, wao huzitumia katika majivuno na ubinafsi wao. Maskini hunyimwa maarifa wanayopaswa kupata

kuhusu huruma za Mungu, kwa sababu amefanya kila mpango ili wasaidiwe kwa kupatiwa mahitaji, ya lazima. Huachwa kusumbuka na ufinyu wa maisha ya umaskini na kuingia katika majaribu ya wivu na kujazwa na dhana Potovu.

### Jinsi ya kutomjali Kristo

Lakini Kristo huona yote hayo, naye huserna, Ni mimi niliyekuwa na njaa, na kiu. Ni mimi niliyekuwa, mgeni. Mlipokuwa mkijilisha kwa karamu za anasa, mimi, nilikuwa nikishinda na njaa kibandani. Mlipokuwa mkijifurahisha katika majumba yenu ya anasa, mimi sikuwa, na mahali pa kulala. Ninyi mlipokuwa mkishughulikia sikukuu, mimi nilikuwa nikisumbuka gerezani. Mlipotoa makombo ya chakula kwa masikini wenye njaa, na mavazi hafifu kwa watu waliopigwa na baridi, je mlitambua kuwa nilimfanyia hayo Bwana wa Utukufu? Katika maisha yenu yote, nilikuwepo miongoni mwa wenye dhiki, lakini hamkujali kunitafuta. Kwa hiyo hamwezi kuingia pamoja nami katika furaha. Siwajui ninyi.

Wengi hutembelea sehemu alizoishi Kristo hapa, duniani, wakiangalia ziwa ambako alikuwa akipenda kufundisha watu kando yake, na vilima na mabonde aliyoyaona. Lakini haitupasi kwenda Nazareti, au Bethania ili kutembea katika nyayo za Yesu. Tutazikuta nyayo zake kando ya kitanda cha mgonjwa, katika vibanda vya maskini, na po pote pale walipo wenye dhiki wanaohitaji faraja.

Wote,watapata jambo moja la kutenda. Watu mamilioni waishio katika kifungo cha ujinga na dhambi hawajapata kusikia habari za upendo wa Yesu kwao. Kanuni ya Kristo ya maisha ambayo kila mtu atahukumiwa nayo ni, "Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo." Mathayo 7:12.

Mwokozi ametoa uhai wake ili kulisimamisha kanisa litakaloweza kuwahudumia wenye kujaribiwa. Waumini waweza kuwa maskini, wasiokuwa na elimu, na wasiojulikana, walakini katika Kristo wanaweza kufanya cho chote kwa majirani zao, na hata "katika nchi za mbali," ambayo matokeo yake yatafika hata katika umilele. Kwa sababu kazi hii imedharauliwa, waamini wapya hawajishughulishi hata kidogo katika kupiga hatua ya uzoefu wa maisha
[363] ya Kik:risto. Juhudi mpya ambayo kila mara huleta hatari inaweza kuelekezwa kuwa vijito vya mibaraka. Ubinafsi ungesahauliwa,

katika juhudi za kuwahudumia wengine. Wale wanaowahudumia wengine wasingekuwa na haja ya kutamani michezo ya msisimko au kuwa na mabadiliko maishani mwao. Kusudi lao kuu lingekuwa namna ya kuwaokoa watu kutoka katika hatari ya upotevu.

Mfalme wa utukufu alikuja kuishi na sisi, ili kutufanya kuwa jamaa moja. Naye alisema: "Mpendane kama nilivyowapenda ninyi." Yohana 15:12. Kama tukiupenda ulimwengu kwa jinsi ile Yesu alivyotupenda, tutatimiza kazi yake. Tutafaa kwenda mbinguni, maana tunayo mbingu katika mioyo yetu. Katika siku ile kuu ya hukumu, wale ambao hawakumfanysia kazi Kristo walioishi kwa ubinafsi kwa kujifikiria wenyewe, watawekwa na Hakimu wa ulimwengu wote katika upande wa watenda maovu.

Kwa kila mtu umekabidhiwa wajibu. Kwa kila mtu Mchungaji mkuu atauliza. "Liko wapi kundi lako ulilopewa, kundi lile zuri?" Yeremia 13:20.

[364] # 71 — Mtumishi wa Watumishi

Kristo pamoja na wanafunzi wake walikuwa wamekusanyika pamoja ili kuadhimisha Pasaka. Mwokozi alijua kuwa saa yake imekuja; Yeye mwenyewe alikuwa ndiye Mwana Kondoo wa kweli wa pasaka, na katika siku ile ya kula Pasaka, ilikuwa budi atolewe kafara. Kulikuwa na saa chache ambazo atazitumia kwa manufaa ya wanafunzi wake.

Maisha ya Kristo yalikuwa ya huduma isiyokuwa na ubinafsi ndani yake. "Kama vile Mwana Adamu asivyokuja kutumikiwa bali kutumika," (Mathayo 20:28), hilo lilikuwa fundisho katika kila tendo lake. Lakini wanafunzi wake walikuwa hawajajifunza fundisho hilo bado. Wakati wa Pasaka hii ya mwisho Yesu alihangaika. Kivuli cha kilimtanda usoni. Wanafunzi walitambua kuwa kulikuwa na jambo zito lilomsumbua sana.

Walipokuwa wamekusanyika mezani, akawambia; "Nimetamani sana kuila pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; kwa maana nawaambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. Akapokea kikombe, akashukuru, akasema, Twaeni hiki, mgawanye ninyi kwa ninyi, maana nawaambia ya kwamba tangu sasa sinywi mazao ya mzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja." Luka 22:15-18.

Sasa Kristo alikuwa katika kivuli cha msalaba, na maumivu ya uchungu yalisonga rohoni mwake. Alijua kuwa ataachwa; alijua kuwa kwa hali ya kudhalalisha mno atahukumiwa kuuawa kama mhalifu. Alijua kutokuwa na shukrani na ukatili, wa wale aliokuja kuwaokoa. Alijua kuwa kwa wengi dhabihu atakayowafanyia haitathaminiwa. Akijua yote yaliyokuwa yako mbele yake, katika hali ya kibinadanu angaliweza kulemewa, na mawazo ya kudhalilishwa
[365] na mateso yake. Lakini hakujifikiria mwenyewe. Bali kuwafikiria wanafunzi wake ndiko kulikokuwa katika moyo wake.

Katika jioni hii ya mwisho, Yesu alikuwa na mambo mengi ya kuwaambia wanafunzi wake. Lakini aliona kuwa hawangeweza kustahimili yote. Alipowaangalia, usoni, maneno yake yalibaki

mdomoni. Wakati ulipita kimya kimya. Wanafunzi walikuwa wenye mashaka makubwa. Walivyokuwa wakitazamana ilionyesha hali ya mashindano na wivu.

Kulikuwa na "mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa." Mabishano haya yalimuumiza na kumhuzunisha Yesu. Kila mmoja aliwania nafasi ya juu katika ufalme. Kule kuthubutu kwa Yakobo na Yohana kuitaka nafasi ya juu kuliwajongeza wale kumi kiasi cha kutaka kuleta kufarakana. Yuda ndiye alikuwa mkali sana dhidi ya Yakobo na Yohana.

Wanafunzi walipoingia chumba cha juu, Yuda alimsogelea Kristo upande wa mkono wa kushoto, Yohana alikuwa mkono wa kulia. Kama kulikuwa na cheo cho chote cha juu Yuda alikusudia kukipata.

Jambo jingine la ubishi lilikuwa limetokea. Ilikuwa kawaida kwa mtumishi kuwaosha miguu wageni. Katika siku hii, mtungi wa maji ulikuwako, chombo cha kunawia, na kitambaa cha kufutia, vyote vilikuwa tayari; lakini mtumishi wa kuhudumu hakuwako kwa hiyo ilikuwa kazi ya wanafunzi kufanya huduma hiyo. Lakini kila mmoja hakutaka kufanya kazi hiyo inayompasa mtumishi. Wote walionyesha hali ya kutojali huduma hiyo. Kukaa kimya kwao kulionyesha kutonyenyekea.

Ni jinsi gani Kristo atawasaidia maskini hawa ili Shetani asiweze kupata ushindi kamili dhidi yao? Atawasaidiaje wajue kuwa kule tu kujidai kwamba ni wanafunzi hakuwafanyi kuwa wanafunzi wa kweli? Atawaamshiaje upendo katika mioyo yao kuwawezesha kutambua kile alichotamani kuwaaambia?

Yesu alingoja kidogo aone watakaofanya nini. Kisha yeye ambaye ni Mwalimu wa mbinguni, aliondoka mezani. Akivua mavazi yake ya juu, alichukua kitambaa cha kufutia. Wanafunzi wakiwa kimya walingoja kuona yatakayofuata. "Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga." Tendo hilo liliwafungua macho wanafunzi. Aibu kuu ikawajaza mioyo na wakajiona katika nuru mpya.

Kristo aliwapa kielelezo ambacho hawangekisahau kamwe. Upendo wake kwao ulikuwa usioweza kuvunjika kirahisi. Alikuwa na [366]
ufahamu hakika wa Uungu wake; lakini aliweka kando taji yake ya ufalme, na akatwaa hali ya mtumwa. Mmojawapo ya matendo yake

ya mwisho ya maisha yake hapa duniani lilikuwa kujifunga kama mtumwa na kutenda kazi ya mtumwa.

Kabla ya Pasaka Yuda alikuwa amekamilisha njama na makuhani na waandishi, ya kumkabidhi Yesu katika mikono yao. Wanafunzi hawakufahamu lo lote kuhusu makusudi ya Yuda. Yesu peke yake ndiye aliyefahamu siri yake, walakini Yesu hakumuumbua Yuda kwa wanafunzi. Alijisikia kuwa na mzigo na Yuda kama alivyousikitikia Yerusalemu na kuulilia mji uliokuwa unakabiliwa na maafa.

Nguvu ya msukumo wa upendo wa Kristo ulimgusa Yuda. Wakati mikono ya Mwokozi ilipomshika miguu na kumtawadha, moyo wake ulisisimka, Yuda akajisikia kuungama dhambi yake. Lakini hakutaka kunyenyekea. Akafanya moyo wake kuwa mgumu dhidi ya toba na kwa mara nyingine tena misukumo ya zamani ikamtawala. Yuda sasa akachukizwa na tendo la Yesu la kuwatawadha miguu wanafunzi wake. Alifikiri kwamba, ikiwa Yesu anajidhili kiasi hicho asingeweza kuwa mfalme wa Israeli. Alipoona hivyo akaridhika kuwa hakukuwa na la manufaa kumfuata Kristo. Alithibitika katika kusudi lake la kumkana Kristo na kuamini amedanganyika. Akiwa amepagawa na pepo mbaya, aliazimia kutekeleza kazi aliyokuwa amekubali kutenda katika kumsaliti Bwana wake.

## Mwujiza mkuu wa Mioyo Iliyobadilika

Yuda katika kuchagua kikao chake mezani, alijaribu kujiweka kuwa wa kwanza, na Kristo aliyetumika kama mtumwa alimhudumia yeye kwanza. Yohana aliachwa mpaka mwisho. Lakini Yohana hakulihesabu tendo hilo kama kemeo kwake. Zamu ya Petro ilipofika, alisema kwa mshangao; "Bwana! Wewe wanitawadha miguu mimi?" Unyenyekevu wa Bwana ulimvunja moyo wake. Alijawa na aibu kuona kwamba hakuna hata mmoja katika wanafunzi aliyejitolea kutenda kazi hiyo. Kristo akasema: "Nifanyalo, wewe hujui sasa; lakini utalifahamu baadaye." Petro hakuvumilia kumwona Bwana wake, Mwana wa Mungu akitenda kazi impasayo mtumwa. Moyo wake wote uliinuka dhidi ya unyenyekevu huu Kwa sauti kuu ya mkazo akasema, "Wewe hutanitawadha miguu kamwe."

Kristo akasema, "Kama nisipokutawadha, huna shirika nami." Kristo alikuwa amekuja kutakasa moyo kutokana na doa la dhambi.

Petro alikuwa akikataa utakaso wa kiroho uliojumulisha na ule wa chini. Kwa kweli hakika alikuwa anamkataa Bwana wake. Siyo udhilifu kwa Bwana kumruhusu kutenda kazi kwa ajili ya utakaso wetu. [367]

Petro akajisalimisha kiburi chake. Kutengana na Kristo kungekuwa mauti kwake. Akasema, "Bwana, si miguu yangu tu, hata na mikono yangu na kichwa changu pia." Yesu "akamwambia, Yeye aliyekwisha kuoga hana haja, ila kutawadha miguu, bali yu safi mwili wote."

Maneno haya yana maana zaidi ya usafi wa mwili. Utakaso wa kiroho unaofananishwa na kuoshwa miguu. Yeye aliyekwisha kuoga yu safi lakini miguu iliyovaa kubazi mara ilihitaji kuoshwa tena. Kwa hiyo Petro na wenzake walikuwa wameoshwa katika chemchemi kuu iliyofunguliwa kwa ajili ya dhambi na uchafu. Lakini majaribu yalikuwa yamewaweka katika uovu, na hivyo walihitaji utakaso wa neema ya Kristo.

Yesu alitamani kusafisha mafarakano, wivu na kiburi kutoka katika mioyo yao. Jambo hili lilikuwa muhimu sana kuliko kuosha mavumbi kutoka katika miguu yao. Kwa roho waliyokuwa nayo, hakuna hata mmoja aliyekuwa tayari kushirikiana na Kristo. Wasipokuwa wanyenyekevu na wenye upendo hawatakuwa tayari kushiriki katika huduma ya ukumbusho ambayo Kristo alikuwa anaianzisha. Kiburi na kujitafutia makuu husababisha kufarakana, lakini yote hayo Yesu aliwasafisha wakati alipowatawadha miguu. Badiliko la hali lilitendeka. Yesu aliweza kusema; "Nanyi mmekuwa safi." Sasa kulikuwa na umoja wa moyo, na kupendana. Isipokuwa Yuda, kila mmoja alikuwa tayari kumuachia mwenzake nafasi ya kwanza. Sasa wangaliweza kupokea maneno ya Kristo.

Hata sisi tumeoshwa kwa damu ya Kristo, walakini mara kwa mara moyo huchafuka. Lazima mioyo yetu michafu iletwe kwa Kristo! Mara ngapi tunamhuzunisha kwa ajili ya mioyo yetu yenye hasira mbaya, ubatili wetu, na kiburi chetu! Walakini upungufu wetu wote na uchafu wote lazima tuvilete kwake. Yeye peke yake aweza kututakasa.

Baada ya Kristo kuwatawadha wanafunzi miguu, allisema: "Je! mmeelewa na hayo niliyowatendea? Ninyi mwaniita, Mwalimu, na Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu,

imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi, mtende vivyo. Amin, amin nawaambia ninyi, Mtumwa si mkuu kuliko Bwana wake; wala mtume si mkuu kuliko yeye aliyempeleka."

[368] Kristo mwenyewe alitoa kielelezo cha unyenyekevu ili watu wasipotoke na kufuata hali zao za ubinafsi. Yeye Mwenyewe akiwa yu sawa na Mungu, alitenda kama mtumwa kwa wanafunzi wake. Kristo ambaye kila goti lazima kumpigia, aliinama kutawadha miguu ya wale waliomwita Bwana. Alitawadha miguu ya msaliti wake.

Mungu haishi kwa nafsi yake. Yeye daima huwahudumia viumbe vyake. Yesu alipewa kusimama mbele ya jamii ya Wanadamu, kusudi kwa kielelezo chake apate kulundisha maana ya kuwa mhudumu. Aliwahudumia wote, na kuwatumikia wote. Kwa hiyo aliishi kwa sheria ya Mungu, na kwa kielelezo hicho alituonyesha jinsi ya kuitii.

Yesu alipomaliza kuwatawadha wanafunzi, miguu, alisema, "kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo." Kwa maneno hayo Kristo alikuwa anaanzisha utaratibu wa huduma ya kidini. Kwa tendo hilo la Bwana wetu huduma hii ya unyenyenevu ilifanywa kuwa agizo takatifu. Ilipaswa ishikwe, na kuadhimishwa na wafuasi wake ili kukumbuka fundisho hilo la unyenyekevu na huduma yake daima.

Agizo hili lilikuwa maandalio ya Kristo ya ushirika mtakatifu wa meza ya Bwana. Wakati kiburi na ufedhuli na mashindano ya vyeo, vinapopendelewa, hatuwezi kuwa tayari kushiriki meza takatifu ya Mwili na damu Yake. Kwa hiyo Yesu aliweka huduma ya unyenyekevu kuwa kitu cha kwanza, kabla ya meza ya Bwana.

Katika moyo wa mwanadamu kuna hali ya kujitukuza mwenyewe na kujiona kuwa bora kuliko mwenzake; kujipendelea, kutafuta ukuu; na mara nyingi huwa na matokeo ya dhana potovu na chuki. Huduma ya kutawadha inayotangulia meza ya Bwana inakusudiwa kumwondoa mtu katika ubinafsi, kumshusha kutoka katika kujiinua nafsi, na kumleta katika unyenyekevu utakaomwezesha kumhudumia ndugu yake. Mwonaji mtakatifu kutoka mbinguni huwapo katika huduma hii kuifanya kuwa ya kutafakari mambo ya kiroho kujutia dhambi na kuwa na uhakika wa msamaha wa dhambi. Kristo huwapo kubadilisha mkondo wa mitiririko wa mawazo ya ubinafsi.

Kadiri unyenyekevu wa Mwokozi kwa ajili yetu unavyokumbukwa, huwa mnyororo wa kumbukumbu, hutujia, kumbukumbu za wema wa Mungu na upole wa rafiki zetu wa duniani. Mibaraka iliyosahauliwa, na fadhili zilizodharauliwa hukumbukwa upya. Upungufu wa tabia, kupuzia wajibu, kutokuwa na shukurani, na ubaridi vyote huletwa katika kumbukumbu. Nia zetu huamshwa upya, ili kuvunja kila kizuizi kilichosababisha utengano. Dhambi hu- [369]
ungamwa; na kusamehewa.

Neema ya Kristo iongoayo huivuta mioyo pamoja. Tamaa huamshwa katika kutafuta maisha ya juu ya kiroho. Moyo huinuliwa. Hivyo huweza kushiriki Meza ya Bwana, mwanga wa haki ya Kristo ukiwa umejaza hekalu la moyo.

Kwa wale wanaopata roho ya huduma hii, haiwezi tena kuwa tu tamasha. Kila huduma hii itakapofanyika kwa moyo wa kweli, watoto wa Mungu watafanya agano kwamba maisha yao yatatolewa katika huduma ya ukarimu kwa wengine.

Ulimwengu umejaa wale wanaohitaji huduma yetu. Wale walioshiriki pamoja na Kristo katika chumba cha ghorofa wataondoka kwenda kuhudumu kama Alivyofanya. "Mkiyajua hayo heri ninyi mkiyatenda."

[370]

# 72 — Meza ya Bwana Yaanzishwa

"Bwana Yesu, usiku ule aliotolewa, alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwiliwangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; Fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo." 1 Wakorintho 11:23-26.

Kristo, Mwana kondoo wa Mungu alikuwa karibu kukomesha desturi ya mifano na ibada za kafara, ambazo kwa muda wa miaka 4,000 zililenga kwa kifo chake, Pasaka, ambayo ilikuwa sikukuu ya taifa la Israeli, ilikuwa ifutika milele. Adhimisho la meza ya Bwana, ambalo Kristo alikuwa ameanzisha ndilo liadhimishwe na wafuasi Wake katika nchi zote na katika vizazi vyote.

Pasaka ilikuwa imeanzisha kuwa ukumbusho wa kukombolewa kwa Waisraeli kutoka katika utumwa wa Misri. Meza ya Bwana ilianzishwa kuwa ukumbusho wa kukombolewa kulikoletwa kama matokeo ya kifo cha, Kristo. Adhimisho la agizo hili ndiyo njia ya kutukumbusha daima kazi yake kuu kwa ajili ya wokovu wetu. Katika, nyakati za Kristo watu walikula Pasaka wakiwa katika hali ya kuketi kwa kuegemea. Wageni waliegemea kwenye kiti kirefu, kilichowekwa karibu na meza, mkono wa kulia ulikuwa huru uweze kutumika kula. Katika hali hiyo mtu aliweza kuegemea kichwa chake kifuani mwa yule aliyekaa karibu naye. Na miguu ilinyoshwa kando ilikuwa wazi kwa kutawadhwa na mtumishi aliyekuwa akitawadha kwa mzunguko upande wa nje ya mduara ule.

Kristo alikuwa angali kwenye meza ambapo chakula cha pasaka
[371] kilikuwa kimeandaliwa. Mikate isiyotiwa chachu ilikuwa mbele yake. Divai safi isiyochachu ilikuwako mezani. Vitu hivyo Kristo alivitumia kufananisha na kafara yake isiyo na kasoro. (Tazama 1 Petro 1:29.)

"Walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili

wangu. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu."

Yuda msaliti alipokea kutoka kwa Yesu mfano wa mwili wake uliovunjika na damu yake iliyomwagika. Msaliti akiwa ameketi mbele ya Mwana Kondoo wa Mungu alitafakari njama zake, na mawazo ya kutaka kisasi.

Wakati wa kutawadha miguu, Kristo alikuwa amedhihirisha kwa dhati kuwa anayafahamu mawazo ya Yuda. Alisema, "Si nyote mlio safi." Yohana 13:11. Sasa Kristo akasema wazi Zaidi: "Sisemi habari za ninyi nyote, nawajua wale niliowachagua; lakini andiko lipate kutimizwa. Aliyekula chakula changu ameniinulia kisigino chake."

Mpaka wakati huu wanafunzi walikuwa hawajamtilia shaka Yuda. Lakini walishikwa na wasiwasi, wakatazamia jambo fulani baya. Walipokuwa wakila katika hali ya ukimya, Yesu akasema, "Amin amin nawaambia, Mmoja wenu atanisaliti." Fadhaa "ikawashika. Inawezekanaje mmoja wao, amsaliti hivyo Mwalimu wao Mtakatifu? Kumsaliti? Kwa nani? Hakika siye mmoja wa hawa wapendwa kumi na wawili!

Walipokumbuka jinsi maneno yake yalivyokuwa ya kweli, hofu na kutojiamini kukawashika. Kwa uchungu wa moyoni walianza kuuliza, mmoja mmoja, "Ni mimi, Bwana?" Lakini Yuda alikaa kimya. Hatimaye Yohana akauliza: "Bwana, ni nani?" Na Yesu akajibu, "Yeye aliyetia mkono wake pamoja nami katika kombe, ndiye atakayenisaliti." Ukimya wa Yuda uliwaelekeza wote kwake. Kutokana na utata wa maswali na butwaa. Yuda hakuwa amesikia jibu la Yesu kwa swali la Yohana. Lakini sasa ili kukwepa uchunguzi wa wanafunzi, naye pia alimwuliza kama walivyo kuwa wameuliza "Ni mimi, Rabi?" Yesu akajibu kwa upole, "Wewe umesema."

Kutokana na mshangao na utata wa kugunduliwa siri yake Yuda aliondoka haraka na kutoka. Kisha Yesu akamwambia "Uyatendayo yatende upesi .... Basi huyo akiisha kulipokea lile tonge, akatoka [372]
mara hiyo. Na kulikuwa ni usiku."

Ulikuwa usiku wakati msaliti alipomuacha Kristo na kwenda katika giza kabisa. Mpaka kufikia hatua hii Yuda alikuwa hajavuka mpaka wa toba. Lakini alipoondoka na kumuacha Bwana wake na wanafunzi wenzake, alikuwa amevuka mpaka wa toba. Hakuna jambo la kumsaidia Yuda lilioachwa kufanywa. Hata baada ya kufanya mapatano mara mbili kumsaliti Bwana wake, Yesu bado alimpa nafasi ya kutubu. Kwa kusoma siri za makusudi ya msaliti, Kristo alimpa ushahidi wa dhati, wa Uungu wake. Huu ulikuwa mwito wa mwisho wa toba. Kutoka katika meza ya Bwana Yuda alienda zake ili kukamilisha kazi ya usaliti.

Katika kumtamkia ole Yuda, Kristo pia alikuwa na kusudi la rehema kwa wanafunzi wake. Alisema: "Nawaambia kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini ya kuwa mimi ndiye." Kama Yesu angalinya-maza, wanafunzi wangalifikiri kuwa Bwana wao hakuwa na uungu wa kujua mbele yatakayokuja, na hivyo alishtushwa. Mwaka mmoja uliopita Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake kwamba aliwachagua watu kumi na wawili, lakini mmoja wao ni Shetani. Sasa maneno yake kwa Yuda yataimarisha imani ya wafuasi wake wa kweli wakati wa dhiki yake. Yuda atakapofikia mwisho wake wa kutisha, watakumbuka ole aliyosema juu ya msaliti.

Mwokozi alikuwa bado ana kusudi jingine. Wanafunzi walipaswa kutafakari jambo jingine kuhusu uvumilivu na rehema za Mungu, juu ya mtu mkosaji mkuu. Msaliti alikuwa amepata nafasi ya kushiriki meza ya Bwana, pamoja na Kristo. Kielelezo hicho ni kwa ajili yetu. Tunapomdhania mtu mmoja kuwa ni mkosaji na mwenye dhambi, haitupasi kumtenga, na kumwacha awe mateka kwa majaribu na kumsukumia, katika uwanja wa mapambano ya Shetani. Kristo aliwatawadha wanafunzi miguu yao kwa sababu walikuwa wakosefu na wenye dhambi, na hivyo wote wakafikishwa katika toba isipokuwa mmoja.

## Kielelezo cha Kristo, hukataza kutenga

Ni kweli kwamba dhambi ya dhahiri humzuia mtu asishiriki katika meza ya Bwana. (Tazama 1 Wakorintho 5: 11.) Lakini zaidi ya hayo hakuna awezaye kuhukumu. Ni nani awezaye kusoma siri za moyo, au kubagua kati ya magugu na ngano? "Lakini mtu ajihoji

mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe." "Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana [373] isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana." "Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupa-rnbanua ule mwili." 1 Wakorintho 11: 28, 29.

Wakati waumini wanapokutana kuadhimisha ibada hizi za dini, kunawezekana kuwamo akina Yuda pia, katika kundi kama ndivyo, wajumbe wa mwovu huwamo vile vile, maana huja kuwaunga mkono wale wote wanaokataa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Malaika wa mbinguni pia huwapo. Hapo wanaweza kuwapo watu ambao si watumishi wa kweli na utakatifu, lakini wanaopenda kushiriki huduma hiyo. Watu kama hao wasizuiwe. Ma-shahidi wako hapo kama walivyokuwako wakati Yesu akitawadha miguu ya wanafunzi.

Kristo huwapo kwa njia ya Roho Mtakatifu, ili kusadikisha na kulainisha moyo. Hakuna hata wazo moja la toba linatoka pasipo kulifahamu. Anawangoja wenye toba na mioyo iliyovunjika. Yeye aliyeosha miguu ya Yuda hutamani kutakasa kila moyo kutokana na doa la dhambi.

Watu wo wote wale wasijitenge wenyewe kutoka katika ushirika wa meza ya Bwana, kwa sababu eti wapo watu wasiostahili kuwapo. Katika mikutano hii, mikutano yake mwenyewe Kristo hukutana na watu wake na kuwatia nguvu kwa kuwako kwake. Mioyo na mikono isiyostahili inaweza hata kuhudumia katika huduma hii, hata hivyo wale wanaokuja wakiwa na imani iliyokazwa juu ya Kristo wataabarikiwa mno. Wote watakaodharau maadhimisho haya, watapata hasara ya kupotea. Huduma ya meza ya Bwana ilikusudiwa kudumisha mbele ya wanafunzi dhabihu isiyo na kikomo iliyotolewa kwa kila mmoja wao binafsi, kama sehemu ya wanadamu wote walioanguka.

### Sababu za kuadhimisha meza ya Bwana

Lakini huduma ya meza ya Bwana haikukusudiwa kuwa wakati wa huzuni. Kadiri wanafunzi wa Yesu watakavyokusanyika Mezani pa Bwana, hawapaswi kuomboleza kwa ajili ya upungufu wao. Hawapaswi kutafakari tofauti zao na wenzao. Huduma ya kutawadhana imeshughulikia yote hayo. Sasa wanakuja kukutana na

Kristo, Hawapaswi kusimama kwenye kivuli cha msalaba bali katika mwanga wake wa wokovu. Wapaswa kufungua mioyo yao kwa nuru itokayo Jua la Haki. Wanapaswa kusikia Maneno yake: "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi si kama ulimwengu utoavyo." Yohana 14:27.

[374] Bwana wetu asema, "Mkiteswa na kuudhiwa kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, kumbukeni upendo wangu, jinsi ulivyo mkuu hata nikatoa maisha yangu kwa ajili yenu. Kazi yenu ikionekana kuwa ngumu mno, na mzigo ukiwalemea, kumbuka kwamba niliuvumilia msalaba kwa ajili yenu, nikiidharau aibu. Mwokozi wenu yu hai akiwaombea.

Huduma ya meza ya Bwana huwaelekeza watu kwenye tukio la kurudi kwake Kristo. Ilikusudiwa kuendeleza tumaini hili mawazoni. "Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo." 1 Wakorinto 11:26.

Kristo aliianzisha huduma hii ili ipate kuzungumza na akili zetu daima juu ya upendo wa Mungu. Haiwezekani kuwa na umoja kati ya roho zetu na Mungu usipokuwa kupitia kwa kristo. Wala hakuna kitu kingine kinachofanya upendo wake uwe na manufaa kwetu isipokuwa kifo cha Kristo. Na ni kwa sababu ya kifo chake tu ndipo tunaweza kukutazamia kurudi kwake kwa furaha. Dhamiri zetu zinahitaji kuamshwa na kuhimizwa kushikilia siri ya utauwa, kutambua zaidi kuliko tunavyotambua, mateso ya kulipia ya Kristo.

Bwana wetu amesema: "Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuiinywa damu yangu, hamna uzima ndani yenu . . . kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli." Yohana 6:53-55. Kwa kifo cha Yesu tunawiwa hata na uzima wa sasa. Chakula tunachokula kimenunuliwa kwa mwili wake uliovunjwa; na maji tunayokunywa, hutokana na damu yake iliyomwagika. Hakuna mtakatifu mmoja au mwenye dhambi alaye chakula chake cha kila siku bila kuboreshwa na mwili na damu ya Kristo. Msalaba wa Kalwari umepigwa chapa juu ya kila kipande cha mkate; na nuru yake huonekana katika kila chemchemi ya maji. Nuru inayong'aa kutoka katika Huduma ya meza ya Bwana huvitakasa vitu vyote vya maisha yetu ya kila siku. Mkusanyiko wa jamaa huwa sawa na meza ya Bwana na kila mlo Ushirika Mtakatifu (Sacrament).

Kuhusu hali yetu ya asili ya kiroho Yesu anasema, "Aulaye mwili wangu, na kuiinywa damu yangu, anao uzima wa milele." Kwa kulipokea neno lake, na kuyafanya maagizo yake, hushirikiana naye. Alisema, "Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake. Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba, kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi." Yohana 6:56, 57. Kadiri imani [375]
itakavyotafakari kafara kuu ya Bwana wetu, moyo huungana na maisha ya kiroho ya Kristo. Kila adhimisho la Meza ya Bwana huleta kiungo hai ambacho kwacho muumini hufunganika na Kristo na hivyo na Baba.

Tunapopokea mkate na divai inayofananishwa na mwili wa Kristo, uliovunjika na damu iliyomwagwa kwa mawazo tunashuhudia mashindano ambayo kwayo upatanisho wetu na Mungu, ulipatikana Kristo huonekana amesulibishwa miongoni mwetu. Wazo la Kalwari huamsha hisia hai na takatifu katika mioyo yetu. Kiburi na ibada ya nafsi haviwezi kusitawi katika roho ambayo daima hutunza kumbukumbu ya matukio ya kalwari. Yeye autazamaye upendo wa Mwokozi usio kikomo atabadilishwa kitabia. Ataondoka kwenda kuwa nuru kwa ulimwengu, akiangaza kwa kiwango fulani upendo huu wa ajabu.

[376] # 73 — "Msifadhaike Mioyoni Mwenu"

Yuda alikuwa ameondoka katika kile chumba cha ghorofa, na Kristo alibaki pekee na wale kumi na mmoja. Alikuwa karibu kuzungumzia kuhusu kutengana kwake na wanafunzi wake; lakini kabla ya haya alitaja kazi yake kuu iliyomleta hapa duniani. Alikumbusha mara kwa mara kuwa kudhalalishwa kwake kote na mateso yake yote vitalitukuza jina la Baba yake. Kwa jambo hili alilielezea kwanza mawazo ya wanafunzi wake.

Bwana, na Mkuu wao, Mwalimu na Rafiki wao mpendwa, alikuwa wa thamani mno kuliko maisha yao. Na sasa alikuwa awaache. Giza la mambo yajayo lilifunika mioyo yao.

Lakini maneno ya Mwokozi yalijaa matumaini. Alijua kuwa mbinu za Shetani hufaulu sana kwa wale wanaotingwa na matatizo. Kwa hiyo aliwaelekeza mawazo yao kwa makao ya mbinguni: "Msifadhaike mioyoni mwenu; Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo." (Yohana 14:1-3). Nikiondoka, bado nitawaangalia kwa dhati. Naenda kwa Baba, kushirikiana naye kwa niaba yenu.

Kuondoka kwa Kristo kulikuwa, kinyume na vile wanafunzi walivyokuwa wakihofia hakukuwa na maana ya kutengana milele. Alikuwa akienda kuwaandalia mahali, ili apate kuwapokea kwake. Wakati akiwaandalia makao, wao watakuwa wakijiandaa tabia zao ili zifananena za mbinguni. Tomaso akisumbuliwa na mashaka, akasema, "Bwana, sisi hatujui uendako, nasi twaijuaje njia? Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi. Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba, tangu sasa mnamjua, tena mmemwona."

[377] Hakuna njia nyingi za kufikia mbinguni. Hakuna uwezekano wa kila mmoja kuchagua njia yake. Kristo alikuwa ndiye njia ambayo kwayo wazee wa zamani na manabii waliokolewa. Yeye ndiye njia pekee ambayo kwayo sisi tunaweza kupitia ili kumfikia Mungu.

Lakini bado wanafunzi hawakuelewa hivyo. ‘’Bwana utuonyeshe Baba, yatutosha,” Filipo akasema ghafula. Kristo aliuliza kwa mshangao wa uchungu: “Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo?” Je, inawezekana kwamba humwoni Baba katika kazi azitendazo kupitia kwangu? “Basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?” “Aliyeniona mimi amemwona Baba,” Kristo hakukoma kuwa Mungu alipofanyika mwanadamu. Utatu mtakatifu ulidumu kuwa wake. Kazi za Kristo zilidhihirisha uungu wake. Katika Yeye Baba alikuwa amefunuliwa.

Kama wanafunzi watauamini mwungano huu muhimu kati ya Baba na Mwana basi, imani yao isingalitikiswa wakati wakiona mateso na kifo cha Kristo. Ni kwa kiasi gani Mwokozi alitafuta kwa bidii kuwaandaa wanafunzi kwa tufani kubwa ya majaribu iliyokuwa ikiwakabili wote. Wote waliokuwapo walijisikia kicho kitakatifu walipoyasikiliza kwa makini maneno yake. Na kwa jinsi mioyo yao ilivyovutwa kwake Kristo kwa upendo zaidi, vilivyo hivyo ndivyo walivyovutwa kila mmoja kwa mwenzake. Walijisikia kuwa mbingu zilikuwa karibu sana nao.

Mwokozi alikuwa na shauku ya kutaka wanafunzi wake waelewe kwa nini Uuungu wake uliungana na ubinadamu. Alikuja ulimwenguni kuonyesha utukufu wa Mungu, ili mwanadamu avutwe kwa uwezo wake kuinuliwa na kurudishwa kwake. Yesu hakuonyesha sifa zo zote zile wala kutumia uwezo wo wote ule ambao mtu hawezi kuupata akiwa na imani kwa Yesu. Hali kamilifu ya ubinadamu wake ni hali ambayo kila mfuasi wake anaweza kuwa nayo, iwapo atajitoa kwa Mungu kama yeye alivyojitoa.

“Na kazi kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa baba”. Kwa maneno haya Kristo alikuwa na maana kuwa kazi ya wanafunzi wake itakuwa na matokeo makubwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Baada ya kupaa kwa Kristo, wanafunzi walitambua utimilizo wa ahadi yake. Walijua kuwa Mwalimu wa mbinguni alikuwa kama vile alivyosema. Kadri walivyoutukuza upendo wa Mungu mioyo ya watu ilitiishwa na makutano wakamwamini Yesu.

## Faida ya ajabu ya Maombi [378]

Mwokozi alieleza siri ya kufaulu kwao itakuwa katika kuomba uwezo na neema katika jina lake. Maombi ya mtu mnyenyekevu

Kristo atayawakilisha mbele za Baba kama yake mwenyewe kwa niaba ya mwombaji. Sala ya unyofu yawezekana isiwe yenye maneno ya ufasaha lakini itapanda mpaka mahali patakatifu, Yesu anakohudumu. Atayawakilisha kwa Baba bila neno hata moja la kupotosha au la kusitasita, yakiwa yenye harufu nzuri ya ukamilifu wake. Njia ya unyofu na uadilifu huwa haikosi kizuizi, lakini katika kila tatizo yatupasa tuone haja ya wito wa kuwa na maombi. Yesu alisema "Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno kwa jina langu,nitalifanya."

Katika jina lake Kristo, wafuasi wake watasimama mbele za Mungu. Kwa sababu ya kuvikwa haki ya Kristo, mwenye dhambi ndani yao. Yeye hutambua sura ya Mwanaye ndani yao ambaye wao humwamini.

Bwana husikitika watu wake wanapojihafifisha. Mungu aliwataka la sivyo asingemtuma Mwana wake katika utume ghali wa kuwakomboa. Yeye hupendezwa na watu wanapomtafuta ili kulitukuza jina lake. Wanaweza kutumaini kuona matendo makuu ikiwa watakuwa na imani katika ahadi zake. Lakini kuomba katika jina la Kristo kuna maana kwamba tunapaswa kutenda kazi zake. Mwokozi huokoa watu, siyo katika dhambi bali kutoka dhambini; na wale wanaompenda huonyesha upendo wao kwa utii. Utii wote wa kweli kutoka moyoni. Kwa Kristo ilikuwa ni kazi ya moyoni. Kama tukikubali ataunganisha mioyo yetu na nia zetu pamoja na mapenzi yake tutawezeshwa kiasi kwamba tunapomtii tutakuwa tunatekeleza msukumo ulio ndani yetu. Tutakapomfahamu Mungu kadiri tupatavyo nafasi kumfahamu, maisha yetu yatakuwa mtiririko wa utii. Kwa kushirikiana na Mungu,dhambi zitakuwa chukizo kwetu.

Jinsi Kristo alivyoishi hali ya kibinadamu akitii sheria, ndivyo nasi tutaishi kama tukiushikilia Mkono wa nguvu wa imani. Lakini hatuwezi kutegemea mashauri ya wanadamu. Bwana atatuelekeza kutenda wajibu utupasao kama anavyopenda kuwaelekeza wengine pia. Tukimwendea kwa imani atatuzungumzia siri zake binafsi. Wale wanaokataa kutenda kitu cho chote cha kumchukiza Mungu baada ya kumwomba watajua jambo la kufanya. Na watapokea siyo tu hekima, bali pia nguvu uwezo wa kutii, na kufanya kazi watapewa kama Kristo alivyoahidi.

## Jinsi Roho Mtakatifu Anavyofanikisha Kazi va Kristo Kwa Ajili Yetu [379]

Kabla Kristo hajajitoa kuwa kafara ya wenye dhambi, alitafuta zawadi muhimu . . . atakayowapa wafuasi wake Alisema: “Nami nitamwomba Baba, naye alawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu (Yohana 14:16-18). Wakati Kristo alipokuwa hapa duniani, wanafunzi hawakuwa na haja na mfariji mwingine. Hata atapokwisha kupaa, ndipo watajisikia wanahitaji Roho, na ndipo Atikapokuja.

Roho Mtakatifu ni mwakilishi wa Kristo, lakini asiyekuwa na hali ya kibinadamu na hivyo huru. Kristo alipokuwa na mwili wa mwanadamu hakuweza kuwa mahali popote kwa wakati uleule. Kwa hiyo ilikuwa kwa manufaa yao kwa Yesu kuondoka na kutumwa Roho badala ya Yesu Hivyo, hakuna ambaye angenu-faika kutokana na mahali alipo. Kwa njia ya Roho Mtakatifu Kristo angepatikana kwa wote.

Yesu alisoma mambo ya mbele ya wanafunzi wake. Aliona kuwa mmoja atanyongwa, mwingine atasulibishwa msalabani, mmoja atafungwa kisiwani katikati ya bahari wengine watateswa na kuangamizwa. Lakini katika matatizo yote hayo Yeye atakuwa pamoja nao. Ikiwa mfuasi wake atapata matatizo kwa ajili ya kweli na kusimamishwa mbele ya mahakama dhalimu Kristo atasimama pamoja naye. Mashutumu watakayo shutumiwa yataanguka kwake. Ikiwa fulani atatupwa gerezani, Kristo atamfariji, kwa pendo lake.

Po pote tutakapokuwa na kwa wakati wo wote, tutakapojisikia wanyonge na hali ya upweke, Mfariji atatumwa katika kujibu ombi la imani. Katika hali fulani tunaweza kutengana na rafiki zetu wa dunia lakini hakuna kitu cha kututenga na Mfariji wetu wa mbinguni. Yuko pamoja nasi siku zote kututia nguvu na kutufariji. Bado Wanafunzi wakashindwa kuelewa maneno ya Kristo, na tena akaeleza: Kwa njia ya Roho atajidhihirisha mwenyewe kwao “Msaidizi huyo Roho Mtakatifu, ambaye na Baba, atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote.” Hamtaweza tena kusema kuwa sikuelewa.

Kristo alikuwa azungumze na watu wote duniani kwa njia ya wanafunzi wake. Lakini katika kifo cha Kristo wanafunzi walikuwa
[380] wakatishwe tamaa mno. Kusudi baada ya hali hiyo neno lao lipate kuwa hakika, Yesu aliahidi, kuwa Msaidizi atakapokuja "atawakumbusha yote, niliyowaambia." "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote mtakayoyasikia atakayoyanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi; kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari" Wanafunzi wa Yesu walizoezwa kuyaamini maneno ya marabi kana kwamba ni maneno ya Mungu, na mambo hayo bado yalikuwa na mvuto akilini mwao. Hawakuelewa aina ya ufalme wa kiroho wa Kristo. Mafundisho yake mengi yalionekana kupita. Yesu aliahidi kuwa mambo haya yote watakumbushwa na Roho Mtakatifu. Msaidizi huitwa "Roho wa Kweli." Kazi yake ni kufafanua na,kudumisha kweli. Kwanza hukaa moyoni kama Roho wa kweli na hivyo kuwa Msaidizi. Kuna faraja katika kweli lakini hakuna faraja katika uwongo.

Kwa mapokeo ya uongo Shetani hutawala akili za watu Kanuni hupotosha tabia. Roho mtakatifu hudhihirisha makosa, na kuyaondoa kutoka moyoni. Kwa njia ya Roho wa kweli, akitenda kazi kwa Neno la Mungu, Kristo huwatiisha kwake mwenyewe watu wake Aliowachagua.

### Kusudi Kuu la Roho Mtakatifu

Yesu alitaka kuwavuvia wanafunzi wake furaha na tumaini lililokuwa moyoni mwake. Alifurahi kwa sababu karama ya Roho Mtakatifu ilikuwa ya juu kabisa kuliko karama zote ambazo angemwuomba Baba yake kwa ajili ya watu wake. Roho anayekuja ni uwezo wa kuhuisha upya maana pasipo huo, kafara ya Yesu ingekuwa bure. Uwezo wa uovu ulikuwa ukiongozeka karne hadi karne, na utiifu wa watu kwa vitendo viovu ulikuwa unashangaza Dhambi ingeweza tu kukabiliwa na kushindwa kwa uwezo wa Nafsi ya tatu ya Utatu Mtakatifu ambayo ingekuja katika uwezo tele wa Uungu. Roho huwezesha mambo yaliyokamilishwa na Mwokozi wa ulimwengu. Moyo hutakaswa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Kristo ametoa Roho wake ili kuleta ushindi dhidi ya dhambi za

kurithi na maelekeo ya kutenda uovu na kupiga chapa ya tabia yake mwenyewe juu ya kanisa lake. Sura hasa ya Mungu sharti ionekane katika wanadamu. Heshima ya Mungu, heshima ya Kristo inahusika katika kukamilisha tabia ya watu wake.

Wakati “Roho wa kweli atakapokuja, atauhakikisha ulimwengu katika habari ya dhambi na haki na hukumu.” Kuhubiri Neno [381] la Mungu hakulafaa kitu bila kuweko kwa Roho Mtakatifu. Ni pale tu Roho Mtakatifu ana poghirikiana na ukweli moyoni ndipo huleta mabadiliko na kuanzisha maisha mapya katika mtu. Roho Mtakatifu asipoiingiza kweli katika moyo wa mtu, hakuna kuanguka mwambani na kuvunjika. Hakuna kiwango cho chote cha elimu, wala manufaa hata kama ni makubwa kiasi gani yanayoweza kuwa njia ya nuru pasipo ushirikiano wa Roho wa Mungu.

Kristo ameahidi kulipa kanisa lake kipawa cha Roho Mtakatifu, na ahadi hiyo inatuhusu na sisi kama ilivyowahusu wanafunzi wa kwanza. Lakini kama ilivyo kila ahadi hutolewa kwa masharti. Wengi wanaodai kuhusika na ahadi ya Bwana huzungumzia habari za Kristo na za Roho Mtakatifu, lakini hawana kitu. Hawatoi mioyo yao iongozwe na nguvu za mbinguni. Sisi hatuwezi kumtumia Roho Mtakatifu, Roho ndiye atutumie sisi. Lakini wengi wanataka kujiongoza -wenyewe. Ni wale tu wanaomngojea Mungu kwa unyenyekevu, ndiyo hupewa Roho. Ahadi hii ya mbaraka, ikidaiwa kwa imani, itakuia na mibaraka mingine pia.

Kabla hajatoka katika chumba cha juu, Mwokozi aliwaongoza wanafunzi kuimba wimbo wa sifa. Sauti yake ilisikika, siyo kama ya maombolezo, bali yenye furaha kamili, ikiimba wimbo wa “Sifa za” Pasaka:

Haleluya Enyi mataifa yote, msifuni BWANA, Enyi watu wote, mhimidini. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu Na uaminifu wa BWANA ni wa milele.” Zaburi 117.

Baada ya kuimba walitoka kwenda katika Mlima wa Mizeituni. Walienda polepole wakitafakari kila mtu mawazoni mwake. Walipoanza kutelemka kuelekea mlimani Yesu alisema: “Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu, kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungaji, na kondoo wa kundi watatawanyika.” (Mathayo 26:3)1. Katika chumba kile cha ghorofani Yesu alikuwa amesema kuwa mmojawapo wa wanafunzi kumi na wawili alamsaliti, na Petro atamkana. Lakini sasa maneno yake yaliwahusu wao wote.

### Dhambi ya Siri ya Petro

Sasa sauti ya Petro ilisikika ikipinga "Hata wajapo kunguwazwa wote, lakini siyo mimi" Yesu alikuwa amemwonya kwamba usiku ule atamkana Mwokozi wake. Sasa akarudia onyo lake akisema, "Amini, nakuambia wewe, Leo usiku huu, kabla ya kuwika jogoo mara mbili utanikana mara tatu." Lakini Petro "akazidi sana kusema,
[382] Ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe. Na wote wakasema vile vile." Marko 14:29-31).

Petro aliposema kuwa atamfuata Bwana wake hata kama ni gerezani au kifoni, alisema kweli, lakini hakujifahamu alivyo. Katika moyo wake kulifichika chembechembe za uovu ambazo hali halisi ya mambo ingezifunua wazi. Asipotahadharishwa juu ya hali hiyo ingemwingiza katika hatari ya kupotea. Mwokozi aliona ndani yake kujipenda ambako kungelemea upendo wake kwa Kristo. Petro alihitaji kuwa na hali ya kutokujiamini na kuwa na imani kamili katika Kristo. Wakati akiwa katika bahari ya Galilaya, alipotaka kuzama, alilalama na kusema: "Bwana uniokoe." Hivyo hivyo na sasa kama angalilia na kusema niokoe katika hali hii ya kujitumainia, angalilindwa. Lakini Petro akaona kama ukatili kule kutoaminika na hivyo akazidi katika kujiamini kwake.

Yesu hakuweza kuwaokoa wanafunzi wake katika majaribu, lakini pia hakuwaacha bila faraja. Kabla ya kumkana walikuwa na uhakika wa msamaha. Baada ya kifo na ufufuo wake Kristo walielewa kuwa wamesamehewa na walikuwa wapenzi wa moyoni wa Kristo.

Yesu na wanafunzi wake walikuwa njiani kwenda Gethsemane, chini ya Mlima wa Mizeituni. Mwezi ulikuwa uking'aa na bustani ya mizeituni iliyositawi ilionekana kwake vizuri sana. Yesu akiwaelekeza wanafunzi wake kwa mizabibu hiyo, alisema "Mimi ndimi mzabibu wa kweli." Mzabibu uliozungukwa kwa vikonyo unamwakilisha yeye Mwenyewe. Miti ya minazi, mierezi na mpingo husimama peke yake; haihitaji kitu cha kuitegemeza. Lakini mizabibu hujisokotesha katika fito na hivyo kupanda kuelekea mbinguni. Vivyo hivyo na Kristo katika hali yake ya kibinadamu aliegemea uwezo wa Mungu. "Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe." Yohana 5:30.

“Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima.” Katika vilima vya Palestine Baba yetu wa mbinguni alikuwa ameupanda Mzabibu huu mzuri. Watu wengi walikuwa wakivutiwa na uzuri wa Mzabibu huu na kuusifia kuwa ni wa kutoka mbinguni. Lakini wakuu wa Israeli waliukanyaga mmea huu chini ya miguu yao miovu. Baada ya watu kudhani kwamba wameuua, Mkulima wa mbinguni aliuchukua na kupanda tena upande mwingine wa kitalu. Shina la Mzabibu lisingeonekana tena. Lilifichika lisionekane na watu wakorofi. Bali matawi yake yalining’inia ukutani ili kupitia kwayo chipukizi ya mizabibu mingine ipandikizwe kwa ule Mzabibu tena. Yesu alisema kuwa mwungano wa shina la mzabibu na matawi hufananishwa na uhusiano ambao wafuasi wake wanapaswa [383]
kudumisha kwake. Mche hupandikizwa katika Mzabibu ulio hai na hivyo kitembwe kwa kitembwe chelewa kwa chelewa hukua na kuzama katika shina la Mzabibu.

Ndivyo moyo hupata uhai kwa kuungana kwake na Kristo. Mwenye dhambi huunganisha udhaifu wake pamoja na nguvu za Kristo, uwazi wake kwa ujazo wa Kristo. Ndipo hupata nia ya Kristo. Ubinadamu wa Kristo umegusa wetu na ubinadamu wetu umegusa Uungu.

Mwungano huu lazima udumishwe. Kristo alisema, “Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu” Huu siyo muungano wa mara kwa mara. Tawi huwa sehemu ya mzabibu ulio hai. Yesu alisema Uhai mliopokea kutoka kwangu unaweza kudumishwa tu kwa muungano wa kudumu. Pasipo Mimi ninyi hamwezi kushinda dhambi, au kupinga majaribu. Lazima sisi tushikamane na Yesu na kupokea hali ya tabia yake kamilifu kwa imani.

Mzizi hupeleka lishe yake kupitia tawi hadi kijiti cha mwisho. Hivo Yesu alisema, “akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyu huzaa sana maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” Tunapoishi kwa imani katika Mwana wa Mungu, matunda ya Roho yataonekana maishani mwetu; hakuna hata moja litakalokosekana.

“Baba yangu ndiye Mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa.” Kuna uwezekano wa kuonekana kuungana na Yesu bila muungano halisi pamoja naye kwa imani. Kule kukiri dini huwawezesha watu kuwemo kanisani, lakini tabia itaonyesha ikiwa

wanao mwuungano mkamilifu na Kristo. Ikiwa hawazai matunda yo yote basi wao ni matawi ya uongo. Kristo alisema “Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya kuyatupa motoni yakateketea.”

“Na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa.” Kutoka katika wanafunzi kumi na wawili waliomfuata Yesu, mmoja kama tawi lililonyauka alikuwa karibu kuondolewa; na waliobaki walikuwa karibu kupitia chini ya kisu kisafishacho cha tanuru kali. Kupogolewa (kupunguza yasiyofaa) huumiza, lakini Baba ndiye anayepogoa. llapogoi kwa mkono wa kuumiza. Majani mengi yanayozidi na kutumia rutuba na hivyo kuhatarisha matunda lazima yaondolewe na kutupwa mbali.

Majani yote kufunika lazima yaondolewe ili yasibane tawi liza-
[384] alo; na kulizuia kupata miali ya Jua la Haki. Mkulima huondoa yale majani yanayozuia kukua kusudi matunda yawe mengi zaidi. “Hivyo hutukuzwa Baba yangu.” Yesu akasema, “kwa vile mzaavyo sana.” Mungu hutamani kujidhihirisha kupitia kwenu utakatifu, ukarimu na huruma ya tabia yake Mwenyewe. Hata hivyo Mwokozi hakuwalazimisha wanafunzi wake wafanye kazi ya kuzaa matunda. Ila huwaambia tu kukaa wao ndani yake. Kwa njia ya Neno Kristo hukaa ndani ya wafuasi wake. Maisha ya Kristo ndani yako huzaa matunda sawa sawa na ya Kristo. Kuishi ndani ya Kristo, kumfuata, ukisaidiwa na Kristo, ukipata rutuba kutoka kwake, utazaa matunda yanayofanana na Kristo.

Amri ya kwanza kabisa Yesu aliyotoa alipokuwa na wanafunzi wake peke yao katika chumba cha ghorofa ilikuwa “Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi nanyi mpendane vivyo hivyo.” Amri hii ilikuwa mpya kwa wanafunzi maana walikuwa hawapendani kama Kristo alivyowapenda. Lakini kwa njia ya maisha yake na kifo chake, wangepata maana mpya ya upendo Amri ya kupendana ilikuwa na nuru mpya kufuatana na kafara yake ya kujitolea.

Watu wanaposhikana pamoja kwa upendo wala si kwa kulazimishwa, huonyesha kutenda kazi kwa mvuto ulio juu kuliko kila mvuto wa kibinadamu. Huonyesha kuwa sura ya Mungu inaumbika ndani ya ubinadamu. Upendo wa jinsi hii ukionekana kanisani, utaamsha ghadhabu ya Shetani. “Iwapo ulimwengu ukiwachukia, mwajua ya kuwa umenichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi.

Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu. Lakini haya yote watawatenda kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliyepeleka. Injili itahubiriwa katika hali zote, katikati ya upinzani, hatari, hasara, na mateso.

Kama Mwokozi wa ulimwengu, Kristo alikabiliwa na uwezekano wa kushindwa dhahiri. Alionekana kuwa anatenda kidogo tu kuhusu kazi aliyotamani kukamilisha. Mivuto ya Shetani ilikuwa akimletea mapingamizi daima. Lakini hakukata tamaa. Kwa njia ya Isaya amesema, "Nimeiitaabisha bure, nimetumia nguvu zangu bure bila faida; lakini hakika hukumu yangu ina Bwana, na thawabu yangu ina Mungu wangu." Isaya 49:4.

Yesu alisimama katika Neno hili na hakumpa Shetani nafasi. [385]
Wakati huzuni kuu ilipoikabili nafasi yake aliwaambia kwa wanafunzi wake; "kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu wala hana kitu kwangu." "Yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa." Sasa . . . atatupwa nje. (Yohana 14:30; 16:11; 12:31.)

Knsto alijua kuwa, atakaposema "Imekwisha". mbingu yote itashangilia. Sikio lake lilisikia kwa mbali nyimbo na shangwe kuu iliyokuwa ikifanywa huko mbinguni kushangilia ushindi. Alijua kuwa jina la Kristo litatangazwa katika sayari zote na kutukuzwa. Alijua kuwa ukweli ulioimarishwa na Roho Mtakatifu utashinda katika vita dhidi ya uovu. Alijua kuwa maisha ya wanafunzi. wake waaminifu yatafanana na maisha yake, mfulululizo wa ushindi ambao haujapata kuonekana hapa lakini utakaotambulikana, hivyo katika siku ile kuu. Kristo hakushindwa wala kukata tamaa, na wafuasi wake wanapaswa kudhihirisha imani stahimilifu. vivyo hivyo. Waishi kama alivyoishi yeye na kufanya kazi kama alivyofanya. Badala ya kusikitikia matatizo, wakabiliane nayo na kushinda kukata tamaa.

Kristo alikusudia kuwa utaratibu wa mbinguni na ushirikiano wa Uungu mbinguni vionekane katika kanisa lake hapa duniani. Ili kwa njia ya watu wake apokee utukufu mwingi. Kanisa lililojaliwa na haki ya Kristo, ndiyo ghala yake ambao utajiri wa neema yake

na, upendo wake vitaonekana kwa dhahiri. Kristo huwaangalia watu wake katika usafi na utimilifu wao kama tunu ya unyenyekevu wake na nyongeza ya utukufu wake.

Kwa maneno mazito na ya tumaini Mwokozi alimalizia mafundisho yake. Alikuwa amekamilisha kazi aliyopewa kufanya. Alikuwa amelidhihirisha jina la Baba na kujikusanyia wale ambao wangeendeleza kazi yake miongoni mwa wanadamu.

Knsto sasa kama Kuhani Mkuu Aliyewekwa wakfu aliwaombea watu wake, "Baba Mtakatifu, kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo." "Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao.. Wote wawe na umoja; "ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi."

Knsto aliliweka kanisa lake teule mikononi mwa Baba. Kwake kulibakia vita ya mwisho na Shetani, naye alitoka kwenda kukabiliana navyo.

## 74 — Pambano la Kutisha Katika Gethsemane [386]

Yesu na wanafunzi wake walikwenda katika bustani ya Gethsemane. Mwezi wa majira ya Pasaka ulikuwa uking'aa sana kwa vile hapakuwepo na mawingu. Alipokaribia Gethsemane, alinyamaza kimya kwa hali isiyo ya kawaida. Katika maisha yake yote hapa duniani alikuwa akitembea katika nuru ya kuwepo Mungu. Lakini sasa alihesabiwa pamoja na wakosaji. Hatia ya wanadamu wote wa ulimwengu walioanguka lazima aibebe. Uzito wa hatia hii ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba alijaribiwa na kuogopa kuwa utamtenga milele na upendo wa Baba yake. Akapaza sauti, "Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa."

Kamwe wanafunzi walikuwa hawajapata kumwona Mwalimu wao akiwa na huzuni kiasi hicho. Mwili wake ulipepesuka kana kwamba alikuwa anataka kuanguka. Walipofika bustanini, wanafunzi walianza kutafuta pale mahali pake pa faragha, kusudi Bwana wao apate kupumzika. Mara mbili wanafunzi wake walimsaidia, la sivyo angeanguka.

Walipofika karibu na mahali pa kuingilia, Yesu aliwaacha wanafunzi wengine na kuingia na watatu akiwasihi wajiombee na kumwombea pia. Akiwa pamoja na Petro, Yakobo na Yohana aliingia ndani zaidi sehemu za faragha. Katika pambano hili kuu, Kristo aliwahitaji wawe karibu naye. Mara nyingi walipitisha saa za usiku pamoja naye mahali hapa. Baada ya kipindi cha maombi walikuwa wakilala bila usumbufu mpaka asubuhi alipowaamsha kwenda kutenda kazi upya. Sasa aliwahitaji wakeshe pamoja naye katika maombi, walakini hakuweza, kustahimili hata washuhudie maumivu makuu yaliyomkabili.

Yesu alisema: "Kaeni hapa, mkeshe pamoja nami." Alisogea [387]
mbali kidogo, ila siyo mbali sana waweze kumwona na kumsikia, akaanguka chini kifudifudi. Alijisikia kuwa kwa sababu ya dhambi alikuwa anatengwa na baba yake. Shimo lilikuwa pana sana, jeusi sana, lenye kina kirefu sana kiasi kwamba roho yake ilitetemeka mbele yake. Maumivu haya hapaswi kutumia uwezo wa kimbingu ili

kuyaepuka. Kama mwanadamu ni lazima apate adhabu ya matokeo ya dhambi ya mwanadamu. Kama mwanadamu lazima astahimili ghadhabu ya Mungu dhidi ya uasi.

## Jaribu la Kutisha

Sasa Kristo alikuwa anasimama katika hali tofauti kabisa kuliko alivyokuwa kwa wakati wote uliopita. Kristo akiwa badala ya mwanadamu alikuwa anachukua adhabu chini ya hukumu ya Mungu. Mpaka hapo alikuwa mtetezi wa wengine; sasa alitamani kupata mtetezi kwa ajili yake mwenyewe.

Huku Kristo akijisikia kuwa mwungano kati yake na Baba yake umekatika, aliogopa kwamba hangeweza kustahimili pambano lile akiwa katika hali ya kibinadamu. Shetani alikuwa amekuja kwa pambano la kutisha mwisho; kama akishindwa, ufalme wa dunia hatimaye utakuwa wa Kristo, na yeye mwenyewe atapinduliwa. Lakini ikiwa Kristo atashindwa, dunia itakuwa ufalme wa Shetani na wanadamu watakuwa chini ya mamlaka yake milele.

Shetani alimwambia Kristo kuwa ikiwa atakuwa mdhamini kwa ajili ya ulimwengu wenye dhambi, atahesabiwa mmoja katika ufalme wa Shetani, na kamwe hatakuwa na uhusiano na Mungu tena. Na sasa kafara hii itakuwa na faida gani? Shetani alizidi kusisitiza hali ilivyo kwa Mkombozi; Akasema, watu wanaojidai kuwa ni matajiri wa mambo ya kiroho kuliko wengine wote wanataka kukuangamiza. Mmoja katika wanafunzi wako atakusaliti. Mmoja katika wanafunzi wako wakereketwa atakukana. Wote watakuacha. Kwamba wale Kristo aliowapenda mno watashirikiana na Shetani katika njama zake, kuliuchoma moyo wa Kristo. Pambano lilikuwa la kutisha mno. Dhambi za watu wote zilimlemea sana Kristo na kule kufahamu ghadhabu ya Mungu juu ya dhambi kulikuwa kunaponda uhai wake.

Katika uchungu wake alikumbatia ardhi, kama kujizuia asiondolewe mbali zaidi na Mungu. Kutoka katika midomo iliyokauka kulitoka kilio cha uchungu, “Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke, nisipokunywa mapenzi yako yatimizwe.”

### Yesu Alitamani Huruma za Kibinadamu [388]

Roho ya binadamu hutamani sana kupata huruma wakati wa mateso. Kristo alishikwa na kiu hii hadi katika kina ya Umbile lake. Aliwajia wanafunzi wake akitamani kusikia maneno yenye faraja. Alitamani kujua kuwa wanamwombea yeye na kujiombea pia. Uovu wa dhambi ulionekana kuwa giza kiasi gani!. Jaribu la kutaka kuwaachia wanadamu wabebe hatia yao wenyewe, wakati Mwenyewe akiwa hana hatia mbele za Mungu lilitisha nmo. Ikiwa tu angelijua kuwa wanafunzi wake wanamwunga mkono, angepata nguvu na kufarijika.

Lakini "akawakuta wamelala usingizi." Kama angaliwakuta wakitafuta maficho kwa Mungu, ili nguvu za Shetani zisiweze kuwashinda, angalifarijika. Lakini lile onyo la "Kesheni, na kuomba." Hawakuwa wamejali wakukusudia kumkana Bwana wao, lakini ilionekana kuwa wamepigwa na fadhaa ambayo wangeishinda kama wangeendelea kumsihi Mungu kwa maombi. Wakati Mwokozi alipohitaji mno maombi yao, walilala usingizi.

Wanafunzi waliamshwa na sauti ya Yesu, lakini hata kidogo hawakumtambua, uso wake ulikuwa umebadilika kwa huzuni. Yesu alimwambia Petro, Je "Simoni, umelala? Hukuweza kukesha saa moja? Kesheni muombe, msije rnkaingia majaribuni; roho i radhi ila mwili ni dhaifu." Yesu aliogopa kuwa katika hali hiyo waliyo nayo hawataweza kustahimili kusalitiwa kwake na kifo chake.

Mara tena Mwana wa Mungu akashikwa na uchungu usiokuwa wa kibinadamu, akizimia' na kutaabika alijikokota kurudi mahali pa pambano lake la awali. Maumivu yake yalikuwa makali kuliko mwanzo. "hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka chini." Miti ya mitende na mingine ilikuwa ndiyomashahidi wa uchungu wake. Kutoka katika majani ya matawi yake yalidondoka matone mazito ya umande, juu ya mwili wake uliodhoofika kana kwamba viumbe vya asili vilimlilia Mwumbaji wao akipambana mwenyewe dhidi ya nguvu za giza.

Muda si kitambo, Yesu alikuwa amesimama imara kama mwerezi, kukabiliana na dhoruba ya upinzani uliokuwa umemalizia hasira yake kwake. Sasa alifanana na mwanzi mwororo ulipigwa na kukunjwa na dhoruba yenye hasira. Kama aliyetukuzwa tayari,

alikuwa amedai umoja na Mungu. Sasa sauti yake ikasikika katika upepo uliotulia wa jioni ikiwa imejaa uchungu wa kibinadamu:

"Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe."

[389] Kwa mara nyingine tena Yesu alitamani maneno ya faraja kutoka kwa wanafunzi wake ambayo yangemwondolea kivuli cha giza lililotanda karibu litamshinda. Lakini macho yao yalikuwa mazito kwa usingizi, "wala hawakujua la kumjibu." Waliuona uso wake umejaa jasho la damu, kutokana na mahangaiko makuu, lakini uchungu wa mahangaiko ya mawazo wanafunzi wake hawakuweza kuelewa. "(Uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu ye yote, na umbo lake zaidi ya wanadamu)." (Isaya 52:14).

## Wakati Hali ya Baadaye ya Ulimwengu ilipotetemeka kwenye Mizani

Yesu akigeuka, kwenda mahali pale pa kuombea alianguka kifudifudi. Hali ya Ubinadamu ya Mwana wa Mungu ilitetemeka katika saa ile ya majaribu. Saa ya kutisha ya kuamua, hali ya baadaye ya ulimwengu ilikuwa imewadia. Hali ya baadaye ya jamii ya walimwengu ilitetemeka katika mizani. Kristo angeweza hata wakati huu akatae kukinywea kikombe kilichogawiwa kwa Mwanadamu mwenye hatia. Angeweza kujipangusa jasho lake la damu na kumwacha mwanadamu kupotea katika uovu wake. Angeweza kusema, muwache mwenye dhambi apokee adhabu ya dhambi yake, mimi nitarudi kwa Baba yangu. Je, asiye na hatia ateseke kwa ajili ya matokeo ya laana ya dhambi, kuwaokoa wenye hatia? "Baba yangu, uniondolee kikombe hiki; walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe."

Mara tatu alinywea kwa hofu asikaribie hatua ya mwisho ya kukamilisha kafara. Lakini sasa anaona kuwa jamii ya mwanadamu haina msaada. Anaona nguvu za dhambi. Misiba ya ulimwengu unaoangamia iliinuka mbele yake, anaona ajali yake iliyo karibu sana, naye anafanya uamuzi. Atamwokoa mwanadamu kwa gharama yo yote ile. Ametoka mbinguni ili kuja kuiokoa dunia moja iliyo anguka katika uasi. Na hawezi kurudi nyuma kwa utume wake. Baada ya kuamua, alianguka chini kama mfu. Wanafunzi wake wako wapi sasa wapate kumwinua Bwana wao aliyezimia? Mwokozi

alikanyaga shinikizo peke yake, wala hakuna mtu aliyekuwa pamoja naye. (Tazama Isaya 63:3).

Lakini Mungu aliteseka na Mwanaye. Malaika waliona masumbuko yake. Mbinguni kulinyamaza kimya. Hakuna sauti ya kinubi iliyosikika huko. Malaika wakinyamaza kwa huzuni, walimwangalia Baba akiondoa miali yake ya nuru upendo na utukufu kutoka kwa Mwanawe mpendwa.

Shetani na jeshi lake ovu waliangalia kwa makini. Maombi ya [390]
Kristo aliyoomba mara tatu kuhusu kikombe yatajibiwaje? Wakati huu wa kutisha, wakati kikombe kile cha siri kilipotingishwa mkononi mwa mteswa, yule malaika mkuu anayesimama mbele za Mungu, alikuja na kuwa kando ya Kristo. Malaika hakuja kumwondolea Kristo kikombe mkononi, bali alikuja kumhakikishia kuwa Baba yake bado anampenda. Alimhakikishia kwamba kifo chake kitamshinda Shetani kabisa, na kwamba ufalme wa ulimwengu huu watapewa watakatifu wa Mwenyezi Mungu, na alimwambia kwamba ataona umati wa watu wa ulimwengu wakiokolewa, na kuokolewa milele.

## Jinsi Sala ya Kristo Ilivyojibiwa

Maumivu ya moyo ya Kristo hayakukoma, ila unyong'onyevu na kukata tamaa vilimtoka. Dhoruba haikuwa imekoma lakini alitiwa nguvu ili kukabili ghadhabu yake. Amani ya mbinguni ilitua juu ya uso wake uliokuwa na damu. Amestahimili mambo ambayo mwanadamu hawezi kuyastahimili; maana alionja mauniivu ya kifo kimpasacho kila mtu.

Wanafunzi waliokuwa wamelala waligutuka, kwa ghafula, wakamwona malaika. Wakamsikia akimwambia Mwokozi maneno ya faraja na tumaini. Sasa hawakuwa na hofu tena kwa ajili ya Bwana wao; maana alikuwa katika ulinzi wa Mungu. Mara nyingine tena wanafunzi wakashindwa na uzito wa usingizi na kwa mara nyingine tena Yesu akawakuta wamelala.

Yesu akiwatazama kwa masikitiko akasema: "Laleni sasa, mpumzike; yatosha, saa imekuja tazama, na Mwana wa Adamu sasa anatiwa mikononi mwao wenye dhambi." Hata alipokuwa akisema hayo, alisikia vishindo kundi kubwa likimtafuta, na akasema, "Ondokeni, twende zetu; tazama yule anayenisaliti amekaribia."

Huzuni na maumivu yaliyokuwako kwa Yesu havikuonekana tena, wakati akienda kukutana na msaliti wake. "Ni nani mnayemtafuta? Wao wakamjibu: "Ni Yesu Mnazareti."

Yesu akawajibu "Ni mimi." Aliposema hivyo, malaika aliyekuwa akimhudumia Yesu alipita kati ya kundi hilo na Yesu. Nuru ya uungu ikaangaza uso wa Mwokozi. Mbele ya utukufu huu kutoka mbinguni, hili kundi la wauaji wenye ghasia, likapepesuka kurudi nyuma. Hata Yuda naye akaaanguka chini.

Malaika akatoweka, na ile nuru ikafifilia mbali. Yesu alikuwa [391] na nafasi ya kutoroka lakini aliendelea kubakia pale pale kati ya wakaidi hao, waliokuwa wakigaagaa chini bila msaada.

Mara moja mambo yalibadilika. Askari wa Kirumi, makuhani, pamoja na Yuda walimzunguka Yesu, wakiwa na wasiwasi kwamba atatoroka. Walikuwa wamepata ushahidi wa kutosha kuwa aliyesimama mbele zao alikuwa Mwana wa Mungu, lakini hawakutaka kusadiki. Kuhusu swali la kuwa "Ni nani mnayemtafuta?" Tena wakajibu, "Yesu Mnazareti." Ndipo Mwokozi akasema "Nimekwisha kuwaambieni ya kwamba ni mimi; basi ikiwa mnanitafuta mimi waacheni hawa waende zao," akiwasonda wanafunzi. Kwa ajili yao alikuwa tayari kujitoa mhanga.

Yuda msaliti hakusahau sehemu yake. Alikuwa amewapa ishara waliokuwa wanamtafuta Yesu, akisema, "Nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni mkamchukue salama." Sasa, akimkaribia Yesu alimshika mkono kama rafiki akisema: "Salamu Rabi, akambusu mara kadhaa, na alionekana kana kwamba analia kwa kumsikitikia katika hatari yake.

Yesu akasema: "Rafiki, fanya ulilolijia." Huku sauti yake ikitetemeka kwa huzuni, akaongeza, Yuda, wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?" Maneno haya yalipasa kugusa dhamiri ya msaliti, lakini heshima na huruma ya kibinadamu vilikuwa vimemtoka. Alikuwa amejitolea kwa Shetani, na hakuwa na uwezo wa kumpinga. Yesu hakukataa busu ya msaliti.

Lile kundi la watu sasa likamkamata Yesu, na kuanza kuifunga mikono ile iliyokuwa ikitumika katika kutenda mema.

Wanafunzi walikatishwa tamaa na kukasirishwa walipoona kamba zikitolewa kufunga mikono ya yule waliyempenda. Petro kwa hasira akatoa upanga na kumkata sikio mtumishi wa Kuhani Mkuu. Yesu alipoona haya aliondoa mikono yake ingawa ilishik-

iliwa na askari wa Kirumi kwa nguvu, akasema: "Mwe radhi kwa hili." Akamgusa sikio akamponya mara moja.

Kisha akamwambia Petro, "Rudisha upanga wako mahali pake; maana wote waushikao upanga wataangamia kwa upanga. Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?" Jeshi badala ya kila mwanafunzi. Aa, Kwa nini, wanafunzi wake walifikiri hajiokoi nafsi yake na sisi? Akijibu mawazo yao akaongeza, "Yatatimizwaje maandiko, ya kwamba hivyo ndivyo vilivyopasa kujiri?" Je! kikombe alichonipa Baba mimi nisikinywee?"

Makuhani wadanganyifu na wazee walikuwa wamefuatana na [392]
polisi wa hekalu na kundi la watu wakipiga makelele katika kumfuata Yuda mpaka Gethsemane. Hawa waheshimiwa walifuatana kundi la ajabu kiasi gani kundi lililojivika silaha, kana kwamba linafukuza mnyama wa porini!

Kristo akiwageukia makuhani na wazee, alisema maneno ambayo hawatayasahau kamwe; "Je, mmetoka kama kumkamata mnyang'anyi, wenye panga na marungu, ili kunishika? Kila siku naliketi hekaluni nikifundisha, msinikamate." Usiku ndio unaowafaa mfanye kazi yenu. Lakini hii ndiyo saa yenu, na mamlaka ya giza."

Wanafunzi walishikwa na hofu walipoona Yesu anajiruhusu kukamatwa na kufungwa. Walichukizwa kwamba anadhalilishwa hivyo pamoja na wao. Ha-wakuweza kuelewa huu msimamo wake, na wakamlaumu kwa kujisalimisha. Katika ghadhabu na woga wao, Petro akapendekeza wajiokoe wenyewe. Wakikubaliana na wazo hilo, "wote wakamwacha, wakakimbia."

[393] # 75 — Kesi Batili Dhidi ya Yesu

Yesu aliharakishwa kupitia mitaa iliyokuwa kimya ya jiji lililokuwa limelala. Ilikuwa baada ya usiku wa manane. Akiwa amefungwa na kulindwa sana, Mwokozi alitembea kwa maumivu mpaka katika jumba la kuhani mkuu mstaafu, Anasi. Anasi alikuwa kiongozi wa jamaa ya ukuhani wa zamu, kwa kuwa alikuwa na umri mkubwa, watu walimheshimu kama kuhani mkuu. Shauri alilokuwa akitoa lilihesabiwa kana kwamba ni sauti ya Mungu. Kwa, hiyo ilimpasa awepo kwenye kumhoji mshitakiwa kwa sababu ya wasiwasi kwamba Kayafa ambaye ndiye kuhani mkuu hana uzoefu mkubwa hivyo angeshindwa kutekeleza kusudi lao. Hila na ujanja wake vilihitajika, maana Kristo lazima apatikane na hatia.

Kristo alikuwa ashitakiwe mbele ya Baraza kuu la Kiyahudi (Sanhedrin) lakini kwanza afikishwe mbele ya Annas kwa kuhojiwa. Chini ya sheria ya Kirumi, baraza kuu la Kiyahudi (Sanhedrin) lilikuwa na uwezo wa kuhoji na kisha kupitisha hukumu ambayo ilibidi kuthibitishwa na mamlaka ya Kirumi. Kwa hiyo ilibidi Kristo ashtakiwe na kosa ambalo lingeonekana kuwa la jinai mbele ya Warumi na pia mbele ya Warumi na pia mbele ya Wayahudi. Sio watu wachache waliongolewa na mafundisho ya Kristo, baina ya makuhani na wakuu. Yusufu wa Arimathaya na Nikodemo, hawataulizwa shauri hili, lakini wengine huenda wakathubutu kusema katika shauri hili. Lazima Sanhedrin liwe na umoja katika kusikiliza shauri dhidi ya Kristo. Makuhani walidhamiria kumshitaki kwa mambo mawili. Kama Yesu atathibitishwa kuwa ni mkufuru atahukumiwa na Wayahudi. Akithibitishwa kuwa ni mhaini, yaani mchochezi ili watu waasi serikali, atahukumiwa na Warumi.

[394] Shitaka la pili Anasi alijaribu kulithibitisha kwanza. Alimhoji Yesu akitumaini kuwa atasema kitu fulani kitakachothibitisha alitaka kuanzisha chama cha siri kwa kusudi la kuanzisha ufalme wake. Na hivyo makuhani watamkabidhi kwa Warumi kuwa ni muanzishaji wa uasi. Kana kwamba anasoma mawazo ya ndani ya aliyemhoji.

Kristo alikana kwamba hakukusanya watu kwa siri ili kuficha nia yake. Akasema "Mimi nimesema na ulimwengu waziwazi; siku zote nalifundisha katika sinagogi na katika hekalu, wakusanyikapo Wayahudi wote; wala kwa siri mimi sikusema neno lo lote."

Mwokozi alitofautisha jinsi ya kazi yake na mbinu za waliomshitaki. Walimwinda ili wampate na kumshitaki mbele ya mahakama ya siri ambapo wangepata kwa uongo kile ambacho wasingekipata kwa haki. Kule kukamatwa usiku wa manane na kundi la watu, dhihaka na matusi aliyokabili hata kabla ya kushtakiwa ilikuwa kawaida yao ya kutenda kazi na siyo yake. Kitendo chao kilikuwa ukiukaji sheria. Hata kanuni zao husema kuwa kila mtu anapaswa kuhesabiwa kuwa hana hatia mpaka athibitishwe kuwa ni mkosaji.

Yesu akimgeukia mshitaki wake, alisema: "Ya nini kuniuliza mimi? Je, wapelelezi hawakuwepo katika kila mkutano na kuwapa habari makuhani juu ya mambo aliyosema na kufanya?" Waulize wale waliosikia ni nini niliyowaambia; wao wanajua niliyonena."

Anas alinyamazishwa kabisa. Mmoja wa maofisa watu wake alikasirika, akampiga Yesu usoni, akisema: "Wamjibu hivi Kuhani Mkuu?" Kristo akamjibu kwa upole:

"Kama nimesema vibaya, ushuhudie ule ubaya; bali kama nimesema vema, wanipigia nini?" Jibu lake la upole lilitoka katika moyo wa usiokuwa na dhambi, mvumilivu na mwungwana; usiowezakuchokozeka.

Mikononi mwa viumbe ambavyo kwavyo, alikuwa anatoa kafara isiyo na kifani, Kristo alipokea kila aina ya dhalilisho. Na aliteseka kadiri ya utakatifu wake na chuki yake dhidi ya dhambi. Kuhukumiwa kwake na watu waliojifanya dhalimu ilikuwa kwake ni kafara ya milele. Kuzungukwa na wanadamu waliokuwa chini ya madaraka ya Shetani lilikuwa jambo la kuchukiza. Na alijua kuwa kwa kuutokeza ghafla uwezo wake na Uungu angewafanya watesi wake wote wakatili kuwa mavumbi. Hali watesi hii ilifanya mateso yake kuwa magumu sana kuvumilia.

Wayahudi walimtazamia Masihi atakayetumia Uungu wake kugeuza mtiririko wa mawazo ya watu na kulazimisha waukubali ukuu wake. Hivyo Kristo alipodhalilishwa, lilimjia kwa nguvu jaribu [395]
la kutaka kudhihirisha uwezo wa tabia yake ya Uungu, kuwashurutisha watesi wake kukiri kuwa alikuwa Bwana juu ya wafalme,

watawala, makuhani na hekalu. Ilikuwa vigumu kudumisha hali aliyoichagua ya kama mmoja na wanadamu.

### Malaika Wangalifurahi Kumwokoa Kristo

Malaika wa mbinguni walitamani kumwokoa Kristo. Kama ingalilazimu kumwokoa, wangaliharakisha kumwondoa kwa upesi gani kiasi katika fedheha hiyo, na kuwaangamiza maadui hao wa Mungu! Lakini waliagizwa wasifanye hivyo. Maana ilikuwa ni sehemu ya kazi yake ya ukombozi kupitia katika fedheha zote hizo, kadiri ambavyo wanadamu wangemtwisha.

Kristo hakusema lo lote kuwapa mwanya waliomshitaki, lakini hata hivyo alifungwa kuonyesha kuwa alikuwa amehukumiwa. Lakini hata hivyo, sharti uwepo mfano wa kusikiliza kesi kisheria. Hilo watawala walikusudia kuharakisha: Walijua watu walivyompenda Yesu, na kuhofia kuwa wangejaribu kumwokoa. Na pia, kama wangekawia kutekeleza hukumu, mara moja, wangalipaswa kungojea kwa juma moja kwa sababu ya Pasaka. Mambo haya yangaliharibu mipango yao. Kama wangalingojea juma jingine, kungetokea upinzani. Wangalitokea mashahidi wengine wenye ushuhuda kuonyesha hana hatia na kudhihirisha matendo makuu aliyotenda Mashitaka ya Sanhedrin yangalikosolewa na Yesu angalifunguliwa. Kwa hiyo Makuhani na wakuu waliazimia kuwa kabla ya kugundulika. kusudi lao, Yesu lazima atiwe mikononi mwa Warumi.

Lakini kwanza, shitaka lazima lipatikane. Mpaka hapo walikuwa hawajapata la kumshitaki. Anasi aliagiza Yesu apelekwe kwa Kayafa. Ingawa hakuwa na tabia nzuri Kayafa alikuwa mkatili na mbaya kama Anasi. Ulikuwa sasa mapambazuko, na bado giza wakati kundi lenye silaha pamoja na mahabusi walipokwenda: kwa kuhani mkuu. Wakati Sanhedrini likikusanyika, Anasi na Kayafa kwa mara nyingine walimhoji Yesu maswali bila mafanikio.

Ndani ya jumba la mahakama Kayafa alikalia kiti. Katika upande walikaa wahukumu na wasikilizaji wah usika. Askari wa Kirumi waliketi juu ya jukwaa chini ya kiti cha hukumu. Yesu alisimama mbele ya kiti cha enzi. Hali ilikithiri sana. Yesu peke yake ndiye aliyekuwa kimya na mmtulivu.

[396] Kayafa alikuwa akimuona Yesu kuwa ni mpinzani wake. Ile hamu ya watu ya kutaka kusikia mafundisho ya Mwokozi, ilichochea

wivu wa kuhani mkuu juu ya Yesu. Lakini sasa Kayafa alipomtazama mshitakiwa aliguswa na hali yake ya heshima na utukufu. Akakiri wazi kuwa mtu huyu ni mwenye asili ya Uungu, Kwa muda uliofuata wazo likatoweka, na kwa kejeli akamtaka Yesu atende mojawapo ya miujiza yake mikuu. Lakini maneno yake yalianguka masikioni pa Mwokozi kana kwamba hakuyasikia. Katika mawazo ya watu hawa wakaidi swali likajitokeza, Je! huyu mtu mwenye mwonekano wa Uungu ahukumiwe kama mhalifu?

Maadui wa Yesu walipigwa butwaa. Jinsi ya kukamilisha hukumu yake hawakujua. Kayafa alitaka kujiepusha na kuanzisha ubishi. Kulikuwa na mashahidi wengi wa kuthibitisha kuwa Yesu aliwaita makuhani na waandishi kuwa ni wanafiki na wauaji lakini haya yasingefaa kwa wakati huu. Ushahidi kama huo haungekuwa na nguvu mbele ya serikali ya Kirumi. Kulikuwa na ushahidi mwingi kuwa Yesu alidharau mambo mengi kuhusu kanuni za Wayahudi. Ushahidi kama huo pia usingekuwa na nguvu mbele ya serikali ya Kirumi. Maadui wa Kristo hawakuthubutu kumshitaki na uvunjaji wa Sabato, kusudi mahojiano yake yasije yakaweka wazi miujiza yake ya kuponya.

Mashahidi wa uongo walikuwa wamenunuliwa ili kutoa ushahidi kuwa Yesu alikuwa na mpango wa kuanzisha serikali nyingine. Lakini ushahidi wao haukuwa dhahiri, na ulipingana. Walipohojiwa walisema uongo.

Mwanzoni mwa kazi yake, Kristo alisema: "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha." Hivyo alikuwa akitabiri juu ya kifo chake, na ufufuo. "Lakini yeye alinena habari za hekalu la mwili wake." Yohana 2:19, 21. Lakini katika mambo yote Kristo aliyosema, makuhani hawakuweza kupata kitu cho chote cha kumkandamizia, isipokuwa hili. Warumi walikuwa wamelijenga upya na kulipamba hekalu na hivyo walilijivunia, hivyo dalili yo yote iliyoonyeshwa juu yake, ingeamsha hasira yao. Katika hilo Warumi na Wayahudi walikubaliana; kwa sababu wote walilitukuza sana. Wali-shirikiana katika kuliheshimu.

Shahidi mmoja aliyenunuliwa kumshtaki Yesu. Akasema, "Mtu huyu alisema kuwa atalivunja hekalu hili la Mungu, na kulijenga katika siku tatu." Kama maneno ya Yesu yalingalinukuliwa vizuri kama alivyoyasema yasingetumiwa kumtia hatiani hata na Sanhedrini. Maneno yake yangeonyesha kuwa ni tamko la ovyo la

kujivuna lakini siyo kufuru. Hata baada ya kuchanganywa uongo na
[397] mashahidi wa uongo maneno yake hayakuwa na lo lote la kufikiriwa na Warumi kuwa ni kosa listahililo kuhukumiwa kifo.

Mwishowe washitaki wa Yesu walichanganyikiwa, wakawa kama wenda wazimu. Ilionekana kuwa njama yao inashindwa. Kayafa akakata tamaa kabisa. Kitu kimoja kilibaki; lazima Kristo alazimishwe ajitie hatiani mwenyewe. Kuhani mkuu alianza kutoka kitini akiwa amekunja uso kwa hamaki; "Hujibu neno?" akaamuru; Hawa wanakushuhudia nini?"

Yesu alikaa kimya "Alionewa, lakini alinyenyekea,

Wala hakufunua kinywa chake;
Kama mwana kondoo apelekwaye machinjoni,
Na kama vile kondoo anyamazavyo Mbele yao wakatao manyoya yake;
Naam, hakufunua kinywa chake."

Isaya 53:7.

Mwishowe Kayafa alimwapisha Yesu akisema: "Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu." Kwa ombi hilo Kristo hakuweza kunyamaza. Alijua kuwa akijibu sasa atahakikisha kifo chake. Lakini ombi lilitolewa na mamlaka kuu ya taifa, na katika jina la Mungu aliye juu. Hivyo lazima adhihirishe wazi tabia yake na utume wake. Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake, "Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni." Mattayo 10:32. Sasa kwa mfano wake mwenyewe akarudia somo hilo. Kila jicho lilikaziwa kwa uso wa Yesu huku akajibu "Wewe umesema; " Ilionekana kana kwamba nuru kutoka mbinguni iliangaza sura yake iliyojaa mfadhaiko, ndipo akaongeza kusema, "lakini nawaambieni, Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni." Kwa muda mfupi kuhani mkuu alitetemeka mbele ya jicho kali la Mwokozi. Kamwe katika maisha yake baadaye hakusahau hili tazamo kali la Mwana wa Mungu aliyekuwa matesoni.

## Kayafa Katibu Kuamini

Wazo kwamba watu wote watasimama mbele ya hukumu ya kiti cha Mungu na kupokea kila kinachostahili matendo waliyotenda lilikuwa tishio kwa Kayafa. Mawazoni mwake aliona siku hiyo ya hukumu ya mwisho. Kwa muda mfupi aliona makaburi yakiwatoa wafu pamoja na siri alizodhani kuwa hazitajulikana milele. Akajisikia kana kwamba Jaji Mkuu alikuwa anasoma moyo wake na kutoboa siri zilizodhaniwa zimefichika katika wafu. [398]

Kayafa alikuwa amekana ufufuo wa wafu, hukumu, na maisha ya baadaye. Sasa alikuwa kana kwamba amepata wazimu. Akirarua mavazi yake, alitamka kuwa mtu huyu anastahili kuhukumiwa kwa kukufuru; "Tuna haja gani tena ya mashahidi?" "Tazameni, sasa mmesikia hiyo kufuru yake; mwaonaje ninyi?" Na wote wakamhukumu kuuawa, Kayafa alighadhabika kwa kule yeye kuyaamini maneno ya Kristo, na badala ya kurarua moyo wake na kukiri kuwa Yesu alikuwa Masihi, akararua Mavazi yake ya kikuhani katika jitihada ya kupinga. Kitendo hiki kilikuwa na maana kubwa. Katika kuhakikisha kuwa Kristo anahukumiwa kifo, kuhani mkuu alikuwa amejihukumu mwenyewe. Chini ya sheria ya Mungu iliyohusu ukuhani alikuwa hafai kuwa kuhani. Alikuwa amejihukumu mwenyewe stahili ya kifo.

Kuhani Mkuu hakupaswa kurarua mavazi yake ya ukuhani. Sheria ya Walawi ilikataza kabisa kuhani kurarua vazi lake. Kristo alikuwa ametoa agizo hilo kwa Musa. (Tazama Walawi 10:6). Mwanadamu aliye na kikomo cha maisha anaweza kurarua moyo wake kwa kujuta kwa kosa lo lote. Lakini vazi la kikuhani haliraruliwi kamwe, maana hili huwakilisha vitu vya mbinguni, na kwa hiyo likiraruliwa huvinajisi. Kuhani mkuu yeyote anayethubutu kuhudumu na hali vazi lake limeraruliwa huwa amejitenga mbali na Mungu. Jambo lililofanywa na Kayafa lilionyesha ufedhuli na upungufu wa kibinadamu.

Kwa kuyararua mavazi yake, ya ukuhani Kayafa, alibatilisha sheria za Mungu, kwa kufuata mapokeo ya kibinadamu. Kanuni ya wanadamu ilisema kuwa mtu akikufuru, kuhani angerarua mavazi yake katika kuonyesha chuki kwa dhambi na asiwe na kosa. Hivyo sheria ya Mungu ilibatilishwa na mapokeo ya wanadamu. Lakini

katika kitendo hiki, yeye mwenyewe alikuwa anatenda kosa la kufuru.

Kayafa aliporarua vazi lake; kitendo hicho kilikuwa na maana ya nafasi itakayochukuliwa baadaye na taifa la Wayahudi mbele za Mungu. Wayahudi walikuwa wamemkataa yule ambaye alikuwa asili ya mifano ya uhakika wa mategemeo yao yote. Waisraeli walikuwa wamejitenga na Mungu. Na huenda Kuhani Mkuu alirarua vazi lake kujihofia binafsi na kwa ajili ya taifa lote.

### Udhalimu wa Hukumu ya Kristo

Baraza la Sanhedrin lilikuwa limemhukumia Yesu kufa, lakini
[399] ilikuwa kinyume cha Wayahudi, kumhukumu mshtakiwa wakati wa usiku. Kisheria hukumu ilitolewa tu wakati wa mchana na mbele ya Baraza lililohudhuriwa na wajumbe wake wote. Hata hivyo Mwokozi sasa alitendewa kama mhalifu aliyehukumiwa, na watu duni. Yesu alipitishwa huku na huko, katika uwanja wa jumba la kuhani mpaka chumba cha askari, na huku akidhihakiwa kutokana na madai ya kuwa Mwana wa Mungu. Maneno aliyosema kuwa watamwona "akija mawinguni kutoka mbinguni", yalikaririwa mara nyingi kwa dhihaka. Alipokuwa amefungiwa chumbani akingojea kuhukumiwa, hakulindwa asitendewe vibaya na wahuni, na hivyo wahuni walimtendea kila aina ya ufedhuli walivyoweza. Hali ya Kristo ya utawa iliwachochea kwa hasira. Huruma na haki vilikanyagwa chini. Hakuna mfungwa aliyepata kutendewa kama alivyotendewa Mwana wa Mungu. Lakini pigo lililoumiza zaidi kuliko ambavyo mkono wa adui ungeleteleza. Wakati alipokuwa akihojiwa na Kayafa, Kristo alikuwa amekanwa na mmoja wa wanafunzi wake.

Petro na Yohana walikuwa wamethubutu kufuata kwa mbali kundi lililokuwa limemkamata Yesu. Makuhani walimtambua Yohana, na kumruhusu aingie katika ukumbi, wakitumaini kuwa akiona jinsi wanavyomtesa, atamkana na kusema kuwa yeye siye Mwana wa Mungu. Yohana alimtambulisha Petro, naye akaingia ndani pia. Pale nje ya ukumbi waliwasha moto, maana ilikuwa baridi, kabla ya mapumziko. Kikundi cha watu wakakusanyika hapo na Petro naye bila kujali akasogea na kuchanganyika nao na kuketi akidhani kuwa atachukuliwa kuwa ni mmoja wapo wa mkutano waliokuwa wamemleta Yesu kuhukumiwa.

## Petro Ashindwa

Lakini mwanamke aliyekuwa bawabu mlangoni, alimwangalia sana Petro, akamwona kuwa mwenye masikitiko na wasiwasi, akamhisi kuwa ni mmoja katika wanafunzi wa Yesu. Akitaka kujua akamwuliza: "Wewe nawe u mmoja wao?" Petro alishituka na kuchanganyikiwa: akijifanya kana kwamba hana habari juu ya mambo hayo. Lakini mwanamke aliendelea kukuzania hivyo. Petro akalazimika kujibu na kusema kwa hasira: "Sijui usemalo." Hili lilikuwa kanusho la kwanza, na mara ile jogoo akawika. Katika hali ya kutojali, Petro alikuwa amejiweka katika hali ya kuwa mwepesi kwa majaribu.

Watu walimkazia macho mara ya pili. Na akasutwa kuwa ni mmojawapo wa wanafunzi wa Yesu. Sasa Petro akaapa, na [400]
kusema: "Mimi simjui mtu huyu." Saa moja ilipita, wakati jamaa ya mtu yule aliyekatwa sikio na Petro huko katika bustani aliposema: "Je! mimi si nimekuona wewe bustanini pamoja naye?" "Hakika na huyu alikuwa pamoja naye, kwa kuwa yeye pia ni Mgalilaya." Kusikia hivyo Petro alijaa hasira. Ili kuwadanganya hasa waliokuwa wanamhoji na kuthibitisha msimano wake, Petro sasa akamkana Bwana wake kwa kuapa na kulaani. Kwa mara nyingine jogoo aliwika. Petro aliposikia jogoo akiwika, aliyakumbuka maneno aliyoambiwa na Yesu, "Kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu." Marko 14:30.

Wakati kiapo cha aibu kilipokuwa kingali kipya mdomoni mwa Petro na mlio wa jogoo ungali ukisikika masikioni, Mwokozi aligeuza uso wake akamtazama usoni masikini mwanafunzi wake. Kwa wakati huo macho ya Petro yakavutwa kumwangalia Bwana wake. Katika ule uso mpole aliona huruma na huzuni na sio hasira.

Kuutazama ule uso wa huzuni, ile midomo iliyotetemeka, moyo wake ulichomwa kama na mshale. Petro alikumbuka ahadi aliyoahidi, muda kitambo uliopita, wakati Mwokozi alipomwambia kuwa, atamkana mara tatu usiku ule. Petro sasa akatambua jinsi Bwana alivyokuwa amesoma sawasawa mawazo yake yenye udanganyifu ambao haukujulikana kwake yeye. Wimbi la kumbukumbu likafunika. Uvumilivu wa Mwokozi, kusitahimili kwake yote hayo yalikumbukwa. Akakumbuka kwa hofu juu ya uongo wake na ushuhuda wake katika kumkana Bwana kwa kuapa. Mara akaona

mkono wa mtu mkorofi ukiinuliwa kumpiga Bwana wake usoni. Akiwa hawezi kuvumilia, zaidi hali hiyo, aliharakisha kutoka katika ukumbi huo akiwa amevunjika moyo. Aliendelea katika upweke na giza akiwa hajui wala kujali aendako. Mwisho akajikuta amefika katika Gethsemani.

Alikumbuka kwa uchungu mwingi jinsi alivyokuwa na maumivu makali akiomba peke yake, pia alikumbuka agizo Yesu alilowaagiza akisema: "Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni." Mathayo 26:41. Jambo hili lilikuwa mateso rohoni mwake akijua kuwa amemwongezea Mwokozi mzigo wa udhilifu na huzuni. Petro akaanguka chini kifudifudi akitamani kufa. Kama saa zile walipokuwa katika bustani wanazitumia katika kukesha na kuomba, Petro asingelikuwa katika hali ya kutegemea nafsi yake dhaifu. Wala asingalimkana Bwana wake. Kama wanafunzi wangalikesha pamoja na Yesu katika
[401] mateso yake wa-ngalikuwa tayari kuyaona pia mateso yake msalabani. Katikati ya saa ngumu ya huzuni, tumaini lingewasha giza lao na kuitegemeza imani yao.

### Jitihada Dhati Kutaka Kumhukumu Yesu

Mara tu kulipopambazuka Sanhedrini ilikutana, tena na Yesu kwa mara nyingine aliletwa mbele yao. Alikuwa amesema kuwa yeye ni Mwana wa Mungu, lakini hawakuweza kumtia hatiani kwa jambo hili, kwa sababu Yesu aliposema hivyo ilikuwa wakati wa usiku na watu wengi hawakuwepo na hivyo hawakuwa wamesikia maneno yake. Na walijua kuwa Warumi hawawezi kuona hilo kuwa ni kosa linalostahili adhabu ya kifo. Lakini watu wengi wakisikia wazi akisema kuwa yeye ni Masihi, wangeatafsiri hilo kuwa ni kosa la uchochezi dhidi ya serikali.

Wakasema, "Kama wewe ndiwe Kristo, tuambie." Lakini Kristo alinyamaza kimya. Wakakazana kumwuliza, maswali. Hatimaye akajibu, "Nijapowa-ambia, hamtasadiki kabisa, tena, nikiwauliza, hamtajibu, wala hamtaniachia." Lakini akaongeza onyo la dhati, "Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa Mungu Mwenyezi." Wakasema, wote "Basi, wewe ndiwe Mwana wa Mungu?" "Akawaambia, Ninyi mwasema kwamba mimi ndiye. Wakasema, "Basi, tuna haja gani tena ya ushuhuda? maana, sisi wenyewe tumesikia maneno ya kinywa chake." Sasa Yesu ali-

paswa kuuawa. Kilichokuwa kimebaki kukamilisha ni kwa warumi kuthibitisha hukumu hii.

Ndipo ikafuata awamu ya tatu ya kumdhihaki mbaya zaidi, kuliko ile aliyofanyiwa mara ya kwanza. Dhihaka hizi zilitendeka mbele ya makuhani na watawala kwa ruhusa yao. Mahakimu walipotangaza kuwa Yesu atakufa, watu waliingiwa na wazimu wa kishetani. Watu walimrukia Yesu, na kama askari wa Warumi wasingaliwazuia, wangalimpasua vipande vipande kabla ya kufika msalabani. Warumi waliwazuia umati wa watu kwa nguvu wasimdhuru Yesu. Watu washenzi walichukizwa na ukatili aliotendewa mtu ambaye hakupatikana na hatia yo yote. Maofisa wa Warumi walisema kuwa ilikuwa kinyume cha sheria ya Wayahudi kumhukumu mtu kwa ushahidi wake mwenyewe. Jambo hili lilituliza fujo kidogo; lakini viongozi wa Kiyahudi walishikamana bila huruma wala aibu.

Makuhani na wakuu walisahau heshima ya vyeo vyao, na wakamdhihaki Mwana wa Mungu kwa sifa mbaya wakimtukania [402]
ukoo wake. Walidai kule kujitangaza kuwa Masihi kulimfanya astahili kifo kibaya mno. Walimvika vazi kuukuu kichwani na wakampiga wakisema “Ewe Kristto, tufumbulie; ni nani alikupiga.” Mshenzi mmoja akamtemea mate usoni.

Malaika waliandika kila dhihaka, neno na tendo waliyomtendea Jemadari wao mpendwa. Siku moja hawa watu duni walioudhihaki uso mtulivu na wa majonzi wa Yesu, watautazama utukufu wake, uking’aa kuliko jua.

[403]

# 76 — Jinsi Yuda Alivyopoteza Roho Yake

Historia ya Yuda huonyesha mwisho wa huzuni wa maisha ya mtu ambaye angeheshimiwa katika kazi ya Mungu. Kama yuda angalikufa kabla ya safari yao ya mwisho ya kwenda Yerusalemu angalihesabiwa kuwa mtu mashuhuri sana kati ya mitume kumi na wawili, ambaye angeacha pengo kubwa sana. Chuki ambayo imemfuata katika karne zote isingekuwako. Lakini tabia yake imedhihirishwa kwa ulimwengu kama onyo kwa wote wale watakaosaliti dhamana takatifu.

Tangu siku ile ya karamu nyumbani kwa Simon Yuda alikuwa amepata nafasi ya kukitafakari kitendo alichokuwa ameagana kukitekeleza, lakini kusudi lake lilikuwa halijabadilika. Kwa bei ya mtumwa akamuuza bwana wa utukufu.

Yuda kwa asili alikuwa na tabia ya kupenda fedha sana, lakini siku zote hakuwa mpotovu kiasi cha kutenda tendo baya kama hili. Aliiilea roho ya uchoyo wa fedha mpaka ikapita upendo wake kwa Kristo. Kwa tendo moja ovu akajitolea mwenyewe kwa Shetani, kutumiwa katika kiwango cho chote kile kutenda dhambi.

Yuda alijiunga na wanafunzi wakati watu wengi walipokuwa wakimfuata Kristo. Alishuhudia matendo makuu ya Kristo ya kuponya watu, na kufukuza pepo wachafu, na kufufua wafu. Aliyatambua mafundisho ya Yesu kuwa bora zaidi ya yote yale aliyopata kusikia. alitamani kubadilishwa tabia na alitegemea kuwa hivyo kwa kujihusisha na Yesu. Mwokozi hamkukataa Yuda, alimpatia nafasi miongoni mwa wale kumi na wawili na alimjalia uwezo wa kuponya wagonjwa na kuwatoa pepo wachafu. Lakini Yuda hakujitoa moyo wake kwa Kristo kikamilifu. Hakuacha tamaa zake za ulimwengu wala kuzipenda fedha. Hakujiweka chini ya mvuto wa mbingu, bali alijitafutia tabia ya kukosoa na kushutumu.

[404] Yuda alikuwa na mvuto mkubwa sana kwa wanafunzi wenzake. alijiona sana kutokana na sifa zake na aliwadharau ndugu zake kama walio duni. Alijisifu kuwa kanisa lisingestawi kama isingekuwa kwa

sababu ya uwezo wake kama msimamizi. Machoni pake alijiona kuwa muhimu na kila mara alipenda mwonekano huo.

Kristo alimweka mahali ambapo angeona udhaifu wake na kujirekebisha, lakini Yuda alijiendeleza katika tamaa. Fedha chache alizokuwa akitunza kila mara zilikuwa zinamtia majaribuni. alipotenda kazi ndogo kwa ajili ya Kristo, alijilipa kutoka katika fedha hizo kidogo. Machoni pake hivi visababu vilitumiwa kama udhuru kwa vitendo vyake, lakini machoni pa Mungu alikuwa mwizi.

Yuda alichagua njia ambayo alitegemea Kristo aifuate katika kazi, alikuwa amepanga kuwa yohana Mbatizaji afunguliwe kutoka gerezani. Lakini Yohana aliachwa akatwe kichwa. Na Yesu, badala ya kulipa kisasi kwa ajili ya kifo cha Yohana aliondoka kwenda mahali pengine. Yuda alitaka hatua za ukakamavu zaidi zichukuliwe. Alifikiri kuwa kama Yesu asingaliwazuia wanafunzi kutekeleza mipango yao kazi ingefanikiwa zaidi. aliona kuwa madai ya viongozi wa kiyahudi hayakupata changamoto wakati walipodai Kristo atoe ishara kutoka mbinguni. Moyo wake ulikuwa wazi kufuata hisia za kutoamini na adui akaujaza uasi. Kwa nini Yesu alitabiri mateso na mashataka dhidi yake mwenyewe na kwa wanafunzi wake? Matumaini yake ya kupata cheo kikuu katika ufalme ujao yakatishwe tamaa?

## Kutenda Kinyume cha Kristo

Yuda alikuwa akiendeleza wazo kwamba Kristo atatawala kama mfalme katika Yerusalemu. Wakati Kristo alipofanya muujiza wa kulisha watu kwa mikate Yuda alikuwa mstari wa mbele katika watu waliotaka kumtawaza Yesu kwa lazima. Matumaini yake yalikuwa makubwa sana, kutokufanikiwa kwake kukawa uchungu. Mazungumzo ya Kristo kuhusu mkate wa uzima, yalikuwa ndiyo kikomo. Alimwona Kristo akielekea katika mambo ya kiroho zaidi kuliko mambo ya kidunia. alidhani kuwa Kristo hakutaka heshima, na wala hakukusudia kuwakuza wafuasi wake. Aliazimu kutoshirikiana sana na Kristo na badala yake kujitenga polepole. Basi aliamua kuwa mtazamaji na hasa alikuwa mtazamaji.

Tangu wakati huo alionyesha mashaka yaliyowachanganya wenzake. Alileta mabishano na mafungu ya Biblia juu ya mambo ambayo hayakuwa na uhusiano na yale yaliyofundishwa na Kristo.

Mafungu ya Biblia hayo yaliwachanganya wanafunzi wa Yesu na [405] kuzidisha kufa moyo kwao kwa sababu yalinyofolewa kutoka katika maana yake. Walakini Yuda alijionyesha kuwa mwaminifu. Hivyo kwa njia ya kuonekana mwenye dini na busara alikuwa anayahusisha na maana ambayo haikukusudiwa na Yesu. Mapendekezo yake yalikuwa yanasisimua na kuongeza msukumo wa kupendelea mambo ya ulimwengu. Mawazo ya nani atakuwa mkuu kwa kawaida yalisisimuliwa na Yuda.

Wakati Yesu alipomwambia yule kijana, mtawala tajiri masharti ya kuwa mwanafunzi. Yuda alidhani kuwa kosa limetendeka. Watu kama mkuu huyu wangesaidia kuendeleza kazi ya Kristo. Yuda alifikiri kuwa yeye binafsi angebuni njia nzuri za kusaidia kanisa dogo hili kufanikiwa. Katika mambo hayo alijidhania kuwa ana hekima kuliko Yesu.

### Nafasi ya Mwisho ya yuda Kutubu

Katika yote yale Yesu aliyosema kwa wanafunzi wake, kulikuwa na kitu fulani ambacho Yuda moyoni hakukubaliana nacho. Chini ya mvuto wake, chachu ya chuki ilikuwa ikifanya kazi yake. Yesu aliona kuwa Shetani alikuwa amefungua njia ya kuwashawishi wanafunzi wengine. Walakini Yuda hakudhihirisha wazi manung'uniko yo yote yale mpaka siku ya karamu nyumbani kwa Simoni. Mariamu alipompaka Yesu mafuta, ndipo Yuda akadhihirisha tamaa yake. Kwa kemeo la Kristo kiburi kilichojeruhiwa na kutaka kulipiza kisasi vilibomoa ukuta wa kinga moyoni mwa Yuda. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa kila anayedumu katika kucheza na dhambi. Lakini Yuda alikuwa bado kufanywa mgumu. Hata baada ya kuahidi mara mbili kumsaliti Mwokozi, bado kulikuwa na nafasi ya toba. Wakati wa kula Pasaka Yesu alimjumuhisha Yuda katika huduma yake kwa wanafunzi wake. Lakini hata hivyo wito wa mwisho wa upendo haukujaliwa. Miguu iliyooshwa na Yesu iliondoka kwenda kufanya kazi ya usaliti.

Yuda alifikiri kuwa ikiwa Yesu atasulibishwa, basi lazima jambo hilo litekelezwe. Wala kitendo chake hicho hakitabadili kitu. Na kama Yesu hatakufa, basi itakuwa kumalazimisha ajitoe Mwenyewe. Yuda alihesabu kuwa alikuwa amechukua hataua dhati katika kumsaliti Bwana wake. Yuda hakudhani kuwa Yesu ataruhusu akamatwe.

Katika kumsaliti Yesu, Yuda alikusudia kumfundisha Yesu somo. Alikusudia kumfanya Mwokozi aanze kumheshimu. Mara kwa mara Mafarisayo na waandishi waliposhika mawe kutaka kumpiga, alitoweka. Na kwa vile alifanikiwa kutoweka mara nyingi, bila shaka [406]
hataruhusu ashikwe.

Yuda alikusudia kujaribu mambo. Ikiwa kweli Yesu alikuwa Masihi, watu watamtawaza kuwa mfalme. Yuda angepata sifa ya kumweka mfalme katika kiti cha enzi cha Daudi, na jambo hili lingempatia nafasi ya kuwa kaaribu na Kristo katika ufalme ujao. Katika bustani, Yuda aliwambia watu wale waliokuja kumkamata Yesu kwamba "Mkamateni." (Mathayo 26:48.) Aliamini kuwa Kristo ataponyoka. Na kama wangemlaumu angewaambia kuwa, Sikuwaambieni kwamba, mkamateni sana?

Kwa mshangao Yuda alimwona Mwokozi akiruhusu akamatwe. Katika kila hatua alitazamia kuwa yesu atawaonyesha uwezo wake, kwa kujifunua kama Mwana wa Mungu. Lakini saa zilipopita bila kuona chao chote, hofu kuu ilimpata msaliti kuona kuwa amemuuza Bwana wake auwawe. Kadiri hukumu ya Yesu ilivyokaribia Yuda hakuweza kuvumilia hatia ya dhamiri yake. Kwa ghafula sauti iliyokauka ikasikika katika ukumbi ule: Hana hatia; Kayafa, muachie! Umbo refu la Yuda lilionekana likipenya katika umati wa watu waliopigwa na butwaa. Uso wake ulionyesha mfadhaiko, na jasho lilimtoka usoni. Kwa kasi alikiendea kiti cha hukumu na kutupa mbele ya kuhani mkuu vipande vya fedha vilivyokuwa gharama ya kumsaliti Bwana wake. Akikamata joho la Kayafa, alimsihi amuachie Yesu. Kwa ghadhabu kayafa alimsukuma, lakini hakujua la kufanya. Uongo wa makuhani ulifunuliwa. Walikuwa wamemhonga huyu mwanafunzi kumsaliti Bwana wake.

Yuda alisema, "Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia." Lakini kuhani baada ya kutulia akasema "Basi, haya yanatupasa nini sisi? Yaangalie haya wewe mwenyewe." Mathayo 27:4. Makuhani waliona vema kumtumia Yuda kama chombo chao, lakini walidharau ubaya wake.

## Uchungu wa Majuto ya Yuda

Sasa Yuda akajitupa miguuni pa Yesu akimkiri kuwa Mwana wa Mungu, na akimsihi ajiondoe katika mikono ya watu hao. Mwokozi

alijua kuwa Yuda hakuwa na majuto ya hakika, kwamba amemsaliti Mwana wa Mungu asiye na mawaa. Walakini hakusema neno lo lote la kumshutumu. Alimtazama Yuda kwa huruma, na kusema, kwa saa hii nalikuja ulimwenguni.

Kwa mshangao watu waliokusanyika pale waliona ustahimilivu wa Kristo kwa msaliti wake. Mtu huyu alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Lakini kwa nini hakujiokoa na kuwashinda watesi wake?

[407] Maombi yake Yuda yakiwa kazi bure, Yuda alikimbia kwa haraka kutoka ukumbini akipiga kelele, Nimechelewa!. Alijisikia kuwa hawezi kuishi na kushuhudia Yesu akisulibiwa, na akiwa amekata tamaa alitoka nje na kwenda kujinyonga.

Baadaye siku hiyo, watu walipokuwa wanampeleka Yesu mahali pa kusulibishwa, waliiona maiti ya Yuda ikiwa chini ya mti mkavu. Uzito wake ulikuwa umekata kamba aliyotumia kujinyonga. Mbwa walikuwa wakiula mwili wake. Malipo yalionekana kuwa yanawapata watu wale waliokuwa na hatia ya damu ya Yesu.

# 77 — Kristo Ashtakiwa Mbele Ya Gavana Wa Kirumi [408]

Katika jumba la hukumu, la Pilato, Gavana wa Kirumi, Kristo alisimama akiwa amefungwa kama mahabusi, huku akilindwa na askari. Jumba lilikuwa limeanza kujaa watazamaji. Nje walisimama mahakimu wa baraza kuu la Kiyahudi (Sanhedrini), makuhani, wakuu na watu wenye ghasia.

Baada ya kumhukumu Yesu kifo wajumbe wa Sanhedrini, walifika kwa Pilato, ili aithibitishe hukumu na kuitekeleza. Lakini maofisa wa Wayahudi hawakupenda kuingia katika jumba la hukumu la Kirumi. Kwa kufuata kanuni zao, wangekuwa najisi na hivyo washindwe kushiriki katika Pasaka. Wao hawakuona kuwa kule kuwa na chuki ya kuua juu ya Yesu kulitia najisi katika mioyo yao. Wala hawakuona kuwa kwa vile walikuwa wamemkataa Kristto Mwana kondoo halisi wa Pasaka, siku kuu ile ilikuwa imepoteza maana yake kwao.

Pilato alimtazama Mwokozi kwa jicho baya. Akiwa ameitwa kwa haraka kutoka usingizini alikusudia kufanya kazi yake kwa haraka ilivyowezekana. Akikaza macho, kwa hasira yake yote, aligeuka kuona ni mtu wa namna gani aliyeletewa kuhoji. Alimkazia Yesu macho kwa makini. Alikuwa akishughulika na aina zote za wahalifu, lakini kamwe alikuwa hajaletewa mtu mwema, mwungwana, mtulivu, kama huyu. Usoni mwake hakuona dalili yo yote ya uhalifu, wala hofu, ushupavu au kutaka shari. Alimwona mtu ambaye uso wake ulikuwa na sura ya mbinguni.

Mtazamo wa Kristo ulimfanya mguso wa pekee kwa Pilato asili yake iliamushwa. Alisha wahi kusikia habari za na matendo ya Yesu. Mke wake alikuwa amemsimulia matendo bora ya nabii huyu wa Galilaya, aliyekuwa akiponya wagonjwa na kufufua wafu. Alikumbuka tetesi alizosikia kutoka kwa watu mbali mbali. Aliwataka [409]
Wayahudi waeleze madai yao dhidi ya mshtakiwa. Mtu huyu ni nani, na kwa nini ameletwa? Walijibu kwamba alikuwa mlaghai aliyeitwa Yesu Mnazareti.

Tena Pilato akawauliza: “Ni mashitaka gani mnayoleta juu ya mtu huyu?” Makuhani hawakujibu swali lake, ila walisema kwa hasira “Kama huyu asingekuwa mtenda mabaya tusingemleta kwako.” Wakati baraza kuu la Kiyahudi (Sanhedrini) linapomleta mtu kwako huwa astahiliye kuuawa, kuna haja gani kuuliza kuwa mnamshitakia nini? Walitumaini kumfanya Pilato aridhike tu bila kufanya uchunguzi zaidi.

Kabla ya haya, Pilato alipata kuidhinisha kwa haraka hukumu ya kifo kwa watu wasiyostahili kifo. Kwake yeye kama mshitakiwa ana hatia au hana hatia halikuwa jambo kubwa. Makuhani walitumaini kuwa sasa Pilatto ataidhinisha adhabu ya kifo dhidi ya Yesu bila ya kumsikiliza.

Lakini kitu fulani ndani ya mshitakiwa kilimfanya Pilato asite. Hakuthubutu kufanya hivyo. Alikumbuka jinsi Yesu alivyomfufua Lazaro, mtu aliyekuwa amezikwa kaburini siku nne; na hivyo alitaka kujua mashtaka dhidi yake na kama yaliweza kuthibitishwa.

Alisema kama hukumu yenu ni kamili, kwa nini mmemleta kwangu? “Haya mtwaeni ninye makamhu-kumu kwa ile torati yenu!” makuhani walisema kuwa wao wamemaliza kumhukumu tayari, lakini ni lazima wapate idhini ya Pilato ili kufanya hukumu iwe halali. Pilato akauliza: “Mlimhukumu nini? Wakajibu “Kufa.” Walitaka Pilato aidhinishe adhabu waliyotoa, na lo lote litakalotokea ni juu yao. Licha ya udhaifu wake kiroho Pilato alikataa kumhukumu Yesu mpaka asikie mashtaka juu yake.

Makuhani walijikuta katika utata. Hawakutaka ijulikane kwamba Kristto amekamatwa kwa sababu za dini, maana hayo hayatakuwa na uzito wowote kwa Pilato. Lazima waonyeshe madai kuwa mashtaka yake yanahusu mambo ya siasa. Warumi waliangalia sana mapinduzi yasitokee. Katika hatua za mahangaiko yao ya mwisho, makuhani wakawaita mashahidi wa uongo. Waliosema: “Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme.” Mashitaka matatu, kila moja lisilo na msingi wo wote. Makuhani walijua hivyo lakini walikuwa tayari kushuhudia uongo.

## Pilato Asadiki kuna Njama [410]

Pilato hakuamini kuwa mshitakiwa alikula njama ya kupindua serikali. Ila aliamini kuwa kulikuwa na njama ya siri kumwangamiza mtu asiye na hatia. Akimgeukia Yesu alimwuliza; "Wewe ndiwe Mfalme wa Wayahudi?" Mwokozi akamjibu: "Wewe ndiwe Mfalme wa Wayahudi?" Mwokozi akamjibu: "Wewe wasema." Aliposema hivyo uso wake uling'aa kana kwamba mwali wa jua umemulika juu yake.

Waliposikia jibu lake Kayafa alimwambia Pilato kuwa hata yeye ni shahidi kuwa Yesu amekubali kosa aliloshitakiwa nalo. Pilato akamwambia: "Husikii ni mambo mangapi wanayokushuhudia?" Lakini Yesu "Asimjibu hata neno moja."

Akisimama nyuma ya Pilato, na kuonekana mbele ya wote, Kristo alisikia matusi yote; lakini kwa yale mashitaka yote ya uongo hakujibu neno. Alisimama imara bila kutikisiwa na mawimbi ya ghasia hiyo yote. Ilikuwa kana kwamba mawimbi mazito ya bahari yaliinuka, na kujibwaga kando yake lakini bila ya kumgusa. Kimya chake kulikuwa nuru iliyomulika kutoka mtu wa ndani mpaka mtu wa nje.

Pilato alishangaa. Mtu huyu hajitetei ili kujiokoa? Alipokuwa akimtazama Yesu, hakuamini kuwa alikuwa mbaya kiasi walichokuwa wanadai makuhani. Katika kukwepa fujo ya watu, Pilato alimchukua Yesu kando na kuhoji zaidi. "Je Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?"

Yesu hakujibu moja kwa moja. Roho Mtakatifu alikuwa akishindana na Pilato, kwa hiyo alimpa nafasi ili apate kukiri imani yake. Yesu aliuliza: "Wewe wasema hivi kwa nafsi yako, au watu wengine walikuambia habari zangu? Pilato alielewa maana ya maneno ya Kristo, lakini hakutaka kukiri ungamo lililokuwa linamsukuma moyoni. Akasema: Ama! Ni Myahudi mimi! Taifa lako na wakuu wa makuhani ndio waliokuleta kwangu. Umefanya nini?"

## Yesu Ajaribu Kumwokoa Pilato

Yesu hakumwacha Pilato bila nuru zaidi, alimweleza kuwa Yeye hakuwa anatafuta ufalme wa dunia hii. Akasema: "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa

ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa. Basi Pilato akamwambia, Wewe mfalme basi? Yesu akajibu Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwengini, ili ni-
[411] ishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu." Kristo alitamani Pilato aelewe kuwa ni kwa njia ya kuiamini kweli na kujitwalia hiyo kweli ndipo hali yake ya asili iliyohaaribiwa ingeweza kujengwa upya.

Pilato alichanganyikiwa mawazo. Moyo wake ulitamani mno upate kuijua hiyo kweli, na jinsi ya kuipata. Aliuliza: "Kweli ni nini?" Lakini hakungoja kujibiwa. Makuhani walipiga makelele wakitaka hukumu itekelezwe mara moja, alipotoka nje kwa Wayahudi alisema kwa dhati, "Mimi sioni hatia yo yote kwake."

Makuhani na wakuu waliposikia hivyo kutoka kwa Pilato walikatishwa tamaa na kupandwa na hasira isiyo na kikomo. Walipoona uwezekano wa kuachiwa yesu, walitaka kumpasua vipande vipande. Walimlaumu Pilato, na kumshutumu kuwa hana uaminifu kwa Serikali ya Warumi. Walimlaumu kwa kutomhukumu Yesu, waliyethibitisha, alikuwa amejiinua kinyume na Kaisari. Walisema kwa hasira kuwa uchochezi wa Yesu dhidi ya Serikali ulikuwa unajulikana katika nchi yote. Wakasema: "Huwalaharisha watu, akifundisha katika Uyahudi wote, tokea Galilaya mpaka huku."

Wakati huo Pilato hakuwa na wazo lo lote la kumtia Yesu hatiani. Alijua kuwa Wayahudi walimshitaki kwa fitina na chuki. Haki ilisema kuwa Yesu afunguliwe. Lakini kama akikataa kumtia Yesu hatiani, watu wangefanya fujo kubwa, na hili ndilo aliloogopa. Aliposikia kuwa Yesu anatoka Galilaya, aliamua kumpeleka kwa Herode, ambaye ndiye alikuwa mtawala wa huko, ambaye kwa wakati huo alikuwa Yerusalemu. Kwa njia hiyo Pilato alitaka kumtupia jukumu hilo Herode. Na ndivyo ilivyotokea. Mahakimu hawa wawili walipatana kutokana na kesi dhidi ya Mwokozi.

Katika ghasia na fujo zilizofuata Yesu aliharakishwa kwenda kwa Herode. "Na Herode alipomwona Yesu alifurahi sana maana amesikia habari zake, akataraji kuona ishara iliyofanywa na yeye." Herode huyu ndiye yule ambaye mikono yake ilikuwa na damu ya Yohana Mbatizaji. Herode aliposikia habari za Yesu kwa mara ya kwanza aliogopa sana na kusema: "Yohana Mbatizaji amefufuka,

katika wafu ....” Hata hivyo alitamani kumwona Yesu. Sasa nafasi ilipatikana ya kumwokoa nabii huyu, na mfalme alitamani kufutilia mbali kumbukumbu ya kichwa chenye damu kilicholetwa kwake juu ya sahani kubwa. Pia aliona kuwa ni nafasi ya kutosheleza shauku yake, na alidhani kuwa ikiwa Kristo angepewa uwezekano wa kuachiwa angeweza kutenda cho chote atakachoombwa. [412]

Mwokozi alipoletwa, makuhani na wazee walihimiza mashitaka yao dhidi yake. Lakini Herode aliamuru kuwe kimya. Aliamuru zile pingu Kristo alizofungwa mikononi zifunguliwe, wakati ule ule akiwakemea adui zake kwa vile walivyomtendea Yesu kikatili hivi. Na yeye kama Pilato pia aliridhika kuwa Kristo ameshitakiwa kwa husuda na wivu tu.

Herode alimwuliza Kristo maneno mengi, lakini Mwokozi alinyamaza kimya tu. Kwa amri ya mfalme aliamuru wadhaifu na vilema waliletwa, na Kristo akaamuriwa athibitishe madai yake kwa kufanya muujiza. Yesu hakuitikia jambo hilo na herode alizidi kusisitiza: tuonyeshe ishara inayothibitisha usemi unaoenea kuwa unao uwezo kweli.” Lakini Mwana wa Mungu alikuwa amechukua asili ya kibinadamu, kwa hiyo inampasa kutenda kama mwanadamu katika hali kama hiyo. Hivyo hawezi kutenda miujiza ili ajiokoe kutokana na apitie maumivu na kudharauliwa ambako mwanadamu hupitia akiwa katika hali kama hii.

Herode alimwahidi yesu kuwa kama akifanya miujiza fulani, atamwachilia. Hofu iliwashika washtaki wa Kristo maana asije akafanya muujiza sasa, kitendo kama hicho kitaangamiza mipango yao kabisa, na labda kitawagarimu hata wao maisha yao pia. Makuhani na wakuu walipaza sauti zao wakasema kwamba yeye ni haini: na mkufuru; hutenda miujiza yake kwa uwezo wa mkuu wa mashetani!

Sasa dhamira ya Herode haikumsumbua sana kama alivyokuwa alipotishika na kutetemeka kutokana na ombi la Herodias kutaka kichwa cha Yohana Mbatizaji, hali yake ya kiroho ilikuwa pungufu kutokana na maisha yake ya uasherati. Hata alijivuna kwa ile adhabu aliyoitoa kwa Yohana Mbatizaji kwa kuthubutu kumkaripia. Na sasa alimtisha Yesu kuwa anao uwezo wa kumhukumu. Lakini Yesu hakuonyesha dalili yo yote, kuwa amesikia neno lo lote.

Herode aliudhika kwa ukimya huu. Ilionekana kana kwamba madaraka yake yalidharaulika. Tena kwa mara nyingine akamtishia

Yesu kwa hasira lakini yeye alibakia kimya na bila kutishika duni. Kazi ya Kristo haikuwa kuridhisha shauku. Kama angalitamka neno la kuponya roho zilizolemewa na dhambi, asingalikaa kimya. Lakini hakuwa na neno kwa wale wanaoukanyaga ukweli chini ya miguu yao. Herode alikuwa amekataa ujumbe uliosemwa kwake na nabii mkuu kuliko wote, na hivyo hakukuwa na ujumbe mwingine tena.
[413] Mkuu wa mbinguni hakuwa na neno kwake. Midomo ile ilikuwa imefungwa kwa mfalme jeuri ambaye hakuhitaji Mwokozi.

Uso wa Herode ulibadilika kuwa mwepesi kwa hamaki Kwa ghadhabu, akamwita Yesu kuwa laghai, Kisha akamwambia Kristo, ikiwa huonyeshi ushahidi wo wole wa dai lako, nitakukabidhi mikononi mwa askari na watu Ikiwa wewe ni laghai, adhabu ya kifo ndiyo unayostahili, ikiwa u Mwana wa Mungu, jiokoe nafsi yako kwa kufanya muujiza. Mara maneno haya yaliposemwa adui zake walimrukia kwa kasi sana, kama wanyama. Yesu alikokotwa huko na huko, Herode akiungana nao katika kumdhalilisha Mwana wa Mungu. Kama askari wa Kirumi wasingeingilia kati, Mwokozi angepasuliwa vipande vipande.

"Herode akamfanya duni, pamoja na askari zake, akamdhihaki, na kumvika mavazi mazuri;" askari wa Kirumi pia walijiunga katika dhihaka hii. Yale yote ambayo askari hawa wapotovu na viongozi wa Kiyahudi waliyoweza kuchochea alipakiwa Mwokozi. Hata hivyo uvumilivu wake haukutetereka.

## Wengine walitetemeka Mbele ya Yesu

Lakini walikuwapo wengine waliotetemeka mbele ya Kristo. Wengine waliokuja kumdhihaki walirudi nyuma, wakiogopa na kunyamaza. Herode alikirishwa. Miali ya nuru ya mwisho ya rehema kwake, ilimulika moyo wake uliofanywa kuwa mgumu na dhambi. Uungu ulikuwa umeng'aa ndani ya ubinadamu. Herode aliona kuwa alikuwa akimwangalia Mungu katika kiti chake cha enzi. Katika hali yake ya ukaidi, hakuthubutu kuidhinisha hudumu dhidi ya Kristo. Alimrudisha Yesu tena katika jumba la hukumu la Kirumi.

Pilato alisikitika sana alipowaona Wayahudi wanarudi kwake wakiwa na mshitakiwa. Aliwakumbusha kuwa alikwisha kumhoji Yesu na kumkuta hana hatia yo yote ile. Mashitaka yao yote ya-

likuwa hayana ushahidi. Hata Herode pia ambaye ni mtu wa taifa lao, hakuona kosa lo lote lililostahili kifo. "Kwa hiyo nitamrudi, kisha nitamfungua." Hapo Pilato alionyesha udhaifu wake. Yesu hakuwa na kosa lo lote, lakini alikuwa tayari kuisaliti haki na kuwapendeza washitaki wake. Hii ilimweka katika upande mgungu. Na ule umati uling'amua sitasita yake. Kama mara ya kwanza Pilato angesimama imara na kukataa kumtia hatiani mtu asiye na hatia, angalikata minyororo wa majuto aliofungwa nao siku zote za maisha yake. Kristo angeuawa, lakini hatia isingalimkalia Pilato. Lakini Pilato alikuwa [414]
amechukua hatua baada ya hatua kudharau dhamiri yake, na sasa alijikuta asiyeweza cho chote mikononi mwa makuhani na wakuu.

### Nafasi ya Mwisho ya Pilato

Hata wakati huo Pilato hakuachwa atende mambo kigizagiza. Mke wake alipewa ndoto na malaika akaona kuwa anaongea na Mwokozi. Mke wa Pilato hakuwa Myahudi, lakini alipomwona Yesu katika ndoto, alimtambua kwamba ni Mwana wa Mungu. Alimwona Pilato akimpiga Yesu mijeledi, baada ya kutamka kuwa: "Sioni hatia kwake." Alimwona akimtia Kristo mikononi mwa wauaji. aliuona msalaba umesimami-shwa na dunia ikiwa imetandwa na giza nene, na alisikia kile kilio cha fumbo; "Imekwisha."

Tena aliona tukio jingine. Alimwona Kristo ameketi katika kiti cha enzi katika wingu cheupe na wale waliomuua wakikimbia mbele ya utukufu wake. Kwa kilio cha kutisha alisituka na mara moja alimwandikia Pilato, maneno yenye onyo. Mtumishi alipenya katikati ya watu kumpatia barua kutoka kwa mkewe, ambayo ilisema: "Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake."

Uso wa Pilato ulibadilika, alichanganyikiwa na michomo moyoni iliyohitilafiana. Wakati alipokuwa akisitasita katika kuamua, makuhani walikuwa wakichochea mawazo ya watu. Sasa alifikiria desturi ingetumika kumwachilia Kristo. Ilikuwa desturi yao wakati wa sikukuu hii kumfungulia mfungwa mmoja aliyependekezwa na watu. Hakukuwa na sheria yo yote katika desturi hii, lakini ilithaminiwa mno na Wayahudi. Katika muda huo Warumi walikuwa na mfungwa mmoja aitwaye Baraba, aliyekuwa akingojea kunyongwa. Mtu huyu alikuwa na kusudi la kupindua serikali. Alikuwa

mwizi na mnyang'anyi aliyejipatia mali kwa nguvu. Alikuwa amechochea watu dhidi ya Serikali ya Warumi na kupata wafuasi. Alikuwa akidai kuwa anaendesha mambo ya dini; lakini alikuwa jambazi sugu aliyefanya vitendo vya uasi na ukatili.

Pilato alidhani kuwa kama akiwapa watu uchaguzi kati ya huyo na Mwokozi, ataamsha hisia ya kutenda haki mioyoni mwao. "Mnataka niwafungulie yupi? yule Baraba, au Yesu aitwaye Kristo?" Watu walijibu kama ngurumo ya wanyama wa porini wakisema: Tufungulie "Baraba!" Akidhani kuwa watu hawakuelewa vizuri swali lake, Pilato aliuliza: "Je! mnataka niwafungulie Mfalme wa
[415] Wayahudi?" Watu wakapiga kelele wakisema: "Mwondoe huyu, utufungulie Baraba!" "nimtendeeje yesu aitwaye Kristo?" Mashetani, wakiwa katika mfano wa wanadamu na kuchangamana na watu walijibu kile kilichotazamiwa: "Asulubishwe."

## Pilato Hakuweza Kuona Matokeo ya Baadaye

Pilato hakudhani kuwa itakuwa hivyo. Alinywea kwa hofu kumtoa mtu asiyekuwa na hatia akateswe na kuuawa kifo cha ukatili kuliko vyote. "Kwani ni ubaya gani alioutenda? Lakini shauri lilikuwa limekwenda mbali kikomo cha ubishi Hata hivyo Pilato alijitahidi kumwokoa Kristo. "Akawaambia mara ya tatu, kwa sababu gani? Huyu ametenda uovu gani?" Lakini kule tu kutaja kufunguliwa kwake, kuliwatia watu wazimu. wakazidi kupaza sauti, "asulubiwe, asulubiwe!"

Yesu akiwa mwenye kuzimia na majeraha, alipigwa mijeledi. "Nao askari wakamchukua ndani ya behewa, ndiyo Praitorio; wakamkusanya kikosi kizima. Wakamvika vazi la rangi ya zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani mwake; wakaanza Salamu, Mfalme wa Wayahudi!" Wakamtemea mate, wakapiga magoti, wakamsujudia." Mara kwa mara mkono wa mkorofi mmoja ulimpiga kichwani na kukandamiza taji ya miiba katika paji lake, na kufanya damu itiririke usoni.

Kundi hilo lililokuwa kama lenye wazimu lilimsonga Mwokozi wa ulimwengu. Dhihaka na kejeli vilichanganyikana na makufuru. Shetani aliongoza kundi hili. Lilikuwa kusudi lake kumchokoza Mwokozi mpaka arudishe kwa ukali kama ikiwezekana, au kumlazimisha atende muujiza na kujiokoa. Doa moja katika maisha

yake kama mwanadamu na Mwana Kondoo wa Mungu angekuwa kafara yenye kasoro na hivyo wokovu wa mwanadamu utakuwa umeshindikana. Lakini alijitoa na kwa uvumilivu akastahimili dhihaka na uovu wote.

Maadui za Kristo walikuwa wamedai ishara kama uthibitisho wa Uungu wake. Walikuwa na ushahidi tosha kabisa kuliko waliomtafuta. Unyofu na uvumilivu wake vilithibitisha udugu wake na Mungu. Matone ya damu yaliyokuwa yanadondoka kutoka katika majeraha usoni pake yalikuwa ni amana ya kupakwa "Mafuta ya shangwe" kama Kuhani wetu Mkuu. (Soma Waebrania 1:9). Hasira ya Shetani ilikuwa kali wakati alipoona kuwa katika kila jambo Mwokozi ametimiza mapenzi ya Baba yake.

### Kuridhia Kwaelekeza Katika Maangamizi [416]

Wakati Pilato alipomtoa Yesu ili apigwe mijeledi alitegemea kuwa ule umati utaamua kuwa adhabu hiyo imetosha. Lakini kwa makini sana Wayahudi waliona udhaifu wa kumwadhibu mtu aliyekuwa ametamkwa kuwa hana hatia, walidhamiria kuona kuwa Yesu haachiliwi.

Pilato sasa aliagiza baraba aletwe mahakamani, na wafungwa wote wawili wakasimama pamoja. Akimsonda Mwokozi kwa kidole akasema "Tazama mtu huyu!" Hapo alisimama Mwana wa Mungu, amefungwa nguo kiunoni tu, mgongo wake ukionyesha majeraha yadamu, umevimba na ukionyesha maumivu, lakini ulikuwa haujapata kupendeza hivyo. Kila sehemu ya uso ilidhihirisha huruma ya upole kwa maadui zake wakatili. Katika jinsi yake kulikuwa na nguvu na heshima ya uvumilivu. Alikuwa tofauti na mfungwa mwenzake aliyesimama pamoja naye. Kila mshipa wa uso wa Baraba ulimtangaza kuwa jambazi sugu. Tofauti kati yao ilikuwa dhahiri kwa kila mtu aliyewaona. Baadhi ya waliomwangalia Yesu walilia mioyo yao ikiwa imejaa huruma. Makuhani na wakuu walisadikishwa kuwa alivyokuwa akidai ndivyo alivyokuwa.

Askari wa Kirumi waliomzunguka Yesu hawakuwa wakaidi wote. Walimtazama mteswa kutoka mbinguni kwa masikitiko na huruma, uvumilivu wake mtulivu uliwagusa mioyo yao. Maono haya kamwe hayatawatoka mpaka ama wamkiri yeye kuwa Kristo au kwa kumkataa wajikatie hukumu wao wenyewe.

Pilato hakuwa na mashaka kuwa hali tofauti ya Mtu huyu na Baraba itawagusa Wayahudi wawe na huruma. Lakini hakufahamu ushupavu wa chuki ya Makuhani. Kwa mara nyingine tena, makuhani, wakuu na watu walipiga kelele cha kutisha: "Asulibishwe, Asulibishwe." Mwishowe Pilato akiwa ameshindwa kuvumilia ukatili wao usiokuwa na maana alipaza sauti kwa kukata tamaa: "Mtwaeni ninyi basi, mkamsulubishe; kwa maana mimi sioni hatia kwake."

Gavana wa Kirumi, ingawa alizoea kuona matukio ya ukatili, alimwonea huruma mfungwa huyu mteswa. Lakini makuhani walipiga kelele, "Sisi tunayo sheria na kwa sheria hiyo amestahili kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu."

## Wema wa Yesu kwa Pilato

Pilato alishtushwa isiwe kwamba anayesimama mbele yake ni mtu kutoka mbinguni! Kwa mara nyingine tena akamwambia Yesu "Wewe umetokapi?" Lakini Yesu hakumjibu. Mwokozi alikuwa amezungumza na Pilato wazi, na kumweleza kazi yake. Pilato
[417] alikuwa amepuuza nuru. Alikuwa amedharau cheo cha uhakimu kwa kuitikia matakwa ya watu wenye makelele. Yesu hakuwa na nuru zaidi kwa Pilato. Akichukizwa na ukimywa wake, Pilato alisema kwa kiburi: "Husemi nami? Hujui ya kuwa mimi nina mamlaka ya kukufungua, nami nina mamalaka ya kukusulibisha?"

Yesu akamjibu, "Wewe hungekuwa na mamlaka yo yote juu yangu, kama usingepewa kutoka juu; kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako yuna dhambi iliyo kubwa zaidi." Kristo alimaanisha Kayafa, aliyekuwa akiliwakilisha taifa zima la Wayahudi. Walikuwa na nuru katika unabii uliomshuhudia Kristo, na ushahidi dhati kuhusu Uungu wake yeye waliyemhukumu kifo. Jukumu kubwa zaidi liliwaangukia wale waliokuwa viongozi wa taifa. Pilato, Herode na, askari wa Kirumi hawakumwelewa Yesu. Hawakupata nuru kama ile taifa la Kiyahudi liliyoipata. Kama askari wale wangalipata nuru hiyo wasingalimtendea Yesu jinsi hiyo.

Kwa mara nyingine tena Pilato akapendekeza kumwachia Mwokozi. "Lakini Wayahudi wakapiga makalele wakisema, Ukimfungua huyu, wewe si rafiki yake Kaisari." Katika watu wote waliowapiga Warumi, Wayahudi walikuwa wakiwachukia kabisa;

lakini kwa kutaka kukamilisha makusudi yao ya kumwua Yesu, walijifanya kuwa waaminifu kwa utawala huo wa kigeni, waliouchukia.

Waliendelea kusema, "kila mtu ajifanyaye kuwa mfalme, humfitini Kaisari." Pilato alikuwa anatiliwa mashaka na Warumi na alijua kuwa habari kama hizo zikisikika ataangamia. Alijua kuwa Wayahudi hawataachia cho chote kile katika kutekeleza azima yao ya kulipiza kisasi.

Tena Pilato akamweka Yesu mbele ya watu akisema, "Tazama, Mfalme wenu!" Mara hii tena kelele za wazimu zilisikika zikisema: "Mwondoshe! Mwondoshe! Msulibishe!" Kwa sauti iliyosikika mbali na karibu Pilato akauliza, "Je! nimsulibishe mfalme wenu!" Lakini kutoka katika midomo ya matusi, kufuru yalisikika yakisema: "Sisi hatuna mfalme, ila Kaisari."

Hivyo kwa kuchagua mtawala wa kishenzi Wayahudi walimkataa Mungu asiwe Mfalme wao. Tangu hapo hawakuwa na mfalme, ila Kaisari. Hivyo ndivyo makuhani na walimu walivyowaongoza watu kufanya. Kwa sababu hiyo waliwajibika, na matokeo yakutisha yaliyofuata. Dhambi na aangamio la taifa vilisababishwa na viongozi wa dini.

"Basi Pilato alipoona ya kuwa haifai lo lote, bali ghasia inazidi [418]
tu, akatwaa maji, akanawa mikono mbele ya mkutano akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe." Pilato akamtazama Mwokozi, na kusema moyoni mwake kuwa huyu ni Mungu. Akawageukia watu, akisema: Mimi sina hatia kwa damu yake. Msulibisheni, lakini natamka kuwa ni mwenye haki. Naye anayemtaja kuwa Baba yake awahukumu ninyi na siyo mimi kwa kazi hii ya leo. Halafu akamwambia Yesu, Nisamehe kwa kitendo hiki; siwezi kukuokoa. Na baada ya kumpiga Yesu mjeledi, akamtoa ili asulibiwa.

Pilato alitamani kumwokoa Yesu, lakini aliona kuwa hawezi kufanya hivyo na kubakia katika cheo chake. Kuliko kupoteza mamlaka yake ya ulimwengu, alichagua kumtoa kafara mtu asiye na kosa. Na watu wangapi hutupilia mambo ya ukweli kwa jinsi hii. Dhamiri na wajibu huelekeza njia moja, na kujipenda nafsi huelekea njia nyingine. Mkondo huelekezwa upande mpotovu, na yeye anayeridhia na uovu hukokotwa kupelekwa katika giza la hatia.

Lakini licha ya tahadhari yake, jambo lile aliloogopa Pilato lilimpata. Aliangushwa kutoka katika cheo chake, na akiumia kwa

masikitiko na machozi haukupita mda mrefu baada ya kusulibishwa Kristo, alijiua mwenyewe.

Wakati Pilato aliposema kuwa hana hatia ya damu ya Kristo, Kayafa alijibu kwa kiburi: "Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu." Maneno yale yaliitikiwa na mkutano wote kwa mngurumo wa sauti zizizo za kibinadamu. Umati wote ukasema, "Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu."

Wana wa Israeli walikuwa wamefanya uchaguzi waoBaraba ambaye alikuwa haramia, na mwuaji mjumbe wa Shetana. Kristo, mjumbe wa Mungu alikataliwa. Katika kufanya uchaguzi huo, walimkubali yule ambaye tangu mwanzo alikuwa mwongo na muuaji. Shetani akawa kiongozi wao, na utawala wake utawaendesha.

Wayahudi walikuwa wamepiga kelele: Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu". Ombi lao lilijibiwa Damu ya Mwana wa Mungu ilikuwa juu ya watoto wao na juu ya wajukuu wao. Katika tukio la kutisha ombi lao hilo lilitimizwa wakati wa uharibifu wa Yerusalemu na hali ya taifa ya Kiyahudi kwa karibu miaka elfu mbili iliyofuata tawi lililokatwa kutoka katika mzabibu lilikauka. Kutangatanga kwao toka nchi hata nchi na toka kizazi hata kizazi wakifa katika uasi na dhambini!

[419] Katika hali ya kutisha ombi hilo litatimzwa katika siku ile ya hukumu ya mwisho. Kristo atakuja katika utukufu wake. Maelfu na maelfu ya malaika, wana uzuri wa Mungu walishinda, wataamsindikiza naye njiani. Watu wa mataifa yote watakusanywa mbele yake. Badala ya taji ya miiba atavaa taji ya utukufu. Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na katika paja lake: "MFLME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA." Ufunuo 19:16.

Makuhani na wakuu wataliona tena matukio lile la jumba la hukumu. Kila jambo litaonekana kana kwamba limechorwa kwa herufi za moto. Kisha wale waliomba, "Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu," watapokea jawabu la ombi lao. Kwa uchungu wa kutisha na wa kuogofya watalilia miamba na milima, Tuangukieni. (Tazama Ufunuo 6:16, 17).

# 78 — Yesu Afa Juu Ya Kalwari [420]

"Na walipofika mahali paitwapo Golgotha, yaani Fuvu la kichwa ndipo walipomsulubisha yeye."

Habari za kuhukumiwa Kristo zilienea, na watu wa hali zote walifurika kwenda mahali pa kusulibiwa. Makuhani na wakuu walikuwa wamefungwa kwa ahadi kwamba hawatawasumbua wafuasi wa Kristo ikiwa Yeye atatolewa kwao, na hivyo wanafunzi na waumini walijumuika kwenye msongamano huo.

Msalaba uliokuwa umetayarishwa kwa ajili ya Baraba, ulitwishwa katika mabega ya Yesu yaliyokuwa yakichuruzika damu. Wenzi wawili wa Baraba waliopaswa kusulubiwa pamoja naye nao walibebeshwa misalaba yao. Tangu alipokula Pasaka pamoja na wanafunzi wake, Yesu alikuwa hajala wala kunywa cho chote. Alikuwa amevumilia uchungu wa kusalitiwa, na alishuhudia wanafunzi wake wakimwacha na kutawanyika. Alikuwa amepelekwa kwa Anasi, kwa Kayafa, kwa Pilato, kwa Herode na kurudishwa kwa Pilato tena. Usiku ule wote palikuwapo tukio baada ya tukio kiasi cha kuweza kudhoofisha roho ya mtu hadi kuzimia. Lakini Kristo hakushindwa. Alikabili fadhaa zote kishujaa. Lakini baada ya kupigwa mara ya pili na kutwishwa msalaba hali ya kibinadamu haikuweza kustahimili zaidi. Alianguka, na kuzimia chini ya mzigo huo.

Makutano hawakuonyesha huruma yo yote. Bali walimdhihaki kwa kushindwa kubeba msalaba. Mara nyingine tena walimtwika msalaba mara ya pili, na akaanguka tena. Watesi wake wakaona kuwa hataweza kubeba mzigo wake zaidi. Ni nani ataubeba huu mzigo wa kudhalilishwa? Wayahudi wasingeliweza, kwa sababu ya kuhofia kutiwa najisi na hivyo kuzuiwa kushiriki Pasaka.

Katika wakati huo mgeni, Simoni, Mkirene akitokea vijijini [421]
alikutana na umati huu. Alisimama kwa mshangao wa lililokuwa linatendeka na alipoonyesha moyo wa huruma, walimkamata, na kumtwisha msalaba mabegani.

Wana wa Simoni walikuwa wafuasi wa Mwokozi, lakini yeye mwenyewe hakuwa mfuasi. Kuubeba msalaba mpaka Kalwari ulikuwa mbaraka kwa Simoni. Mbaraka huo ulimuongoza achukue msalaba wa Kristo na kwa hiyari na tangu hapo alisimama chini ya mzigo wake kwa furaha.

Sio wanawake wachache waliokuwemo katika umati ulimfuata asiye na hatia mpaka kufikia kifo chake cha ukatili. Baadhi yao walikuwa wamemletea wagonjwa wao na wenye kuteseka. Wengine walikuwa wameponywa wao wenyewe. Hivyo walishangazwa na chuki aliyoonyeshwa na makutano. Na bila ya kujali maneno makali ya makuhani na wakuu, pale Yesu alipoanguka na msalaba, wanawake hawa waliangusha kilio. Kristo aliguswa na kilio hiki. Alijua kuwa hawakumlilia kwa vile ni Mwana wa Mungu, lakini hata hivyo hakudharau kule kumhurumia kwao. Kilio chao kiliamsha huruma moyoni mwake kwa ajili yao, akasema; "Enyi binti za Yerusalemu, msinililie mimi, bali jililieni nafsi zenu na watoto wenu." Kristo aliutazama wakati Yerusalemu utakapoangamizwa ambapo wengi katika hao waliokuwa sasa wanalia wataangamia pamoja na watoto wao.

## Hukumu Pana Zaidi

Mawazo ya Yesu yalisafiri kutoka wakati wa kuangamia kwa Yerusalemu na kufikia hukumu pana zaidi.

Katika kuharibiwa mji wa Yerusalemu usiotubu aliona mfano wa uharibifu wa mwisho utakaoupata ulimwengu. "Ndipo watakapoanza kuiambia milima, Tuangukieni, na vilima, Tufunikeni kwa kuwa kama wakitenda mambo haya katika mti mbichi, itakuwaje katika mti mkavu?" Mti mbichi ulikuwa mfano wake yeye mwenyewe, Mwokozi asiye na hatia. Ghadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi ilimwangukia Mwanawe mpendwa. Basi ni taabu kiasi gani basi, atakayoibeba mwenye dhambi ambaye akidumu katika dhambi? Wasiotubu watapata huzuni ambayo lugha itashindwa kuielezea jinsi yake.

Katika umati uliomfuata Mwokozi mpaka Kalwari, walikuwamo wale waliokuwa katika maandamano ya Hosana, wakiwa na matawi ya mitende, wakati alipoingia Yerusalemu kwa shangwe. Sio wachache waliomsifu siku hiyo kwa sababu ilikuwa hoihoi, sasa

wanatuna katika kupiga kelele wakisema; "Msulibishe, Msulibishe." Wakati Kristo alipoingia Yerusalemu kwa shangwe wanafunzi wa- [422] likuwa wakimsongasonga, wakiona kuwa ni heshima kuambatana naye. Sasa katika kudhalilishwa kwake wanamfuata kwa mbali.

### Uchungu Wa Mama Wa Kristo

Katika mahali pa kusulibishiwa, wale wezi wawili walishindana sana na watu waliowawamba misalabani; lakini Yesu hakushindana. Mama wa Yesu akitegemezwa na Yohana amemfuata nyayo za mwanaye mpaka Kalwari. Alitamani sana kuweka mikono yake chini ya kichwa chake kilichojeruhiwa lakini hakupata nafasi hii ya kuomboleza. Bado alitazamia kuwa Yesu atajiokoa mwenyewe kutoka kwa watesi wake. Mara roho yake ilizimia alipokumbuka kwamba Yesu alitabiri matukio yaliyokuwa yanatendeka sasa.

Wale wezi walipokuwa wanafungwa msalabani aliangalia kwa wasi wasi wa uchungu. Je! yeye aliyewapa wafu uhai mwenyewe ataruhusu asulibishwe. Je! lazima atupe imani yake kwamba ni Masihi? Aliona mikono yake ikinyooshwa juu ya msalaba nyundo na misumari vililetwa, na wakati misumari ilipopigiliwa katika nyama nyororo wanafunzi walimwondoa mama yake Yesu kutoka pale akiwa amezimia.

Mwokozi hakulalamika, lakini matone makubwa ya jasho yalionekana usoni pake. Hapakuwapo na mkono wenye huruma kuweza kufuta umande wa mauti kutoka katika uso wake; maneno yenye huruma na uaminifu kutuliza moyo wake wa kibinadamu. Wakati askari walipokuwa wakitenda kazi yao ya kuogofya Yesu aliomba, "Baba uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo." Mawazo yake yalipita kutoka katika yale yaliyokuwa, yanamsibu hadi malipo yatakayokuwa sehemu yao. Hakuna laana iliyowashukia askari hao, waliokuwa wanamtendea ukatili, wala hakuwa kulipiza kisasi kulikotajwa juu ya makuhani na wakuu. Alipumua tu ombi la msamaha kwa ajili yao "maana hawajui watendalo."

Lakini kutofahamu kwao haukuwaondolea hatia yao, kwa sababu ilikuwa nafasi yao kumfahamu na kumpokea Yesu kama Mwokozi wao. Baadhi yao wangeona dhambi zao, watubu na kuongoka. Wengine kwa ukaidi wao wangedumu kuwa hivyo na kufanya sala ya Yesu isijibiwe kwa ajili yao. Hata hivyo, kusudi la Mungu

lilikuwa linafikia utimilifu wake. Yesu alikuwa anapokea haki ya mwombezi wa wanadamu mbele za Baba.

Lile ombi la Kristo kwa adui zake lilimhusu kila mwenye
[423] dhambi, tangu mwanzo wa ulimwengu mpaka mwisho wa nyakati. Watu wote wanahusika na kusulubishwa kwa Mwana wa Mungu. Msamaha hutolewa kwa wote bure.

Mara tu baada ya Yesu kuambwa msalabani, msalaba ulinyanyuliwa na watu wenye nguvu ukasimikwa kwa kishindo katika shimo lililoandaliwa. Hali hii ilisababisha maumivu makali sana. Kisha Pilato aliandika anwani kwa Kiebrania, Kigiriki na Kilatini, akaiweka msalabani juu ya kichwa cha Yesu. Anwani hiyo ilisomeka hivi, "YESU MNAZARETI, MFALME WA WAYAHUDI." Jambo hili liliwachukiza Wayahudi waliopiga kelele, "Sisi hatuna mfalme ila Kaisari." Lakini Pilato aliandika yale waliyosema. Hakuna kosa lo lote lililotajwa, isipokuwa kwamba Yesu alikuwa Mfalme wa Wayahudi, ukubali wa dhati kwamba waliapa utii, kwa Warumi. Hii ilitangaza kuwa ye yote atakayejitangaza kuwa mfalme wa Israeli atapata hukumu ya kifo. Katika juhudi ya kumwangamiza Kristo, makuhani walikuwa tayari hata kupoteza jadi ya taifa lao.

Makuhani walimwomba Pilato abadili maandiko hayo yasiwe kwamba: "Mfalme wa Wayahudi;" bali ya kwamba yeye alisema; "Mimi ni mfalme wa Wayahudi." Lakini Pilato akiwa na ghadhabu, alijibu bila kujali "Nilivyoandika, nimeyaandika."

Kwa majaliwa ya Mungu maandiko hayo yalikusudiwa kuamsha shauku ya kuchunguza Maandiko Matakatifu. Watu kutoka pande zote walifika Yerusalemu, na tangazo hilo likitaja Yesu kuwa ndiye Masihi, lingeonekana na kusomeka nao. Tangazo hilo liliandikwa kwa uongozi wa Mungu.

Katika mateso ya Kristo msalabani, unabii huu ulitimia, "Kusanyiko la waovu wamenisonga; wamenizuia mikono na miguu" "Wanagawanya nguo zangu, na vazi langu wanalipigia kura." Zaburi 22:16-18. Nguo zake zilipewa askari. Koti lake lilifumwa bila upindo au mshono, basi wakaambiana "Tusilipasue, lakini tulipigie kura liwe la nani."

Katika unabii mwingine Mwokozi alisema; "Nikangoja aje wa kuhurumia, wala hakuna; Na wa kunifariji, wala sikumwona mtu. Wakanipa uchungu kuwa chakula changu; Nami nilipokuwa na kiu wakanimywesha siki." Zaburi 69:20, 21. Kwa wale waliohukumiwa

kifo cha msalaba walikuwa wakinyweshwa aina ya siki kuwafanya wasisikie maumivu makali. Lakini Yesu alipoionja alikataa. Imani yake lazima iwe kwa Mungu tegemeo lake la pekee. Kufifisha akili zake kungetoa nafasi kwa Shetani. Makuhani, wakuu na waandishi [424] waliungana na makutano kumdhihaki Mwokozi aliyekuwa anakufa. Sauti ya Baba kutoka mbinguni kumshuhudia Kristo kuwa ni Mungu ilikuwa kimya. Hakuna ushuhuda wo wote kwa ajili yake uliosikika. Aliteseka peke yake.

Watu walisema; "Ukiwa wewe ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani." "Na ajiokoe mwenyewe, kama ndiye Kristo Mwana wa Mungu mteule wake." Shetani na malaika zake wakiwa katika mfano wa wanadamu walikuwako pale msalabani wakiungana na makuhani na wakuu katika dhihaka hizi za wazimu.

Yesu aliwasikia makuhani wakitangaza "Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. Yeye Kristo Mfalme wa Israeli na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini." Kristo angeweza kushuka kutoka msalabani. Lakini kwa sababu hakujiokoa mwenyewe mwenye, dhambi analo tumaini la msamaha wa dhambi na kukubalika na Mungu.

### Mwizi Mmoja Aliyesulibiwa Aamini

Faraja moja ilimpata Yesu akiwa msalabani, nayo ilikuwa ombi la mwizi aliyetubu. Wezi wote wawili waliosulibishwa na Yesu, mara ya kwanza walimshu-. tumu; mmoja katika maumivu yake alizidi kukata tamaa na kuwa mkaidi. Lakini mwenzake hakuwa mhalifu mkaidi; hakuwa na hatia kama wengi waliokuwako pale msalabani. Mtu huyu alikuwa amemwona na kumsikia Yesu, lakini makuhani na wakuu walikuwa wamemzuia asimwamini. Katika ukaidi wake, mwisho alitumbukia katika makosa akakamatwa na kuhukumiwa.

Pale msalabani aliwaona waongozi wa dini wakimdhihaki Kristo. Alisikia hotuba ya dhihaka ikiungwa mkono na mhalifu mwenzake "Je! wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi." Miongoni mwa wapita njia aliwasikia watu wengi wakirudia maneno ya Yesu na kusimulia miujiza aliyotenda. Mawazo, yakamrudia kuwa huyu ndiye Kristo. Akimgeukia mhalifu mwenzake akasema; "Wewe humwogopi hata Mungu nawe u katika hukumu hiyo hiyo". Wale

wezi waliokuwa wanakufa hawakuwa na cha kuogopa kutoka kwa mwanadamu. Lakini kwa mmoja lilikuja wazo dhati, kwamba kuna Mungu wa kuogopa, na kisha ya kumfanya atishike. Na sasa historia ya maisha yake ilikuwa karibu kufungwa. "Kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu? Nayo ni haki kwetu sisi; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa?"

Wakati yule mwizi alipohukumiwa kwa kosa lake alikata tamaa,
[425] lakini sasa kwa taratibu wazo la ajabu likamjia. Roho Mtakatifu akaangaza moyo wake na pole pole mnyororo wa ushahidi ukajiunga pamoja. Katika Yesu aliyedhihakiwa na kuangikwa msalabani, aliona Mwana kondoo wa Mungu. Tumaini likachanganyikana na huzuni katika sauti yake huku roho iliyokuwa inakufa ikijitupa kwa Mwokozi. "Ee Yesu, nikumbuke utakapokuja katika ufalme wako."

Mara moja jibu likatoka, sauti ya upole yenye sauti ya wimbo, iliyojaa upendo na uwezo maneno: "Amini, nakuambia leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi." Luka 23:43. Yesu alikuwa amengoja kwa hamu kusikia maneno ya faraja kutoka kwa wanafunzi wake. Alikuwa amesikia maombolezo tu, "Tulitumaini kwamba huyu ndiye ambaye angekomboa Israeli." Maneno ya imani na upendo kutoka kwa mwizi anaye kufa msalabani yalileta faraja kuu kiasi gani kwa Mwokozi! Wakati ambapo hata wanafunzi walikuwa na mashaka, maskini mwizi alimwita Yesu "Bwana." Hakuna aliyemkiri akiwa msalabani isipokuwa mwizi mwenye toba aliyeokolewa saa ya mwisho kabisa. Sauti ya huyu mtu mwenye kutubu, iliwasitua waliosimama kando kando. Wale waliokuwa wakigombea mavazi ya Kristo waliakoma ubishi wao wakangojea jibu kutoka katika mdomo wa Kristo anayekufa. Aliposema maneno ya hadi giza lililokuwa limeufunika msalaba lilichomwa na mwanga hai. Kristo katika hali yake ya kudhalalishwa alitukuzwa. Yule ambaye aliyeonekana machoni pa wote kuwa ameshindwa alikuwa Mshindi. Alitambulika kuwa Mchukua Dhambi. Wanaweza kugawana nguo zake, lakini wasingaliweza kunyakua uwezo wake wa kusamehe dhambi. Ni haki yake ya kifalme kuwaokoa wote wanaomjia Mungu kwa nia yake!

"Amini nakuambia leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi." Kristo hakumwahidi yule mwizi kuwa atakuwa pamoja naye peponi siku hiyo. Yeye mwenyewe hakuenda peponi siku hiyo. Alilala kaburini, na asubuhi ya siku ya kufufuka, alisema, "Sijapaa

kwenda kwa Baba yangu bado." Yohana 20:17. Lakini katika siku iliyoonekana ya kushindwa, ahadi ilitolewa. "Leo" wakati akifa msalabani kama mwizi, Kristo alimhakikishia mwenye dhambi, "Utakuwa pamoja nami peponi." Mahali Kristo alipowekwa msalabani katikati ya wale wezi, palipangwa na makuhani na wakuu, kuonyesha kuwa alikuwa mhalifu mkuu kati yao watatu. Lakini jinsi alivyowekwa "katikati" vivyo hivyo msalaba wake ulisimikwa katikati ya ulimwengu unaokufa dhambini. Na maneno ya msamaha yaliyosemwa kwa yule mwizi aliyetubu, yaliwasha mwali wa nuru [426]
itakayong'aa mpaka kufikia pande zote za ulimwengu.

Katika kudhalalishwa kwake, Yesu kama nabii alikuwa amewazungumza na binti za Yerusalemu; kama kuhani na mwombezi alikuwa amemsihi Baba awasamehe wauaji wake; na kama Mwokozi alikuwa amesamehe dhambi za yule mwizi aliyetubu. Chini ya msalaba mama yake alisimama akiegemea kwa Yohana. Hakuweza kuvumilia kuwa mbali na mwanawe, na Yohana akijua ya kuwa mwisho uko karibu, alikuwa amemleta tena. Akiutazama uso wenye majonzi alimwambia; "Mama tazama mwanao." Kisha akamwambia Yohana: "Tazama, mama yako." Yohana alielewa na akaukubali wajibu huo. Tangu wakati huo Yohana alimchukua na kumtunza kwa huruma. Mwokozi hakuwa na fedha za kumhifadhia mama yake, lakini alitoa kile alichokihitaji sana huruma za mtu aliyempenda kwa sababu alimpenda Yesu. Na Yohana alipata mbaraka mkubwa kwa sababu Mariamu daima alinikumbusha Bwana wake mpendwa. Kwa muda wa miaka karibu thelathini Yesu alimhudumia katika kazi za nyumbani. Na sasa hata katika taabu yake ya mwisho alimfikiria mama yake mjane mwenye huzuni. Wale wanaomfuata Yesu watawaheshimu na kuwatunza wazazi wao. Kutoka katika moyo ambapo upendo wake unathaminiwa, baba na mama hawatakosa matunzo na huruma ya upendo. Na sasa Bwana wa utukufu alikuwa karibu kufa. Yote yalikuwa ni huzuni tupu. Siyo hofu ya kifo, wala ya maumivu ya msalaba iliyosababisha uchungu moyoni mwake. Mateso yake yalitokana na ubaya wa dhambi. Kristo aliona jinsi ambavyo ni watu wachache watakaoweza kuzishinda nguvu zake. Bila ya msaada kutoka kwa Mungu, wanadamu wataangamia tu, na aliona maelfu wakiangamia huku wakiwa karibu na msaada.

### Mzigo wa Kuogofya Alioubeba Kristo

Juu ya Kristo ambaye ni badala yetu na mdhamini wetu yalitwikwa maovu yetu yote. Hatia ya kila mzao wa Adamu, iliuelemeza moyo wake. Katika maisha yake yote, Kristo alikuwa akitangaza habari njema ya msamaha wa upendo wa Baba, lakini sasa akiwa amelemewa na uzito wa hatia ya ulimwengu hakuweza kuuona uso wa upatanisho wa Baba. Hili liliuchoma moyo wake kwa uchungu usioweza kueleweka kwa mwanadamu. Uchungu huu wa rohoni ulikuwa mkubwa mno kiasi kwamba maumivu ya mwilini hayakuweza kusikika.

[427] Shetani alisonga moyo wa Yesu kwa majaribu makali Tumaini halikuonyesha kufufuka kutoka kahurim kama mshindi au kumjulisha kuwa amekubalika na Baba.

Kristo alisikia uchungu ule wenye dhambi watakaosikia wakati ule huruma zitakapokoma kuwatetea wenye dhambi. Ilikuwa ni ile hali ya dhambi, iliyoleta ghadhabu ya Baba dhidi yake akiwa badala ya mwanadamu, ndiyo iliyoupasua moyo wa Mwana wa Mungu.

Majeshi ya mbinguni yalifunika nyuso zao wasione lile tukio la kutisha. Jua pia lilikataa kuangalia hali hiyo ya kutisha. Nuru yake ilikuwa ikimulika dunia wakati wa adhuhuri wakati ilipozimika ghafla. Kukawa giza kamili lilifunika msalaba. "Palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa." Hapakuwa na sababu za kawaida kuhusu giza hilo ambalo lililokuwa nene kama giza la usiku wa manane usiokuwa na mbalamwezi au nyota. Ulikuwa muujiza uliotolewa na Mungu ili kwamba imani ya vizazi vijavyo ithibitike.

Katika giza hilo nene kuwako kwa Mungu kulifichika. Mungu na malaika watakatifu walikuwako kando ya msalaba. Baba alikuwa pamoja na Mwanawe. Lakini kuwako kwake hakukufunuliwa. Katika saa hiyo ya kutisha Kristo hakupaswa kufarijiwa kwa kuwako kwake Baba. Katika giza hilo nene kuwako kwa Mungu kulifichika. Mungu pamoja na malaika watakatifu walikuwepo kando ya msalaba. Wote waliomwona Kristo katika mateso yake walisadikishwa juu ya Uungu wake. Wakati wote wa maumivu yake, alikuwa akitazamwa na umati uliomzomea. Sasa kwa rehema za Mungu alifichwa kwa vazi la Mungu.

Hofu isiyosemeka iliwapata wale waliokuwa pale msalabani. Mizaha na matusi vilikoma. Radi ilimulika mara kwa mara kutoka

katika wingu na kumfanya Mkombozi aliyesulubiwa kuonekana. Makuhani, wakuu wanyongaji na ile halaiki wote wakidhani kuwa siku ya upatilizo wao imefika. Wengine walinong'ona kuwa sasa Yesu atatelemka kutoka msalabani. Panapo saa tisa giza likatoweka sehemu waliyokuwa watu, ila likawa bado linamzunguka Mwokozi. Hakuna jicho lililoweza kupenya utusitusi ulioifunika roho iliyoteseka ya Kristo. Kisha "Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akasema, Eloi, Eloi, lama sabakthani?" yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Wengine wakasema kuwa adhabu ya mbinguni inamkalia kwa sababu alijiita kuwa Mwana wa Mungu! Wengi waliomwamii walisikia kilio chake cha kukata tamaa. Matumaini yakawatoka. Ikiwa Mungu amemwacha Yesu, wafuasi wake watatumaini nini?

### Nafasi ya Mwisho Kuonyesha Huruma ya Kibinadamu [428]

Giza lilipomalizika, Kristo alisikia uchungu mwilini mwake, akasema, "Naona kiu." Mmoja wa askari wa Kirumi akaona huruma, akachukua ufito wa hisopo uliokuwa na sifongo juu yake na akauchovya katika siki akampa. Lakini makuhani walidhihaki maumivu yake. Maneno aliyosema; "Eloi, Eloi, lama sabakthani?" waliyatafsiri visivyo, wakasema: "Huyu anamwita Eliya." Wakakataa nafasi ya mwisho ya kupooza maumivu yake. "Acha; na tuone kama Eliya anakuja kumwokoa."

Mwana wa Mungu asiye na mawaa alitundikwa msala-bani, mwili wake ukiwa umepasukapasuka kwa kupigwa mijeledi; mikono ile ambayo mara kwa mara ilitumika katika kubariki, ikiwa imepigiliwa katika msalaba kwa misumari; ile miguu iliyotembea bila kuchoka katika huduma ya upendo, ikiwa imekongomewa mtini; ile midomo iliyotetemeka ilitoa kilio cha ole. Na yale yote aliyavumilia matone ya damu yaliyotiririka kutoka katika kichwa chake, mikono yake; miguu yake maumivu ya uchungu yalitikisa mwili wake, na uchungu usioelezeka ulioujaza moyo wake kwa sababu ya kufichika uso wa Baba yake humwambia kila mtoto wa Adamu, yakitangaza kwamba sababu yako Mwana wa Mungu alikubali kubeba mzigo huu wa hatia; kwa ajili yako aliangamiza mamlaka ya mauti; kwa ajili yako alifungua malango ya Paradiso; kwa ajili yako alijitoa mwenyewe kuwa kafara kutoka upendo kuja kwako.

## Kristo Afa Kifo cha Ushindi

Ghafla giza lilitoweka msalabani. Na kwa sauti kama ya tarumbeta ambayo ilisikika kuvuma ulimwenguni kote, Yesu akapaza sauti, "Imekwisha." "Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." Nuru ikauzingira msalaba, na uso wa Mwokozi ukang'aa kwa utukufu kama jua. Kisha akainamisha kichwa chake akakata roho. Katikati ya giza hilo la kutisha, Kristo alikuwa amekunywa mashudu yote katika kikombe cha msiba wa wanadamu. Katika saa hizo za kutisha alikuwa ametegemea ushuhuda wa kukubalika na Baba yake uliokuwa umetolewa kwake hapo awali. Akiwa anaifahamu tabia ya Baba yake, kwa imani alimtumaini yeye ambaye ilikuwa daima furaha yake kumtii. Na kadiri alivyojitoa kwa Mungu, ile hali ya kupoteza upendeleo wa Baba yake ilitoweka. Kwa imani, Kristo alikuwa mshindi.

Tena giza likaifunika nchi, na kukatukia tetemeko kuu la nchi. [429] Kukawa na wasiwasi. Katika milima ya karibu miamba ilipasuka mapande na kuviringika mabondeni. Makaburi yalifunguliwa na wafu wakatupwa nje. Makuhani, askari, wanyongaji, na watu wote waliokuwapo hapo walianguka kifudifudi. Wakati sauti ya kilio "Imekwisha" iliposikika kutoka mdomoni mwa Kristo, ilikuwa ni wakati wa kutoa dhabihu ya jioni. Kondoo anayemwakilisha Kristo alikuwa ameletwa kuchinjwa. Kuhani alisimama na kisu tayari hali watu wakiangalia.

Lakini nchi ilitetemeka kwa sababu Bwana Mwenyewe alikaribia karibu. Kwa sauti ya mpasuko, pazia la hekalu likapasuliwa kwa mkono usioonekana vipande viwili toka juu hata chini; na kukifungua wazi kwa macho ya watu chumba cha patakatifu pa patakatifu palipokuwa pakijaa utukufu wa Mungu. Mahali patakatifu mno pa hekalu la dunia hapakuwa patakatifu tena.

Kote kukawa na hofu kuu na kuchanganyikiwa. Kuhani alikuwa karibu kumchinja kondoo wa kafara; lakini kisu kilianguka kutoka mkononi mwa kuhani na yule kondoo akakimbia; Mfano ulikuwa umekutana na kilicho asili ya mfano. Sadaka kuu ilikuwa imetolewa. Sasa njia mpya na iliyo hai ilikuwa imetolewa kwa wote. Tangu sasa Mwokozi atahudumu kama kuhani na mtetezi katika mbingu za mbingu. "Kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika

Patakatifu, akiisha kupata baada ya kupokea ukombozi wa milele" (kwa ajli yetu). Waebrania 9:12.

## [430] 79 — Jinsi Kifo Cha Kristo Kilivyomshinda Shetani

Kristo alikuwa ametimiza kazi aliyokuja kuifanya na kwa pumzi yake ya mwisho akasema kwa sauti kuu "Imekwisha." Yohana 19:30. Alikuwa ameshinda vita. Mbingu yote ilishangilia kwa ushindi wa Mwokozi. Shetani alijua kuwa utawala wake umekwisha. Ilikuwa ni kwa ajili ya malaika, sayari ambazo hazikuanguka na kwa ajili yetu pia kwamba kazi kubwa ya ukombozi ilikuwa imekamilishwa. Hadi ya kifo cha Kristo, Shetani alikuwa amejificha kabisa asijulikane jinsi alivyo, hata malaika watakatifu hawakufahamu kanuni zake wala kuona kwa wazi asili ya uasi wake. Lusifa alikuwa kerubi wa kusitiri, mwenye hadhi ya juu kuliko viumbe vyote. Alikuwa msitari wa mbele katika kuelezea makusudi ya Mungu katika ulimwengu. Baada ya kufanya dhambi uwezo wake wa kudanganya ulikuwa mwerevu mno na kugundua tabia yake ilikuwa vigumu zaidi kwa sababu ya utukufu aliokuwa nao pamoja na Baba hapo awali.

Mungu angeweza kumwangamiza Shetani na malaika waliomuunga mkono, lakini hakufanya hivyo. Kutumia nguvu na kulazimisha hupatikana tu chini ya serikali ya Shetani. Utawala wa Mungu umejengwa katika wema, rehema, upendo, na kanuni hizi ndizo zinazotumika. Serikali ya Mungu ni adilifu, na kweli na upendo, ndizo kanuni za mamlaka yake. Katika baraza la mbinguni iliamriwa kuwa lazima muda utolewe kwa Shetani kuweza kudhihirisha kanuni za utawala wake waziwazi. Maana alikuwa amedai kuwa utawala wake ulikuwa bora zaidi kuliko wa Mungu. Muda ulitolewa kwa kanuni za Shetani kutenda kazi, kusudi wakazi wa mbinguni wapate fursa ya kuona matokeo ya utawala wake. Kwa muda wa miaka 4,000 Kristo alikuwa akifanya kazi ya kumwinua mwanadamu na Shetani akidhamiria kumwangamiza. Walioko mbinguni walikuwa wakiyaangalia hayo.

Tangu wakati ule Yesu alipoonekana kama mtoto huko
[431] Bethlehemu, Shetani alijitahidi kumwangamiza. Alitafuta njia ya kumzuia asiendeleze tabia njema akiwa mtoto, mtu mzima mkamilifu huduma takatifu, na kafara isiyo na mawaa. Lakini Shetani

alishindwa. Hakuweza kumshawishi Yesu afanye dhambi. Juhudi zote za Shetani dhidi ya Yesu zilidhihirisha kwa nuru ya wazi tabia isiyokuwa na kasoro.

Kwa hamu kuu wakaaji wa mbinguni na wa sayari zingine ambazo hazikuanguka waliangalia hatua za mwisho za hili pambano kuu. Walisikia kilio chake cha uchungu, "Baba, yangu ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Mathayo 26:39. Walimwona akihuzunika kwa uchungu uliopita pambano la mwisho dhidi ya mauti. Jasho la damu, lililazimika kuchuruzika usoni na mara tatu ombi la kuokolewa lilimtoka. Mbingu zilishindwa kuendelea kuvumilia hali hiyo na mjumbe alitumwa kuja kumfariji, Mwana wa Mungu.

### Dunia Tamasha; Mbingu Watazamaji

Mbingu iliangalia Kafara akisalitiwa na kwa ukatili akikimbizwa kutoka mahakama moja hadi nyingine. Mbingu zilisikia dhihaka za watesi wake na kukanwa kwa kiapo na mmoja wa wanafunzi wake. Mbingu ilimwona Mwokozi akikokotwa huku na huko kutoka Ikulu mpaka jumba la hukumu, mara mbili kwa makuhani, mara mbili kwa Sanhedrini, mara mbili mbele ya Pilato na mara moja mbele ya Herode, akidhihakiwa, kupigwa, kuhukumiwa na kupelekwa kusulibiwa.

Mbingu iliangalia kwa mshangao Kristo, akiwa ametundikwa msalabani, damu ikitiririka kutoka katika jeraha za kichwani, mikononi na miguuni. Majeraha yake yaliachama kutokana na uzito wa mwili wake kuning'inia kwa mikono peke yake. Roho yake ilitweta chini ya uzito wa dhambi za ulimwengu. Mbingu yote ilijazwa na mshangao wakati Kristo alipoomba katikati ya mateso yake makali, kuwa "Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo" (Luka 32:34).

Nguvu za giza zilizozunguka msalaba zilitupa kivuli cha kutokuamini mioyoni mwa watu. Wakala wa Shetani waliwafanya watu waamini kuwa Yesu ni mwenye dhambi mkuu hivyo amefanywa awe mtu wa kuchukiwa. Wale waliokuwa wakimdhihaki Kristo walijazwa na roho ya mwasi mkuu wa kwanza. Alichochea dhihaka zao. Lakini pamoja na hayo yote hakufaulu jambo lo lote.

Kama Kristo angaliruhusu jambo lo lote la Shetani ili kuepukana na mateso ya kutisha yaliyomsibu, adui angelishinda. Kristo ali- [432]

inamisha kichwa chake na kukata roho, lakini alishikilia kikamilifu imani yake. "Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu mchana na usiku." Ufunuo 12:10.

Shetani aliona kuwa hila zake zote zimefichuliwa. Alikuwa amejidhihirisha mwenyewe kuwa ni mwuaji. Kwa kuimwaga damu ya Mwana wa Mungu, alikuwa amejing'oa mwenyewe kutoka katika fadhili za wakaaji wambinguni. Tangu hapo hawezi tena kuwatokea njia ni malaika wakitoka mbele za Mungu na kuwashitaki ndugu za Yesu kuwa wamefunikwa kwa unajisi wa dhambi. Kiungo cha mwisho cha fadhili kati ya Shetani na wenyeji wa mbinguni kilikatwa.

Hata hivyo malaika hawakuelewa yale yote yaliyohusika katika hili pambano kuu. Kanuni zilizohatarishwa lazima zidhihirike waziwazi. Mwanadamu na pia malaika lazima waone wazi tofauti iliyoko kati ya Mkuu wa nuru na mkuu wa giza. Kila mtu hana budi kuchagua yule atakayemtumikia.

Mwanzoni mwa pambano kuu, Shetani alitangaza kwamba sheria ya Mungu haiwezekani kushikwa, na kwamba haki haipatani vema na rehema, na kwamba ikiwa sheria itavunjwa, itakuwa vigumu kwa mwenye dhambi kusamehewa. Ikiwa Mungu ataondoa adhabu ya dhambi, Shetani alisisitiza, hawezi kuwa Mungu wa haki. Shetani alisema kuwa watu wanapovunja sheria ya Mungu, ni uthibitisho kuwa sheria hiyo haiwezekani kushikwa; mwanadamu hawezi kusamehewa. Kwa sababu yeye, baada ya uasi wake, alifukuzwa kutoka mbinguni, Shetani alidai kuwa, binadamu sharti angetengwa milele na fadhili za Mungu. Mungu hawezi kamwe kuwa mwenye haki, na wakati ule ule aonyesha rehema kwa mwenye dhambi.

Lakini mwanadamu alikuwa katika hali tofauti na ile ya Shetani. Lusifa alifanya dhambi katika utukufu wa Mungu. Shetani aliamua kufuata mapenzi yake ya ubinafsi huku akiwa anaielewa tabia ya Mungu. Hakuna jambo lo lote zaidi ambalo Mungu angelifanya ili amwokoe. Lakini mwanadamu alidanganywa, mawazo yake yakiwa yamefumbwa kwa werevu wa Shetani. Hakuelewa urefu wala kina

cha upendo wa Mungu. Kwa kuangalia tabia ya Mungu huenda ataweza kuvutwa amrudie Mungu.

### Jinsi Haki Ilivyochangamana na Rehema [433]

Rehema za Mungu zilidhihirika kwa wanadamu kwa njia ya Yesu; lakini rehema haziwezi kutangua haki. Sheria isingeweza kubadilika, lakini Mungu alijitoa kafara mwenyewe kwa njia ya Kristo kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." 2 Wakorintho 5:9. Sheria huhitaji maisha ya haki na tabia kamilifu, na haya yasingeweza kutolewa na mwanadamu. Lakini Kristo, kama mwanadamu, aliishi maisha matakatifu na kukuza tabia kamilifu. Hali hizi huzitoa kama karama ya bure kwa watu wote wanaompokea. Maisha yake yanasimama badala ya maisha ya wanadamu. Kwa hiyo hufutiwa makosa yao ya zamani. Zaidi ya hayo, Kristo huwajaza wanadamu kwa sifa za Mungu. Huumba tabia ya mwanadamu kwa mfano wa tabia ya Mungu. Hivyo "haki itokayo kwa sheria" hutimilika katika yeye aaminiye katika Kristo. Mungu anaweza kuwa "mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yeye amwaminiye Yesu." Warumi 3:26.

Lilikuwa kusudi la Shetani kutenganisha rehema kutoka katika kweli na haki. Lakini Kristo alionyesha kuwa katika mpango wa Mungu mambo hayo huungana pamoja; moja haliwezi kuwepo pasipo jingine. "Haki na amani zimebusiana." Zaburi 85:10.

Kwa maisha yake na kifo chake, Kristo alithibitisha kuwa haki ya Mungu haikuangamiza rehema zake, bali kwamba dhambi inaweza kusamehewa, na kwamba sheria ni ya haki, na inaweza kushikwa kikamilifu. Mashitaka ya Shetani yalikanushwa.

Udanganyifu mwingine ulikuwa sasa uletwe. Shetani alidai kuwa kifo cha Kristo kilitangua sheria ya Baba. Kama ingaliwezekana kwa sheria kubadilishwa ama kutanguliwa basi kusingekuwa na haja ya Kristo kufa. Lakini kutangua sheria kungedumisha milele uasi na kuuweka ulimwengu chini ya mamlaka ya Shetani. Kwa kuwa sheria haibadiliki, Yesu aliinuliwa juu ya msalaba. Hata hivyo kwa njia ile Kristo aliyoimarishia sheria, Shetani alitumia kuonyesha kuwa ni kufutwa kwa sheria. Hapa ndipo litakapotokea pambano kuu la mwisho kati ya Kristo na Shetani.

## "Mtindo Mpya" wa Uongo wa Shetani

Kuwa sehemu fulani ya sheria iliyotamkwa na sauti ya Mungu mwenyewe imewekwa kando ndilo dai ambalo Shetani sasa hujitahidi kulitoa. Haihitaji kuishambulia sheria yote; ikiwa anaweza kuwaongoza wanadamu kutoijali kanuni moja, kusudi lake hutimia.
[434] Kwa "Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akijikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10. Kule kukubali kuvunja amri moja wanadamu huwa mateka chini ya mamlaka ya Shetani. Unabii huonya juu ya ile nguvu kuu ya uasi, itendayo kazi kwa niaba ya Shetani. "Naye atanena maneno kinyume chake Akaye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mkononi mwake." Daniel 7:25. Watu wataweka sheria zao kutenda kazi kinyume cha sheria ya Mungu, na katika juhudi zao kulazimisha utii kwa sheria hizi watawatesa wanadamu wenzao.

Vita dhidi ya sheria za Mungu itaendelea mpaka mwisho wa dunia. Watu wote watatakiwa wachague baina ya sheria za Mungu na zile za wanadamu. Kutakuwa na makundi mawili tu. Kila tabia itadhihirika kikamilifu. Wote wataonyesha ikiwa wamechagua kuwa watii au kuwa waasi.

Kisha mwisho utakuja. Mungu ataidhibitisha sheria yake, na kuwaokoa watu wake. Shetani na wale wote wanaomuunga mkono katika uasi watakatiliwa mbali. Dhambi na wenye dhambi vitaangamizwa, shina na tawi." (Tazama Malaki 4:1.) Hili silo tendo dhalimu kwa upande wa Mungu. Wakataaji Wa rehema zake wanavuna walichopanda. Mungu ni chemichemi ya uzima, na mtu akichagua dhambi, hujiondoa mwenyewe kutoka uzima. Kristo anasema, "Na wao wanichukiao hupenda mauti." Mithali 8:36. Mungu huwapa maisha ili wapate kukuza tabia yao na kudhihirisha kanuni zao. Hii ikikamilika, watapokea thawabu ya uchaguzi wao wenyewe. Shetani na wale wote wanaojiunga naye hujikinga kando na amani ya Mungu kiasi kwamba kuwako kwake Aliye upendo kutawaangamiza.

Mwanzo wa pambano kuu, malaika hawakulielewa vema. Kama Shetani na wafuasi wake wangaliangamizwa papo hapo, mashaka kuhusu wema wa Mungu yangalibaki mawazoni mwao na hivyo kuwa mbegu mbaya ambayo ingezaa tunda lake la dhambi ya mauti.

Lakini haitakuwa hivyo baada ya pambano kuu kumalizika. Hapo mpango wa Mungu wa ukombozi ukiwa umekamilika, tabia ya Mungu imedhihirika kwa viumbe wote. Kanuni za sheria yake zinaonekana kuwa kamilifu na zisizobadilika. Dhambi imedhihirisha asili yake, Shetani tabia yake. Kuangamizwa kwa dhambi kutathibitisha upendo wa Mungu na kuanzisha heshima yake mbele za ulimwengu wote.

Hapo basi, huenda malaika wakafurahia kumtazama Mwokozi [435]
akiwa msalabani; kwa sababu hata kama hapo mwanzo hawakuelewa yote, walifahamu kuwa kuangamizwa kwa Shetani kulihakikishwa, ukombozi wa mwanadamu hakika, na ulimwengu kufanywa salama milele.

Kristo Mwenyewe alitambua matokeo ya kafara iliyofanywa Kalwari. Aliyatazamia haya yote alipolia kwa sauti ya kushangilia akiwa msalabani na kusema, “Imekwisha.”

[436] # 80 — Yesu Apumzika Katika Kaburi La Yusufu

Hatimaye siku ya fedheha na mateso ilikwisha. Wakati jua lilipokuwa likikaribisha Sabato, Mwana wa Mungu alipumzika katika kaburi la Yusufu; kazi yake ikiwa imemalizika. Mwanzoni Baba na Mwana walipumzika baada ya kazi yao ya uumbaji. (Tazama Mwanzo 2: 1.) Mbingu yote ilishangilia kutafakari tukio hilo la utakatifu. Sasa Yesu alipumzika baada ya kazi ya ukombozi: ingawa duniani kulikuwa na huzuni kwa wale walionipenda, lakini mbinguni kulikuwa na shangwe kuu. Mungu na malaika waliliona taifa lililokombolewa ambalo baada ya kuishinda dhambi, kamwe wasingeweza kushindwa hii ikiwa ni matokeo yatakayotokana na kazi ya Kristo iliyokamilika.

Wakati "vitu vyote vitafanywa upya." Mnd 3:21. Sabato ya uumbaji, siku ambayo Yesu alilala akipumzikia katika kaburi la Yusufu, bado itakuwa ni siku ya kupumzika na kufurahi. "Sabato hadi Sabato." Isaya 66:23. Mataifa ya waliookolewa watasujudu kwa furaha kumwabudu Mungu Mwana kondoo. Katika matukio ya mwisho ya siku ya kusulibishwa ushahidi mpya juu ya Uungu wa Kristo ulitolewa. Kilio cha mwisho cha Yesu kukata roho kilipotolewa, sauti nyingine ilisikika ikisema: "Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu." Mathayo 27:54. Maneno hayo hayakusemwa kwa kunong'oneza. Ni nani aliyeyasema? Ni (akida) askari wa Kirumi. Uvumilivu wa Uungu wa Mwokozi, kifo chake cha ghafula, kilio kikuu cha ushindi kilichotoka mdomoni mwake vilimthibitishia Mrumi huyu mshenzi. Katika mwili wenye majeraha uliongikwa msalabani huyu akida alimtambua Mwana wa Mungu. Katika siku ile ya kifo chake Mkombozi, watu watatu walitangaza imani yao yule aliyekuwa mkuu wa kikosi cha ulinzi cha Kirumi, yule aliyebeba msalaba na yule aliyekufa kando yake. Jioni ilipokaribia hali ya kimya isiyokuwa ya kawaida ilitulia juu ya Kalivari. Watu wengi
[437] walikuwa wamekusanyika kutokana na udadisi na wala siyo kutokana na chuki kwa Yesu. Hata hivyo walimwangalia Yesu kama mkosaji. Wakiwa chini ya msisimko usio wa asili walikuwa wameju-

muika katika kumdhihaki. Lakini giza lilipofunika nchi, walijisikia wenye hatia ya kosa kubwa. Giza lilipotoweka walielekea nyumbani kwao wakiwa kimya, huku wakiamini kuwa mashitaka ya makuhani yalikuwa ya uongo, kwamba Yesu hakuwa mwenye kujifanya. Majuma machache baadaye, wakati

Petro alipohubiri siku ya Pentekoste walikuwa miongoni mwa maelfu walioongoka kumfuata Kristo.

Lakini wakuu wa Wayahudi hawakubadilika; chuki yao ilikuwa bado kupungua. Giza lililofunika nchi wakati wa kifo cha Kristo lilikuwa dogo kuliko giza lililofunika mioyo yao. Vitu vya asili visivyo na uhai vilikuwa vimeshuhudia Uungu wa Kristo. Lakini makuhani na wakuu wa Israeli hawakumjua Mwana wa Mungu. Walimwua Kristo; lakini hata katika saa ya kile kilichoonekana kama ushindi wao, walisumbuliwa na mashaka. Kutatokea nini tena? Walisikia sauti ikisema, "Imekwisha." (Yohana 19:30). Walikuwa wamesikia tetemeko kuu la nchi, na walikuwa na hofu. Walitishika na Kristo aliyekuwa marehemu zaidi kuliko walivyomwogopa Kristo aliyekuwa hai. Walihofia jambo lo lote lile lililohusiana na kusulibishwa kwake.

Kwa hali yo yote ile wasingeacha mwili wake uwe msalabani na Sabato. Lingekuwa jambo la kuvunja utakatifu wa Sabato kuiacha miili ikiangikwa msalabani. Kwa hiyo wakitumia hili kama kisingizio, viongozi wa Kiyahudi walimwomba Pilato kwamba kifo cha waliosulibishwa kiharakishwe, na miili yao iondolewe kabla ya jua kuchwa. Kibali chake kikiwa kimetolewa, miguu ya wale wezi wawili ilivunjwa ili kuharakisha kifo chao; lakini Yesu alikuwa tayari amekwisha kufa. Askari wale jeuri, wakiwa wamepoozwa na waliyoyasikia na kuyaona juu ya Kristo, walijizuia wasivunje viungo vyake. Na hivyo sheria ya Pasaka ikatimia, "Wasisaze kitu chake cho, chote hata asubuhi, wala wasimvunje mfupa wake." Hesabu 9:12.

Makuhani na wakuu walishangaa kumkuta Kristo amekufa. Ilikuwa haijasikiwa kwamba mtu aliyesulubishwa amekufa saa sita tu baada ya kusulibishwa. Makuhani walitaka kuhakikisha kwamba Yesu amekwisha kufa kweli, kwa hiyo walimshauri askari amchome mkuki ubavuni. Kutoka katika jeraha hilo, kulichuruzika vijito viwili mbali mbali, kimoja cha damu na kingine cha maji. Yohana anaeleza: "Lakini askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki;

[438] na mara ikatoka damu na maji. Naye aliyeona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli, .... Kwa maana hayo yalitukia ili andiko litimie. Hapana mfuko wake utakaovunjwa." Na tena andiko lingine lanenwa, "Watamtazama yeye waliomchoma." Yohana 19:34-37.

Baada ya kufufuka kwake, makuhani walieneza habari kwamba Kristo hakufa msalabani, bali alizimia tu na baadaye alihuishwa. Kitendo cha askari wa Kirumi kili-thibitisha kuwa alikuwa amekufa hakika. Kama asingekuwa amekufa, lile jeraha la mkuki lingesababisha kifo cha mara moja.

Lakini Kristo hakufa kwa kuchomwa mkuki, au kutokana na maumivu ya msalabani. Kile kilio kilichotolewa kwa sauti tena kwa nguvu (Mathayo 27:50; Luka 23:46), wakati wa kukata roho na mchuruziko wa damu na maji vilitangaza kuwa alikuwa amekufa kutokana na kupasuka kwa moyo, uliopasuka kwa uchungu wa mawazo, akiwa ameuawa na dhambi za ulimwengu.

## Wanafunzi Wakata Tamaa

Matumaini ya wanafunzi yalitoweka wakati Kristo alipokufa. Mpaka mwisho hawakuwa wameamini kuwa atakufa; sasa ilikuwia vigumu kuamini amekufa. Wakiwa wamelemewa na huzuni hawakuweza kufarijika kwa neno lo lote Yesu alilolisema. Imani yao kwa Yesu ilikuwa imepotea kabisa, lakini walikuwa hawajapata kumpenda Bwana wao kama sasa au kujisikia hitaji la kuwako kwake. Wanafunzi wa Kristo walitamani sasa kumpatia mazishi ya heshimu, ila hawakufahamu jinsi ya kufanya hivyo. Watu waliouawa kwa sababu ya uhaini dhidi ya serikall ya Warumi walizikwa katika ardhi ya kuzikia waalifu. Yohana na wanawake kutoka Galilaya wasingeweza kuuacha mwili wa Bwana wao ushughulikiwe na askari wasiyo na huruma na kuzikwa katika kaburi lisilo na heshima. Walakini hawakuweza kupata upendeleo wo wote kutoka kwa viongozi wa Wayahudi na wala hawakuwa na ushawishi wo wote na Pilato.

Katika hali isiyotazamiwa, Yusufu wa Arimathaya pamoja na Nikodemo walijitokeza kutoa msaada kwa wanafunzi. Wote walikuwa wajumbe wa Baraza kuu la Kiyahudi (Sanhedrini,) wote walikuwa matajiri na walioheshimiwa, na wote walifahamiana na

Pilato. Waliazimia kwamba mwili wa Yesu upate mazishi ya heshima.

### Msaada Kutoka Sehemu Isiyotazamiwa

Yusufu alikwenda kwa Pilato kiujasiri akamwomba mwili wa Yesu. Kwa mara ya kwanza, Pilato akajua kuwa Yesu amekwisha kufa. Habari za kifo cha Yesu ziliachwa kuelezwa kwa Pilato kwa makusudi. Alipopata ombi la Yusufu, alimwita yule akida aliyepewa jukumu la ulinzi pale msalabani na akapata maelezo ya mambo na matukio ya Kalivari ili kuthibitisha ushuhuda wa Yusufu. Yusufu akapata ruhusa ya Pilato kuuchukua mwili wa Kristo, na Nikodemo naye akaja na manukato na udi ya thamani yapata ratli mia ili kupaka mwili wa Yesu. Mheshimiwa kushinda wote katika Yerusalemu hangeheshimiwa kiasi hicho katika mazishi yake. Wanafunzi walishangaa sana. [439]

Wakati Mwokozi alipokuwa angali hai Yusufu wala Nikodemo hawakujidhihirisha kuwa walimkubali. Hatua kama hiyo ingesababisha watolewe katika Sanhedrini, na wao walitaka kumlinda na mvuto wao. Lakini Wayahudi wenye hila walikwamisha mipango yao. Wakiwa hawapo Yesu alihukumiwa. Sasa Yusufu na Nikodemo hawakuweza tena kuficha uhusiano wao kwake. Sasa wakajitokeza kijasiri kuwasaidia wanafunzi masikini. Kwa taadhima na taratibu kwa mikono yao weyewe wakaushusha mwili wa Yesu kutoka msalabani. Machozi ya huruma yaliwatoka walipoutazama mwili uliochubuliwa na kujeruhiwa. Yusufu alikuwa na kaburi jipya lililochongwa mwambani kwa ajili yake binafsi. Nalo lilikuwa karibu na Kalvari, na sasa akaliandaa kwa ajili ya Yesu. Hapo wale wanafunzi watatu walinyosha viungo vyake, na kuikunjia kifuani mwake mikono iliyochubuliwa na kumweka kaburini. Kisha jiwe zito liliviringishwa na kuwekwa mlangoni mwa kaburi, na Mwokozi kaachwa apumzike.

Wakati giza la jioni lilipokuwa linasogea, Mariamu Magdalena na Mariamu wengine walivinjari mahali alipolala Bwana wao wakiwa wanatiririkwa na machozi ya huzuni. "Wakarudi . . . wakastarehe siku ya Sabato kama ilivyoamriwa." Luka 23:56.

Hiyo ilikuwa Sabato isiyoweza kusahaulika kamwe kwa wanafunzi wake, na makuhani, wakuu, waandishi na watu wote. Pasaka

iliadhimishwa kama ilivyokuwa ikifanyika kwa karne zote, wakati aliyemwakilisha alikuwa amelala katika kaburi la Yusufu. Viwanja vya hekalu vilijaa watu waliokuja kuabudu. Kuhani mkuu alikuweko pale, akiwa amevalia mavazi yake rasmi. Makuhani wakiwa wenye shughuli nyingi waliendelea kuhudumu. Ingawa hivyo wengine hawakuwa na mapumziko licha ya damu za ng'ombe na mbuzi kwa
[440] ajili ya dhambi. Walikuwa hawana habari kuwa mfano ulikuwa umekutana na sadaka halisi, kwamba, Sadaka ya thamani mno ilikuwa imetolewa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. Lakini kamwe huduma hiyo haikupata kushuhudiwa na hisia zilizopingana hivyo. Hali isiyo kawaida ilitawala kila kitu. Patakatifu mno palipokuwa pakifichwa pasiingiwe, sasa kutokana na pazia kupasuka toka juu mpaka chini, palionekana kwa macho ya watu wote, Bwana alikuwa hapatambui tena. Kule kufunuliwa kwa patakatifu kuliwatia hofu makuhani kwa kutazamia maafa kuwafika.

# 81 — “Bwana Amefufuka” [441]

Usiku wa siku ya kwanza ulikuwa umepita pole pole. Kristo alikuwa bado mfungwa katika gereza la kaburi lake. Muhuri wa Kirumi ulikuwako kwenye jiwe la kaburini; na askari wa Kirumi wakiwa katika zamu yao ya kulinda kaburi. Kama ingewezekana mkuu wa giza angeendelea milele kumfungia Mwana wa Mungu kaburini. Lakini malaika wa mbinguni wenye uwezo mwingi zaidi walikuwa wanasubiri kumkaribisha Mkuu wa uzima.

“Na tazama palikuwa na tetemeko kubwa la nchi, kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni.” Nuru kuu ya utukufu wa Mungu iliangaza njia yake. “Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji.” Na kwa kumwogopa wale walinzi, wakatetemeka wakawa kama wafu.”

Mjumbe huyu ndiye aliyechukua cheo Shetani alichokuwa nacho mbinguni kabla hajaasi. Alipokuwa akiliviringisha lile jiwe lililowekwa kaburini, mbingu ilionekana kana kwamba inashuka chini. Askari walimwona akiliondoa jiwe lile kubwa kana kwamba anaondoa kijiwe cha changarawe, na wakamsikia akinguruma na kusema; “Mwana wa Mungu, toka uje; Baba yako anakuita.” Walimwona Yesu akitoka kaburini, na wakasikia akitangaza juu ya kaburi lililopasuka, “Mimi ndimi huo ufufuo na uzima.” Alipotoka kwa fahari na utukufu jeshi la malaika likamlaki kwa nyimbo za shangwe.

Walinzi wa Kirumi walipowaona wale malaika na Yesu mwenye utukufu walizimia wakawa kama wafu. Wakati msururu wa utukufu ulipokwisha kutoweka machoni pao ndipo askari waliamka na kuondoka hali wakipepesuka kama walevi, kwenda mjini, wakiwaeleza watu waliokutana nao habari za ajabu zilizowatokea. Walikuwa wanaelekea kwa Pilato, lakini makuhani na wakuu wakawaita kwanza waletwe kwao. Askari wakiwa wanatetemeka na kutweta [442]
waliwaeleza mambo yote waliyona yalivyotokea. Askari walisema: “Hakika aliyesulibishwa alikuwa Mwana wa Mungu, tulisi-kia malaika akimtaja kwamba ni Mtukufu wa mbinguni, Mfalme wa utukufu.

## Kayafa Ahimiza Udanganyifu

Kayafa alijaribu kusema jambo. Midomo ilitikisika, lakini bila neno kutoka. Askari walikuwa tayari kutoka kwenda zao, ndipo Kayafa akasema. Ngojeni, ngojeni kwanza. Msimwambie mtu ye yote mliyoona.

Makuhani wakasema: "Semeni ya kwamba wanafunzi wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipo kuwa tumelala." Hapa makuhani walivuka mpaka. Maana kama walikuwa wamelala watajuaje? Na kama wanafunzi walikuwa na hatia ya kuuiba mwili wa Kristo, makuhani wasingalikuwa wa kwanza kuwahukumu? Au kama walinzi walilala, makuhani wasingaliwachukulia na kuwashitaki kwa Pilato?

Askari waliogopa sana. Kulala katika zamu lilikuwa kosa baya listahililo hukumu ya kifo. Je, watakubali kushuhudia uongo, na kujiweka katika hatari ya kufa? Je, watawezaje kukabili hata kama ni kwa kulipwa fedha ikiwa wanajishuhudia uongo wenyewe?

Makuhani waliahidi kuwalinda askari walinzi hawa, wakisema kuwa Pilato hatataka kusikia habari hizo zikienea kama wao wasivyotaka. Askari wa Kirumi waliuliza uaminifu wao kwa fedha. Walikuja kwa makuhani wakiwa na mzigo wa habari za ukweli wa kushtusha; wakaondoka kurudi wakiwa na mzigo wa fedha, na katika vinywa vyao taarifa ya uongo.

Wakati huo habari za kufufuka kwake Yesu zilikuwa zimefika kwa Pilato. Ingawa alimhukumu Mwokozi bila kutaka, hakuwa na majuto yo yote mpaka sasa. Kwa hofu sasa alijifungia nyumbani mwake, wala hakutaka kuonana na mtu. Lakini makuhani walikwenda kwake, wakamsihi asijali habari za walinzi kutoangalia kazi yao. Yeye mwenyewe aliwauliza walinzi kwa siri, wala hawakumficha neno lo lote, na Pilato alielezwa yote yaliyotokea. Hakuyajali, wala kuyashughulikia mambo hayo, lakini tangu siku hiyo hapakuwa na amani kwake.

Makuhani kwa kumwua Kristo, walijifanya kuwa vyombo vya Shetani. Sasa walikuwa watu wake kamili, wakiwa wamenaswa katika mtego ambao hawakuweza kujinasua, ila tu kuendelea na vita vyao juu ya Kristo. Usalama wao ni kuonyesha kuwa Kristo ni
[443] laghai kwa kukanusha kuwa hakufufuka. Hivyo waliwahonga askari na kumfanya Pilato akae kimya.

Lakini palikuwapo mashahidi wasioweza kuwa nyamazisha. Wengi walikuwa wamesikia ushuhuda wa askari kuhusu kufufuka kwa Kristo. Na hakika ya wafu waliofufuka pamoja na Kristo, walionekana na wengi na kutangaza kuwa Kristo amefufuka. Makuhani na wakuu walikuwa wakihofu daima kuwa siku moja wanaweza kukutana na Kristo mwenyewe njiani. Makufuli na vyuma vilivyowekwa milangoni havikuweza kumzuia Mwana wa Mungu. Daima mchana na usiku lile tukio la kutisha wakati walipopaza sauti kwamba: "Damu yake iwe u yetu na juu ya watoto wetu." Mathayo 27:25. Lilikuwa mbele zao.

## Dhamana ya Ufufuo Wetu

Wakati sauti ya malaika mkuu iliposikika pale kaburini kuwa "Baba yako anakuita", Mwokozi alitoka kaburini akiwa na uzima aliokuwa nao. Kristo alikuwa ametangaza kwa ushindi kwamba "Mimi ndimi huo ufufuo na uzima." Maneno haya yanatamkwa na Mungu peke yake. Viumbe wote walioumbwa hupata uzima kutoka kwa Mungu tu. Ni yeye aliye mamoja na Mungu ndiye awezaye kusema kwamba: Nautoa uzima wangu na kuutwaa tena. (Yohana 10: 18.)

Kristo alifufuka katika wafu kama malimbuko yao waliolala, na ufufuo ulitokea siku ile ile ambayo mganda ungeletwa mbele za kwa Bwana. Kwa muda wa miaka zaidi ya elfu moja, wakati watu walipokuwa wakienda Yerusalemu kwa Pasaka, mganda wa kwanza ulitolewa kama sadaka ya shukurani kwa Bwana. Mganda uliotolewa wakfu kwa Mungu uliwakilisha mavuno. Kwa hiyo ufufuo wa Kristo ni mfano na dhamana ya ufufuo wa wenye haki wote waliokufa. "Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye." (I Wathesalonike 4:14).

## Wengi Walifufuka Pamoja na Yesu

Jinsi Kristo alivyofufuka, aliwaleta wengi wa wafungwa waliolala. (Tazama Mathayo 27:52.) Ni wale walioshuhudia ukweli mpaka wakatoa maisha yao. Sasa watamshuhudia aliyewafufua kutoka katika wafu.

Wakati wa huduma yake, Yesu alikuwa amefufua wafu. Lakini hawa waliofufuliwa hawakuvikwa hali ya kutokufa. Lakini wale [444] waliofufuka wakati wa kufufuka kwa Yesu, walivikwa hali ya kutokufa milele. Walipanda pamoja na Yesu kama nyara wa ushindi wake dhidi ya mauti na kaburi. Waliingia mjini, wakawatokea wengi, wakitangaza kwamba Kristo amefufuka, kutoka kwa wafu nao wamefufuka pamoja naye. Watakatifu waliofufuka walishuhudia ukweli wa maneno; "Wafu wako wataishi, maiti zangu zitafufuka." Isaya 26:19.

Katika Mwokozi wetu, uzima uliopotea kwa sababu ya dhambi, unarudishwa. Alipewa uwezo wa kuwapa watu hali ya kutokufa. Asema: "Mimi Nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele." Yohana 10:10. "Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho." Yohana 6:54. Kwa mkristo kifo ni kulala usingizi wakati wa ukimya na giza. "Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu." Wakolosai 3:4.

Sauti iliyopazwa msalabani, "Imekwisha", itapenyeza makaburi na kuyabomoa, na wafu waliokufa katika Kristo watafufuka. Wakati Kristo alipofufuka makaburi machache yalifunguliwa, lakini wakati wa kuja kwake mara ya pili, watu wake wote walio wateule, watasikia sauti yake, nao watatoka, wakiwa na hali ya utukufu ya kutokufa. Uwezo ule ule uliomwamsha Kristo kutoka kwa wafu utaliinua kanisa lake juu ya nguvu zote, siyo katika dunia hii, bali pia katika ulimwengu ujao.

## 82 — “Mama Unalilia Nini? [445]

Katika siku ya kwanza ya juma, asubuhi na mapema wanawake waliokuwa wamesimama kando ya msalaba, walikwenda kaburini kuupaka mwili wa Mwokozi marhamu. Hawakuwa wanafikiria juu ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu. Jua la matumaini yao lilikuwa limekuchwa. Wala hawakukumbuka maneno yake kuwa, “lakini mimi nitawaona tena.” Yohana 16:22.

Bila hata ya kufahamu kilichokuwa kinatendeka walilikaribia bustani, huku wakisema: “Ni nani atakayetuviringishia lile jiwe mlangoni pa kaburi?” Lo, tazama mbingu zikang’aa kwa utukufu. Nchi ikatetemeka. Jiwe lile kubwa lilikuwa limeviringishwa mbali, na kaburi lililokuwa tupu!

Mariamu Magdalena ndiye aliyefika kaburini mara ya kwanza, na walipoona jiwe limevingirishwa, aliharakisha kwenda kuwaambia wanafunzi, habari hizo. Wakati huo pia wale wanawake wengine wakafika. Nuru ilikuwa iking’aa kaburini, lakini mwili wa Yesu haukuwemo.

Walipokuwa wakizungukazunguka hapo, ghafula wakajikuta kuwa hawako peke yao, kijana mmoja mwenye mavazi meupe alikuwa ameketi kando ya kaburi. Kumbe ni malaika aliyelivingirisha lile jiwe. Alikuwa na umbo la kibinadamu ili asiwaogopeshe watu hawa. Hata hivyo kando yake utukufu wa mbinguni ulikuwa uking’aa, na wale Wanawake waliogopa. Malaika akajibu, akawaambia: “Msiogope, ninyi, kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka, kama alivyosema. Njoni mpatazame mahali alipolazwa. Ninyi nendeni, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu.”

Walipoangalia kaburini malaika mwingine mwenye sura ya kib- [446]
inadamu, alisema: “Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa akaliko Galilaya, akasema: Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu.

Wanawake wale wakakumbuka sasa, Alisema kuwa atafufuka tena! Ni siku ya furaha kiasi gani kwa ulimwengu! "Wakaondoka upesi kutoka kaburini., kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari. Mariamu alikuwa hajasikia habari hizi njema. Aliwaendea Petro na Yohana na habari za huzuni kwamba wamemwondoa Bwana kaburini, wala hatujui walikomweka." Wanafunzi wakakimbia kwenda kaburini wakaona vitambaa na leso ila hawakumwona Bwana wao. Hata hivyo huu ulikuwa ushahidi kuwa Amefufuka. Sanda yake haikuwa imetupwa ovyo, bali ilikunjwa na kuwekwa vizuri. Yohana "akaona akaamini." Sasa akakumbuka maneno ya Mwokozi alivyotabiri kuwa atafufuka.

Kristo Mwenyewe aliweka sanda ile kwa hali ya mpangilio hivyo. Malaika mwenye uwezo alipokuja kutoka mbinguni na hakulivingirisha jiwe, malaika mwingine aliingia na kufungua sanda mwili wa Yesu. Lakini ni mikono ya Mwokozi mwenyewe ndiyo iliikunja sanda na kuiweka katika hali ya safi. Kwake yeye ambaye hata hupanga nyota zote na kuongoza mwendo wao hakuna kisicho na muhimu.

Mariamu alikuwa amewafuata Yohana na Petro mpaka kaburini; waliporudi Yerusalemu, yeye alibakia kaburini. Huzuni ilizidi. Alipotazama ndani ya kaburi aliwaona wote malaika wawili wakiwa wameketi humo, mmoja upande wakichwa na mwingine upande wa miguuni Yesu alipokuwa amelazwa. Wakamwuliza "Mama unalilia nini? Akawaambia "Kwa sababu wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka."

Kisha aligeuka ili kutafuta mtu wa kuuliza kile kilichoupata mwili wa Yesu. Sauti nyingine ikamwambia, "Mama unalilia nini." Unamtafuta nani? Mariamu huku akitokwa na machozi akamwona mtu ambaye alidhani kuwa ni mtunza bustani, akamwambia, "Bwana ikiwa umemchukua wewe uniambie ulipomweka, nami nitamwondoa." Ikiwa kaburi hili la mtu tajiri halitakiwi kumzika Yesu, yeye atampatia mahali pa kuzikwa. Kulikuwa na kaburi ambalo sauti ya Yesu mwenyewe ililifanya tupu, kaburi ambamo Lazaro alikuwa amelazwa.

Lakini sasa kwa sauti yake iliyozoeleka Yesu alijibu "Mariamu".
[447] Akigeuka alimwona Yesu aliye hai. Kwa shangwe akamrukia akitaka kumkumbatia miguu akasema: "Raboni! Lakini Kristo aliinua mikono yake akasema: "Usinishikilie" "kwa maana sijapaa kwenda

kwa Baba. Lakini nenda kwa ndugu zangu ukawaambie; Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu." Mariamu akaenda zake akiwa na ujumbe wa nderemo.

Yesu alikataa kuheshimiwa na watu wake, kabla hajapaa kwenda mbinguni na kutoka kwa Baba mwenyewe apate uthibitisho kuwa kafara yake kwa ajili ya dhambi za wanadamu imetosha kabisa na kwamba kwa ajili ya damu yake wanadamu wote watapokea uzima wa milele. Baba akathibitisha agano lililofanywa na Kristo, kwamba atawapokea wanadamu wenye toba, na utii na kuwapenda kama anavyompenda Mwana wake. Uwezo wote mbinguni na duniani alipewa mkuu wa Uzima ili aweze kuwapa uwezo wake na utukufu wafuasi wake.

Wakati Mwokozi alipokuwa mbele ya Mungu, akipokea vipawa kwa ajili ya kanisa lake, wanafunzi walikuwa wakiomboleza na kulia. Siku ya mashangilio makuu mbinguni, kwao ilikuwa ni siku ya kiwewe na utata. Kutokuamini kwao ushuhuda wa wanawake kulidhihirisha jinsi imani yao ilivyokuwa imeshuka. Hawakuweza kuamini taarifa ile. Ilikuwa nzuri mno kuweza kuwa kweli walidhani. Waliishasikia dhana nyingi za Masadukayo kiasi kwamba hawakuweza kujua maana ya ufufuo kutoka kwa wafu.

Malaika waliwaambia wale "Lakini enendeni, zenu, mkawaambie wanafunzi wake, na Petro ya kwamba awatangulia kwenda Galilaya, huko mtamwona, kama alivyowaambia." Ujumbe wa malaika hawa kwa wanafunzi ulipaswa kuwasadikisha juu ya ukweli wake. Maneno kama haya yangaliweza tu kuelea na wajumbe wa Bwana wao Aliyefufuka.

Tangu kifo cha Kristo, Petro alikuwa amelemewa na majuto makuu. Aibu ya kumkana Bwana wake ilikuwa daima mawazoni mwake. Alikuwa ameteseka sana kuliko wanafunzi wote. Kwake uthibitisho ulitolewa kuwa toba yake imekubalika. Alitajwa kwa jina.

Mariamu Magdalena alipowaambia wanafunzi kuwa amemwona Bwana, alirudia wito wa kukutana kule Galilaya. Tena ujumbe ulitumwa kwao mara ya tatu. Baada ya kupaa kwa Baba, Yesu aliwatokea wanawake wengine akawaambia: "Nendeni mkawaambie ndugu zangu, waende Galilaya huko watakutana nami.

Kazi ya Yesu ya kwanza baada ya kufufuka ilikuwa
[448] kuwadhihirishia wanafunzi wake juu ya upendo wake usiofifia na kuwajali kwake. Ataendelea kuwavuta kwake kwa kamba za upendo. Alisema; Nendeni mkawaambie ndugu zangu kuwa tukutane Garilaya.

Lakini hata wakati huu wanafunzi walikuwa bado wangali na utata na mashaka. Hata wakati wanawake walipowaambia; kwamba wamemwona Bwana, waliwadhania kuwa wameona mazingaombwe.

Taabu ilionekana kuongezeka juu ya taabu. Walikuwa wamemwona Bwana wao akifa; walijikuta wamepokonywa mwili wake; na walikuwa wameshitakiwa kwa kuiiba mwili wake kusudi kuwadanganya watu. Walikata tamaa kuwa kamwe hawataweza kusahihisha uongo huu uliokuwa unazagaa. Waliogopa uhasama wa makuhani na ghadhabu ya watu. Walitamani mno kuwepo Yesu.

Mara nyingi walirudiarudia maneno haya, "Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli." Luka 24:21. Wakijisikia wapweke na wenye mashaka moyoni, walikutana pamoja katika chumba cha ghorofa, na kufunga milango kwa hofu kuwa yaliyompata Mwalimu wao mpendwa yangeweza kuwapata wakati wo wote ule.

Na kwa wakati wote wangekuwa na furaha katika kufahamu kuwa Mwokozi amefufuka. Watu wengi bado wanafanya kile walichokifanya wanafunzi hawa. Mwokozi yuko kando yao, lakini macho yao yaliyofumbwa na machozi hayamtambui. Anazungumza nao lakini hawaelewi.

"Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka. " Usitazame kaburi lililotupu. Kutoka katika mioyo yenye furaha, kutoka katika midomo iliyoguswa na moto mtakatifu, hebu wimbo wa shangwe usikike, Kristo Amefufuka! Yu hai kutuombea.

## 83 — Kutembea Kwenda Emau [449]

Jioni ya siku ile ile ya kufufuka kwake Kristo, wanafunzi wawili walikuwa njiani wakienda Emau mji mdogo umbali wa maili nane kutoka Yerusalemu. Wanafunzi hawa waliokuwa wamekuja kuadhimisha Pasaka, walikuwa na hali ya wasiwasi mkubwa kuhusu mambo yaliyokuwa yametokea. Walikuwa wamesikia habari za mwili wa Kristo kuondolewa kaburini, pia habari zingine kutoka kwa wanawake waliosema wamewaona malaika na kwamba wamekutana na Yesu. Na sasa wakiwa njiani kurudi nyumbani walikuwa wakiongea matukio ya kesi na kusulibishwa kwa Kristo. Walikuwa hawajapata kukatishwa tamaa hivyo.

Katika kwenda kwao walikutana na kufuatana na mtu wasiyemjua, na kwa vile walikuwa na wasiwasi sana hawakushughulika kumhoji. Waliendelea kuzungumzia yaliyokuwa mioyoni mwao na mafundisho yaliyotolewa na Kristo, ambayo walionekana kutofahamu. Yesu alitamani kuwafaariji. Alielewa utata waliokuwa nao mawazoni, na shauku lililokuwa mioyoni mwao "Mtu huyu, Aliyekabili kudhalalishwa hivyo anaweza akawa ndiye Kristo?" Wakalia. Yesu alitamani kuyafuta machozi yao, na kuwajaza furaha na shangwe. Lakini lazima kwanza awape fundisho ambalo hawatalisahau.

"Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayoseme-zana hivi mnapotembea? Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata hujui yaliyotukia humo siku hizi? Wakamweleza huzuni yao juu ya Bwana wao, "aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote; lakini "wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya kufa, wakamsulibisha." Kwa midomo iliyotetemeka wakaongeza, "Nasi tulikuwa [450]
tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo yote leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo." Ni ajabu kwamba hawakukumbuka maneno ya Kristo, na kwamba

Alikuwa Ametabiri kuwa siku ya tatu Atafufuka. Makuhani na wakubwa hawakusahau!

### Bila Kutambulika, Yesu Afafanua Maandiko

"Kisha akawaambia, Enyi msiofahamu wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii! Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya, na kuingia katika utukufu wake?" Huyu anaweza kuwa nani mwenye kueleza mambo haya kinaganaga hivi na kwa huruma? Kwa mara ya kwanza wakaanza kuwa na tumaini. Kila mara walimtazama kwa makini mtu huyu, na kufikiri kuwa maneno kama hayo ndiyo ambayo yangesemwa na Kristo.

Akianzia kwa Musa, aliye Mwanzo wa unabii wa Biblia, Kristo alifafanua mambo yote katika Maandiko yaliyomhusu Yeye Mwenyewe. Kama angalijijulisha kwao tangu mwanzo, wasingehangaika na haja ya maelezo zaidi. Lakini ilikuwa lazima kwanza waelewe mifano na unabii wa Agano la Kale. Maana kwa hayo ndiyo imani yao ithibitike. Kristo hakufanya muujiza wo wote kuwasadikisha; kazi yake ilikuwa kuyaelezea Maandiko kwanza. Aliwafunulia kutoka kwa manabii kwamba kifo chake kilikuwa ndicho ushahidi wa dhati kwa imani yao.

Yesu alionyesha umuhimu wa Agano la Kale kama shahidi kwa kazi yake. Mwokozi anafunuliwa katika Agano la Kale wazi sawa kama katika Agano Jipya. Nuru kutoka katika unabii wa kale, hudhihirisha maisha ya Kristo na mafundisho ya Agano Jipya, kwa wazi na dhahiri. Uthibitisho wa dhati kuliko miujiza ya Kristo hupatikana katika kulinganisha unabii wa Agano la Kale na historia ya Agano Jipya.

Matazamio ya wanafunzi juu ya Masihi atakayetawala kwa mamlaka ya kifalme kama watu wanavyotamani yalikuwa yamepotoshwa. Wanafunzi wake lazima waelewe kikombe cha mateso alichopaswa kukinywea. Aliwaonyesha kuwa pambano hili la kutisha lilikuwa ni kutimizwa kwa agano lililotolewa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Kristo budi afe, sawa na kila mwenye dhambi atakavyokufa kama akidumu dhambini. Yote lazima yawe hivyo, lakini si katika kushindwa, bali katika ushindi wa utukufu. Yesu aliwaambia kuwa kila juhudi lazima ifanyike ili kuuokoa ulimwengu kutoka dhambini.
[451] Wafuasi wake lazima waishi kama alivyoishi yeye, na kutenda kazi

kama alivyotenda kwa juhudi thabiti.

Hivyo Kristo aliwaeleza wanafunzi wake ili wapate kuyaelewa Maandiko. Alipokuwa akiwaambia juu yo kuangamizwa kwa Yerusalemu, waliutazama mji kwa huzuni. Lakini hata hivyo hawakufahamu mtu wanayesafiri naye ni nani, maana Kristo alijizungumzia kana kwamba ni mtu mwingine. Alitembea kwa uangalifu sana katika njia ya mawe kama wao, hapa na pale akisimama kupumzika kidogo.

## Mioyo Yao Ilivutiwa Kwa Mgeni Huyu

Walipokuwa wakisafiri jua lilikuwa limekuchwa na wafanya kazi mashambani walikwisha rejea kutoka makazini mwao. Wanafunzi walipokaribia kwao, mgeni wao alifanya kana kwamba ana haja kuendelea mbele Lakini wanafunzi wale walitamani kusikia maneno zaidi kutoka kwake. Ndipo wakamshawishi wakisema: "Kaa pamoja nasi." Lakini alielekea kukataa, nao wakamshurutisha, "Kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha." Yesu akakubali, "Akaingia ndani kukaa nao." Kama wanafunzi wasingelimshurutisha kukaa nao, wasingalifahamu kuwa aliyefuatana nao alikuwa Bwana Aliyefufuka. Kristo hajilazimishi kuwa pamoja na mtu ye yote. Ataingia kwa furaha katika nyumba yo yote, lakini ikiwa watu hawajali kumsihii akae, atapitiliza.

Chakula cha kawaida cha jioni kiliandaliwa na kuwekwa mbele ya mgeni aliyekuwa ameketi mahali pa heshima. Sasa aliweka mikono yake juu, akakibariki chakula, kama vile Bwana wao alivyokuwa akifanya. Wanafunzi wakashangaa sana. Walitazama tena kuona mikono iliyopigiliwa kwa misumari. Wakaona Lo, kumbe ni Bwana Yesu! Waliondoka kumwangukia miguuni, lakini akatoweka mbele yao. Wakapatazama mahali alipokuwa ameketi yule ambaye hivi karibuni mwili wake ulikuwa umelala kaburini, nao wakaambiana, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani na kutufunulia Maandiko?"

Wakiwa na habari hizi moto moto za kutawanya, uchovu wao na njaa vilitoweka. Walikiacha chakula bila kukionja wakaharakisha kupitia njia ile ile waliyoijia, kwenda kuwapasha habari wanafunzi wenzao mjini. Walipandisha miinuko, wakiteleza juu ya miamba, wakitamani kwenda haraka kuliko walivyoweza. Wakapotea

njiani, lakini wakaipata njia tena. Wakati mwingine wakikimbia, na
[452] kuteleza, waliendelea na safari, huku mwenzao asiyeonekana akiwa kando kando yao njiani kote.

Usiku ulikuwa wa giza nene, lakini Jua la Haki liliku wa likiwamulikia. Walijiona kana kwamba wamo katika ulimwengu mpya. Kristo amefufuka walirudia rudia kusema hivyo. Ni lazima wawambie wale wenye huzuni kisa cha ajabu kilichotukia njiani kwenda Emau. Ni lazima waeleze juu ya yule Aliyejiunga nao njiani. Walibeba ujumbe mkuu uliowahi kutolewa habari njema ambazo kwazo tumaini la jamii ya wanadamu lilitegemea tangu sasa na milele.

## 84 — Kristo Aliyefufuka Atokea [453]

Wale wanafunzi wawili walipofika Yerusalemu waliingia kupitia katika lango la mashariki wakatembea kupitia barabara nyembamba wakimulikiwa na mng'ao wa mwezi, wakaenda hadi katika chumba cha juu mahali Yesu alipokula pasaka ya mwisho kabla ya kifo chake. Walijua kuwa ndugu zao wangekuwa hapo. Mlango ulikuwa umefungwa kabisa. Walibisha, lakini bila kusikia sauti. Palikuwa kimya. Hivyo walijitaja kwao, mlango ukafunguliwa kwa pole pole sana, wakaingia ndani, na mwingine asiyeonekana akaingia pamoja nao. Kisha mlango ukafungwa ili wapelelezi wasiingie.

Wasafiri hawa waliwakuta wale wengine walikuwa wote wameshikwa na msisimko. Sauti mle chumbani zilisema Bwana amefufuka kweli naye amemtokea Simoni! "Kisha wale wawili wakiwa wanahema kwa haraka haraka waliwaeleza jinsi Yesu alivyowatokea. Wengine walikuwa wakieleza kuwa haiwezekani kuwa kweli, wakati kwa ghafla Mtu mwingine akasimama mbele yao. Hakuna mgeni aliyekuwa amefunguliwa mlango, wala hakuna kishindo cha kutembea mtu kilichosikika akitembea huko nje. Wanafunzi wakashituka. Kisha, wakasikia sauti ya Bwana, kwa wazi na dhahiri "Amani iwe kwenu."

Lakini wakashituka, na kuogopa sana wakidhani ya kwamba wameona roho. Ndipo "Akawaambia, Mbona mnafadhaika? na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa, ni mimi mwenyewe! Nishikeni shikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake."

"Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula cho chote hapa?" Wakampa kipande cha [454]
samaki wa kuokwa. Akakitwaa akala mbele yao. Ndipo wanafunzi walifurahi walipomwona Bwana. Imani ikachukua mahali pa kutoamini, na wakamkubali Mwokozi wao Aliyefufuka.

## Tutawatambua Wapendwa Wetu

Sura ya Mwokozi aliyefufuka, hali yake, usemi wake vyote hivyo wanafunzi wake walivitambua. Jinsi Yesu alivyofufuka kutoka kwa hofu ndivyo wale waliolala katika Kristo watakavyofufuka. Tutawafahamu rafiki zetu, na kuwatambua kama vile wanafunzi wa Yesu walivyomtambua. Katika hali ya utukufu wa mwili, sura zao zitabaki zile zile. Tutawata-mbua wapendwa wetu.

Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake maneno aliyowaambia kabla ya kifo chake. "Ndipo Akawafungulia akili zao wapate kuelewa na Maandiko. Akawaambia: Ndipo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu, na mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia Yerusalemu. Nanyi ni mashahidi wa mambo haya." Maisha Kristo, kifo chake na ufufuo wake, unabii ulioonyesha mambo haya, na utakatifu wa sheria ya Mungu, siri ya mpango wa wokovu, na uwezo wa Yesu wa kusamehe dhambi, yote haya lazima yahubiriwe na kujulishwa kwa ulimwengu wote.

"Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu. Wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wo wote mtakaowafungia dhambi, wamefungiwa." Kumpokea Roho kwa wingi hakukutokea mpaka baada ya kupaa kwa Yesu kwenda mbinguni. Lakini Kristo aliwavuvia Roho wake kuwathibitishia kuwa pasipo Roho Mtakatifu hawataweza kukamilisha kazi yao ya kulijenga kanisa.

Kumwagiwa Roho ni kumwagiwa maisha ya Kristo. Humwezesha mwenye kumpokea awe na sifa za Kristo. Ni wale wanaokuwa na Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yao, na ambao maisha ya Kristo yanadhihirishwa kwao ndiyo watakaolihudumia kanisa.

Kristo alisema: "Wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa; na wo wote mtakaowafungia dhambi wamefungiwa." Hapa Kristo hakumpa mtu ye, yote ruhusa ya kuwahukumu wengine. Hii ni haki ya Mungu tu. Lakini katika kanisa lililopangwa huweka wajibu umpasao kila mshiriki. Kwa wale wenye kuanguka katika makosa kanisa lina haki ya kuwaonya, kuwafundisha na ikiwezekana
[455] kuwarudisha tena kuwa waaminifu. Shughulikia dhambi kwa dhati. Taja dhambi kwa jina lake. Eleza jinsi Mungu asemavyo dhidi ya mwongo, mvunja sabato, mwizi, na maovu mengine yote. Kama

wakidumu dhambini hukumu unayowakatia kufuatana na Neno la Mungu hupitishwa mbinguni. Kanisa lazima lionyeshe kuwa halikubaliani na matendo ya jinsi hiyo la sivyo litamdhalilisha Bwana wake. Kanisa lazima lishughulikie dhambi kama Mungu anavyoagiza na hatua hiyo huthibitishwa mbinguni.

Lakini kuna upande wa furaha. "Wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa." Jambo hili liwe la muhimu. Mchungaji amwambie mkosaji juu ya rehema za Mwokozi. Hebu na wamtie moyo mwenye dhambi atubu na kumwamini yeye awezaye kusamehe dhambi. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote." 1 Yoh. 1:9. Hebu mkono wenye kutetemeka wa atubuye uwekwe katika mkono wenye upendo wa Yesu. Toba ya jinsi hiyo huthibitishwa mbinguni.

## Mungu Peke Yake Aweza Kusamehe

Ni kwa njia hii tu ndiyo kanisa linakuwa na uwezo wa kumwondolea dhambi mwenye dhambi. Ondoleo la dhambi linaweza tu kupatikana kwa sifa njema za Kristo. Uwezo wa kusamehe dhambi haukutolewa kwa mtu yeyote, au kwa kundi fulani la watu. Jina la Yesu ndilo jina pekee "chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." Mdo 4:12.

Mara ya kwanza Yesu alipokutana na wanafunzi katika chumba cha ghorofa, Tomaso hakuwako. Alisikia kutoka kwa wengine kwamba Yesu amefufuka, lakini huzuni na kutoamini vilijaza moyo wake. Ikiwa Yesu amefufuka kweli, hakutakuwa na tumaini la ufalme wa duniani. Na ilimuudhi kufikiria kwamba Bwana wake afufuke na kujidhihirisha kwa wengine wote isipokuwa yeye. Kwa hiyo aliamua kutoamini, na kwa juma zima alinung'unikia huzuni yake.

Alirudia mara kwa mara akisema: "Mimi nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia kidole changu katika mahali pa misumari na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki hata kidogo." Hakutumia imani kutokana na ushuhuda wa ndugu zake. Alimpenda Bwana wake lakini aliruhusu wivu na mashaka yajae moyoni mwake.

Siku moja jioni Tomaso alikusudia kukutana na wenzake katika
[456] chumba cha ghorofa. Alikuwa na tumaini kidogo sana kwamba kuwa habari hizo zilikuwa za kweli. Wakiwa wanakula chakula cha jioni, walikuwa wanaongea kuhusu ushahidi wa unabii alioutoa Kristo. "Kisha Alikuja Yesu na milango imefungwa, Akasimama katikati Akasema; Amani iwe kwenu."

Akamgeukia Tomaso na kusema; "Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu lete na mkono wako uutie ubavuni mwangu; wala usiwe asiyeamini bali aaminiye". Mwanafunzi mwenye mashaka alijua kuwa hakuna mwanafunzi mwingine ambaye angeweza kumwambia Bwana juu ya kutoamini kwake. Hakuwa na haja tena ya ushahidi zaidi. Moyo wake ukafurika kwa furaha, na akaanguka miguuni pa Yesu akilia: "Bwana wangu na Mungu wangu!"

Yesu alipokea ungamo lake, lakini kwa upole akakemea kutokuamini kwake: "Tomaso, wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki." Ikiwa ulimwengu sasa utafuata mfano wa Tomaso, hakuna mtu atakayeamini, kwa maana wote wale wanaompokea Kristo lazima wafanye hivyo kwa ushuhuda wa wengine. Wengi ambao, kama Tomaso hungojea mpaka kila shaka limeondolewa kamwe hawatafikia tumaini lao. Kwa taratibu huthibitika katika kutoamini kwao. Wanapanda mbegu za mashaka, na watavuna mashaka yao. Wakati imani na matumaini ni ya muhimu, wengi watajikuta pasipo kuwa na nguvu za kutumaini na kuamini.

Jinsi Yesu alivyomtendea Tomaso huonyesha namna ambavyo tunapaswa kuwatendea wale wanaokuza mashaka yao. Tomaso hakuwa na busara katika kuweka masharti ya imani yake, lakini Yesu, kwa wema wake alivunjilia mbali vizuizi vyote. Kwa nadra sana kutoamini huondolewa kwa mabishano. Lakini hebu mruhusu Yesu, katika upendo wake na rehema, adhihirishwe kama Mwokozi Aliyesulibishwa, na kutoka katika midomo ambayo hapo kwanza haikuwa tayari kusikike ungamo la Tomaso, "Bwana wangu na Mungu wangu."

## 85 — Kando Ya Bahari Tena [457]

Yesu alikuwa amepanga kukutana na wanafunzi wake huko Galilaya. Kutokuwako Yerusalemu wakati wa Juma la Pasaka kungesababisha wanafunzi kueleweka kuwa ni waasi wakana imani. Lakini baada ya kumalizika shughuli za Pasaka wanafunzi walifurahi kurudi nyumbani kukutana na Mwokozi kama alivyoagiza. Wanafunzi saba walifuatana. Walikuwa maskini kulingana na utajiri wa dunia hii lakini matajiri katika maarifa ya ukweli. Kwa muda wa miaka mitatu walikuwa wamefundishwa na Mwalimu Mkuu ambaye ulimwengu ulikuwa haujapata kumwona. Walikuwa wenye uwezo na makini, wakala ambao kwao wanadamu wataongozwa kupata maarifa ya kweli.

Wanafunzi walikusanyika mahali patulivu ambapo pasingekuwa na ghasia yo yote. Mbele yao ilikuwa ni pwani ambapo watu zaidi ya elfu kumi walilishwa kwa mikate michache na samaki. Siyo mbali sana na ulipokuwa mji wa Kapernaumu, kulikofanywa miujiza mingi.

Petro ambaye bado alikuwa anapenda sana mashua na hamu ya kuvua alipendekeza kuwa waende baharini wakavue kidogo. Walihitaji chakula na mavazi, ambavyo vingepatikana kutokana na mauzo ya kazi hiyo. Hivyo walienda; lakini usiku kucha walisumbuka bila kuambulia cho chote. Katika saa ya taabu zao waliongea juu ya kutokuwepo kwa Bwana wao. Walizungumzia hali yao ya siku za mbele, wakawa na wasiwasi jinsi mambo yalivyokuwa yakiwaendea.

Hatimaye kukapambazuka Mashua ikakaribia pwani, wanafunzi wakaona mgeni amesimama pwani, ambaye aliwasemesha kwa kuwauliza “Wanangu mna kitoweo?” Walipojibu kuwa La, “akawaambia, “Litupeni jarife upande wa kuume wa chombo, nanyi mtapata.” Basi, Wakatupa; wala sasa hawakuweza kulivuta tena
kwa sababu ya wingi wa samaki. Yohana akamtambua mtu yule na [458]
akamwambia Petro, “Ndiye Bwana.” Petro alifurahi kiasi kwamba akajitupa majini na kuogelea, kitambo alimfikia Bwana. Wanafunzi

wengine walikuja wakilikokota jarife lao lililojaa samaki. Wakaona huko moto wa makaa na juu yake pametiwa samaki na mkate.

"Yesu akawaambia, Leteni hapa baadhi ya samaki mliowavua sasa hivi." Petro akakimbilia jarife na kuvuta mpaka pwani. Baada ya hayo Yesu akamega mkate na kuwagawia wote, na wote saba wakamtambua. Lakini walishikwa na mshangao sana, na kwa kimyakimya wakamtazama Mwokozi aliyefufuka.

Wakakumbuka vizuri wakati ule Yesu alipowaita kando ya bahari na kuwaambia, "Wamfuate." Alikuwa amewaita waziache nyavu na mashua zao, na alikuwa ameahidi akawafanya wavuvi wa watu. Ili kuwakumbusha kisa hiki na kukazia wito wao, alirudia tena kufanya muujiza ili kufanya upya wito wake kwao. Kifo cha Bwana wao hakika hakikuondoa wajibu wa kufanya kazi aliyowapa. Ijapokuwa walikosa kazi ya kupatia mahitaji yao ya kila siku, kutokana na kuacha kazi yao ya awali, Mwokozi aliyefufuka atawapatia mahitaji yao yote. Ikiwa watatenda kazi pamoja naye, hawatashindwa kufaulu.

### Petro Alirudishwa Katika Hali ya Kutumainika

Kristo alihitaji kutoa fundisho jingine. Kwa Petro kumkana Bwana wake ilikuwa aibu na kinyume kabisa na madai yake ya awali ya kuwa mtiifu. Alikuwa amemdhalalisha Bwana wake, na ndugu zake hawakudhani kuwa Petro hatarudia kuwa mmoja wao tena. Hata yeye mwenyewe pia aliona kuwa amepoteza imani yake. Yampasa adhihirishe mbele zao ushahidi wa toba yake. Bila hivyo dhambi yake ingeadhiri mvuto wake kama mhudumu wa Kristo. Mwokozi alimpa nafasi tena ya kurudisha hadhi yake mbele ya ndugu zake, kadri iwezekanavyo aondoe aibu aliyoleta kwa kazi ya injili. Hapa liko fundisho kwa wafuasi wote wa Kristo. Dhambi za siri lazima ziungamwe kwa Mungu kwa siri; bali kwa dhambi za wazi toba ya wazi huhitajika. Dhambi ya mwanafunzi humfanya Shetani ashinde na roho zenye kusita kujikwaa. Kwa kuonyesha ushahidi wa toba mwanafunzi ataondoa aibu hii.

Wakati Kristo na wanafunzi walipokuwa wakila pamoja, Mwokozi akamwambia Petro," Je! Simoni wa Yohana, wewe wanipenda kuliko hawa?" akiwa na maana ya wanafunzi wen-
[459] zake. Akamwambia, Naam, Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda.

Akamwambia, Lisha wana kondoo wangu. Hakukuwa na msisitizo kuwa upendo wake ulikuwa mkuu kuliko ule wa wenzake.

Tena Mwokozi akarudia mtihani, "Simoni wa Yohana, wanipenda? Jibu la pili lilikuwa kama lile la kwanza, lisilokuwa na kujitapa; "Ndiyo, Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda." Yesu "Akamwambia, chunga kondoo zangu."

Kwa mara nyingine tena Mwokozi akauliza swali la mtihani; "Simoni wa Yohana, wanipenda? Petro akahuzunika. Alijua kuwa Bwana wake alikuwa na sababu ya kutomwamini, na kwa moyo uliouma akajibu; "Bwana, wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda. Yesu akamwambia tena, "Lisha kondo zangu.

Petro alikuwa amemkana wazi Bwana wake mara tatu, na mara tatu Yesu alimsonga na lile swali lilichoma moyo wake uliojeruhiwa kama mshale. Mbele ya kusanyiko la wanafunzi Yesu alifunua kina cha toba ya Petro na kuonye-sha jinsi yule mwanafunzi jeuri na mwenye kujitapa alivyokuwa ameshushwa.

Muda kitambo kabla ya kuanguka kwa Petro, Yesu alikuwa amemwambia, "Nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako," (Luka 22:32). Badiliko katika Petro lilikuwa dhahiri. Kwa sababu ya kunyenyekea na toba, Petro alijiandaa vizuri zaidi kuliko hapo awali kama mchungaji wa kundi.

Kazi ya kwanza Kristo aliyomkabidhi Petro ilikuwa kulisha "wana kondoo" kuhudumia wale waliokuwa wachanga katika imani, kuwafundisha wasiojua, kuyafungua Maandiko kwao na kuwaelimisha wafae katika huduma ya Kristo. Mateso yake pamoja na toba vilikuwa vimemwandaa kwa ajili ya kazi.

Kabla ya anguko lake, Petro siku zote alikuwa tayari kuwasahihisha wengine na kutoa maoni yake. Lakini Petro mwongofu alikuwa tofauti kabisa. Alidumisha mwamko wake wa kwanza, lakini neema ya Kristo ilirekebisha juhudi zake. Sasa aliweza kuwalisha wana kondoo pamoja pia na kondoo wa kundi la Kristo.

Namna ya Mwokozi ya kumshughulikia Petro iliwafunza wanafunzi kumkabili mkosaji kwa uvumilivu, huruma, na upendo unaosamehe. Akikumbuka udhaifu wake mwenyewe, Petro angeshughulikia kundi lake kwa upole jinsi Kristo alimshughulikia yeye.

## Kristo Aeleza Jinsi Petro Atakavyokufa

[460] Kabla ya kufa kwake, Yesu alimwambia Petro, "Niendako mimi huwezi kunifuata sasa, lakini utanifuata baadaye." Kuhusu jambo hili alikuwa amejibu Petro Bwana, kwa nini mimi nisiweze kukufuata sasa? Mimi Nitautoa uhai wangu kwa ajili yako," (Yohana 13:36, 37). Jaribu lilipokuja alishindwa lakini alikuwa apate nafasi nyingine ili athibitishe upendo wake kwa Kristo. Ili kwamba aimarishwe kwa ajili ya jaribu la mwisho la imani yake. Mwokozi alimfunulia maisha yake ya siku za usoni. Baada ya maisha yenye mafanikio, wakati ambapo uzee utamsogelea kwa hakika atamfuata Bwana wake. Yesu akasema; "wakati ulipokuwa kijana, ulikuwa ukijifunga mwenyewe na kwenda utakako; lakini utakapokuwa mzee, utainyoosha mikono yako na mwingine atakufunga na kukuchukua usikotaka." Alisema neno hilo kwa hali ya kuonyesha ni mauti gani atakayomtukuza Mungu."

Na hivyo Yesu alitabiri kunyosha mikono kwa Petro juu ya msalaba. Kisha akamwambia mwanafunzi wake, "Nifuate." Petro hakuvunjwa moyo na ufunuo huo. Alijisikia kuwa radhi kupata mateso ya kifo cho chote kile kwa ajili ya Bwana wake. Hapo awali Petro alikuwa amempenda Kristo kama mwanadamu; sasa alimpenda kama Mungu. Sasa alikuwa tayari kushiriki pamoja na Bwana katika utume wake wa kafara. Na hatimaye alipoletwa msalabani kutokana na ombi lake mwenyewe alisulibishwa kichwa chini. Aliona kuwa ni heshima kuu mno kuteseka kama Bwana wake alivyoteseka. Kabla ya hapo Petro alijaribu kupanga kazi ya Mungu badala ya kungojea kufuata mpango wa Mungu. Lakini Yesu alimwambia "Nifuate." Usinitangulie mbele. Acha mimi nitangulie mbele yako, na hutashindwa na adui. Petro alipokuwa akitembea kando kando ya Yesu alimwona Yohana akifuata nyuma yake. Naye akatamani kujua mambo yake ya mbele, na akamwambia Yesu, "Bwana, na huyu je? Yesu akamwambia, Ikiwa nataka huyu akae hata nijapo, imekupasa wewe? Wewe unifuate mimi.

Petro alipaswa kutambua kuwa Bwana wake atamfunulia yale yote aliyopasa kuyafahamu. Kule kusema juu ya Yohana kuwa "Ikiwa nataka huyu akae hata nijapo" Yesu hakutoa uthibitisho wo wote kuwa mwanafunzi huyu ataishi mpaka kurudi mara ya pili kwa Bwana na hata kama ni mapenzi yake kuwa iwe hivyo,

haingehusiana kwa vyo vyote vile na kazi ya Petro. Utii ulikuwa ndiyo wajibu wa kila mmoja.

Ni watu wangapi siku hizi wanapenda kufahamu mambo ya watu wengine, wakiwa na shauku kutaka kujua majukumu yao, huku wakiwa katika hatari ya kupuuza wajibu wao! Ni jukumu letu [461]
kumtazama Kristo na kumfuata. Kwa kumwangalia yeye, tutabadilishwa.

Yohana aliishi mpaka kushuhudia kuharibiwa kwa Yerusalemu na hekalu lake, ambao ni mfano wa uharibifu wa mwisho wa ulimwengu. Alimfuata Bwana wake mpaka siku zake za mwisho. Petro alikuwa amerejeshwa katika utumishi wa utume wake lakini heshima aliyokuwa amepokea kutoka kwa Kristo haikumpa ukuu wo wote dhidi ya ndugu zake. Kristo alikuwa ameliweka hili wazi katika kujibu swali la Petro, "Bwana, na huyu je?" Alimwambia, "Imekupasaje wewe? Wewe unifuate mimi." Petro hakutukuka kama kiongozi wa kanisa. Alikuwa na mvuto mkubwa katika kanisa, lakini somo Kristo alilomfundisha kando ya bahari ya Galilaya, Petro alilizingatia katika maisha yake yote.

Akiyaandikia makanisa, Petro alisema; "Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo . . . lichungeni kundi la Mungu ... si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka." Petro 5:1-4.

[462]

## 86 — “Enendeni . . . Mkawafanye Mataifa Yote”

Kristo akiwa amesimama hatua chache kutoka kiti chake cha enzi cha mbinguni, alitoa agizo, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, wafanye mataifa yote kuwa wanafunzi.” “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Marko 16:15. Maneno haya yalirudiwa mara kwa mara ili wanafunzi wapate kuona umuhimu wake. Nuru ya mbinguni lazima imulike kwa ukamilifu na nguvu kwa wakazi wote wa ulimwenguni.

Agizo hilo lilikuwa limetolewa kwa wale wanafunzi kumi na wawili kwanza katika chumba cha ghorofa, lakini sasa linatolewa kwa watu wengi zaidi. Katika mkutano huu uliofanyika katika mlima wa Galilaya waumini wote walioweza kuhudhuria walikuwepo. Malaika waliofika kaburini waliwakumbusha wanafunzi juu ya ahadi yake ya kukutana nao huko Galilaya. Ahadi hii pia ilirudiwa kwa waumini waliofika Yerusalemu wakati wa Pasaka na kwa kupitia kwao ahadi iliwafikia watu wote waliokuwa wanaomboleza kifo cha Bwana wao. Wote waliutazamia mkutano huu kwa hamu kubwa. Watu walikuja kutoka kila mahali wakiwa na mioyo yenye shauku.

Wakati ulipowadia kadiri ya waumini mia tano, walijikusanya vikundi vikundi kando ya mlima wakiwa na hamu ya kujua yote kutoka kwa wale waliomwona Kristo tangu kufufuka kwake.

Ghafla Yesu alisimama kati yao bila mtu kujua alitoka wapi na alifikaje. Wengi walikuwa hawajawahi kumwona, lakini mikono na miguu yake waliona alama za kusulibishwa; na walipomwona walimwabudu.

Lakini wengine walikuwa na mashaka. Na ndivyo itakavyokuwa siku zote. Kuna wale wanaona vigumu kuonyesha imani na hujiweka upande wa kutokuwa na imani. Nao hupoteza mengi kwa sababu ya kutoamini kwao.

[463] Msingi wa sura hii hupatikana katika Mathayo 28:16-20 Huu ulikuwa mkutano pekee ambao Yesu alikuwa nao pamoja na wengi wa waumini baada ya kufufuka kwake. Maneno yake yaliyokuwa yanatoka katika kinywa kilichokuwa kimefungwa katika mauti, yali-

wachangamsha. Sasa akatangaza kwamba "mamlaka yote" alikuwa amepewa. Mawazo ya wasikilizaji wake yaliinuliwa hadi dhana za juu zaidi za heshima na utukufu wake.

Maneno ya Kristo yalikuwa tangazo kwamba, dhabihu yake kwa ajili ya wenye dhambi, ilikuwa kamili na timilifu. Kazi aliyokuja kuifanya ulimwenguni imekamilika. Sasa alikuwa njiani kwenda kwa kiti cha enzi cha Mungu. Alikuwa ameanza kazi yake ya uombezi. Akiwa amevikwa utukufu kamili, Alitoa agizo, "Basi Enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:19, 20. Aliwaagiza wanafunzi wake wafundishe imani isiyokuwa na ubaguzi wa rangi wala nchi. Imani ihusuyo watu wote mataifa yote, na tabaka zote za watu.

Kristo alidhihirisha aina ya ufalme wake. Kusudi lake lilikuwa kuanzisha ufalme wa kiroho, na siyo mtawala wa kidunia katika kiti cha enzi cha Daudi. Aliwaambia waangalie yote aliyosema na kuyafunua kama Masihi na jinsi watu walivyomkataa, yalivyotumia. Aliyayasema kuhusu, kudhalalishwa, mateso na kifo chake yamethibitika. Siku ya tatu alifufuka tena. Katika mambo haya yote unabii ulikuwa umetimizwa.

Kristo aliwaagiza, wanafunzi wake wafanye kazi aliyowaachia kuanzia Yerusalemu. Yerusalemu palikuwa ndipo mahali pa unyenyekevu wake kwa ajili ya jamii ya wanadamu. Ni wachache waliokuwa wametambua jinsi mbingu ilivyoikaribia dunia wakati Yesu alipokuwa miongoni, mwao. Kazi ya wanafunzi lazima ianzie Yerusalemu. Wanafunzi wangeweza kuomba mahali pazuri zaidi pa kuanzia kazi, lakini hawakufanya ombi kama hilo. Kristo alikuwa ametawanya mbegu ya ukweli, nayo itatoa mavuno tele. Nafasi ya kwanza ya msamaha lazima itolewe kwa wauaji wa Mwokozi.

Wengi katika Yerusalemu walimwamini Yesu, kwa siri na wengi pia walipotoshwa na udanganyifu wa makuhani na wakuu. Watu kama hao walitakiwa watubishwe. Wakati Yerusalemu nzima ilikuwa inataharuki kwa sababu ya matukio ya majuma machache yaliyopita, mahubiri ya injili yangefanya mwamko mkubwa.

Lakini kazi isingekomea hapo. Kazi ingeendelea mpaka, kona [464]
zote. Kristo alikuwa amewaambia wanafunzi wake kuwa. In-

gawa taifa la Israeli limenikataa kama Maandiko yalivyotabiri, bado watakuwa na nafasi nyingine ya kumkubali Mwana wa Mungu. Kwenu ninyi wanafunzi wangu nawakabidhi ujumbe wa, rehema. Lazima utolewe kwanza kwa Waisraeli, halafu kwa mataifa yote na lugha na jamaa. Waaminio wote lazima wakusanywe katika kanisa moja.

## Roho Mtakatifu Afanikisha Kazi Yao

Kwa njia ya Roho Mtakatifu ushuhuda wa wanafunzi ulikuwa uthibitishwe kwa ishara na miujiza. Miujiza haitafanywa na mitume peke yao, bali na wale wote watakaopokea ujumbe wao. "Kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; washika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono iuu ya wagonjwa nao watapa afya." Marko 16:17, 18.

Nyakati hizo watu wabaya hawakusita kuwaondoa kwa sumu wale waliowazuia kutimiza malengo yao. Yesu alisema kuwa wengi watadhani kuwa, kuwaua mashahidi wake ni kumfanyia kazi Mungu. Kwa hiyo aliahidi kuwalinda na hatari hii. Aliwaahidi majaliwa mapya: wanafunzi walipaswa kuhubiri kwa mataifa mengine, na hivyo watapewa kipawa cha lugha zingine Mitume na wasaidizi wao walikuwa watu wasiyo na elimu lakini kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, Aliyemwagwa katika siku ya Pentekoste hotuba zao iwe ni katika lugha yao au ngeni, zilikuwa safi, sahihi, kwa maneno na :fasihi.

Hivyo Kristo aliwapa wanafunzi wake vifaa vya kufanyia kazi vilivyo kamili, naye mwenyewe alichukua jukumu la kuifanikisha. Aliwaagiza, Enendeni mkawafanye mataifa yote. Enendeni kwa kila sehemu ya ulimwengu inayokaliwa lakini mkijua kuwa kuwako kwangu kutakuwepo. Fanyeni kazi kwa imani na tumaini

Agizo la Mwokozi huwahusu waumini wote mpaka mwisho wa wakati. Ni kosa kubwa kudhani kwa kazi ya kuokoa roho inawategemea wachungaji wenyewe. Kanisa lilianzishwa kwa ajili ya kufanya kazi hii. Wote wanaochukua imani hii wanayo dhamana ya kuwa watenda kazi pamoja na Kristo. Potelea mbali mtu awe na kazi gani, jukumu lake la kwanza linapaswa kuwa, kuongoa roho kwa ajili ya Kristo. Inawezekana asiweze kuhutubia mikutano, lakini anaweza kutenda kazi kwa mtu mmoja mmoja. Mbali na karibu kuna roho

zilizolemewa na hatia. Siyo maisha magumu au umaskini vinavyodalilisha wanadamu. Ball ni hatia, kutenda uovu. Kristo anatamani watenda kazi wake wahudumie roho zinazougua kwa dhambi. [465]

Kila mtu ni lazma aanzie pale alipo. Katika jamaa zetu wanaweza kuwamo watu walio na njaa ya mkate wa uzima. Katika ujirani wetu wanaweza kuwapo walio makafiri. Kazi ikitendeka kwa imani matokeo yake yatasikika duniani pote. Mungu mara nyingi hutumia njia za kawaida ili kuleta mafanikio makubwa. Mtenda kazi aliye mnyenyekevu akiongozwa na Roho Mtakatifu atagusa kamba ambazo zitatoa wimbo utakaoenea katika vizazi vyote.

## Maisha ya Afya ni Sehemu ya Injili

Katika namna ya Mwokozi kuponya kulikuwa na mafundisho kwa wanafunzi wake. Uponyaji ulitoka tu kwa Uwezo wa yule Mponyaji mkuu, lakini Kristo alitumia njia za kawaida tu za kuponya. Alifundisha kuwa ugonjwa huletwa na kuvunjwa kanuni za Mungu, sheria za kiroho na za kimwili. Matatizo ya watu ulimwenguni yangaliepukika kama watu wangeishi kulingana na mpango wa Muumbaji. Alifundisha kuwa afya njema ni zawadi ya utii kwa kanuni za Mungu. Mganga Mkuu alikuwa amezungumza na watu wake kutoka wingu la moto, "Kwamba utaisikiliza kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake,... mimi sitatia juu yako maradhi yo yote" kwa kuwa mimi ndimi BWANA nikuponyaye." (Kutoka 15:26.) Kwa wagonjwa tunaweza kuwapa dawa Mungu alizoziweka katika mimea, na kuwaelekeza kwake mwenye uzima na aliye Mponyaji hasa. Tuwafundishe kuamini katika Mponyaji Mkuu na kutegemea uwezo wake.

Ni pale tu tunaposhiriki katika upendo wa Kristo kwa imani ndipo nguvu ziletazo uzima zitakapotiririka kutoka kwetu kwenda kwa watu wengine. Kulikuwa na sehemu zingine pengine ambapo Mwokozi hakuweza kufanya miujiza yake kwa sababu ya kutoamini kwao. Vivyo hivyo sasa kutoamini kanisa hulitenga kutoka kwa Msaidizi wa mbinguni. Kwa kanisa kutokuwa na imani humsikitisha Mungu na kumnyang'anya utukufu wake Uhai wa kanisa hutegemea uaminifu wake katika kutekeleza utume wa Bwana. Mahali ambapo hakuna juhudi ya kuwahudumia wengine upendo hupoa na imani

hufifia. Malaika hushangaa kwa sababu ya watu kukosa shukrani
[466] kwa upendo wa Mungu. Mama na baba wangejisikiaje kama mtoto wao aliyepotea katika baridi na theluji alitekelezwa aangamie na watu ambao wangalimsaidia? Mateso ya kila mtu ni mateso ya Mtoto wa Mungu, na wale wasiojali kuwasaidia wanadamu wenzao wanaoangamia husababisha hasira takatifu ya Mungu.

### Injili Ilivyo Na Uwezo

Kristo aliwapa wanafunzi wake ujumbe wake. Alisema Wafundishe watu "kuyashika yote niliyowaamuru ninyi;" Yale aliyosema siyo kwa mdomo tu, bali pia katika Agano la Kale yanahusika hapa. Hakuna nafasi kwa hadithi za mapokeo, mawazo ya watu, au sheria zilizopitishwa na mamlaka za kidini. "Torati na manabii," pamoja na taarifa za maneno na matendo yake mwenyewe, ndiyo hazina inayopaswa kupewa ulimwengu.

Injili isitolewe kama kitu ambacho hakina uhai, bali itolewe kama kitu hai chenye kubadili maisha ya watu. Wale walioishi maisha ya yanayomchukiza Mungu hukubaliwa. Wakitubu atawajaza roho yake ya mbinguni, halafu huwatuma katika mahali pa watu wakorofi kutangaza rehema zake zisizo na kikomo. Kwa njia ya neema yake watu wanaweza kupokea tabia ya Kristo, na hufurahi katika pendo lake kuu.

Yesu hatosheki kutangaza mibaraka hii tu; bali huitoa kwa njia ile ipendezayo inayowavutia watu kuipata. Kwa hiyo watumishi wake watangaze kipawa hiki kisicho na kifani. Upendo wa Yesu wa ajabu utalainisha na kutiisha mioyo ya watu ambapo kuyakazia mafundisho hakutafanikisha lo lote. Maneno matupu hayawezi kuelezea. Kristo anahitaji kuchorwa katika kila mfuasi wake. Upendo uonekane wazi katika maisha ya kila mtu, upendo na uvumilivu wake, rehema zake na kweli vinapaswa kudhihirishwa katika ulimwengu.

Wanafunzi wa kwanza walijiandaa kwa kazi yao. Kabla ya siku ya Pentekoste walikusanyika pamoja na wakaondoa tofauti zao zote. Wakaomba kwa nia moja kwa imani na wakiwa na mzigo kwa roho za watu. Ndipo Roho Mtakatifu akamwagwa kwao, na watu maelfu waliongoka kwa siku moja.

Na ndivyo inavyoweza kuwa na sasa pia. Hebu Neno la Mungu na lihubiriwe. Hebu Wakristo na waondoe tofauti zao, wajitoe kwa Mungu, kuongoa watu waliopotea. Hebu kwa imani na waombe mibaraka nayo itakuja. Kumwagwa kwa roho katika siku za mitume ilikuwa “mvua ya vuli” na matokeo yalikuwa ya utukufu, lakini “mvua ya masika” itakuwa tele. (Yoeli 2:23.)

Wote wanaojiweka waklu nafsi mwili na Ii” I.».ikwa [467]

Mungu daima watakuwa wanapokea uwezo mpya, wa kimwili na kiakili. Kwa kushirikiana na Kristo, katika udhaifu wa kibinadamu wanawezeshwa kutenda matendo ya Mwenyezi Mungu.

Mwokozi atamani kudhihirisha neema yake na kuwapa chapa ya tabia yake katika ulimwengu wote. Anatamani kuwafanya wanadamu wawe huru, safi na watakatifu. Kwa njia ya damu iliyomwagika kwa ajili ya ulimwengu, kuna ushindi wa kufikiwa ambao utamletea utukufu Mungu na Mwana Kondoo. Kristo “Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika.” Isaya 53:11.

[468] ## 87 — Kristo Aingia Mbinguni Kwa Ushindi

Muda ulikuwa umefika kwa Kristo kupaa, kwenda kwa kiti cha enzi cha Baba yake kama Mungu mshindi. Baada ya kufufuka kwake alikaa duniani kwa muda ili wanafunzi wake wamzoee akiwa na mwili wa utukufu. Sasa alifikia wakati wa kuondoka. Wanafunzi wake hawakupaswa tena kuendelea kumhusisha na kaburi. Waanze kumfikiria kama aliyetukuka mbele za mbingu. Kama mahali pa kupalia kwenda mbinguni Yesu alichagua pale alipokuwa akizoea kwenda alipoishi duniani, yaani Mlima wa Mizeituni. Vichaka na vibonde vyake vilikuwa vimewekwa wakfu kwa maombi na majozi yake. Katika bustani ya Gethsemani, chini ya mlima huu alikuwa ameomba kwa uchungu mkuu peke yake. Juu ya kilele chake ndipo miguu yake itakapokanyaga arudipo mara ya pili, akiwa Mfalme wa utukufu wakati haleluya za Waebrania zitakapounganika na Hosana za wamataifa na jeshi kubwa litakapoitikia kwa sauti, Mvikeni taji Bwana wa wote!

Sasa Yesu na wanafunzi wake walianza safari kuelekea mlimani. Walipokuwa wakipita katika malango ya Yerusalemu watu wengi walikuwa wakiwaangalia kwa mshangao wakiongozwa na yule ambaye majuma machache kabla ya hapo wakuu walikuwa wamemsulibisha. Wanafunzi hawakujua kuwa hiyo ndiyo ilikuwa mara ya mwisho kuzungumza na Bwana wao. Yesu alitumia muda akikaa pamoia nao, akiyarudiarudia mafundisho yake. Walipokaribia Gethsemane, Alisimama. Aliuangalia mzabibu aliokuwa ameufananisha na mwungano wa kanisa lake na yeye na Baba yake. Tena akarudia ukweli aliokuwa ameufunua.

Kristo akiishi ulimwenguni kwa miaka thelathini na mitatu alikabiliana na fedheha, matusi na dhihaka. Alikuwa amekataliwa na
[469] kusulibishwa. Sasa alikumbuka hali ya utovu wa shukrani ya watu aliokuja kuwaokoa, je atawaondolea huruma yake na upendo wake? La; ahadi yake ni kwamba "Mimi nipo pamoja nanyi siku zole hata ukamilifu wa dahari." Mathayo 28:20.

Walipofika Mlima wa Mizeituni, Yesu aliwaongoza mpaka kileleni kukabili jirani na Bethania. Hapa alisimama na wanafunzi wakamzunguka. Aliwatazama kwa upendo. Hakuwalaumu kwa makosa yao au kushindwa kwao; maneno ya huruma kuu, rehema aliyowambia yalikuwa ndiyo ya mwisho kudondoka kutoka kinywani mwa Bwana wao. Akiinyosha mikono yake juu yao katika kuwabariki, na kana kwamba anawahakikishia ulinzi wake kwao, Aliinuliwa taratibu kutoka kwao, akivuta kwenda mbingu kwa nguvu kuu kuliko uvutano wo wote wa duniani. Alipokuwa akipanda wanafunzi walimkodolea macho mara ya mwisho Bwana wao. Wingu la utukufu likamficha na alipokuwa akipokelewa na gari la wingu tukufu la malaika maneno yafuatayo yakasikika "Tazamia mimi nipo pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari." Wakati huo huo wimbo mtamu kuliko zote ukawamwagikia kama burudiko tulivu kutoka kwa kwaya ya malaika.

## Alipokewa Kwa Magari ya Malaika

Wanafunzi walipokuwa wangali wakikaza macho mbinguni, malaika wawili wenye sura ya wanadamu, wakasema: "Enyi watu Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."

Malaika hawa ambao ni wenye hadhi kuu katika malaika wote, walikuwa ni wale waliokuja kaburini kwa Yesu wakati wa kufufuka kwake. Walitamani kuungana na kundi la malaika waliokuja kumlaki Yesu, lakini katika kuwahurumia wale walioachwa na Yesu walibakia kuwafariji.

Kristo alikuwa amepaa juu katika mwili wa binadamu Yesu yule yule aliyekula pamoja nao, na aliyekuwa siku ile amepanda mlima wa Mizeituni pamoja nao. Malaika waliwahakikishia kuwa, ni Yule Yule waliyemwona akienda zake mbinguni, ndiye atakayekuja tena jinsi iyo hiyo alivyokwenda mbinguni. Atakuja "na mawingu; na kila jicho litamwona." "Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." "Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote, pamoja naye ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake." [470]

Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4:16; Mathayo 25:31.

Hivyo ndivyo itakavyotimizwa ahadi yake Bwana kwa wanafunzi wake; “Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.” Yohana 14:3.

Baada ya mateso na kusulibishwa kwa Kristo maadui wa wanafunzi walitumaini kuwaona wakionyesha huzuni na kukata tamaa. Lakini badala ya hayo waliwaona wakichangamka na kufurahi kwa ushindi na nyuso zao ziking’aa kwa furaha isiyokuwa ya duniani. Kwa shangwe walisimulia hadithi ya ajabu ya kufufuka na kupaa kwa Kristo, na ushuhuda wao ulipokelewa na wengi.

### Hofu ya Wanafunzi Ilitoweka!

Wanafunzi hawakuwa na mashaka tena juu ya siku za usoni. Walifahamu kuwa Yesu yuko mbinguni, na ya kuwa fadhili zake ziko pamoja nao. Walijua kuwa walikuwa na rafiki karibu na kiti cha enzi cha Mungu, na walikuwa na hamu ya kuyapeleka maombi yao katika jina la Yesu. Kwa kicho waliomba walisujudu kuomba wakikariri ahadi yake, kwamba: “Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu . . . Ombeni, nanyi mtapata, furaha yenu iwe timilifu.” Yohana 16:23, 24. Na Pentekoste iliwaletea furaha timilifu mbele ya Mfariji, kama Kristo alivyoahidi.

Mbingu yote ilikuwa inangojea kumpokea Mwokozi. Alipopaa aliongoza njia, na umati wa mateka waliokombolewa wakati wa kufufuka kwake ukiwa unafuata. Na walipokaribia karibu na mji wa Mungu, changamoto ilitolewa na malaika wasindikizaji.

“Inueni vichwa vyenu, enyi malango;
Inukeni, enyi malango ya milele;
Mfalme wa utukufu apate kuingia.”

Kwa shangwe Mababawabu waliitikia:

Ni nani Mfalme wa utukufu?

Walisema hivi si kwa sababu hawamjui yeye Alikuwa ni nani bali walitamani kusikia jibu la kutukuza.

Bwana mwenye nguvu hodari,
Bwana hodari wa vita!
Inueni vichwa vyenu enyi malango.

Naam, viinueni, enyi malango ya milele,
Mfalme wa utukufu apate kuingia.

Kisha malango ya mji wa Mungu yalifunguliwa wazi, na jeshi la [471] Malaika likaingia kwa shangwe za nyimbo. Majemadari wa majeshi ya malaika, na wana wa Mungu wanaowakilisha sayari za viumbe ambavyo havikuanguka dhambini ‘ walikusanyika ili kumkaribisha Mwokozi na kusherekea ushindi wake.

Lakini aliwapungia mkono akisema: Bado siyo sasa.” Aliingia mbele ya Mungu Baba. Akaonyesha makovu ya kichwa chake, ubavu uliochomwa, miguu iliyokuwa na majeraha; Akainua mikono yenye alama za misumari. Aliwaonyesha wale waliofufuka pamoja naye kama wawakilishi wa umati wa wale watakaofufuka kutoka makaburini akija mara ya pili. Kabla ya kuweka misingi ya dunia Baba na Mwana walishikana mikono wakaahidi kuwa Kristo atakuwa arbuni wa wanadamu. Pale msalabani Kristo alipolia “Imekwisha”, Alikuwa akimwambia Baba yake. Mapatano yalikuwa yamekamilishwa. Na sasa akatamka, Baba nimeikamilisha kazi ya ukombozi.

“Hao ulionipa nataka wawe pamoja nami po pote nilipo.” Yohana 17:24.

Sauti ya Mungu ikatangaza kwamba haki imetimizwa na Shetani sasa ameshindwa. Wafuasi wa Kristo wanaotaabika na kujitahidi duniani wamekubalika “Katika huyo Mpendwa.” Waefeso 1:6. Mikono ya Baba ikamkumbatia Mwanaye, na tamko likatolewa: Na wamsujudu Malaika wote wa Mungu.” Waebrania 1:6.

Mbingu ilionekana kujazwa kwa furaha, na sifa. Upendo ulikuwa umeshinda. Mpotevu amepatikana. Sauti zikajaa tele mbinguni zikitangaza kwa sauti nzuri zikisema: “Baraka, na heshima, na utukufu na uweza na nguvu una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana Kondoo, hata milele na milele.” Ufunuo 5:13.

Kutoka katika hilo tukio la furaha ya mbinguni, mwangwi wa maneno ya Kristo huturudia duniani ukisema, “Ninapaa kwenda kwa Baba yangu naye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu.” Yohana 20:17. Jamaa ya mbinguni imeunganika na jamaa ya duniani. Kwa ajili yetu Bwana wetu alipaa, na kwa ajili yetu anaishi. “Kwa sababu hii aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao

Mungu kwa njia ya yeye, maana yu hai siku zote ili awaombee." Waebrania 7:25.